

**UCHANGANUZI WA MOFOSINTAKSIA YA LUGANDA KATIKA MATUMIZI YA
KISWAHILI SANIFU WILAYANI KAMPALA, UGANDA**

**NA
MULEI MARTIN**

**TASNIFU ILIYOSILISHWA KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI**

SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII

CHUO KIKUU CHA MASENO

©2023

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo chochote kutosheleza mahitaji ya shahada ya Uzamifu katika Kiswahili

Mulei Martin

PHD/FA/00087/2016

(Mtahiniwa)

Sahihi: Tarehe.....

Idhini

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa kirasmi na Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya.

Dkt. Debora Nanyama Amukowa

Chuo Kikuu cha Maseno,

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Shule ya Sanaa na Sayansi Jamii.

(Msimamizi)

Sahihi: Tarehe.....

Dkt. Asiko Beverlyne Ambuyo

Chuo Kikuu cha Maseno,

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Shule ya Sanaa na Sayansi Jamii.

(Msimamizi)

Sahihi: Tarehe.....

SHUKRANI

Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na hekima wakati wote wa masomo yangu. Ninatoa shukrani zangu za dhata kwa wasimamizi wangu wote. Mchango na ukwasi wao kitaluuma uliniendeleza na kuniwezesha kuzingatia utafiti huu kwa dhata. Sina maneno maalumu ambayo ninaweza kutumia kuwashukuru Dkt. Debora Nanyama Amukowa na Dkt. Asiko Beverlyne Ambuyo ambao walishiriki kikamilifu kuniongoza na kunielekeza kufikia mwisho wa utafiti huu. Aidha, ningependa kutoa shukrani zangu za dhata kwa Prof. Kinene wa Mutiso, Dkt. Ayub Mukwana, Dkt. Chacha Learnard Mwita na wahadhiri wengine waliotoa mchango wao kimashauri na kimwongozo kufanikisha tasnifu hii.

Walimu wangu katika shahada ya Uzamili pamoja na wasimamizi wakiwemo, Assoc. Prof. Beja Karisa (Mungu ailaze roho yake mahali pema), Prof. Kitula King'ei, Prof. Kineene wa Mutiso, Daktari Mukwana Ayub, Dkt. Matasi Badru Haroon, na walimu wengineo. Mungu azidi kuwaangazia neema ya ufanisi kwa maarifa yenu. Ninawashukuru wahadhiri wangu katika chuo kikuu cha Makerere kwa kunipa mafunzo yangu ya shahada ya Kwanza. Miongoni mwao wakiwemo, Prof. Ruth Mukama, Austine Bukonya, Dkt. Mukuthuria (Mungu ailaze roho yake mahali pema), Dkt. J.C Nsookwa (Mungu ailaze roho yake mahali pema) na wengineo. Mungu azidi kuwaangazia neema ya ufanisi kwa maarifa yenu.

Vilevile ninawashukuru wazazi wangu Patrick Mulei, Jane Nasimuyu (roho yake ilazwe mahali pema peponi na Imelda Nasimiyu kwa ushauri wenu pamoja na kunipa moyo na kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha elimu. Walezi wangu na wafadhili katika maisha na elimu, John Nakisisa, Jane Nandutu, Bwana Ibrahim Kafeero, Dkt. Masaba Sowedi, Dkt. Madanda, Dkt. Bashir Kishabale, Familia ya Waniale na Nambalu, Beatrice Nekesa na wazamifu wenzangu kwa mawaidha yenu. Ninaomba Mungu awabariki sana kwa mashauri yenu yaliyoniwezesha kufikia hatima hii ya kielimu. Aidha, sitawasahau wanafunzi wenza Mutenyo Aidah na Atukunda Edwin tuliosukuma mkondo huu wa elimu pamoja. Mungu awabariki kwa ushirikiano wenu tulipokuwa katika harakati hii ya masomo hadi mwisho. Kwa Mke wangu Khatundi Sulea na watoto wangu hasa Aliyah Halima Mulei walioniamsha kila mara kutekeleza kazi hii. Mungu awape neema na amani maishani. Mwisho, ni kwa wale wote walionisaidia kwa hali moja au nyingine kufanikisha utafiti huu. Marafiki wengineo ambao sikuwataja kwa majina, Mungu awabariki kwa msaada wenu kufikia kilele cha elimu yangu.

TABARUKU

Naitabarukia kazi hii kwa familia yangu

IKISIRI

Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye mifumo na miundo ya kiisimu ambayo ina upekee wake. Upekee huu husababisha tofauti za kiisimu na lugha nyinginezo za Kibantu kimuundo na kimfumo na kujenga athari za mwingiliano wa kimofosintaksia unaodhihirika katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Ingawa Kiswahili sanifu kinafundishwa shuleni nchini Uganda, matokeo ya matumizi yake yanadhihirisha athari za mwingiliano wa miundo na kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Azma ya utafiti huu ilikuwa kuchanganua miundo na kanuni za mofosintaksia za Luganda na Kiswahili ili kubaini athari za mwingiliano wa utafiti huu ilikuwa: Kwanza, kufafanua jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda sanifu hufanana na kutofautiana na vya Kiswahili sanifu. Pili, kuchanganua miundo na kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili, tatu kutathimini athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu uliongozwa na mihimili miwili ya Ubia na Upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na Uganifu ya Chomsky (1981). Mihimili ya sarufi bia na upatanifu ilizingatiwa katika kufafanua na kuchanganua kanuni za mofosintaksia ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Muundo wa kimaelezo ulitumika katika utafiti huu. Utafiti huu ulifanyika katika kata tano za wilaya ya Kampala, Uganda. Ulijikita katika taaluma ya isimu linganishi na tumikizi. Ulichunguza jinsi isimu ya lugha za Kibantu huchangiana, kuingiliana na kuathiriana katika matumizi. Mbinu ya usampulishaji nasibu ilitumika kuteua shule 12 ambazo zinafundisha Kiswahili katika kidato cha sita. Mbinu ya kimaksudi na dhamirifu ilitumika kuwateua wanafunzi 54 wa kidato cha sita ambao L1 ni Luganda na watumiaji wa Kiswahili kama L2. Data ilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini kutumia kifaa cha kudondoa data cha orodhahakiki chenye sifa za kimofosintaksia zinazotambulisha vipashio vya kimofosintaksia, miundo yake na kanuni za matumizi kudodoa data kulingana na malengo matatu ya utafiti. Nyanjani data ilikusanywa kutoka kwa wanafunzi kupitia kwa mijarabu na mijadala. Mijadala iliandaliwa kwa wanafunzi kujadili matokeo ya mijarabu ili kutathimini athari za mwingiliano wa kimofosintaksia wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika maandishi na mazungumzo shiriki. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kutumia mbinu ya kimaelezo ikishirikisha majedwali na michoro kudhihirisha jinsi kanuni na miundo ya mofosintaksia ya Luganda inavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda. Utafiti huu ulibaini kuwa licha ya Luganda na Kiswahili sanifu kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti za Kibantu zenye vipashio, miundo na kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia zinazofanana na kutofautiana. Uchanganuzi ulibaini athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Tathimini ya mwingiliano ulidhihirisha athari za uhamishaji, ujumlishaji, uchopekaji, udondoshaji, uchanganyaji, uongezaji wa fonimu na maumbo, miundo na kanuni za mifanyiko ya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Athari hizi zilidhihirisha ukiukaji wa matumizi ya maumbo, miundo na kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu na kusababisha matumizi ya Kiswahili kisicho sahihi hasa katika mazungumzo na maandishi ya wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Matokeo haya ni mchango mkubwa katika taaluma ya isimu linganishi ya lugha za Kibantu kwa kutambua athari za mwingiliano wa vipashio, miundo na kanuni za mifanyiko ya mofosintaksia ya Luganda kudhihirisha jinsi inavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, kukuza na kuendeleza umilisi na matumizi ya Kiswahili sanifu nchini Uganda. Utafiti huu ulipendekeza tafiti zaidi kufanywa kuhusiana na mwingiliano wa L1 katika matumizi ya L2 ili kuweka mikakati na misingi ya kukuza na kuendeleza umilisi na matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi unaotokana na mchango na athari za L1.

ABSTRACT

Kiswahili is a Bantu language with linguistic systems and structures that have unique characteristics. This uniqueness makes Kiswahili language to possess linguistic differences from other Bantu languages in terms of its systems and structures hence building morphosyntactic interference which manifests in the use of standard Kiswahili. Although standard Kiswahili is taught in schools in Uganda, research conducted on the outcome of its use reveals linguistic interferences of systems of linguistic categories and structures of Luganda morphosyntactic units in the writing and communication of students whose L1 is Luganda. The purpose of this study was to analyze the morphosyntactic interference of Luganda on Kiswahili usage in Kampala- Uganda, to determine the influence of Luganda structure and principles on the use of standardized Kiswahili. The objectives of the study were; first, to explain how the morphosyntactic units of standard Luganda are similar and different from those of standard Kiswahili. Secondly, to examine Luganda and Kiswahili morphosyntactic processes and subsequently evaluate how morphosyntax structures and principles of Luganda interfere with those of standard Kiswahili. The research was guided by two tenets of government and binding theory (Chomsky 1981) which analyses language on the basis of the native speakers' competence. The theory explains that certain parts of a sentence relate on the basis of several principles, and every constituent is understood from the perspective of structural relations, whereby, the head governs the forms of its arguments. The research adopted a descriptive research design. The study was conducted in five divisions of Kampala district, Uganda focusing on the field of comparative and applied linguistics. The study population consisted of 12 secondary schools in Kampala district and 54 'A' Level Kiswahili students whose L1 is Luganda. Random Purposive sampling was used to select 12 'A' Level schools and Purposive snowballing to select 54 'A' Level Kiswahili students whose L1 is Luganda. The third sample were 34 selected books and texts on Luganda Grammar and standard Kiswahili. The books and texts were purposively selected to analyze the morphosyntactic characteristics, principles and structures of Luganda and Kiswahili morphosyntactic units to meet the research objectives. Data was collected from the students through morphosyntactic tests and discussions, text analysis and observation schedules to students to explain, examine and analyze the impact of Luganda's system interference on the use of standardized Kiswahili from learners writing and communications. The data was analyzed and presented using descriptive approaches involving tables and diagrams to demonstrate how Luganda morphosyntactic principles and structures interfere and influence the use of standard Kiswahili among Kiswahili students whose L1 is Luganda. The study found out that despite Luganda and standard Kiswahili being languages of the same family, they are two different Bantu languages with similar and different elements, structures and morphosyntactic principles. The analysis revealed the linguistic interferences of Luganda morphosyntax in the use of standard Kiswahili. The evaluation found the interlanguage of Luganda morphosyntax structures and principles in the use of Kiswahili language in writing and communication of students whose L1 is Luganda. The findings of the study is an evidence on the Bantu comparative and applied study between Luganda and Kiswahili linguistic interferences, promote and support the development of competencies and standardized Kiswahili usage for L2 speakers in Kampala Uganda. This study recommended more research to be done in the field of linguistic interferences in order to set strategies and foundations to promote and develop the mastery and the use of standard Kiswahili among students resulting from language contact and influences of L1.

YALIYOMO

| | |
|---|-----------|
| IKIRARI | ii |
| SHUKRANI..... | iii |
| TABARUKU | iv |
| IKISIRI | v |
| ABSTRACT..... | vi |
| YALIYOMO..... | vii |
| ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMI..... | xiv |
| MAELEZO YA ISTILAHU..... | xv |
| ORODHA YA MAJEDWALI..... | xvii |
| SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI | 1 |
| 1.1 Utangulizi..... | 1 |
| 1.1.1 Usuli wa Suala la Utafiti | 1 |
| 1.1.1.1 Athari za mwingiliano wa lugha ya kwanza kwa lugha ya Pili | 1 |
| 1.1.1.2 Dhana ya mofosintaksia ya lugha | 2 |
| 1.1.1.3 Luganda na Kiswahili sanifu | 5 |
| 1.1.1.4 Uwiano na Tofauti za Lugha za nasaba moja | 6 |
| 1.2 Suala la utafiti | 10 |
| 1.3 Maswali ya utafiti | 11 |
| 1.4 Madhumuni ya utafiti..... | 11 |
| 1.5 Umuhimu wa utafiti | 12 |
| 1.6 Upeo wa utafiti..... | 14 |
| 1.7 Misingi ya Nadharia..... | 15 |
| 1.7.1 Nadharia ya Umilikifu na Unganifu | 15 |
| 1.7.2 Mihimili ya nadharia ya Umilikifu na unganifu | 17 |
| 1.7.3 Ufaafu wa Nadharia kwa utafiti | 19 |
| 1.8 Hitimisho..... | 19 |
| SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI | 21 |
| 2.1 Utangulizi..... | 21 |
| 2.2 Kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya mofosintaksia vya lugha | 21 |
| 2.3 Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya mofosintaksia ya lugha | 31 |
| 2.4 Tathimini za kanuni za mofosintaksia, mwingiliano na athari katika matumizi | 45 |
| 2.5 Hitimisho..... | 54 |

| | |
|--|-----|
| SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI | 56 |
| 3.1 Utangulizi..... | 56 |
| 3.2 Muundo wa Utafiti..... | 56 |
| 3.3 Eneo la Utafiti..... | 57 |
| 3.4 Kundi Lengwa..... | 57 |
| 3.5 Usampulishaji na Sampuli..... | 58 |
| 3.5.1 Mbinu za Usampulishaji..... | 58 |
| 3.5.2 Sampuli..... | 59 |
| 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data..... | 60 |
| 3.6.1 Uchanganuzi Matini..... | 60 |
| 3.6.2 Mbinu ya Mjarabu na Mjadala..... | 61 |
| 3.7 Vifaa vya Ukusanyaji Data..... | 62 |
| 3.7.1 Mjarabu ya Kimofosintaksia..... | 62 |
| 3.7.2 Kifaa cha Orodha ya Uchunzaji cha Vipashio vya Mofosintaksia..... | 62 |
| 3.8 Ufaafu na Utegemezi wa Vifaa vya Kukusanya Data za Utafiti..... | 63 |
| 3.9 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data..... | 64 |
| 3.10 Maadili ya Utafiti..... | 67 |
| 3.11 Hitimisho..... | 68 |
| SURA YA NNE: VIPASHIO VYA MOFOSINTAKSIA VYA LUGANDA NA | |
| KISWAHILI SANIFU | 69 |
| 4.1 Utangulizi..... | 69 |
| 4.1.1 Ufafanuzi wa uwiano na tofauti za ngeli za nomino za Luganda na Kiswahili..... | 69 |
| 4.1.1.1 Kufanana na kutofautiana kwa ngeli mkabala wa mfumo wa uainishaji..... | 70 |
| 4.1.1.2 Uwiano na tofauti mkabala wa vibainishi ngeli na viambishi ngeli..... | 73 |
| 4.1.1.3 Kufanana na kutofautiana kwa ngeli mkabala wa uwiano wa Kisarufi..... | 75 |
| 4.1.1.4 Kufanana na kutofautiana kuzingatia nafasi ya uambishaji kimofosintaksia..... | 79 |
| 4.1.1.5 Kufanana na kutofautiana kuzingatia uidadishaji wa nomino katika ngeli..... | 81 |
| 4.1.1.6 Uwiano na tofauti wa nomino katika ngeli kimfumo wa kimofosintaksia..... | 84 |
| 4.1.2 Uwiano na tofauti ya aina mbalimbali za vivumishi vya Luganda na Kiswahili..... | 87 |
| 4.1.2.1 Uwiano na tofauti za Vimilikishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu..... | 87 |
| 4.1.2.2 Uwiano na tofauti za vivumishi vya –a Uganifu vya Luganda na Kiswahili Sanifu..... | 93 |
| 4.1.2.3 Uwiano na Tofauti za Vivumishi Vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu..... | 97 |
| 4.1.2.4 Uwiano na Tofauti za Vivumishi vya Sifa vya Luganda na Kiswahili..... | 101 |
| 4.1.2.5 Uwiano na tofauti za Vivumishi vya Idadi vya Luganda na Kiswahili Sanifu..... | 104 |

| | |
|--|------------|
| 4.1.2.5.1 Vivumishi vya idadi isiyodhahiri..... | 104 |
| 4.1.3 Uwiano na tofauti za Viwakilishi vya Luganda na Kiswahili sanifu Kimofosintaksia | 110 |
| 4.1.4 Vikanusho | 113 |
| 4.1.4.1 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa nomino za Luganda na Kiswahili..... | 113 |
| 4.1.4.2 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa Vivumishi vya Luganda na Kiswahili | 116 |
| 4.1.4.3 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa Viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili | 119 |
| 4.1.4.4 Uwiano na Tofauti ya Ukanushaji wa Njeo na Hali katika Luganda na Kiswahili | 122 |
| 4.2 Hitimisho..... | 127 |
| SURA YA TANO: KANUNI ZA MIFANYIKO YA KIMOFOSINTAKSIA YA | |
| LUGANDA NA KISWAHILI SANIFU | 128 |
| 5.1 Utangulizi..... | 128 |
| 5.1.1 Uwiano na utofauti wa Kanuni za mofosintaksia za ngeli nomino za Luganda na Kiswahili sanifu | 128 |
| 5.1.1.1 Kanuni ya Kimofosintaksia ya Uundaji wa Nomino na mofolojia ya uambishaji .. | 129 |
| 5.1.1.2 Kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kimofosintaksia | 137 |
| 5.1.1.3. Kanuni ya sarufi miundo..... | 144 |
| 5.1.1.4 Kanuni ya umiliki na usabaki wa viambajengo | 148 |
| 5.1.1.4.1 Kanuni ya uambishaji amilifu | 152 |
| 5.1.1.4.2 Kanuni ya upatanishi wa kisarufi wa viambishi yambwa..... | 154 |
| 5.1.1.5 Athari ya kimofosintaksia ya Kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji..... | 157 |
| 5.1.1.6 Kanuni ya kisarufi ya uwakilishi dhima na matumizi ya vibainishi na viambishi .. | 159 |
| 5.1.1.7 Kanuni ya ukuu na darajia za vijenzi vya maumbo ya maneno na utokeaji wake .. | 163 |
| 5.1.2 Uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya aina za vivumishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu | 165 |
| 5.1.2.1 Vivumishi vimilikishi | 165 |
| 5.1.2.1.1 Kanuni ya mofolojia ya uambishaji viambishi kwenye vivumishi..... | 165 |
| 5.1.2.1.2 Kanuni ya kifonolojia | 167 |
| 5.1.2.1.3 Kanuni ya umiliki na usabaki | 169 |
| 5.1.2.1.4 Kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai..... | 171 |
| 5.1.2.2 Uwiano na tofauti za kanuni za vivumishi vya a-Uganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu | 174 |
| 5.1.2.2.1 Kanuni ya kisintaksia ya umilikishi au upatanishi wa kisarufi..... | 175 |
| 5.1.2.2.2 Kanuni ya kimofolojia ya uambishaji viambishi katika mzizi wa kivumishi..... | 177 |
| 5.1.2.2.3 Kanuni ya kimofonolojia ya uambishaji wa KPM | 179 |

| | |
|---|-----|
| 5.1.2.2.4 Kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa neno kuu na maneno mengine katika tungo..... | 182 |
| 5.1.2.3 Uwiano na tofauti wa kanuni za matumizi ya Vivumishi Vionyeshi | 183 |
| 5.1.2.3.1 Kanuni ya nafsi na ngeli nomino | 184 |
| 5.1.2.3.2 Kanuni ya kimofosintaksia ya maumbo ya vivumishi vionyeshi | 186 |
| 5.1.2.3.3 Kanuni ya kimofofonolojia ya vionyeshi..... | 189 |
| 5.1.2.3.4 Kanuni ya utaratibu wa kidarajia ya utokeaji wa vionyeshi katika tungo. | 192 |
| 5.1.2.3.5 Kanuni ya umilikishi au upatanishi wa kisarufi wa Vivumishi Vionyeshi..... | 195 |
| 5.1.2.4 Uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya Vivumishi vya Sifa..... | 198 |
| 5.1.2.4.1 Kanuni za Kimofosintaksia ya vivumishi vya sifa | 198 |
| 5.1.2.4.2 Kanuni ya kofonolojia..... | 201 |
| 5.1.2.4.3 Kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa vivumishi vya sifa | 203 |
| 5.1.2.4.4 Kanuni ya upatanishi wa kisarufi..... | 205 |
| 5.1.2.5 Uwiano na tofauti ya kanuni za matumizi ya Vivumishi vya Idadi isiyodhahiri.... | 207 |
| 5.1.2.5.1 Kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa vivumishi | 207 |
| 5.1.2.5.2 Kanuni ya darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai..... | 209 |
| 5.1.2.5.3 Kanuni ya uambishaji wa vivumishi vya idadi isiyodhahiri katika tungo. | 212 |
| 5.1.3 Uwiano na tofauti ya kanuni za matumizi ya viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu Kimofosintaksia..... | 213 |
| 5.1.3.1 Kanuni ya umiliki na usabiki | 214 |
| 5.1.3.2 Kanuni ya urejeshi | 218 |
| 5.1.3.3 Kanuni ya muungano wa viwakilishi na maneno mengine | 221 |
| 5.1.3.4 Kanuni ya uambishaji | 223 |
| 5.1.3.5 Kanuni ya kimofolojia (kimaumbo) ya viwakilishi nafsi | 225 |
| 5.1.4 Uwiano na tofauti za kanuni za Vikanusho kimofosintaksia..... | 227 |
| 5.1.4.1 Uwiano na tofauti ya kanuni za Ukanushaji wa Ngeli za Luganda na Kiswahili... | 227 |
| 5.1.4.1.1 Kanuni ya uambishaji (uongezaji) vikanushi kifonolojia | 228 |
| 5.1.4.1.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa viambishi vikanushi | 230 |
| 5.1.4.1.3 Kanuni ya kimofofonolojia | 232 |
| 5.1.4.1.4 Kanuni ya upatanishi wa mofimu kanushi na KPM cha nomino..... | 233 |
| 5.1.4.1.5 Kanuni ya mofolojia ya vikanushi na utokeaji wake katika tungo | 235 |
| 5.1.4.2 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa Vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu | 237 |
| 5.1.4.2.1 Kanuni ya Kimapokezi masharti ya uongezaji vikanushi nyuma ya vivumishi ... | 237 |
| 5.1.4.2.2 Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa vikanushi katika vivumishi..... | 238 |

| | |
|---|-----|
| 5.1.4.3 Uwiano na tofauti ya kanuni za Ukanushaji wa Viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili | 240 |
| 5.1.4.3.1 Kanuni ya upatanishi nafsi..... | 240 |
| 5.1.4.3.2 Kanuni ya kifonolojia ya maumbo ya viambishi nafsi na mofu kanushi..... | 243 |
| 5.1.4.3.3 Kanuni ya maumbo wakilishi ya vikanushi | 245 |
| 5.1.4.3.4 Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa mofu kanushi | 247 |
| 5.1.4.4 Uwiano na tofauti ya ukanushaji wa Njeo na Hali katika Luganda na Kiswahili .. | 249 |
| 5.1.4.4.1 Kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi za njeo na hali..... | 249 |
| 5.1.4.4.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi katika nyakati na hali..... | 251 |
| 5.1.4.4.3 Kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji wa nyakati na njeo..... | 254 |
| 5.1.4.4.4 Kanuni ya muktadha na dhima ya utokeaji wa vikanushi..... | 256 |
| 5.1.4.4.5 Kanuni ya uambishaji/uongezaji wa mofu kanushi | 257 |
| 5.1.4.4.6 Kanuni ya udondoshaji wa mofu ya nafsi ya I na kihusishi [ni] katika kauli yakinishi | 260 |
| 5.1.4.4.7 Kanuni ya kubadilisha viwakilishi vya njeo na hali | 261 |
| 5.2 Hitimisho..... | 262 |
| SURA YA SITA: KANUNI ZA MIFANYIKO YA KIMOFOSINTAKSIA YA LUGANDA NA ATHARI ZAKE KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU | |
| 6.1 Utangulizi..... | 263 |
| 6.1.1 Mwingiliano na athari za kanuni za ngeli nomino za Luganda katika matumizi ya Kiswahili | 263 |
| 6.1.1.1 Kanuni ya Kimofosintaksia ya Uundaji wa Nomino | 264 |
| 6.1.1.2 Kanuni ya sarufi maumbo / mofolojia ya uambishaji maneno | 269 |
| 6.1.1.3 Kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofosintaksia (Kanuni ya Urejeshi) | 278 |
| 6.1.1.4. Kanuni ya sarufi miundo..... | 284 |
| 6.1.1.5 Kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji | 289 |
| 6.1.1.6 Kanuni ya uwakilishaji dhima wa matumizi ya nomino katika tungo..... | 291 |
| 6.1.2 Mwingiliano wa kanuni za vivumishi vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili ... | 294 |
| 6.1.2.1 Kanuni ya kimofolojia ya uambishaji VPM vya ngeli za nomino..... | 295 |
| 6.1.2.1.1 Athari za Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vimilikishi..... | 295 |
| 6.1.2.1.2 Athari za Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya –a unganishi | 298 |
| 6.1.2.1.3 Athari za Mwingiliano wa kanuni Katika matumizi ya vivumishi vionyeshi | 301 |

| | |
|--|-----|
| 6.1.2.1.4 Athari za Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya sifa | 302 |
| 6.1.2.1.5 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya Idadi isiyodhahiri.... | 306 |
| 6.1.2.2 Kanuni ya kifonolojia..... | 310 |
| 6.1.2.2.1 Mwingiliano wa kanuni ya kimofolojia katika matumizi ya vivumishi vimilikishi | 310 |
| 6.1.2.2.2 Mwingiliano na athari katika matumizi ya vivumishi –a unganifu | 312 |
| 6.1.2.2.3 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vionyeshi | 313 |
| 6.1.2.2.4 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya sifa | 315 |
| 6.1.2.2.5 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri.... | 316 |
| 6.1.2.3 Kanuni ya umiliki na usabaki | 318 |
| 6.1.2.3.1 Umiliki na usabaki wa nomino na vivumishi vimilikishi | 319 |
| 6.1.2.4 Kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai..... | 330 |
| 6.1.3 Mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili Sanifu..... | 333 |
| 6.1.3.1 Kanuni ya umiliki na usabiki | 333 |
| 6.1.3.2 Kanuni ya urejeshi | 337 |
| 6.1.3.3 Kanuni ya muungano wa viwakilishi nafsi na maneno mengine..... | 341 |
| 6.1.3.4 Kanuni ya uambishaji | 343 |
| 6.1.3.5 Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa viwakilishi nafsi..... | 345 |
| 6.1.4 Mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya Vikanusho vya Kiswahili Sanifu | 347 |
| 6.1.4.1 Mwingiliano wa Kanuni za Luganda katika Ukanushaji wa Ngeli nomino za Kiswahili sanifu | 347 |
| 6.1.4.1.1 Kanuni ya uambishaji (uongezaji) wa maumbo ya vikanushi kifonolojia..... | 347 |
| 6.1.4.1.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa viambishi vikanushi katika tungo | 350 |
| 6.1.4.1.3 Kanuni ya upatanishi wa mofimu kanushi na KPM cha nomino..... | 352 |
| 6.1.4.1.4 Kanuni ya mofolojia ya vikanushi na utokeaji wake katika tungo | 353 |
| 6.1.4.2 Kanuni za Ukanushaji wa Vivumishi vya Luganda sanifu | 355 |
| 6.1.4.2.1 Kanuni ya kimapokezi masharti ya uongezaji vikanushi nyuma ya vivumishi | 355 |
| 6.1.4.2.2 Kanuni ya kuongeza maumbo kanushi ya kipekee kukanusha vivumishi..... | 357 |
| 6.1.4.3 Mwingiliano wa kanuni za ukanushaji wa Viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu..... | 358 |
| 6.1.4.3.1 Kanuni ya upatanishi nafsi..... | 358 |
| 6.1.4.3.3 Kanuni ya maumbo wakilishi ya vikanushi | 363 |

| | |
|--|------------|
| 6.1.4.4 Mwingiliano wa Kanuni za ukanushaji wa Njeo na hali za Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu..... | 366 |
| 6.1.4.4.1 Kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi za njeo na hali..... | 366 |
| 6.1.4.4.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi katika nyakati na hali..... | 368 |
| 6.1.4.4.3 Kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji wa nyakati na njeo..... | 371 |
| 6.1.4.4.4 Kanuni ya uambishaji/uongezaji wa mofu kanushi | 372 |
| 6.1.4.4.5 Kanuni ya udondoshaji wa mofu kanushi katika kauli yakinishi | 374 |
| 6.2 Hitimisho..... | 375 |
| SURA YA SABA: MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO UTAFITI .. | 377 |
| 7.1 Utangulizi..... | 377 |
| 7.2 Muhtasari wa matokeo | 377 |
| 7.3.1 Kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu..... | 377 |
| 7.3.2 Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi | 378 |
| 7.3.3 Tathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu | 378 |
| 7.4 Mahitimisho | 380 |
| 7.4.1 Kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu..... | 381 |
| 7.4.2 Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi | 381 |
| 7.4.3 Tathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu | 382 |
| 7.5 Mchango wa utafiti | 384 |
| 7.6 Mapendekezo ya utafiti wa baadaye | 385 |
| 7.7 Hitimisho..... | 386 |
| MAREJELEO | 387 |
| VIAMBATISHO | 409 |

ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMI

| | |
|----------------|---|
| AB | Viambajengo vinavyohusiana kiupatanifu |
| FY | Fasili yangu |
| GWP | Government White Paper |
| KN | Kundi nomino |
| KPM | Kiambishi kipatanishi cha nomino kwa mujibu wa utafiti huu |
| KT | Kikundi tenzi |
| S | Sentensi |
| L1 | Lugha ya kwanza (Luganda) |
| L2 | Lugha ya pili (Kiswahili) |
| M1 | Mchoro wa Sheria ya vifundo |
| M2 | Mchoro wa Njia ya Vifundo |
| Mh/wah. | Mhariri/wahariri |
| N | Nomino |
| NCDC | National Curriculum Development Centre |
| NML | Nadharia ya Mwingiliano Lugha |
| NPHC | National Population and Housing Census |
| T | Kitenzi |
| VPM | Viambishi vipatanishi vya nomino kwa mujibu wa utafiti huu |
| X | Kwa mujibu wa Chomsky (1970) Alama ya (X) husimamia kichwa au neno kuu katika kirai au sentensi |
| XY | Viambajengo vya sentensi au kirai |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TUKI | Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili |
| UNEB | Uganda National Examination Board |
| UWAKI | Chama cha Walimu wa Kiswahili, Uganda |

MAELEZO YA ISTILAHU

Anafora: Ni urejeleo nyuma wa mofu yoyote kwenye KN (kirejelewa) linalotangulia kirejeleo. Ni kijenzi cha kisarufi kinachohitaji kufungamwa kwa kisabiki chake ili maana yake ifasirike.

Kanuni: Sheria au taratibu za matumizi ya lugha

Kategoria ya kisarufi: Ni kundi la maneno lenye sifa za kisarufi za kimofolojia au kisintaksia zinazobeba dhima moja katika tungo.

Kifundo kikuu: Ni kategoria ya umilikifu, yaani kifundo kilicho juu ya vifundo vingine (*maximal projection*).

Kifundo: Kifundo huwakilisha mahali ambapo viambajengo sisizi hutengana. Hujitokeza hasa katika kielelezo matawi

Kipashio: Kipengele cha kisarufi chenye sifa fulani ya lugha

Kirejelewa Kundi: Nomino iliyo katika sehemu ya kiima au hutangulia anafora na hurejelewa na anafora (kirejeleo) hiyo.

Kisabiki: Kipashio kinachorejelewa na kipashio kingine ili kipate maana.

Kiwango: Ni mgawanyo wa lugha katika mifumo midogo midogo inayoweza kujitegemea wakati wa kufanyiwa uchambuzi, kama vile: katika mgao wa fonolojia, sintaksia na semantiki.

Luganda: Pia Kiganda, tafsiri ya Kiswahili ya 'Luganda'. Utafiti huu ulitumia Luganda ambayo ni L1

Lugha kadirifu: Ni lugha potovu anayotumia mwanafunzi anapojaribu kuizungumza au kuiandika lugha lengwa.

Lugha ya kwanza: Lugha ya mama. Lugha aliyojifunza mtu katika mazingira ya nyumbani kabla ya L2 (Gass and Selinker, 2008). Lugha ya kwanza hapa ikiwa ni Luganda na L2 ikiwa ni Kiswahili.

Lugha ya pili: Lugha anayojifunza mtu baada ya upataji wa lugha mama, ambayo ni Kiswahili katika kazi hii.

Mawanda ya Umilikifu: Ni kategoria ya umilikifu inayohusiana na vipashio vya kianafora kuwa katika nafasi mahsusi katika sentensi ndipo kuwepo urejeleo enza baina yao.

Mofosintaksia: Ni uhusiano wa vipashio vya lugha vinavyoingiliana kimofolojia na kisintaksia. Ni vipashio vipashio vya mofolojia ambavyo uamilifu wake hubainika katika sintaksia kuonyesha uhusiano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo kudhihirisha dhima za kisarufi za umoja na wingi, upatanishi wa kisarufi, uakinishi, mabadiliko ya mofimu wakilishi ya sifa za kisarufi nk.

Mwingiliano wa lugha: Ni ile hali ya kuwepo kwa makutano ya lugha mbapo jamii lugha yenye nguvu huathiri jamii lugha ambayo ina nguvu ndogo, na mwingiliano wa lugha zenye mtagusano hujitokeza katika nyanja anuwai za kiisimu. Mwingiliano wa vipashio vya kimofosintaksia vya L1 (Luganda) katika L2 (Kiswahili).

Mzungumzaji asilia: Ni mwanafunzi wa kidato cha sita anayejifunza Kiswahili kama L2, mzaliwa na mkaazi wa eneo la Kampala, mwenye uamilifu wa kutumia Luganda kama L1, anayejitambulisha kutoka katika kabila la Wabaganda, anayedhihirisha sifa za kitaipolojia katika matumizi ya Luganda.

Sarufi bia: Ni sifa, vigezo na kanuni sawia ambazo lugha zote hudhihirisha kuonyesha kufanana na kutofautiana baina yake.

Sarufi: Mfumo unaosisitiza ujuzi wa matumizi ya kanuni zilizokubalika na wazawa wa lugha fulani. Kwa mujibu wa utafiti huu ni mfumo wa kanuni za Luganda na Kiswahili sanifu zinazomwezesha mtumiaji wa lugha hizi kutunga sentensi zisizo na kikomo ambazo hukubalika na wazawa wa lugha hizi vyema.

Sintaksia: Ni tawi la isimu linalojishughulisha na uchanganuzi, mpangilio wa kidaraja unaozingatia kanuni maalumu wa kuonyesha uhusiano wa vipashio vya kisarufi kuunda tungo na sentensi zenye maana katika lugha.

Ufungami: Kanuni zinazotawala uhusiano baina ya pronomino na visabiki vyake.

Umilisi: Uwezo au ujuzi wa lugha alionao mwanafunzi unaomwezesha kuwasiliana

Usanifu wa lugha: Uzungumzaji na uandikaji wa lugha bila makosa. (TY)

Vigezo: Sifa bayana zinazotofautisha sarufi za lugha mbili au zaidi.

Vipashio vya kimofosintaksia: Ni vipengele vya lugha ambavyo maumbo yake yote hudhihirika katika muundo wa sentensi kuwakilisha sifa za kisarufi zinazoonyesha uhusiano wa mofolojia na sintaksia

ORODH YA MAJEDWALI

| | |
|---|-----|
| Jedwali 4.1: Uwiano na tofauti za ngeli za nomino za Luganda na Kiswahili mkabala wa mfumo wa kimofolojia na kisintaksia..... | 71 |
| Jedwali 4.2: Kufanana na kutofautiana kwa viambishi vya ngeli za Luganda na Kiswahili kimofolojia na Kisintaksia..... | 76 |
| Jedwali 4.3: Uwiano na tofauti za uainishaji wa ngeli za Luganda na Kiswahili Kisintaksia..... | 78 |
| Jedwali 4.4: Uwiano na tofauti za uainishaji wa ngeli za Luganda na Kiswahili kijozi kimofolojia..... | 81 |
| Jedwali 4.5: Kufanana na kutaofautiana mkabala wa mfumo wa ngeli kijozi..... | 84 |
| Jedwali 4.6: Uwiano na tofauti za vivumishi vimilikishi kati ya Luganda na Kiswahili..... | 88 |
| Jedwali 4.7: Tofauti za vivumishi vimilikishi vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia..... | 89 |
| Jedwali 4.8: Viambishi vipatanishi vya ngeli, vipatanishi, vimilikishi na vimilikishi nafsi..... | 92 |
| Jedwali 4.9: Uwiano na tofauti ya vivumishi vipatanishi vya –a unganifu vya Luganda na Kiswahili..... | 95 |
| Jedwali 4.10: Uwiano na tofauti za viwakilishi vya vivumishi vionyeshi vya Luganda na Kiswahili..... | 98 |
| Jedwali 4.11: Uwiano na tofauti ya viambishi awali vya sifa vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia..... | 102 |
| Jedwali 4.12: Uwiano na tofauti ya vipatanishi na mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu..... | 106 |
| Jedwali 4.13: Uwiano na Tofauti za Viwakilishi vya Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia..... | 110 |
| Jedwali 4.14: Uwiano na tofauti ya viwakilishi nafsi huru, funge na yambwa vya Luganda na Kiswahili..... | 111 |
| Jedwali 4.15: Uwiano na tofauti za vikanushi vya ngeli vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia..... | 113 |
| Jedwali 4.16: Uwiano na tofauti za Viwakilishi vikanushi vipatanishi vya nafsi vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia..... | 119 |
| Jedwali 4.17: Vikanushi vya viwakilishi nyakati katika Kiswahili kimofosintaksia..... | 122 |
| Jedwali 4.18: Njeo na hali kimofosintaksia pamoja na maumbo kanushi katika Luganda na Kiswahili Sanifu..... | 124 |
| Jedwali 5.1: Kanuni ambazo zimejitokeza katika sentensi (a-c)..... | 170 |
| Jedwali 5.2: Kanuni za kimofonolojia za kivumishi cha [-a] unganifu za Luganda..... | 181 |

| | |
|---|-----|
| Jedwali 5.3: Kanuni ya kifonolojia ya vivumishi vionyeshi rejeshi katika Luganda..... | 191 |
| Jedwali 5.4: Kanuni ya kifonolojia ya vivumishi vionyeshi rejeshi vya Kiswahili sanifu... | 192 |
| Jedwali 5.5 Uwiano na tofauti za viwakilishi vipatanishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu..... | 217 |
| Jedwali 5.6 : Viwakilishi vya nafsi na ngeli rejeshi..... | 218 |
| Jedwali 5.7: Kanuni ya upatanshi wa kisarufi wa viambishi vikanushi baina ya Luganda na Kiswahili..... | 241 |
| Jedwali 6.1: Viambishi awali vya ngeli vya Luganda vilivyoathiri muundo wa nomino za Kiswahili sanifu na maneno mengine katika tungo..... | 266 |
| Jedwali 6.2: Maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya ngeli nomino na mwingiliano wake..... | 271 |
| Jedwali 6.3: Viwakilishi vya nafsi na ngeli rejeshi..... | 338 |
| Jedwali 6.4a: Maumbo ya wakati uliopita ya Kiswahili sanifu..... | 364 |
| Jedwali 6.4b: Maumbo ya ukanushaji vya wakati uliopo vya Kiswahili sanifu..... | 365 |
| Jedwali 6.4c: Maumbo ya vikanushi vya hali timilifu [-me-]..... | 365 |
| Jedwali 6.4d: Maumbo ya vikanusho vya wakati ujao..... | 365 |

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti.

1.1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Usuli wa suala la utafiti umehusisha masuala anuwai ya kutoa msingi wa kudhihirisha pengo na suala la kutafitiwa. Umegawanywa katika sehemu msingi zinazohusisha athari za L1 kwa L2, ukieleza usuli wa kihistoria wa mada, ufasiri wa dhana anuwai za athari za mwingiliano, mofosintaksia, maelezo kuhusu Luganda na Kiswahili na suala la maingiliano ya L1 kwa L2.

1.1.1.1 Athari za mwingiliano wa lugha ya kwanza kwa lugha ya Pili

Lugha ya pili huonekana kuathiriwa na vipengele vya lugha kwa namna mbalimbali. Thompson na Kaufman (2001) na Siemund (2008), wanafafanua mwingiliano wa lugha kuwa matumizi ya zaidi ya lugha moja katika sehemu moja na katika wakati mmoja. Aidha, wanaendelea kueleza kuwa, lugha ambazo huathiriana kiisimu ni zile lugha ambazo zipo katika makutano ya karibu kwa kipindi cha zaidi ya miaka mia moja hadi mia mbili. Walibainisha aina za athari ambazo hujitokeza katika kuathiriana huku na kueleza kuwa, athari huwa hazijitokezi katika maneno tu bali katika vipashio vyote vya kimuundo vya kiisimu vya mfumo wa sauti, muundo wa maneno, muundo wa sentensi na semantiki ya kileksika.

Athari za lugha ya kwanza (L1) kwa lugha ya pili (L2) hutokana na maingiliano ya vipashio na mifumo anuwai vya kiisimu, viwango tofauti vya upataji wa umilisi wa L2 unaokabiliwa, uhamishaji hasi wa vipashio na kanuni za matumizi ya vipashio vya kiisimu kutoka kwa lugha mbalimbali za kwanza katika L2. Athari hizi hutokana na maingiliano ya lugha asili katika matumizi kutokana na kufanana na kutofautiana kwa kanuni na miundo ya vipashio vya kiisimu vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Matokeo ya utafiti juu ya mwingiliano wa lugha yanadhihirisha kuwa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili huathiriwa na L1, hasa inapotokea kwamba mfumo wa lugha ya asili hutofautiana na ule wa Kiswahili sanifu (Odeo & Maina, 2008; Mulei, 2014; Ontieri, 2016; Oduor, Inyani na Kobia, 2017)

Corder (1967:1981) akizungumzia mwingiliano wa lugha na upataji wa lugha ya pili anatambua kuwa, makosa katika lugha ya pili yanaonyesha hali fulani ya matatizo aliyo nayo mzungumzaji katika L2 kutokana na kuhamisha sifa fulani za L1 hadi kwenye L2. Pia, mwingiliano wa lugha huweza kujitokeza kutokana na uhamishaji wa vipashio na kanuni za kisarufi za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Uhamishaji huu hutokana na tajiriba au umilisi wa vipashio na kanuni za lugha alizonazo mjifunzaji lugha baina ya L1 na L2. Uhamishaji huu ni mikakati ya urahisishaji wa matumizi ya L2 unaofanywa na mmilisi wa L1 (Richards, 1974; Ontieri, 2016). Kwa hiyo, ufafanuzi wa sifa za vipashio na uchanganuzi wa kanuni za matumizi ya vipashio vya kisarufi vya lugha asili na Kiswahili sanifu hasa baina ya lugha ambazo zimekuwa na mtagusano wa muda mrefu na ambazo hutokana na nasaba moja kama Luganda na Kiswahili sanifu ni muhimu katika kutathimini mwingiliano na athari katika matumizi ya L2. Uchanganuzi huu huweka bayana mikakati ya urahisishaji wa matumizi ya lugha, na ugumu wa matumizi ya lugha unaotokana na mwathiriano wa mifumo ya lugha mbili ambazo huweza kuwa na uwiano na tofauti za sifa za vipashio vya kisarufi ambayo hujitokeza katika matumizi kimofolojia na kisintaksia.

Nyanda (2015), anaeleza kuwa mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti hutokana na ukaribu ama mwingiliano baina ya wanajamii na lugha. Kwa mtazamo wake, wazungumzaji wa lugha zilizo karibu wazungumzapo huwa wanadhihirisha tofauti za kiisimu katika viwango vya kiisimu vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Mara nyingi wanaisimu hueleza tu kuwa lugha za Kibantu ambazo zimekuwa na mtagusano wa karibu wa muda mrefu huingiliana na kuathiriana. Hata hivyo, kiwango na taathira ya mwingiliano wa lugha za Kibantu kama ulivyo katika Luganda na Kiswahili haujawekwa bayana. Uchunguzi wa mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ulifanywa kwa ajili ya kutathimini mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti zenye nasaba moja kutegemea vipashio na kanuni za kimofosintaksia kubaini madai hayo.

1.1.1.2 Dhana ya mofosintaksia ya lugha

Mofosintaksia ni mwingiliano wa vipashio vya mofolojia na sintaksia katika muundo wa lugha (Collins & White, 2015). Kulingana na Crystal (2011) na Egara (2016), mofosintaksia ni istilahi ya kiisimu inayorejelea kategoria za kisarufi zinazohusisha misingi ya kiisimu ya mofolojia na sintaksia ikichunguza uhusiano uliopo kati ya vipashio vya mofolojia na sintaksia. Mofosintaksia huchanganua kategoria za kisarufi ambazo zinahusisha sifa za kiisimu za kimofolojia na kisintaksia. Sintaksia ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na

uchanganuzi wa utaratibu na kanuni za mahusiano yaliyopo baina ya maneno katika usemaji wa lugha yoyote (Kihore, Massamba, & Msanjila, 2001). Habwe & Karanja (2004) wanaifasili sintaksia kuwa taaluma inayohusika na uchambuzi wa sentensi na viambajengo vyake kama vile virai na vishazi.

Kwa upande mwingine, Collins & White (2015) wanasema kwamba, mofosintaksia ni mwingiliano wa mofolojia na sintaksia. Ni dhahiri kwamba uelewaji wa miundo ya kisintaksia hutokana na kuelewa viambajengo mbalimbali vya kimofolojia ambavyo hujenga tawi la isimu la sintaksia. Kwa hiyo uchunguzi wa kategoria za kisarufi za taaluma ya mofolojia ni msingi wa miundo na kanuni za kisintaksia. Hivyo basi utafiti huu ulichukulia kuwa mofosintaksia ni dhana ya isimu inayorejelea kategoria za kisarufi ambazo zina sifa za kimofolojia na kisintaksia. Kwa hiyo, utafiti huu ulichunguza na kueleza mifanyiko ya mofosintaksia inayotokana na kategoria mbalimbali za kimofosintaksia zinazoweza kusababisha athari za mwingiliano kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Hali hii inatokana na kuwa, ingawa viwango hivyo vya kiisimu vinatofautiana kiisimu, vinategemeana kuunda kategoria ya sifa za kisarufi katika lugha na matumizi yake. Pia hali hii inatokana na uhusiano wa miundo ya vipashio vya mofolojia kuungana na vipashio vya sintaksia kuunda kipengele cha mofosintaksia ambapo kipengele kikuu humiliki na kutawala vipashio vingine katika tungo.

Mwingiliano wa kimofosintaksia hutokana na hali ya lugha zinazoingiliana kutofautiana kimuundo na kikanuni. Kwa kurejelea fasili ya Collins na White (Washatajwa), utafiti huu ulijikita katika kuchanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili kutathimini athari za ukuruba wa lugha hizi ambazo ni za Kibantu, ili kuweka bayana jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali hii inatokana na kuwa vipashio vya mofolojia hutangamana na sintaksia na kuibua michakato inayoweza kuchanganuliwa katika kipengele cha mofosintaksia kuonyesha uhusiano uliopo wa muungano wa vipashio vya mofolojia na sintaksia unaoweza kuchanganuliwa kupitia kwa kanuni husika ya kipashio kikuu kutawala na kumiliki vipashio vingine katika tungo.

Utafiti huu ulichanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutokana na umilisi wa vipashio na kanuni za lugha alizonazo mtumiaji baina ya L1 na L2 na kutathimini mwingiliano na athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali hii inatokana na kuwa kila lugha huwa na miundo ya vipashio na kanuni ambazo

zikikiukwa usahihi wa matumizi ya lugha hupotoshwa na kujenga lugha isiyo sanifu. Utafiti huu unatokana na tafiti za awali ambazo zilidhihirisha kuwa uwiano na tofauti za matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu kimofosintaksia husababisha mwingiliano katika matumizi ya Kiswahili sanifu (Chepkwony, 2012; Barno, 2013; Ntawiyanga, 2015; Chebet, 2016; Egara, 2016; Oduor, Inyani & Kobia, 2017).

Barno (2013), anaeleza kuwa mofosintaksia ni vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hubainika katika sintaksia kama vile, njeo, hali, ukanushi na kadhalika ambavyo kwayo huathiri ufasiri wa sentensi. Kwa mujibu wa utafiti huu, mofosintaksia ni dhana ya isimu inayochanganua kategoria za kisarufi ambazo zinahusisha sifa za vipashio na kanuni za kiisimu za kimofolojia na kisintaksia. Mofolojia hushughulikia vipashio vya lugha katika kuunda maneno. Kipashio cha msingi cha mofolojia ni mofimu ambayo hutumika kuundia darajia za sintaksia. Mofimu hufanya kazi ya kutambulisha idadi ya umoja na wingi, nyakati, nafsi, hali, ukanushi na upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na maneno mengine katika tungo. Sintaksia ina uhusiano na mofolojia kwa sababu vipashio vya mofolojia ndivyo vinavyosaidia katika uundaji wa vipashio vya kiisimu vya sintaksia. Kipashio kikuu cha msingi katika sintaksia ni neno. Vipashio vya mofolojia ndivyo vinavyounda neno (Rubanza, 1999; Philipo na Kuyenga 2017).

Mwingiliano wa mofosintaksia ni ile hali ya kanuni na miundo, baina ya L1 na L2 kushirikisha vipengele vya kisarufi vya mofolojia na sintaksia katika matumizi kutokana na athari kuu za mtagusano, ukuruba na tofauti za kimuundo ama kitaipolojia. Utafiti huu ulichochea na dhana ya mwingiliano wa mofosintaksia kati ya lugha mbili za Kibantu ambazo zimekuwa katika makutano na ukinzani wa miaka mingi kuanzia miaka ya 1844, na ambayo ina ukuruba wa sifa za kiisimu kimuundo (Guthrie, 1967-71; Gérard, 1981; Mukama, 1995; Katamba, 2003; Mukuthuria, 2004 na Jerro, 2018). Utafiti huu ulifafanua vipashio vya kiisimu vya mofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni na miundo ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia ili kutathimini mwingiliano na athari za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Hii ilitokana na kuwa kanuni za mfuatano na mpangilio wa vipashio vya kimofosintaksia ukizingatiwa, matokeo ya matumizi sahihi ya lugha hudhihirika na usipozingatiwa, kanuni ya matumizi ya vipashio hukiukwa na kujenga miundo ya lugha isiyo sahihi, ambayo hudhihirisha matatizo ya kisarufi inayotokana na fonolojia, mofolojia na sintaksia (Onyango 1997 na Mutugu 2001).

1.1.1.3 Luganda na Kiswahili sanifu

Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za Kibantu za familia ya Niger – Kordofanian kutoka katika jamii lugha za Kibantu za Benue Kongo. Luganda ni lugha ya Kibantu ambayo inazungumzwa zaidi katika eneo la kusini na kati, nchini Uganda. Lugha hii hufunzwa na kuzungumzwa na jamii ya Wabaganda wenye idadi ya wazungumzaji asili takribani milioni nne. Luganda ni lugha asili ya ukoo wa njoro-Ganda iliyoainishwa katika kundi la J nambari JE15 (Guthrie 1948; Katamba 2006; Lewis 2009; Van der Wal & Namyalo, 2016). Luganda ina lahaja kuu sita za lahaja ya Kampala, Olukooki/ Olunabuddu, Ludiope, Lussese, Luvuma na Luruli. Miongoni mwa lahaja hizi, lahaja ya Kampala ni lahaja ambayo imekubalika kutumika kama lahaja sanifu kulingana na kamati ya Lugha ya Luganda, mwaka 1947 (Ssekiryango, 2006; Baertlein & Ssekitto, 2014).

Ufafanuzi wa vipashio na kanuni za mofosintaksia za lahaja sanifu ya Kampala ndio iliozingatiwa katika utafiti huu. Luganda sanifu ilituuliwa kwa sababu inafundishwa na kutumika katika mfumo wa elimu kuanzia shule za awali za madarasa ya chini ya darasa la kwanza hadi tatu na kutahiniwa katika viwango vya kidato cha nne na sita. Lahaja hii hutumika katika vyombo vya habari na maandishi anuwai ikiwemo vitabu vya sarufi, fasihi na magazeti. Lahaja hii hutumika vilevile katika maeneo anuwai ya eneo la kati (Katamba, 2006; Namugala, 2014; Kiyinikibi, 2021) Aidha, Luganda ni lugha ambayo inabishana na lugha za Kiingereza na Kiswahili katika matumizi yake kiisimu (Hyman & Katamba, 2001; Katamba, 2006; Lewis, 2009; Kiyinikibi, 2021). Wananchi wengi nchini Uganda hutumia lugha hizi tatu kutegemea umilisi wao na hata kubadili msimbo na kuchanganya lugha hizi wanapowasiliana.

Kwa upande mwingine, Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye asili ya pwani ya Afrika Mashariki ambayo inafundishwa na kuzungumzwa katika nchi za Afrika Mashariki na Afrika ya kati kama lingua franca. Lugha hii imeainishwa katika kundi kubwa la Kibantu la ukanda G nambari ya G42 (Ashton, 1954; Guthrie 1948; Greenberg, 1963; Guthrie, 1971; Kihore, Massamba, na Msanjila, 2001; Kihore na Massamba, 2003; Lusesa, 2014; Otiende, 2013). Hivi sasa, Kiswahili ni lugha rasmi ya pili ya Uganda. Vile vile Kiswahili kinafundishwa kama somo la lazima katika kidato cha kwanza na pili katika shule za upili na kutahiniwa katika kidato cha nne na sita (NCDC, 2019). Kiswahili sanifu kiliteuliwa kutumika katika utafiti huu kwa sababu ndiyo lugha inayoathirika na lugha asili kutokana na uwiano na tofauti za vipashio na kanuni za kimofosintaksia baina ya L1 na L2. Ili kutathimini mwingiliano na

athari za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, vipashio na kanuni za lugha mbili zililinganishwa na kulinganuliwa, kutambua uwiano na tofauti za vipashio na kanuni, kwa ajili ya na kutathimini jinsi mofosintaksia ya L1 ambayo ni Luganda inavyoathiri mofosintaksia ya Kiswahili sanifu ambayo ni L2. Luganda ni lugha ya mzawa (lugha ya mama) inayotumika na mzungumzaji/mwanafunzi tangu utotoni akiwa nyumbani na katika mazingira yake. Kiswahili ni lugha ya pili anayojifunza na kutumia mwanafunzi katika mazingira yake kando na lugha ya kigeni

Uainishaji wa Luganda na Kiswahili sanifu unadhihirisha kuwa lugha hizi zinawiana na kutofautiana kiisimu. Uwiano ni kuwa lugha zote ni za nasaba moja. Utofauti ni kuwa lugha hizi zimewekwa katika makundi tofauti ambapo Luganda inapatikana katika kundi la J na Kiswahili kuwekwa katika kundi la G. Uainishaji huu unadhihirisha kuwa, licha ya kuwa lugha hizi ni za nasaba moja, zina sifa za kiisimu ambazo zinafanana na kutofautiana. Hii ina maana kuwa lugha kuwa katika nasaba moja haifanyi lugha hiyo kukosa kuwa na sifa maalumu zinazoweza kuipambanua na kuitambulisha kama lugha mahsusi yenye mifumo ya kipekee ya kisarufi.

1.1.1.4 Uwiano na Tofauti za Lugha za nasaba moja

Uwiano na tofauti za kiisimu za lugha za nasaba moja unaweza kusababisha mwingiliano na athari katika matumizi baina ya L1 na L2. Aidha, kulingana na Hyman na Katamba (2001), Jerro (2018), Katamba (2006) na Lewis (2009), Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha mbili tofauti zenye mifumo ya kipekee ya kiisimu ya fonolojia, mofolojia na sintaksia zinazotofautiana hata ingawa zote ni lugha za Kibantu. Upekee wa lugha hizi ndio unaozitambulisha na kuzitofautisha lugha hizi kiisimu hasa katika matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu. Hivyo ni muhimu kutambua data za uchanganuzi wa vipashio, miundo na kanuni za mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili ili kuonyesha kufanana na kutofautiana kwa lugha pamoja na kutathimini mwingiliano na athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Jjingo & Visser (2017) wanaeleza kuwa, licha ya Kiswahili kupewa hadhi ya kuwa lugha rasmi ya pili kulingana na katiba ya Uganda ya mwaka wa 2005, mchakato wa ufundishaji shuleni unaanzia katika kidato cha kwanza, mchakato ambao umesababisha matumizi yake kupatwa na changamoto za mtagusano wa L1 katika matumizi yake miongoni mwazo ikiwa mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulichunguza mwingiliano wa vipashio na kanuni kutoka katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi

ili kutathimini mwingiliano na athari za vipashio na kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Mwingiliano wa lugha ni ile hali ya kuwepo kwa makutano ya lugha mbapo jamii lugha yenye nguvu huathiri jamii lugha ambayo ina nguvu ndogo (Selinker, 1972). Mwingiliano wa lugha zenye mtagusano hujitokeza katika nyanja anuwai za kiisimu katika viwango anuwai. Katika muktadha huu, Luganda ni mojawapo wa lugha inayotumika zaidi na wanafunzi wakiwa nyumbani, huku Kiswahili kikifundishwa shuleni na kutumika na wanafunzi katika shughuli za ujifunzaji pamoja na mawasiliano shuleni (Mulei, 2014; Mulei, Amukowa & Ambuyo, 2021). Maingiliano ya lugha hutegemea sana uhusiano wa mofolojia na sintaksia ambapo maumbo ya kimofolojia huungana na kumiliki vipashio vya kisintakisa kutegemea kanuni na miundo ya lugha husika (Mbaabu, 1995: 2007). Hivyo basi, mofosintaksia inahusu kuchunguza vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hubainika katika sintaksia ambao utafiti huu ulishughulikia.

Luganda sanifu na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja (Gibson, Mapunda, Marten & Taji, 2019). Hata hivyo, ni lugha mbili tofauti zenye sifa za vipashio na kanuni za kipekee ambazo zinastahili kuwekwa wazi. Uchanganuzi huu ni msingi wa kutathimini mwingiliano na athari katika matumizi ya vipashio na kanuni za kimofosintaksia kutoka lugha moja hadi nyingine. Hali hii inatokana na kuwa, matokeo ya ufafanuzi wa uwiano na tofauti ya vipashio na uchanganuzi wa kanuni za kisiimu ya kimofolojia ya Luganda na Kiswahili, unavyoshirikiana na vipashio vya kisintaksia katika tungo kudhihirisha uhusiano wa neno kuu kumiliki na kutawala meneno mengine katika tungo, na jinsi uhusiano huo unavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, hujawekwa bayana kuonyesha jinsi mofosintaksia ya Luganda inavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti ambapo kila moja hushirikisha vipashio vyake na kanuni zake za kimofosintaksia katika matumizi, kuonyesha uhusiano wa vipashio vya mofolojia kumiliki na kutawala vipashio vya kisintaksia (Hyman & Katamba, 2001:2006). Uchunguzi wa uwiano na tofauti pamoja na muundo wa kisarufi wa mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu ni nguzo msingi katika kutathimini mwingiliano na athari za kiisimu baina ya L1 na L2 katika matumizi. Hii ni kwa sababu, mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti ambazo ni jirani husababisha mwathiriano wa lugha hizo kutokana na kuwa kila lugha huchukua baadhi ya vipashio na kanuni kutoka lugha nyingine na kuingiza katika lugha yake. Aidha, mwingiliano wa lugha unapojitokeza, lugha inayoathiri na inayoathiriwa

hupokea athari katika miundo yake katika viwango vya kiisimu anuwai (Mukuthuria, 2004 na Nyanda, 2015).

Miundo na kanuni za vipashio vya kiisimu vya L1 na L2 vinapofanana, matumizi ya L2 hurahisishwa. Hii ni kwa sababu wanafunzi wana uwezo wa kuhamisha kanuni na miundo ya vipashio vya kiisimu vya L1 katika matumizi ya L2 (Kariuki, 2012). Kwa upande mwingine, tofauti za kanuni na miundo ya lugha baina ya L1 na L2 husababisha ugumu katika matumizi ya L2. Hali hii inatokana na kukiuka kanuni za L2 hasa mwanafunzi anapohamisha kanuni na miundo ya vipashio vya kiisimu vya L1 katika maandishi na mazungumzo ya L2 (Ellis Rod & Shintani Natsuko, 2013).

Ugumu katika matumizi ya kaida za lugha ni kikwazo ambacho kila mtumiaji lugha hupitia. Vikwazo hivi husababisha matumizi potovu ya lugha ambayo hukiuka kanuni na miundo ya vipashio vya kiisimu vya lugha baina ya L1 na L2. Mtazamo mwafaka wa kuchunguza athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya lugha ni ule wa kufafanua vipashio na kanuni za matumizi ya lugha kama yanavyotolewa na mtumiaji lugha. Hii ni kwa sababu kanuni na vigezo vya sarufi ya lugha hutawala uhusiano wa kategoria za maneno katika muundo na uamilifu wa sentensi (Kariuki, 2012). Ukuruba na mtagusano huu umejitokeza katika matumizi ya lugha hizi katika maeneo ya Kampala hasa shuleni ambako Luganda na Kiswahili sanifu hutumika (Mukama, 1995). Aidha, lugha zinapotumika katika eneo la ujirani kwa muda mrefu hazina budi kuathiriana kiisimu (Thompson na Kaufman, 2001). Kutokana na mtagusano na ukuruba huu, kulihitajika ufafanuzi wa vipashio na uchanganuzi wa kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia, kuonyesha mfanano na tofauti baina ya lugha husika (L1 na L2), ili kuweza kutathimini mwingiliano na athari zinazojitokeza katika matumizi. Uchunguzi huu wa mwingiliano wa vipashio na kanuni za kiisimu za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ni mkakati wa kuzuia changamoto za mwathiriano wa lugha, umilisi wa kukuza na kuendeleza matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu nchini Uganda.

Utafiti huu ulifanywa katika mazingira ya shuleni eneo ambamo matumizi ya lugha huzingatia kanuni na miundo ya vipashio vya kiisimu. Kanuni na miundo ndio nguzo ya kisarufi inayosisitizwa na kulazimishwa kupokelewa na watumiaji lugha. Kiswahili kinachofundishwa shuleni ni kile kinachozingatia kanuni na miundo ya matumizi ya vipashio vya kisarufi kiusahihi (Egara, 2016). Ukiukaji wa matumizi ya kanuni na miundo hizo husababisha adabu hasa wakati wa kuwatahini wanafunzi katika mifumo ya elimu (Philipo & Kuyenga, 2017). Ukiukaji wa kanuni hupotosha maumbo ya kimofolojia ya maneno pamoja

na matumizi yake katika tungo. Upotovu huu ndio unajenga misingi ya mwingiliano au kuathiriana kwa lugha baina ya L1 na L2.

Wanafunzi ambao L1 Luganda hujifunza Kiswahili sanifu kilicho na vipashio vyake na kanuni zake katika matumizi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita. Kanuni za matumizi ya vipashio vya maumbo ya kimofolojia ya kumiliki na kutawala vipashio vya kisintaksia huzingatiwa katika matumizi. Mwanafunzi ambaye amefundishwa juu ya vipashio na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili anatarajiwa kuonyesha umilisi wake katika maandishi na mazungumzo anapotumia Kiswahili sanifu. Ukiukaji wa matumizi ya vipashio na kanuni huathiri usahihi katika matumizi. Hii ni kwa sababu vipashio na kanuni hizi ndizo zinazotumika katika upimaji wa umilisi wa wanafunzi katika mfumo wa kielimu.

Matokeo ya matumizi ya Kiswahili kinachozungumzwa na kuandikwa na wanafunzi shuleni nchini Uganda kimeripotiwa kuwa kibovu kisichozingatia matumizi sahihi ya kanuni za vipashio vya kiisimu ambapo lugha asili huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu (Chomi 2016; Mulei 2014). Aidha, mchakato wa ujifunzaji na upataji wa L2 isipokuwa L1, hukumbwa na changamoto mbalimbali za kiisimu zinazotokana na umilisi wa kanuni na vipashio vya kiisimu vya L1 miongoni mwazo ikiwa ni mwingiliano wa L1 katika matumizi ya L2 (Kuhl, 2004; Chebet, 2016; Ontieri 2016)

Tafiti za awali zilidhihirisha kuwa uwiano na tofauti za matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu kimofosintaksia husababisha mwingiliano katika matumizi ya Kiswahili sanifu (Chepkwony, (2012); Ntawiyanga, 2015; Chebet, 2016; Egara, 2016; Oduor na Wenzake, 2017). Utafiti ulifafanua; uwiano na tofauti za matumizi ya vipashio, kuchanganua kanuni za kimofosintaksia kama kipengele cha kiisimu cha Luganda kama lugha asili katika matumizi ya Kiswahili sanifu na kutathimini mwingiliano wa vipashio na kanuni za mofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu nchini Uganda hujabainika.

Mohamed (1988) na Ntawiyanga (2015) wanaeleza kuwa kipengele cha mofosintaksia ndicho kiini cha lugha yoyote ile na kuwa vipashio vingine vya sarufi huingiliana nacho na kukitegemea kwa kiwango kikubwa. Aidha, wote wanafafanua kuwa maingiliano baina ya vipashio vya lugha hutegemea kwa kiasi kikubwa mofolojia na sintaksia. Kulingana na maoni yao, mofosintaksia ni muhimu katika kuchunguza vipashio vya kimofolojia vya maneno na

kuonyesha jinsi ambavyo vinaweza kuungana kwa ajili ya kuunda kipashio kikubwa zaidi ambacho ni sentensi (Sintaksia). Muungano huu wa vipashio huweza kuonyesha uhusiano wa kipashio kikuu katika tungo kutawala na kumiliki vipashio vingine katika tungo. Kwa hivyo, uchanganuzi wa mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ulitekelezwa kwa ajili ya kuweka sura kamili ya ukiukaji wa matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili ambao L1 ni Luganda, nchini Uganda. Kwa hiyo, utafiti huu ulichanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kwa kufafanua uwiano na tofauti za vipashio, kuchanganua mifanyiko ya kanuni za matumizi ya vipashio vya Luganda na Kiswahili na kudhihirisha jinsi mofosintaksia ya Luganda inavyoingiliana na kuathiri Kiswahili kinachozungumzwa na kuandikwa na wanafunzi wa shule za upili ambao L1 ni Luganda nchini Uganda. Utathimini huu ulitokana na kuwa mifumo na miundo ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu ni ya kipekee ambayo huzitambulisha na kuzitofautisha lugha hizi kama lugha mbili tofauti zinazotoka katika nasaba moja ya lugha za Kibantu. Uchanganuzi ulizingatia mifumo ya kielimu inayofafanua na kuchanganua sheria za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu. Sheria hizi ni za kisarufi ambazo ni kubalifu na zilizowekwa kupima umilisi wa matumizi sahihi ya lugha katika viwango vyote. Uchanganuzi wa uhusiano wa kanuni za mfuatano na mpangilio wa vipashio vya mofolojia kuungana kumiliki na kutawala viambajengo vya sintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu ulizingatiwa.

1.2 Suala la utafiti

Ukuruba na tofauti baina ya lugha mbili tofauti zenye mtagusano wa muda mrefu husababisha mwathiriano wa lugha husika kuchukua baadhi ya sifa za vipashio vya kiisimu vya kimofosintaksia kutoka lugha nyingine na kuingiza katika matumizi ya lugha hiyo. Ukuruba huu unaonekana baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye kanuni na miundo ya kiisimu ambayo ina ukuruba na lugha nyinginezo za Kibantu kama ilivyo Luganda. Kanuni hizi ni zile zinazofundishwa shuleni na kutumika kupimia umilisi wa upataji na matumizi ya lugha. Ingawa kanuni hizi za matumizi ya vipashio vya kisarufi vya Kiswahili sanifu hufundishwa kwa wanafunzi wa shule za upili nchini Uganda, Kiswahili kinachozungumzwa na kuandikwa na wanafunzi ni kile kinachoonekana kukiuka kanuni na miundo ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu.

Tafiti juu ya mwingiliano wa lugha zinadhihirisha kuwa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili huathiriwa na L1, hasa inapotokea kwamba mfumo wa lugha ya asili hutofautiana na ule wa Kiswahili sanifu. Mara nyingi wanaisimu hueleza tu kuwa lugha za Kibantu ambazo zimekuwa na mtagusano wa karibu wa muda mrefu huingiliana na kuathiriana. Hata hivyo, kiwango na taathira ya mwingiliano wa Luganda na Kiswahili ambazo ni lugha za Kibantu zilizo katika mnasaba mmoja hazijashughulikiwa kwa kina kwa mtazamo wa kinadharia kudhihirisha athari za mwingiliano wa kimofosintaksia. Mathalani, utafiti kuhusu ufafanuzi wa uwiano na tofauti za vipashio na uchanganuzi wa kanuni za kisiimu ya kimofolojia ya Luganda na Kiswahili, unavyoshirikiana na vipashio vya kisintaksia katika tungo kudhihirisha uhusiano wa neno kuu kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo, na jinsi uhusiano huo unavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, hujawekwa bayana kuonyesha jinsi mofosintaksia ya Luganda inavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Kwa hiyo utafiti huu ulichanganua mofosintaksia ya Luganda sanifu katika matumizi ya Kiswahili sanifu ili kuweka bayana athari za mwingiliano wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli katika nomino, viwakilishi nafsi, vivumishi na vikanushi katika maandishi na mazungumzo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyotumika na mwanafunzi ambaye L1 ni Luganda.

1.3 Maswali ya utafiti

- i) Ni kwa namna gani vipashio vya mofosintaksia vya Luganda vinafanana na kutofautiana na vipashio vya mofosintaksia vya Kiswahili sanifu katika matumizi?
- ii) Ni kanuni zipi zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na mifanyiko ya kimofosintaksia ya Kiswahili sanifu katika matumizi?
- iii) Ni vipi ambavyo kanuni za kisarufi zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda huingiliana na kuathiri Kiswahili sanifu katika matumizi?

1.4 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu ulidhamiria:

- i) Kufafanua jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda sanifu hufanana na kutofautiana na vya Kiswahili sanifu.
- ii) Kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi.

iii) Kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

1.5 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu una umuhimu kwa maendeleo ya taaluma ya isimu linganishi na tumikizi. Utafiti huu ulibainisha namna lugha jirani zinavyoathiriana kiisimu, jambo ambalo halijashughulikiwa kwa mapana hasa kati ya Luganda na lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Aidha, utafiti huu ulionyesha jinsi vipashio vya mofosintaksia vya Luganda hufanana na kutofautiana katika matumizi na jinsi kufanana na kutofautiana kunavyosababisha mwingiliana na athari katika matumizi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Udhahirishaji wa athari za mwingiliano wa vipashio na kanuni za mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu una umuhimu wa kukuza, kuendeleza na kuchangia taaluma ya isimu linganishi ya lugha za Kibantu na isimu miundo kwa kubainisha kufanana na kutofautiana kwa kanuni, miundo na athari za mofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, katika viwango vya kiisimu vya mofosintaksia.

Utafiti huu uliweka msingi thabiti kwa tafiti za baadaye katika uwanja wa miundo na usanifu wa matumizi ya Kiswahili sanifu kama L2. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yamepewa kipaumbele na jamii nchini Uganda. Hadhi hii inatokana na mahitaji ya Kiswahili kutumiwa kama lugha ya mawasiliano, lingua franca na lugha rasmi ya pili ya taifa nchini. Matumizi ya Kiswahili kama lugha ya pili miongoni mwa wanafunzi wilayani Kampala unatokana na sera ya serikali ya kufundisha Kiswahili kama lugha ya lazima katika shule za upili, (Jjinga & Visser, 2017; The Republic of Uganda, 1992). Kwa hiyo, utafiti huu ulifanyika kuweka misingi ya matumizi ya vipashio vya mofosintaksia na kanuni za matumizi ambayo kwayo ndiyo nguzo mwafaka katika maandishi na mazungumzo ya Kiswahili sanifu.

Utafiti huu una manufaa kwa lugha za Kiafrika na hasa kwa lugha za Kibantu za Afrika Mashariki kwa kukuza na kuendeleza matumizi sanifu ya lugha husika miongoni mwa lugha ambazo zimekuwa katika makutano na ukinzani wa muda mrefu. Udhahirishaji wa mwingiliano na athari za miundo na kanuni za vipashio vya mofosintaksia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu utawaongoza wanafunzi na wataalamu wa lugha za Kiafrika kuweka mikakati ya kukuza na kuendeleza matumizi sanifu ya kanuni na miundo ya vipashio vya kisarufi vya lugha za Kiafrika inayotokana na mwingiliano wa lugha zilizo na ukuruba na ukinzani wa muda mrefu kama ilivyo Luganda na Kiswahili sanifu nchini Uganda.

Ubainishaji wa uchanganuzi wa mofosintaksia ya Luganda na jinsi inavyoingiliana na kuathiri Kiswahili sanifu ulitekelezwa na utafiti huu. Uliweka wazi kanuni za matumizi ya vipashio na miundo ya vipashio kati ya Luganda na Kiswahili, kufafanua uwiano na tofauti za vipashio na kanuni za matumizi ya kila kipashio cha kimofosintaksia pamoja na kuonyesha mwingiliano ambao ulisababisha athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, inatarajiwa kuwa utafiti huu utaweka mikakati ya matumizi sanifu ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wilayani Kampala, kuboresha Kiswahili kinachoandikwa na kuzungumzwa na wanafunzi wa shule za sekondari ambao L1 ni Luganda wilayani Kampala, nchini Uganda.

Utafiti huu vilevile unatarajia, kuendeleza na kuchangia taaluma ya isimu miundo kwa kubainisha kanuni, miundo na athari za mofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika viwango vya kiisimu vya mofosintaksia. Wanafunzi na walimu wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda pamoja na wanaisimu miundo wanatarajiwa kufaidika na uchanganuzi wa mofosintaksia ya Luganda ambao utawaongoza kutambua miundo ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda, kanuni za matumizi ya kila kipashio cha kimofosintaksia na jinsi kinavyotumika kuonyesha uhusiano wa vipashio kuungana kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo.

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwafaidi wanafunzi na wanaisimu kutambua jinsi lugha ya Kiswahili inavyoathirika na lugha za nasaba moja za Kibantu au lugha asili hasa lugha ambazo zimekuwa katika makutano na ukinzani wa muda mrefu kutokana na sera za matumizi ya lugha katika nchi ya Uganda na Afrika mashariki. Pengine, utawasaidia wanaisimu na watafiti mbalimbali kujifunza, kuchanganua pamoja na kulinganisha Luganda na Kiswahili sanifu katika kiwango cha mofosintaksia na kujidokeza na matokeo yatakayokuza na kuendeleza matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili sanifu sambamba na lugha asili (Luganda) bila kusababisha mwathiriano unaoweza kusababisha kufa kwa lugha, kumezwa kwa lugha, uundaji mpya wa lugha na au uibukaji wa lugha kadirifu isiyo Kiswahili sanifu au lugha asili ambayo ni L1. Hali hii inatokana na utafiti huu kufafanua uwiano na tofauti za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu na kuchanganua kanuni za mifanyiko ya vipashio vya mofosintaksia ambao ni muhimu katika kutambua na kutumia kipashio na kanuni ya lugha sahihi bila kuathiri lugha nyingine kwa sababu ya kutambua tofauti za vipashio na kanuni za lugha husika katika matumizi.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoa mchango wa lugha asili katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu na tathimini ya jinsi lugha asili inavyoingiliana na kuathiri lugha ya Kiswahili sanifu nchini Uganda. Matokeo haya yatawasaidia watafiti kufanya uchunguzi zaidi wa kiisimu juu ya mchango wa lugha asili katika matumizi ya lugha ya Kiswahili pamoja na kuchanganua jinsi lugha asili ambazo zimekuwa katika mtagusano na ukinzani wa muda mrefu na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri Kiswahili sanifu katika viwango mbalimbali vya kiisimu hasa katika matumizi ili kukuza na kuendeleza matumizi sanifu ya lugha husika.

1.6 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulishughulikia athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulifanyika wilayani Kampala. Ulichunguza vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili, kutathimini athari za mwingiliano wa miundo na kanuni za L1 kwa L2 miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama L2 nchini Uganda, na wala sio lugha nyingine. Data ya utafiti ilichunguza matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili katika maandishi na mazungumzo kama yanavyotumika na kutolewa na mwanafunzi anayejifunza Kiswahili ambaye L1 ni Luganda. Utafiti huu ulifananganisha na kutofautisha vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili na kuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio husika vya Luganda na Kiswahili sanifu ili kuweza kutathimini mwingiliano na athari za Luganda katika Kiswahili sanifu. Utafiti ulichunguza matumizi ya Kiswahili shuleni, miongoni mwa wanafunzi wala sio mitaani. Hii ni kwa sababu, Kiswahili hufundishwa na kutumika shuleni na mitaani katika shughuli za mawasiliano. Shuleni, Kiswahili kinafundishwa katika shule za upili kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita kama L2. Mitaani, Kiswahili hutumika katika shughuli rasmi na za kibinafsi. Mtafiti alichagua sampuli ya wanafunzi ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili kama L2 kutoka kidato cha sita.

Mbali na kuwepo kwa sababu nyinginezo zinazoathiri usanifu wa matumizi ya L2, utafiti huu uliegemea kuchunguza vipengele vya kiisimu vya kimofosintaksia vya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanusho na vivumishi ukiongozwa na mihimili miwili ya Ubia na Upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Uganifu ya Chomsky (1981). Vipashio hivi vilichaguliwa kwa sababu ni vipashio vya kimsingi vya kimofosintaksia ambavyo vina uhusiano wa karibu, vyenye uwezo wa kuonyesha uhusiano wa kisarufi wa neno kuu kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo. Aidha, vipashio hivi vilichaguliwa kwa sababu ni vipashio vya kimsingi ambavyo huathiri ufasiri wa sentensi kimuundo, kikanuni na kidhima

(Barno, 2013; Taaita Toweet). Vipashio hivi ni vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake huweza kubainika katika sintaksia na ambavyo vinaweza kuchanganuliwa katika mofosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu katika tungo. Mathalani ukiukaji wa matumizi ya miundo na kanuni ya vipashio hivi amilifu vya kisintaksia katika tungo, huweza kuathiri ufasiri wa sentensi kama inavyotambulika na kukubaliana na watumiaji wa lugha lugha mahususi (Comrie, 1976; Palmer, 1986; Lyons, 1995; Chomsky, 1995; Oduor na Wenzake, 2017).

Utafiti huu ulikusanya data za madhumuni ya kwanza na pili kwa kutumia mjarabu na mijadala. Mjarabu ya kisarufi inayohusiana na vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu iliandaliwa kwa ajili ya kujibiwa na wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Baada ya zoezi la mjarabu kusahihishwa, data za mjarabu zilielekeza utafiti huu katika mijadala kwa ajili ya kupata data za madhumuni ya pili na tatu ya kuchanganua kanuni na athari za mwingiliano wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya L2 kama inavyotumika na kuelezwa na wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda. Orodha ya uchunzaji yenye sifa za kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili ilitumika katika kuhakiki na kudondoa taarifa muhimu kutoka katika vitabu teule vya Kisarufi vya Luganda na Kiswahili sanifu kwa ajili ya kupata data za madhumuni ya kwanza. Utafiti huu ulifanyika maktabani na nyanjani katika eneo la wilaya ya Kampala, Uganda. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kubainisha athari za mwingiliano wa kanuni na miundo ya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umilikifu na Unganifu ya Chomsky (1981). Nadharia hii hueleza kwamba viambajengo vya sentensi viko katika nafasi ama sehemu mbalimbali za sentensi na huletwa pamoja na kanuni fulani ya lugha. Vilevile nadharia hii husisitiza kuwa muundo wa sentensi hutegemea ama huathiriwa na kuwemo kwa mofu fulani katika sehemu za sentensi ambazo huathiri maumbo ya vijenzi vingine katika virai, vishazi ama sentensi. Nadharia hii iliongoza utafiti huu katika kuchunguza matumizi ya sifa za vipashio vya kiisimu miongoni mwa wanafunzi ikiegemea katika miundo na kanuni katika matumizi.

1.7.1 Nadharia ya Umilikifu na Unganifu

Nadharia ya Umilikifu na unganifu ni nadharia ya kisintaksia inayotokana na sarufi zalishi na ambayo ina misingi yake katika sarufi geuza maumbo iliyoasisiwa na Chomsky mnamo mwaka wa 1981. Nadharia hii ina mikondo miwili ya kimsingi ambayo ni mkondo wa

Nadharia ya Umilikifu inayoshughulikia uhusiano wa kisintaksia ambapo neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo (Massamba, 2004). Mkondo wa pili ni wa nadharia ya Uhusisho au Unganifu ambayo hushughulikia vitu halisi vinavyowakilishwa na viwakilishi, mrejeosabiki na maelezo rejeshi. Nadharia ya unganifu ina kanuni moja kwa kila mojawapo ya kategoria hizi. Radford (1981:1997) alifafanua kanuni tatu kuu za nadharia ya unganifu na kila kanuni ikidhibiti mtawanyiko na ufafanuzi wa aina moja mahususi ya KN (kundi nomino).

- i) Kanuni ya kwanza ni ya mrejeosabiki ambayo hudhibiti ufafanuzi wa vipengele ambavyo kiurejeleo ni tegemezi, kama vile viwakilishi jirejeele. Kanuni hii inashikilia kuwa, lazima kirejeosabiki (Anafora) kifungamane na kategoria inayokimiliki katika tungo. Kwa mfano katika sentensi;

Tumwebaze alipika chakula mwenyewe

Katika sentensi hii kirejeosabiki ni *mwenyewe* na *Tumwebaze* ni kategoria inayorejelewa kama mpishi ama mtendaji. *Mwenyewe* ni kiwakilishi jirejee kinachohusiana na au kufungamana na nomino katika KN au tungo.

- ii) Kanuni ya pili ni kwamba lazima kiwakilishi kiwe huru katika kategoria inayokimiliki (Kiwakilishi nomino). Kiwakilishi nomino huchukua nafasi ya nomino katika sentensi, na mara nyingi huathiri upatanisho wa kisarufi na maumbo ya maneno mengine katika utungo wa sentensi. Kwa mfano katika sentensi

“Ukarimu alionao Amoni unafaa”.

Katika sentensi ‘*Ukarimu*’ ni kiwakilishi cha nomino ambacho kinamrejelea *Amoni* na ambacho kinasababisha upatanishi wa kisarufi /u-/ katika sentensi hiyo.

- iii) Kanuni ya tatu ni kanuni ya tamkio rejeleo ambayo Oduor na wenzake (2017) wameiita maelezo rejeshi ambayo ni lazima yawe huru. Tamkio rejeleo ni majina halisi yanayotaja majina ya vitu, watu, mahali na hali.

Nadharia ya Umilikifu na Unganifu ina misingi yake katika mtazamo wa Kanuni na Vigezo ambao ni kiunzi katika Isimu Zalishi. Chomsky, Lasnik, Jacobs, von Stechow, Sternefeld, & Vennemann (1993) wanaeleza kuwa jambo la muhimu katika mkabala wa kanuni na vigezo ni kuwa umilisi wa kisintaksia wa mtu unaweza kuonyeshwa kupitia kwa njia mbili rasmi. Njia ya kwanza ni njia ya kimsingi ya sifa bia ya lugha ambazo ni kanuni za kimsingi zinazopatikana katika lugha zote. Katika msingi huu inaaminika kuwa sifa ya sentensi zote za lugha lazima ziwe na kundi nomino na kundi tenzi ambazo zinawakilisha umbo ndani la

sentensi. Kanuni ya pili ni ya upatanifu wa kisarufi ambapo vigezo vya kimsingi hubainisha tofauti ya kisintaksia miongoni mwa lugha. Mkabala huu unajaribu kuzingatia tofauti ya kisintaksia iliyoko baina ya lugha kwa kuchunguza jozi ya vigezo na kanuni za lugha kama inavyotumika na mmlisi wa lugha na mwanafunzi anayejifunza na kutumia lugha.

Crystal (2004:2011) anaeleza kuwa nadharia ya Umilikifu na Unganifu ni mkabala wa sarufi zalishi ambao ulianza katika miaka ya 1980 na iliyopata jina kutokana na jinsi inavyoshirikisha masharti ambayo huunganisha vipashio vya sentensi, na miktadha ya kimiundo ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutokea. Umilikifu hujishughulisha na uhusiano baina ya neno kuu na shamirisho zake, ilhali unganifu unahusiana na urejeleo wa vipashio katika sentensi. Nadharia hii inahusisha viambajengo ambavyo vinapatikana katika sehemu tofauti za sentensi ambavyo vinaunganishwa na sheria fulani ambazo husababisha umilikifu na uunganishaji wa viambajengo hivyo na jinsi vipashio mbalimbali vya sentensi vinavyopangwa pamoja, na uhusiano wa vipashio hivyo.

Haegeman na Atkinson, (1994) wameifupisha dhana ya umilikifu kwa kusema kwamba: A humiliki B ikiwa A ni neno kuu; A na B ni vifundo dada, na kwamba maneno-milikifu ni maneno makuu. Umilikifu una msingi wake katika neno kuu katika kirai ambacho huyamiliki maneno mengine yote katika kundi husika. Kifundo ambacho kipo juu ya kingine katika kielelezo cha matawi husemekana kuwa kinakimiliki kile kilicho chini yake. Viambajengo vyote vinavyomilikiwa na kifundo kimoja huunda kategoria ya umilikifu ya kifundo hicho. Kikundi tenzi (KT) ndilo kategoria ya umilikifu ya kitenzi.

1.7.2 Mihimili ya nadharia ya Umilikifu na unganifu

Nadharia ya Umilikifu na Unganifu ina mihimili mikuu miwili ambayo ndiyo msingi wa mihimili mingine midogo:

- a) Mhimili wa kwanza mkuu wa nadharia ya Umilikifu na Unganifu ni ule unaozingatia sifa za sarufi bia ambayo huchukulia kuwa kanuni zile zile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo, yaani kuna vigezo vinavyozitofautisha lugha. Kwa sababu hiyo, Crystal (2011), anasema kwamba, nadharia ya Umilikifu na Unganifu aghalabu hujulikana kama *Mkabala wa kanuni na vigezo (TY)* ambao una msingi wake katika sarufi bia. Mhimili huu wa kwanza umejengekeka kwa vijenzi vya sifa bia za lugha ambavyo;
- i) Huchunguza lugha kwa kuzingatia umbo ndani na umbo nje.

- ii) Hufafanua kanuni za kisintaksia zinazotawala urejeleo nyuma ambao hujikita katika makundi nomino katika sentensi.
- iii) Huegemea sana katika upatanifu wa kisarufi ambao neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo.
- iv) Huamini kuwa umilikifu ambajengo ni uhusiano wa miundo ya kisarufi unaotokana na vipashio kuvitangulia na kuvimiliki vingine na ambavyo hutumiwa kueleza uhusiano wa kianafora katika sentensi.
- v) Dhana ya umilikifu ambajengo inaeleweka bayana kwa mkabala wa kifundo kikuu kuzimiliki kategoria za kisarufi zilizo katika vifundo vinavyopatikana chini yake. KN lenye urejeleo ena linapaswa kumiliki kiwakilishi chake moja kwa moja bila kizuizi chochote.
- b) Muhimili mkuu wa pili wa nadharia ya Umilikifu na Unganifu huchunguza kanuni na vigezo kuegemea sana katika umilisi alionao mtumiaji wa lugha husika. Umilisi ni ule ujuzi wa lugha ambao wazawa wa lugha fulani huwa wanao. Kila mzungumzaji wa lugha fulani anazifahamu sheria za lugha yake bila kufundishwa sheria hizo, bali kutokana na uelewahisi. Sheria za lugha ni za kiasilia. Kwa kutumia umilisi wake, mzawa wa lugha anafahamu sheria zinazotawala vipengele fulani vya sarufi ya lugha yake. Anaweza kuchanganua sentensi sahihi na zile ambazo si sahihi. Kwa mujibu wa Naom Chomsky (1982), mwanasarufi ana jukumu la kujaribu kueleza ujuzi huu, kuelewa na kujaribu kujifundisha sheria za lugha husika ili aweze kuufafanua ujuzi huu wa mzungumzaji asilia wa lugha fulani.

Mhimili huu hufafanua namna vipashio vya kianafora vinavyomilikiwa, jinsi kiambajengo humiliki kingine. Uhusiano huu unajulikana kiisimu kama umilikifu ambajengo. Hakuna kiambajengo kinachoweza kumiliki vipashio vingine nje ya kifundo kikuu cha kiambajengo hicho. Kifundo kikuu hujulikana kama kategoria ya umilikifu. Neno linalomiliki vipashio vingine hujulikana kama neno milikifu. Nadharia ya unganifu huongozwa na kanuni tatu na kila kanuni hudhibiti mtawanyiko na ufafanuzi wa aina moja mahususi ya KN (kundi nomino). Kwa kutumia mhimili huu, utafiti huu ulichunguza kanuni za kimofosintaksia za Luganda kama zinavyotumiwa na mwanafunzi wa kidato cha sita ambaye L1 ni Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kanuni zilizochunguzwa ni zile za matumizi ya vipashio vya kianafora kudhihirisha jinsi viambajengo/neno humiliki vingine. Msisitizo ulichunguza kanuni za muunganiko wa viambajengo au neno milikifu kujenga upatanishi wa kisarufi wa viambajengo vya mofolojia na sintaksia katika tungo.

1.7.3 Ufaafu wa Nadharia kwa utafiti

Utafiti huu ulitumia mihimili ya umilisi; upatanifu; umbo ndani na umbo nje katika nadharia ya *Unganifu* kubainisha mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kuchunguza madhumuni ya kwanza na pili. Kwa ajili ya kufanikisha madhumuni ya utafiti huu, kanuni mbili za mhimili wa pili wa nadharia hii zilitumika hasa *kanuni ya kwanza* ambayo inahusu vipashio vya lazima (anafora na kirejelewa) mtawanyiko wao katika sentensi; na *kanuni ya pili* inayohusu umilikifu wa viwakilishi huru katika kategoria zao za umilikifu ili kubainisha uamilifu wa kianafora unaomilikiwa nje ya kategoria zao za umilikifu. Aidha, kanuni hizi mbili zilitumiwa kuchanganua upatanifu baina ya anafora na kirejelewa chake kuhusu vipengele vya ngeli na nafsi, na vile umilikifu huo unavyochochea mifanyiko (muundo) ya kimofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Mhimili wa kwanza wa ubia wa sifa za lugha za Kibantu ulitumika kufafanua uwiano na tofauti za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu na kuchangana mifanyiko ya kanuni za matumizi ya vipashio vya Luganda na Kiswahili ili kudhihirisha jinsi mofosintaksia ya Luganda inavyoingiliana na kuathiri Kiswahili kinachozungumzwa na kuandikwa na wanafunzi wa shule za upili ambao L1 ni Luganda wilayani Kampala, nchini Uganda.

1.8 Hitimisho

Sura hii ilibainisha mada ya utafiti ya uchanganuzi wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kiupeo, utafiti huu ulifanyika wilayani Kampala, Uganda. Ulichunguza vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili, kutathimini athari za mwingiliano wa miundo na kanuni za L1 kwa L2 miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2 nchini Uganda, na wala sio lugha nyingine. Katika sura hii, nadharia iliyouongoza utafiti huu ilielezwa na ufaafu wake kuwekwa bayana. Usuli wa utafiti huu ulibainisha pengo la utafiti la kuchanganua kiwango na taathira ya mwingiliano wa Luganda na Kiswahili ambazo ni lugha za Kibantu zilizo katika mnasaba mmoja kudhihirisha athari za mwingiliano wa kimofosintaksia ambazo hazijawekwa bayana. Iidhihirisha kuwa athari za L1 kwa L2 hutokana na mwingiliano wa vipashio vya kanuni anuwai vya kiisimu, viwango tofauti vya upataji wa umilisi wa lugha unaokabiliwa, uhamishaji hasi wa vipashio na kanuni za matumizi ya vipashio vya kiisimu kutoka lugha mbalimbali za kwanza katika L2. Aidha, usuli ulibainisha kuwa udhihirishaji wa athari za mwingiliano wa vipashio na kanuni za mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu una umuhimu wa kukuza, kuendeleza na kuchangia taaluma ya isimu linganishi ya lugha za Kibantu na isimu miundo kwa kubainisha

kufanana na kutofautiana kwa kanuni, miundo na athari za mofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, katika viwango vya kiisimu vya mofosintaksia. Utafiti huu ulijikita katika isimu linganishi na isimu tumikizi. Madhumuni ya kufafanua jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda sanifu hufanana na kutofautiana na vya Kiswahili sanifu. Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi na utathimini wa kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu zilifafanuliwa.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mapitio ya kitaaluma na mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na mada yetu. Marejeleo ya makala na vitabu vinavyohusiana na mofosintaksia, kategoria na mifanyiko ya mofosintaksia na athari za mofosintaksia za L1 katika matumizi ya L2 yalikusika. Sura hii ilionyesha mtazamo wa wataalamu mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti, upekuzi, machapisho na vitabu vya kitaaluma na ya kazi tangulizi. Mapitio haya yamepangwa kwa mujibu wa madhumuni matatu.

2.2 Kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya mofosintaksia vya lugha

Lado (1957), akielezea juu ya uchunguzi wa ujifunzaji na matumizi ya lugha ya kwanza (L1) na lugha ya pili (L2), alifafanua kuwa miundo ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia inayofanana na ile inayotofautiana pamoja na mifumo ya jamii ya matumizi ya lugha ni muhimu sana katika ujifunzaji na matumizi ya lugha L1 na L2. Anaeleza kuwa utambuzi wa uwiano na tofauti za mifumo hii ni muhimu katika kutabiri miundo inayorahisisha ujifunzaji na matumizi na ile inayowatatiza wanafunzi. Alitambua kuwa kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya lugha ndiko kunakosababisha uhamishaji wa miundo na mifumo ya matumizi ya lugha kati ya L1 na L2 ambayo ni muhimu sana. Kulingana na msimamo wake, asili ya makosa yanayojitokeza katika matumizi ya L2 ni tofauti za vipashio vya lugha kati ya L1 na L2. Lado (keshatajwa) anapendekeza kuwa matatizo ya wanafunzi katika matumizi ya lugha yao hutokana na kutofautiana kunakojitokeza baina ya lugha mbili yaani L1 na L2.

Maelezo na mapendekezo ya Lado, ni muhimu sana kwa utafiti huu. Kupitia kwa maelezo yake ambayo yalikuwa yamejikita katika ujifunzaji na matumizi ya lugha kutokana na kufanana na kutofautiana kwa vipashio au vipengele vya lugha, utafiti huu uliweza kutambua vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu, kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipashio hivyo vya kimofosintaksia na kisha, kutathimini mwingiliano wa mofosintaksia ya vipashio vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulitambua uwiano na tofauti za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na jinsi vinaingiliana na vya Kiswahili sanifu na kuvunja kanuni za matumizi ya Kiswahili sanifu.

Mukuria (1987) alilinganisha mpangilio wa ngeli za Kikikuyu cha Kiambu na Kiswahili sanifu. Ulinganishi wake ulijishughulisha na uainishaji wa ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu kisintaksia na kisemantiki kuzingatia vigezo vya idadi za ngeli,

uwiano wa kisarufi na misingi ya kimaana inayotokea katika ngeli za lugha hizo. Utafiti wake ulitambua kuwa kimuundo kiambisho kilichoko kwenye jina hukaririwa kwenye vipande vingine vya sarufi ambavyo hutawaliwa na jina. Aidha, kisemantiki, kila mojawapo ya ngeli inahusiana na dhana moja au zaidi. Utafiti wake pia ulitambua kuwa lugha za Kibantu kama vile Kiswahili na Kikikuyu zina takiriri za viambishi kwenye vipande vya sarufi. Matokeo ya utafiti wa Mukuria (keshatajwa) ulichangia pakubwa katika kuainisha ngeli za Kiswahili na kutoa mwelekeo wa kulinganisha ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu ili kubaini jinsi nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu hufanana na kutofautiana. Hii ilitokana na sababu kuwa utafiti wa Mukuria (keshatajwa) ulijihusiha na isimu linganishi ya lugha mbili ambazo ni za Kibantu (Kikuyu na Kiswahili) huku utafiti huu nao ukichunguza Luganda na Kiswahili sanifu.

Katamba (1993) katika uchunguzi wake juu ya mofolojia na mahusiano ya leksia na sintaksia, alitambulisha vipashio vinavyohusisha sifa za kimofosintaksia katika kiwango cha neno kuwa nomino, idadi, njeo, kitenzi, kivumishi, na jinsia. Uchanganuzi wake kuhusu vipashio hivi ulikuwa wa kimofolojia na jinsi vipashio hivyo huhusiana kileksia na sintaksia katika lugha. Tofauti na ufafanuzi wake, utafiti huu ulichunguza uhusiano wa vipashio hivi kimuundo kwa kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya Luganda na Kiswahili sanifu na jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Uchunguzi wa Katamba (keshatajwa) ulizingatia mahusiano ya leksia na sintaksia peke yake. Utafiti huu ulijikita kueleza jinsi vipashio vya leksia huhusiana na sintaksia, kuingiliana na kuathiri matumizi ya lugha kati ya L1 na L2 kutokana na kufanana na kutofautiana. Mbali na kuwa utafiti wa Katamba (keshatajwa) alionyesha tu uhusiano wa vipashio kimuundo na namna vinajenga nomino na uhusiano wake, Utafiti wake uliusaidia utafiti huu katika kuainisha vipengele vya kimofosintaksia vilivyohusika katika kueleza sifa za kisarufi za Luganda na jinsi vipashio hivyo vya mofosintaksia huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu na ambao L1 ni Luganda.

Massamba, Kihore & Hokororo (1999) wakishughulikia viambajengo vya sentensi, walibaini kuwa lugha za Kibantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Wanaeleza kuwa lugha za Kibantu huwa na mfuatano wa viambishi ambavyo huambikwa kabla ya mizizi kuwakilisha sifa za kisarufi. Kazi ya waandishi hawa ilikuwa muhimu katika kueleza viambajengo vya vipashio vya mofosintaksia vinavyounganika na vipashio vingine katika sentensi kuwakilisha sifa za

kimofosintaksia za sentensi za Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, utafiti wao ulinufaisha utafiti huu kuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio au viambajengo vya mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na muundo wa sentensi kama ulivyoielezwa na wataalamu hawa. Maelezo haya yalikuwa msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kutokana na muundo wa sentensi zinazotolewa na mwanafunzi wa kidato cha sita ambaye L1 ni Luganda. Hii ni kwa sababu, viambajengo vya sentensi vilivyotajwa na wataalamu hawa ni miongoni mwa vipashio vya mofosintaksia ya lugha za Kibantu zilizohusika katika utafiti huu.

Tofauti na uchunguzi wa Massamba na wenzake (washatajwa) uliofafanua miundo ya sentensi kwa jumla kwa kufafanua viambajengo vya sentensi za lugha za Kibantu pamoja na kuangazia viambishi vinavyopachikwa kwenye vipashio vya mofosintaksia (maneno), Kiswahili kikiwakilishwa, utafiti huu ulieleza matumizi ya vipashio vya sentensi ambavyo ni vya kimofosintaksia vya Luganda na jinsi huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu kazi yao ilirahisisha utafiti huu katika kufafanua vipashio vya muundo wa sentensi za Luganda na Kiswahili sanifu zinazodhihirisha sifa za kimofosintaksia. Uchanganuzi wa uhusiano huo ulisaidia sana katika kuchanganua kanuni zinazounganisha vipashio, na kutathimini jinsi kanuni za matumizi ya vipashio hivyo vya mofosintaksia vya Luganda huingiliana na jinsi zinavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, utathimini ambao haikuelezwa hapo awali.

Oichoe (2005) katika utafiti wake alilinganisha ngeli za Kiswahili na Ekegusii na kudhihirisha kuwa mpangilio wa nomino katika makundi ngeli katika lugha hizi yanatofautiana. Aidha, ilibainika kuwepo kwa mfanano na tofauti katika mpangilio wa makundi ya ngeli katika lugha ya Kiswahili sanifu na Ekegusii. Kiswahili kilidhihirisha makundi ya ngeli machache kuliko yale ya Ekegusii. Utafiti wake ulidhihirisha viambishi tofauti vinavyotumika baina ya Lugha hizi mbili ambapo ilidhihirika kwa mfano Kiswahili kutumia viambishi vitatu vya ngeli ya mahali, huku Ekegusii ikitumia viwili. Nomino zilibadilishana ngeli baina ya lugha hizi ambapo nomino moja ya Kiswahili inaweza kupatikana katika Ekegusii lakini katika ngeli tofauti. Pia baadhi ya nomino kuchukua viambishi ngeli vya umoja na wingi kutofautiana. Matokeo ya utafiti wa Oichoe (keshatajwa) ulielekeza utafiti huu katika kuainisha na kutambua makundi ya ngeli, viambishi ngeli vya nomino na uainishaji wa kila nomino katika ngeli ili kueleza uwiano na tofauti za nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia.

Okumu (2006) katika uchunguzi wake wa kutathimini mpangilio wa ngeli kuzingatia mifumo ya uainishaji wa kimofolojia na kisemantiki pamoja na kisintaksia, aligundua kuwa wanafunzi wangali wanatatizwa na funzo la kipashio cha ngeli kimatumizi hasa katika kuendeleza sentensi sahihi kisarufi kutokana na kukanganywa kwao na maumbo yanayotambulisha ngeli pamoja na kutoelewa maana ya ngeli. Alipendekeza haja ya walimu wa Kiswahili kuzua mbinu za kuwawezesha wanafunzi kuelewa maumbo na maana ya nomino hizi na kufanywa utafiti zaidi kuhusiana na ufundishaji wa kipashio cha kisarufi cha ngeli kuimarisha ujifunzaji na kuondokana na athari za ujumlishaji na uhamishaji wa lugha za kijamii katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Matokeo na mapendekezo ya utafiti wa Okumu (keshatajwa) uliweka misingi ya utafiti huu na filsofia ya kuchunguza vipashio vya kiisimu vya lugha za Kibantu, kuonyesha uwiano na tofauti za vipashio kwa ajili ya kuonyesha mchango wa L1 katika matumizi ya L2. Aidha, kutokana na utafiti wake, utafiti huu uliweza kutambua uainishaji wa nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili na kudhihirisha athari katika matumizi ya ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Hali hii ili ilisaidia na kuongoza utafiti huu kueleza uwiano na tofauti za nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu.

Katamba & Stonham (2006) wanaeleza kwamba lugha zote huwa na vipashio, ila vinatofautiana katika baadhi ya lugha hizo kutokana na mofimu inayovijenga vipashio hivyo kuwakilisha sifa za kisarufi. Malekezo ya Katamba na Stonham (2006) kuhusu kutofautiana kwa vipashio vya lugha zote, yalikuwa ya muhimu sana katika utafiti huu. Maelezo yao, yaliuongoza utafiti huu kutambua na kueleza vipashio vya mofolojia na sintaksia vya Luganda na kudhihirisha jinsi vinavyofanana na kutofautiana na vipashio vya Kiswahili sanifu. Maelezo ya utafiti huu yalizingatia mofimu katika maneno ya kimofolojia, na kanuni zinazoviunganisha vipashio hivyo katika sentensi kuonyesha kumiliki na kumilikiwa kwa vipashio vya kimofosintaksia katika tungo kudhihirisha sifa za kimofosintaksia.

Ferrari-Bridgers, F. (2008), naye alichunganganua sintaksia ya ngeli nomino za Kiitalia na Luganda. Utafiti wa wataalamu (washatajwa) uliongoza utafiti huu kuainisha nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili na kuonyesha uwiano na tofauti za uainishaji na matumizi ya nomino katika ngeli husika na kuongoze kueleza jinsi kipashio cha kimofosintaksia cha ngeli za Luganda huwiana na kutofautiana na Kiswahili sanifu.

Wanaisimu wengine waliolinganisha ngeli kimofosintaksia ni pamoja na Crisma Paola, Marten Lutz & Sybesma Rint (2011). Wataalamu hawa walichunguza uainishaji wa ngeli za

Kibantu Kiromansi na Kichina. Utafiti wao uligundua kuwa, ingawa lugha zote hushirikisha uainishaji wa mofolojia na sintaksia, zote huegemea katika kigezo cha semantiki katika uainishaji. Aidha ilibainika kuwa pia walizingatia kigezo cha matumizi kuainisha ngeli kiidadi na kuzingatia jinsi ya kisarufi za nomino kama neno kuu. Katika uchunguzi wao, walibainisha ngeli 15 za Kiswahili kulingana na Ashton (1947), Mohamed (2001) na Schadeberg (1992).

Kwa upande mwingine Barno (2013) anabainisha vipengele vya kimofosintaksia ambavyo huathiri kategoria za kisarufi katika virai na sentensi. Vipashio anavyobainisha na ambavyo vina uwezo wa kuathiri muundo wa kirai au sentensi ni hali, wakati, ukanushi, uyakinifu na vipatanishi. Katika uchunguzi wake juu ya muundo wa mofosintaksia wa kitenzi cha Kinandi alitambua kuwa vipengele hivi vikipachikwa kwenye kitenzi vina uwezo wa kuathiri muundo wa kirai au sentensi katika kiwango cha uamilifu. Kutokana na utafiti wake, utafiti huu ulinufaika katika kuchanganua vipengele vyenye sifa za kimofosintaksia vya Luganda na kuchunganua, vipashio vya kisarufi, kanuni, miundo na kuchanganua namna vinaingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wa Barno (keshatajwa) kinadharia, lugha na vipashio vya kisarufi vilivyochunguzwa kujadili athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Barno (keshatajwa) ulichunguza muundo wa kimofosintaksia wa kitenzi cha Kinandi kwa kutumia kiunzi cha Kanuni finyu huku utafiti huu ukieleza, kuchanganua na kutathimini athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutumia nadharia ya Umilikifu na Unganifu.

Namugala (2014) katika utafiti wake kuhusu hali za udogo na ukuzaji wa ukubwa katika Luganda anaelezea kuwa majina yote katika Luganda yamewekwa katika ngeli za majina na kila nomino inayo kiambishi cha upatanifu ambacho huitofautisha nomino moja na nyingine. Aidha, nomino katika Luganda hufuata mfumo wa ngeli za majina ambayo hudhihirisha umoja na wingi wa nomino pamoja na upatanifu wake ambao hujitokeza katika tungo. Viambishi vya ngeli vinavyodhihirisha upatanifu hujitokeza katika vivumishi, vitenzi na vipashio vingine vya kisarufi. Tofauti na utafiti wa Namugala (keshatajwa), uliodhihirisha viambishi vya ngeli za majina ya Luganda iliyoonyesha udogo na ukuzaji wa ukubwa wa nomino katika muktadha wa kipragmatiki, utafiti huu ulifananaisha na kutofautisha kipashio cha nomino katika ngeli kuonyesha jinsi ngeli za Luganda na Kiswahili hufanana na kutofautiana na kusababisha mwingiliano na athari katika matumizi ya Kiswahili kama L2.

Licha ya tofauti hizo, utafiti wa Namugala (*keshatajwa*) ulikuwa kielelezo kwa utafiti huu kwa kuwa ulielekeza katika uainishaji na uchanganuzi wa ngeli za majina ya Luganda na Kiswahili na kujadili miundo kanuni na athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Ntawiyanga (2015), katika uchunguzi wake wa Changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda, alibainisha viambishi vya ngeli na vipatanishi vya kisarufi pamoja na virejeshi vya ngeli kama vipashio vya kimofosintaksia vya lugha ya Kiswahili na Kinyarwanda ambavyo hutumika kuonyesha uhusiano kati ya nomino na maneno mengine katika tungo. Uhusiano huo ni ule unaochunguzwa kwa kuzingatia vipashio ambavyo ni viambishi awali vya nomino vinavyoathiri viambishi vya upatanishi vya ngeli vinavyowekwa katika maneno mengine. Kutokana na utafiti wake, makosa ya kimofosintaksia ya uchopekaji wa vipashio vya kisarufi katika tungo, udondoshaji wa vipashio katika tungo, mchanganyiko na matumizi mabaya ya viambishi. Vilevile, utafiti wake ulitambua kuwa wanafunzi walihamisha baadhi ya vipashio (vipengele) na miundo ya kiisimu ya Kinyarwanda na kuvitumia katika Kiswahili. Aidha, kulingana na Ntawiyanga (*keshatajwa*), makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi yalitokana na miundo fanani na tofauti zilizopo kati ya mfumo wa ngeli za Kiswahili na Kinyarwanda ambapo maswala ya kimofolojia, ya kisintaksia na kisemantiki huingiliana na kukamilishana kiasi cha kumkanganya mwanafunzi.

Utafiti wa Ntawiyanga (*keshatajwa*) ni utafiti ambao unahusiana na utafiti huu kwa kiasi kikubwa kwa sababu tafiti hizi zote zinachunguza kipengele cha sarufi ya isimu tumikizi. Ntawiyanga akichunguza changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi Wanyarwanda, nchini Rwanda na hii ya sasa ikichunganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika Kiswahili sanifu, nchini Uganda. Utafiti wa awali ulichunguza changamoto za kimofosintaksia ukilenga kutambua makosa, aina za makosa, Asili cha makosa na mikakati ya kupunguza makosa. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu uliegemea kutathimini mwingiliano wa mofosintaksia ya Kiswahili katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Uliegemea katika kueleza uwiano na tofauti ya vipashio vya kimofosintaksia, kanuni za mifanyiko ya matumizi ya vipashio na kutathimini mwingiliano wa vipashio vya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Muhimu ni kwamba, utafiti wa Ntawiyanga ulichangia pakubwa utafiti huu kutambua vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili na kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipashio hivi ili kuweza kutathimini mwingiliano wa

vipashio hivyo katika matumizi ya Kiswahili, ili kuweka wazi makisio ya kuwa tofauti ya vipashio ndiyo nguzi inayosababisha mwingiliano wa L1 katika L2, na hali kuwa uwiano na tofauti za matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu kimofosintaksia husababisha mwingiliano katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Kitsao (2015) katika utafiti wake juu ya uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi na yanavyochangia matokeo mabaya ya mitihani, alitambua makosa ya kisarufi katika kipengele cha mofosintaksia ya ukiukaji wa mfuatano wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia katika tungo. Katika maelezo yake juu ya makosa yaliyojitokeza, ilitambulika kuwa tofauti za kimuundo za vipashio vya L1 huathiri matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia katika L2. Utafiti wake alishughulikia vipashio vya mofolojia vya maneno ambayo huundwa kutokana na mofimu katika Kiswahili na ruwaza zinazoongoza matumizi ya kila kipashio kulingana na majukumu yake katika mfuatano wake kudhihirisha mfuatano sahihi wa vipashio katika sentensi. Ufafanuzi wa Kitsao (keshatajwa) kuhusu vipashio na aina za vipashio vinavyojitokeza katika muundo wa sentensi ni wa kimofosintaksia. Uchunguzi wake ulielekea kuonyesha makosa ya kimofosintaksia ya L1 katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu na utafiti wa Kitsao (keshatajwa) ulishughulikia kipengele kimoja cha mofosintaksia ukichunguza matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia katika tungo. Kitsao alichunguza makosa ya matumizi ya vipashio unaovunja kaida za matumizi ya Kiswahili, sababu na asili ya makosa yanayosababisha matokeo mabaya ya Kiswahili sanifu. Uchunguzi wake haukuegemea katika ulinganishi na ulinganuaji wa vipashio kutegemea jamii katika eneo la utafiti wake na Kiswahili. Utafiti huu ulichanganua uwiano na tofauti za vipashio, mifanyiko ya kanuni za kimofosintaksia ya vipashio vya Luganda na Kiswahili na kutathimini jinsi unavyosababisha athari za mwingiliano wa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Muhimu ni kuwa, utafiti wake Kitsao (keshatajwa) ulikuwa nguzo katika kutambua vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu na ruwaza maalumu ya matumizi ya vipashio husika kulingana na majukumu yake katika tungo. Hii ni kwa sababu katika Kiswahili, kila kipashio hubeba jukumu ambalo hufuata ruwaza maalumu kulingana na mfuatano wa maneno katika sentensi.

Matasi na Furaha (2016), walilinganisha viwakilishi-nafsi vya Kiswahili na Kibantu kimofosintaksia na kutambua kwamba Kiswahili kilikuwa na viwakilishi nafsi ambavyo vinafanana na vile vya Kiarabu. Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa, licha ya kuwepo

kwa mfanano wa viwakilishi vya nafsi, Kiarabu hudhihirisha kuwepo kwa viwakilishi vya ziada jumla 37 ambavyo pamoja na kuwakilisha nafsi hizo hizo tatu kwa umoja na wingi, vinatofautiana na vya Kiswahili kilicho na jumla ya 12. Walitambua pia kuwa upatanifu wa kisarufi katika Kiarabu hutetegemea jinsia ya mtu (kiume na kike) au kitu kinachowakilishwa tofauti na Kiswahili. Kimuundo, Kiarabu vilevile kinazingatia hali ya uwili ambapo nomino za Kiarabu hugawanywa katika umoja, uwili na wingi tofauti na Kiswahili kinachozigawa nomino katika umoja na wingi.

Kazi ya Matasi & Furaha (Washatajwa) inahusiana na utafiti huu kwa sababu ilijihusisha na isimu linganishi kwa kulinganisha lugha mbili katika kipashio cha kimofosintaksia cha viwakilishi nafsi. Tofauti iliyopo ni kwamba utafiti huu umejikita katika kueleza kufanana na kutofautiana kwa kipashio cha kimofosintaksia cha viwakilishi nafsi cha Luganda na Kiswahili sanifu. Utafiti wao ulikuwa muhimu katika kutambua na kueleza muundo, aina na idadi za viwakilishi nafsi vya Kiswahili sanifu ambavyo vilitumika kulinganishwa na vile vya Luganda kwa madhumuni ya kubainisha kufanana na kutofautiana kimofosintaksia.

Oduor, Inyani & Kobia (2017), wakichunguza uhamishaji wa mofosintaksia ya Kiluo kwa Kiswahili, walitambua kuwa uhamishaji wa mofosintaksia ya Kiluo kwa Kiswahili huathiri miundo ya maneno na tungo za Kiswahili kutokana na tofauti ya kimuundo ya vipashio vya kisarufi vya uambishaji vya ngeli, nafsi na idadi baina ya Kiswahili na Kiluo kimofosintaksia. Kwa kutumia nadharia ya Umilikifu na Uhusisho ya Chomsky, (1981) ambayo hudhihirisha hali ya vipashio fulani vya kisarufi kutawala vipashio vingine katika tungo, utafiti wao ulibaini athari ya uhamishaji wa sarufi ya Kiluo kwenye sarufi ya Kiswahili katika viwango vitatu vya kisarufi vya ngeli, nafsi na idadi.

Utafiti wao ulichangia pakubwa katika uchanguzi wa Luganda kama lugha ya eneo la kati na ambayo hutumika zaidi katika mazingira ya Kampala, utambuzi wa baadhi ya vipashio vya kisarufi vya mofolojia na sintaksia kama ngeli na virai au Sentensi, kuchanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti wao uliochunguza uhamishaji wa mofosintaksia ya Kiluo ambayo ni lugha ya Kinailotiki kwa Kiswahili ambayo ni lugha ya Kibantu katika miundo ya maneno na tungo, utafiti huu ulichunguza athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, zote zikiwa ni lugha za Kibantu nchini Uganda. Utafiti huu uliegemea kuchunguza vipashio vya kimofosintaksia, kanuni za mifanyiko ya Luganda na Kiswahili, na kutathimini athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Jerro (2018), katika uchunguzi linganishi wa vipashio vya kimofolojia na kifonolojia vya Kiswahili na lugha zingine tano za Kibantu ikiwemo Luganda, Kinyarwanda, Gikuyu, Kihaya na Proto- Bantu, alitambua kuwa Kiswahili hudhihirisha tofauti za kiisimu ikilinganishwa na lugha nasaba kinyume na matarajio kuwa lugha zilizo na makutano na mtagusano huathiriana na kusababisha mabadiliko. Akilinganisha ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu, alitambua kuwa Kiswahili kimeainishwa kikiwa na ngeli 16, ikilinganishwa na Luganda iliyo na ngeli 21 kama zilivyo lugha za Proto-Bantu kimofolojia na kifonolojia. Aidha, Luganda hushirikisha matumizi ya vibainishi vya ngeli katika tungo kimofosintaksia kubainisha neno kuu na maneno mengine katika tungo pamoja na dhana za uyaikinishi na ukanushaji. Utafiti wake Jerro (Keshatwajwa) ulikuwa kielelezo cha kuchanganua uwiano na tofauti za ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kwa madhumuni ya kubaini jinsi kipashio cha nomino katika ngeli hufanana na kutofautiana kimofosintaksia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Asiimwe (2019) alilinganisha ngeli za lugha ya “Runyaçitara” inayozungumzwa magharibi mwa Uganda ambayo inajumuisha lugha nne za Kinyankole, Rukiga, Rutooro na Lunyoro kwa kuzingatia viambishi, maana na dhima za viambishi hivyo katika lugha hizo. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kwamba lugha hizo zina mfanano wa hali ya juu unaodhihirisha mahusiano ya karibu wa lugha hizi za Kibantu. Ingawa Asiimwe (keshatajwa) alilinganisha lugha za Kibantu nchini Uganda, hakuhusisha ngeli za Kiswahili na lugha aliyolinganisha pamoja na kuonyesha uwiano na tofauti za lugha hiyo ya “Runyaçitara ama lugha nyingineyo na Kiswahili sanifu. Hata hivyo, utafiti wake unawiana na utafiti huu kwa kuwa unajihusisha na isimu linganishi ya lugha za Kibantu. Utafiti wake uliweka misingi ya uainishaji na ulinganishi wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia na kuonyesha jinsi ngeli za Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana katika matumizi kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo.

Gibson, Mapunda, Marten & Taji (2019) walielezea kiwango cha mfanano na tofauti katika mofolojia na sintaksia baina ya lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki kutumia vigezo 142 vinavyohusisha sehemu maalumu za mfumo wa sarufi. Matokeo ya ulinganishi wao ulibainisha kwamba, kwa upande mmoja lugha hizi zinafanana kisarufi, lakini kwa upande mwingine zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya ulinganishi wa lugha za Uganda ulibainisha kwamba lugha za kundi la kaskazini za Kinyoro (JE11), Kinyole (E35), na Kiganda (JE15), zote zina uhusiano zaidi ya asilimia 70 baina yao kimofolojia na kisintaksia. Utafiti wao ulisababisha pengo la mahitaji ya kufanya ulinganishi baina ya lugha za kundi ya

JE (Kaskazini) na kundi la G (Kusini) ili kubaini uwiano na tofauti kwa ajili ya ujifunzaji hasa baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Lugha hizi ni lugha ambazo zina ukuruba na zinazotumika katika mazingira ya kijiografia tofauti moja ikiwa lingua franka na nyingine lugha asili ya Kijamii na ambazo zote zinafundishwa na kutumika nchini Uganda.

Chege (2020), akichunguza Pragmatiki ya kirai nomino katika sintaksia ya Kiswahili, alibainisha kuwa sentensi ni kipashio cha juu kabisa katika tungo chenye muundo wa kiima na kiarifu ambacho hutoa taarifa kamili. Katika maelezo yake juu ya kiima, alitambua kuwa kiima hubeba kirai nomino na nomino ni kipashio muhimu katika kiima ambacho hutawala mpangilio wa maneno mengine katika sentensi nzima. Kulingana na mtazamo wake, nomino hufanya muundo wa kirai nomino kuwa na mchango chanya katika sintaksia ya Kiswahili. Utafiti wake ulitambua nomino kama kipashio cha kirai nomino na sintaksia kama kipashio cha kimofosintaksia. Mbali na kuwa utafiti wake ulichunguza pragmatiki ya kirai nomino katika sentensi za Kiswahili kwa kujadili pragmatiki ya kirai nomino kimatumizi katika Kiswahili kutokana na mpangilio wa virai nomino na changamoto zinazowatinga wanafunzi wa shule za upili, vyo na vyo vikuu, ulisaidia kutoa mwanga kwa utafiti huu katika kutambua na kueleza vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu ambavyo vimekitwa katika mfumo wa sentensi ili kubaini kufanana na kutofautiana kwa vipashio hivyo kimofosintaksia, kanuni za mifanyiko ya matumizi ya vipashio hivyo na mwingiliano wa vipashio hivyo katika mfumo wa sentensi za Kiswahili ili kutathimini mwingiliano wa vipashio vya kisintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili wilayani Kampala, Uganda.

Uchanganuzi wa kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia kwa mujibu wa mapitio kunadhihirisha kuwa, kufanana na kutofautiana kwa miundo ya kimofosintaksia ya lugha na mifumo ya jamii ya matumizi ya lugha ni muhimu sana katika ujifunzaji na matumizi ya lugha L1 na L2. Utambuzi wa uwiano na tofauti za mifumo hii ni muhimu katika kutabiri miundo inayorahisisha ujifunzaji na matumizi na ile inayowatatiza wanafunzi. Aidha, licha ya natija za uchanganuzi huu, umebainika kuwa kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya lugha ndiko kunakosababisha matatizo katika matumizi miongoni mwake ikiwa uhamishaji wa miundo na mifumo ya kimofosintaksia ya L1 katika matumizi ya L2.

2.3 Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya mofosintaksia ya lugha

Guthrie (1971) anafafanua kuwa sintaksia za lugha za Kibantu huhusiana katika mpangilio wa vipashio vinavyounda sentensi. Kwa kuzingatia madai haya, utafiti huu ulichunguza mpangilio wa vipashio vinavyounda sentensi za Kiswahili na kanuni maalumu katika sentensi kati ya Luganda na Kiswahili ambazo ni lugha za Kibantu kuchanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi shuleni kutathimini athari za mwingiliano wa L1 katika L2. Aidha, utafiti huu ulichanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi, ili kutathimini namna mwanafunzi ambaye L1 ni Luganda na ambaye anajifunza Kiswahili kama L2 anavyotumia vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi katika muundo wa sentensi za Kiswahili. Ulichunguza uhusiano wa kanuni za matumizi ya vipashio vinavyounda sentensi kati ya Luganda na lugha ya Kiswahili, kuchanganua jinsi muundo wa sentensi za Luganda na Kiswahili huhusiana, kuingiliana na kuathriri matumizi ya Kiswahili sanifu kama inavyoundwa na kutolewa na mwanafunzi ambaye anajifunza Kiswahili kama L2 na ambaye L1 ni Luganda.

Nurse & Spear (1985) walitambua kuwa mfumo wa ngeli za majina katika lugha za Kibantu hasa katika uundaji wa msamiati na upachikaji wa maumbo ya umoja na wingi na upatanishi wa kisarufi unahusiana katika uambishaji wa viambishi. Nurse na Wenzake (1985) wanatoa maelezo juu ya ngeli na upachikaji wa maumbo ya umoja na wingi na upatanishi wa kisarufi katika sentensi. Matokeo ya utafiti wao yalikuwa kielelezo cha utafiti huu unaohusu uchanganuzi wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika kiwango cha matumizi ya ngeli katika miundo ya maneno na sentensi kuonyesha uundaji wa maneno na upatanifu wa kisarufi. Aidha, utafiti huu ulitathimini mwingiliano wa mikondo na maumbo ya upachikaji wa viambishi vya umoja na wingi katika maumbo na vipatanishi vya kisarufi vya Luganda katika matumizi ya sentensi za lugha ya Kiswahili sanifu katika vipashio vya kisarufi vya ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi hali ambayo haijawekwa bayana na utafiti wa awali ili kuwekaka bayana athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wazungumzaji ambao L1 ni Luganda na ambao wanatumia Kiswahili kama L2.

Cummins (2000) & Obondo (2007) waligundua kuwa umilisi na tajiriba ya lugha ya mama huathiri usanifu na matumizi ya lugha ya pili. Hali hii inathibitishwa na Tembe & Norton (2008) katika uchunguzi wa upataji wa lugha ya pili, wanaonyesha kuwa kiwango cha umilisi

na usanifu wa lugha ya kwanza (L1) una athari za moja kwa moja katika matumizi na usanifu wa lugha ya pili (L2). Mbali na kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha zinazotoka katika asili moja ya lugha za Kibantu, zinatofautiana katika viwango vya umilisi, moja ikiwa L1 na nyingine L2. Hii ina maana kuwa lugha hizi mbili zina uwezo wa kuingiliana na kutagusana kutokana na umilisi na viwango vya kimofosintaksia vinavyojenga misingi ya kisarufi. Pili, usawia wake unatokana na kuwa lugha hizo zote ni lugha za Kibantu, moja ikiwa na hadhi ya juu na nyingine ikiwa na hadhi ya chini. Sababu za upungufu wa usanifu miongoni mwa watumizi hazijulikani na hivyo ni muhimu kuchunguza ili kuchanganua kisarufi matokeo ya matumizi kuzingatia dhana kuwa lugha mbili zinazokaribiana huweza kuingiliana katika kiwango cha mofosintaksia. Utafiti huu ulizingatia umilisi na tajiriba ya wazungumzaji, kufafanua na kueleza mwingiliano wa kimofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili hasa ukiegemea katika ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi kama vipashio vya kimofosintaksia.

Kulingana na Hyman & Katamba (2001), Katamba (2006) na Lewis (2009) Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha mbili tofauti zenye mifumo ya kipekee ya kiisimu ya fonolojia, mofolojia na sintaksia zinazotofautiana hata ingawa zote ni lugha za Kibantu. Upekee wa lugha hizi ndio unaozitambulisha na kuzitofautisha lugha hizi kiisimu hasa katika matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu. Aidha, ulinganishi wa mofolojia na sintaksia baina ya lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki kukiwemo Luganda na Kiswahili, zilidhihirisha kwamba kwa upande mmoja lugha hizi zinafanana kisarufi, lakini kwa upande mwingine zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya ulinganishi baina ya Luganda ambayo ni lugha ya kaskazini ya kundi la Kibantu la JE15 na Kiswahili ambayo ni lugha ya kusini ya kundi G42, ulibaini kuwa lugha hizi hutofautiana kwa asilimia 57 (Gibson, H., Mapunda, G., Marten, L., & Taji, J., 2019). Licha ya kueleza juu ya kufanana na kutofautiana, mataokeo yao hayakuonyesha wala kuchanganua kanuni za mofosintaksia ya Luganda na jinsi inavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulichunganua kanuni za Luganda na kuonyesha jinsi kanuni za Luganda na Kiswahili huingiana na kauthiri matumizi ya vipashio vya Kisarufi vya Kiswahili sanifu.

Katamba (2003) katika kueleza muundo wa Luganda kama lugha ya Kibantu, alijaribu kueleza kuhusu sintaksia ya Luganda na kusema kuwa lugha ya Luganda kama lugha za Kibantu hushirikisha vipatanishi vya kisarufi vya ngeli katika muundo wa sentensi. Anaonyesha mfumo wa kuzingatiwa hasa kwa kufuata mofimu za umoja na wingi katika

sentensi. Vile vile anaeleza kuwa katika kila ngeli ishirini na moja za Luganda, kila ngeli imepewa mofimu ya kuianisha kama ngeli tofauti na ngeli zingine, na kila nomino katika kila ngeli huwa na kipatanishi chake kinachowakilisha kundi la nomino ama ngeli husika. Kwa mujibu wa Katamba kama inavyofafanuliwa katika Nurse na Philippon (2006), kila nomino ina viambishi vinavyowakilisha umoja na wingi wa nomino na umoja na wingi wa nomino katika sentensi ambayo huwa na Kiima – kiarifa – Kiima. Ingawa Katamba alieleza swala la ngeli kimofolojia na kisintaksia, hakuweka bayana mwingiliano uliopo wa kanuni za matumizi ya kipashio cha ngeli kati ya Luganda na lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulichanganua kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia za Luganda katika Kiswahili sanifu, uhusiano na tofauti zilizopo kati ya kanuni za Luganda na lugha ya Kiswahili ili kudhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu.

Wanaisimu Kihore & Massamba, (2003) wanafafanua ngeli kuwa mgawanyo wa aina mbalimbali za nomino katika mitazamo ya kisarufi. Aidha, wanaendelea kueleza ngeli kama kundi moja la majina yaliyo na upatanishi wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana. Peterson (2017) naye anafafanua ngeli kuwa utaratibu wa kugawanya majina katika makundi kwa kuzingatia vigezo vya kisarufi vya mofolojia, sintaksia na semantiki. Kwa mujibu wa maelezo hayo, ngeli za nomino ni utaratibu wa kuianisha nomino katika makundi mbalimbali kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Kila lugha huwa na ngeli za nomino ambazo hutofautiana na kuingiliana. Kutofautiana huku na kuingiliana husababisha athari za lugha moja kwa nyingine. Kulingana na Adewole (1986), upangaji wa nomino katika makundi kadha unategemea kwa kiasi kikubwa uhusiano uliopo baina ya nomino na maneno mengine. Uhusiano huo hutegemea uainishaji wa nomino na matumizi yake yanayozingatia uhusiano wa nomino kama neno kuu kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo. Uhusiano huo unatokana na uambishaji wa viambishi au mofimu za ngeli zinazowakilisha maana ya umoja na wingi kama vile uhusiano wa nomino na kitenzi, nomino na kivumishi, nomino na kiwakilishi, nomino na kihusishi. Muundo wa nomino na matumizi yake katika sentensi ni muhimu sana kwa sababu matumizi yake hubeba vipashio vya kimofosintaksia unaodhihirisha muunganiko wa nomino na maneno mengine katika tungo kuonyesha jinsi nomino inavyomiliki na kutawala maneno mengine katika sentensi. Uhusiano huo hubeba sifa za kimofosintaksia kutokana na nomino kuanishwa katika makundi ya ngeli mbalimbali kimofolojia na kisintaksia.

Utafiti huu ulichukulia kwamba, kufanana na kutofautiana kwa vipashio vinavyowakilisha nomino katika muundo wa sentensi husababisha mwingiliano ambao husababisha athari za lugha moja kwa nyingine. Kwa hivyo uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu kuhusiana na matumizi ya nomino katika sentensi. Uchanganuzi huu hudhihirisha uhusiano wa nomino kumiliki na kutawala maneno mengine kutokana na vipashio vya kimofosintaksia vya nomino vinavyojitokeza katika tungo. Aidha, uchanganuzi huu ni msingi wa kutathimini jinsi kanuni za kimofosintaksia za Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Kutokana na Maelezo ya wataalamu hawa (wemeshatajwa), utafiti huu kuchanganua kanuni na miundo ya uainishaji wa nomino kama kipashio cha kimofosintaksia katika ngeli za Luganda na Kiswahili, kueleza, kuchanganua na kutathimini athari za kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama inavyotumika katika mchakato wa mofosintaksia miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda na ambao ni wanafunzi wanaotumia Kiswahili kama L2 shuleni.

Trommer (2003) katika utafiti wake uliohusiana na mwingiliano wa mofolojia na sintaksia katika utaratibu wa upangaji wa viambishi vya kiima katika sentensi, aligundua kuwepo kwa mwingiliano wa mofosintaksia ambao hufuata upatanifu wa kisarufi wa nomino katika kiima hasa katika sarufi ya karibu lugha zote za Kibantu na katika lugha mahususi hasa lugha za Kibantu kimaandishi na kimazungumzo. Utafiti wa Trommer (keshatajwa), ulichunguza kwa ujumla kanuni ya upatanifu wa kisarufi wa viambishi vya kiima wa lugha kwa jumla kutambua ikiwa vinafuata kanuni ya upatanifu kama inavyoelezwa na wanaisimu wakongwe katika sehemu za sentensi, huku utafiti huu ukichunguza mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili fasaha. Utafiti wake ulichangia katika kutambua kanuni na miundo ambayo utafiti huu ulichunguza kutambua athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili. Aidha, utafiti huu ulikuwa kielelezo cha utafiti huu hasa kuchunguza kanuni za mofosintaksia ya Luganda na jinsi inavyotumika katika matumizi ya Kiswahili fasaha ikiongozwa na nadharia ya upatanifu na uhusisho ya Chomsky ya 1981.

Nicola & Montermini (2005), walijadili sifa za jumla za kimofolojia za uambishaji wa viambishi katika maneno na tungo. Katika utafiti wao, walijadili uwiano wa sifa za matumizi ya viambishi kutoka lugha mbalimbali. Uchanganuzi wao uligundua kuwa lugha nyingi hutumia vibainishi zaidi kuliko viambishi awali katika muundo wa kimofosintaksia. Aidha, walitambua kuwa lugha nyingi hupenda kutumia viambishi tamati kuliko viambishi katikati

au kuweka viambishi baada ya mzizi. Kwa mujibu wa uchanganuzi wao, lugha ambishi huzingatia utaratibu wa kutanguliwa na kitenzi kama neno kuu likifuatwa na yambwa au kiwakilishi cha kiima, huku lugha ambazo huambisha viambishi tamati hutanguliwa na kiima kama neno kuu likifuatwa na kitenzi katika mfumo wa kisintaksia. Utafiti wao ulichunguza viambishi kimofolojia na kisintaksia na hivyo kutoa mwelekeo wa kuchanganua vipashio vya kisarufi vilivyohusika kimofolojia na kisintaksia katika tungo. Aidha, utafiti huu ulichunguza lugha mbili Luganda na Kiswahili ambazo ni lugha ambishibainishi. Uliegemea kuchunguza uambishaji wa viambishi ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi, njeo na vikanushi katika mchakato wa matumizi ya vipashio hivi na wanafunzi kuzingatia kanuni za mifanyiko husika katika utungo.

Utafiti wao ulichangia pakubwa vipashio vya mofosintaksia vya uambishaji na utaratibu wa upangaji wa vipashio katika tungo za lugha ambishibainishi bila kudhihirisha kanuni za uambishaji. Kwa hivyo, utafiti wao uliusukuma utafiti huu kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu kwa kuzingatia matumizi ya viambishi katika mpangilio wa vipashio vya sentensi kuonyesha uhusiano wa vipashio vikuu kuunganika kumiliki na kutawala vipashio vingine katika tungo. Ulichanganua kanuni za uambishaji wa viambishi vipatanishi vya kisarufi vya nomino (ngeli), vivumishi na viwakilishi na viambishi (mofu) vikanushi na njeo katika sentensi kuzingatia sifa za kila lugha. Aidha utafiti huu ulichanganua kanuni za mifanyiko au taratibu zinazohusika katika uambishaji viambishi na mofu za njeo na ukanushaji na kuuwongoza utafiti huu kutathimini athari ya matumizi ya vipashio vya kisarufi vya mofosintaksia vya Luganda katika Kiswahili sanifu.

Rapando (2005), akichunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi, aligundua kwamba baadhi ya makosa ya kimofosintaksia yalisababishwa na ujumlishaji wa vipashio na matumizi ya kanuni za lugha ya kwanza, Kiingereza na Sheng ambayo yalijitokeza katika kirai kitenzi. Tofauti na utafiti wa Rapado uliochunguza makosa ya kimofosintaksia za wanafunzi wa shule za upili waliokuwa na asili anuwai ambao huenda hawana makosa ya sampuli ya kutabirika, utafiti huu ulichanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutumia mihimili ya nadharia ya ufungami na utawala miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda. Utafiti wa Rapando (2005) ulichangia utafiti huu katika kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu

katika matumizi kama msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Aikhenvald (2006) alitambua kuwa hata ingawa ngeli za nomino huwakilisha upatanishi, kuna idadi ndogo sana za ngeli ambazo hufuata mfumo huo. Kila nomino katika lugha imewekwa kwa ngeli moja na nyingine kuwekwa katika zaidi ya ngeli moja. Mbali na kuainisha ngeli kuzingatia kanuni za kimofolojia na kisintaksia, uainishaji wa kisemantiki pia umetumika katika baadhi ya maneno kuwakilisha uana. Kwa maoni yake, uainishaji wa ngeli hutegemea lugha husika kwani lugha hutofautiana. Matokeo ya utafiti wake kuhusu ngeli uliungoza utafiti huu katika kulinganisha na kulinganua ngeli za lugha ya Kiswahili na Luganda ambazo ni lugha za Kibantu kwa madhumuni ya kuchanganua kanuni za mwingiliano wa mofolojia na sintaksia ya Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kiisimu. Utafiti huu uliainisha ngeli kimofolojia na kisintaksia kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ili kubaini mwingiliano wa lugha kimofolojia na kisintaksia. Utafiti huu ulieleza, kuchanganua na kutathimini muundo wa nomino na mpangilio wake kisarufi katika mchakato wa vishazi na sentensi kubaini umantiki wa upatanisho wa kisarufi, hasa kwa kuchunguza uambishaji wa viambishi kisintaksia na kimofolojia, kuchanganua uhusiano na tofauti zinazosababisha mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Ambuyo (2007) akiwanukuu wanaisimu Noam Chomsky (1981) na Habwe na Karanja (2004), wanaeleza kuwa sintaksia inaweza kuelezwa kwa misingi ya vijenzi vya kisarufi ambavyo utafiti huu unavitambua kuwa vipashio vya kisarufi, miundo ya kisintaksia na kanuni za uundaji wa virai na sentensi. Aidha, anaeleza kuwa sintaksia hujihusisha na namna ambavyo maneno huunganishwa ili kuunda virai na sentensi kamili pamoja na kanuni zinazotawala ufasiri kamili wa viambajengo vya sentensi na virai. Anaeleza kuwa kipashio cha sintaksia ni cha muhimu katika lugha kwani hushirikiana na mofolojia na fonolojia kwa kuongozwa na kanuni kujenga sentensi sanifu ya lugha. Ili kuthibitisha madai haya, alifanya utafiti juu ya uamilishi dhima katika sentensi ya Luloogoli na kutambua kuwa muundo wa kisintaksia wa sentensi za Luloogoli hutawaliwa na kanuni bia za utegemezi muundo, ufungami na kanuni leksia zote zikifungamana na kanuni ya upatanisho wa kisarufi. Vilevile alitambua kuwa uhamisho dhima wa sentensi ya Luloogoli huongozwa na kanuni ya upatanishi wa kisarufi na huathiri muundo wa sentensi kwa ujumla. Anapendekeza utafiti zaidi kufanywa ili kubainisha ikiwa kunaweza kuwepo na uhamisho katika lugha nyinginezo

ili kubainisha bayana vibainishi na vipatanishi. Matokeo ya utafiti wa Ambuyo (keshatajwa) uliuongoza utafiti huu kuchanganua kanuni za vipashio vya kisarufi alivyoeleza vya uundaji wa sentensi kama vile vivumishi, ngeli, viwakilishi nafsi na vikanushi, miundo na kanuni ya matumizi ya Luganda katika Kiswahili sanifu, kutathimini athari za mwingiliano wa vipashio, kanuni na miundo ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Ingawa utafiti wake na utafiti huu unachunguza kanuni na muundo katika matumizi ya vipashio vya kisarufi, unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa utafiti wake ulichunguza uamili dhima katika sentensi ya Luloogoli huku utafiti huu ukichunguza athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Downing (2011) alifanya utafiti wa kina wa kiarudhi kwa kuchunguza uhusiano wa kiarudhi wa fonolojia na sintaksia na kueleza tofauti kati ya mofosintaksia, fonolojia na sintaksia ya lugha za Kibantu kuhusu miundo wa kiulizi 'nini'. Utafiti wa Downing ulichunguza sifa za kiarudhi za lugha za Kibantu za Chimwiini, Luganda, chewa, Fiba, Tumbuka, na situ. Utafiti wao unatofautiana na huu kwa kuwa utafiti huu ulichunguza sifa za kiarudhi za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Ulijikita kuchunguza kanuni na miundo ya matumizi ya vipashio vya kisarufi vya Luganda katika Kiswahili. Utafiti wao ulichunguza fonolojia na sintaksia na tofauti za sifa za kiarudhi zinazojitokeza katika fonolojia, sintaksia na mofosintaksia huku utafiti huu ukichunguza sifa za mofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Downing ulijaribu kuelezea mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda na Lahaja ya Chimwiini ambayo ni mojawapo ya lahaja ya Kiswahili Somalia. Utafiti wake licha ya kuwa tofauti ulichangia pengo la kuchunguza mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Mchango wa utafiti wa Downing ni kuwa ulichunguza arudhi za mofosintaksia hali ambayo uchunguzi huu umejikita hasa kuchunguza kanuni na miundo ya Luganda na jinsi zinavyoathiri matumizi katika lugha ya Kiswahili.

Joy (2012) akichunguza dosari za kisintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiidakho waishio Kenya, alibaini dosari za matumizi yasiyo sahihi ya viambishi awali vinavyowakilisha mtenda, matumizi yasiyo sahihi ya viambishi vinavyobeba dhana ya ukubwa, udogo na vimahali na uchanganyaji wa ngeli za nomino za Kiidakho na za Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti wa Joy, uliochunguza dosari za kisintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiidakho, nchini Kenya, utafiti huu ulitathimini kanuni za

kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu nchini Uganda. Hata ingawa utafiti wa Joy (keshatajwa) unatofautiana na utafiti huu, Utafiti wake, ulinufaisha utafiti huu katika kuchanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika kuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio vya sintaksia vya nomino na matumizi ya viambishi awali vinavyowekwa katika vipashio vya kimofosintaksia vya tungo za Luganda na Kiswahili sanifu kuwakilisha umiliki na utawala wa vipashio vikuu katika tungo. Kwa kuzingatia matumizi ya vipashio vya kisintaksia vya nomino na viambishi awali vililivyochunguzwa na Joy, utafiti huu uliweza kuchanganua na kutathimini kanuni zinazofafanua matumizi ya nomino na uambishaji wa viambishi katika vipashio vya kimofosintaksia vinavyounganika na vipashio vingine kuonyesha uhusiano wa kipashio kikuu kumiliki maneno mengine (upatanishi wa kisarufi) katika tungo hasa katika nomino za ngeli ya i-zi na nomino zinginezo, kudhihirisha jinsi matumizi haya huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Kithuku (2012) katika uchanganuzi wake juu ya mofosintaksia ya ngeli ya 9/10, alichanganua ngeli ya 9/10 ya N/N kwa kutumia kigezo cha uainishaji wa kimofolojia. Kanuni ya uingizaji wa nomino za mkopo na nomino asili za Kibantu na zilizobuniwa ambazo huwekwa katika ngeli ya 9/10 na utata wa upatanishi wa kisarufi unaohusiana na ngeli hii na nomino za ngeli zingine ulichunguzwa. Utafiti wake uligundua athari za mwingiliano wa ngeli hii na ngeli zingine. Vilevile iligunduliwa kuwa ngeli hii ilikuwa na nomino nyingi za mkopo na chache za Kibantu kwa kukosa viambishi (M) na (N) na kuwatatiza wanafunzi wa shule za upili katika kuchanganua upatanishi wa kisarufi wanapotumia nomino hizo kimsamiati, mpangilio wa maneno katika utungaji sentensi, uteuzi wa msamiati usiofaa na uainishaji wa nomino zingine katika makundi ya ngeli. Hivyo, utafiti wake ulinufaisha utafiti huu katika kuchunguza kanuni za utungaji wa sentensi, uchanganuzi wa kanuni za matumizi ya ngeli na uainishaji wa nomino katika makundi ya ngeli kama vipashio muhimu vya mofosintaksia vya Luganda kama msingi wa kutathimini mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Vilevile, utafiti wake kama ulivyo utafiti huu, uliongozwa na mihimili ya nadharia pana ya utawala na ufungami ya Chomsky (1981). Aidha, utafiti wa Kithuku (ametajwa) ulitofautiana na utafiti huu katika upeo wa vipashio vya uchunguzi ambapo, alichunguza tu mofosintaksia ya ngeli ya 9/10 na ngeli nomino zingine kwa kuhusisha nadharia ndogo za uhusika, eksibaa, ufungami na utawala, huku utafiti huu ukichanganua mwingiliano wa kanuni za mofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika vipashio vya kisarufi vya Nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi ili

kuchanganua mwingiliano wa ngeli za Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili ukihusisha mihimili ya nadharia ya ufungami na utawala ya ubia wa lugha na upatanisho.

Mulei (2014) katika uchunguzi wake kuhusu uchanganuzi wa athari za Kigisu katika mazungumzo kwa Kiswahili, alitambua kuwepo kwa athari za Kigisu uliojitokeza katika uhamishaji wa kanuni za ukanushaji kutoka L1 hadi L2, pamoja na athari za maneno na sauti katika mazungumzo ya Kiswahili. Utafiti wa Mulei ulipendekeza kufanyika kwa tafiti kuhusu lugha zingine za Kibantu katika jamii za Uganda ili kuchanganua athari zinazojitokeza katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti wa awali, utafiti huu ulichunguza athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili shuleni na hasa miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda ukichunguza vipengele vya mofosintaksia vya mofolojia na sintaksia vya nomino katika ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi. Utafiti wa Mulei (keshatajwa), ulichangia utafiti huu katika kuchanganua kanuni za kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Licha ya kuwa utafiti wa awali ilichunguza kipashio cha kisarufi cha ukanunusaji wa Kigisu ambayo ni lugha ya Kibantu katika ujifunzaji na mazungumzo ya Kiswahili, utafiti huo wa awali hukushughulikia miundo na kanuni za kimofosintaksia na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Aidha, utafiti huu ulichukulia kuwa mfanano na tofauti za kanuni za L1 huweza kusababisha mwingiliano wa mofosintaksia katika matumizi ya L2. Kwa hivyo utafiti huu ulichanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi kwa sababu ya upana wa matumizi ya Luganda, ili kutathimini mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda na jinsi inavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Aidha, Utafiti huu ulichagua kuchanganua kanuni za kimofosintaksia ya Luganda kama lugha ya Kibantu ambayo hutumika katika mawasiliano zaidi. Mathalani, matokeo ya athari za mwingiliano ungeweza kupokelewa kwa upana zaidi kuliko lugha nyingineyo ya kibantu nchini Uganda tofauti na utafiti wa awali uliochagua Kigishu ambayo ni lugha ya eneo moja.

Masanja (2014) katika utafiti wake wa mofosintaksia ya ruwaza ya ukanushi katika vitenzi vya lugha ya kisukuma, alibaini kanuni za ukanushaji unaojitokeza katika lugha ya Kisukuma. Matokeo ya utafiti wake yalibaini mofimu kanushi katika lugha ya Kisukuma kujitokeza baada ya mofimu ya nafsi zinapotokea kama mofimu awali, na baada ya mzizi wa kitenzi zinapotokea kama mofimu tamati. Utokeaji huu wa mofimu kanushi ndiyo huruhusu

kuzalisha maumbo kanushi yaliyofikia upeo wa ukubalifu katika lugha ya Kisukuma. Aidha, Kisukuma kama zilivyo baadhi ya lugha za Kibantu inaruhusu utokeaji wa mofimu kanushi zenye kubeba dhima nyingine kama vile njeo au hali katika kitenzi husika. (ukanushaji). Utafiti wake msanjila (keshatajwa) uliongoza utafiti huu kutambua kanuni za utokeaji wa mofimu kanushi katika Luganda na Kiswahili, maumbo kanushi na dhima zake. Ni kutokana na utambuzi huu ndio ulioelekeza katika kueleza kanuni, kuonyesha uwiano na tofauti kwa ajili ya kutathimini mwingiliano wa Luganda katika Kiswahili sanifu.

Obara (2014) akichanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika insha za wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii, aligundua kuwa wanafunzi ambao L1 ni Ekegusii walifanya makosa ya kisarufi katika viwango vyote vya kiisimu vilivyotokana na athari za L1 kwa matumizi ya Kiswahili kama L2. Wanafunzi walihamisha na kujumlisha kanuni za kiisimu za L1 katika matumizi ya vipashio vya kiisimu fonimu, muundo wa maneno, virai, vishazi na sentensi za Kiswahili. Obara (keshatajwa) alipendekeza utafiti zaidi kufanyika ili kuchanganua ubia wa makosa na kueleza zaidi makosa yanayojitokeza katika matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika imla kuchanganua matatizo kwa kina na viwango husika vya athari za L1 katika matumizi ya Kiswahili.

Matokeo na mapendekezo ya Obara (keshatajwa) yaliusukuma utafiti huu kuchanganua kanuni za vipashio vya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika viwango vya maandishi na mazungumzo ya Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti wa Obara uliochunguza vipashio vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia vya fonimu, muundo wa maneno, virai, vishazi na sentensi, na kutathimini kiwango cha athari za lugha ya Ekegusii na jinsi inavyochangia makosa ya kimaandishi katika Kiswahili sanifu, utafiti huu ulichanganua kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda vya nomino, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi katika matumizi ya Kiswahili sanifu ili kutathimini athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Obara, ulichangia katika vipashio vya mofosintaksia vya nomino (ngeli), njeo na upatanishi wa vipashio vyake katika uchanganauzi wa mofosintaksia ya Luganda katika Kiswahili sanifu.

Kirabi (2015) akitathimini na kuchanganua makosa ya kimofosintaksia katika lugha ya maongezi dhidi ya kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu miongoni mwa walimu na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika kata ndogo ya Kangemi, aligundua kuwa makosa mengi ya kimofosintaksia yalitokana na athari za L1. Aligundua kuwa makosa mengi ya

kimofosintaksia yalisababishwa na athari za L1 ya Kikuyu na mazingira dhidi ya kanuni za maongezi za lugha ya Kiswahili sanifu. Ugunduzi wake ulibaini makosa ya kifonolojia na kimofolojia kuathiri kanuni za kimofosintaksia za Kiswahili sanifu. Utafiti wa Kirabi (keshatajwa) uligundua makosa ya kimatamshi ya kuhamisha kanuni za miundo ya lugha ya Kikuyu hadi lugha ya Kiswahili sanifu. Uhamishaji huu wa kanuni ulitokana na uchukuo kuwa lugha ya Kikuyu na Kiswahili sanifu zinafanana kimuundo.

Licha ya kuwa utafiti wa Kirabi, (2015) ulichunguza jinsi lugha asili zinavyoathiri kanuni au miundo ya L1 hasa lugha za Kibantu kama ilivyo utafiti huu, Utafiti wake ulichunguza makosa ya kifonolojia na kimofolojia yanayoathiri kanuni za kimofosintaksia za lugha ya kimaongezi ya lugha ya Kiswahili sanifu, tofauti na utafiti huu uliotathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi. Aidha, utafiti wake ulifanywa miongoni mwa wanafunzi na walimu wa shule za msingi na upili ambao L1 ni Kikuyu, huku utafiti huu ukichunguza mwingiliano wa kanuni ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Utafiti wa Kirabi (keshatajwa) ulichangia pakubwa katika uchanganuzi wa ngeli za Kiswahili na matumizi ya nomino na maneno mengine katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa neno kuu kutawala maneno mengine katika tungo, kueleza kanuni za matumizi ya nomino katika ngeli na kuongoza kutathimini mwingiliano na athari za L1 katika matumizi ya L2 na jinsi kipashio cha mofolojia huathiri sintaksia kuzingatia kanuni za mofosintaksia.

Nyanda (2015) alitambua kuwa mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha mwathiriana wa lugha kutokana na kuwa kila lugha kuchukua baadhi ya msamiati na kanuni kutoka lugha nyingine na kuuingiza katika lugha yake. Aidha, anasisitiza kuwa lugha huathiriana katika viwango vya kiisimu kuanzia fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki kutokana na mwingiliano baina ya wanajamii wa lugha hizo. Vile vile anaeleza kuwa mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti hutokana na ukaribu ama mwingiliano baina ya wanajamii na lugha. Makutano haya ama ukaribu huu husababisha mwingiliano baina ya lugha husika. Kwa mtazamo wake, wazungumzaji wa lugha zilizo karibu wazungumzapo huwa wanadhihirisha tofauti za kiisimu katika viwango vya kiisimu vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki.

Utafiti wa Nyanda (keshatajwa) ulidhihirisha pengo la utafiti huu kwani mara nyingi wanaisimu hueleza tu kuwa lugha za Kibantu ambazo zimekuwa na ukaribu wa muda mrefu

huathiriana na kuingilia. Hata hivyo, kiwango na taathira ya mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu haujawekwa bayana. Kwa hiyo, utafiti wa Nyanda (keshatajwa) ulichochea kufanyika kwa utafiti huu kwa kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimfosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Uchanganuzi huu ulikuwa msingi wa kutathimini mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti katika viwango vya kiisimu vya mofolojia na sintaksia kutokana na ukaribu baina ya wanajamii wa Luganda na lugha husika ya Kiswahili sanifu katika matumizi. Aidha, uchanganuzi wa kanuni ulisaidi kutathimini jinsi kanuni za Luganda na Kiswahili huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu katika vipashio vya kisarufi vya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi.

Onyango (2018) alitambua kuwa ujifunzaji lugha ni tukio la kiutambuzi la mtu kufahamu au kutambua kuwa anajifunza lugha kwa kuzingatia kanuni na muundo wa lugha. Matokeo ya Onyango (keshatajwa) yanatiliwa mkazo juu ya lengo kuu la taaluma ya isimu ambalo linahusiana na uwekaji wazi kanuni zinazotawala lugha ambazo wazungumzaji wanazitumia bila wao wenyewe kujua. Vilevile katika kuweka kanuni hizi, Besha (1994) anasisitiza kuwa jambo la msingi na awali ya yote ni kuwa lazima isimu iendeleze namna gani lugha inavyotumika katika jamii bali sio jinsi ya kuzungumza lugha husika. Besha na Onyango (wametajwa) wanaamini juu ya udhihirishaji wazi wa isimu unaotegemea matokeo ya utafiti juu ya matumizi ya lugha katika jamii kuhifadhi kanuni hizo. Matokeo ya Besha na Onyango yanadhihirisha pengo la utafiti huu juu ya dhima ya isimu. Utafiti huu ulichanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimfosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Ulichunguza mwingiliano wa kanuni za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulikuwa na madhumuni ya kuweka wazi na kuhifadhi kanuni za lugha kutokana na matokeo ya matumizi ya lugha kati ya Luganda na Kiswahili katika vipashio vya mofosintaksia vya ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi na namna wanafunzi wanaojifunza L2 wanavyotumia lugha ya Kiswahili katika vipengele vya kiisimu vya mofosintaksia shuleni.

Abdallah (2018) akichunguza uwiano na utofauti wa kiisimu kati ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi, aligundua kuwa kifonolojia lugha hizi mbili hutofautiana kifonimu na katika baadhi ya kanuni za fonolojia na mofolojia hasa katika matumizi ya vipashio vya kisarufi vya nomino, vitenzi na vivumishi vimilikishi. Vilevile, utafiti wake Abdallah (keshatajwa) ulitambua kuwa Kimakunduchi na Kipaje vinatofautiana katika umiliki wa alomofu za nafsi

ya kwanza na ya pili pamoja na viambishi vya ung'oekaji wa o-rejeshi. Aidha, kisemantiki, ilibainika kuwa Wapaje wameathiriwa na Kiswahili sanifu katika utoaji na uwakilishi wa maana zao. Utafiti wa Abdallah (keshatajwa) ulichunguza uwiano na tofauti za kiisimu za lugha za Kibantu katika nyanja za fonolojia, mofolojia na semantiki tofauti na utafiti huu uliochunguza kanuni za mifanyiko ya vipashio vya kimofosintaksia. Utafiti wake ulitoa mchango wa kimadhumuni wa kubainisha mfanano na utofauti wa vipashio vya kisarufi vya nomino na vivumishi vimikilishi pamoja na kanuni za matumizi na kusaidi utafiti huu katika kutathimini mwingiliano wa vipashio vya mofolojia vilivyo na uamilifu katika sintaksia kudhihirisha athari za L1 katika matumizi ya kanuni za L2.

Utafiti wa Abdallah (keshatajwa) uliuongoza utafiti huu kufananisha na kutofautisha kanuni za kimofolojia za Luganda katika kipashio cha nomino na vivumishi vimilikishi kudhihirisha jinsi zinavyoathiri sintaksia ya Kiswahili sanifu. Kanuni za kifonolojia na kimofolojia zinazotawala mofu zinazounda maneno, udondoshaji, uyeyushaji na umiliki wa alomofu za nafsi ya kwanza na ya pili pamoja na viambishi vya nomino na vimilikishi jinsi hufanana na kuingiliana kuaathiri matumizi ya kanuni ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda ulizingatiwa.

Hyman (2018), akichunguza mwingiliano wa viwakilishi vya nafsi vya lugha za Kibantu baina ya Luganda, Lusoga na Kiswahili sanifu, waliotambua kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili kwa watu wazima hutegemea mfumo wa kisarufi wa lugha yao ya kwanza wa kuhamisha kaida za kisarufi za lugha ya kwanza katika ujifuzaji wa vipashio vya kisarufi vya L2. Matokeo ya utafiti wa wataalamu hawa ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa ulitoa mwanga wa utafiti kufanywa kuhusiana na uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia za matumizi ya vipashio vya Luganda katika kiswahili sanifu, kutathimini kanuni za mofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Mutwiri (2019) katika utafiti wake wa uchanganuzi wa muundo wa sentensi za Kîngembe katika sintaksia, ulibainisha miundo tofauti ya sentensi za Kîngembe na kubainisha sheria zinazotawala uunganishaji wa vipashio vinavyojaliza sentensi ya Kîngembe. Kwa kutumia nadharia ya Eksibaa, Mutwiri (keshatajwa) alitambua vipashio vya sentensi za Kîngembe alivyoviita viambajengo vya virai na vishazi na kufafanua miundo yake kuonyesha jinsi kichwa humiliki viambajengo vingine ili kuunda sentensi mbalimbali. Mchango wa utafiti wake ni kuwa alishughulikia muundo wa sentensi za Kîngembe ambayo ni lugha ya Kibantu

na kutoa mchango kwa utafiti huu kutambua vipashio vya mofosintaksia vya Luganda na Kiswahili ambao umekitwa katika taaluma isimu ya sintaksia, kueleza muundo wa mpangilio wa vipashio hivyo kuzingatia sheria zinazounganisha vipashio hivyo husika kudhihirisha vipashio vikuu kumiliki na kutawala vipashio vingine katika tungo na kuweza kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Utafiti wa Mutwiri (kehstajwa) ulitofautiana na utafiti huu kwa kuwa, ulijishughulisha na muundo wa sentensi ya Kîngembe kwa kubainisha vipashio vya sentensi na kufafanua miundo yake bila kulinganisha na lugha nyingine yoyote ile au kushughulikia uamilifu wa sentensi. Utafiti huu ulichanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kwa kueleza vipashio vya sentensi kiuamilifu kwa kuonyesha sifa za kimofosintaksia za Luganda na Kiswahili ambazo zimekitwa katika miundo ya sentensi na kanuni zinazounganisha vipashio kumiliki na kutawala vingine, ili kutathimini mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Mapitio maandishi kuhusiana na kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia ya lugha yalibainisha kuwa, ingawa kuna tafiti ambazo zimefanyika kuhusiana na kanuni za mifanyiko ya vipashio vya kimofosintaksia za lugha za Kibantu, Kiswahili na Luganda zikiwemo, hakuna utafiti uliofanywa kuchanganua na kudhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za mifanyiko ya vipashio vya Luganda na Kiswahili sanifu. Uchanganuzi na mapitio ya maandishi yalidhihirisha kanuni za upatanishi, kanuni za uhamishaji, kanuni ya uainishaji, kanuni ya uundaji na kanuni ya vijenzi vya kimofolojia na kisintaksia katika mapitio ya maandishi ambazo zilikuwa muhimu katika utafiti huu. Aidha, mapitio ya maandishi haya yalidhihirisha kuwa licha ya kuwa tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusiana na kanuni, ni chache ambazo zimedhihirisha moja kwa moja athari za mwingiliano wa vipashio vya kimofosintaksia vya L1 katika matumizi ya L2. Nyingi zimechunguza moja kwa moja athari ambazo zinajitokeza katika matumizi bila kudhihirisha kanuni mwafaka katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia. Kwa hiyo utafiti huu ulichanganua kanuni za mifanyiko ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda na Kiswahili kwa ajili ya kutathimini athari za mwingiliano wa vipashio vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

2.4 Tathimini za kanuni za mofosintaksia, mwingiliano na athari katika matumizi

Scottman (1970) alifanya utafiti juu ya vikwazo vya upataji wa Kiswahili kama lugha ya pili miongoni mwa jamii za Baganda wanaopatikana nchini Uganda na Baluhya wa Kenya kubaini viwango vya matatizo baina ya Baganda na Baluhya katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha matatizo ya kifonolojia ya mabadiliko ya matamshi ya fomimu /c/ na /k/ miongoni mwa Baganda, huku Baluhya wakiwa na matatizo ya kimatamshi ya fonimu /t/ na /d/. Hali hii ilitokana na wazungumzaji wa lugha hizi kukosa kutambua matamshi ya fonimu kamili ya lugha ya Kiswahili sanifu. Vilevile, utafiti wake uligundua kuwa maingiliano ya leksia na mofolojia yalidhihirika zaidi miongoni mwa Baganda kuliko Baluhya. Aidha matatizo ya upatanishi wa kisarufi ulijitokeza zaidi katika jamii ya Baganda hasa katika vionyeshi vya nafsi tatu, udododshaji wa mofimu za nafsi na matumizi ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili visivyo sahihi katika matumizi. Utafiti wa Scottman (1970) ulinufaisha utafiti huu hasa katika uchanganuzi wa vipashio vya kimofosintaksia vya viwakilishi nafsi, leksia na mofolojia vya Luganda na Kiswahili sanifu kama vinavyotumika na mwanafunzi ambaye anajifunza Kiswahili kama L2 na ambaye L1 ni Luganda ili kutathimini kanuni za mofosintaksia za matumizi ya vipashio hivyo na jinsi huingiliana na kuathitri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Tofauti na utafiti wa Scottman (keshatajwa) uliolinganisha viwango vya matatizo ya ujifunzaji wa Kiswahili baina ya Baganda wa Uganda na Baluhya wa Kenya, utafiti huu ulichanganua mwingiliano wa kimofosintaksia wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ukiegemea kueleza mfanano na tofauti za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni zinazofafanua matumizi ya vipashio na kutathimini kanuni za mofosintaksia za Luganda na jinsi huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Nurse, Hinnebusch na Philippon (1993) wanaeleza kuwa Kiswahili ni lugha ambayo asili yake ni kutoka katika kundi mama la Sabaki. Sabaki ni mama wa makundi ya lugha za Kibantu. Nurse na Philippon (2006) wanaeleza kuwa kuna ithibati za kihistoria, kiakiolojia na kiisimu ambazo zinaonyesha mahusiano ya karibu ya Mame – Swahili na lugha zingine za Kibantu hasa katika vipengele anuwai vya kiisimu vya utaratibu wa unyambulishaji na uambikaji, ngeli za majina, orodha za msamiati wa msingi nakadhalika. Maelezo ya wataalamu hawa yaliweka msingi wa kufafanua mahusiano na mwingiliano wa vipashio vya lugha za Kibantu za Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia, kuchanganua kanuni

zinazofafanua mifanyiko ya matumizi ya vipashio vya kiisimu vya uambishaji, msamiati na ngeli na kutathimini kanuni zinazofafanua matumizi ya vipashio hivyo, kudhihirisha jinsi vinaingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wao Vile vile uliuongoza utafiti huu kuchanganua mofolojia ya maneno na uambikaji wa viambishi vya kisarufi kati ya Luganda na lugha ya Kiswahili ili kuchanganua athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu katika vipashio vya kisarufi husika.

Were (1996) katika utafiti kuhusu athari za L1 katika uandishi wa insha za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili sanifu ambao L1 ni Kibukusu kutoka Kanduyi, Bungoma, alitambua athari za kimatamshi, kisarufi, na kimaendelezo za lugha ya Kibukusu katika maandishi ya insha ya Kiswahili sanifu. Makosa mengi yaliyojitokeza yalitokana na mwingiliano wa lugha hasa makosa ya maendelezo na msamiati yaliyotokana na sauti za lugha ya Kibukusu. Aidha, utafiti wake ulibaini makosa ya wanafunzi kujumlisha sheria na pia kuhamisha sheria kutoka L1 ya Kibukusu hadi L2 ambayo ni Kiswahili Sanifu. Uhamishaji na ujumlishaji huu uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu hasa kaatika tahajia, matumizi ya misamiati na sarufi ya Kiswahili sanifu.

Utafiti wa Were (1996) ulinufaisha utafiti huu katika kueleza na kuchanganua kanuni za vipashio vya kisarufi vinavyodhihirisha uhusiano wa kimofosintaksia wa vipashio vikuu kumiliki na kutawala vipashio vingine (vipashio vya upatanishi wa kisarufi) katika tungo. Utafiti huu ulieleza na kuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya viambishi vipatanishi vya ngeli, vivumishi, viwakilishi vya njeo na ukanushaji kama unavyojitokeza katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi wa Kiswahili sanifu na kutathimini kanuni za mofosintaksia za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia hivyo vya Luganda, kudhihirisha mwingiliano na jinsi matumizi yake yanavyoathiri Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti wa Were uliochunguza makosa ya kisarufi, msamiati na maendelezo katika jamii ya Wabukusu nchini Kenya. Utafiti huu ulijikita katika kutathimini kanuni za mofosintaksia za matumizi ya vipengele vya kisarufi vya Luganda vya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi miongoni mwa wanafunzi nchini Uganda na kudhihirisha jinsi vipashio hivyo vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Tofauti na maelezo ya Nurse & Philippon (2006), yaliyotambua kuwepo kwa mahusiano ya karibu ya kiisimu baina ya Kiswahili na lugha za kibantu, utafiti huu ulieleza mahusiano ya vipashio hivyo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ili kuweza kufafanua uwiano na tofauti

ambazo zinajitokeza katika vipashio vya kiisimu vilivyotajwa, kuchanganua kanuni zinazofafanua matumizi yake na kutathimini kanuni za mofosintaksia za matumizi ya vipashio vya uambishaji, msamiati na ngeli kama vinavyojitokeza katika mazungumzo na maandishi ya wanafunzi wa Luganda ambao wanajifunza Kiswahili sanifu kudhihirisha jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Masebo & Nyangwine, (2008) walitambua kuwa lugha ya Kiswahili ina maingiliano ya muda mrefu na jamii lugha za Kibantu. Hii inatokana na makutano ya lugha ya Kiswahili na jamii lugha za Kibantu ambazo huchukulia Kiswahili kuwa lugha ya pili ama Lingua Franca ya shughuli mbalimbali za kijamii. Katika maelezo yao wanaeleza kuwa athari za lugha za Kibantu zinadhihirika zaidi katika matamshi, maana, msamiati na sarufi. Utambuzi wao ulinufasiha utafiti huu kuchanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika vipashio vya msamiati na kisarufi vya Luganda na Kiswahili sanifu kudhihirisha jinsi vinaingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Aidha utafiti wa Masebo na Nyangwine (washatajwa) ulinufaisha utafiti huu katika vipashio vya uchanganuzi na utathimini vya msamiati na kisarufi. Vipashio hivi ni miongoni mwa vipashio ambavyo ni vya kimofosintaksia ambavyo hutumika kwa pamoja kudhihirisha sifa za kimofosintaksia vya Sentensi. Vipashio hivi huunganika katika tungo kudhihirisha umiliki na utawala wa vipashio vya mofolojia na sintaksia katika miundo ya sentensi. Licha ya kuwa wataalamu hawa (washatajwa) walizungumzia juu athari za lugha za Kibantu katika Kiswahili sanifu katika vipashio vya kiisimu vya matamshi, maana, msamiati na sarufi, Uchunguzi wao haukuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio vya msamiati na kisarufi na jinsi vilivyoingiliana na kuathiri Kiswahili sanifu. Hii inatokana na kuwa kila lugha huwa na kanuni zinazotumika kudhihirisha mpangilio wa vipashio katika tungo kuonyesha uhusiano wa maneno katika tungo kudhihirisha umiliki na utawala wa vipashio vya mofosintaksia. Aidha, tofauti na utafiti wa wao uliochunguza maingiliano ya lugha za Kibantu kwa jumla katika viwango vya fonolojia, semantiki, mofolojia na sintaksia, utafiti huu ulitathimini kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na kuonyesha jinsi huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda.

Chapetón (2008) alichunguza matumizi ya lugha ya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiingereza na ambao L1 ni Kiitaliano. Katika uchunguzi wake, aligundua kuwepo kwa mwingiliano wa L1 katika L2 kisintaksia na kimsamiati miongoni mwa

wanafunzi wa Kiitaliano wanaojifunza Kiingereza kama L2. Wanafunzi hawa walihamisha muundo na maana ya L1 kwa L2 na kusababisha athari za mwingiliano wa L1 kwa L2. Ingawa utafiti wa Chapetón unahusu athari za L1 kwa L2, unatofautiana na utafiti huu. Chapetón alifanya utafiti wake katika jamii ya Wataliano kuchanganua athari za kisintaksia na kimsamiati katika ujifunzaji wa Kiingereza. Huku utafiti huu ukichanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Chapetón (keshatajwa) ulinufaisha utafiti huu katika kutathimini kanuni za kimofosintaksia zinazojikita katika vipashio vya sintaksia na matumizi ya msamiati katika tungo, kuonyesha jinsi vipashio mbalimbali huunganika katika tungo kumiliki na kutawala vipashio vingine katika tungo. Aidha, tathimini ya kanuni za mofosintaksia ya matumizi ya vipashio hivi katika Luganda ilisaidia utafiti huu katika kudhihirisha jinsi vipashio hivyo huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Musa (2008) akichunguza athari za lugha ya Kigweno katika Kiswahili na jinsi zinavyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne, aligundua kwamba, athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili, huathiri matokeo ya mtihani kwa kiwango kikubwa. Kwa kutumia Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ikisaidiwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, alichanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Ugweno katika vipashio vya kitahajia, kimsamiati na kisarufi. Hata ingawa utafiti wa Musa ulishughulikia athari za L1 kwa L2 za lugha za Kibantu kama ulivyo utafiti huu, utafiti wake unatofautina na utafiti huu kinadharia na katika vipengele vikuu vya kiisimu. Utafiti huu ulichanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika vipashio vya kisarufi vya mofolojia na sintaksia vya Nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi katika tungo. Utafiti huu uliegemea kuchunguza mwingiliano wa vipashio vya kiisimu, miundo na kanuni za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Tofauti na utafiti wa Musa (keshatajwa), uliochunguza athari za Kigweno kama L1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 na jinsi zinavyoathiri matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili katika kidato cha nne, utafiti huu ulichanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika kidato cha sita. Musa alichunguza athari za lugha ya Kigweno na jinsi inavyoathiri matokeo mabaya katika mitihani, huku utafiti huu ukichunguza jinsi mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda unavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Katika vipengele vya kiisimu vilivyoshughulikiwa, Musa alishughulikia vipengele vya kisarufi, msamiati na tahajia. Huku utafiti huu ukieleza vipashio vya

mofosintaksia vya Nomino, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanushi. Utafiti wa Musa kwa jumla, ulinufaisha utafiti huu katika uchanganuzi wa vipashio vya kisarufi na kimsamiati ambavyo vinajitokeza katika isimu mofolojia na sintaksia na kuchangia katika kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulichukulia kuwa athari za L1 katika matumizi ya L2 ambayo ni ya kisarufi yalitokana na uwiano na tofauti ya miundo ya vipashio na kanuni za matumizi ya kimofosintaksia baina ya lugha ambazo zinaingiliana na kutofautiana kiisimu.

Gaiza (2011) alionyesha jinsi wajifunzaji wa L2 wanavyojifunza na kupata umilisi wa L2. Katika maelezo yake, alitambua kuwa wanafunzi wanaojifunza L2 hutumia usanifu wa L1, mbinu ya ujifunzaji wa L2 kama vile ujumuishaji, ukopaji, utohozi, kuchanganya ndimi na kadhalika katika kupata umilisi wa L2. Msimamo wa Gaiza (imeshatajwa) ndio uliomsukuma mtafiti nyanjani kuchunguza athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu kuthibitisha msimamo wa Gaiza. Utafiti ulichunguza mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutathimini matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli, njeo, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi kama vinavyotumika na wanafunzi wa Kiswahili ambao lugha yao ya kwanza ni Luganda kuthibitisha madai hayo.

Lusesa (2013), katika utafiti wake juu ya mwingiliano wa L1 na L2 kati ya Kisukuma na Kiswahili nchini Tanzania, alitambua kuwa asili ya tatizo la mwingiliano wa L1 katika ujifunzaji na matumizi ya lugha ya Kiswahili kama L2 miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili, ni hali zao za kutumia lugha ya kwanza kila mara katika mawasiliano yao badala ya kutumia Kiswahili wanachojifunza darasani kama lugha ya pili. Utafiti huu ulitambua athari za kimatamshi, kimsamiati na uhamishaji wa vitamkwa na viambishi kutoka L1 hadi L2, na matumizi ya lugha zaidi ya moja. Tofauti na utafiti wa Lusesa uliochunguza athari za lugha mama ya Kisukuma katika ujifunzaji wa Kiswahili kutokana na mwingiliano wa lugha mbili tofauti za nasaba moja, utafiti huu ulichanganua mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kwa kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya mofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya mofosintaksia ya Luganda katika Kiswahili sanifu kama msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Kulinganana na matokeo ya Lusesa, athari za matumizi ya misamiati na uhamishaji wa vitamkwa kutoka L1 kwa L2 ni wa kimofolojia na vinapotumika katika sentensi huchukua

sifa za kimofosintaksia. Kwa hiyo, utafiti wa Lusesa (keshatajwa) ulitoa mwanga wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika vipashio vya kisarufi vya mofolojia na sintaksia vya matumizi ya viambishi na misamiati ya Luganda katika Kiswahili sanifu kuzingatia jinsi misamiati na viambishi husika huunganika na vipashio vingine katika tungo kudhihirisha sifa za kimofosintaksia za neno kuu kutawala na kutawala maneno mengine katika tungo.

Otiende (2013) katika utafiti wake wa athari za kimofonolojia za Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu, alitambua kuwa uainishaji wa majina katika ngeli ndiyo sifa kuu inayozitambulisha lugha za Kibantu. vile vile, utafiti wake ulibaini idadi ya ngeli 17, zenye viambishi vitangulizi ambavyo hufuatwa na viambishi vibainishi vya ngeli za Kiolusuba. Aidha, kwa kutumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia, Otiende alitambua athari za kifonolojia na kimofolojia ambazo zilijitokeza katika imla, mazungumzo na maandishi ya wanafunzi wa shule za msingi ambao L1 ni Kiolusuba. Vilevile alitambua kuwa tofauti kati ya mifumo ya fonimu na mifanyiko ya kofonolojia ya Kiswahili na Kiolusuba, huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Utafiti huu ulichanganua athari za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya Umilikifu na Unganifu kueleza, na kutathimini athari za vipashio vya kimofolojia na kisintaksia za Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Utafiti wa Otiende (keshatajwa) licha ya kuwa uliainisha na kulinganisha ngeli za Kiswahili na Kiolusuba kimofolojia kama sifa kuu ya kutambulisha nomino katika lugha za Kibantu, utafiti wake uliegemea kuonyesha jinsi nomino hizo zinavyoathirika na baadhi ya mifanyiko ya kifonolojia. Tofauti na utafiti huu ambao kwa kunufaishwa na uainishaji na ulinganishi wa ngeli za Kiolusuba na Kiswahili kimofolojia, uliainisha nomino za Luganda na Kiswahili kimofolojia na kisintaksia, kulinganisha na kulinganua nomino za Luganda na Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia za nomino kama msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoathiri matumizi ya kipashio cha nomino katika tungo za Kiswahili sanifu. Aidha, tofauti na utafiti wa Otiende ulioshirikisha nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia kuchanganua athari za mofofonolojia ya ngeli nomino ya Kiolusuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu, utafiti huu ulishirikisha nadharia ya umilikifu na unganifu katika kuchanganua muunganiko wa nomino na maneno mengine katika tungo kuonyesha uhusiano wa nomino kuunganika na kumiliki maneno mengine katika tungo. Msingi ambao ulitumika kutathimini jinsi kanuni za matumizi ya

nomino (kipashio cha kimofosintaksia) katika Luganda huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kimofosintaksia.

Muriungi & Mbui (2013) walitambua kuwa L1 huingiliana na matumizi ya L2 katika ujifunzaji na umilisi wa L2 miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari katika wilaya ya Imenti Kusini, Kenya. Utafiti wao ulitambua makosa ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia miongoni mwa wanafunzi hasa wakati wanapotumia lugha ya Kiingereza. Aidha, katika utafiti wao walieleza asili ya athari husika kuwa ilitokana na wanafunzi kutumia sana lugha mama ambayo ni L1 katika mawasiliano yao ya kawaida badala ya kutumia Kiingereza wanachojifunza kama L2. Utafiti wao unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa wao walichunguza athari za mwingiliano wa lugha mama (Kibantu) katika ujifunzaji na uzungumzaji wa lugha ya Kiingereza. Tofauti na utafiti wao, utafiti huu uliazimia kuchanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, lugha mbili za kibantu ambazo zimekuwa katika ukuruba na ukinzani wa muda mrefu. Utafiti wao ulichangia upeo wa uchunguzi wa mofolojia na sintaksia, mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Utafiti wao ulinufaisha utafiti huu katika kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu ukiegemea katika vipengele vya kisarufi vya mofolojia na sintaksia vya ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi, ukijikita katika kanuni na miundo ya kimofosintaksia katika matumizi ya vipashio husika.

Chebet (2016) katika uchanganuzi wa mofosintaksia na changamoto za isimu-saikolojia zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Kinandi katika upataji wa Kiswahili kama L2, alibaini kuwa ukiukaji wa kanuni na miundo ya vipashio vya kisarufi vya lugha ambazo ni sheria za sarufi, hupotosha usanifu katika matumizi ya lugha husika, kufa kwa lugha, uundaji wa lugha mpya na kadhalika. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi ambao L1 ni Kinandi wanapotumia Kiswahili sanifu yanatokana na changamoto za isimu-saikolojia, mwingiliano na athari za Kinandi katika Kiswahili sanifu, uchanganuano wa muundo na mchakato wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu.

Utafiti wake ulishughulikia matokeo ya matumizi ya lugha ya mwanafunzi ambaye lugha yake ya kwanza ni Kindandi na ambaye anajifunza Kiswahili kama L2. Utafiti wake ulichunguza vipashio 23 vya kimofosintaksia ambavyo humtatiza mwanafunzi wa Kinandi katika matumizi ya Kiswahili sanifu na changamoto za isimu-Saikolojia ambazo husababisha

mwanafunzi ambaye L1 ni Kinandi kukiuka kanuni na sarufi ya matumizi sahihi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu. Aidha, utafiti wake ulijikita kubainisha vikawazo vya matumizi ya vipashio vya mofosintaksia na sababu za isimu- saikolojia zinazokwamiza upataji wa Kiswahili sanifu kama L2 miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Kinandi. Tofauti na Utafiti wa Chebet (keshatajwa), ulioshirikisha nyanja tatu za kiisimu za isimu mtagusano, mofosintaksia, ujifunzaji na upataji wa L2 na Isimu-Saikolojia kachanganua mwingiliano na athari za matumizi ya vipashio vya Kimofosintaksia katika insha za wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Kinandi, Utafiti huu ulichanganua kanuni za vipashio vya mofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Mbali na kuwa utafiti wa Chebet (2016) unatofautiana kiupeo, utafiti wake Chebet (2016) ulinufaisha utafiti huu katika utambuzi wa baadhi ya vipashio vya kimofosintaksia vya L1 vinavyoathiri matumizi ya Kiswahili I sanifu na kuelekeza utafiti huu katika kutathimini kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya nomino, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanushi vya Luganda, kudhihirisha mwingiliano wa matumizi yake na jinsi mwingiliano huo huathiri matumizi ya vipashio hivyo katika Kiswahili sanifu.

Mpangala (2018) akichunguza mwingiliano wa lugha ya Kimakonde katika kujifunza lugha ya Kiswahili, anaeleza kuwa jamii za lugha mbili zinapojenga uhusiano wa karibu kimawasiliano, mwingiliano hujitokeza. Mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha kuathiriana kwa lugha hizo kutokana na kila lugha kuchukua baadhi ya msamiati kutoka lugha nyingine na kuingiza katika lugha yake. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ya Hooper (1976), utafiti wake ulidhihirisha athari za lugha ya Kimakonde katika viwango vya matamshi, msamiati na maana. Tofauti na utafiti wa Mpangala (keshatajwa), utafiti huu ulichanganua mwingiliano wa kimofosintaksia wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Mpangala, ulinufaisha utafiti huu katika kuchanganua kanuni za matumizi ya misamiati ambayo ni kipashio cha kisarufi kinachotokana na miundo ya maneno kimofolojia na kisintaksia. Uchanganuzi huu wa kanuni ulisaidia katika kuchunguza matumizi ya misamiati (maumbo ya maneno) na jinsi inavyoingiliana na vipashio vingine katika sentensi kudhihirisha sifa za kimofosintaksia, kuweka msingi wa kutathimini kanuni za mofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Ssempuuma (2019), alichanganua mchakato wa matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya uhamishaji wa vipashio vya sentensi kidhima na kisemantiki, vihusishi na hali ya mazoea

kama vinavyotumika na wazungumzaji wa lugha tatu za Luganda, Runyankore- Rukiga na Acholi katika Kiingereza cha Uganda. Matokeo ya utafiti wa Ssempuuma (keshatajwa), yalidhihirisha utokeaji wa mwingiliano wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya uhamishaji wa vipashio vya sentensi kidhima na kisemantiki, vihusishi na hali ya mazoea kutoka L1 hadi L2 kwa kiwango kikubwa. Mwingiliano huu uliathiri Kiingereza kinachozungumzwa nchini Uganda kutofautiana kutegemea asili za lugha hizi. Tofauti na utafiti wa Ssempuuma, utafiti huu ulichanganua na kutathimini kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Ssempuuma ulinufaisha utafiti huu katika uchanganuzi wa kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya sentensi, vihusishi na hali ya mazoea kama yanavyojitokeza katika mazungumzo na maandishi ya wanafunzi wa Kiswahili sanifu ambao L1 ni Luganda. Uchanganuzi huu ulitumika kama msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali hii ilitokana na kuwa vipashio vya kimofosintaksia vilivyochanganuliwa katika Luganda na Ssempuuma ni miongoni mwa vipashio ambavyo utafiti huu ulizingatia katika kutathimini kanuni za mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kudhihirisha mwingiliano na athari za matumizi ya vipashio hivi katika tungo za Kiswahili sanifu. Uchanganuzi ilizingatia matumizi ya vipashio husika katika muundo wa sentensi yenye sifa za kimofosintaksia kudhihirisha jinsi vipashio huunganika kuonyesha uhusiano wa meneno kumiliki na kutawala mengine katika tungo.

Mulei, Amukowa & Ambuyo (2021) wakichunguza athari za kimofosintaksia za ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, walibaini kuwa, Luganda na Kiswahili huainisha ngeli kutumia mfumo mmoja na matumizi yake kuzingatia sheria za kuonyesha upatanishi wa kisarufi wa nomino na maneno mengine katika tungo kimofosintaksia. Aidha, walitambua kuwa uwiano na tofauti za mifumo na matumizi ya sheria za nomino katika ngeli baina ya Luganda ambayo ni lugha asili na Kiswahili sanifu uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Tathmini ya athari za mwingiliano wa kanuni za matumizi ya ngeli yalidhihirishwa miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda waliohamisha maumbo ya ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Walihamisha viambishi vya ngeli tofauti na kuvitumia pasipo, kutumia maumbo ya ngeli kwa njia ya mbadilishano baina ya Luganda na Kiswahili, kuuchanganya maumbo ya ngeli na kujumlisha matumizi ya viambishi vya msingi vya ngeli ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yaliathiri kanuni na matumizi ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya makala haya ya Mulei, Amukowa na Ambuyo

(washatajwa) yalithibitisha na kuongoza utafiti huu katika kutathimini na kuonyesha jinsi kanuni za matumizi ya kanuni za ngeli za Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya ngeli kama kipashio cha kimofosintaksia cha Kiswahili sanifu.

Mapitio haya ya maandishi yalibaini kuwa jamii za lugha mbili zinapojenga uhusiano wa karibu kimawasiliano, athari za mwingiliano hujitokeza. Athari za mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha kuathiriana kwa lugha hizo kutokana na kila lugha kuchukua baadhi ya msamiati kutoka lugha nyingine na kuingiza katika lugha yake. Mathalani tofauti kati ya mifumo na mifanyiko ya vipashio vya kisarufi vya lugha huweza kuathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji. Kwa ujumla matokeo ya mapitio ya wali kuhusiana na kanuni za mifanyiko yalibainisha kuwa ukiukaji wa kanuni na miundo ya vipashio vya kisarufi vya lugha ambazo ni sheria za sarufi, hupotosha usanifu katika matumizi ya lugha husika, kufa kwa lugha, uundaji wa lugha mpya na kadhalika. Licha ya tafiti awali kuchunguza kuhusu kanuni za mofosintaksia na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili, tathimini ya kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika Kiswahili sanifu havijawekwa bayana. Hali ambayo utafiti huu ulitathimini kuweka wazi kanuni na athari za mwingiliano katika matumizi.

2.5 Hitimisho

Mapitio ya maandishi ya utafiti huu yameripoti tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusiana na mwingiliano wa L1 katika matumizi ya L2. Mawazo na utafiti wa wataalamu hawa wote yamefafanua baadhi ya vipashio vya kisarufi vya L1 jinsi huingiliana na kuathiri ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili sanifu. Miongoni mwa tafiti za awali zilichanganua mofosintaksia za L1 katika matumizi ya lugha na jinsi zinavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Tafiti zote hizo zimedhihirisha jinsi mtagusano kati ya lugha moja na nyingine zinavyosababisha mwingiliano na athari za kisarufi za L1 katika matumizi ya L2. Msingi wa mawazo na tafiti za wataalamu hawa yamedhihirisha pengo la kuchanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kudhihirisha namna lugha mbalimbali za Kibantu zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Hata ingawa tafiti za awali zilichangia data zilizodhihirisha athari za mwingiliano wa lugha za Kibantu katika ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili na data kuhusiana na utafiti huu hasa katika kufafanua vipashio vya kimofosintaksia, kuchanganua kanuni na kutathimini kanuni za kimofosintaksia za L1 katika matumizi ya L2, hakuna utafiti uliofanywa kuchanganua mwingiliano wa vipashio vya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu

wala kutathimini kanuni na kuweka bayana athari za mwingiliano wa vipashio na kanuni katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu. Katika mapitio ya maandishi, utafiti uliokaribiana na utafiti huu ulikuwa utafiti wa Scottman (1970) uliochunguza vikwazo vya upataji wa Kiswahili kama lugha ya pili miongoni mwa jamii za Baganda wa Uganda na Baluhya wa Kenya kubaini viwango vya matatizo baina ya Baganda na Baluhya katika ujifunzaji wa Kiswahili kama L2, Chebet (2016) aliyechanganua mofosintaksia na changamoto za isimu-saikolojia zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Kinandi katika upataji wa Kiswahili kama L2, Rapando (2005), aliyechunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi na Oduor, inyani na Kobia (2017) aliyechunguza mofosintaksia ya Kiluo katika Kiswahili sanifu. Hata hivyo, tafiti zao zilitofautiana na utafiti huu hasa katika uchanganuzi wa vipashio vya kiisimu kimofosintaksia kutegemea jamii lugha. Aidha, utafiti huu ulichukulia kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja (za Kibantu) ambazo hufanana kimuundo na kiupatanishi na kutofautiana kutokana na upekee wake kiisimu hasa katika kanuni za matumizi.

Utafiti huu ulichunguza vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hubainika katika sintaksia. Ulitathimini mwingiliano wa kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda kwa kutazama jinsi huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Ulijikita katika kuchunguza mwingiliano wa vipengele vya mofosintaksia vya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi vya Luganda, katika matumizi ya Kiswahili kama L2 katika maandishi na mazungumzo kama yanavyotumika na mwanafunzi ambaye lugha yake ya kwanza ni Luganda. Utafiti huu unatokana kuwa, lugha ni mfumo wenye vijenzi vya msingi vinavyotenda kazi pamoja kwa namna inavyoeleweka kwa utaratibu. Kwa hiyo lugha kama mfumo huwa na vijenzi vyenye sifa ambazo hutegemea sheria fulani zilizowekewa mipaka katika utendaji na ambavyo hujumlisha mfumo wa kifonolojia, kimofolojia, mfumo wa kisemantiki, na mfumo wa kisitaksia na ambao ukiukaji wake husababisha matumizi ya lugha isiyo sanifu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua na kubainisha mbinu mbalimbali zilizotumika katika usampulishaji, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data kuhusu athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda. Utafiti huu ulifanyika nyanjani na maktabani kukusanya data za kimsingi ili kufumbua swala na kutimiza madhumuni ya utafiti. Sehemu hii inaeleza juu ya muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya utafiti na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mkabala wa uchambuzi wa data, uchambuzi wa data na vikwazo vya utafiti.

3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu uliegemezwa katika muundo wa kimaelezo. Kothari (2004) anaeleza kuwa utafiti unaozingatia muundo wa kimaelezo ni ule utafiti wa sayansi jamii ambao huchunguza ili kufahamu tabia, mahusiano na mienendo ya makundi mbalimbali ya wanajamii na sehemu mbalimbali duniani. Cohen & Arieli (2011) wanaeleza kuwa muundo wa maelezo ni hali ya kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na wasailiwa wa utafiti lengwa. Ulitumika nyanjani kukusanya data, kueleza data, kuchanganua data, na kutathimini tabia, mahusiano na kanuni za matumizi ya vipashio vya kiisimu ili kubaini athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Muundo huu ulipangwa kutegemea madhumuni ya utafiti kama ilivyotolewa na wasailiwa walengwa. Muundo huu ulitumika kueleza jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda hufanana na kutofautiana na vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, maelezo hayo yalitumika kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda, kueleza jinsi kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Ufafanuzi na uchanganuzi wa kufanana na kutofautiana pamoja na uchanganuzi wa kanuni ulielezwa moja kwa moja kulingana na jinsi ilivyoandikwa na kufafanuliwa katika vitabu teule vya kiisimu vya Luganda na Kiswahili na mapitio ya kazi za wataalamu maktabani. Matokeo yalifafanuliwa na mifano kutolewa kuonyesha ithibati kutoka vitabuni au data za nyanjani kutokana na mijadala ya wanafunzi. Tathimini ya mwingiliano na athari za kimofosintaksia zilielezwa kutokana na maandishi na mazungumzo ya wanafunzi kama inavyojitokeza kupitia kwa mijarabu na mijadala ya wanafunzi.

3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti lilihusu eneo la kijiografia na mada ya kutekelezwa. Eneo la utafiti ni mahala ambapo kuna data zinazohitajika katika utafiti husika. Utafiti huu ulifanyika Wilayani Kampala, nchini Uganda katika kata tano za Kampala ya kati: Nakawa, Makindye, Kawempe na Rubaga. Utafiti ulifanyika miongoni mwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili katika kiwango cha A. Data ilikusanywa maktabani na nyanjani. Data ilikusanywa kutoka shule teule zinazofundisha Kiswahili Wilayani Kampala. Eneo hili liliateuliwa kwa sababu Kampala ni eneo asilia, makazi asilia, eneo la wazungumzaji asilia wa Luganda kama L1 na makao makuu ya nchi ya Uganda (Katamba, 2003; Kiyinikibi, 2021). Vilevile eneo hili lilichaguliwa kutokana na kwamba shule nyingi zikiwemo shule za msingi, za upili na vyuo vikuu hufundisha Kiswahili kama L2.

Utafiti huu ulijikita katika kuchanganua mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ukiegemea tu kuchunguza baadhi ya vipashio vya kisarufi, kimuundo na kanuni za kimofosintaksia. Utafiti huu upo katika eneo la kithematiki wa isimu linganishi na tumikizi ambao unachanganua mofosintaksia ya lugha za Kibantu za Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, ulichunguza jinsi isimu ya lugha za Kibantu huchangiana, kuingiliana na kuathiriana katika matumizi. Kwa hiyo, ulifafanua jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu hufanana na kutofautiana, kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu na kutathimini jinsi kanuni za mofosintaksia za Luganda zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

3.4 Kundi Lengwa

Kothari (2004) anaelezea kuwa, uteuzi wa walengwa ni utaratibu ambao utafiti hutumia kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli. Kwa mujibu wa fasili hii, kundi lengwa ni jumla ya idadi ambayo kwayo sampuli huchaguliwa. Kundi lengwa katika utafiti huu ni jumla ya wanafunzi wote wa kidato cha sita ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili Wilayani Kampala na ambao L1 ni Luganda. Kundi hili liliateuliwa kulingana na sifa ya kuwa ni wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili, wenye uzoefu wa kiwango cha juu cha kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao na ambao wanatumia Luganda kama lugha asilia nyumbani na wakaazi wa wilayani Kampala. Utafiti huu ulizingatia rekodi ya data ya idadi ya walimu na wanafunzi. Data hii ya idadi ya wanafunzi ilitokana na ripoti ya Chama cha Kiswahili Nchini Uganda, (2019), iliyotambua kuwa idadi ya wanafunzi wa kidato cha sita ni

178. Wilaya ya Kampala ina jumla ya shule 133 za kiwango cha A, miongoni mwa shule hizi, shule 46 pekee ndizo zinazofundisha Kiswahili katika kiwango hiki. Kwa hiyo, Idadi lengwa ni shule za upili 46 zinazofundisha Kiswahili wilayani, na wanafunzi 178 ambao wanajifunza Kiswahili katika kiwango cha A pamoja na vitabu vya sarufi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Licha ya kuwa kuna vitabu vingi vya kisarufi, vitabu nane (8) vya Kiswahili na nane (8) vya Luganda viliteuliwa kwa kusaidiwa na wanafunzi na walimu kidhamirifu. Vitabu vya ziada na matini 8 ya Luganda na 10 ya Kiswahili yenye kutoa sifa za kimofosintaksia za vipashio vya kimofosintaksia viliteuliwa. Kwa jumla vitabu na matini kumi na sita (16) vya Luganda na kumina nane (18) vya Kiswahili viliteuliwa kimakusudina kidhamirufu kutoa taarifa za sifa za kimofosintaksia za Luganda sanifu na Kiswahili sanifu (tazama kiambatisho cha 10)

3.5 Usampulishaji na Sampuli

Usampulishaji ni utaratibu wa kuwapata watafitiwa kutoka kwenye kundi lengwa (Masasa, 2017). Katika utafiti huu, wahusika wa jumla waliochunguzwa ni wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama L2 na ambao L1 ni Luganda, wazungumzaji asilia wa Luganda na wanaoishi Wilayani Kampala. Sampuli ni kundi dogo lililoteuliwa kutoka kwa kundi la jumla ambalo kwalo utafiti huu ulipata data husika kulingana na maelongo ya utafiti.

3.5.1 Mbinu za Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi ndogo au walengwa wa utafiti kutoka katika kundi la jumla au kubwa lenye sifa za kutafitiwa kutegemea madhumuni ya utafiti (Haule, 2014, Athumani, 2015). Walengwa wa utafiti huu waligawanywa katika makundi matatu, kundi la kwanza ni shule za kutafitiwa, kundi la pili likiwa sampuli ya wanafunzi na kundi la tatu likiwa vitabu vya sarufi. Baada ya kupata sampuli ya jumla ya shule za kiwango cha A wilayani Kampala, taksimu za shule za wilayani Kampala zinazofundisha Kiswahili ziliteuliwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu ambapo kutokana na jumla ya shule 46 zinazofundisha Kiswahili katika kiwango cha A, shule 12 ziliteuliwa kushiriki katika utafiti kuwakilisha idadi ya jumla ya shule katika wilaya ya Kampala. Majina ya shule 46 yalipewa nambari na kwa kutumia jedwali la ndio au la, shule 23 ziliteuliwa zikiwa na nafasi sawa ya kushiriki katika utafiti. Kwa kuwa idadi ya shule 23 ilikuwa bado kubwa, mtafiti alihusisha tena mbinu ya usampulishaji nasibu ambapo shule 12 zilipata nafasi ya kushiriki katika utafiti. Mbinu hii ilitumika kuteua sampuli ya shule bila ubaguzi kwa kuwa kila shule na mwanafunzi alikuwa na nafasi sawa ya kushiriki katika utafiti.

Mbinu ya usampulishaji mpokezano dhamirifu ilitumika kuwatambua wanafunzi ambao L1 ni Luganda na wanaojifunza Kiswahili kama L2 katika kidato cha sita. Kwa kutumia mbinu ya mpokezano dhamirifu, utafiti uliteua msailiwa katika eneo la utafiti, na kuwaongoza kuwateuwa wasailiwa walengwa wengine wenye sifa za kuwa na umilisi wa Luganda kama L1 miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha sita wilayani Kampala. Uchaguzi wa wasailiwa walengwa ulizingatia vigezo vya asili na eneo la kijiografia kwa mujibu wa Guthrie (1948), umilisi wa kiisimu, matumizi, utambulisho, sifa za kitaipolojia kwa mujibu wa Chomsky (1965), Brown (2005), Nicuolo (1991), Pokorn (2005) na Skutnabb-Kangas (1981). Wanafunzi asili na wazaliwa wa eneo la Kampala, ambao wana uamilifu wa kutumia Luganda kama L1, wanaojitambulisha kutoka katika kabila la Wabaganda na wanaodhihirisha sifa za kitaipolojia katika matumizi ya Luganda na ambao ni wanafunzi wa kidato cha sita wanaojifunza Kiswahili kama L2 ndio waliochaguliwa kushiriki katika utafiti huu.

Kwa jumla wanafunzi 54 waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu kutokana na sifa zao za kuwa wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha sita na ambao L1 ni Luganda kutoka kwa jumla ya wanafunzi 178. Kwa kutumia usampulishaji dhamirifu kufikia kiwango kinachotosheleza mahitaji ya utafiti ambapo hakuna swala lingine jipya linalojitokeza, vitabu nane (8) vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu kutumika katika ufundishaji wa sarufi ya Luganda pamoja, vitabu na makala ya ziada nane (8) viliteuliwa kutumika katika utafiti huu. Kwa upande wa Kiswahili, Vitabu nane (8) vya Kiswahili sanifu vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu kutumika katika ufundishaji wa sarufi ya Kiswahili, vitabu na makala ya ziada 10 iliteuliwa. Aidha, kutokana na sifa za kimfosintaksia za vipashio vya kisarufi, matini na vitabu vya ziada vinavyodhihirisha sifa za sarufi katika Luganda na Kiswahili sanifu viliteuliwa. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji dhamirifu iliyoongozwa na orodhahakiki kutumia kifaa cha kudondoa data, vitabu na matini kumi na sita (16) ya Luganda na kumi na nane (18) ya Kiswahili vyenye kueleza na kufafanua vipashio vya kimfosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu viliteuliwa kutumika katika utafiti huu. Kwa jumla vitabu na matini ya kisarufi 34 yalitumika katika kutoa taarifa za vipashio vya kimfosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu (Tazama kiambatisho 10).

3.5.2 Sampuli

Sampuli ni idadi ndogo inayoteuliwa kutoka kwa idadi ya jumla ya kundi lengwa. Aidha, sampuli ni sehemu ya idadi ya watu au vitu inayomwezesha mtafiti kupata data za utafiti wake. Utafiti huu unahusisha sampuli ya watafitiwa 54 kutoka kundi nzima la wanafunzi wa kidato cha sita. Sampuli hii ni ya shule 12 kutoka kwa shule 46 zilizoteuliwa kutumia mbinu

ya usampulishaji nasibu. Wanafunzi wa kidato cha sita 54 kutoka kwa jumla ya wanafunzi 178 waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu. Wanafunzi hawa walichaguliwa kimaksudi na kidhamirifu kutokana na sifa ya kuwa wanafunzi wa Kiswahili wenye kiwango cha umilisi ulioimarika na ambao L1 ni Luganda. Idadi ya shule na kundi lengwa la wasailiwa lilitolewa kukidhi mahitaji na madhumuni ya utafiti huu.

Sampuli ya tatu ni ya vitabu na maandishi 34 ambayo yaliteuliwa kutoka kwa vitabu na maandishi anuwai kushiriki katika utafiti huu kufafanua sifa na kanuni za kimfosintaksia za vipashio vya kimfosintaksia vya Luganda na Kiswahili. Vitabu na maandishi haya yaliteuliwa kidhamirifu kukidhi mahitaji ya jumla ya utafiti huu kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji data ni zoezi la awali linaloweza utafiti kupata taarifa zilizokusudiwa kufikia azma ya utafiti (Kothari 2009). Mbinu za ukusanyaji wa data ni njia zinazotumika na utafiti katika kukusanya data zinazotarajiwa kutoka nyanjani. Ukusanyaji wa data unahusu kupata taarifa mahsusi zilizokusudiwa kutoka kwa wasailiwa kutoa au kupinga uhalisia wa mambo fulani (Kombo & Tromp 2006). Utafiti huu ulikusanya data kutoka maktabani na nyanjani. Utafiti huu ulichunguza tabia ya matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili. Ulifafanua uwiano na tofauti za vipashio vya kimfosintaksia vya Luganda na Kiswahili, kuchanganua kanuni na kutathimini jinsi kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Data iliyohitajika katika utafiti huu ni ile ya athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili katika kiwango cha mofosintaksia. Mbinu kuu zilizotumiwa kupata data za kutathimini mwingiliano na athari za mofosintaksia za Luganda katika Kiswahili sanifu zilikuwa mbinu za mjarabu na mijadala iliyotumika kukusanya data kutoka kwa wanafunzi na uchanganuzi wa matini maktabani kama inavyojadiliwa hapa chini

3.6.1 Uchanganuzi Matini

Vitabu vya kiisimu vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu kutumika katika ufundishaji wa Luganda na Kiswahili sanifu pamoja na maandishi au matini ya utafiti wa kisayansi kuhusu vipashio na kanuni za kimfosintaksia mbalimbali yalipekuliwa na kusomwa. Maktabani utafiti huu ulishirikisha usomaji wa kazi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti kama vile; vitabu, magazeti na majarida, machapisho na tasnifu mbalimbali zinazodhihirisha au kuchanganua sifa za vipashio vya mofosintaksia vya Luganda na Kiswahili. Data hizi

zilitolewa katika mitandao, maktaba ya umma, vyuo vikuu na shule za upili, mashirika ya uchapishaji ya serikali na ya kibinafsi kama ilivyodhihirishwa na wataalamu kama Chege (2020), Lupogo, (2021), Majaliwa (2021) na Oberhauser & Wenzake, (2015).

Uchunguzi na uchanganuzi wa maandishi na vitabu husika (Uchanganuzi matini) uliongoza utafiti huu kueleza jinsi vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu hufanana na kutofautiana na kuchanganua kanuni zinazofanua mifanyiko ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda sanifu na Kiswahili sanifu.

3.6.2 Mbinu ya Mjarabu na Mjadala

Mjarabu ni zoezi la kupima umilisi wa wanafunzi kuhusu ufasaha na kiwango cha matumizi ya lugha ili kuweka mikakati ya kukuza ufasaha na usanifu wa matumizi (TY). Majadiliano ni mazungumzo ya watu wawili au zaidi wanaobadilishana mawazo kuhusu mada fulani (Mangi, 2019 na Nyanda, 2015). Utafiti ulinukuu data zinazohusiana na mada husika mawandani kwani ili kupata taarifa sahihi ni lazima mtafiti atumie viungo vyake, hisia, busara katika kuwa makini kusikiliza na mwishowe kuchambua data husika (Adam & Kamuzora, 2008).

Utafiti huu uliandaa mjarabu ya kupima matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vivumishi na vikanusho. Kwa kusaidiwa na mwalimu wa Kiswahili, data ilikusanywa kutoka kwa wanafunzi kimaandishi na kimazungumzo. Mjarabu ya kimaandishi ilitolewa kwa ajili ya kuweza kupata data za kutosha kuhusiana na matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia husika katika maandishi. Kila mjarabu ulipewa muda wake wa kutosha kufanywa na wanafunzi darasani. Mjarabu hiyo ilikusanywa na kusahihishwa kwa kutumia kifaa cha kudondoa data chenye sifa za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia.

Kimazungumzo wanafunzi waliulizwa maswali yaliyoandikwa ubaoni na kila mwanafunzi kupewa muda kutafakari na kuandika jibu. Baada ya kuandika jibu, data iliyojitokeza ilielekeza mijadala. Kila mwanafunzi aliulizwa kueleza majibu yake kuonyesha muundo na kanuni. Utafiti huu ulihusika katika kusahihisha mjarabu, kusikiliza maelezo na mijadala kuhusu muundo wa vipashio na kanuni na hata kupima usanifu wa matumizi ya wanafunzi katika maelezo kuchanganua mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Baada ya kusikiliza, utafiti huu ulinukuu taarifa muhimu iliyoelezwa katika daftari. Baadaye, taarifa hizo kuelezwa kulingana na malengo ya utafiti kutumia kifaa cha kudondoa data

kinachodhihirisha sifa na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu.

Mwisho, mijadala wazi ya kuzungumzwa na wanafunzi thelathini na wanne (34) kuhusiana na vipashio vya kimofosintaksia uliandaliwa kwa ajili ya kujadiliwa na wanafunzi. Mwalimu wa Kiswahili aliongoza mijadala, akisaidiwa na mtafiti ambaye alielekeza mijadala kufanikisha malengo ya utafiti wake. Kwa kutumia orodha ya uchunzaji, utafiti huu ulidondoa data kulingana na madhumuni ya utafiti hasa katika kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya Luganda na Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu. Katika mijadala hii, utafiti huu ulinukuu mfanano na tofauti za vipashio, kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu na kutathimini mwingiliano na athari za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili.

3.7 Vifaa vya Ukusanyaji Data

Sehemu hii inaeleza juu ya vifaa vilivyotumika maktabani kukusanya data za kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu kutoka kwa vitabu na maandishi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu. Mathalani, inaorodhesha vifaa vilivyotumika nyanjani kukusanya data za athari za mwingiliano wa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

3.7.1 Mijarabu ya Kimofosintaksia

Utafiti huu uliandaa mijarabu na mijadala ya kimofosintaksia kukusanya data kutokana na matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili. Kwa kusaidiwa na walimu wa Kiswahili nyanjani, wanafunzi walipewa mijarabu ya kimofosintaksia iliyoandaliwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Matokeo ya mijarabu hii ilisahihishwa kutumia kifaa cha uchunzaji chenye orodhahakiki ya sifa na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia kwa mujibu wa vitabu na maandishi sanifu. Matokeo ya mijarabu hii iliongoza mijadala ya mazungumzo kuweza kutambua athari za mwingiliano wa vipashio vya Luganda katika Kiswahili sanifu.

3.7.2 Kifaa cha Orodha ya Uchunzaji cha Vipashio vya Mofosintaksia

Kifaa cha kudondoa data cha orodhahakiki chenye sifa zinazotambulisha matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia, miundo yake na kanuni za matumizi kilitumika kudondoa data

kulingana na malengo matatu ya utafiti. Kifaa hiki kilikuwa mwongozo wa uchanganuzi matini kilichotoa taarifa sahihi za kisarufi kuhusu muundo wa vipashio na kanuni zinazofafanua mifanyiko ya vipashio husika kutoka kwa vitabu vilivyoteuliwa kutoka katika maktaba ya shuleni na ya kijamii. Uteuzi wa mbinu hii ulitokana na madai ya Momanyi, Ambuyo & Chimerah (2019) wanaodai kuwa data za maktabani zinapendelewa kwa sababu zinadhihirisha ufasaha kwa matumizi ya lugha zaidi kuliko data ya nyanjani na uteuzi wa vitabu vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu ni wa msingi katika ujifunzaji na ufunzaji wa lugha kwa sababu hutoa taarifa sahihi za kisarufi kinyume na taarifa zinazopatikana nyanjani.

3.8 Ufaafu na Utegemezi wa Vifaa vya Kukusanya Data za Utafiti

Ufaafu na utegemezi wa vifaa vya kukusanya data za utafiti ulizingatia mijaribu ya awali iliyofanywa kwa lengo la kupata na kutathimini ubora wa kila kifaa na ufaafu wake katika kupata data madhubuti inayowiana na madhumuni yote ya utafiti huu na isiyokuwa na shaka. Utafiti alitumia mijarabu na mijadala ya kimofosintaksia kupima matumizi ya lugha ya Kiswahili hasa kuchanganua miundo na kanuni pamoja na matumizi ya vipashio vya Luganda na Kiswahili. Upimaji huu ulipelekea uchanganuzi wa mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Ufaafu wa vifaa hivi ulitokana na uneni wa Wilkins (1972) anayeeleza kuwa kasoro au dosari za kiisimu za lugha hutokana na mazungumzo na maandishi ambayo yakichunguzwa yanaweza kubainisha athari za L1 (lugha mama) pamoja na kuchukulia kwa ujumla sheria za maumbo ya lugha, kunakopelekea maumbo yanayorandana kuhamishiwa lugha nyingine. Kwa hiyo, mijarabu ya kimofosintaksia ya kuandikwa na kujadiliwa kimazungumzo iliandaliwa katika vipindi mbalimbali vya kupima matumizi ya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vivumishi na vikanushi baada ya kuhojiana na wasimamizi ambao walipitia mijarabu na mijadala husika kabla ya shughuli ya ukusanyaji data kutumia vifaa hivi. Katika kuamua kuhusu kifaa na utaratibu wa kuzingatiwa, walimu wanaofundisha Kiswahili na ambao L1 ni Luganda waliteuliwa kupitia vifaa husika kwa ajili ya kutathimini ufaafu na utegemezi wake kwa utafiti huu kwa wanafunzi wao. Mapendekezo yao yaliyoendana na malengo ya utafiti huu yalitiliwa maanani na kuzingatiwa.

Orodha ya uchuzaji ya kimofosintaksia ilitumika katika utafiti huu kuchunguza mijadala ya wanafunzi kutambua mwingiliano wa kanuni na miundo ya kimofosintaksia. Utafiti huu ulichunguza matokeo ya mijarabu na mijadala iliyojitokeza kimaandishi na kimazungumzo. Matokeo haya yalitumika kueleza, kuchanganua na kutathimini matumizi ya vipashio vya

kisarufi, miundo na kanuni kama inavyotumika na wanafunzi wanaojifunza na kutumia Kiswahili kama L2. Utafiti huu ulipima, ufaafu na uthabiti wa vifaa na mbinu za utafiti kwa walimu na wanafunzi. Mijarabu iliyoandaliwa ilipitiwa na mwalimu wa Kiswahili shuleni ambaye alihakikisha kuwa mjarabu huo ni faafu katika kupima vipengele vya mofosintaksia, kiwango cha wanafunzi na uwezo wa wanafunzi kuweza kujibu mjarabu husika. Ni kutokana na upimaji huu ambapo suala la mijadala baada ya kila mjarabu lilijitokeza kupima mazungumzo ya wanafunzi ili kutambua zaidi mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Baada ya kupitia mjarabu na kuandaa mijadala lengwa, utafiti uliweza kupata fursa ya kufanya marekebisho zaidi ya vifaa, kuandaa miadi na ratiba ya kukusanya data kutoka kila shule.

Kuaminika kwa data za utafiti huu kulitokana na ufaafu na uthabiti wa mbinu za utafiti kuzalisha matokeo yale yale kutoka katika shule zote sawa kutumia mjarabu mmoja, utaratibu na mbinu sawa katika kukusanya data kama ilivyoelezwa katika mbinu za ukusanyaji wa data. Hali hii ilitokana na maelezo ya wataalamu Mugenda & Mugenda (2003), Mogere & Wasike, (2018) wanaoeleza kuwa kuaminika kwa kifaa ni kiwango cha kifaa kutoa matokeo ya kutegemewa au data baada ya majaribio kadhaa. Ufaafu hutegemea uhusiano wa taarifa zilizotolewa na wahojiwa wale wale katika muda tofauti, vifaa, utaratibu na mbinu za utafiti. Utochelevu wa kifaa kupata taarifa zinazohitajika ni uthabiti uliozingatiwa katika matumizi ya kifaa. Kwa sababu hiyo, utafiti huu ulichunguza wasailiwa wanafunzi wa kidato cha sita ambao ni wanafunzi wa Kiswahili na ambao L1 ni Luganda.

3.9 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data ya kimofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili ilichanganuliwa kithamano kupitia kwa mjarabu, mijadala na orodhahakiki ya kupima matumizi ya miundo na kanuni za vipashio vya kimofosintaksia kwa mujibu wa madhumuni. Utafiti uliweza kutathimini athari za mwingiliano wa vipashio vya mofosintaksia kama inavyodhihirika katika matokeo ya mjarabu na mijadala ya wanafunzi wa Kiswahili kama L2 kutegemea miundo na kanuni kati ya Luganda na Kiswahili. Katika utafiti huu, mifumo na kanuni ya Luganda na Kiswahili kama inavyotumika na mwanafunzi ilishirikishwa katika kuchanganua data iliyokusanywa na kujadili athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kutumia njia ya maelezo kwa mujibu wa madhumuni na nadharia ya Umilikifu na Unganifu. Mfumo huu ulifuata hatua kuu tatu kama ilivyoelezwa na Britain, Press, Keller, Cnrs, & Appliquete, (1992). Data zilizopatikana zilibainishwa, kuchanganuliwa

na kuwasilishwa kutumia mbinu ya kitahamano na kuwasilishwa kutumia njia ya kimaielezo kuonyesha matokeo ya utafiti.

Utaratibu wa uchanganuzi na uwasilishaji data kithamano ulizingatia mihimili ya nadharia ya Umilikifu na Unganifu kwa kutumia mbinu ya msingi ya Barney Glaser & Anselm Strauss 1967 ya kanuni na vigezo kama inavyorejelewa na kutumika na Hallberg, 2006; Levers, 2013 na Chebet 2016. Mbinu hii ni mbinu ya uchanganuzi wa data ambayo huwezesha utafiti kuibuka na nadharia ya kueleza hali kama inavyojitokeza katika muktadha ambao hauwezi kufafanuliwa na nadharia na mbinu zinazohusika katika utafiti. Mbinu hii ilihusika katika kuorodhesha data na vyanzo vyake, kutambua mifumo ya data, uundaji wa kategoria kutokana na mifumo ya utokeaji wa data, ulinganishi na ulinganuzi wa kategoria za data kama zinavyojitokeza katika mikutadha, kurekebisha na kuibuka na data sahihi kutokana na data mpya wakati wa uchanganuzi. Chebet (2016); Chepyegon, Khaemba & Bartoo, (2021) wanaoeleza kuwa mbinu hii ni msingi ambao hutoa mwelekeo wa kuchanganua na kuwasilisha data kithamano kwa kutumia hatua rahisi za kutambulisha data, kueleza kategoria za data/kuainisha, kulinganisha na kulinganua data na kuirekebisha ili kufikia data halisi au mada kuu kama inavyojitokeza katika muktadha halisi kwa ajili ya kuchanganua data kamili isiyo na dosari. Kwa kutumia mbinu hii, utafiti huu ulitambulisha data kama ilivyojitokeza katika mijarabu kuwa msingi ambao hutoa mwelekeo wa kuchanganua na kuwasilisha data kithamano kwa kutumia hatua rahisi mijadala na orodha ya uchunzaji; kueleza mifumo ya utokeaji wa data; kulinganisha na kulinganua mifumo ya utokeaji wa data, kurekebisha data kutokana na data mpya na kujitokeza na data kamili iliyohusu mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu isiyo na dosari na ambayo haikuweza kuelezwa na nadharia ya utafiti huu kwa ajili ya kueleza, kuchanganua na kutathimini data za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika Kiswahili sanifu kimuktadha.

Mbinu ya uhakiki wa yaliyomo ya Woodrum (1984) ilitumika kuchanganua sifa za Mwingiliano wa kimofosintaksia ya Luganda kama ilivyodhihirishwa katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi katika vitabu vilivyoidhinishwa na serikali kufundisha sarufi ya Kiswahili sanifu, upekuzi wa matini ya kisayansi kuhusiana na sarufi ya Luganda na Kiswahili, mijarabu na mijadala ya kupima muundo na kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia katika Kiswahili sanifu darasani. Mbinu hii inahusu uchambuzi wa jumbe zilizomo katika vitabu, nyaraka, majarida, magazeti na maudhui ya maneno ambayo

yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo (Jilala, 2014). Kwa kutumia mbinu hii, utafiti huu ulibainisha ukiukaji wa muundo na kanuni za matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Kiswahili kwa kupigia mstari ukiukaji kutoka kwa mijarabu na mazungumzo yaliyokiuka miundo na kanuni kutoka kwa mijadala kunukuliwa au kuandika chini kwa ajili ya kuchanganuliwa. Mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu vilevile uliainishwa na kuwekwa katika kategoria maalumu. Uchanganuzi wa mwingiliano wa muundo na kanuni za matumizi ya vipashio kuelezwa kulingana na mihimili ya umiliki na unganifu na tathimini ya jinsi muundo na kanuni za mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili kuingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kuwekwa bayana. Uchambuzi wa yaliyomo katika utafiti huu uliwezesha kwa kuelekezwa na mwongozo wa maswali yaliyotokana na madhumuni ya utafiti.

Kwa kutumia mbinu ya ukaguzi wa sifa za sarufi wa neno kuu kufafanua sifa zote za kisarufi za neno katika tungo kama ilivyoielezwa na Chomsky, 1993; 1995). Kila lugha huwa na sifa za kisarufi za kategoria fulani ambazo ni thabiti na zinazoongozwa na kanuni fulani. Katika isimu, matumizi yoyote ya lugha iwe ya kimaandishi au mazungumzo hutawaliwa na sheria ambazo hutawaliwa na muundo na matumizi ya vipashio. Kauli hii inadhibitishwa na Hacker & Baker (2009) wanaosisitiza kuwa sheria za kisarufi zinazohusisha, matumizi ya njeo, uambishaji, unyambuzi, upatanishi wa maneno, mpangilio wa maneno katika tungo na muundo wa neno hubainisha lugha ambapo usarufi hutawaliwa na sheria.

Kwa hiyo, kwa kutumia mbinu hii, vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili kutoka katika vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia sarufi na maandishi mengineyo ya ziada ya sarufi ya Luganda na Kiswahili sanifu ilibainishwa, muundo wa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu kuelezwa, kanuni zinazoongoza matumizi ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu kuchanganuliwa, data za kimaandishi na mazungumzo kama ilivyojitokeza katika muktadha wa matumizi ya wanafunzi nyanjani kudondolewa, uwiano na tofauti za muundo na kanuni za matumizi kutokana na data za wanafunzi zilibainishwa, kuweka mwingiliano katika kategoria maalumu ya vipashio husika ulianishwa, mwingiliano kuelezwa na athari za mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutokana na mijarabu na mijadala ya kupima muundo na kanuni za kimofosintaksia za matumizi ya vipashio kama yanavyotumika na wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha sita ambao L1 ni Luganda ulitathiminiwa. Mihimili ya sarufi bia na upatanisho ya nadharia ya umilikifu na unganifu

iliongoza mbinu hii kujitokeza na orodha ya upimaji wa muundo na kanuni za kimofosintaksia za Luganda na Kiswahili kubainisha vipashio vya kimofosintaksia na uamilifu wake katika tungo kudhihirisha sifa za kimofosintaksia na Mwingiliano wake.

Data iliyokusanywa katika utafiti huu iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo, majedwali na vielelezo matawi kuonyesha mwingiliano wa muundo na kanuni za vipashio vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Mifumo ya vipashio ilielezwa na kanuni kuchanganuliwa kuonyesha mwingiliano na athari za matumizi ya muundo na kanuni za vipashio vya mofosintaksia vya Luganda kutathiminiwa. Mifano mbalimbali ya data ilitolewa na hatimaye mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kuelezwa kutumia majedwali au michoro matawi kuonyesha jinsi vipashio vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Njia za uwasilishaji data zilizingatia madhumuni ya utafiti ya kueleza jinsi vipashio vya Luganda na Kiswahili hufanana na kutofautiana, kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya vipashio vya mofosintaksia na kutathimini mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika maandishi na mazungumzo.

3.10 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alizingatia maadili ya utafiti ya kitengo cha Chuo Kikuu cha Maseno wakati wa kutekeleza mchakato mzima wa kupanga, kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya data yake. Mtafiti alipata barua ya kuidhinisha pendekezo na tamko la kufanya utafiti wake kirasmi kutoka chuoni, kuomba ruhusa ya kufanya utafiti katika eneo la kijiografia la utafiti. Kidesturi, mtafiti alijitambulisha kwa wasailiwa waliosaidia katika upataji wa data lengwa nyanjani; kupata idhini ya shule teule ya kushiriki katika ukusanyaji data shuleni na darasani. Umuhimu wa utafiti katika ukuzaji na uendelezaji wa matumizi sanifu ya lugha na isimu shuleni, vyuoni na njanja zinginezo za kiakademia zilelezwa. Wasailiwa waliombwa kuwa huru kushiriki katika utoaji wa majibu na kushiriki katika mijadala baada ya kuelezwa juu ya umuhimu wa utafiti, dhima yao katika utafiti, faida yao katika utafiti, heshima wanayotunukiwa kutokana na mchango wao kwa utafiti kulingana na kanuni ya utafiti. Vilevile, mtafiti alihakikisha uhifadhi na ulinzi wa haki za wasailiwa kwa kuheshimu siri na utambulisho wao kuhusiana na data waliyotoa, majina na kutambua haki na madhumuni ya kazi yake kama ilivyoelezwa na Adam & Kamuzora (2008). Wasailiwa waliombwa kwa hiari yao kushiriki kwenye utafiti huu bila kulazimishwa. Wasailiwa waliombwa kujaza ungamo kuonyesha kuwa walikuwa tayari kushiriki katika utafiti huu kwa hiari yao bila kulazimishwa. Wale waliokataa na waliokubali kushiriki katika utafiti huu vilevile

waliruhusiwa kushiriki kwa hiari yao. Vyanzo vya data husika za utafiti huu vilirejelewa, kunukuliwa na kuhifadhiwa katika marejeleo.

3.11 Hitimisho

Sura hii iliweka wazi mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato mzima wa tasnifu hii. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Ulifanyika katika eneo la Kampla, Uganda miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha sita wanaojifunza Kiswahili na ambao L1 ni Luganda. Data ilikusanywa maktabani kutumia mbinu ya uchanganuzi matini ya usomaji na udondoaji wa taarifa muhimu za miundo na kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu. Kifaa cha kudondoa data cha orodhahakiki chenye sifa zinazotambulisha matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia, miundo yake na kanuni za matumizi kilitumika kudondoa data kulingana na malengo matatu ya utafiti kutokana na usimaji na uhakiki wa vitabu na makala. Aidha, mbinu ya mijarabu na mijadala ilitumika kukusanya data kutoka nyanjani. Kifaa cha mijarabu na mijadala ya kimofosintaksia ilitumika kukusanya data kutokana na matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili. Matokeo ya mijarabu hii ilisahihishwa kutumia kifaa cha uchunzaji chenye orodhahakiki cha sifa na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia kwa mujibu wa vitabu na maandishi sanifu. Matokeo ya mijarabu hii iliongoza mijadala ya mazungumzo kuweza kutambua athari za mwingiliano wa vipashio vya Luganda katika Kiswahili sanifu kama ilivyoelezwa katika sura ya nne tano na sita.

Data iliyokusanywa katika utafiti huu iliwasilishwa kwa njia ya kimaielezo, majedwali na vielelezo matawi kuonyesha mwingiliano wa muundo na kanuni za vipashio vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Mifumo ya vipashio ilielezwa na kanuni kuchanganuliwa kuonyesha mwingiliano na athari za matumizi ya muundo na kanuni za vipashio vya mofosintaksia vya Luganda kutathiminiwa kama ilivyoelezwa katika sura ya nne tano na sita.

SURA YA NNE

VIPASHIO VYA MOFOSINTAKSIA VYA LUGANDA NA KISWAHILI SANIFU

4.1 Utangulizi

Uwasilishaji wa matokeo na mijadala ya data ulizingatia madhumuni matatu ya utafiti na maswali yanayoambatana na madhumuni hayo. Uwasilishaji wa matokeo na mijadala ya data ya kila madhumuni imeshughulikiwa katika kila sura. Sura hii imeangazia data kuhusu madhumuni ya kwanza ya kufafanua jinsi vipashio vya kimofosintaksia katika Luganda vinavyofanana na kutofautiana na vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili. Madhumuni ya pili ya kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia na madhumuni ya tatu ya kutathimini kanuni za mifanyiko ya mofosintaksia ya Luganda na athari zake katika matumizi ya Kiswahili sanifu, iliwasilishwa na kujadiliwa katika sura ya tano na sita mtawaliwa. Data za sura ya nne ni data za maktabani. Data zote zilikusanywa kutoka kwa usomaji wa vitabu na uhakiki matini teule. Kwa kurejelea orodhahakiki ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu, data za kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili ziliwasilishwa na kujadiliwa kimaelezo kutumia majedwali na michoro. Uwasilishaji wa data ulijikita katika matumizi. Uliegemea katika mihimili miwili ya Ubia na upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Uganifu ya Chomsky, (1981).

Uwasilishaji wa kufanana na kutofautiana ulizingatia vigezo vya matumizi ya vipashio, maumbo na muundo wa matumizi ya nomino na maneno mengine katika tungo kudhihirisha umilikifu na unganifu wa nomino na maneno hayo katika tungo. Kwa kutumia kifaa cha kudondoa data chenye sifa zinazotambulisha matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia, matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha hali ya kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili vya ngeli katika nomino, vivumishi (vimilikishi, visifa, -a' unganifu, vionyeshi na viidadi) viwakilishi nafsi na vikanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu vilihusika:

4.1.1 Ufafanuzi wa uwiano na tofauti za ngeli za nomino za Luganda na Kiswahili

Ulinganishi wa ngeli za nomino baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu ni muhimu sana katika matumizi ya sarufi ya Kiswahili sanifu (Mukuria 1987; Besha 1996). Utafiti huu ulifafanua kufanana na kutofautiana kwa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kwa kuchunguza sifa za kitaipolojia za mfumo wa ngeli za nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu kimofolojia na kisintaksia. Uainishaji wa kimofolojia ni mfumo wa uainishaji wa

nomino kwa kuzingatia viambishi vya ngeli za nomino ambavyo huwekwa mwanzoni mwa mzizi wa nomino kiozi kuwakilisha idadi ya umoja na wingi. Uainishaji wa ngeli za nomino kisintaksia ni ule mfumo wa kuainisha ngeli nomino kwa kuzingatia uambishaji wa viambishi vipatanishi vya msingi vya ngeli nomino, ambavyo huwekwa kwenye maneno mengine katika tungo kuwakilisha dhana ya kisarufi ya umoja na wingi. Uainishaji huu unatokana na kuwa viambishi vya ngeli za nomino kimofolojia huathiri viambishi vya upatanishi ambavyo huwekwa kwenye maneno mengine katika tungo, kuonyesha uhusiano milikifu na Unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Uligemea kuchunguza mofolojia na sintaksia kando kando ili kuweza kuibuka na sifa za kufananisha na kutofautisha vipashio vya kimofosintaksia vya lugha kwa kutumia kanuni ya kukagua sifa za sarufi kwa kutazama mofimu za maneno (Chomsky, 1965). Aidha, vigezo vya uainishaji wa ngeli wa Aikhenvald, (2017) pamoja na Grinevald, (2000) ulihusika. Miongoni mwa vigezo vilivyohusika ni pamoja na kigezo cha uainishaji wa nomino/ubantu, uwiano wa kisarufi wa nomino, idadishaji za nomino (idadi za nomino ujozi/takwimu), matumizi ya viambishi vya nomino yaani viambishi wakilishi (mofimu) wakilishi wa ngeli nomino (uambishaji wa nomino) na nafasi ya uambishaji. Matokeo na mjadala wa kila kipashio ni kama unavyorejelewa hapa chini:

4.1.1.1 Kufanana na kutofautiana kwa ngeli mkabala wa mfumo wa uainishaji

Data kutoka maktabani kuhusu kufanana na kutofautiana kwa ngeli mkabala wa mfumo wa uainishaji umeonyeshwa katika Jedwali (4.1). Mkabala huu mfumo wa kimofolojia na kisintaksia kama ifuatavyo.

Jedwali 4.1: Uwiano na tofauti za ngeli za nomino za Luganda na Kiswahili mkabala wa mfumo wa kimofolojia na kisintaksia

| Uainishaji | Uainishaji kimofolojia | | Uainisaji Kisintaksia | |
|------------|------------------------|-------------------|-----------------------|---------------|
| | Luganda | Kiswahili | Luganda | Kiswahili |
| Idadi | | | | |
| Umoja | (o) mu-/m-/mw- | mu-/m-/mw- | a- | Yu-/a- |
| Wingi | (a)ba- | wa- | ba- | wa- |
| Umoja | (o) mu-/m/mw- | Mu-/m/mw- | gu- | u- |
| Wingi | (e) mi- | mi- | gi- | i- |
| Umoja | (e) li-/ri-/ Ø- | Ji-/ Ø- | li- | li- |
| Wingi | (a) ma | Ma- | ga- | ya- |
| Umoja | (e) ki | Ki- | ki- | ki- |
| Wingi | (e)bi | Vi- | bi- | vi- |
| Umoja | (e) n-/m-1 | N-/ Ø | e- | i- |
| Wingi | (e) n-/m-2 | N-/ Ø | zi- | zi- |
| Umoja | (o)lu | U- | en- | u- |
| Wingi | (a)ka | N- | ka- | zi- |
| Umoja | (o)tu | - | tu- | - |
| Wingi | (o)bu | - | bu- | - |
| Umoja | (o)ku | Ku- | ku- | ku- |
| Wingi | Wa- | Pa | wa- | pa- |
| Umoja | - | Ku- | ku- | ku- |
| Wingi | - | Mu- | Mu- | mu- |
| Umoja | (o)gu- | - | - | - |
| Wingi | (a)ga- | - | gu- | |
| 23 | E | - | Ø | Ø |

Asili: Data za uchanganuzi wa Mulei, Ambuyo & Amukowa, (2021) na Kyagaba (1996)

Matokeo ya uchanganuzi kwa mujibu wa Namugala (2014), Besha, (1996) na Bernander, Rasmus, Maud Devos & Hannah Gibson (2018) na Habwe & Karanja (2004, utafiti huu uligundua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huainisha ngeli zake kwa kuzingatia mfumo mmoja wa kimofolojia na kisintaksia. Kwa mujibu wa jedwali Na.(4.1), maumbo yaliyokolezwa yanadhihirisha kufanana kwa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kugemea mfumo wa uainishaji ngeli wa kimofolojia na kisintaksia. Hata hivyo, mfumo wa mpangilio wa nomino katika lugha hizi yanatofautiana kwa mengi. Tofauti inayojitokeza ni kuwa licha ya kuwa mfumo huu unadhihirisha maumbo yanayofanana, yanadhihirisha tofauti katika matumizi hasa katika uambishaji wa viambishi vya msingi vya upatanishi wa kisarufi kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo. Nomino inaweza kupatikana katika Kiswahili katika kundi fulani la ngeli, lakini nomino hiyo iliyotajwa ikawa inapatikana katika kundi tofauti la ngeli ya Luganda lisilokuwa katika Luganda. Kwa mfano, nomino za majina ya wanyama, samaki na wadudu ambayo yameanishwa katika ngeli ya 9/10. Nomino hizi hupatikana katika ngeli ya 1 /2 katika Kiswahili hata hivyo kimatuzi,

Luganda inayatumia katika ngeli ya {N-/i-zi} ambayo ni ngeli ya 9/10 katika Kiswahili na Luganda.

Kwa kuongozwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya umilikifu na ufungami (Chomsky, 1981) unaozingatia sifa za sarufi bia na ambao huchukulia kuwa kanuni zilezile za kimofosintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Utafiti huu uligundua kuwa, nyingi kati ya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu zina sifa nyingi zinazofanana kwa kuzingatia mfumo wa uainishaji wa ngeli kimofolojia na kisintaksia ingawa zinatofautiana sana katika kiwango cha viambishi vipatanishi vya msingi vya nomino vinavyotumika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo.

Matokeo haya yanashadidiwa na ufafanuzi wa Mulei, Ambuyo na Amukowa, (2021) nao wanaokubaliana na matokeo haya kufafanua jinsi ngeli za Luganda na Kiswahili hufanana na kutofautiana hasa kimaumbo kimofosintaksia. Wanafafanua kuwa;

Luganda na Kiswahili hutumia mfumo wa kimofolojia na kisintaksia katika uainishaji na matumizi ya ngeli nomino. Aidha wanaeleza kuwa; Nyingi kati ya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu zina sifa nyingi zinazofanana kimofolojia na kisintaksia ingawa zinatofautiana sana katika kiwango cha viambishi vipatanishi vya msingi vya nomino pamoja na maana. (Mulei, Ambuyo na Amukowa, 2021: 15).

Matokeo haya yanashadidiwa vile vile na wataalamu Mukuria, (1987), Oichoe, (2005) na Otiende, (2013) wanaoeleza ubia wa lugha za Kibantu wa kuainisha nomino zake katika ngeli za nomino. Hali ambayo inaendana na mhimili wa ubia na upatanishi wa nadharia ya Umilikifu na Ufungami ya Chomsky, (1981). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa, lugha za Kibantu huainisha nomino zake katika ngeli na hii ndiyo sifa ya kipekee ya kuzitambulisha na kuzitofautisha lugha za Kibantu. Aidha, Basweti, (2005) naye anakubaliana na madai haya akieleza juu ya dhima ya uainishaji wa nomino katika lugha kuwa, uainishaji wa nomino katika ngeli ni muhimu hasa kuonyesha uhusiano wa kiupatanifu wa nomino na maneno mengine ya kisarufi katika tungo, kutofautisha nomino moja na nyingine katika lugha na hata kutofautisha nomino hiyo moja na nyingine baina ya lugha moja na nyingine kimofolojia na kisintaksia. Matokeo haya ni muhimu katika kubainisha usahihi wa matumizi ya nomino katika ngeli kudhihirisha hali ya umilikifu na unganifu baina ya neno kuu na maneno mengine katika tungo. Sifa ambayo ni ya nadharia ya umilikifu ya kuonyesha uhusiano wa kimofolojia na kisintaksia wa nomino moja kutawala maneno mengine katika tungo

kuonyesha uhusiano wa kimofosintaksia. Aidha, uchunguzi ulitambua kuwa, hata ingawa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja za Kibantu, kulitokea uwiano na tofauti katika mifumo wa kimofolojia na kisintaksia wa ngeli uliopambanua na kudhihirisha sifa maalumu zinazotambulisha Luganda na Kiswahili kama lugha mbili tofauti zinazojitegemea kiisimu.

4.1.1.2 Uwiano na tofauti mkabala wa vibainishi ngeli na viambishi ngeli

Data ya Uchanganuzi matini wa Uwiano na tofauti za ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kwa mkabala wa vibainishi ngeli na viambishi ngeli ni kama unavyojitokeza katika data ya Jedwali Na. (4.1 Uk 71 na Mifano ya Data Na (4.1Uk. 73).

- | | |
|-----------------------------------|---|
| a) <i>Omwenge gwanyogoga</i> | <i>Mvinyo ulikuwa baridi</i> |
| b) <i>Omwenge ogwanyogoga.</i> | <i>Mvinyo uliokuwa baridi</i> |
| c) <i>Ogogwoka omuti murungi</i> | <i>Huo ndio mti pekee ulio mzuri</i> |
| d) <i>Egyogyoka emiti mirungi</i> | <i>Hiyo ndiyo miti pekee iliyo mizuri</i> |
| e) <i>Omucungwa guwooma.</i> | <i>Mchungwa mtamu</i> |
| f) <i>Eryenvu riwooma.</i> | <i>Ndizi tamu</i> |
| g) <i>Embuzi etambula.</i> | <i>Mbuzi anatembe</i> |

Asili: Baertlein & Ssekitto (2014), Bochnak (2013), Leah & Sseguya (2015)

Uchanganuzi wa kimaumbo kulingana na Namugala (2014) na Katamba, (2003) na Baertlein na Ssekitto (2014) ulibaini kuwa, mbali na kutumia viambishi ngeli vya nomino katika kuainisha na kupangilia ngeli za nomino kuzingatia mfumo wa kimofolojia na kisintaksia, Luganda imetumia pia vibainishi vya ngeli (a)-, (o)-na (e)- ambavyo hupachikwa (huambishwa) nyuma ya kiambishi ngeli kutegemea aina ya nomino inayotajwa katika mfumo wa neno au sentensi kuwakilisha umoja na wingi wa nomino na katika sentensi kuwakilisha upatanishi wa kisarufi.

Kwa kuongozwa na mhimili wa Sarufi bia na upatanifu wa nadharia ya umilikifu na ufungami ya (Chomsky, 1981), data Na.(4.1) kiupatanifu, ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu zimetumia viambishi ngeli vya upatanishi wa kisarufi ambavyo hupachikwa katika viwakilishi nafsi, vivumishi, vitenzi, vimilikishi, viwakilishi nomino na elementi zingine za sentensi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa neno kuu na maneno mengine katika tungo. Hata hivyo, maumbo yake hutofautiana pale ambapo vibainishi katika Luganda huathiri upatanishi wa kisarufi huku Kiswahili kikitumia viambishi wakilishi vya ngeli

kuathiri upatanishi wa kisarufi. Matokeo haya yanashadidiwa na Namugala, (2014) anayesema kuwa;

Luganda has a noun class system that involves singular and plural patterns as well as agreement marking triggered by the noun classes. The agreement markers are manifested on syntactic constituents like adjectives, numerals, verbs and others (Namugala, 2014: 11).

Luganda ni lugha ambayo huainisha nomino zake kimofolojia kudhihirisha umoja na wingi wa nomino na upatanifu wa kisarufi ambao hujitokeza katika muundo wa kisintaksia (TY).

Maelezo ya Namugala (keshatajwa) yanaungwa mkono na Bernander, Rasmus, Maud Devos na Hannah (2018) wanaoeleza kuwa:

The Bantu languages are also characterised by a system of noun classes – a form of grammatical gender (Bernander na Wenzake, 2018: 2).

Lugha za Kibantu zinadhahirisha hulka za kuainisha nomino zake katika mfumo wa ngeli, mfumo ambao unaonyesha upatanifu wa kisarufi wa nomino kwa umoja na wingi (TY). Aidha, maelezo haya yanakubaliana na ya Habwe na Karanja (2004) na Besha (1996) wanaoeleza kuwa, Kiswahili huanisha ngeli zake kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Besha (keshatwajwa) naye anasema kuwa:

Ipo misingi mitatu ambayo wanasarufi wametumia katika kuainisha nomino za kiswahili: (a) Msingi wa kimofolojia au maumbo; (b) msingi wa kisemantiki au dhana; (c) Msingi wa kisintaksia au uwiano wa nomino na maneno mengine katika tungo (Besha, 1996:2).

Kwa kuzingatia mhimili wa sarufi bia na upatanifu, utafiti huu ulitambua kufanana na kutofautiana kwa ngeli za nomino kuzingatia mfumo huu wa uainishaji kimofolojia na kisintaksia wa ngeli nomino kijozi na kitakwimu ambapo kiambishi awali hutumika kuonyesha idadi ya umoja na wingi wa nomino kimofolojia na kisintaksia. Sifa hii inakubaliana na mhimili wa upatanishi wa nadharia ya Umilikifu na Unganifu wa maumbo ya nomino kutumika kutawala maneno mengine katika tungo.

Matokeo ya utafiti huu yanashadidiwa na Bochnack, (2013) na Jerro, (2018) wanaofafanua kuwa tofauti na lugha za Kibantu zinazotumia viambishi vya ngeli vya umoja na wingi Luganda hutumia vibainishi ambavyo hufanya kazi ya kuathiri maumbo ya upatanishi wa kisarufi wa tungo kama inavyoelezwa na Jerro (2018) ambaye anakubaliana na maelezo ya Katamba, (2003). Anaeleza kuwa :

As for the phonological shape of the morphemes, Swahili lacks the pre-prefix that is found in Luganda and Rwanda. At a first glance, this could be argued to be an instance of phonological reduction in Swahili (Jerro, 2018:11).

Kifonolojia, Kiswahili hakina mambo ya vibainishi vya ngeli kama vinavyojitokeza katika Luganda na Kinyarwanda (TY).

Utafiti huu wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu unakubaliana na ufafanuzi wa Guthrie, (1967) na Lukamika (2015) wanaohusisha ngeli na uhusiano wa lugha za Kibantu pamoja na Mukuria (1987) ambaye alilinganisha ngeli za Kiswahili na Kikikuyu cha Kiambu kimofolojia na kisemantiki. Aidha, wataalamu mbalimbali wamelinganisha na kufafanua mifumo ya uainishaji kama vile Otiende (2013), Obara (2014), Mdee, Njogu, & Shafi (2011) na Bochnack (2013), Oduor & Wenzake, (2017) na wengineo wanaonyesha vigezo vya uainishaji. Licha ya wataalamu hawa (washatajwa) kudhihirisha matokeo ya kufanana na kutofautiana kwa mifumo ya uainishaji na matumizi. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha upekee wa kuwa licha ya Kuwa Luganda na Kiswahili kuainishwa katika nasaba moja ya lugha za Kibantu pamoja na kuainisha nomino katika ngeli, Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti zilizodhihirisha matumizi ya nomino katika ngeli kwa upekee wake kimaumbo na kimiundo kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino kutawala maneno mengine katika tungo.

4.1.1.3 Kufanana na kutofautiana kwa ngeli mkabala wa uwiano wa Kisarufi

Data ya kufanana na kutofautiana kwa ngeli mkabala wa uwiano wa kisarufi umedhihirishwa katika data ya Jedwali Na. (4.2).

Jedwali 4.2: Kufanana na kutofautiana kwa viambishi vya ngeli za Luganda na Kiswahili kimofolojia na Kisintaksia

| Ngeli | Luganda Sanifu | | Kiswahili sanifu | |
|-------|-----------------|-----------------------|---------------------------------|-----------------------|
| | Viambishi awali | Viambishi vipatanishi | Viambishi awali vya kimofolojia | Viambishi vipatanishi |
| 1 | (o)mu- | a- | m-/mu-/mw-/n-/ Ø | Yu-/a- |
| 2 | (a)ba- | ba- | wa-/ ma | wa- |
| 3 | (o) mu- | gu- | m-/ mu/mw | u- |
| 4 | (e)mi- | gi- | mi- | i- |
| 5 | Li; (e)ri-/ Ø | li- | ji-/ Ø | li- |
| 6 | (a)ma- | ga- | ma- | ya- |
| 7 | (e)ki- | ki- | ki- | ki- |
| 8 | (e)bi- | bi- | vi- | vi- |
| 9 | (e)n- | e- | n-/ Ø | i- |
| 10 | (e)n- | zi- | n- Ø | zi- |
| 11 | (o)lu- | en- | u- | u- |
| 12 | (a)ka- | ka- | n-/ Ø | zi- |
| 13 | (o)tu- | tu- | - | - |
| 14 | (o)bu- | bu- | - | - |
| 15 | (o)ku- | ku- | ku- | ku- |
| 16 | wa- | wa- | pa- | pa- |
| 17 | ku- | ku- | ku- | ku- |
| 18 | mu- | Mu- | mu- | mu- |
| 20 | (o)gu- | gu- | | |
| 22 | (a)ga- | ga- | | |
| 23 | E | | | |

Asili: Besha, (1996); Juma, (2017) na Jerro, (2018)

Data ya uchanganuzi wa data kutokana na Namugala, (2014), Kiyinikibi, (2021) na Mulei na wenzake (2021), Mgullu (1999), Leah & Sseguya (2015) ni kuwa, ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu zimedhihirisha uwiano na tofauti za viambishi vya mofosintaksia vya nomino katika uainishaji wake tofauti na Kiswahili kama unavyojitokeza katika data ya Jedwali Na. (4.2).

Kwa kuegemea mihimili ya ubia na upatnifu ya Chomsky (1981), data katika Jedwali Na (4.2) inadhihirisha uwiano wa kisarufi wa ngeli baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kiuwiano, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili hudhihirisha viambishi vya mofosintaksia vya nomino katika uainishaji wake kimofolojia na kisintaksia. Viambishi awali vya kimofolojia husababisha mabadiliko ya viambishi vya upatanishi wa kisarufi wa nomino na maneno mengine katika tungo kuwakilisha sifa za mofosintaksia ya Kiswahili. Hii ina maana kwamba, uamilifu wa viambishi ngeli vya nomino kwa umoja na wingi huathiri maumbo ya viambishi vinavyopachikwa kwenye maneno mengine kama vitenzi, vivumishi na viwakilishi katika tungo. Tofauti ni kuwa viambishi vya kimofolojia na kisintaksia vya Luganda

vimedhihirishwa kwa matumizi ya viambishi ngeli na viambishi awali vibainishi vya ngeli. Matumizi haya ni tofauti na ya Kiswahili ambacho hutumia viambishi nomino na vipatanishi vyake kimofosintaksia kama katika data Na (4.2).

Luganda

Kiswahili sanifu

a) *Ente eletendwa kussomero*

Ngo'mbe ameletwa shuleni

b) *Ente ziretendwa kussomero*

Ngo'mbe wameletwa shuleni

c) *Omuti gugude ne gumenya enyumba*

Mti ulianguka na kuvunja nyumba

d) *Emiti gigude ne gimenya amayumba*

Miti ilianguka na kuvunja nyumba

Asili: Data za upatanishi wa kisarufi kutokana na Kiyinikibi, (2021:23)

Nomino 'ente' ni nomino ambayo inapatikana katika Luganda na Kiswahili sanifu. Licha ya kuwa nomino hii ni kiumbe hai, imeainishwa katika ngeli ya 9/10 ikichukua viambishi vya e-zi kisintaksia na kiambishi cha kimofolojia kapa ikiwa haina maumbo wakilishi ya umoja na wingi. Hata hivyo katika Kiswahili, nomino hii imeainishwa katika ngeli ya 1 na 2 ikiwakilishwa na maumbo kapa kimofolojia kuwakilisha umoja na wingi na (a) ya upatanishi wa wingi. Aidha, nomino *nyumba* imeainishwa katika ngeli ya 9/10 katika Luganda na Kiswahili. Hata hivyo, Luganda inatumia maumbo wakilishi ya umoja na wingi (en-) kwa umoja na maumbo (ema-) ya wingi ambayo imetokea kutokana na mabadiliko ya kifonolojia. Hata hivyo, Kiswahili hutumia maumbo kapa kuwakilisha umoja na wingi kimofolojia na kutumia kiambishi kipataishi (i-zi) kwa umoja na wingi. Nomino 'mti' imeainishwa katika ngeli ya 3 na 4 katika Luganda na Kiswahili sanifu.

Ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kiuwiano au kiupatanifu zilidhihirisha kutofautiana katika kiwango cha viambishi viashiria vya nomino vinavyowakilisha umoja na wingi kimofolojia na mofimu zinazowakilisha nomino kwenye vipande vingine vya maneno katika tungo kisintaksia vikiwa na sifa za kisarufi za kimofosintaksia. Mpangilio wa nomino katika ngeli katika Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana kwa kiasi kikubwa sana kama inavyojitokeza katika ngeli za 1 (*m-mu*); 3 (*m-mu*); 4 (*mi-mi*); 5 (*li-li*); 6 (*ma-ma*); 7 (*ki-ki*); 9 (*n-n*); ngeli ya 10 (*n-n*); 15 (*ku-ku*) na ngeli ya 18 (*mu-mu*) kutokana na Namugala (2014 na Mgullu (1999). Ngeli hizi zinadhihirisha uwiano wa maumbo wakilishi ya nomino za Luganda na Kiswahili sanifu kimofolojia. Iitambulika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huainisha ngeli zake kwa kutumia maumbo ya kimofolojia ambayo hufanana na kimpangilio kuchukua mfumo wa kitakwimu ulio mmoja kama unavyojitokeza katika jedwali. Uwiano huu unadhihirisha ubia wa lugha ya Luganda na Kiswahili kwa mujibu wa nadharia ya umilikifu na unganishi. Tofauti inavyojitokeza ni kuwa, licha ya kuwa Luganda na Kiswahili

zinadhihirisha maumbo na mpangilio wa kisarufi, viambishi awali vya ngeli nomino zinazohusika hutofautiana na hata matumizi yake katika tungo hutofautiana kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino kutawala maneno mengine katika tungo. Aidha, tofauti nyingine ni kuwa, Luganda huogeza umbo la ziada linalobainisha maumbo ya ngeli nyuma ya kiambishi ngeli kudhihirisha jinsi nomino kama neno kuu humiliki na kutawala maneno mengine katika tungo. Hali hii ilidhihirisha kuwa lugha hizi za Kibantu zinatofautiana licha ya kuwa na mpangilio wa ngeli na maumbo sawa ya uainishaji wa nomino katika ngeli.

Kisintaksia, data ya ya kifaa cha kudondoa data kuhusu viambishi vya kisintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu kwa mujibu Namugala, 2014; Ssekiryango, 2006; Katamba, 2003; Bochnack 2013; Ssentumbwe, ByeongMan & Lee (2019). ulidhihirisha vilevile kufanana na kutofautiana kwa viambishi vya ngeli za kisintaksia kama katika data ya Jedwali (4.3).

Jedwali 4.3: Uwiano na tofauti za uainishaji wa ngeli za Luganda na Kiswahili Kisintaksia

| Uainishaji | Uainishaji wa Kisintaksia wa Luganda na Kiswahili | |
|-------------------|--|--|
| Nambari | Viambishi ngeli vya upatanishi vya Luganda | Viambishi ngeli vya upatanishi vya Kiswahili |
| 1. | a- | yu-, a- |
| 2. | ba- | wa- |
| 3. | gu- | u- |
| 4 | gi- | i- |
| 5 | li- | li- |
| 6 | ga- | ya- |
| 7 | ki- | ki- |
| 8 | bi- | vi- |
| 9 | e- | i- |
| 10 | zi- | zi- |
| 11 | lu- | u- zi |
| 12 | ka- | - |
| 13 | tu- | - |
| 14 | bu- | u-ya |
| 15 | ku- | ku-ku |
| 16 | wa- | Pa- |
| 17 | ku- | Ku- |
| 18 | mu- | Mu- |
| 20 | gu- | |
| 22 | -ga | |
| 23 | wa- | |

Asili: Leah & Sseguya (2015), Namugala (2014), Beshu (1996) na Mgullu (1999)

Uchanganuzi wa data Na. (4.3) ya maumbo ya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kuhusu uainishaji wa kisintaksia wa nomino katika ngeli kwa mujibu wa mihimili ya ubia na upatanifu ilidhihirisha kuwa, Kisintaksia, ngeli za 1, 5, 7, 10, 15, 17 na 18 zinatumiya viambishi vya upatanishi wa kisarufi unaofanana kimaumbo na kimpangilio. Ngeli hizi zilidhihirisha ubia wa kutumia maumbo ya viambishi vya upatanishi wa kisarufi ulio sawa kimpangilio katika Luganda na Kiswahili sanifu. Hata hivyo kimfumo, maumbo haya yalionekana yakitofautiana kutokana na mifumo tofauti ya uainishaji wa nomino na nomino zinazoainishwa katika ngeli husika.

Matokeo haya yanashadidiwa na Baertlein & Ssekitto (2014) ambao wanaeleza kuhusu upekee wa Luganda kutumia vibainishi ngeli na viwakilishi vya ngeli katika uainishaji wa ngeli na matumizi ambapo vibainishi ngeli vya Luganda huathiri upatanishi wa kisarufi. Aidha, licha ya kuwepo kwa kufanana na kutofautiana kwa maumbo ya nomino kimofolojia na kisintaksia ambapo maumbo awali ya nomino hutawala maneno mengine katika tungo kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu kama inavyoshadidiwa na wataalamu Kapinga, (1983), Mbaabu, (1992), Beshu, (1996), Mgullu, (1999), na Mohamed, (2001), Kihore & wenzake, (2003), Oichoe, (2005); Kisakwah, (2014), matokeo haya yanathibitisha tofauti baina ya Luganda na Kiswahili. Uwiano na tofauti hizi zilidhihirisha kuwa lugha zenye mnasaba moja huwiana na kutofautiana kiisimu katika maumbo na matumizi. Luganda na Kiswahili kwa hiyo ni lugha mbili tofauti ambazo huwiana na kutofautiana kimofosintaksia kwa kuzingatia kipashioa cha kimofosintaksia cha ngeli

4.1.1.4 Kufanana na kutofautiana kuzingatia nafasi ya uambishaji kimofosintaksia

Utafiti huu ulibainisha data Na. (4.3) kuonyesha kufanana na kutofautiana kuzingatia nafasi ya uambishaji kimofosintaksia kwa muhibu wa mihimili ya ubia na upatanifu ya Chomsky (1981);

- | | |
|---------------------------------------|--------------------------------|
| a) <i>Omwana akabila mamawe</i> | <i>Mtoto a-na-m-lilia mama</i> |
| b) <i>Maama amuwadde taata ssente</i> | <i>mama amempa baba pesa</i> |
| c) <i>Maama azi-mu-wadde Ssente</i> | <i>Mama amempa pesa</i> |

Asili: Data za utafiti kutokana na Ssekiryango, (2006)

Uchanganuzi wa data ya Oichoe (2005), Kiyinikibi (2021), Katamba (2003) na Baertlein & Ssekitto, (2014), ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili hutumia viambishi vya nomino katika utungo kudhihirisha upatanishi wa kisarufi wa nomino kwa njia ya urejeshaji ambapo kila nomino huwakilishwa na kiwakilishi nomino cha umoja na wingi katika nafasi moja. Lugha

hizi mbili zilidhihirisha ubia wa kuzitambulisha ngeli kimofolojia na kisintaksia kwa kutumia maumbo ya viambishi ambavyo huwekwa mwanzoni mwa mzizi wa nomino na vivumishi kuwakilisha uainishaji wa kimofolojia na kuweka viambishi mwanzoni mwa mizizi ya vitenzi kuainisha nomino katika ngeli kisintaksia kama inavyojitokeza katika data Na. (4.3).

Aidha, tofauti inayojitokeze ni ile ya kubadilishana kwa virejeshi ambapo kirejeshi nafsi cha Kiswahili kinachomrejelea *mama* [-m-] kimebainishwa ila katika Luganda hakijajitokeza ila kinajitokeza kidhahania na kisemantiki. Aidha katika sentensi (b) ya Luganda kiambishi kiambishi (mu) na (mu) ya Kiswahili inarejelea baba ambaye amepewa pesa. Hata hivyo nafasi ya utokeaji ni tofauti baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Katika mfano wa (c), Luganda imedhihirisha kutumia viambishi viwili vya kuwakilisha pesa (-zi-) na (-mu-) mpokezi wa pesa ambaye ni baba.

Kwa mujibu wa uchanganuzi wa matini kuhusiana na matumizi ya viambishi na nafasi ya utokeaji, utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiana na kutofautiana katika matumizi ya kipashio cha ngeli kimofosintaksia. Aidha, tofauti inayojitokeze ni ile ya kubadilishana kwa virejeshi ambapo kirejeshi nafsi cha Kiswahili kinachorejelea nomino huweza kubainishwa katika Kiswahili huku kiambishi kikijitokeza kidhahania. Kama katika mfano (a) ambapo nomino [mtoto] ya Kiswahili na [*Omwana*] ya Luganda zimewakilishwa na kiambishi [a-] cha upatanishi wa kisarufi kuwakilisha umoja katika ngeli ya kwanza ya lugha hizi mbili. Aidha, nafasi ya utokeaji wa viambishi na idadi inaweza vile vile hutofautiana.

Kinadharia utafiti huu ulibainisha kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili hufanana na kutofautiana katika matumizi ya viwakilishi vya nomino katika tungo, lugha huzi hudhihirisha ubia na upatanifu wa matumizi ya viambishi kudhihirisha uhusiano milikifu na unganishi wa nomino na maneno mengine katika tungo. hii ni mojawapo wa sifa za mihimili ya nadharia ya umilikifu na unganifu.

Matokeo haya yanawiana na yale ya Oduor & Wenzake (2017) ambao katika utafiti wao wanaeleza kuwa: *Uhusiano baina ya nomino na kitenzi hubainika kupitia viambishi vipatanishi vinavyoambatishwa kwenye mzizi wa kitenzi. Viambishi hivi hutangulia viambishi vya wakati.* Maelezo yake Oduor & wenzake (Washatajwa) yanashadidia kuwa maumbo ya upatanishi wa ngeli huwekwa mwanzoni mwa maneno mengine kutegemea nomino inayotajwa. Viambishi awali huwekwa mwanzoni mwa nomino kuwakilisha umoja na wingi

na vilevile kiambishi hicho huwekwa mwanzoni mwa maneno mengine kuwakilisha sifa za upatanishi wa kisarufi na sifa za nomino kuu kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo. Matokeo haya yanaungwa mkono na Namugala, (2014) na Kisakwah, (2014), Mukuthuria, (2004) ambao wanaelezea juu ya nafasi ya utokeaji wa viambishi vipatanishi vya ngeli nomino katika mzizi wa nomino na maneno mengine katika tungo.

4.1.1.5 Kufanana na kutofautiana kuzingatia uidadishaji wa nomino katika ngeli

Data za kufanana na kutofautiana kwa kuzingatia uidadishaji wa nomino katika ngeli ulidhihirisha data inayojitokeza katika Jedwali Na. (4.4).

Jedwali 4.4: Uwiano na tofauti za uainishaji wa ngeli za Luganda na Kiswahili kijozi kimofolojia

| Luganda Sanifu | | | Kiswahili sanifu | | |
|----------------|-----------------------|-----------------------|------------------|------------------|---------------|
| Jozi | Umoja | Wingi | Jozi | Umoja | Wingi |
| 1 | (o) m-/mw-/mu | (a)ba- | 1 | m-/mw-/mu | Wa |
| 2 | (o) mu-/mw- m | (e)mi- | 2 | Mu-/Mw- M | Mi |
| 3 | (e)li-/ Ø- | (a) ma- | 3 | Ji/ Ø- | Ma- |
| 4 | (e) ki- | (e)bi- | 4 | Ki- | Vi- |
| 5 | (e) n-/m-1/ Ø- | (e) n-/m-2/ Ø- | 5 | N-/ Ø- | N-/ Ø- |
| | Umoja | Wingi | | Umoja | Wingi |
| 6 | (o)lu- | (e)n-/m-/ Ø- | 6 | U- | u- |
| 7 | (a)ka- | (o)bu- | 7 | U- | ma- |
| 8 | (o)ku- | (a)ma- | 8 | U- | Zi- |
| 9 | (a)gu- | (o)ga- | 9 | Ya- | Ya- |
| 10 | (o)tu- | - | 10 | i- | i- |
| | (a)wa | | 11 | Ku- | Ku- |
| | E | | 12 | Pa- | Pa- |
| | Ku | | | Ku- | Ku- |
| | Mu | | | Mu | Mu- |

Asili: Byamugisha, Keet, na DeRenzi (2018) na Jerro (2018)

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanisho, data katika jedwali Na. (4.4) ulidhihirisha kuwa Kiswahili na Luganda hufanana katika kuainisha ngeli zake kitakwimu na kijozi katika upangaji wa ngeli kimofolojia na kisintaksia. Ujozi unadhihirisha idadi ya umoja na wingi na idadi wakilishi ya kimosintaksia ya upatanishi wa kisarufi. Kwa kurejelea mfumo huu, matokeo ya uchanganuzi wa data kutokana kifaa cha kudondoa data za maktabani za Katamba, (2003) na Ssentubwa na HyuanLee (2019) iligunduliwa Luganda kuwa na jozi za ngeli 10. Kwa upande mwingine, Kiswahili sanifu kiliorodhesha jozi 12 kwa mujibu wa Mgullu (1999) na Besha (1996).

Ngeli hizi zote zimepangwa katika mkabala wa viambishi vya idadi ya umoja na wingi kuzingatia maumbo ya kimofolojia na uhusiano wa kiupatanifu wa nomino kumiliki na

kutawala maneno mengine katika tungo kisintaksia. Uainishaji huu unadhihirisha kuwa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kutoka ngeli 1 hadi 10 zinadhihirisha utaratibu wa kijozi wa viambishi vya umoja na wingi wa nomino unaowiana. Jozi hizo ni jozi za 1/2, 2./3, 4/5, 6/7 na 9/10. Ngeli nomino kuanzia ngeli ya 11 na kuendelea haidhihirishi utaratibu kamili wa ujozi. Jozi hizi hupangwa kiidadi kudhihirisha maumbo ya mofu wakilishi ya nomino katika umoja ambayo huchukua maumbo ya wingi wa nomino hiyo kutokana na uambishaji wa mofu hizi wakilishi wa mofimu nyuma ya mizizi ya nomino na maneno mengine katika tungo.

Uchanganuzi wa data za Katamba, (2003), Namugala, (2014), Mgullu, (1999) Namugala, (2014a) na Ssentumbwe, Kim, na Lee, (2019) kutumia orodhahakiki ya kutambua utaratibu wa mpangilio wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu, ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia utaratibu wa kijozi na kitakwimu katika upangaji wa ngeli zake kimofolojia na kisintaksia. Uainishaji huu ni ule unaozingatia uhusiano wa nomino na nomino (mofolojia) na uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo (Katamba 2003; Mgullu, 1999). Katika utaratibu huu, data zilidhihirisha utaratibu wa kutumia nambari na maumbo yanayowakilisha idadi ya ngeli kwa umoja na wingi kimofolojia na kisintaksia kama inavyojitokeza katika Jedwali Na. (4.4).

Matokeo ya uchanganuzi wa data kuhusu mpangilio wa ngeli kijozi ulibaini Luganda kuwa na jozi za 1/2, 3/4, 5/6, 7/8, 9/10, 11/10, 12/13, 15/6 na 20/22 za ngeli ambazo zinadhihirisha upatanishi wa kisarufi unaotokana na maumbo nomino wakilishi ya idadi ya umoja na wingi na Kiswahili kuwa na jozi za 1/2, 3/4, 5/6, 7/8, 9/10, 11/10, 14/6. Tofauti inayojitokeza ni kuwa Kiswahili hakina jozi ya 12 na 13 ya {ka-tu}na vile vile idadi ya jozi inatofautiana licha ya kuwa lugha hizi mbili zinadhihirisha utaratibu wa kupanga nomino kuanzia nomino ya 1 hadi 10 kudhihirisha maumbo ya umoja na wingi wa nomino kimofolojia. Jozi zingine katika Kiswahili ni jozi kapa ambazo hazidhihirishi maumbo ya umoja na wingi kimofolojia. Jozi hizi ni zile za ngeli za mahali {pa-ku-mu}, ngeli ya vitenzi jina {ku-} jozi za ngeli ya {i, u, na ya}. Aidha, kwa sababu utaratibu wa kijozi huongozwa na dhana ya maumbo ya nomino na semantiki katika uainishaji, ilibainika pia kuwa kimatumizi maumbo haya hufanana na kutofautiana kutoka jozi za ngeli moja na nyingine.

Matokeo haya ya utaratibu wa uainishaji wa kimpangilio wa ngeli kijozi na kitakwimu unashadidiwa na Bussmann (2006) na Hendrikse na Poulos (1990) wanaofafanua kuwa, kwa kawaida lugha ambazo zina zaidi ya ngeli 20 huainishwa kijozi zikiwa na viambishi

vinavyowakilisha umoja na wingi. Aidha utaratibu wa uainishaji wa ngeli za Luganda wa Jerro (2018) Leah & Sseguya (2015) na utaratibu wa uainishaji wa ngeli za Kiswahili wa Mgullu (1999), Kisakwah (2014) uliuongoza utafiti huu katika kutambua ngeli na kuweza kufananisha na kulinganisha ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kijozi na kitakwimu. Aidha, Sseguya & Leah, (2015) anathibitisha usemi kwa kueleza kuwa:

As a Bantu-language, Luganda is highly orientated on Classes. There are 10 Classes in Luganda that contain different nouns and Class 1 to 9 also have a plural to them(Rose, 2009:8).

Wataalamu hawa wanathibitisha kuwa: Ngeli za Luganda kijozi ni 10 na kitakwimu ni ngeli 21 kama ilivyoelezwa na Marten, (2018): Kiuwiano, kwa mfano, Luganda ina ngeli 21 huku .Kiswahili ikidhihirisha 15.

Kwa mujibu wa Beshu, (1996), Namugala, (2014), utafiti huu uligundua kuwa kijozi, muundo wa kimofolojia wa nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu ni ule ambao nomino moja hujitokeza zaidi ya mara moja katika ngeli tofauti ikiwakilisha maana au dhana tofauti na hivyo viambishi ngeli vya kimofolojia vya ngeli za Luganda na Kiswahili hujipata katika ngeli kadhaa. Muundo huu uliibua mfumo wa viambishi asili vya ngeli ya Luganda na vile vya upatanishi wa kisarufi kuanzia ngeli ya kumi na moja na kuendelea kutofautiana kimofolojia na kisintaksia baina ya Luganda na Kiswahili. Kwa mfano, Ngeli za 1 na 3 na ngeli ya 9 na 10, hutumia viambishi vya umoja ambavyo hufanana ila maumbo yake katika wingi hutofautiana kimofolojia. Aidha viambishi vipatanishi vinavyotumika katika ngeli hizi baina ya Luganda na Kiswahili ndivyo vinavyoweza kutofautisha nomino husika katika ngeli hizi kimaumbo na kisintaksia kama katika data ya maktabani Na.(4.4).

| <i>Luganda sanifu</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|---|--|
| a) Om wana oli agenda okunnywa amata | M toto yule anaenda kunywa maziwa |
| b) Om wezi gunatera okurabika | m wezi unakaribia kuonekana |
| c) Om untu ono akunoonya | m tu huyu anakutafuta |
| d) Om ulingoti gunateera okugwa | M lingoti unakaribia kuanguka |
| e) Em buzi erinya akasozi | M buzi anapanda kilima |

Asili: Data kutokana na usomaji na Baertlein & Ssekitto, (2014)

Mifano (4.4) inadhihirisha maumbo ya ngeli za 1/ 3 na 9/10 kufanana ila yameainishwa katika ngeli mbili tofauti kwa umoja. Utafiti huu uligundua kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili sanifu hudhihirisha kufanana kwa maumbo ya viambishi vya ngeli katika jozi za maneno, uainishaji na tofauti zake kujitokeza katika matumizi kisintaksia. Baadhi ya nomino

zilizoainishwa katika ngeli hizi zimeainishwa katika ngeli tofauti za Luganda na Kiswahili na pia matumizi ya viambishi vipatanishi hutofautiana. Kwa mfano ngeli ya 9/10 katika Luganda ni ya wanyama. Hata hivyo ngeli hizi licha ya kuwa zinadhihirisha maumbo kapa ya ngeli ya 9/10 kimofolojia kwa umoja na wingi, yameainishwa katika ngeli ya kwanza kama ilivyo baadhi ya nomino katika ngeli ya 7/8 ya viumbe hai kama ilivyo katika mfano wa sentensi ya (e). Matokeo haya yanalingana na yale ya Grinevald's (2000), Aikhenvald (2000), Katamba (2003), Rose (2009) Namugala (2014) Vittrant Alice (2005), wanaoeleza kuwa, kitaipolojia ngeli za lugha za Kibantu zimepangiliwa kijozi na kitakwimu.

4.1.1.6 Uwiano na tofauti wa nomino katika ngeli kimfumo wa kimofosintaksia

Data ya uchanganuzi wa uainishaji wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kuegemea kigezo cha maumbo kimofosintaksia ulidhihirisha huwiana na kutofautiana katika matumizi kama inavyojitokeza katika data ya Jedwali Na (4.5).

Jedwali 4.5: Kufanana na kutaofautiana mkabala wa mfumo wa ngeli kijozi

| NGELI ZA LUGANDA KIJOSI | | | | NGELI ZA KISWAHILI KIJOSI | |
|-------------------------|------|---------------------------|---------------------------|---------------------------|---------------------------|
| Ngeli | Jozi | Kiambishi Ngeli cha umoja | Kiambishi ngeli cha Wingi | Kiambishi ngeli cha Umoja | Kiambishi ngeli cha wingi |
| 1 /2 | 1 | (o)mu-a | (a)ba-ba | Mu-/ Mw- M-a | Wa |
| 3/ 4 | 2 | (o)mu- gu | (e) mi-gi | m- u | mi- i |
| 5/6 | 3 | (e)li- li | (a)ma-ga | Ji/Ø- li | Ma- ya |
| 7/8 | 4 | (e) ki-ki | (o)bi- bi | Ki- | vi- |
| 9/10 | 5 | (e)n-/m-1- (e-) | (e)n-/m-2 (zi-) | N-i | N-zi |
| 11/10 | 6 | (o)lu –lu | (e)n-/m-2 (zi) | - | - |
| 12/13 | 7 | ka- ka | (o)bu- bu | u- u | N-zi |
| 14/15 | 8 | (o) tu- | (o)bu | U –u | M-ya |
| 16/17 | 9 | (o)ku- | (a)ma- | Ku | Ku |
| 18/19 | 10 | (a)ga- | (o)gu- | Pa | Pa |
| 20/21 | - | (o) tu-/(a)wa/e/ku | - | Ku | Ku |
| | | Mu | | Mu | Mu |

Asili: Data kutoka na Mulei, Amukowa & Ambuyo (2021) na Jerro, 2018

Jedwali Na. (4.5) linaonyesha uwiano na tofauti wa maumbo wakilishi ya ngeli za nomino za Luganda na Kiswahili sanifu. Luganda imewakilishwa na maumbo mawili ambayo ni vibainishi vya ngeli na viambishi viwakilishi vya ngeli. Kiswahili kimetumia maumbo wakilishi ya ngeli kwa umoja na wingi kimofolojia na maumbo ya upatanishi ambayo huonyesha uhusiano milikifu na unganifu. Matumizi haya ya maumbo wakilishi ya nomino yanadhihirisha sifa bia za maumbo ya nomino ya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu.

Uchanganuzi kwa mujibu wa Namugala, (2014), Besha, (1996) na Bernander, Rasmus, Maud Devos & Hannah Gibson (2018) na Habwe & Karanja (2004) ilidhihirika kuwa, Luganda na Kiswahili sanifu huainisha nomino zake katika ngeli kwa kutumia msingi wa uainishaji wa maumbo kama kitambulisho wakilishi cha nomino katika umoja na wingi. Msingi huu ni ule ambao unapatikana katika lugha zote za Kibantu na ambao hudhihirisha maumbo kijozi na kitakwimu kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu wa maumbo ya kimofolojia ya nomino na maneno mengine kisintaksia. Aidha, kulingana na wataalamu hawa, Luganda na Kiswahili sanifu huweka msingi wa kuainisha nomino katika ngeli kwa sababu nomino ni kipashio kikuu cha kimuundo katika sarufi ya lugha za Kibantu ambapo kiambishi chake hukaririwa kwenye vipande vingine vya sarufi kubeba sifa za kimofosintaksia. Licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huainisha nomino katika ngeli kwa umoja na wingi kutumia maumbo ya kimofolojia na Kisintaksia yanayooshesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo kimofosintaksia, maumbo haya

Kimatumizi, Luganda imetumia viambishi ngeli ambavyo hupachikwa kwa kategoria za maneno kuwakilisha umoja na wingi wa nomino kimofolojia na kiambishi cha upatanishi wa kisarufi wa nomino kisintaksia kuwakilisha sifa za kisarufi za nomino kwa umoja na wingi kama inavyojitokeza katika data Na.(4.5):

| <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|--|-------------------------------------|
| a) <i>Omwana Omulungi asoma ekitabo</i> | <i>Mtoto mzuri anaosma kitabu</i> |
| b) <i>Omusomesa wange agenze kuyimba</i> | <i>Mwalimu wangu ameenda kuimba</i> |
| c) <i>Abasomesa baffe bagenze okuyimba</i> | <i>Walimu wetu wameenda kuimba</i> |
| d) <i>Abaana bange bombi balungi.</i> | <i>Watoto wangu wawili wazuri</i> |
| e) <i>Obulamu bwange bulungi.</i> | <i>Maisha yangu mazuri</i> |
| f) <i>Ebitabo byange byonna birungi.</i> | <i>Vitabu vyangu vyote vizuri</i> |

Asili: Data za utafiti kutokana na Leah & Sseguya (2015), Kiyinikibi (2021)

Mifano Na. (4.5) inadhihirisha maumbo ya kimofolojia na sintaksia yanayobeba sifa za kisarufi za Lugha. Maumbo yaliyokolezwa katika nomino kama vile {Omwa-, omu-} na {aba-} katika Luganda na {m-, mw-} na {wa-} ni maumbo ya mofolojia ya nomino kwa umoja na wingi. Maumbo hayo yametumika katika maneno mengine kama vile vivumishi {**Omulungi-balungi**}, {**wange- baffe**} katika Luganda na {**Mzuri- Wazuri**}, {**Wangu- Wetu**} katika Kiswahili sanifu. Maumbo haya yameathiri maneno mengine katika tungo kama vile vitenzi ambavyo vimechukua viambishi {a-ba} katika Luganda na {a-wa} katika Kiswahili sanifu. Maumbo haya ndiyo yanajenga uainishaji wa nomino katika ngeli kisintaksia na kisemantiki.

Maumbo haya yanaathiri uainishaji wa semantiki kwa sababu sifa za kisarufi zilizokitwa kwenye viambishi hivi ni vya kisemantiki.

Tofauti ambayo inajitokeza katika data ni kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili sanifu huzingatia mofolojia kama msingi wa uainishaji wa nomino katika ngeli kisintaksia, maumbo yanayotokea katika nomino na maneno mengine katika tungo baina ya lugha hizi za Kibantu hutofautiana. Kwa mfano; Luganda hutumia maumbo {Omu- na Omw-} kuainisha nomino katika ngeli kwa umoja na {ba-} kwa wingi kimofolojia na maumbo {a-ba} kwa wingi kisintaksia. Maumbo haya yanafanana na maumbo ya {m-/mu- na mw} yanayoainisha nomino kwa umoja kimofolojia na umbo {a-} la umoja kisintaksia katika Kiswahili, ila hutofautiana katika mfumo wa uainishaji ambapo Luganda huongeza irabu {a, o na a} nyuma ya viambishi ngeli kuainisha ngeli kimofolojia na kisintaksia. Kisintaksia, Kiswahili hutumia kiambishi cha wingi {wa-} kuainisha nomino kisintaksia tofauti na Luganda inayotumia kiambishi {ba-} kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo. Aidha, matokeo haya yanashadidiwa na Namugala (2014) akimnukuu Katamba (2003) kuwa:

According to Katamba (2003), Bantu nouns are categorized into noun classes on the basis of the prefixes that they take and it is the system of noun class prefixes that is the hallmark of Bantu nominal morphology. Katamba perceives a noun class to be signaled by; (1) a pre-prefix and a prefix attached to the nominal stem for both singular and plural cases, (2) grammatical agreement elements including subject pronouns, object pronouns, possessive pronouns, adjective prefixes, and other sentence elements. (Namugala, 2014:6).

Kwa mujibu wa Katamba (2003), Nomino katika lugha za Kibantu zimeainishwa katika ngeli kwa msingi wa viambishi awali vya nomino. Uainishaji huu ni mfumo wakilishi wa ngeli za nomino zenye sifa kuu za kimofolojia za nomino za Kibantu. Nomino hizi huwakilishwa na (1) kibainishi na kiambishi ngeli ambayo huambishwa kenye mzizi wa nomino kwa umoja na wingi (2) viwakilishi vya upatanishi wa kisarufi ambavyo hujumuisha viwakilishi vipatanishi vya kisarufi vya nafsi, nomino, vimilikishi, na vipengele vingine vya sentensi (Namugala, 2016) (TY).

Matokeo haya yanaendana na nadharia ya umilikifu na unganifu ambayo hushikilia mofolojia kuwa nguzo ya uchanganuzi wa ubia na upatanishi wa kisarufi wa nomino kama inavyoelezwa na Chomsky, (1965). Nguzo yenyewe ilibaini ukweli kuwa kiambishi ngeli cha kimofolojia katika Luganda na Kiswahili sanifu huweza kuathiri utokeaji wa maumbo ngeli

mengine katika sentensi kuwakilisha sifa za kisintaksia na kisemantiki. Uchanganuzi vile vile ulitambua kuwa maumbo ya nomino ambayo ni viambishi vya kimofolojia yanayoambishwa kwenye mzizi wa nomino za Luganda na Kiswahili sanifu, kwa kiasi kikubwa hutawala maumbo mengine katika sentensi. Maumbo hayo ya nomino huweza kukaririwa kwenye maneno mengine kuwakilisha upatanishi wa kisarufi katika tungo kama vile vivumishi. Matokeo haya yanaungana na maoni ya wataalamu Mukuthuria, (2004), Oduor na Wenzake, (2017) Kihore na wenzake, (2001) wanaofafanua kuwa maumbo yanayowekwa mwanzoni mwa vitenzi na vionyeshi ndiyo yanavyojenga sintaksia ya nomino na kujenga kigezo cha uainishaji wa nomino kisintaksia.

4.1.2 Uwiano na tofauti ya aina mbalimbali za vivumishi vya Luganda na Kiswahili

Data za utafiti huu zilikusanywa maktabani. Utafiti huu ulichanganua na kufafanua vivumishi vitatu vya umilikaji, a-unganifu, idadi, vionyeshi na sifa. Utafiti huu ulitumia kifaa cha kudondoa data cha orodhahakiki kutambua aina za vivumishi kuegemea mihimili ya Usarufi bia na Upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Unganifu. Data za uchanganuzi matini kutumia kifaa cha kudondoa data cha uchunzaji cha sifa za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia, kutoka kwa vitabu teule ulibaini kuwa, licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, matumizi ya aina mbalimbali ya vivumishi ulidhihirisha kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye aina, maumbo na miundo ya kipekee ya vivumishi ambayo matumizi yake katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo huwiana na kutofautiana kama inavyowasilishwa na kujadiliwa hapa chini.

4.1.2.1 Uwiano na tofauti za Vimilikishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu

Uchanganuzi wa data za maktabani kwa mujibu wa Mgullu (1999), Leah & Sseguya (2015), utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za Kibantu ambazo hutumia vimilikishi kuzingatia nafsi tatu kwa umoja na wingi. Luganda na Kiswahili hutumia mizizi ya kipekee ambayo hutumika kama viwakilishi vya umilikaji na ambayo huwekewa viambishi vipatanishi vya ngeli nyuma yake kulingana na nomino, nafsi na idadi kama inavyojitokeza katika jedwali Na(4.6).

Jedwali 4.6: Uwiano na tofauti za vivumishi vimilikishi kati ya Luganda na Kiswahili

| <i>Umoja/Wingi</i> | <i>Mizizi ya vimilikishi kwa umoja</i> | | <i>Mizizi ya vimilikishi kwa wingi</i> | |
|--------------------|--|------------------|--|------------------|
| | <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> | <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> |
| <i>1</i> | <i>-ange</i> | <i>-angu</i> | <i>-affe</i> | <i>-etu</i> |
| <i>2</i> | <i>-o</i> | <i>-ako</i> | <i>-ammwe</i> | <i>-enu</i> |
| <i>3</i> | <i>-e</i> | <i>-ake</i> | <i>-aabwe</i> | <i>-ao</i> |

Asili: Data za maktabani kutokana na Kyagaba (1996:2015) na Mgullu (1999)

Jedwali Na.(4.6) linadhihirisha uwiano na tofauti za mizizi ya vimilikishi ambayo hubeba maana ya kileksika iliyosetiri maana au maudhui ya umilikaji kutegemea nafsi na idadi ya nomino inayomilikiwa ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kwa kuzingatia mihimili ya sarufi bia na upatanishi, utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili huwiana katika matumizi ya vimilikishi na kutofautiana. Kiuwiano, vivumishi hivi ni vya aina moja (vyote ni vimilikishi) ambavyo vimewekwa katika nafsi tatu kwa umoja na wingi na kutegemea nafsi tatu. Hata hivyo maumbo wakilishi ya mizizi hii ya kileksika baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana. Vimilikishi hivi hubadilika katika kila nomino inayokumushwa kutokana na viambishi tofauti vinavyoambishwa katika kila mzizi ambapo viambishi hivyo hujitokeza kuwakilisha sifa za kisarufi za ngeli za nomino inayokumushwa.

Uchanganuzi wa vimilikishi vya Luganda na Kiswahili kutokana na Namugala (2014) na Mdee na Wenzake (2011), utafiti huu uligundua kuwepo kwa uwiano na tofauti za mizizi ya vivumishi vimilikishi vya Luganda na Kiswahili kwa umoja na wingi kutegemea nafsi. Uwiano na tofauti za mizizi hii ni kama inavyojitokeza katika data ya jedwali Na (4.7):

Jedwali 4.7: Tofauti za vivumishi vimilikishi vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia

| Ngeli | Vipatanishi Nafsi | Nafsi kwa Umoja | | | Nafsi kwa wingi | | |
|-----------|-------------------|------------------------|-----------------------|----------------------|-----------------------|-----------------------|-----------------------|
| Ngeli | Lug/Kisw | N1 | N2 | N3 | N1 | N2 | N3 |
| (O)mu/a | W-/w- | Owange/ wangu | Owuwo/ wako | Owuwe/ Wake | Owaffe/ Wetu | Owammwe/ wenu | Owambwe/ Wao |
| (a)ba-/wa | Ba/w- | Abange/ wangu | Ababo/ wako | Ababe/ Wao | Abaffe/ wetu | Abamwe/ Wenu | Abaabwe/ Wao |
| (o)mu-/m | Gwa/w- | Ogwange/ wangu | Ogugwo/ wako | Ogugwe/ wake | Ogwaffe/ wetu | Ogwabwe/ wenu | Ogwaabwe/ wao |
| (e)mi-/mi | Gya/y- | Egyange/ yangu | Egigyo/ yako | Egyabwe/ yenu | Egyaffe/ yetu | Egyabwe/ Yenu | Egyaabwe/ Yao |
| n-/m-1 | Ya/y- | Eyange/ Yangu | Eyiyo/ Yako | Eyiye/ Yake | Eyaffe/ Yetu | Eyamwe/ yenu | Eyaabwe/ yao |
| n-/m-2 | Za/z- | Ezange/ zangu | Ezizo/ Zako | Ezize/ zake | Ezaffe/ zetu | Ezamwe/ zenu | Ezaabwe/ Zao |
| Ki | Kya/ch- | Ekyange/ change | Ekikyo/ chako | Ekikye/ chake | Ekyaffe/ chetu | Ekyamwe/ Chenu | Ekyaabwe/ chao |
| Bi | Bya/vy- | Ebyange/ vyetu | Ebibyo/ vyako | Ebibye/ Vyake | Abyaffe/ vyetu | Ebyamwe/ vyenu | Ebyaabwe/ Vyao |
| li- | Lya/l- | Elyange/ langu | Elilyo/ lako | Alilye/ lake | Elyaffe/ letu | Elyamwe/ lenu | Elyaabwe/ lao |
| Ma | Ga/y- | Agange/ yangu | Agago/ yako | Agage/ yake | Agaffe/ yetu | Agamwe/ yenu | Agaabwe/ yao |
| Ka- | Ka- | Akange | Akako | Akake | Akaffe | Kamwe | Kaabwe |
| Bu- | Bwa | Obwange | Obubwo | Obubwe | Obwafe | Obyamwe | Obwaabwe |
| Lu- | Lwa | Olwange | Olulwo | Olulwe | Olwaffe | Olwamwe | Olwaabwe |
| n-/m- | Za/z- | Ezange/ zangu | Ezizo/ zako | Ezize/ zake | Ezaffe/ zetu | Ezzamwe/ Zenu | ezaabwe/ zao |
| Ku | Kwa/kw- | Okwange/ kwangu | Ogugwo / kwako | Ogugwe/ kwake | Okwaffe/ kwetu | Okwamwe/ kwenu | okwaabwe/ kwao |
| Ma | Ga | Agange | Agago | Agage | Agaffe | Agamwe | Agaabwe |
| Ga | Ga | Agange | Agabo | Agabwe | Agaffe | Agamwe | Agaabwe |
| Gu | Gwa | Ogwange | Ogwabo | Ogwabwe | Ogwaffe | Ogwamwe | Ogwaabwe |
| Tu | Twa | Otwange | Otutwo | Otutwe | Otwaffe | Otwamwe | Otwaabwe |

Asili: Data kutokana na Leah & Sseguya (2015), Habwe & Karanja (2004)

Aidha, kwa kuzingatia mihimili ya usarufi bia na upatanifu ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo kutokana na uhusiano wa kimiundo wa sheria zinazounganisha vipashio vya kisarufi, utafiti huu ulibaini kuwa vimilikishi vya Luganda na Kiswahili hufanana na kutofautiana. Kwa mujibu wa Jedwali (4.7) kunadhihirika uwiano na tofauti katika uambishaji wa viambishi katika mizizi ya kileksika inayobeba sifa za nomino inayokumushwa kati ya Luganda na Kiswahili kwenye mizizi ya vimilikishi. Data hii inadhihirisha uwiano wa kufanana kwa uambishaji wa

viambishi vya ngeli za nomino kwenye mizizi au shina la kivumishi chenye kubeba maana ya kileksika ya kivumishi. Mizizi ya vimilikishi huunganika na kisabiki chake na huwekewa viambishi vya upatanifu wa ngeli ya nomino inayotajwa mwanzoni. Aidha, viambishi vya kimofolojia vinavyokaririwa kwenye nomino kuwakilisha umoja na wingi (viambishi vya ngeli nomino) ndivyo vinavyowekwa kwenye mizizi maalumu inayoonyesha umilikaji kwa nafsi ya kwanza hadi ya tatu. Uambishaji huu hutegemea ngeli kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa nomino na kimilikishi.

Licha ya uwiano huu, ilidhihirika pia kuwa Luganda na Kiswahili hutumia viambishi ambavyo ni tofauti na viambishi ngeli vya nomino. Isitoshe, vivumishi vimilikishi vya nafsi katika Luganda huwekewa viambishi vibainishi nyuma ya mizizi ya vivumishi huku Kiswahili kikitumia moja kwa moja viambishi vya umilikaji nyuma ya mzizi kudhihirisha umilikaji kutegemea nafsi na idadi ya nomino inayokumushwa kama inavyojitokeza katika data Na (4.6).

- | | |
|---|--|
| a) <i>Engatto zange nnungi, naye ezizo si nnungi.</i> | <i>Viatu vyangu ni vizuri, ila vyako si vizuri</i> |
| b) <i>Ng'enda kutwala ewaffe.</i> | <i>Nitakupeleka kwetu</i> |
| c) <i>Ayagala kugenda ewo.</i> | <i>Anataka kwenda kwako</i> |
| d) <i>Obulamu obwange/ obubwo/obubwe</i> | <i>Maisha yangu/yako/yake</i> |
| e) <i>Essomero eryange/eriryo/erirye</i> | <i>Shule yangu/yako/yake</i> |

Asili: Leah & Sseguya, (2015)

Mifano ya data Na.(4.6) inadhihirisha Uwiano na tofauti ya uambishaji wa mizizi ya vimilikishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Uwiano na tofauti hizi zinakubaliana na mihimili ya Ubia na Upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Unganifu ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo kutokana na uhusiano wa kimofolojia na kimiundo wa sheria zinazounganisha vipashio vya kisarufi wa matumizi ya vimilikishi katika Luganda na Kiswahili Sanifu.

Matokeo haya yanashadidiwa na maelezo ya Philipo (2017) ambaye anakubaliana na Khamisi na Kiango (2002) anayesema kuwa;

vivumishi Kuhusiana na vivumishi vinavyochukua viambishi patanishi ...huchukua aina mbalimbali za viambishi patanishi kulingana na ngeli ya nomino inayokumushwa...

Aidha, Kiango (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa:

Vivumishi hivi hubadilika umbo kufuatana na ngeli ya nomino. Hii ni kutokana na tabia ya Kiswahili kujenga mfumo wa upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi (Philipo, 2017: 130-131).

Matokeo ya utafiti huu yanaendana na ufafanuzi wa Kiyinikibi (2021), Obara (2014) wanaoeleza juu ya mfanano wa muundo wa vivumishi vya Luganda na Kiswahili ambavyo vimeundwa kwa viambishi na mizizi ya kileksika za vivumishi. Kwa kuongezea, Ssentumbwe na Hyunah (2019), Kiyinikibi (2021) Khamisi & Kiango, (2002), Mgullu, (1999) na Obara, 2014) wanaoshadidia kuwa uambishaji wa mizizi ya kileksika ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu huzingatia aina mbalimbali za viambishi vinavyowekwa mwanzoni mwa mzizi wa kileksika wa kivumishi kuonyesha maumbo ya umoja na wingi wa vivumishi na upatanishi wa kisarufi kutegemea ngeli ya nomino inayokumushwa. Aidha, kutokana na maelezo yao, utafiti huu uliweza kufafanua kufanana na kutofautiana kwa vivumishi vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia kutumia viambishi.

Kimatumizi, uchanganuzi wa data kwa mujibu wa Leah na Sseguya, (2015), Ssentumbwe & Hyunah (2019) na Mgullu, (1999) Philipo, (2012), ulidhihirisha uwiano na tofauti za vimilikishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu, Kiuwiano, Vivumishi hivi vyote ni vimilikishi na vimewekwa katika nafsi tatu kwa umoja na wingi. vivumishi hivi vyote vimeathirika na viambishi wakilishi vya nomino ambavyo huwekwa nyuma ya mzizi kuonyesha uhusiano wa nomino na vivumishi kama katika data Na (4.7).

Mizizi ya vimilikishi vya Luganda

- a) *Omwana w-**{ange}** afunye essanyu*
- b) *Abaana b-**{affe}** bafunye essanyu*
- c) *Omusenyu gw-**{o}** mulungi nnyo*
- d) *Omusenyu gw-**{amwe}** mulungi nnyo*
- e) *Ekitanda ky-**{e}** kimennyesse*

Mizizi ya vimilikishi vya Kiswahili

- Mtoto w-**{angu}** amepata furaha*
- Watoto w-**{etu}** wamepata furaha*
- Mchanga w-**{ako}** ni mzuri sana*
- Mchanga w-**{enu}** ni mzuri sana*
- Kitanda ch-**{ake}** kimevunjika*

Asili: Ssentumbwe & Hyunah (2019), Namugala, (2014), na Mgullu, (1999).

Data za mifano (4.7) zinadhihirisha uwiano na tofauti za mizizi ya vivumishi vimilikishi kati ya Luganda na Kiswahili kwa umoja na wingi. Maumbo haya ya nje yanaendana na sifa za sarufi bia ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo, yaani kuna vigezo vinavyozitofautisha lugha. Muundo wa umbo la nje la maumbo patanishi na ya vimilikishi yanachukua mfumo mmoja ila yanatofautiana katika maumbo.

Tofauti iliyojitokeza katika matumizi haya ya viambishi vya kimofolojia ni kuwa, licha ya kuwepo kwa uwiano wa uambishaji wa viambishi wakilishi vya vimilikishi kudhihirisha umilikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo, viambishi vilivyoambikwa kwenye mizizi ya kileksika ya vimilikishi kuwakilishi umilikifu na unganifu wa nomino kutawala vivumishi hutofautiana kutoka lugha moja na nyingine kama inavyodhihirika katika Jedwali Na (4.8).

Jedwali 4.8: Viambishi vipatanishi vya ngeli, vipatanishi, vimilikishi na vimilikishi nafsi

| Luganda | | | | | Kiswahili Sanifu | | | |
|---------|----------------------|--------------------------|--------------------------------------|----------------------------------|----------------------|--------------------------|--------------------------------------|----------------------------------|
| Ngeli | Viambishi vya nomino | Viambishi vya upatanishi | Viambishi vimilikishi Vya upatanishi | Viambishi vimiliki shi vya nafsi | Viambishi vya nomino | Viambishi vya upatanishi | Viambishi vimilikishi Vya upatanishi | Viambishi vimiliki shi vya nafsi |
| 1 | (o)mu- | a- | mu- | a- | m/mu/mw | A | M | w- |
| 2 | (a)ba- | ba- | ba- | b- | Wa | Wa | w- | w- |
| 3 | (o)mu- | gu- | mu- | Gw- | m/mu | U | m- | w- |
| 4 | (e)mi- | gi- | mi- | gy- | Mi | I | mi- | y- |
| 5 | (e)li-/ri- | li- | li- | ly- | Ji/ | Li | Li | l- |
| 6 | (a)ma | ga- | ma- | g- | Ma | Ya | Ya | y- |
| 7 | (e)ki | ki- | ki- | ky- | Ki | Ki | ki- | ch- |
| 8 | (e)bi | bi- | bi- | by- | Vi | Vi | vi- | vy- |
| 9 | (e)n-/m-1 | e- | n- | y-/z | N-N | i-zi | n- | y-/z |
| 10 | (e)n-/m-2 | e- | n- | y-/z- | U- Ø | u-zi | M | w-/z |
| 11 | (o)lu | lu- | lu-/zi | lw-/z | | | | |
| 12 | (a)ka | ka- | Ka/bu- | k/bw | | | | |
| 13 | (o)tu | tu- | Tu | tw- | | | | |
| 14 | (o)bu | bu- | bu- | bw- | | | | |
| 15 | (o)ku | ku/ga | ku-/ma- | kw-/g- | Ku | Ku | ku- | kw- |
| 16 | Wa- | Wa | wa- | w- | Pa | Pa | pa- | p- |
| 17 | Ku | Ku | Ku | kw- | Ku | Ku | ku- | kw- |
| 18 | Mu | Mu | Mu | mw- | Mu | m/mu | M | Mw- |
| 20 | (o)gu- | Gu | gu- | gw- | | | | |
| 22 | (a)ga | ga- | ga- | g- | | | | |
| 23 | (o)tu/e | Tu | Tu | Tw | | | | |

Asili: Leah & Sseguya, (2015), Kyagaba (1996), Namugala, (2014), Mgullu, (1999)

Kwa mujibu wa jedwali (4.8), imedhihirika wazi kuwa licha ya Luganda na Kiswahili sanifu kutumia viambishi vya ngeli nomino katika kuambisha kwenye mizizi ya kileksika ya vimilikishi kutegemea mpangilio wa ngeli za nomino, maumbo ambayo hutumika hufanana na kutofautiana kutoka ngeli moja hadi nyingine.

Matokeo haya yanaendana na ufafanuzi wa Habwe & Karanja, (2007) na Nurse & Philippon, (2014) wanaohibitisha ya kuwa Luganda na Kiswahili hutumia viambishi tofauti vya kimofolojia ambavyo hukaririwa katika matumizi ya vivumishi vimilikishi kuwakilisha upatanishi wa kisarufi. Aidha, kulingana na wataalamu hawa Luganda na Kiswahili huwa haitumii viambishi vya kisintaksia kwenye vivumishi vimilikishi bali vivumishi vya kimofolojia. Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Ssentumbwe na Hyunah (2019), Kiyinikibi (2021), Mgullu (1999) na Obara (2014) ambao walifafanua juu ya kuambisha mizizi ya kileksika ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu kwa kutumia aina mbalimbali za viambishi vinavyowekwa mwanzoni mwa mzizi kuonyesha maumbo ya umoja na wingi wa vivumishi na upatanishi wa kisarufi kutegemea ngeli ya nomino inayokumushwa. Matokeo ya utafiti huu ulidhihirisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kutumia vimilikishi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo, lugha hizi ni lugha mbili tofauti ambazo hudhihirisha tofauti za maumbo ya mizizi na uambishaji wa viambishi ngeli vinavyokaririwa kwenye mizizi ya vivumishi vimilikishi. Hali ambayo inadhihirisha kuwa, Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti ambazo licha ya kuwa na vipashio vilivyo na uwiano, matumizi yake hutofautiana kutokana na upekee wa kiisimu wa lugha za Kibantu ambazo ni za nasaba moja.

4.1.2.2 Uwiano na tofauti za vivumishi vya –a Unganifu vya Luganda na Kiswahili Sanifu

Kwa mujibu wa utafiti huu, uchanganuzi wa matini ulibainisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia {a-}unganifu kuonyesha uhusiano wa nomino na nomino katika utungo kimofosintaksia. Kivumishi hiki kimofosintaksia kilitumika kwa kukiunganisha na mofu zinazowakilisha aina ya ngeli inayohusika kiupatanifu kuonyesha uhusiano wa nomino, umilikaji au kutoa taarifa zinazohusu nomino au kiwakilishi chake katika utungo. Mfano (4.8) wa data za uchanganuzi zinadhihirisha madai haya kama yalivyotolewa na Kisakwah (2014) na Abudonia, (2014) na Baertlein & Ssekitto, (2014) na Sendanda & Asiimwe (2016)

- | | |
|---------------------------------------|--|
| a) <i>Omwana w'omutanda ayinginde</i> | <i>Mtoto wa Mfalme ameingia</i> |
| b) <i>Ennyumba ya Katikiro ewedde</i> | <i>Nyumba ya waziri mkuu imejengwa</i> |

Asili: Data kutokana na Abudonia, (2014)

Kwa mujibu wa data katika mfano Na (4.10), mofu {w'/wa} katika sentensi ya kwanza na {ya} katika sentensi ya pili ni viunganishi vilivyotumika kianafora kutokana na upatanisho wa kisarufi wa nomino na ngeli inayohusika. Kutokana na mifano hii, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili hutumia {-a} unganifu kutegemea upatanisho wa kisarufi wa ngeli

nomino kuonyesha umilikaji, aina, hali na daraja ya nomino inayotajwa katika kirai au utungo. Maelezo haya vilevile yanashadidiwa na Kisakwah (2014) katika maelezo yake ya vivumishi vya –a unganifu. anapoeleza kuwa: “...*Hivi ni vivumishi ambavyo huundwa kwa kiambishi tamati {-a}.*” Anaendelea kueleza kuwa: “..*{-a} ni aina ya kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno.*”

Vilevile, data kutokana na Abudonia (2014), Kiyinikibi (2021) ilidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya {-a} unganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu katika tungo. Iligunduliwa kuwa kiunganifu {-a} kilijitokeza kama kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi ya maneno mbalimbali kimatumizi kama inavyojitokeza katika data Na (4.9).

- | | |
|---|---|
| a) <i>Mukwano gw-a taata Waffe.</i> | <i>Rafiki w-a baba yetu.</i> |
| b) <i>Mikwano gya taata waffe.</i> | <i>Marafiki wa baba zetu.</i> |
| c) <i>Emmere y-o Uganda ewooma nyoo</i> | <i>Chakula cha Uganda ni tamu sana</i> |
| d) <i>Omupiira guno gw-a ddala.</i> | <i>Mpira huu wa kweli</i> |
| e) <i>Ekyo ekitabo ky-a ddala</i> | <i>Hicho kitabu ni cha kweli</i> |
| f) <i>Enyambala y-a musomesa wange.</i> | <i>Kuvaa kw-a mwalimu wangu.</i> |
| g) <i>Enyambala y-a basomesa abaffe .</i> | <i>Kuvaa kw-a walimu wetu .</i> |
| h) <i>Engatto y-a mugaso ebuze.</i> | <i>Kiatu ch-a muhimu kimepotea.</i> |
| i) <i>Engatto z-a mugaso zibuze.</i> | <i>Viatu vy-a muhimu vimepotea.</i> |
| j) <i>Enyumba y-a Kabaka erongoseddwa.</i> | <i>Nyumba y-a Mfale(Kasri)</i> <i>imekarabatiwa.</i> |
| k) <i>Enyumba z-a kabaka zirongozeddwa.</i> | <i>Nyumba z-a Mfalme zimekarabatiwa.</i> |

Asili: Abudonia, (2014), Kiyinikibi, (2021) na Leah & Sseguya (2015)

Aidha, uchanganuzi wa upekuzi wa maandishi ya Mbwillow (2017), Philipo (2012) Leah & Sseguya (2015) na Kisakwah (2014) kuhusiana na vimilikishi vya {-a} unganifu, ilidhihirika kuwa, kiambishi {-a} kimewekwa mwishoni mwa kiambishi cha ngeli cha upatanisho wa ngeli za nomino inayotajwa katika utungo. Hali hii inayoonyesha kuwa kiambishi hiki huwekwa mwishoni mwa kiambishi cha upatanisho wa kisarufi wa nomino inayotajwa kueleza taarifa kuhusu nomino. Hii ina maana kuwa katika lugha zote mbili, kiunganifu {-a} hujitokeza kama kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi ya

maneno mbalimbali. Tofauti inayojitokeza ni kuwa mofu zinazowakilisha aina ya ngeli inayohusika kiupatanifu inayoambikwa kwenye kiunganishi tamati {-a} cha Luganda na Kiswahili hutofautiana kwa sababu ya mfumo au mpangilio tofauti wa ngeli za Luganda na Kiswahili.

Matokeo haya yanashadidiwa na Mbwillow (2017) kuwa vivumishi kama ilivyo kwa aina nyingine za maneno kama vile vitenzi, vina viambishi awali kama vya kwenye nomino. vivumishi hupokea viambishi tamati kama nomino. Viambishi hivyo vya vivumishi huwa sawa na vya nomino kwa kuwa huambikwa kutokana na kurejelea kwa ngeli za nomino (Mbwillow, 2017:13). Tofauti iliyojitokeza ni kuwa, viunganishi vipatanishi vinavyotangulia na ambavyo huambikwa kiunganishi {-a} hutofautiana kati ya Luganda na Kiswahili. Jedwali (4.9) linadhihirisha uwiano na tofauti za vivumishi vipatanishi vya {a-} unganifu vya Luganda na Kiswahili kutokana na Rose (2009), Asimwe (2016) kuhusu viambishi vipatanishi vya {-a} Uganifu.

Jedwali 4.9: Uwiano na tofauti ya vivumishi vipatanishi vya -a unganifu vya Luganda na Kiswahili

| Jozi | Ngeli | | a-unganifu | |
|------|------------|-----------|--------------|--------------|
| | Luganda | Kiswahili | Luganda | Kiswahili |
| 1 | a-ba | a-wa | wa/ba | wa/wa |
| 2 | gu-gi | u-i | gwa/gya | wa/ya |
| 3 | li-ga | li-ya | lya/ga | la/ya |
| 4 | ki-bi | Ki-vi | kya/bya | cha/vya |
| 5 | e-zi | i-zi | ya/za | ya/za |
| 6 | ka-bu | u- | ka/bwa | wa/wa |
| 7 | lu-zi | u-ya | lwa/za | wa/ya |
| 8 | ku-ga | u-zi- | kwa/gwa | wa/za |
| 9 | gu-ga | Ya-ya | gwa/ga | ya/ya |
| 10 | tu- | i-i- | Twa | ya/ya |
| 11 | Ku- | ku-ku | - | kwa/kwa |
| 12 | Wa/e-ku-mu | pa-ku-mu | - | pa/kwa/mwa |

Asili: Data za Utafiti kutokana na Kisakwah, (2014), Leah & Sseguya, (2015)

Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Kisakwah (2014), Habwe na Karanja, (2004), Namugala (2014) na Kiyinikibi (2021) wanaoeleza kuwa; Kiambishi {-a} cha tamati huambishwa kwenye viambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa kwenye

upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno. Uwiano na tofauti za matumizi ya {-a} unganifu ilidhihirisha sifa za mihimili ya Ubia na Upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Unganifu. Mihimili ya nadharia hii huchukulia kuwa, kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo kutokana na uhusiano wa kimofolojia na kimiundo wa sheria zinazounganisha vipashio vya kisarufi.

Kutokana na uchanganuzi wa Baertlein & Ssekitto, (2014) na Leah & Sseguya (2015), tofauti nyingine iliyojitokeza ni kuwa katika Luganda, nomino huweza kuathiri a-unganifu kimuundo na kimofolojia na kusababisha a-unganifu ambayo imedondoshwa na badala yake kiambishi tamati –a kubadilika na kuwa –e. kama inavyojitokeza katika data) (4.10)

- a) *Emmotoka ye somelo* *Gari la shule*
- b) *Emmotoka ze ssomero* *Magari ya shule*
- c) *Ente ye Kampala* *Ng'ombe wa Kampala*

Asili: Data za utafiti kutokana na Baertlein & Ssekitto, (2014)

Kwa mujibu wa mfano huu, kibainishi cha gari ambacho ni ‘e-’ kimeathiri matumizi ya kiambishi tamati cha kuunganisha nomino husika na kusababisha kubadilika kwa kiambishi tamati ‘-a’. Hata hivyo, kibainishi hicho cha ngeli kikidondoshwa, kiambishi tamati ‘-a’ kinabaki katika hali yake kama ilivyo katika Kiswahili. Mabadiliko haya hutokea hasa kwa kuonyesha a-unganifu ya kudhihirisha mahali pa umilikaji wa nomino katika Luganda, hali ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu. Tofauti hii hujitokeza hasa kutokana na kibainishi na hali ya kuashiria mahali inayomiliki nomino. Sifa hii ni ya Ubia na Upatanifu wa nadharia ya Umilikifu na Unganifu ambayo inaonyesha kuwa licha ya kivumishi hiki hutumika katika lugha ya Luganda na Kiswahili sanifu, inadhihirisha tofauti za maumbo ya matumizi ambayo hujitokeza katika Luganda ambapo badala ya kutumia {-a}, kibainishi cha nomino kimechukua nafasi yake. Hali ambayo haijitokezi katika Kiswahili sanifu.

Tofauti nyingine ambayo inajitokeza katika matumizi ya -a unganishi ni kuwa Luganda hudondosha sauti {-a} wakati neno linapongezwa kwenye vimilikishi. Katika mchakato huu, kibainishi cha ngeli nomino hakibadiliki ila kiambishi tamati cha umilikaji hudondoshwa huku Kiswahili kikibakisha mfumo wa matumizi ya {-a} unganifu’ ya umilikaji wa nomino inayotajwa bila kudondosha kiambishi tamati cha uhusiano au unganifu kutokana na upekuzi wa maandishi maktabani kama inavyojitokeza katika data (4.11) kutokana na Leah & Sseguya (2015: 27).

| | |
|---------------------------------|----------------------------|
| a) <i>Omwana wa omusajja.</i> | <i>Mtoto wa mwanamume.</i> |
| <i>Omwana w'omusajja</i> | <i>Mtoto wa mwanamume</i> |
| b) <i>Embuzi ya omulimi</i> | <i>Mbuzi ya mkulima</i> |
| <i>Embuzi y'omulimi</i> | <i>Mbuzi ya mkulima</i> |
| c) <i>Ekitabo kya omusomesa</i> | <i>Kitabu cha mwalimu</i> |
| <i>Ekitabo ky'omusomesa</i> | <i>Kitabu cha mwalimu</i> |

Asili: Kutokana na uchanganuzi wa maandishi ya Leah & Sseguya, (2015: 27)

Kwa mujibu wa sentensi za hapo juu, kiambishi {-a} cha umilikaji katika Luganda kinadhihirishwa kudodoshwa wakati kinapongezwa nyuma ya nomino inayomiliki kitembo au jambo au kitu husika. Hali hii inatofautiana na Kiswahili ambacho huwa hakidhihirishi matumizi haya. Uwiano na tofauti hizi zilidhihirisha kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili huzingatia usarufi bina na upatanishi wa kutumia kivumishi cha -a unganifu, matumizi yake katika Luganda huchukua maumbo tofauti ya kudodoshwa kiunganishi, huku Kiswahili kikibakisha hadhi ya -matumizi ya -a unganishi bila kubadilisha umbo lake, wala kudodoshwa. Matokeo haya yanaendana na matokeo ya Rose, (2009), Kiyinikibi, (2021) na Katamba, (2003) na kushadidiwa na Baertlein & Ssekitto, (2014) ambao wanaelezea juu ya muundo na matumizi ya kivumishi cha {-a} unganishi.

Matokeo haya yanashadidiwa na yale ya Kisakwah (2014) aliyetambua kushabihiana kwa matumizi ya kiunganishi -a ambacho ni kivumishi cha {-a} unganifu baina ya Kiolusuba na Kiswahili sanifu. Kushabihiana kwa matumizi ya kivumishi cha {-a} unganifu baina ya Luganda na Kiswahili kulitokana na uambishaji wa viambishi vya ngeli ambavyo viliwekwa kabla ya mzizi huu kuwakilisha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo kama inavyoelezwa na Kisakwah (keshatajwa kuwa, “Kiunganifu {-a} hujitokeza kama kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi ya maneno mbalimbali” (Kisakwah, 2014: 36). Tofauti iliyojitokeza ni kuwa {-a} unganifu ya Luganda huwa haidodoshwi kama ilivyo Luganda. Uibukaji wa wiano na tofauti za kipashio hiki kulidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti kiisimu licha ya kuwa ni lugha za nasaba moja.

4.1.2.3 Uwiano na Tofauti za Vivumishi Vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu

Matokeo ya uchanganuzi wa maandishi ya maktabani kutokana na Leah & Sseguya (2015) na Habwe & Karanja, (2004) kutimbia kifaa cha kudodoa data, utafiti huu uligundua kuwa

Luganda na Kiswahili sanifu hudhihirisha aina kuu mbili za vionyeshi. Vionyeshi vilivyoainishwa ni vionyeshi vya karibu na vionyeshi vya mbali. Vionyeshi vya mbali kiubia ni vya aina mbili, mbali na mbali zaidi. Vionyeshi vya karibu ni vile viashiria ambavyo vipo karibu sana na mtoaji kauli ambaye hana hata uwezo wa kuviona na kuvigusa vitu au nomino inayozungumziwa. Vilevile, kuna vionyeshi vya mbali ambavyo hutumika kuashiria nomino ambayo ipo mbali kidogo na vile vya mbali sana ambapo mzungumzaji au msikilizaji hana uwezo wa kuvigusa kutokana na umbali wake. Kwa mujibu wa uchanganuzi, vionyeshi hivi vimepangwa kimuundo kutegemea nafasi ya mzungumzaji na viambishi vya ngeli nomino kwa umoja na wingi kama inavyojitokeza katika data ya jedwala (4.10) kutokana na Kisakwah, (2014); Obara, (2014) na Katamba, (2003); Leah & Sseguya (2015) na Kyagaba (1996).

Jedwali 4.10: Uwiano na tofauti za viwakilishi vya vivumishi vionyeshi vya Luganda na Kiswahili

| <i>Ngeli Kimofosintaksia</i> | | <i>Nomino</i> | <i>Nafasi</i> | | |
|------------------------------|------------------|---------------------------|-------------------|---------------------|--------------------|
| <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> | <i>Nomino</i> | <i>Karibu</i> | <i>Mbali kidogo</i> | <i>Mbali zaidi</i> |
| <i>a-</i> | <i>A</i> | <i>Omusomesa/ mwalimu</i> | <i>Ono/huyu</i> | <i>Oyo/Huyo</i> | <i>Oli/Yule</i> |
| <i>ba-</i> | <i>Wa</i> | <i>Abasomesa/ walimu</i> | <i>abo/hawa</i> | <i>abo/Hao</i> | <i>bali/wale</i> |
| <i>gu-</i> | <i>U</i> | <i>Omugati/mkate</i> | <i>Guno/ huu</i> | <i>ogwo/ huo</i> | <i>guli/ ule</i> |
| <i>gi-</i> | <i>I</i> | <i>Emigati/Mikate</i> | <i>Gino/ hii</i> | <i>egyo /hiyo</i> | <i>giri / ile</i> |
| <i>li-</i> | <i>Li</i> | <i>Linnyo/jino</i> | <i>Lino/ hili</i> | <i>Eryo / hilo</i> | <i>Liri /lile</i> |
| <i>ga-</i> | <i>Ya</i> | <i>Amannyo/meno</i> | <i>Gano/ haya</i> | <i>Agwo / hayo</i> | <i>Gali / yale</i> |
| <i>ki-</i> | <i>Ki</i> | <i>Ekikopo/kikombe</i> | <i>Kino/ hiki</i> | <i>Ekyo / hicho</i> | <i>Kiri /kile</i> |
| <i>bi-</i> | <i>Vi</i> | <i>Ebikopo/vikombe</i> | <i>Bino/ hivi</i> | <i>Ebyo /hivyo</i> | <i>Biri /vile</i> |
| <i>e-</i> | <i>I</i> | <i>Enyumba/nyumba</i> | <i>eno /hii</i> | <i>Eyo/hiyo</i> | <i>Eri/ ile</i> |
| <i>-</i> | <i>Zi</i> | <i>Nyumba</i> | <i>Zino/Hizi</i> | <i>Ezo/Hizo</i> | <i>Zili/Zile</i> |
| <i>-</i> | <i>U</i> | <i>Ukuta</i> | <i>Huu</i> | <i>Huo</i> | <i>Ule</i> |
| <i>zi-</i> | <i>Zi</i> | <i>Nyumba/ Kuta</i> | <i>Zino/ hizi</i> | <i>ezo/hizo</i> | <i>ziri /zile</i> |
| <i>lu-</i> | | <i>Olulimi/Ulimi</i> | <i>Luno/huu</i> | <i>Olwo/huo</i> | <i>Luli/ule</i> |
| <i>Zi</i> | <i>-</i> | <i>Endimi/ndimi</i> | <i>Zino/hizi</i> | <i>Ezo/hizo</i> | <i>Zili/zile</i> |
| <i>ka-</i> | <i>Ka-</i> | <i>Akaana</i> | <i>Kano</i> | <i>Ako</i> | <i>Kali</i> |
| <i>tu-</i> | | <i>Otulo</i> | <i>Tuno</i> | <i>Otwo</i> | <i>Tuli</i> |
| <i>bu-</i> | | <i>Butale</i> | <i>Buno</i> | <i>Obwo</i> | <i>Buli</i> |
| <i>ku-</i> | <i>Ku</i> | <i>Kusoma</i> | <i>kuno/ huku</i> | <i>okwo /huko</i> | <i>Kuli /kule</i> |
| <i>wa-</i> | <i>Pa</i> | <i>Awantu/ pahali</i> | <i>Wano/ apo</i> | <i>awo/ hapo</i> | <i>wali/ pale</i> |
| <i>ku-</i> | <i>Ku</i> | <i>Kukyalo/ ahali</i> | <i>Kuno/huku</i> | <i>okwo/huko</i> | <i>kuli/kule</i> |
| <i>mu-</i> | <i>m/mu</i> | <i>Munyumba/chumbani</i> | <i>Muno/ humu</i> | <i>omwo/ humo</i> | <i>muli/ mle</i> |

Asili: Data kutokana na Kisakwah, (2014) na Leah & Sseguya (2015)

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya Chomsky (1981) utafiti huu ulibaini kuwa, vivumishi vimilikishi vya Luganda na Kiswahili vimepangwa katika nafasi tatu ya

karibu, mbali kidogo, na mbali sana kutegemea mahali aliko mzungumzaji na msikilizaji. Pia, imetambulika kuwa vionyeshi hivi hutumika kulingana na ngeli kwa umoja na wingi. Aidha, katika utaratibu wa ngeli, kila kiashiria kimechukua kiambishi ngeli cha upatanishi wa nomino inayozungumziwa. Hata hivyo, maumbo ya vionyeshi vya Luganda na Kiswahili yanatofautiana kutokana na viambishi tofauti vya ngeli na vipatanishi vyake kulingana na lugha husika katika matumizi. Hali ambayo inadhihirisha kuwa, licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, zinawiana na kutofautiana katika mizizi wakilishi ya vivumishi na viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi hiyo kuwakilisha umilikifu na unganifu wa vipashio vya kisarufi wa lugha hizi mbili. Hii inatokana na kuwa, viashiria vya karibu vya Kiswahili vimeundwa kwa mzizi wa kivumishi [**h-**], kikifuatwa na irabu ya upatanishi kutegemea kipatanishi cha nomino tajwa na kipatanishi cha nomino inayozungumziwa. (vipatanishi vya ngeli). Luganda inatumia kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino inayozungumziwa na mzizi wake [**-no**] ambao huwekwa baada ya kiambishi ngeli cha upatanishi ijapokuwa ngeli ya kwanza ambayo hutumia viambishi tofauti vya [**ono** na **oyo**] karibu na mbali sana.

Kwa kuzingatia viashiria vya mbali kidogo, Kiswahili kimeundwa na mzizi wa kivumishi [**h-**], kivumishi kirejeshi cha mbali kidogo na kirejeshi cha nomino iliyotajwa. Luganda inatumia mzizi [**-li**] ambao unaambishwa kiambishi ngeli cha upatanishi nomino kuashiria nomino katika nafasi ya pili au mbali kidogo na mahali aliko mzungumzaji. Mwisho, vionyeshi vya mbali vya Kiswahili vina kipatanishi cha nomino kulingana na ngeli, na mzizi [**-le**]. Hata hivyo, viashiria vya Luganda vinaonekana kutumia vibainishi vya nomino, vikifuatwa na maumbo ya viambishi vya ngeli ambavyo huathirika kifonolojia na mwisho kiishio [**-o**] kutumika katika kila ngeli kuashiria umbali kidogo wa nomino inayozungumziwa.

Ugunduzi huu unafanana na maelezo ya wataalamu Dixon (1982: 2010), Rose (2009), Habwe & Karanja (2004) na Mgullu, (1999) ambao wanaeleza kuwa kila aina ya kivumishi katika lugha za Kibantu huwa na umbo na muundo wake unaotofautisha kivumishi kimoja na kingine katika orodha ya vivumishi vilivyoainishwa katika kila lugha. Vile vile wataalamu Rose (2009), Katamba (2003), Mgullu (1999) na Obara, (2014) wanaungana na utafiti huu ambao unakubaliana na matokeo ya awali. Kwa mujibu wa utafiti huu, kila lugha hudhihirisha maumbo na miundo tofauti za mizizi ya kileksika ya vivumishi ambavyo haumbishwa viambishi vya kimofolojia na kisintaksia kuwakilisha uhusiano umilikifu na unganifu wa vipashio vya kisarufi. Aidha viambishi hivi ni vile viambishi vipatanishi

vinavyoambikwa kwenye mizizi husika kulingana na nomino ngeli ya nomino inayokumushwa kwenye kivumishi kionyeshi kuonyesha uhusiano wa nomino na kionyeshi katika tungo.

Vilevile, orodhahakiki kuhusiana na nafasi ya vivumishi vionyeshi kutokana na upekuzi wa matini ya Abudonia (2014) uligunduliwa kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika huweka vionyeshi baada ya nomino katika lugha hizi mbili hata hivyo, utokeaji wa kiwakilishi cha kionyeshi mwanzoni mwa nomino hutokana na muktadha na dhana inayohusiana na matumizi yake. Kwa kuzingatia mihimili ya Ubia na Upatanifu, ilibainika kuwa vivumishi vionyeshi vya Luganda na Kiswahili vina sifa za nafasi za matumizi zinazofanana. Hata hivyo, kila lugha ilikuwa na maumbo ya viashiria vyake ambavyo vinatumika kulingana na upatanisho wa kisarufi wa ngeli za nomino kianafora na kuzingatia muktadha wa matumizi ya vionyeshi. Mfano wa data Na. (4.12) unadhihirisha kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya vionyeshi vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia: (4.12)

a) *Omukyaala* **ono** agala emerre *Mwanamke* **huyu** anataka chakula
 N **V** **T** **N** **N** **V** **T** **N**

b) **Ono** omukyaala agala emerre **Huyu** mwanamke anataka chakula
 V **N** **T** **N** **V** **N** **T** **N**

Asili: Data za utafiti kutokana na Kiyinikibi, (2021) na Leah & Sseguya (2015)

Kimofosintaksia, sentensi ya kwanza imezingatia kanuni ya anafora ambapo nomino inayozungumziwa imedhihirishwa kwa uwazi kwa kutoa taarifa inayohusu nomino [*mwanamke/Omukyaala*] tofauti na sentensi ya pili ambayo mbali na kuwa imetumia kionyeshi, kionyeshi hiki hakifanyi kazi kimofosintaksia bali kisemantiki kati ya Luganda na Kiswahili. Kionyeshi hiki kimedhihirisha kanuni ya katafora ya nomino mwanamke.

Matokeo haya yanafafanuliwa katika kazi za (Abudonia, (2014), Katamba, (2003), Dixon, (2010), Habwe & Karanja, (2004), Kisakwah, (2014) wanaoshadidia juu ya muundo wa vionyeshi na nafasi ya utokeaji katika matumizi ya vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Licha ya kuwa hawakufanananisha na kutofautisha, maelezo yao yalikuwa msingi wa kufanananisha na kutofautisha vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo ya uchanganuzi huu kuhusu vionyeshi vya Luganda na Kiswahili vinashadidiwa na Sternefeld na Nickshere (2015) ambaye anaeleza kuwa:

...even the demonstrative pronouns of Luganda highly depend on the class of the noun the pronoun is referring to. Every class and number has its own pronoun. order to form this pronoun, the adjective prefix is added to –no. referring to a person within sight or being close to the speaker ... while ‘oyo’ is referring to somebody more distant or absent (‘omukazi oyo’, ‘that woman’). Anaendelea kusema kuwa: In Luganda it is common to drop the noun: ‘on’ani?’ ‘who is this?’; ‘on’agambye..’ (this one said..). As we have learned, there are some objects in the first class that don’t have the prefix ‘mu’ and are certainly not people: Caayi (tea), Ffene (jackfruit), balansi (balance), . Even in this case ‘ono’ or ‘oyo’ is used (Leaha na Sseguya, 2015:61).

Naye Kisakwah (2014) akieleza jinsi vionyeshi vya Kisuba vinavyotofautiana na vya Kiswahili, anaeleza kuwa:

Kiswahili kina vivumishi vionyeshi vya namna tatu, yaani vivumishi vionyeshi vya karibu na msemaji, vivumishi vionyeshi vya karibu na msikilizaji, kadhalika kuna vivumishi vionyeshi visivyokuwa karibu na msemaji wala msikilizaji. Kwa upande mwingine, pekee. Vivumishi vionyeshi huweza kuwa katika nafsi tatu kutegemea upatanisho wa ngeli. Vivumishi hivi huonyesha dhahiri kinachozungumziwa mathaalani, ni nani au nani kafanya jambo gani (Kisakwah, 2014:37).

Matokeo ya uchanganuzi huu yalidhihirisha kuwa, licha ya Luganda na Kiswahili kudhihirisha mfanano wa kuainisha vionyeshi vyake katika nafsi tatu kimofosintaksia kutegemea viambishi vya ngeli ambavyo huwekwa katika mwanzoni kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu, Vionyeshi hivi hutofautiana kimaumbo na katika matumizi yake ya kimofosintaksia kutegemea ngeli za nomino na upatanishi wa kisarufi wa nomino inayozungumziwa wakati wa matumizi. Aidha, vionyeshi vya Luganda na Kiswahili vina maumbo ya kimofolojia inayotofautisha kiashiria cha karibu na mbali kutegemea nafasi ya mzungumzaji na ngeli za nomino kiupatanisho. Hii ina maana kuwa kila kionyeshi katika Luganda na Kiswahili huwa na kionyeshi cha aina yake kinachotofautiana kulingana na ngeli nomino inayotajwa katika utungo na nafasi ya mzungumzaji.

4.1.2.4 Uwiano na Tofauti za Vivumishi vya Sifa vya Luganda na Kiswahili

Uchanganuzi wa data za utafiti kuhusiana na vivumishi vya sifa vya Luganda na Kiswahili sanifu, Utafiti huu uligundua kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha ambazo huwiana na kutofautiana katika kutumia vivumishi vya sifa kueleza zaidi juu ya nomino. Vivumishi hivi hutumika kuonyesha hulka au jinsi au mwonekano wa nomino tajwa katika mazungumzo na

maandishi yao. Aidha, vivumishi hivi huchukua viambishi ngeli vya nomino vinavyovumishwa kimaumbo na kimuktadha. Viambishi hivi huwekwa kwenye mzizi unaobeba maana ya kilekiska ya kivumishi husika katika utungo kama inavyojitokeza katika data ya jedwali Na. (4.11).

Jedwali 4.11: Uwiano na tofauti ya viambishi awali vya sifa vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia

| JOZI | Ngeli ya Luganda | Ngeli ya Kiswahili | Nomino | Kivumishi cha sifa | Viambishi awali vya sifa |
|------|------------------|--------------------|--|---|--------------------------|
| 1 | omu- /aba | Mu-/ Mw-/ M- Wa | Omusomesa/abasomesa Mwalimu/walimu | omulungi/abalangi Mzuri/wazuri | omu-/aba- m-/wa- |
| 2 | omu-/emi | M- Mi | Omuti/emiti Mti/miti | Omulungi/emirungi Mzuri/mizuri | omu/emi m- /mi- |
| 3 | eli-/ama | Ji/Ø- Ma- | Elinyo/amanyo Jino/meno | Eddungi/amarungi Nzuri/mazuri | ed-/ama n-/ma- |
| 4 | eki-/ebi | Ki- Vi- | Ekitabo/ebitabo Kitabo/vitabu | Ekilungi/ebirungi Kizuri/vizuri | Eki-/ebi-Ki- /vi- |
| 5 | en-/en | N- N- | Enkoko/enkoko Nyumba/nyumba | Ennungi/ennungi Nzuri/nzuri | en-en N-N |
| 6 | aka-/obu | U- | Akantu/obuntu Utajiri | Akalungi/obulingi Mzuri | aka-/obu- m- |
| 7 | olu-/en-/m- | U-Ma- | Olugelo/engelo Upendo/mapenzi | Olulungi/ennungi Mzuri/mazuri | olu-/en- m-/ma |
| 8 | ogu-/aga | U- zi | Oguwala/agawala Ubao/mbao | ogulungi/agalungi Mzuri/nzuri | Agu-/aga- m-/n |
| 9 | Oku-/ama | Ya-Ya- | Okutu/amatu Maji | Okulungi/amalungi Mazuri | oku-ama ma- |
| 10 | otu-/out | i-i- | Otulo Sukari | Otulungi Nzuri | Out n- |
| 11 | - | Ku-ku | Kusoma | Kuzuri | ku- |
| 12 | Wa | Pa-pa | Awantu Pahali | Awalungi Pazuri | awa- pa- |
| | Ku | Ku-ku | Mahali | Kuzuri | ku- |
| | Mu | Mu-mu | Shuleni/mahali | Mzuri/mwema | m- |

Asili: Data za Utafiti kutokana na Leah & Sseguya(2015); Mgullu, (1999); Besha, (1996)

Kwa kuzingatia mihimili ya Ubia na Upatanisho, data katika Jedwali (4.11) inadhihirisha uwiano na tofauti za viambishi vipatanishi vya msingi vinavyowekwa kwenye vivumishi vya sifa kuonyesha umilikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Kila kivumishi kimewakilishwa na mzizi wake wa kileksika wa kivumishi cha sifa na kila

kivumishi kuambishwa kiambishi cha nomino inayokumushwa. Lugha zote zina vivumishi ambavyo huundwa kwa kiambishi awali cha kivumishi ambacho hufanana na kiambishi awali cha nomino inayovumishwa na mzizi wa vivumishi ambao hubeba maana ya kileksika ya vivumishi hivyo.

Hata hivyo, utafiti huu uligundua kuwa viambishi vinavyoambikwa kwenye mizizi ya vivumishi hutofautiana kutokana na maumbo ya ngeli pamoja na athari za kifonolojia ambazo hutokea katika lugha kati ya Luganda na Kiswahili sanifu (Nurse na Philippon, 2014; Katamba, 2003). Kwa mfano, nomino ‘*Maji*’ katika Kiswahili huchukua kiambishi [ma-] inapowekwa kwenye mzizi wa kivumishi. *Maji* katika Luganda ni ‘*Mazzi*’ ambayo huchukua kiambishi {ama-}. Luganda imetumia sana vibainishi na viambishi ngeli kama viambishi awali vinavyoambikwa kwenye mizizi ya vivumishi vya sifa tofauti na Kiswahili, ingawa vyote vinatokea katika nafasi moja ya kimofolojia. Aidha, nomino katika ngeli ya 5, 8 na 9 ni majina ambayo ni tofauti na majina katika ngeli ya Kiswahili. Tofauti hii ya nomino huathiri maumbo ya kimofosintaksia ya kuambisha viambishi vya kileksika vya vivumishi vinavyoambishwa na hivyo kuonyesha tofauti kati ya Luganda na Kiswahili kimatumizi. Matokeo haya ynatokana kazi za Mgullu (1999), Besha, (1996), Kiyinikibi, (2021), Namgala, (2014), Leah & Sseguya (2015), Habwe & Karanja (2004) na kushadidiwa na maelezo ya Nurse & Philippon, (2003) na Katamba, (2003) wanaoeleza kuwa Viambishi vinavyoambikwa katika kivumishi cha sifa katika lugha za Kibantu hubadilika kutokana na aina ya nomino inayotajwa kwani kila nomino ina kiambishi chake kutegemea ngeli inamotokea. Vilevile Mukuthuria (2004) naye anashadidia kwa kusema kuwa mfumo wa mpangilio wa nomino fulani katika lugha asilia unaweza kuwa tofauti ikiwa nomino hiyo itakopwa katika lugha nyingine. Kila kivumishi kimewakilishwa na mzizi wake wa kileksika wa kivumishi cha sifa na kila kivumishi kuambishwa kiambishi cha nomino inayokumushwa. Aidha, Kisakwah (2014) na Rose, (2009) katika kueleza juu ya vivumishi vya Luganda walidhihirisha kuwa kimofosintaksia, Luganda na Kiswahili huambisha maumbo ya viambishi awali vya nomino kwenye mizizi inayobeba maana ya kileksika ya vivumishi vya sifa kutoa taarifa zaidi za kisarufi za nomino inayotajwa kuonyesha uhusiano wa kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo.

Matokeo haya yanathibitisha kuwa licha ya Luganda kuwa na vipashio vya kimofosintaksia ambavyo huwiana, upekee wa lugha hizi kiisimu hudhihirisha kutofautiana kiisimu. Licha ya kuwa kisarufi lugha hizi mbili zilidhihirisha ubia wa sifa, kiupatanifu maumbo yaliyojitokeza

yalidhihirisha kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti licha ya kuwa ni lugha za nasaba moja hali inayoendana na mihilimi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya sarufi bia na upatanisho.

4.1.2.5 Uwiano na tofauti za Vivumishi vya Idadi vya Luganda na Kiswahili Sanifu

Vivumishi vya idadi ni vivumishi ambavyo hututajia idadi ya nomino inayokumushwa katika utungo (Habwe & Karanja 2004; Kisakwah, 2014; Mgullu, 1999). Kuna aina kuu mbili za vivumishi vya idadi katika Kiswahili na Luganda, vivumishi vya idadi dhahiri na isiyodhahiri, Utafiti huu uliegemea kuchunguza vivumishi vya idadi isiyodhahiri vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia ili kuweza kubaini uwiano na tofauti katika matumizi.

4.1.2.5.1 Vivumishi vya idadi isiyodhahiri

Matokeo ya data za uchanganuzi wa matini ya vivumishi vya idadi kiuainishaji kutokana na Mgullu (1999) Snoxall (1955), Leah & Sseguya (2015) uligundua kuwa, maumbo na matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo kamili baina Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana kama inavyojitokeza katika data Na. (4.13):

| Luganda | Kiswahili |
|----------------|------------------|
| <i>-ngi</i> | -ingi |
| <i>-tono</i> | -chache |
| <i>-tono</i> | -dogo |
| <i>-lala</i> | -ingine |
| <i>-onna</i> | -ote |
| <i>-onna</i> | -o-ote |
| <i>-ku</i> | -kiasi |

Asili: Data za Utafiti kutokana na Mgullu, (1999) na Leah & Sseguya, (2015)

Kwa kurejelea nadharia ya Ubia na upatanishi inayoshikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika, utafiti huu ulibaini kuwa Luganda hutumia mizizi saba kudhihirisha idadi ya vivumishi visivyodhahiri. Mizizi hii ni *-ngi (-ingi)* inayotumika kueleza zaidi juu ya wingi wa nomino, *-tono (-chache na -dogo)* ambayo hutumika kimkutadha kutoa taarifa ya nomino inayokumushwa kuhusu uchache wake na udogo wa nomino tajwa kiidadi sifa ambayo inapatikana katika lugha nyingi za Kibantu. *-lala*

(*-ingine*), mzizi ambao hutumika kudhihirisha idadi *-ingine* ya nomino inayokumshwa na mzizi *onna (-ote na -o-ote)*, mzizi unaodhihirisha idadi *-ote* na *-o-ote* ya nomino inayokumshwa. Aidha, Luganda hutumia silabi **[ku]** kimkutadha na kileksika kumaanisha *kiasi* cha idadi isiyodhahiri ya nomino au kutaja baadhi ya idadi bila kutaja idadi kamili. Kwa mujibu wa Mgullu, (1999) Kiswahili kina jumla ya mizizi saba ya vivumishi ambayo hubeba maana ya kileksika ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri. Licha ya kuwepo kwa uwiano, ilibainika kuwa maumbo na matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo kamili baina Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana.

Kimofosintaksia, uchanganuzi wa maelezo ya Ssentumbwe na Hyunah, (2019), Habwe & Karanja, (2004) na Oichoe (2005) ulibaini kuwa vivumishi vya idadi isiyodhahiri vya Luganda na Kiswahili vina sehemu kuu mbili kimofosintaksia ambavyo hutumika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na kivumishi katika tungo. Sehemu ya kwanza ni ya kiambishi awali ambacho pia ni kipatanishi cha wingi wa nomino kinachowekwa kabla ya mzizi wa kivumishi na mizizi ya vivumishi ambavyo hubeba maana ya kileksika ya kivumishi cha idadi ya nomino inayotajwa. Kiambishi hiki ni kiambishi ambacho kinaendana na mhimili wa upatanishi wa nadharia ya umilikifu na unganifu kama inavyojitokeza katika jedwali Na. (4.12).

Jedwali 4.12: Uwiano na tofauti ya vipatanishi na mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu

| <i>Ngeli za Kiswahili/Luganda</i> | <i>Nomino za Kis/Lug</i> | <i>Kip Kis/Lug</i> | <i>Mzizi ya Kis/Lug</i> | <i>Kiswahili (Kis)/Luganda(Lug)</i> |
|-----------------------------------|--------------------------|--------------------|-------------------------------|---|
| <i>M-wa/mu-ba</i> | <i>Watu/abantu</i> | <i>wa-/ba-</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Wengi/bangi</i> |
| | | <i>Wa/ba</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Wachache Batono</i> |
| | | <i>i/by</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>wote /wowote /byonna</i> |
| | | <i>Wa/ba</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Wengine/Balala</i> |
| | | <i>Ku/ba</i> | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidodgo Ku bantu/batono</i> |
| <i>M-mi/Omu-emi</i> | <i>Miti/emititi</i> | <i>Mi/emi</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Mingi/emingi</i> |
| | | <i>Mi/emi</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Michache/emitono</i> |
| | | <i>I</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>Yote/yoyote/gyona</i> |
| | | <i>Mi/emi</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Mingine/emilala</i> |
| | | <i>Ku/emi</i> | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidogo Ku emititi/ emitono</i> |
| <i>Ji-Ma/eli-/ama-</i> | <i>Macho/amaaso</i> | <i>Ma</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Mengi/mangi</i> |
| | | <i>Ma</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Machache/matono</i> |
| | | <i>Ya/g</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>Yote/yoyote/gonna</i> |
| | | <i>Ma</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Mengine/malala</i> |
| | | <i>Ku/ma</i> | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidodgo Ku amaaso/matono</i> |
| <i>Ki-Vi/eki-ebi</i> | <i>Vitabu/ebitabo</i> | <i>Vi/bi</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Vingi/bingi</i> |
| | | <i>Vi/bi</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Vichache/bitono</i> |
| | | <i>Vi/by</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>Vyote/vyovote/byonna</i> |
| | | <i>Vi/bi</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Vingine/bilala</i> |
| | | <i>Ku/bi</i> | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidogo Ku bitabu/bitono</i> |
| <i>U-N/N-N</i> | <i>Nyumba</i> | <i>n/n</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Nyingi/enyingi</i> |
| | | <i>N</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Chache/entono</i> |
| | | <i>Zi/zo</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>zote/zozote/ zonna</i> |
| | | <i>Zi/n</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Zingine/endala</i> |
| | | <i>Ku/n</i> | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidodgo Ku nyumba/entono</i> |
| <i>U- Ø</i> | <i>Ukuta</i> | <i>N</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Nyingi</i> |
| | | <i>Ø</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Chache</i> |
| | | <i>Zi</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>Zote/zozote</i> |
| | | <i>Zi</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Zingine</i> |
| | | | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidodgo</i> |
| <i>U-Ma</i> | <i>Ugonjwa</i> | <i>Ma</i> | <i>-ingi/-ngi</i> | <i>Mengi</i> |
| | | <i>Ma/n</i> | <i>-chache/-tono</i> | <i>Machache/ntono</i> |
| | | <i>Ya/zo</i> | <i>-ote/-o-ote/-onna</i> | <i>Yote/zonna</i> |
| | | <i>Ma/nd</i> | <i>-ingine/-lala</i> | <i>Mengine/ndala</i> |
| | | <i>Ku/n</i> | <i>Kiasi/kidogo -tono</i> | <i>Kiasi/kidogo Ku bulwade/ntono</i> |

Asili: Ssentumbwe & Hyunah, (2019); Oichoe, (2005)

Kwa kurejelea mihimili ya Ubia na upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na unganifu wa data katika (4.12) utafiti huu ulibaini kuwa maumbo ya viambishi hutegemea maumbo ya ngeli

ambamo nomino huainishwa. Vilevile, iligunduliwa kuwa maumbo wakilishi yanayowakilisha maana ya kileksika ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri hutofautiana baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kila lugha ilidhihirisha maumbo ya kipekee ya vivumishi hivi. Hata hivyo, kwa kuzingatia kanuni ya ubia na upatanisho, viambishi awali vya upatanishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya Luganda na Kiswahili sanifu kuwakilisha idadi hutofautiana kimofolojia na kisintaksia. Aidha, vivumishi vya idadi isiyodhahiri katika Luganda hutumia viambishi awali vya nomino na viambishi vipatanishi vya nomino na vingine kutoambishwa kwa sababu ni mizizi ambayo ni huru yenye kubeba maana ya kileksika ya kivumishi cha idadi isiyokamili.

Tofauti inayojitokeza ni kuwa, viambishi vingi katika Luganda hutanguliwa na vibainishi na kufuatwa na viambishi awali vya nomino tofauti na Kiswahili kinachotumia viambishi awali vya nomino kutegemea ngeli inomojitokeza nomino tajwa. Aidha, Luganda ina mizizi michache inayotumia viambishi vipatanishi vya nomino kuliko Kiswahili. kwa mfano majina ya kiasi na udogo hutumika kuzingatia upatanishi wa nomino pamoja na kuwekea vipatanishi katika Mzizi [-onna] ambayo ni sawa na –ote na –o-ote katika Kiswahili. Luganda huongeza nomino kwenye silabi kuonyesha kiasi cha uchache [ku] ambayo lazima kuongezwa nomino kwa wingi ili kubeba maana inayohusika kama katika (g na h) katika Mifano Na (4.14) inayodhihirisha kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo kamili baina ya Luganda na Kiswahili sanifu: (4.14)

- a) *Ebitabo byange byonna birungi.* *Vitabu vyangu vyote vizuri*
- b) *Ndowooza eneebaayo abantu bangi* *Nafikiri kutakuwepo na watu wengi dukani*
- c) *Ente zange zona nzirugavu* *Ngombe wangu wote weusi*
- d) *Ekisa ekingi* *Huruma nyingi*
- e) *Bimu birungi, ebilala bibi* *vingine ni vizuri na vingine vibaya*
- f) *Balina ebintu ebingi ebirungi?* *Wana vitu vingi vizuri?*
- g) *Ku bintu bino* *kwa vitu hivi vyote*
- h) *Mpa ku mmere,* *Nipe kiasi cha chakula au nipe chakula kidogo*

Asili: Leah & Sseguya (2015), Snoxall (1955)

Kwa kurejelea mhimili wa ubia na upatanifu wa kisarufi, mifano (a-h) inabainisha matumizi ya vivumishi visivyo vya idadi katika Luganda na Kiswahili. Hata hivyo, mfano wa data inadhihirisha kutofautiana kwa maumbo wakilishi ya viidadi visivyo dhahiri baina ya Luganda na Kiswahili. Mfano (d, e na f) inaonyesha uongezaji wa vibainishi vya ngeli nyuma ya kiambishi ngeli kinachowekwa nyuma ya mzizi wa wakilishi wa vivumishi vya idadi isiyo

kamili katika Luganda tofauti na Kiswahili kinachoweka moja kwa moja kiambishi cha ngeli ya nomino tajwa nyuma ya mzizi wa maumbo wakilishi wa viidadi visivyo dhahihiri. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa, licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zenye kutumia viashio vya kimofosintaksia kwa upekee wake kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa vipashio katika tungo.

Kwa kuzingatia matumizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri, uchanganuzi wa nafasi ya utokeaji wa vivumishi hivi kulingana na Obara, (2014), Abudonia (2014) na Zerbian & Krifka (2008) iligunduliwa kuwa, kivumishi hiki hufuata nomino katika muktadha wa utungo au hata kuwekwa mwishoni mwa utungo kutegemea muktadha. Data za uchanganuzi na upekuzi wa maandishi katika mifano (4.15):

- | | |
|---|--|
| a) <i>Monica alidde emmere yonna</i> | <i>Monica amekula chakula chote</i> |
| b) <i>Leeta emmere entono</i> | <i>Leta chakula kidogo au kiasi</i> |
| c) <i>Abaana bonna bagenze kuzanya</i> | <i>Watoto wote wameenda kucheza</i> |
| d) <i>Omuyizi ono y'asinga bonna obugezi.</i> | <i>Mwanafunzi huyu ni mwerevu kwa wote</i> |

Asili: Data za Utafiti kutokana na Zerbian & Krifka (2008) na Obara, (2014)

Kwa mujibu wa tungo hizi, imedhihirika kuwa vivumishi vya idadi isiyodhahiri hutokea katika mazingira kati ya Luganda na Kiswahili ambapo, vivumishi hutokea mwishoni au katikati ya sentenzi baada ya nomino kutajwa kutegemea muktadha au dhana inayohusika. Katika kipengele cha vivumishi vya idadi isiyodhahiri, vivumishi vyenye mzizi –ingi na –*ingine* yenye kubeba maana ya kileksika ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri vilichunguzwa. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilibainika kuwa matumizi ya vivumishi hivi huwiana katika matumizi kimuktadha kuleta maana ya kimofosintaksia ya kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo baina ya Luganda na Kiswahili. Mzizi –*ingi* ni mzizi ambao hutumika kudhihirisha wingi wa nomino inayokumushwa bila kutaja idadi kamili ya wingi. Mzizi –*ingine* hubeba maana tofauti kwa kutegemea muktadha wa matumizi yake. Pia mzizi huu hubeba maana tatu za ‘sehemu ya’ ’baadhi ya’ na ‘zaidi ya’. Hali kadhalika, aina hii ya mofu huonyesha vitu vilivyojitenga na kundi la vitu vinavyofanana.

Aidha, mizizi, ‘-ote’ na ‘–o-ote’ na ‘-ingine’ mbali na kufanya kazi ya kuvumisha nomino kiidadi katika Luganda na Kiswahili, ilibainika kuwa vile vile hufanya kazi kama aina nyingine ya kivumishi kiitwacho kivumishi cha pekee. Hivi ni vivumishi ambavyo huwa na matumizi mengine ya kipekee ya kuwa vivumishi vya nomino. Kutokana na upekee wake, kila mzizi huwa na kanuni za upekee katika upatanishi wa kisarufi. Kwa mfano mzizi ‘-

ingine' hubeba maana tatu kuu za kueleza nomino kuwa, “*sehemu ya, baadhi ya na zaidi ya*” na kueleza hali ya nomino inayotajwa kujitenga na kundi kuu la vitu vinavyofanana, ‘-ote’ kuonyesha uhusika wa kutenda jambo katika wingi wake bila salio. –ote hutumika pamoja na viwakilishi nafsi kwa wingi. Tofauti inayojitokeza ni kuwa Luganda hutumia –ote na –o-ote kama –onna kimuktadha bila kuhusisha viwakilishi nafsi bali kutaja nomino moja kwa moja.

Matokeo haya yanashadidiwa na Zerbian & Krifka (2008). Anayesema kuwa:

In Swahili, adjective stems (which include numerals) show nominal prefixes in agreement with the head noun. Anaendelea kusema kuwa: Numeral agreement differs from nominal agreement in morphological form. In Swahili, e.g., the stem -ote (‘all’) does not agree with the head noun according to adjective formation in contrast to stems like -engi (‘many’) and the basic number words. Instead, -ote (‘all’) requires, like demonstratives, pronominal concord, which may point at a different status of these two items, ‘all’ being more determiner like, and ‘many’ being more adjectival. (Zerbian na Krifka, 2008: 4-5).

Katika Kiswahili, mashina ya vivumishi (ambayo yanajumuisha idadi) huonyesha viambishi awali vya nomino kukubaliana na nomino kuu. Upatanisho wa idadi hutofautiana na upatanisho wa nomino katika umbo la kimofolojia. Kwa mfano katika Kiswahili, shina -ote (‘yote’) haioani na nomino kama nomino kuu kulingana na uundaji wa vivumishi ambayo ni kinyume na mashina kama -engi (‘nyingi’) na maneno ya idadi msingi. Badala yake, -ote (‘yote’) inahitaji, kama vile maonyesho, mapatano ya kimatamshi, ambayo yanaweza kuashiria hali tofauti ya vitu hivi viwili, ‘yote’ yakiwa ya kuamua zaidi kama, na ‘nyingi’ kuwa kivumishi zaidi.

Matokeo ya utafi huu yanafanana na maelezo ya awali ya Kisakwah, (2014), Oichoe, (2005), Habwe & Karanja, (2004) na Mgullu, (1999) ambao walieleza juu ya vivumishi vya idadi vya Kiswahili sanifu kimaumbo na kimatumizi kimofosintaksia. Maelezo ya aina, maumbo na matumizi ya vivumishi vya idadi katika Luganda vilevile vimefafanuliwa na Ssentumbwe na Hyunah, (2019) na Zerbian & Krifka (2008). Licha ya kueleza juu ya viidadi, Uchanganuzi uligundua kuwa Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana katika mizizi na uambishaji wa vipatanishi vya vivumishi visivyo dhahiri. Ulinganishi huu na ulinganuo ulionyesha kuwa, licha ya lugha hizi kuwa lugha za Kibantu ni lugha mbili tofauti kiisimu.

4.1.3 Uwiano na tofauti za Viwakilishi vya Luganda na Kiswahili sanifu Kimofosintaksia

Utafiti huu ulibaini kufanana na kutofautiana kwa viwakilishi vya Luganda na Kiswahili kimaumbo na kimiundo kama inavyojitokeza katika data ya jedwali Na.(4.13) linaonyesha mifano ya uwiano na tofauti za viwakilishi katika makundi manne vya Luganda na Kiswahili sanifu.

Jedwali 4.13: Uwiano na Tofauti za Viwakilishi vya Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia

| Nafsi | Lugha | Huru | | Funge/vipatanishi | | Yambwa/Vionyeshi | | Milikifu | |
|-------|-------|-------|--------|-------------------|-------|------------------|-------|----------|--------|
| | | Umoja | Wingi | Umoja | Wingi | Umoja | Wingi | umoja | Wingi |
| 1 | Lug | Nze | Ffe | n- | tu- | -n- | -tu- | -ange | -affe |
| | Kis | Mimi | Sisi | Ni | Tu | Ni | Tu | -angu | -etu |
| 2 | Lug | Ggwe | Mmwe | o- | mu- | -ku- | -ba- | -o | -ammwe |
| | Kis | Wewe | Nyinyi | U | M | Ku | Wa | -ako | -enu |
| 3 | Lug | Ye | Bo | a- | ba- | -mu- | -ba- | -e | -abwe |
| | Kis | Yeye | Wao | A | Wa | M | Wa | -ake | -ao |

Asili: Data kutokana na Matasi na Furaha (2016), Kiyinikibi, (2021), Chesswas (1963:1)

Kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na Unganifu ya Chomsky (1981), utafiti huu ulibaini kuwiana kwa matumizi ya viwakilishi vya Luganda na Kiswahili kutokana na Uchanganuzi matini za kazi za Kiyinikibi, (2021), Matasi & Furaha (2016), Oichoe, (2005), Habwe & Karanja, (2004) kutumia kifaa cha kudondoa data chenye sifa za kimofosintaksia makatabani. Ilibainika kuwa, viwakilishi vya Luganda na Kiswahili sanifu vinapotumika kimofosintaksia, nomino zinazowakilishwa na viwakilishi hivyo huwa hazitajwi. Viwakilishi hivi kwa mujibu wa uchanganuzi wa Kiyinikibi, (2021), Matasi na Furaha (2016), Oichoe, (2005), Habwe na Karanja, (2004) viwakilishi husika vimewekwa katika kategoria kuu nne ambapo kuna viwakilishi nafsi huru, funge, yambwa na vimilikishi. Hata hivyo, licha ya kuwiana, maumbo ya viwakilishi hivi yalitofautiana.

Kwa kurejelea jedwali (4.13) Mifano katika jedwali inaonyesha kufanana na kutofautiana kwa viwakilishi katika Luganda na Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulibaini kuwa Viwakilishi vya Luganda na Kiswahili ni viwakilishi ambavyo vimegawanywa kuzingatia nafsi kuu nne kwa umoja na wingi vikifanya kazi ya kusisitiza nomino tendaji. Nafsi ya kwanza ambayo inahusu habari ya mtu binafsi na habari za watu wenyewe (kwa wingi). Nafsi hii ya kwanza huwakilishwa na viwakilishi *nze ya Luganda na mimi* ya Kiswahili kwa umoja na *ffe ya Luganda na sisi* ya Kiswahili kwa wingi. Viwakilishi hivi ni huru na haviwezi kuambishwa

ili kuleta maana. Kuna viwakilishi vya nafsi ya pili ambavyo huwakilishwa na viwakilishi **ggwe ya Luganda na wewe** ya Kiswahili kwa umoja na **mwe ya Luganda na ninyi** au **nyinyi** ya Kiswahili kwa wingi. Viwakilishi hivi hudhihirisha mtu wa pili unayezungumza naye kwa kusikiliza habari zake au zao kwa wingi. Mwisho, kuna kiwakilishi cha nafsi ya tatu ambacho huwakilishwa na viwakilishi nafsi **ye ya ya Luganda na yeye** kwa Kiswahili kwa umoja na **bba ya Luganda na wewe ya Kiswahili** kwa wingi. Nafsi hii huhusu mtu au watu mnaozungumzia wakiwa hawapo nanyi.

Uchanganuzi wa kutokana na maelezo ya wataalamu Matasi & Furaha (2016) na Ngonyani (2001), Kiyinikibi, (2021), Habwe & Karanja, (2004). Data Jedwali (4.13) vile vile yalidhihirisha kuwa viwakilishi vyote vya Luganda na Kiswahili hufanya kazi moja ya kimfosintaksia ya kuwakilisha nomino na kusisitiza nomino inayotajwa katika mazungumzo. Hata hivyo, ingawa viwakilishi nafsi vya Luganda vina sifa zinazofanana yaani ni viwili ambavyo vimewekwa katika makundi manne kutegemea nafsi tatu kwa umoja na wingi na viwakilishi huru kutoambishwa na huru kuambishwa, kufanya kazi ya kimfosintaksia ya kuonyesha uhusiano wa umilikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo, maumbo wakilishi ya aina na makundi ya viwakilishi na maumbo ya viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya maneno mengine kuwakilisha nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu ya viwakilishi tegemezi au funge hutofautiana kama katika Jedwali Na.(4.14).

Jedwali 4.14: Uwiano na tofauti ya viwakilishi nafsi huru, funge na yambwa vya Luganda na Kiswahili

| <i>Nafsi</i> | <i>Lugha</i> | <i>Viwakilishi vya nafsi huru kwa Umoja</i> | <i>Viwakilishi nafsi funge kwa Umoja</i> | <i>Viwakilishi nafsi huru kwa Wingi</i> | <i>Viwakilishi nafsi funge kwa Umoja</i> | <i>Viwakilishi nafsi yambwa Umoja na wingi</i> |
|--------------|--------------|---|--|---|--|--|
| 1 | Luganda | Nze | N | Ffe | Tu | -n-/-tu- |
| | Kiswahili | Mimi | Ni | Sisi | Tu | -ni-/-tu |
| 2 | Luganda | Ggwe | O | Mwe | Mu | -ku-/-ba- |
| | Kiswahili | Wewe | U | Ninyi/nyinyi | M | -ku-/-wa- |
| 3 | Luganda | ye | A | Bbo | Ba | -mu-/-ba- |
| | Kiswahili | Yeye | A | Wao | Wa | -m-/-wa- |

Asili: Data kutokana na Kyagaba (1996) na Matasi na Furaha (2016)

Jedwali (4.14) linadhihirisha kuwa vivumishi Viwakilishi nafsi huru, funge na yambwa vya Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika idadi ya mofu ya viwakilishi ambavyo ni vitatu

na umbo la viwakilish vya nafsi ya tatu umoja na nafsi ya kwanza wingi. Tofauti iliyojitokeza ni ile ambayo hujitokeza katika matumizi katika utungo na maumbo.

Uchanganuzi wa data za matumizi ya viwakilishi nafsi vya Luganda kutokana na Leah & Sseguya (2015) na Kiyinikibi, (2021) maktabani ulidhihirisha utokeaji wa uwiano na tofauti katika matumizi kama inavyojitokeza katika data ya Na.(4.16):

| Luganda | Kiswahili Sanifu |
|-----------------------------------|-------------------------------|
| a) <i>Ng'ende ku ssomero</i> | N inaenda shuleni |
| b) T ugenda ku ssomero. | T unaenda Shuleni |
| c) <i>Osabba kugenda kuyimba</i> | U naomba kwenda kuimba |
| d) M usaba kugenda kuyimba | M naomba kwenda kuimba |
| e) <i>Atunda Ebibala</i> | A nauza matunda |
| f) B atunda ebibala. | W anauza matunda. |

Asili: Data Kutokana na Leah & Sseguya (2015)

Kwa kurejelea mhimili wa upatanishi na kwa mujibu wa Kiyinikibi, (2021), viwakilishi vya nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu huchukua nafasi ya kwanza kimuundo katika utungo kuwakilisha nomino kwa umoja na wingi. Viwakilishi nafsi huru hutangulia katika tungo vikifuatwa na viwakilishi nafsi funge kutegemea muktadha wa sentensi. Aidha, viwakilishi vya nafsi vinaweza pia kutumika kurejelea nomino kwa kauli mbalimbali za utendaji. Kwa kurejelea viwakilishi nafsi vya vivumishi, inadhihirika kuwa kimatumizi, viwakilishi hivi huchukua upatanishi wa kisarufi wa viwakilishi vya nomino kwa umoja na wingi kuwakilisha au kuonyesha au kutaja nomino inayomiliki nomino, kitu au matendo. Viwakilishi hivi hutumika kisarufi kuzingatia maumbo ya ngeli za nomino kuwakilisha uhusiano wa nomino na kimilikikishi kama inavyodhihirikaa katika mfano Na (4.18) hapo juu.

Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Kyagaba (1996); Mgullu (1999); Matasi & Furaha (2016); Kisakwah (2014) na Oichoe (2005) ambao walianisha na kufafanua kuhusu maumbo na miundo ya viwakilishi mbalimbali katika matumizi ya Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, matokeo haya yanathibitishwa na Riedel, (2009) anayedai kuwa wakilisho yambwa zote katika Kibantu ni za madhumuni ya upatanisho wa kisarufi. Hali hii pia inathibitishwa na maelezo ya Egara, (2016) aliyefafanua kuwa uhusiano kati ya yambwa na mofimu wakilisho yambwa hulingana na uhusiano wa kisabiki na anafora. Matokeo haya yanakubaliana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya Umilikifu na Unganifu ambayo kwa mujibu wa utafiti huu ilibainika kuwa, licha ya Luganda na Kiswahili sanifu

kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti za Kibantu zenye vipashio, miundo na kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia zinazofanana na kutofautiana kiisimu.

4.1.4 Vikanusho

Matokeo ya data za uchanganuzi wa matini na maandishi ya kisarufi kuhusiana na ukanushaji katika Luganda na Kiswahili sanifu yalidhihirisha hali ya kufanana na kutofautiana kwa maumbo na miundo ya vikanusho kama kipashio cha kimofosintaksia. Uwiano na tofauti ulizingatia mihimili miwili ya usarufi bia na upatanishi ambao huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo kutokana na uhusiano wa kimofolojia na kimiundo wa sheria zinazounganisha vipashio vya kisarufi Chomsky (1981). Uchanganuzi wa data ulizingatia vipashio vya kimofosintaksia vya nomino, vivumishi, viwakilishi nafsi, na nyakati na hali vya Luganda na Kiswahili Sanifu kama inavyojadiliwa hapa chini.

4.1.4.1 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa nomino za Luganda na Kiswahili

Data ya uchanganuzi data za maktabani ulidhihirisha uwiano na tofauti za maumbo, nafasi na taratibu za ukanushaji wa nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data ya Jedwali Na. (4.15).

Jedwali 4.15: Uwiano na tofauti za vikanushi vya ngeli vya Luganda na Kiswahili kimofosintaksia

| VIKANUSHI NGELI VYA LUGANDA | | VIKANUSHI NGELI VYA KISWAHILI | |
|-----------------------------|----------------------------|-------------------------------|----------------------------|
| <i>Ngeli ya Luganda</i> | <i>Kiambishi kikanushi</i> | <i>Ngeli ya Kiswahili</i> | <i>Kiambishi kikanushi</i> |
| <i>a-ba</i> | <i>Ta-/teba-</i> | <i>a-wa</i> | <i>ha-/hawa-</i> |
| <i>gu-gi</i> | <i>tegu-/tegi-</i> | <i>U-I</i> | <i>hu-/hai-</i> |
| <i>li-ga</i> | <i>Teli-/tega</i> | <i>li-ya</i> | <i>hali-haya-</i> |
| <i>ki-bi-</i> | <i>Teki-/tebi-</i> | <i>ki-vi-</i> | <i>haki-/havi-</i> |
| <i>e-zi</i> | <i>te-/tezi</i> | <i>i-zi</i> | <i>hai-/hazi</i> |
| <i>Ka-bu</i> | <i>teka-/tebu</i> | <i>u-zi</i> | <i>hu-/hazi-</i> |
| <i>lu-zi</i> | <i>telu-tezi</i> | <i>u-ya</i> | <i>hu-haya-</i> |
| <i>Ku-ga</i> | <i>teku-/tega-</i> | <i>u-u</i> | <i>hu-/hu-</i> |
| <i>Tu</i> | <i>tetu-</i> | <i>i-i</i> | <i>hai-/hai</i> |
| - | - | <i>Ya-ya</i> | <i>haya/haya-</i> |
| - | - | <i>Ku-ku</i> | <i>haku-/haku-</i> |
| <i>Wa-</i> | <i>Tewaliwo-</i> | <i>Pa</i> | <i>hapa-</i> |
| <i>Ku</i> | <i>Teku</i> | <i>Ku</i> | <i>haku-</i> |
| <i>Mu</i> | <i>Temulimo</i> | <i>Mu</i> | <i>hamu-</i> |

Asili. Matokeo ya utafiti kutokana na Sakwa & wenzake (2013) na Mugerwa (2012)

kwa kurejelea Mihimil ya ubia na upatanifu ya Nadharia ya umilikifu na ufungamanifu, uchanganuzi wa data za Jedwali Na.(4.15), unadhihirisha kuwa, ingawa taratibu za ukanushaji katika Luganda na Kiswahili zilishabihiana, kulidhihirika tofauti za kimaumbo za vikanusho kama inavyojitokeza katika jedwali Na.(4.15). Kiutaratibu, lugha hizi huongeza viwakilishi vikanushi mwanzoni mwa viambishi ngeli vya upatanishi wa nomino kiidadi. Hata hivyo, Kiswahili hutumia kikanushi [ha-] ambacho huwekwa nyuma ya kiambishi cha upatanishi cha ngeli nomino mwanzoni kuwakilisha kauli kanushi na alomofu [hu-] ambayo hutumika katika kukanusha viambishi vipatanishi vya ngeli ambavyo huwakilishwa na kiambishi cha upatanishi ngeli kwa umoja kinachianza na [u-] hasa katika ngeli za kisintaksia za [u-i, u-zi na u-ya]. Kiambishi kipatanishi cha umoja [u] kinaambishwa kikanushi [hu] + [u] na kudondosha fonimu /u/ ya pili na hivyo kuwa na kikanushi [hu-] ambacho ni alomofu ya kikanushi [ha-] kinachotumika kuwakilisha kauli kanushi kama inavyoshadidiwa na Kihore, Msanjila & Massamba (2009); Mgullu (1999; Leah & Sseguya (2015) na Ngonyani (2001). Tofauti na uambishaji wa kikanushi [ha-] au [hu-] kwenye vipatanishi vya ngeli nomino katika Kiswahili, Luganda husisitiza kanuni ile ya kuongeza fonimu [t-] kwenye viambishi awali au vibanishi vya upatanishi wa kisarufi unaoanza na vokali na [te-] mwanzoni mwa kiambishi kipatanishi cha ngeli kinachotanguliwa na konsonanti kama viwakilishi awali vya upatanishi wa nomino (Hyman, 2018).

Tofauti nyingine iliyojitokeza ni kuwa Kiswahili mbali na kuambisha viambishi vikanushi [ha- na hu-] mwanzoni mwa viambishi vipatanishi vya ngeli kwa umoja na wingi, viambishi viwakilishi vya nyakati na hali vilevile huwakilishwa na viwakilishi vikanushi vyake ambavyo hutokea katikati na mwishoni mwa kitenzi kinachotajwa katika kauli husika (Mulei, 2014; Lupongo, 2021; Kihore, Msanjila na Massamba, 2001). Tofauti na utokeaji wa ukanushaji katika Kiswahili Hyman, (2018) anaelezea kuwa Luganda huwa na uwakilishi kapa wa nyakati ambao hujitokeza tu katika vikanushi vyake kama unavyojitokeza katika data Na.(4.17).

| Luganda sanifu | Kiswahili sanifu |
|--------------------------|------------------|
| a) <i>Omuntu asomye</i> | Mtu amesome |
| <i>Abantu basomye</i> | Watu wamesoma |
| b) <i>Omuntu tasomye</i> | Mtu hajasoma |
| <i>Abantu tebasomye</i> | Watu hawamesoma |

Asili: Data Kutokana na uchanganuzi wa Kiyinikibi (2021).

Kiubia na Kiupatanifu, data (a na b) inadhihirisha uwiano na tofauti za ukanushaji katika Luganda na Kiswahili sanifu. Sentensi ya kwanza ni yakinishi iliyo na sifa za kimofosintaksia. Kuna kitenzi *asomye* ambacho hutokana na kitendo halisi *soma*. Kuna kiambishi kipatanishi cha ngeli {a-} ya kisintaksia umoja na {ba-} kwa wingi inayoonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino ‘*Omuntu na Abantui*’ na kitenzi (asomye na Basomye) kwa umoja na wingi. Kuna vilevile kiwakilishi cha wakati {-me-} ambacho kimewakilishwa na {-ye} ambayo imewekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi (*som--*). Katika ukanushaji, sauti {t-} ya ukanushi wa viambishi vinavyoanza na irabu imeambishwa kuwakilisha ukanushaji ila kiambishi cha hali {-e} hakijakanushwa. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambapo nafasi ya kiwakilishi cha wakati (hali ya -me-) kimewakilishwa na kikanushi {-ja}. Hali hii inadhihirisha kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye mifumo na miundo ya kipekee ya sifa za kimofosintaksia inayopambanua na kutofautisha lugha moja na nyingine miongoni mwa lugha za Kibantu.

Mwisho, Luganda huwa na umuhimu wa ukanushaji wa nomino ambazo huundwa kwa vitenzi jina. Ngeli hizi ni ngeli za jozi ya sita ambalo huwakilishwa na [ku-] / (o) ku na kukanushwa kwa kutumia kikanushi [-ta-] ambacho hufuatwa kiambishi kipatanishi cha ngeli kama inavyojitokeza katika daya Na.(4.18).

Luganda sanifu

Kiswahili sanifu

- | | |
|--|--|
| a) <i>Abasajja a-ba-ta-a-leeta</i> migugu. | <i>Wanaume ambao ha-wa-ku-leta</i> mizigo. |
| b) <i>Emigugu abasajja gye-ba-ta-a-leeta.</i> | <i>Mizigo ambayo ha-i-ku-letwa</i> na wanaume. |
| c) <i>Mwana y'a-ta-soma</i> kitabo. | <i>Ni mtoto ambaye ha-kusoma</i> kitabu |
| d) <i>Maama agambye nti asobola obu-ta-ja.</i> | <i>Mama amesema kuwa anaweza ku-to-kuja</i> |
| e) <i>Obu-ta-laba ngo</i> | <i>ku-to-ona chui.</i> |
| f) <i>Bye-ba-ta-laba</i> | <i>Vitu ambavyo ha-wa-kuona</i> |
| g) <i>Obu-ta-nseera</i> | <i>Ku-to-niuzia</i> kwa bei ghali |
| h) <i>Abantu obu-ta-manya bunnuma</i> | <i>watu ku-to-jua</i> kunaniudhi |

Asili: Data kutokana na Hyman na Katamba (1999) na Pak, (2007) na Kiyinikibi, (2021)

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanishi, data (a na b) inaonyesha matumizi ya kikanushi {-ta-} ambacho hutokea katika Luganda tofauti na Kiswahili ambayo inadhihirisha tofauti ya kutotumia mfumo huu mmoja na wa Luganda. Data ya (c -e) inaonyesha pia tofauti ambapo ingawa vikanushi vinatokea katika nafasi moja, maumbo ya Luganda {-ta-} ni tofauti

na Kiswahili sanifu {-to-}. Ukanushaji wa aina hii unalinganishwa na ukanushaji wa vitenzi maalumu katika Kiswahili ambapo kikanushi [-to-] huwekwa kati ya kitenzi na kiambishi [ku-] ambapo pia hujitokeza nje ya muktadha wa ngeli. Hii ni kwa sababu hivi ni vitenzi vinavyoonyeshwa kutobanwa kwa tendo katika hali maalumu (vitenzi maalumu) na wala sio vitenzi-jina kama inavyoelezwa na Lupogo, (2021). Aidha, kanuni ya ukanushaji wa nomino hizi hujitokeza kwa kuambisha kiambishi {obu-} nyuma ya kiwakilishi kanushi vya nafsi ya tatu umoja katika Luganda ikifuatwa na kikanushi {-ta-} na mzizi wa kitenzi maalumu.

Matokeo haya yanashadidiwa na wataalamu Matasi na Furaha (2016) na Kyagaba (1996; 2015) katika ufafanuzi wao wa ukanushaji katika Kiswahili na Luganda. Licha ya kuwepo kwa ufafanuzi wao, utafiti huu ulitofautiana nao hasa katika kufafanua kufanana na kutofautiana kwa ukanushaji katika Luganda na Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu, ilidhihirisha kuwepo kwa uwiano na tofauti kubwa inayojitokeza baina ya ukanushaji wa nomino za Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, Licha ya kuwa lugha hizi ni za nasaba moja zilizo na sifa za Kibantu zinazofanana kimofolojia na kisintaksia, Maumbo na miundo ya ukanushaji ilitofautiana kimofosintaksia.

Matokeo haya yanashadidiwa na Lupogo (2021) ambaye licha ya kukosa kueleza mazingira ambamo vikanushi hutumika, aliainisha maumbo ya ukanushaji tisa katika Kiswahili. Anaeleza kuwa: “ imebainika kwamba Kiswahili sanifu kina maumbo tisa (9) ya ukanushi: si, ha, ku, kuto (to), ta, si, ku, hapana na ja.” Aidha, Leah na Sseguya, (2015), nao wameainisha maumbo ya vikanushi kutegemea nje na maneno maneno huru katika Luganda tofauti na maumbo ya Kiswahili yaliyoanishwa na Lupogo (keshatajwa). Uchanganuzi wa ulinganishi wa maumbo ya ukanushaji baina ya Luganda ulibainisha kuwepo kwa uwiano na tofauti za ukanushaji katika Luganda na Kiswahili kimofosintaksia. Uwiano na tofauti hii ilidhihirisha kuwa Lugha za nasaba moja huweza kudhihirisha upekee wa kiisimu wa matumizi ya vipashio vyake ambao kwa hali moja au nyingine huweza kusababisha athari za mwingiliano katika matumizi kiisimu.

4.1.4.2 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa Vivumishi vya Luganda na Kiswahili

Matokeo ya uchanganuzi wa data kutokana na upekuzi wa maandishi na tafiti za Lupogo, (2021), Matasi na Furaha, (2016), Ngonyani, (2001) na Leah & Sseguya (2015) kuhusiana na ukanushaji wa vivumishi ulibaini kufanana na kutofautiana kwa maumbo kanushi baina ya Luganda na Kiswahili kama inavyojitokeza katika data Na. (4.19).

| Luganda sanifu | Kiswahili Sanifu |
|-----------------------------|---------------------------|
| a) <i>Omusajja mulungi.</i> | Mwanamume mzuri |
| <i>Omusaja si mulungi</i> | <i>Mwanamume si</i> mzuri |
| b) <i>Caayi mulungi.</i> | Chai nzuri. |
| <i>Caayi si mulungi.</i> | Chai si nzuri. |
| c) <i>Abaana basuffu</i> | Watoto bora. |
| <i>Abaan si basufu.</i> | Watoto si bora. |
| d) <i>Omucungwa guwooma</i> | Chungwa tamu. |
| <i>Omucugwa teguwooma.</i> | Chungwa si tamu. |
| e) <i>Emmere ewooma.</i> | Chakula kitamu. |
| <i>Emerre tewooma.</i> | Chakula si kitamu. |

Asili: Kutokana na data za Leah na Sseguya, (2015)

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya Nadharia ya Umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981), utafiti huu ilibaini uwiano wa Luganda na Kiswahili hutumia kiambishi [si] ambacho huwekwa nyuma ya kivumishi baada ya nomino kuwakilisha kauli ya kukataa au kukanusha sifa au kivumishi kinachokumusha nomino kwa umoja na wingi kama katika mfano wa data (a, b na c). Ilibainika pia kuwa, ikiwa kivumishi kimewakilishwa na kitenzi, kanuni ya kuongeza vikanushi mwanzoni mwa kiwakilishi cha nomino kilichoambishwa kwenye kitenzi huzingatiwa kama inavyojitokeza katika (d na e) iliyodhihirisha kufanana kwa nafasi ya utokeaji wa viambishi vikanushi vya Luganda na Kiswahili vinavyowekwa nyuma ya viambishi vya nomino katika ngeli vinavyoambishwa kwenye vitenzi na tofauti ya kimaumbo ya vikanusho vinavyotumika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na kivumishi hasa vivumishi vilivyowakilishwa na vitenzi. Licha ya kuwepo kwa uwiano, ilibainika kuwa maumbo yanayoambishwa kwenye vitenzi hivi hutofautiana kutoka lugha moja na nyingine kama inavyofafanuliwa na Leah na Sseguya, (2015) katika ufafanuzi wake wa maumbo ya ukanushaji katika Luganda na Massamba na wenzake, (2012) katika maelezo ya ukanushaji katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Data za uchanganuzi wa matumizi ya vivumishi vya nafsi vinavyotokana na ngeli husika kwa mujibu wa Leah & Sseguya (2015), Ngonyani (2001) na Hyman, (2018) maktabani, ulibaini tofauti za ukanushaji wa vivumishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu wa maumbo wakilishi ya ukanushaji wa vivumishi vya nafsi Kama inavyojitokeza katika data Na.(4.20).

| <i>Hali yakinishi</i> | <i>Kanushi</i> | <i>Yakinishi</i> | <i>Kanushi</i> |
|-----------------------|---------------------|---------------------|-----------------------|
| <i>Ndi muwanvu</i> | <i>Siri muwanvu</i> | <i>Tuli Bawanvu</i> | <i>Tetuli bawanvu</i> |
| Mimi ni mrefu | mimi si mrefu | Sisi ni warefu | Sisi si warefu |
| <i>Oli muwanvu</i> | <i>Toli muwanvu</i> | <i>Muli Bawanvu</i> | <i>Temuli bawanvu</i> |
| Wewe ni mrefu | Wewe si mrefu | Nyinyi ni warefu | Nyinyi si warefu |
| <i>Ali muwanvu</i> | <i>Tali muwanvu</i> | <i>Bali Bawanvu</i> | <i>Tebali bawanvu</i> |
| Yeye ni mrefu | yeye si mrefu | Wao ni warefu | Wao si warefu |

Asili: Data kutokana na Leah na Sseguya, (2015) na Hyman, (2018)

Kwa mujibu wa maelezo ya Leah na Sseguya, (2015) Luganda huongeza [siri] nyuma ya kivumishi katika nafsi ya kwanza, [toli] katika nafsi ya pili na [tali] katika nafsi ya tatu kwa umoja. Katika wingi, Luganda hutumia kikanushi {te-} kinachowekwa nyuma ya konsonanti ya wingi ya nafsi ya kwanza nafsi na kutumia {tetuli}, nafsi ya pili, {temuli} na nafsi ya tatu, {tebali}. Vinginevyo, Luganda huzingatia kanuni ya kuongeza {t-} kwenye viwakilishi nafsi vinavyoanza na vokali na {te-} kwa vile vinavyoanza na konsonanti. Maumbo haya ni tofauti na Kiswahili ambacho hutumia kikanushi {si} kinachowekwa nyuma ya kivumishi baada ya kiwakilishi nafsi kama inavyoelezwa na Ngonyani (2001) na Hyman, (2018) kuwa kuhusu kikanushi {si-} katika Luganda na Kiswahili ambapo kikanushi {si-} huwekwa nyuma ya kivumishi baada ya nomino kukanusha kikanushi. Data hii inadhihirisha uwiano na tofauti za ukanushaji wa vivumishi vya nafsi vinavyotokana na ngeli husika. Kwa kurejelea Nadharia ya Umilikifu na Unganifu, ilibainika wazi kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili ni lugha za Kibantu zenye vipashio vya kimofosintaksia vinavyodhihirisha ukuruba katika matumizi, kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia hufanana na kutofautiana kutokana na upekee wa kiisimu wa kila lugha.

Aidha, ilibainika kuwa kukaribiana kufanana kwa maumbo, nafasi ya utokeaji na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ukanushaji wa Luganda havidhihirishi kufanana na Kiswahili sanifu. Hii inatokana na kuwa hizi ni lugha mbili tofauti zenye sifa za kiisimu zinazotambulisha na kuzitofautisha na lugha zingine za Kibantu. uwiano na tofauti hizi zimethibitishwa na Lupogo, (2021) na Massamba na wenzake, (2012) wanaoeleza kuwa, lugha nyingi za Kibantu zina namna inayokaribia kufanana katika mpangilio wa vipashio vyake vikiwemo vya ukanushi. Matokeo ya ufafanuzi wa Lupogo na Leah na Sseguya, (washatajwa), utafiti huu uliweza kubaini kuwa licha ya baadhi ya vikanushi kama {si-} kuwiana baina ya Luganda na Kiswahili sanifu, matumizi ya kikanushi hiki pamoja na vikanushi vinginevyo vya {ha-, si-, to, sipo, na maumbo mengineyo 9 ambayo hutokea katika

hali mbalimbali ilidhihirika uwiano wa maumbo na taratibu ya Ukanushaji, lugha hizi mbili ambazo ni za nasaba moja hutofautiana katika misingi ya kimfosintaksia.

4.1.4.3 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa Viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili

Matokeo ya uchnanganuzi wa maandishi maktabani kuhusiana na ukanushaji wa viwakilishi nafsi nyanjani ulibaini kufanana na kutofautiana kimaumbo na kimuundo katika ukanushaji licha ya kuwa lugha za nasaba moja kama inavyojitokeza katika Jedwali Na.(4.16) linaonyesha uwiano na tofauti za mofu za ukanushaji wa vipatanishi vya nafsi kwa umoja na wingi kati ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Jedwali 4.16: Uwiano na tofauti za Viwakilishi vikanushi vipatanishi vya nafsi vya Luganda na Kiswahili kimfosintaksia

| <i>Nafsi (Luganda)</i> | <i>Kiwakilishi</i> | <i>Kikanushi</i> | <i>Kimatumizi</i> | <i>Kiwakilishi</i> | <i>Kikanushi</i> | <i>Kimatumizi</i> |
|--------------------------|--------------------|------------------|-------------------|--------------------|------------------|-------------------|
| 1 | N- | Si- | S- | Tu | Tetu | Tetw- |
| 2 | O- | To- | Tew- | Mu | Temu | Temw- |
| 3 | A | Te | Tey- | Ba | Teba | Teb- |
| <i>Nafsi (Kiswahili)</i> | <i>Kiwakilishi</i> | <i>Kikanushi</i> | <i>Kimatumizi</i> | <i>Kiwakilishi</i> | <i>Kikanushi</i> | <i>Kimatumizi</i> |
| 1 | Ni | Si | | Tu- | Hatu | |
| 2 | U | Hu | | M- | Ham | |
| 3 | A | Ha | | Wa- | Hawa | |

Asili: Data za maktabani kutokana na Hyman, (2018); Matasi na Furaha, (2016)

Kiubia na kiupatanishi, ukanushaji wa nafsi katika Luganda na Kiswahili ni ule unaozingatia uwiano wa mofu za upatanishi wa nafsi unaodhihirisha sifa za kimfosintaksia, uambishaji wa vikanushi vya kila nafsi mwanzoni mwa viwakilishi nafsi kwa umoja na wingi na uambishaji wa vipatanishi vya nafsi ambavyo huwekwa kwenye shina au mizizi ya vitenzi vinavyobeba maana au dhamira ya kisarufi kulingana na wakati na hali. Jedwali (4.16) linaonyesha maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya viwakilishi nafsi na mofu kanushi kwa kila nafsi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kila nafsi imewakilishwa na mofu kanushi kwa umoja na wingi ikionyesha uhusiano wa umilikifu na unganifu wa kiwakilishi cha nafsi na kitenzi. Mofu kanushi hubadilika kulingana na viambishi awali vya shina au mzizi wa kitenzi. Kanuni iliyojitokeza katika Luganda ni kuwa, mzizi wa kitenzi unaoanza na konsonanti kwa umoja {N-} hubadilika na kuwa {Si} na katika matumizi kiambishi {s-} hutumika kwa mfano. {Ng'eenda} hubadilika na kuwa; {Sigeenda}. Aidha, {t-} huongezwa kwenye mizizi ya vitenzi vinavyoanza na vokali. Kwa mfano nafsi ya pili O- huongezwa {t-} nyuma yake na kuwa {to-} huku nafsi ya tatu A ikiongezwa {te-}. Kwa muhtasari, kanuni

ya ukanushaji wa nafsi katika Luganda ni kuwa {te-} huongezwa ikiwa kiambishi awali cha nafsi inayohusika kinaanza na konsonanti na ikiwa kiambishi kiwakilishi cha nafsi kinaanza na vokali, {t-} huongezwa (Hyman, 2018 na Katamba, 2003). Tofauti na kanuni ya ukanushaji katika Luganda, ukanushaji katika Kiswahili hutokana na dhamira, hali, njeo na uwakilishi wa nafsi kwa umoja na wingi. Tofauti iliyojitokeza ni kuwa maumbo wakilishi ya viwakilishi nafsi vipatanishi na maumbo kanushi ya Luganda na Kiswahili sanifu yalitofautiana.

Matokeo haya yanaendana na maelezo ya Taher, (2013), Katamba, (2003) na Lupogo, (2021) Kiswahili kinatofautiana na Luganda kikanuni ambapo Kiswahili huongeza viambishi au mofu ya ukanushaji {ha-} na alomofu yake {hu-} nyuma ya viwakilishi vipatanishi vya nafsi kimofosintaksia, huku Luganda ikizingatia aina ya viambishi viwakilishi vya nafsi kuwa ama irabu au konsonanti. Ugunduzi huu unafanana maelezo ya Massamba na wenzake (2012) wanaofafanua kuwa, ukanushaji wa utungo wenye vipatanishi vya kisarufi vya nafsi hutokea au kubadilika kulingana na viambishi awali vya shina au mzizi wa kitenzi.

Kwa kuzingatia nafasi ya matumizi ya vikanushi, utafiti huu ulibaini pia kuwa kikanushi cha Luganda {te-} huweza kubadilika na kutumia umbo la {ta-} kutegemea dhamira ya kishazi kimofosintaksia. Hyman, (2018) anaeleza kuwa Kikanushi {te-} huwekwa mwanzoni mwa kitenzi nyuma ya kiwakilishi kipatanishi cha nomino au idadi, nafsi na njeo kikifuatwa na kitenzi (Kiima) ikiwa dhamira ya utungo inajitokeza katika kirai kitenzi. Aidha, kikanushi {-ta-} huwekwa kati ya kiwakilishi kipatanishi kirejeshi cha nomino kutegemea idadi (Umoja /Wingi) kikifuatwa na kiwakilishi cha njeo na kitenzi ikiwa kishazi kikuu kinaelezea zaidi juu ya nomino. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambacho huweka viambishi vikanushi nyuma ya vitenzi na viwakilishi vipatanishi vya ngeli nomino kwa umoja au wingi kimofosintaksia kutegemea nafsi, nyakati au hali husika kama ilivyodhihirishwa katika ufafanuzi wa Hyman, (2018); Lupogo, (2021) na Ngonyani, (2001). Data katika mifano (4.19, Uk. 117) inawasilisha mifano ya Uwiano na tofauti ya ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na Hyman, (2018); Matasi & Furaha, (2016) na Leah & Sseguya, (2015) kuhusu ukanushaji wa Luganda na Kiswahili sanifu. (4.21)

| Luganda | Kiswahili |
|--|---|
| a) <i>Abayizi ba-a-leeta e-bitabu byabwe.</i> | Wanafunzi wa-li -leta vitabu vyao. |
| b) <i>Abayizi te-ba-a-leeta e-bitabu byabwe.</i> | Wanafunzi ha-wa-ku -leta vitabu vyao. |
| c) <i>Emigugu abasitusi gye-ba-a-leeta.</i> | Mizigo ambayo i-li -letwa na hamali. |
| d) <i>Emigugu abasitusi gye-ba-ta-a-leeta</i> | Mizigo ambayo ha-i-ku -letwa na hamali. |

Asili: Data kutokana na Hyman, 2018; Leah na Sseguya, 2015 na Rose, 2009

Data (a na b) zinazungumzia juu ya dhamira ya kuleta vitabu huku, data (c na d) zikizungumzia juu ya mizigo ambayo ililetwa. Hali hii katika Luganda hubadilisha nafasi ya matumizi ya kikanushi [te-] na kubadilika kifonolojia na kuwa [-ta-] kutegemea dhamira. Tofauti na Kiswahili kilichozingatia viwakilishi vipatanishi na mahali pa ktumia kikanushi nyuma ya kipatanishi bila kubadilisha nafasi yake. Ukanushaji huu ni ule wa urejeshi wa viwakilishi katika tungo ukiwakilishwa na viwakilishi vipatanishi vya nafsi, njeo na kiishio cha Kibantu cha ukanushaji kama katika mfano (4.22).

| | | | |
|------------------|-----------------------|---------------|------------------------------|
| <i>A-</i> | <i>li-</i> | <i>tak-</i> | <i>a</i> |
| <i>Nafsi3-</i> | <i>wkt uliopita-</i> | <i>mzizi-</i> | |
| <i>ha-</i> | <i>ku-</i> | <i>let-</i> | <i>a</i> |
| <i>-KNafsi3-</i> | <i>-wkt uliopita-</i> | <i>mzizi-</i> | <i>kiambishi cha kibantu</i> |

Tanbihi: KNafsi (Kiambishi nafsi) wkt (wakati)

Asili: Data za Utafiti kutokana na Hyman, (2018)

Mifano ya sentensi hii ambayo imo katika nafsi ya kwanza wakati uliopita, inatumia kikanushi {ha-} ambacho kimewekwa nyuma ya kiwakilishi nafsi (KNafsi3), kiambishi cha wakati uliopita {-li-} kimehifadhi hadhi ya nafsi yake na kikanushi chake {-ku-} kutumika, mzizi wa kitenzi kubakisha hadhi yake bila kubadili kiambishi tamati cha Kibantu {-a}. Ikiwa ni wakati uliopo, kiambishi tamati cha Kibantu kinachojitokeza katika kitenzi hubadilika na kuwa {-i} bila kubadilisha nafasi yake. Kishazi hiki kimebeba vikanushi viwili, kikanushi cha nafsi {h-a-} na kikanushi cha wakati uliopita {-ku-}. Hii ina maana kuwa Kiswahili huzingatia uwili katika ukanushaji tofauti na Luganda (Lupogo, 2021; Massamba na wenzake, 2012).

Matokeo haya yanakubaliana na ufafanuzi wa Hannah (1975), Lupogo, 2021 na Massamba na wenzake, (2012) wanaeleza kuwa ukanushaji katika lugha ya Kiswahili sanifu hutokea

katika sehemu kuu tatu. Mwanzoni mwa shina la kitenzi, ndani au kati na mwishoni mwa shina au mzizi wa kitenzi ikiwakilishwa na mofu vokali ya ukanusho [-i]. Kwa kuongezea, Lupogo, (2021), inathibitisha tofauti hizi kwa kueleza kuwa Kiswahili huzingatia uwili katika ukanushaji tofauti. Kutokana na maelezo yao, utafiti huu uliweza kufafanua uwiano na tofauti za ukanushaji wa viwakilishi nafsi baina ya Luganda ba Kiswahili sanifu. Matokeo haya yalithibitisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili kimofosintaksia huwa na kanuni za ukanushaji wa viwakilishi nafsi kutegemea maumbo ya nafsi tatu kwa umoja na wingi, vikanushi vya kila nafsi na nafasi ya uambishaji wa vikanusho kutokea katika nafasi moja kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu wa viwakilishi nafsi na vitenzi au na maneno mengine katika tungo, lugha hizi zinadhihirisha kufanana na kutofautiana kimaumbo na kimiundo licha ya kuwa lugha za nasaba moja.

4.1.4.4 Uwiano na Tofauti ya Ukanushaji wa Njeo na Hali katika Luganda na Kiswahili

Data ya mapitio ya maandishi na vitabu vya kisarufi kwa kurejelea kifaa cha kudondoa data chenye sifa za kimofosintaksia ilibaini kuwa, ukanushaji wa njeo na hali katika Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana kimaumbo, utaratibu na athari za kimofonolojia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa neno kuu na maneno mengine kudhihirisha sifa za kimofosintaksia kama inavyojitokeza katika data ya maumbo ya ukanushaji wa Luganda na Kiswahili katika majedwali Na.(4.17):

Jedwali 4.17: Vikanushi vya viwakilishi nyakati katika Kiswahili kimofosintaksia

| <i>Kiwakilishi njeo</i> | <i>Kikanushi chake</i> | <i>Kikanushi cha kitenzi</i> | <i>Mfano</i> |
|--|---|------------------------------|---|
| <i>-li-</i> | <i>-ku-</i> | <i>Hau-hu</i> | <i>Hu-ku-ni-fundisha</i> |
| <i>-na-</i> | \emptyset – [-a] tamati kuwa [-i] | <i>Ha</i> | <i>Ha-[-]-ku-<i>pend-i</i></i> |
| <i>Hali ya kuendelea -kuwa na -na-</i> | <i>-kuwa na -na- ya [wakati uliopita na ujao]</i> | <i>Ha-</i> | <i>H-a-kuwa anaimba h-a-ta-kuwa anaimba</i> |
| <i>-me-</i> | <i>-ja-</i> | <i>Ha</i> | <i>Ha-ja-m-pig-a</i> |
| <i>-sha-</i> | <i>-ja-</i> | <i>Ha</i> | <i>A-sha-ondok-a Ha-ja-ondok-a</i> |
| <i>-ta-</i> | <i>-ta-</i> | <i>Ha</i> | <i>U-ta-pit-a Hu-ta-pit-a</i> |
| <i>hu-</i> | <i>Kama -na-: [-a] tamati kuwa [-i] pamoja na kikanushi [ha-]</i> | <i>Ha</i> | <i>[Huwa] -ha-chez-i</i> |

Asili: Data za maktabani kutokana na Matasi & Furaha, 2016 na Kyagaba, (1996) Lupogo, (2021)

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanifu wa nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981), data katika Jedwali (4.17) linadokeza viambishi vya wakati na hali pamoja na vikanushi vyake katika Kiswahili ambavyo ni tofauti na Luganda. Aidha, kulingana na Mulei, (2014) na Lupogo, (2021), wingi wa vikanushi vya Kiswahili ni kutokana na uwili wa ukanushaji ambapo kila njeo imewakilishwa na kikanushi na kiwakilishi cha nomino katika kitenzi kikitumia kikanushi [h] kinachowekwa mwanzoni kabla ya kipatanishi. Maumbo haya ni {-i} ya kitenzi jina, na udondoshaji wa njeo ya {na-}, {-ja} ya hali timilifu {-me-}, {ku-} ya wakati uliopita {-li-}, na {-ta-} wakati ujao. Viwakilishi hivi vya njeo na hali hukanushwa kwa vikanushi vyake pamoja na kuongeza kikanushi [ha-] au [hu-] mwanzoni mwa kitenzi husika. Hali ambayo inaonyesha ukanushi uwili ambapo vikanushi viwili hutokea ndani ya kitenzi kimoja. Yaani kikanushi cha njeo na kikanushi [ha/hu] kinachowekwa mwanzoni mwa kipatanishi cha nomino kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu. Maumbo haya ya vikanushi, hayapatikani katika Luganda.

Tofauti na Kiswahili, Luganda huwakilishwa na maumbo ya viambishi vya njeo na vikanushi vinavyotofautiana na vya Kiswahili sanifu. Hyman (2018) na Leah na Sseguya, (2015) wanaeleza kuwa Luganda ina jumla ya njeo tatu. Hata hivyo wanadai kuwa Luganda ina jumla ya njeo sita pamoja na hali. Njeo hizi ni wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Mbali na njeo, Luganda ina jumla ya hali mbalimbali ambazo hujitokeza katika nyakati hizi. Hali hizi ni hali ya kuendelea, hali ya masharti, hali ya kuamrisha, hali tegemezi ambayo ni hali ya ‘-nge-’ katika Kiswahili na hali ya kuarifu. Jedwali (4.18) linaonyesha maumbo ya njeo na hali, maumbo yakinishi na kanushi na mtawanyiko wake katika tungo za Luganda kutokana na Hyman (2018), Leah na Sseguya, (2015).

Jedwali 4.18: Njeo na hali kimfosintaksia pamoja na maumbo kanushi katika Luganda na Kiswahili Sanifu

| Njeo na hali | Kiwakilishi yakinishi | Kiwakilishi kanushi na mifano | Mfano | Kikanushi |
|--|---|---|---|--|
| | WAKATI ULIOPO | | | |
| Wakati uliopo, sasa hivi | Kiambishi kipatanishi – Mzizi wa kitenzi cha kukanushwa- a (Kkp-Mz-a) | te-/t- -Kkp-Mz-a tasamba ha- -chez-i | Omuyizi a-samb-a omupiira Abayizi ba-samb-a emipiira | Omuyizi t-a-samb-a omupiira Abayizi te-ba-samb-a emimupiira |
| Wakati uliopo hali ya kawaida | | sisamba si--chez-i | nsamba omupiira | Sisaamba |
| Wakati uliopo hali ya kuendelea | Kkp-Mz-a | te-/t- -Kkp-Mz-a sili- mukuzanya\tetuli mukuzanya niko si-chez-i tuko tunacheza | Ndi –mu- ku-samb-a Tuli- mu- ku-samb-a omupira | sili mu kusamba omupira Tetuli mu kusamba omupira |
| | WAKATI ULIOPITA | | | |
| WAKATI ULIOPITA (kawaida) | Kkp-Mz-YE | te-Kkp-Mz-YE t-a-samb-ye ha- ku-chez-a | Omuyizi a-samb-ye omupiira ABayizi ba—a-samb-ye emipiira | Omuyizi ta-samb-ye omupiira Abayizi te-ba-samb-ye emipiira |
| Wakati uliopita muda mfupi uliopita | Kkp-aa-Mz-YE | te-Kkp-aa-Mz-YE te-ya-saamb-ye ha-ku-chez-a | Omuyizi y-a-a-samb-ye Abayizi ba-a-samb-ye | Omuyizi te-ya-a-samb-ye Abayizi te-ba-a-samb-ye |
| Wakati uliopita (zamani) | Kkp-aa-Mz-a | te-Kkp-aa-Mz-a te-y-aa-samb-a -ha-ku-chez-a | Omuyizi y-aa-samb-a omupiira | Omuyizi te-y-a-a-samb-a omupiira |
| | | te-Kkp-aa-Mz-a s-aa-samb-a te-tw-a-a-samba si-ku-chez-a ha-tu-ku-chez-a | Nnasamba Twasamba Yasaamba Mwasamba Wasaamba Baasamba | te-Kkp-aa-Mz-a sa-a-samb-a te-tw-a-a-samba te-y-a-a-samb-a te-mw-a-asamb-a te-w-a-a-samb-a te-ba-a-samb-a |
| | WAKATI TIMILIFU | | | |
| Wakati uliopita hali timilifu- (muda mfupi uliopita) | Kkp-aa-badde Kkp-Mz-YE | Kkp-aa-badde te-Kkp-Mz-YE te-ba-a-samb-ye ha-wa-ku-chez-a | Omuyizi y-a-a-sambye umupiira Abayizi ba-a-samb-ye omupiira | Omuyizi tey-a-a-sambye umupiira abayizi te-ba-a-samb-ye umupiira (mkazo wa irabu) |
| Wakati uliopita zamani, hali timilifu) | Kkp-aa-li Kkp-mz-YE | Kkp-aa-li te-Kkp-Mz-YE y-aa-li t-a-samb-ye ha-kuwa a-me-chez-a | Omuyizi yaali asambye omupiira Bayizi ba-ali -ba-samb-ye Omupiira | Omuyizi yaali t-a-samb-ye omupiira Bayizi ba-ali te-ba-samb-ye Omupiira |
| Wakati ujao hali timilifu – Muda | Kkp-naa-ba Kkp-Mz-YE | Kkp-naa-ba te-kkp-Mz-YE | Omuyizi anaa-ba asambye | Omuyizi a-naa-ba ta-samb-ye |

| | | | | |
|---|------------------------------|--|--|---|
| <i>mfupi unaotarajiwa</i> | | <i>Anaaba ta-samb-ye h-a-ta-kuwa amecheza</i> | <i>omupiira Bayizi ba-naa-ba ba-samb-ye omupiira</i> | <i>omupiira Bayizi ba-naa-ba te-ba-samb-ye omupiira</i> |
| <i>Wakati ujao hali timilifu (muda mrefu uliotarajiwa)</i> | <i>Kkp-li-ba Kkp-Mz-YE</i> | <i>kkp-li-ba te-Kkp-Mz-YE a-li-ba ta-samb-ye h-a-ta-kuwa amecheza</i> | <i>Omuyizi aliba asambye omupiira Bayizi ba-li-ba ba-samb-ye omupiira</i> | <i>Omuyizi a-li-ba ta-samb-ye omupiira Bayizi ba-li-ba te-ba-samb-ye omupiira</i> |
| | HALI YA KUENDELEA | | | |
| <i>Wakati timilifu, (hali ya kuendelea)</i> | <i>Kkp-badde Kkp-Mz-a</i> | <i>te-kkp-li-R-a t-a-li-samb-a amekuwa-</i> | <i>Omuyizi abadde asamba omupiira Abayizi babadde basamba emipiira</i> | <i>Omuyizi talisamba omupiira Abayizi te-ba-li-samb-a emipiira</i> |
| <i>Wakati uliopita hali ya kuendelea-Muda mfupi uliopita)</i> | <i>Kkp-aa-badde Kkp-Mz-a</i> | <i>Kkp-aa-badde te-Kkp-Mz-a ba-a-badde te-ba-samb-a h-a-waamekuwa h-a-wa-chez-i</i> | <i>Omuyizi a badde a-samb-a omupiira. Bayizi ba-a-badde ba-samb-a</i> | <i>Omuyizi a badde ta-samb-a omupiira. Bayizi ba-a-badde te-ba-samb-a</i> |
| <i>Wakati uliopita zamani, hali ya kuendelea</i> | <i>Kkp-aa-li Kkp-Mz-a</i> | <i>Kkp-aa-li te-Kkp-Mz-a Ta-kyali samb-a Yungali/angali</i> | <i>Omuyizi a kyali samb-a omupira Bayizi bakyali samb-a omupiira</i> | <i>Omuyizi takyali samb-a omupira Bayizi te-ba-a-kyali samb-a omupiira</i> |
| <i>Wakati ujao hali timilifu- muda mfupi, unaotarajiwa</i> | <i>Kkp-naa-ba Kkp-Mz-a</i> | <i>Kkp-naa-ba te-Kkp-Mz-a a-naa-ba ta-samb-a h-a--ta-kuwa a-me-chez-a</i> | <i>Omuyizi anaa-ba asambye omupiira Bayizi ba-naa-ba ba-samb-ye omupiira</i> | <i>Omuyizi a-naa-ba ta-samb-a omupiira Bayizi ba-naa-ba te-ba-samb-a omupiira</i> |
| <i>Wakati ujao hali timilifu (muda mrefu unaotarajiwa)</i> | <i>Kkp-li-ba Kkp-Mz-a</i> | <i>Kkp-li-ba te-Kkp-Mz-a a-li-ba ta-samb-a h-a-ta-kuwa a-na-chez-a badala ya a-me-chez-a</i> | <i>Omuyizi aliba a-samb-a omupiira Bayizi ba-li-ba ba-samb-a omupiira</i> | <i>Omuyizi a-li-ba ta-samb-a omupiira Bayizi ba-li-ba te-ba-samb-a omupiira</i> |
| | WAKATI UJAO | | | |
| <i>Wakati ujao wakati mrefu unaotarajiwa)</i> | <i>SP-li-R-a</i> | <i>te-kkp-li-Mz-a t-a-li-samb-a h-a-ta-chez-a</i> | <i>Omuyizi alisamba omupiira bayizi ba-li-samb-a omupiira</i> | <i>Omuyizi t-a-li-samb-a omupiira bayizi te-ba-li-samb-a omupiira</i> |
| <i>Wakati ujao, muda mfupi unaokuja</i> | <i>Kkp-naa-Mz-a</i> | <i>te-Kkp-naa-Mz-e t-a-naa-samb-a ha-ta-chez-a</i> | <i>Omuyizi a-naa-samb-a Omupiira. bayizi ba-naa-samb-a emipiira.</i> | <i>Omuyizi t-a-naa-samb-a Omupiira. bayizi teba-naa-samb-a emipiira.</i> |

Asili: Data kutokana na Hyman (2018), Leah & Sseguya ,(2015).

Jedwali (4.18) linabainisha kuwa Luganda hutumia mofu zaidi katika kudhihirisha mofu za njeo na hali tofauti na Kiswahili. Kwa mfano, wakati uliopo hali timilifu [-me-] katika Luganda huwakilishwa na viambishi nyambuizi [-zze, -a- na -ye] ambavyo huwekwa

mwishoni mwa mzizi (Mz) wa kitenzi elekezi. Wakati ujao huwakilishwa na [-li-ba na -ye], [li-ba na -a] ambazo huwekwa baada ya kiambishi kipatanishi (Kkp) na kiambishi tamati na [-naa-ba na -YE] na [-naa-ba na -a]. Viambishi vya mwanzo hutokea baada ya vipatanishi na viambishi vya mwisho kuwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi kuwakilisha wakati au hali ya wakati uliopita. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambacho hutumia kiwakilishi [-ta-] au hali ya [-kuwa] ya wakati ujao. Viwakilishi vya njeo ya wakati huu huwa havina mofu kanushi bali ukanushaji hujitokeza tu katika vitenzi kwa kutumia vikanushi [t- na te-] huku Kiswahili ikiweka kikanushi [ha au hu] kabla ya kiambishi cha kimofosintaksia cha upatanishi wa kisarufi mwanzoni, kikifuatwa na njeo yenyewe [-ta-] kwa mfano; [a-ta-imb-a] inakuwa [ha-ta-imb-a].

Katika Luganda, viambishi vya njeo na hali huweza kutokea mwishoni mwa kitenzi, baada ya kiambishi kipatanishi cha nafsi au ngeli nomino kiidadi. Kanuni ya ukanushaji nayo hutangulia mofu ya ukanushaji mwanzoni, ikifuatwa na kiambishi kipatanishi cha nafsi (Kkp) au ngeli nomino kiidadi na mzizi wa kitenzi ambao huisha na kiambishi tamati cha njeo au nyambuizi. Aidha, Luganda hutumia vikanushi vya [t- au te] kutegemea aina ya sauti inayotangulia mzizi wa kitenzi kinachokanushwa. Ukanushaji katika Luganda huweza pia kuathirika na maswala ya kifonolojia kama ilivyo katika wakati uliopita ambapo badala ya kusema [si-a-lim-a] utasema [saa-lim-a] ambapo kuna mvutano wa sauti inayoathiri sauti dhaifu na kusababisha toni ya juu ya sauti irabu zinazofuatana kuonyesha ukanushaji.

Matokeo haya yanashadidiwa na utafiti wa Lupogo, (2021) ambaye anazungumzia juu ya upekee wa uwili katika ukanushaji wa Kiswahili tofauti na lugha zingine za Kibantu na Kiingereza. Hyman, (2018) na Hassan, (2016) wanaofafanua tofauti baina ya ukanushaji wa Luganda na Kiswahili. Ufafanuzi wa wataalamu hawa uliongoza utafiti huu katika kubaini na kufafaua kufanana na kutofautiana kwa ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo yalibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu kuwiana katika ukanushaji, kimaumbo, kimpangilio na kimatumizi na katika uambishaji wa viambishi viwakilishi vya ukanushaji kutegemea njeo na hali. Matokeo haya yanaonyesha kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti kiisimu ambapo kila moja hudhihirisha upekee wake licha ya kuwiana kiunasaba.

4.2 Hitimisho

Sura hii imeangazia data kuhusu madhumuni ya kwanza ya kufafanua jinsi vipashio vya kimofosintaksia katika Luganda hufanana na kutofautiana na vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili. Data katika sura hii ni data ya maktabani. Jumla ya vitabu na Makala thelathini na manne (34) yanayofafanua miundo na kanuni za matumizi ya vipashio vya Kimofosintaksia vya Ngeli, Viwakilishi nafsi, vivumishi na ukanushaji vilichambuliwa na taarifa za miundo na kanuni katika matumizi kuchunzwa. Utafiti huu ulibaini kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, kila lugha ina upekee wa kimiundo na kikanuni katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli za nomino, viwakilishi vivumishi na vikanushi. Upekee huu unadhihirisha kuwepo kwa tofauti za kiasilia za vipashio vya kimofosintaksia kati ya Luganda na Kiswahili kimuundo na kimaumbo.

Aidha, ilidhihirika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu licha ya kudhihirisha maumbo na mpangilio wa kisarufi wa vipashio vya kisarufi, vipashio hivi hutofautiana katika matumizi. Uchunguzi wa maumbo ya ngeli kimofosintaksia yalidhihirisha kufanana kwa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu kugemea mfumo wa kimofolojia na kisintaksia. Hata hivyo, mfumo wa mpangilio wa nomino katika lugha hizi yanatofautiana kwa mengi. Tofauti inajitokeza katika matumizi ya uambishaji wa viambishi vya msingi vya upatanishi wa kisarufi kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo pamoja na idadi ya ngeli baina ya lugha hizi.

Uchanganuzi wa vivumishi ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili zina vivumishi ambavyo huundwa kwa kiambishi awali cha kivumishi ambacho hufanana na kiambishi awali cha nomino inayovumishwa na mzizi wa vivumishi ambao hubeba maana ya kileksika ya vivumishi hivyo. Hata hivyo, viambishi vinavyoambikwa kwenye mizizi ya vivumishi hutofautiana kutokana na maumbo ya ngeli pamoja na athari za kifonolojia ambazo hutokea katika lugha hizi kimaumbo. utafiti huu ulibaini kufanana na kutofautiana kwa viwakilishi vya Luganda na Kiswahili kimaumbo na kimiundo licha ya kufanya kazi moja ya kimofosintaksia ya kuwakilisha nomino na kusisitiza nomino inayotajwa katika mazungumzo. Aidha, matokeo kuhusu ukanushaji yalibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu kuwiana na kutofautiana katika ukanushaji, kimaumbo, kimpangilio na kimatumizi na katika uambishaji wa viambishi viwakilishi vya ukanushaji kutegemea njeo na hali.

SURA YA TANO
KANUNI ZA MIFANYIKO YA KIMOFOSINTAKSIA YA LUGANDA NA
KISWAHILI SANIFU

5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data ya madhumuni ya pili ambayo ni kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi. Data za madhumuni hii ilitokana na uchanganuzi wa matini kutumia kifa cha kudondoa data chenye sifa ya vipashio vya kimofosintaksia. Vitabu vya kiisimu vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu kufundishia sarufi na vitabu vya ziada vya kufundishia sarufi ya Luganda na Kiswahili sanifu viliteuliwa kidhamirifu. Makala ya ziada kama vile tasnifu, majarida, upekuzi wa maandishi na tafiti mbalimbali zilizoandikwa kuhusiana na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu maktabani na mtandaoni zilikusika. Data za utafiti huu ziliwasilishwa na kujadiliwa kwa kuzingatia matokeo ya uchanganuzi wa sheria za kimuundo za kipashio kimofolojia na kisintaksia, kuchunguza mpangilio wa matumizi ya kipashio katika utungo, utokeaji wa kipashio katika mazingira ya utungo na dhima au uwakilishaji wa kipashio husika katika tungo. Uwasilishaji na mijadala ilizingatia mihimili miwili ya ubia na upatanishi ya nadharia za unganifu na umilikifu ya Chomsky, 1981. Matokeo ya Uchanganuzi wa kanuni ulidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kila kipashio kilidhihirisha kanuni ya kipekee inayotumika kuonyesha uhusiano milikifu na Unganifu ya neno kuu na maneno mengine katika tungo. Miongoni mwa kanuni zilizochanganuliwa ni pamoja na kanuni ya uambishaji, uainishaji wa viambishi, sarufi miundo, uambishaji amilifu, viambishi yambwa, kifonolojia ya udondoshaji nakadhalika

5.1.1 Uwiano na utofauti wa Kanuni za mofosintaksia za ngeli nomino za Luganda na Kiswahili sanifu

Kanuni za mofosintaksia ni sheria za kiisimu au sarufi zinazoeleza uhusiano uliopo baina ya vipashio vya mofolojia na sintaksia zinazoelekeza na kufafanua usanifu au usahihi katika matumizi ya lugha. Usahihi huu hujitokeza katika utungaji wa tungo zenye mantiki unaozingatia viwango vya mofolojia na sintaksia kimaandishi na kimazungumzo. Umantiki huu hurejelea jinsi vipashio vya mofolojia vinavyoingana na kuhusiana kuunda tungo zenye maana (Barno, 2013; Mulei, Ambuyo & Amukowa 2021 na Oichoe, 2005). Aidha, kwa Mujibu wa Mulei na wenzake, (2021), Jerro (2018) na Kiyinikibi, (2021) Luganda na

Kiswahili ni lugha za Kibantu ambazo hutumia mfumo mmoja wa uainishaji nomino katika ngeli. Ngeli katika nomino ni kipashio cha kimofosintaksia ambacho ni muhimu sana katika sarufi ya lugha za Kibantu. Matumizi ya nomino katika ngeli huwiana na kutofautiana kutoka lugha moja na nyingine. Uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya ngeli kimofosintaksia huweza kusababisha athari za mwingiliano katika matumizi baina ya lugha mbili. Matumizi haya yanatokana na kanuni mbalimbali zinazoongoza mpangilio wa nomino katika ngeli na matumizi yake kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa neno kuu na maneno mengine katika tungo. Matokeo ya uchanganuzi wa upekuzi wa Mulei na Wenzake (2021), Leah & Sseguya, (2015) Hyman & Katamba (2001) kuhusu kanuni za matumizi ya nomino za Luganda na Kiswahili sanifu, ulitambua kufanana na kutofautiana kwa kanuni za matumizi ya kipashio cha ngeli katika nomino za Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyochanganuliwa hapa chini. Uwiano na tofauti hizi unatokana na mihimili ya sarufi bia na ya upatanishi. Uhusiano wa kimiundo wa maumbo ya nje na ndani ya viambishi ngeli ulidhihirisha Uwiano na tofauti kutokana na kauli ya mihimili wa sarufi bia unaochukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo.

5.1.1.1 Kanuni ya Kimofosintaksia ya Uundaji wa Nomino na mofolojia ya uambishaji

Kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino inashikilia kuwa, Nomino huundwa kutokana na kupachika viambishi mbalimbali vyenye sifa za kiuamilifu za mofolojia na sintaksia kwenye mizizi ya maneno katika tungo. Kidhima, kanuni hii hueleza kuwa uambishaji wa viambishi huwakilisha upatanishi wa kisarufi, ngeli na idadi ya umoja na wingi katika utungo kimofosintaksia kama katika data Na (4.1 Uk. 73); (4.2, Uk. 77) na (4.3, Uk 79). Licha ya nomino hizi kuundwa kwa mujibu wa kanuni hii, maumbo ya uundaji wa nomino yana dhihirisha uwiano na tofauti kutokana na mshiko wa mhimili wa kwanza wa nadharia ya Chomsky (1981) unazingatia sifa za sarufi bia ambao huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Data za maumbo katika (4.1 Uk. 73) yanadhihirisha tofauti husika.

Kanuni ya mofolojia ya uambishaji na kanuni ya sarufi miundo ni kanuni zinazotokana na utaratibu wa uundaji wa maneno kwa kuzingatia uambishaji wa viambishi kwenye maneno na aina za maneno katika tungo. Kanuni hizi zinaweza pia kutambulika kama kanuni ya sarufi miundo. Kanuni ya uambishaji hujenga uundaji wa nomino, uainishaji wa maneno na

mahusiano ya viambishi vya maneno na aina zake kisarufi. Kanuni hizi mbili hushikilia kuwa; Kila lugha huwa na maumbo ya kipekee yanayotumika kuunda vipashio vya kisarufi vya lugha kuwakilisha usahihi wake kimatumizi. Kanuni hii inatokana na ufafanuzi wa Massamba na wenzake, (1993) wanaoeleza kuwa maneno ya lugha huundwa kwa vipande vidogo vidogo vinavyowekwa pamoja kwa mpangilio na utaratibu maalumu (uambishaji) kujenga maana ya msingi ya maneno ya lugha. Pia, kanuni hii hushikilia kuwa uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi (uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno kutokana na nomino kama neno kuu. Hii ina maana kuwa kila nomino huwakilishwa na viambishi na shina au mzizi kimuundo na utaratibu wa matumizi ya viambishi katika mizizi hutokana na utaratibu wa uundaji wa nomino ambapo nomino huundwa kwa viambishi awali vya unominishaji wa nomino kuwakilisha maana ya kisarufi katika utungo. Viambishi vya nomino huweza kuwakilishwa na maumbo dhahiri na maumbi kapa. Viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi huwakilisha maana za kisarufi ambapo majina yanayoainishwa huzingatia maumbo yaliyo na upatanishi wa kisarufi wa maneno mengine ulio sawa kiurejeshi. Katika utungo, mfanano wa kimaumbo wa viambishi awali na vyenye upatanishi wa kisarufi huwakilisha ngeli, idadi na dhima ya umoja na wingi huzingatiwa (Massamba na wenzake, 2012; Mgullu, 1999; Katamba, 2003; Kiyinikibi; 2021). Utafiti huu umeunganisha kanuni hizi mbili kutokana na uwiano na utendakazi wake kisarufi.

Kwa kuzingatia mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya Chomsky, (1981), matokeo ya uchanganuzi wa data za mapitio ya Namugala (2014), Jerro (2018), Mulei na Wenzake (2021), Baertlein & Ssekitto (2014), Leah & Sseguya (2015), ilidhihirisha kuwepo kwa uwiano wa Luganda na Kiswahili sanifu kuunda nomino zake kwa kuweka viambishi mbalimbali kwenye mizizi ya nomino kutumia kanuni ya kimofolojia ya uambishaji katika uundaji wa nomino kama inavyojitokeza katika data Na. (4.1, Uk. 73), (4.2, Uk. 77), (4.3, 79), (4.4, Uk. 83) (4.6, Uk. 90).

Aidha, matokeo ya kimatumizi yalidhihirisha uwiano wa Luganda na Kiswahili sanifu kutumia viambishi amilifu vya awali kwa kuvipachika mwanzoni mwa mizizi ya nomino kuwakilisha ngeli, idadi ya umoja na wingi kisarufi, viambishi rejeshi, kurejelea nomino kama neno kuu katika tungo. Viambishi vipatanishi vya kisarufi ambavyo huwekwa katika maneno mengine katika utungo kama vitenzi na viwakilishi kutegemea neno kuu. Viambishi

hivi na viambishi vinginevyo vya uamilifu wa matumizi ya ngeli au idadi ya umoja na wingi vilitumika kuwakilisha sifa za kisarufi za kimofosintaksia zinazodhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo. Viambishi vilivyotumika ni viambishi vya nomino katika ngeli na idadi za umoja na wingi wa nomino pamoja na viambishi vya uwakilishi wa sifa za upatanishi wa kisarufi wa nomino na maneno mengine katika utungo.

Matokeo ya uchanganuzi wa upekuzi wa Mgullu (1999), Kihore & wenzake (2004), Massamba na wenzake (2003), Habwe & Karanja (2004), Kiyinikibi (2021) na Katamba (2003), ulidhihirisha pia kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huainisha nomino zake kwa kuzingatia msingi wa kanuni ya kimofolojia ya uambishaji wa maneno katika tungo kuwakilisha sifa za kimofosintaksia na kanuni ya uundaji wa nomino. Kwa kurejelea mihimili ya ubia na upatanifu wa Nadharia ya Umilikifu na Unganifu, ilibainika kuwa nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu ziliainisha na kutumia nomino kutokana na sifa za kimofolojia na kimuundo za nomino hiyo ambapo kila nomino iliwekwa katika kundi lake likiwa na mabadiliko ya aina moja ya viambishi vya umoja na wingi vyenye kuleta upatanishi wa kisarufi wa namna moja katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi (maneno mengine katika tungo). Nomino zimegawanywa kwa kuzingatia mfanano wa kifonolojia wa maumbo unaohusisha viambishi awali vya nomino na idadi ya umoja na wingi kama inavyorejelewa katika mfano (4.2, Uk. 77 na 4.3, Uk. 79), katika sura ya nne. Aidha, Viambishi hivi na viambishi vinginevyo vya uamilifu wa matumizi ya ngeli au idadi ya umoja na wingi vilitumika kuwakilisha sifa za kisarufi za kimofosintaksia zinazodhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo kama inavyorejelewa katika data Na (5.1):

- a) *O-mu-yimb-i a- yimb-ye o- lu- yimb-a*
Kb-Kng1-Mz- Kwk3- Mz- njeo(li) Kb-Kng5- Mz- kiambishi tamatii
Kibainishi-kiambishi cha ngeli ya kwanza- mzizi- kiwakilishi- njeo (-li-)
kibainishi- kiambishi cha ngeli ya 5- mzizi- kiambishi tamati)
- b) *a- ba- yimb-i ba- yimb-ye en -nyimb-a*
Kb- Kng2-Mz- Kwk3- Mz- njeo(li) Kb-Kng5- Mz- kiambishi tamatii
- c) ***Mw- imb-a-ji a- me -imb-a wimbo***
Kng1-Mz- Viambishi nominishaji Kng1 + Kwk3- Mz- njeo(me) wimbo
- d) ***Wa -imb-a-ji wa- me- imb-a nyimbo***
Kng2-Mz- Viambishi nominishaji Kng2 + Kwk3- hali (me) Mz- nyimbo
- e) *O-mu-yimb-i o-mu-lungi ayimbye oluyimba a-ba-yimbi a-ba-lungi ba-yimbye*
en-nyimba

| | |
|--|--|
| <i>Kb-Kng1- mz (Kisifa (V))</i> | <i>Kb-Kng2- mz (Kisifa (V))</i> |
| f) Mw-imbaji m-zuri ameimba wimbo | Wa-imbaji wa-zuri wa-meimba wimbo |
| <i>Kng1- mz (V)</i> | <i>Kng2- mz (V)</i> |
| g) <i>O-mu-yimbi o-no a-yimbye oluyimba</i> | <i>a-ba-yimbi a-bo ba-yimbye o-lu-yimba</i> |
| <i>Kb +Kng1- Kkny (Kionyeshi)</i> | <i>Kb+Kng1-Kkny (Kionyeshi)</i> |
| h) Mw-imb-(a-ji) | hu-yu a-me-imb-a wimbo |
| <i>Kng1-Mz+ (Viambishi nominishaji)</i> | <i>Kwk Kionyeshi1 Kng2-me-mz-a wimbo</i> |
| <i>Wa- imb-(a-ji)</i> | <i>ha-wa wa-me-imb-a wimbo</i> |
| <i>Kng2-Mz+ (Viambishi nominishaji)</i> | <i>Kwk Kionyeshi2 Kng2-hali-mz-a wimbo</i> |

Tanbihi:

Kibainishi (Kb) kiambishi cha ngeli ya kwanza (Kng1), mzizi (Mz), kiwakilishi nafsi ya tatu (Kwk3), njeo (-li-), kiambishi cha ngeli ya 5 (Kng5), Kwk Kionyeshi2 kionyeshi cha wingi

Asili: Data imeboreshwa kutoka kwa Kiyinikibi, 2021: Katamba, 2003; Chomi, 2003

Mifano ya data Na.(5.1), imebainisha wazi kuwa: Mpangilio na aina za viambishi katika Luganda na Kiswahili sanifu hufuata utaratibu au mpangilio fulani ambao ukipotoshwa usanifu wa lugha hiyo huwa umepotoshwa pamoja na dhima katika utungo. Data hii inadhihirisha kuwa Luganda hutumia vibainishi na viambishi ngeli kutenda kazi moja ya kutambulisha ngeli nomino na idadi ya umoja na wingi huku Kiswahili ikitumia viambishi ngeli nomino pekee. Hata hivyo, vibainishi hivi na viambishi ngeli huambisha mwanzoni, vikifuatwa na viambishi vinginevyo vinavyowakilisha sifa za kisarufi. Uimbukaji wa uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni hii unakubaliana na mhimili wa sarufi bia unaoshikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo kama tofauti za maumbo yanavyojitokeza katikamifano ya data Na.(5.1)

Kwa mujibu wa utafiti huu, Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika utaratibu wa kuweka pamoja vipande vidogo vidogo (vitamkwa, mizizi na viambishi) kuunda maneno kama nomino, vitenzi, vivumishi, viwakilishi na maneno mengineyo kutumia utaratibu wa uambishaji na unyambulishaji (kanuni ya uambishaji na miundo sarufi). Watumiaji hudhihirisha kuongeza mofu za kisarufi kwenye mizizi ya maneno kujenga maana msingi za kisarufi za maneno husika bila kuunda maneno mapya au bila kubadilisha aina za nomino. Katika uambishaji huu, nomino zimegawanywa kwa kuzingatia mofolojia yake na viambishi awali vya idadi vya umoja na wingi katika nomino. Hali ambayo ilidhihirisha kanuni ya

sarufi maumbo kama ilivyoielezwa na wanaisimu Katamba, (1993), Mgullu,(1999) na Kihore, Massamba & Msanjila, (2003) hasa katika uainishaji na matumizi ya ngeli nomino.

Matokeo ya uchanganuzi wa maelezo ya Leah na Sseguya, (2014), Obara, (2014), Kiyinikibi, (2021), Besha, (1996), Bochnack, (2013) na Katamba (2003), Lukamuka, (2015) Oduor na Wenzake (2017) na Mulei na Wenzake, (2021) kuhusu sifa kimofosintaksia za uambishaji na uundaji nomino, utafiti huu uligundua kuwa viwakilishi vya nafsi na viambishi vya upatanishi wa nomino katika vitenzi katika Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana kinafasi na mahali pa utokeaji. Viambishi hivi huwekwa mwanzoni mwa mzizi wa nomino na kitenzi, nomino na kivumishi nomino na viwakilishi; na huwa vinaonyesha uhusiano wa moja kwa moja na nomino na maneno mengine katika tungo. Pia, viambishi vya vivumishi kama vya sifa, vya nomino hukaririwa katika vivumishi na huwekwa mwanzoni mwa mizizi huru au mizizi tegemezi ya vivumishi husika kudhihirisha sifa za kimofosintaksia. Tofauti iliyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu katika kanuni ya sarufi maumbo na uambishaji ni kuwa Luganda ilishirikisha sana matumizi ya vibainishi awali {a, o na e} ambavyo hupachikwa nyuma ya viambishi ngeli vinavyowakilisha maumbo ya maneno kisarufi katika mazungumzo na maandishi, huku Kiswahili ikitumia viambiahsi ngeli vya umoja na wingi pamoja na viambishi vipatanishi vya kisarufi vya nomino kutegemea aina ya nomino katika tungo kuwakilisha maumbo ya kimofolojia na kisintaksia kiuamilifu katika tungo kama inavyorejelewa katika mfano wa data ya (4.2, Uk. 77 na 4.3, Uk. 79), Luganda hutumia viambishi vibainishi {o na a} kwenye nomino {mwana na baana} vibainishi hivi vimetumika pamoja na viambishi ngeli {mw na ba} vya ngeli ya kwanza na pili kuwakilisha umoja na wingi wa nomino kisarufi. Aidha, viambishi hivi vimepachikwa mwanzoni mwa mzizi {-an-} na kiambishi tamati cha kibantu {-a} kuunda mofolojia ya nomino kuwakilisha seti za sifa za kisarufi za nomino kimofolojia kuwakilisha umoja na wingi.

Matokeo ya uambishaji na uundaji nomino mwingine ambao ulijitokeza katika Luganda na Kiswahili kwa kuambisha viambishi vipatanishi kwenye kategoria za maneno kama ilivyoielezwa na Katamba, (2003), Jerro, (2018), Oichoe, (2005), Rose (2009), Namugala, (2014) wanaoeleza kuwa lugha za Kibantu ni lugha ambazo zina muundo wa ngeli nomino ambazo huambisha viambishi awali katika mizizi au mashina ya maneno katika utungo kuwakilisha upatanishi wa kisarufi na ujenzi wa vipengele vinginevyo vya kisarufi. Ngeli nomino kwa hiyo haiwezi kubainishwa tu kwa viambishi awali vinavyopachikwa kwenye mizizi au mashina ya maneno kimofolojia bali pia katika utungo kisintaksia kuwakilisha

nomino kuwa ama kiima au neno linaloashiria kitendwa au kitendewa katika utungo (yambwa). Katika Kiswahili, uambishaji wa viambishi vipatanishi kwenye kategoria ya maneno ya kisarufi hutegemea viambishi ngeli vya nomino tajwa kimofolojia na kisintaksia. Kimofolojia, vivumishi huchukua maumbo sawa ya viambishi ngeli vya nomino kimofolojia kwa umoja na wingi, huku vionyeshi, viwakilishi na vitenzi vikichukua viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya ngeli kisintakisa. Sifa hii ni ya mhimili wa upatanifu wa Nadharia ya Umilikifu na Uganifu ya Chomsky, (1981) kama inavyojitokeza katika data Na. (5.2)

Kutokana na matokeo ya mijarabu ya utafiti huu, (2021)

- a) \emptyset -Ng'ombe *m-nono a-nakimbia* \emptyset -Ng'ombe *wa-nono wa-nakimbia*
- b) *M-kate m-kubwa u-meletwa* *Mi-kate mi-kubwa imeletwa*
- c) \emptyset -tunda \emptyset -tamu *limeuzwa* *Ma-tunda ma-tamu yameuzwa*

Kwa mujibu wa data za mifano (5.2) ya tungo (a-c) nomino 'ng'ombe' imepata kiambishi chake [\emptyset] ambapo kimofolojia ngeli hii inastahili kuwekwa katika ngeli ya 9 na 10 hata hivyo kisemantiki, nomino hii ni ya viumbe wenye uhai ambapo inapatikana katika ngeli ya 1 na 2. Kwa hiyo, upatanishi wake ukawa unatokana na mofu za kimofolojia za umoja na wingi wa ngeli ya kwanza {m} kimofolojia na {a-} kisintaksia ambapo wingi wake ni {wa-}. Sentensi ya (b) imepata viambishi vyake vya kimofosintaksia vya {M- na U-} kwa umoja na [Mi-na I-] kwa wingi huku sentensi ya (c) ikichukua viambishi vya { \emptyset } ya ngeli ya {ji-} kwa umoja na wingi wake kimofosintaksia ukiwakilishwa na viambishi {ma- na ya} kwa wingi. Hali hii inadhihirisha kuwa kimofosintaksia, mwanafunzi anastahili kuambisha viambishi vya nomino vya kimofolojia na kisintaksia kwa kutegema viambishi ngeli ambamo nomino husika inapatikana katika kategoria za maneno ya kisarufi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Tofauti na Luganda, Kiswahili kimejenga mofolojia ya maneno kutumia viambishi ngeli vya awali kuwakilisha sifa za kisarufi za ngeli nomino na idadi ya umoja na wingi wa nomino katika utungo. Kwa mfano; kiambishi {m na wa} vimetumika kuwakilisha maumbo ya umoja na wingi wa nomino ambapo viambishi hivi vimewekwa mwanzoni mwa mzizi. Kiuamilifu, Kiswahili kimetumia viambishi vya upatanishi wa kisarufi wa nomino katika utungo kwa kutumia maumbo ya kisarufi {a na wa} ya ngeli ya kwanza na pili. Luganda imetumia maumbo ya vibainishi pamoja na viambishi ngeli na idadi kujenga upatanishi wa kisarufi wa nomino kisintaksia katika utungo. Viambishi hivi vimetumika kimofosintaksia katika utungo ambapo umbo la kisintaksia linajitokeza kiurejeshi kutokana na maumbo ya kimofolojia ya nomino kama neno kuu. Hali kama hii inadhihirisha tofauti kati ya Lugha ya Luganda na Kiswahili hata ingawa lugha zote ni zenye sifa bia za Kisarufi.

Tofauti nyingine iliyogunduliwa ni kuwa Kiswahili sanifu ilidhihirisha matumizi ya uambishaji wa nomino zaidi ya moja kutoka ngeli tofauti zilizowekwa pamoja kwa kuambisha viambishi awali kwenye vitenzi vilivyofuata nomino ya mwisho katika mfuatano au orodha. Katika utaratibu huu wa uambishaji wa maneno katika tungo kutegemea orodha ya nomino zilizo katika mfululizo, nomino ya mwisho katika mfuatano au mfululizo ndiyo iliyoathiri upatanisho wa kisarufi wa utungo (Besha, 1996). Hali hii ni kinyume na Luganda ambayo hutumia kiambishi kielezi cha kisemantiki cha nomino tajwa kama inavyofafanuliwa na Kiyinikibi, (2021) na Asiimwe, (2016).

Matumizi haya yalisababishwa na kanuni ya utaratibu wa uambishaji wa nomino zaidi ya moja za ngeli tofauti za nomino kulingana na Chomsky, (1995) iliyoshikilia kuwa ikiwa nomino zaidi ya moja zinazotoka katika ngeli tofauti katika mfuatana, nomino ya mwisho ndiyo inayoathiri upatanishi wa kisarufi wa nomino na kitenzi na viwakilishi katika utungo. Kanuni hii hushikilia kuwa upatanishi wa kisarufi wa nomino na kitenzi au nomino na maneno mengine hutokana na nafasi na dhima ya utokeaji wake katika tungo (Chomsky; 1995). Mkabala huu unashadidiwa na na wataalamu kama Besha (1994) na Habwe & Karanja (2004) ambao wameonyesha kuwa maarifa aliyonayo mjua lugha ni pamoja na kujua muundo sahihi wa sentensi za lugha yake pamoja na kubaini mfuatano wa maneno katika sentensi, uainishaji wa maneno katika makundi na uhusiano wa maneno yanayojenga sentensi. Aidha, wanashikilia kuwa mjua lugha ana umilisi wa kuweza kuchanganua sentensi kwa mujibu wa ujirani wa viambajengo na mahusiano yake kujenga usanifu wa mazungumzo na maandishi sanifu ya lugha sanifu. Data Na. (5.3) inadhihirisha uwiano na tofauti kuhusu uambishaji wa nomino zaidi ya moja. (5.3):

a) *Omusomesa, akambe, ebendera **byona** bintu bya gavumenti*

Mwalimu, kisu, **bendera** inamilikiwa na serikali ya Uganda.

b) *Enyumba, emmotoka ne sukali **byona** batesseza kubeyi **yabyo bikulibwe kubeyi ya wansi***

Chumba, gari na **sukari** vilipikiwa bei kwa nia ya kupunguza gharama.

Asili: Data Imeboreshwa kutokana na Kiyinikibi, (2021)

Mifano hii inadhihirisha kuwa, nomino ya mwisho ‘bendera’ ndio iliyosababisha au kuathiri kipatanishi cha kisarufi [i-] cha kutumika katika orodha au mfululizo wa nomino ambazo hazipatikani katika ngeli moja kimofolojia. Aidha, katika sentensi ya pili, kiambishi cha upatanisho wa kisarufi cha [vi-] kimetumika kuwakilisha orodha ya bidhaa kwa hivyo semantiki ya ‘bidhaa’ imesababisha kiambishi cha upatanisho wa kisarufi wa [vi-]

uliopachikwa katika kitenzi kuwakilisha upatanisho wa kisarufi kimofosintaksia. Tofauti ya kanuni hii ya Kiswahili na Luganda ni kuwa nomino za hadhi ya juu katika ngeli ya vitu hisivu hutangulia nomino iliyo na hadhi ya chini katika muundo wa sentensi katika Luganda.

Kwa mujibu wa mapitio ya Mgullu (1999), Habwe & Karanja, (2003) na Kapinga (1983), Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika kutumia kanuni ya uainishaji wa nomino kuzingatia viambishi vya kimofolojia vya viambishi awali kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi wa nomino. Aidha, lugha hizi huwiana kwa kuzingatia kanuni ya kutumia viambishi vipatanishi vya kisarufi katika maneno mengine kama vitenzi, vivumishi, vionyeshi na viwakilishi katika mazungumzo na maandishi kuwakilisha ngeli, idadi na jinsi ya kisarufi ya umoja na wingi. Viambishi ngeli nomino na vya upatanisho wa kisarufi vilitumika kuwakilisha maumbo tofauti kulingana na ngeli kwa umoja na wingi kimofolojia na kisintaksia kutumia njia ya kijozi. Maumbo haya yalibadilika kwa kuwakilisha umoja na wingi kimofosintaksia na hata kuathiri muundo au maumbo ya maneno katika utungo kuwakilisha upatanishi wa kisarufi kimatumizi. Viambishi vilivyopachikwa kwenye maneno yote yaliyotumika katika Lugha hizi, yalionyesha upatanifu (uhusiano) wa kisarufi na viambishi vya nomino na idadi katika utungo kimofolojia na kisintaksia. Hii ilitokana na kuwa kanuni hii ilishikilia kuwa ni lazima kila neno kuwakilishwa na vibainishi na/au viambishi ngeli vyake vinavyoonyesha upatanishi wa kisarufi hasa vinapotumika katika utungo kimaandishi au kimazungumzo kama ilivyofafanuliwa na Katamba (2003) na Namugala (2014). Mifano ya data kuwakilisha uwiano katika matumizi ya kanuni hii ni kama unavyorejelewa katika mfano (4.2, Uk. 77) wa data za upekuzi wa maandishi.

Kwa mujibu wa mapitio ya kazi za Sekiryango, (2006), Bochnak, (2013), Mulei na wenzake (2021), Licha ya Luganda kuwiana katika matumizi ya kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino kwa kutumia viambishi patanishi kimofolojia na kisintaksia, kuainisha ngeli kimuundo kutokana na kufanana kwa viambishi awali na viwakilishi vyake vya ngeli, viambishi vya nomino vya upatanishi wa kisarufi kupachikwa mwanzoni mwa maneno mengine hasa vivumishi, vionyeshi, viunganishi au viwakilishi wakati nomino fulani inapotumika katika utungo kutegemea ngeli ambamo nomino hiyo hupatikana, utafiti huu ulibaini tofauti iliyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kuhusiana na kanuni ya uundaji wa nomino na mofolojia ya uambishaji. Ilibainika kuwa Luganda hutumia vibainishi na viambishi awali vya nomino kuunda nomino (kuwakilisha idadi na ngeli ya nomino) huku Kiswahili kikitumia kiambishi kimoja (kiambishi awali) cha nomino pekee katika nomino na

maneno mengine katika kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi, na dhima ya kisarufi katika utungo. Matokeo haya yanashadidiwa na Kihore, Massamba na Msanjila, (2003) ambao kulingana na maelezo yao, kanuni hizi huchunguza mpangilio na taratibu za kutumia vitamkwa, mizizi, viambishi na mifanyiko ya uambishaji na unyambulishaji katika uundaji wa maneno kuwakilisha ngeli husika na idadi. Kidhima kanuni hii huchunguza taratibu za kuongeza mofu za kisarufi kwenye mizizi ya maneno kujenga maana fulani za kisarufi za maneno husika bila kuunda maneno mapya au bila kubadilisha aina za nomino, maneno na aina za maneno, taratibu zinazohusika katika uundaji wa maneno na matumizi ya maneno katika utungo.

Matokeo haya yanashabihiana na ufafanuzi wa matumizi ya viambishi kutokana na kanuni au msingi wa uainishaji wa nomino katika ngeli na matumizi ya maneno mengine kisarufi kama ilivyoelezwa na Ssekiryango, (2006), Katamba (2003), Kapinga (1983), Yule, (1996) na Underson (1992) wanaoeleza kuwa, maneno ya lugha yoyote yana uwakilishi wa kimofosintaksia ambao huainisha sifa zote ambazo ni muhimu kwa kanuni za uundaji wa maneno kimofolojia na ya kisintaksia; na taarifa za neno hutumiwa kueleza taarifa za kimofolojia na sintaksia kuwakilisha sifa za kimofosintaksia za neno kimatumizi na uwakilishi wa kimofosintaksia wa neno huonekana katika sintaksia, na njia pekee ambayo kwayo sintaksia yaweza kuathiri umbo la neno ni kumiliki uwakilishi wake wa kimofosintaksia katika tungo. Utafiti huu uligundua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika matumizi ya kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino ila hutofautiana katika maumbo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Uwiano na tofauti hizi zinadhahirisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja zilizo na kanuni sawia katika uundaji wa nomino, lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye sifa za kiisimu zinazotofautiana kama inavyorejelwa katika mihimili wa sarufi bia. Ukiukaji wa matumizi au uhamishaji wa kanuni moja kwa moja bila kuzingatia sifa bainifu za kimatumizi za lugha baina ya Luganda na Kiswahili, huweza kuathiri matumizi sanifu ya lugha ama ya Luganda au ya Kiswahili sanifu.

5.1.1.2 Kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kimofosintaksia

Kanuni hii inashikilia kuwa: Uambishaji unaohusika katika maneno katika utungo kimofosintaksia lazima ubebe sifa za kimofosintaksia kutegemea vibainishi awali au viambishi awali vinavyopachikwa kwenye maneno na aina za maneno katika tungo. Kulingana na kanuni hii, nomino zote zilizo na viambishi awali vya umoja na wingi

vinavyofanana huwekwa katika kundi moja ambalo huitwa ngeli. Pia, viambishi ambavyo havina maumbo ya umoja au wingi au kinyume kuwekwa katika kundi lake (Mgulu, 1999; Kiyinikibi, 2021; Habwe & Karanja, 2004; Katamba, 2003 na Besha, 1996). Kanuni ya uainishaji inatokana na uainishaji wa ngeli nomino ambapo misingi mbalimbali ya matumizi ya viambishi hutumika katika nomino na katika utungo kuwakilisha sifa za kisarufi za lugha. Kanuni ya uainishaji ni msingi wa kimofolojia wa kutumia viambishi nomino kuwakilisha idadi na ngeli kwa umoja na wingi, matumizi ya jozi za viambishi, uainishaji wa kisintaksia wa kutumia viambishi vya upatanishi wa kisarufi, msingi wa kutumia viambishi nomino kimofolojia na viambishi nomino kisintaksia katika utungo kuwakilisha ngeli, jinsi ya kisarufi, idadi ya umoja na wingi na sifa zinginezo za kisarufi (Baertlein na Ssekitto, 2014; Kihore, Massamba & Msanjila, 2003).

Uainishaji wa kimofosintaksia wa viambishi ngeli hutumia mofu zinazopachikwa kwenye maumbo ya nomino kimofolojia kuwakilisha ngeli na idadi nomino kwa umoja na wingi na vipatanishi vyake katika utungo kwa njia ya urejeshi au uwakilishi nyuma wa nomino. Kupitia kwa kanuni hii, ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu zimeainishwa kwa kutumia njia ya ujozi kuwakilisha idadi ya umoja na wingi na uainishaji wa ngeli kisintaksia au kwa kuzingatia viambishi nomino vya upatanishi wa kisarufi kubeba sifa za kisarufi za nomino kama ilivyojitokeza katika jedwali la (4.1, Uk. 71 na 4.2, Uk. 76) na mifano ya data za sentensi kutokana na uainishaji wa ngeli kutokana na Besha (1996), Oichoe, 2004 na Leah & Sseguya (2015) na Abudonia (2014) kama katika Data Na. (5.4):

- a) **Omuzanyi omulungi** **Abazanyi abalungi** [ngeli o(mu)-a(ba)]
- b) **Mchezaji mzuri.** **Wachezaji wazuri** [Ngeli ya M-Wa]
- c) **Ekitabo ekirungi kikuume Ebitabo ebirungi bikuume** [Ngeli ya e(ki)-e(bi)]
- d) **Kitabu kizuri kitunze.** **Vitabu vizuri vitunze** [Ngeli ya Ki-Vi]
- e) **Ennyumba ennungi** **Ennyumba ennyungi** [Ngeli ya en-en]
- f) **Nyumba nzuri.** **Nyumba nzuri** [Ngeli ya N-N]
- g) **Omuti omuwanvu Emiti emiwanvu** [Ngeli ya o(mu)-e(mi)]
- h) **Mti mrefu** **Miti mirefu** [Ngeli ya M-Mi]

Asili: Data za utafiti kutoka kwa data za Abudonia, (2014)

Mifano ya data (5.4) inaonyesha uhusiano wa kimiundo wa viambishi vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hujitokeza katika sintaksia. Maumbo ya kimofolojia ya nomino imeathiri maumbo ya kiupatanishi ya vivumishi vya sifa vya Luganda na Kiswahili sanifu.

Aidha, kwa mujibu wa maumbo haya, nomino imetumika kama neno kuu ambapo viambishi vya kimofolojia huathiri viambishi vya upatanishi wa kisarufi. Viambishi ambavyo vimepachikwa mwanzoni mwa vivumishi vya sifa na kitenzi katika sentensi ya (b) na maumbo ya nomino tajwa, yaani viambishi vya nomino. Hii ina maana kuwa viambishi hivyo vyote vilivyokolezwa vimetumiwa katika tungo kama viwakilishi jirejee vya ngeli nomino na maneno mengine husika katika utungo vikiwa na sifa za kimofosintaksia vya nomino tajwa kuwakilisha aina ya ngeli na idadi au hali ya umoja na wingi. Viambishi hivi vimetumia mofu zilizobeba sifa za upatanishi wa kisarufi (mofosintaksia) wa idadi kwa umoja na jinsia ya kisarufi kwa njia ya urejeshi wa nomino. Sifa hii ni sifa ya mhimili wa upatanishi wa nadharia ya umilikifu na unganifu wa kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo. Mofu zilizokolezwa za kimofolojia zimetumika kiupatanifu kutokana na uhusiano wa neno kuu kuathiri maumbo mengine yanayowekwa katika maneno mengine kuonyesha uhusiano patanifu wa nomino na vivumishi. Tazama maumbo yaliyokolezwa katika sentensi (a-h). Matumizi haya yanadhihirisha ubia na upatanishi wa maumbo ya Luganda na Kiswahili sanifu. Licha ya Luganda na Kiswahili kushirikisha maumbo na kanuni ya uainishaji na uambishaji, matumizi ya kanuni yanatofautiana baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Uwiano na tofauti hizi zinaendana na mhimili wa sarufi bia ambao huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Hali ambayo inadhihirisha tofauti baina ya Luganda na Kiswahili katika matumizi ya kanuni hii ya uainishaji wa viambishi ngeli.

Matokeo ya uchanganuzi wa kazi za Kiyinikibi (2021), Bochnak, (2013), Katamba, (2003), Mgullu, (1999), Baertlein & Ssekitto, (2014) zilidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni hii ya uainishaji wa viambishi vya nomino katika ngeli. Kwa kuzingatia mihimili ya Ubia na upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Unganifu, utafiti huu ulitambua kuwa, Luganda na Kiswahili huainisha na kutumia nomino kulingana na aina za viambishi ngeli kuonyesha idadi ya umoja na wingi wa nomino kimofolojia na kisintaksia. Aina za maumbo ya viambishi vya kimofolojia ndivyo vilivyoathiri aina za maumbo ya viambishi vilivyopachikwa kwenye nomino na maneno mengine katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino kama neno kuu na maneno mengine katika tungo. Tofauti iliyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa, Luganda ilidhihirisha matumizi ya nomino katika utungo kutokana na uainishaji wa nomino kutumia vibainishi awali vya ngeli na viambishi ngeli katika matumizi, huku Kiswahili kikizingatia aina moja ya viambishi

vya nomino katika ngeli ambavyo pia viliathiri sintaksia ya matumizi ya nomino katika tungo kuonyesha dhima ya kisarufi ya idadi ya umoja na wingi, uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo kama inavyojitokeza katika data za mifano ya data (4.1, Uk. 73), (4.2, Uk. 77), (4.3, Uk. 79) katika data za sura ya nne.

Kulingana na utafiti huu, maumbo ya viambishi wakilishi vya ngeli ni vipatanishi au maumbo maalumu ambayo huwekwa katika maneno mengine wakati nomino fulani inapozungumziwa au kutumika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Utafiti huu ulichunguza aina ya viambishi vipatanishi ambavyo hupachikwa hasa kwenye vitenzi, vivumishi na viwakilishi katika utungo na vikanusho vyake. Uambishaji huu ni wa kimofosintaksia ambao hujitokeza katika utungo ambapo viambishi awali vya nomino na viambishi vya upatanishi wa kisarufi hutumika kujenga usanifu au sarufi ya lugha kuzingatia kaida za lugha husika. kama katika data Na. (5.5) kutokana na Leah & Sseguya (2015), Namugala (2014) Mgullu (1999), Kisakwah (2014), Oichoe, (2005) na Egara (2016): (5.5)

Luganda

Kiswahili

- a) *Omuzannyo guno mulungi guzanyibwa.* Mchezo huu mzuri unachezwa.
- b) *Ekitabo Kino Kirungi kigume.* Kitabu hiki kizuri kitunze.
- c) *Abazzadde bange balungi bayimba.* Wazazi wangu wazuri wanaimba.

Sentensi hizi za Luganda na Kiswahili zinaonyesha uhusiano wa kimiundo wa viambishi nomino ambapo viambishi vilivyopachikwa kwenye maneno mengine vinatokana na nomino iliyotumika kama neno kuu. Viambishi ambavyo vimepachikwa mwanzoni mwa vionyeshi, vimilikishi, visifa na vitenzi katika tungo vimetokana na maumbo ya uainishaji wa nomino tajwa. Viambishi hivi ni viambishi vya kimofosintaksia ambavyo kimatumizi viambishi {omu-} na {m-} vya nomino katika Luganda na Kiswahili vimeathiri maumbo ya kipatanishi ya vionyeshi, visifa, vimilikishi na maumbo yaliyowekwa kwenye vitenzi vya Luganda na Kiswahili sanifu kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu. Uhusiano huu wa viambishi vya kimofolojia kupata uamilifu wake katika sintaksia ya tungo za Luganda na Kiswahili vinaendana na Nadharia ya Umilikifu na Unganifu (Chomsky, 1981) ambayo husisitiza sehemu za sentensi kuhusiana na kanuni kadhaa, na kila kipashio kueleweka kwa msingi wa uhusiano wa kimiundo ambapo neno kuu humiliki maumbo ya shamirisho zake. Matumizi haya yanaendana na kanuni inayoshikilia kuwa, lazima kirejeosabiki (Anafora) kifungamane na kategoria inayokimiliki katika tungo. Kanuni hii ni ya mhimili wa upatanishi ambayo

hufafanua kanuni za kisintaksia zinazotawala urejeleo nyuma unaojikita katika makundi nomino katika sentensi.

Utafiti huu uligundua kuwepo kwa uwiano na tofauti uliojitokeza katika uainishaji wa nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili kimofosintaksia. Ilibainika kuwa viambishi vyote vinavyotumiwa katika umbo nomino katika Luganda na Kiswahili hutawala viambishi vyote vinavyotumiwa katika tungo kama viwakilishi jirejee. Mpangilio huu huzingatia kigezo cha mantiki cha maumbo ya mofu za ngeli, kimofolojia na kiupatanishi wa kisarufi kwa umoja na wingi (kisintaksia) (Egara 2016); Kiyinikibi 2021; Baertlein & Ssekitto 2014). Aidha, utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili huanisha ngeli zake kisintaksia kwa kutumia kigezo cha uainishaji wa kisintaksia. Kwa mujibu wa uainishaji huu, lugha hizi zilidhihirisha kupanga nomino ngeli zilizo na mianzo tofauti pamoja kwa kufuata mantiki ya upatanisho wa kisarufi kama inavyojitokeza katika data za (4.1 Uk. 73 na 4.2, Uk. 77) kwa mujibu wa data kutokana na Katamba, (2003), Namugala, (2014), Assimwe, (2016) na Mgullu, (1999), Baertlein & Ssekitto, (2014).

Kwa kuongezea ingawa kanuni hii huwiana katika matumizi baina ya Luganda na Kiswahili, kanuni ya uambishaji wa viambishi ngeli ambavyo hubeba sifa za kimofosintaksia za maneno ya kisarufi yenye sifa za upatanisho wa kisarufi katika tungo hutofautiana. Kiswahili sanifu kinaonekana kutofautiana na Luganda katika utaratibu wa kuambisha viambishi hivi katika maneno kama vile vionyeshi ambapo kiwakilishi jirejee huwekwa mwishoni mwa mofu ya uwakilishi wa kionyeshi. Aidha, Kiswahili kinaonekana kutotumia vibainishi vya ngeli, huku Luganda ikitumia vibainishi na viambishi ngeli kudhihirisha idadi na jinsia ya kisarufi ya uwakilishi wa umoja na wingi wa nomino tajwa. Uainishaji huu ni ule wa kutambulisha nomino katika msingi wa nafasi na dhima au kazi ya nomino hiyo katika sentensi kisemantiki (Chomi, 2003). Uainishaji huu unajenga kanuni ya nafasi na dhima ya nomino katika utungo kisemantiki. Viambishi kapa ni viambishi ambavyo haviwezi kutamkwa wala kuandikwa bali hudhihirika akilini mwa mzungumzaji kuwakilisha dhima ya kisarufi ya ngeli, idadi ya umoja na wingi pamoja na upatanishi wa kisarufi. Viambishi hivi hujitokeza katika maneno kama vile nomino, vitenzi, viwakilishi, vivumishi na kiima. Viambishi hivi huwakilishwa na alama ya kisarufi ya [Ø] kama inavyojitokeza katika data Na. (5.6) ya data ya maktabani kutokana na Baertlein & Ssekitto, (2014), Kiyinikibi, (2021), Obara, (2014), Mgullu (1999) na Besha (1996).

Kwa Mfano nomino za Kiswahili

| | |
|---------------------------|-------------------------------|
| <i>Omuchungwa</i> | <i>emichungwa</i> |
| Ø-chungwa | m chungwa |
| Ø <i>Deleeva</i> | <i>Badeleeva</i> |
| Ø-dereva | M dereva |
| <i>Enngoye nnuungi</i> | <i>enngoye nnuungi</i> |
| Ø Nguo ø safi | Ø Nguo ø safi |
| <i>Omuntu omuzira</i> | <i>abaantu abazira</i> |
| Mtu ø- jasiri | M tu ø- jasiri |
| Ø <i>Jjakumkuba omubi</i> | Ø <i>tujjakubakuba ababbi</i> |
| Nitampiga mwizi | tutawapiga wezi |

Kwa mujibu wa (Kiyinikibi, 2021; Katamba, 2003) na Mgullu (1999) utafiti huu ulitambua kuwa tofauti na Kiswahili, maneno mengi katika Luganda yanaweza kuchukua viambishi kapa yanapotajwa kama nomino na yanapowekwa katika utungo, maneno hayo huweza kuchukua viambishi vya upatanishi wa kisarufi tofauti na Kiswahili ambapo nomino ikiwa haiambishwi na viambishi ngeli na idadi ya umoja na wingi inabakia vivyo hivyo katika utungo wa kimofosintaksia. Aidha, yafaa itambulike kuwa maneno mengi yasiyoambishwa katika Luganda ni maneno ya mkopo kutoka lugha za kiarabu, Kihindi na hata Kiingereza kama inavyojitokeza katika uchanganuzi wa kazi za Kiyinikibi, (2021), Katamba, (2003) katika Data Na. (5.7)

| Luganda | Kiswahili |
|---|--|
| <i>Umoja</i> | <i>Wingi</i> |
| ø- <i>Taata (Baba)</i> | <i>Bataata</i> (kina baba) |
| ø- <i>maama (Mama)</i> | <i>Bamaama</i> (Kina mama) |
| ø- <i>caayi (Chai)</i> | ø- <i>caayi</i> (Chai) |
| <i>Palamenti (Bunge)</i> | <i>Palamenti</i> (mabunge) |
| Ø <i>Ettayi eno ennungi egudde</i> | Ø <i>Ettayi zino ennungi zigudde (Luganda)</i> |
| Ø Tai hii nzuri imeanguka | Ø tai hizi nzuri zimeanguka. (Kiswahili) |
| <i>Omukyala yafumba caayi.</i> | <i>Abakyala bafumba caayi (Luganda)</i> |
| Mwanamke alipika ø-chai | Wanawake walipika ø- chai (Kiswahili) |
| <i>Buuzako ø-taata akubuulire.</i> | Muulize baba akueleze |
| <i>Asili: Data kutokana na Kiyinikibi, (2021:29, 31 na 92)</i> | |

kwa mujibu wa mifano hii ya Luganda ilidhihirika wazi kuwa baadhi ya nomino zinazochukua viambishi kapa ni zile zinazotajwa, kimofosintaksia nomino hizo hupokea

vibainishi vya ngeli kuwakilisha umoja na wingi wake zinapotumika kimazungumzo na kimaandishi. Vilevile, katika utafiti huu ilitambulika kuwa nomino hizo zinapotumia vibainishi, vitenzi hupewa viambishi vya upatanishi wa kisarufi na vivumishi kuchukua vibainishi na viambishi ngeli ambamo ngeli hiyo imeainishwa, hali ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu. kama katika mfano wa sentensi *ϕ-Maama o-mu-lungi a-fumbye e-mmere e-woma* (Mama Mzuri amepika chakula kitamu) Katamba, (2003) na Kiyinikibi, (2021). Matumizi haya yanaendana na mihimili wa sarufi bia ambao huegemea sana katika upatanifu wa kisarufi ambao neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo. Aidha, licha ya lugha hizi kushirikisha matumizi ya kanuni hii, kila lugha hutofautiana kimatumizi. Kutofautiana huku kunatokana na mihimili wa sarufi bia unaochukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo.

Licha ya kuwa nomino [mama] imechukuwa kiambishi kapa kuwakilisha umoja, kivumishi kimetumia kibainishi [o-] na kiambishi ngeli nomino cha ngeli ya kwanza [mu-] kinachokaririwa katika nomino ambamo nomino [maama] imeainishwa na kiambishi kipatanishi cha kisarufi cha nafsi ya tatu [a-] umoja kutumika. Vilevile, kivumishi cha nomino [emmere] kimetumia kibainishi na kiambishi ngeli [e-] cha ngeli katika kivumishi tegemezi [-woma]. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambapo nomino zisipowekewa viambishi ngeli, basi hata katika utungo haviwezi kupachikwa vibainishi wala viambishi ngeli. Mshabihiano unaojitokeza ni kuwa nomino hizo zinapotumika katika utungo na maneno mengine dhana ya uwakilishi wa nafsi, uwakilishi wa dhima ya umoja na wingi hudhahirika. Aidha, vivumishi vinaweza kuchukua viambishi awali vya nomino au visichukue kutegemea idadi. Kivumishi cha sentensi ya kwanza katika mfano wa hapo chini imechukua kiambishi cha ngeli [N] na umoja wingi [ma] huku sentensi ya pili ikiwa na kivumishi kisichochukua kiambishi ngeli kama katika data (5.8) wa data kutokana na Abudonia (2014) na Kiyinikibi, (2021) (5.8):

ϕ-Gari n-zuri limezimwa.

Ma-gari ma-zuri ya-mezimwa.

ϕ-Nyumba ϕ-Kubwa imejengwa.

ϕ-Nyumba ϕ-kubwa zi-mejengwa.

Asili: Abudonia (2014) na Kiyinikibi, (2021)

Utafiti huu ulitambua kuwa matumizi ya viambishi kapa katika utungo hutegemea maneno mengine katika utungo na hujitokeza kisemantiki kutokana na umilisi wa watumiaji wa lugha husika kuwakilisha nafsi, ngeli na idadi ya nomino, dhima na jinsi ya kisarufi katika utungo kutokana na muundo na uainishaji wa nomino husika kama neno kuu. Aidha, ilitambulika

kuwa nomino nyingi zinazotumia viambishi kapa ni maneno ya mkopo (Katamba, 2003; Rose, 2009).

Matokeo haya yanashadidiwa na maelezo ya watalaamu kama vile Mgullu, (1999), Beshu, (1996), Katamba, (2003), Kiyinikibi, (2021), wanaeleza kuwa uainishaji wa nomino katika ngeli mbalimbali hujikita katika mfanano wa kimaumbo wa viambishi awali vya idadi ya umoja na wingi. Nomino zenye mianzo ambayo inawakilisha viambishi awali vya nomino mbalimbali huweza kuwekwa katika kundi moja kama ngeli na matumizi yake kujikita katika uainishaji ambamo nomino hiyo imeanishwa. Ukiukaji wa kutumia viambishi visivyoiweka nomino hiyo katika kundi ambamo nomino hiyo imeanishwa huweza kuharibu usanifu au usahihi wa matumizi ya nomino husika (Habwe & Karanja, 2004 na Mgullu, 1999). Uwiano na tofauti hizi zinashadidiwa na Kisakwah, (2014) anayefafanua kuwa nomino ni kipashio cha kisarufi ambacho ni muhimu kwa kuwa huathiri vipashio vingine katika sentensi na jinsi ambavyo vipashio mbalimbali vya lugha huchukuana na hukubaliana katika sentensi. Nomino hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Utafiti huu ulibaini kuwa licha ya kuwepo kwa uwiano wa Luganda na Kiswahili kutumia kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kimofosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na neno kuu katika tungo, matokeo ya upatanishi wa kisarufi yanadhihirisha kuwiana na kutofautiana, kutofautiana huku kulidhihirisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili sanifu kuwa lugha za nasibu moja, ni lugha mbili tofauti zilizo na kanuni za mifanyiko ya kipekee ambayo isipozingatiwa, usarufi wa lugha hizi hupotoshwa.

5.1.1.3 Kanuni ya sarufi miundo

Kanuni hii inashikilia kuwa mpangilio wa maumbo ya kimofolojia katika kategoria ya maneno huathiri vipashio na umbo linalofuata katika muundo wa utungo. Vilevile kanuni hii inadai kuwa upatanifu wa kisarufi katika utungo hutawaliwa na vipashio vya kimofosintaksia na vipashio hivyo huathiriana ambapo kipashio cha kwanza hutegemea sana kipashio cha pili ili kuleta maana. Kanuni hii ni kanuni ya uhusiano wa kiusabiki ambapo umbo moja huwakilisha umbo jingine katika tungo kwa njia ya kiurejeleo sabiki (anafora na katafora) kujenga utungo ambao ni wa upatanishi wa kisarufi (Beshu, 1996; Massamba na wenzake, 2012; Philipo, 2017).

Matokeo ya mapitio ya maandishi ya Beshu, (1996), Philipo, (2017), Massamba na Wenzake, (2012), Kiyinikibi, (2021), Leah & Sseguya, (2015) Namugala, (2014), Baertlein & Ssekitto, (2014), utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiana na kutofautiana

katika matumizi ya kanuni ya sarufi miundo. Ilibainika kuwa Lugha hizi hutumia kanuni hii kuunda nomino, kuainisha nomino na kutumia nomino katika tungo kwa kuzingatia utaratibu wa uambishaji wa viambishi katika neno kuu na maneno mengine, pamoja na kutumia kategoria ya maneno katika tungo kwa usahihi. Kila kiambajengo yaani neno, kirai au sentensi kimetumika kikiwa na maana kamili. Aidha, Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kanuni hii kuunda kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi kisicho na uhusiano wa kiima na kiarifu (Kirai). Matokeo haya yanaendana na sifa za sarufi bia ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Data Na. (5.9) inadhihirisha data za kutokana na Philipo (2017), Massamba na wenzake, (2003), Namugala, (2014), Baertlein & Ssekitto, (2014), Mgullu (1999) kudhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya sarufi miundo. (5.9):


- | | |
|---------------------------------|------------------------------|
| <i>a) O-mw-ana wange a-lina</i> | <i>A-lina omunwa omutono</i> |
| <i>b) Mtoto wangu ana</i> | <i>A-na</i> |
| <i>c) Omugati gugudde wanzi</i> | <i>Gu-gudde wansi</i> |
| <i>d) MKate umeanguka chini</i> | <i>Umeanguka chini</i> |

Asili: Data za utafiti kutokana na Namugala, (2014:122)

Mifano (5.9) inaonyesha data za sentensi zinazodhihirisha aina tofauti ya maneno ambayo ni nomino {N}, vitenzi {T}, kihusishi {KH} na kadhalika. Maneno haya yameunganishwa kuunda virai. Uchanganuzi wa virai hivi unaonyesha uhusiano kati ya mtenda, tendo na kitendo. Uhusiano huu unajitokeza kutokana na muunganiko wa maneno haya kuunda virai, vishazi na sentensi. Kwa mfano, kwa kuchunguza sentensi ya kwanza; {Omwana/Mtoto} ni nomino za Luganda na Kiswahili ambazo zimewakilishwa na maumbo ya kimofolojia {mw-/m-} na {-ana/-toto}. {Mw-/M-} ni viwakilishi vya idadi au ngeli ya kwanza umoja na viambishi hivi vimewakilishwa na umbo {a-} la upatanifu wa ngeli za kisemantiki za majina yenye uhai ambayo yamepachikwa kwenye mzizi wa kitenzi na kiishio chake cha Kibantu {-a-}. {a-}ya upatanishi wa kisarufi imetumika kwa kurejelea umbo la idadi la nomino iliyotangulia katika utungo na {a-} ya upatanisho wa kisarufi imetumika kutokana na umbo la mofolojia ya nomino iliyotangulia kurejelea idadi, yaani maumbo ya viambishi {mw-/m-} yamesababisha matumizi ya umbo {a-} linatokana na umbo la awali {m-} kimofosintaksia. Maumbo haya yanatokana na sarufi miundo ya virai mbapo kuna kirai nomino kilichoundwa kwa nomino peke yake na kikundi tenzi {KT} ambacho kimeundwa na vitenzi viwili na nomino mbili. Hata hivyo uhusiano wa kiima kiarifu umejitokeza baina ya Nomino ya kundi KN na kitenzi [T] kilicho karibu sana na nomino kama neno kuu. Data hii inashabahi sifa za

sarufi bia ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Tofauti za maumbo zinadhihirisha uwiano na tofauti baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Mifano ya uchanganuzi umetolewa katika mchoro wa matawi ifuatayo ikiwakilisha sifa za kimfosintaksia za maneno kuunganika kuunda maana kamili kutokana na Mgullu (1999), Massamba na wenzake (2003) kama katika mchoro (M5.1)

Mchoro M5.1: Matawi inayodhihirisha kanuni ya sarufi maumbo



Asili: Mchoro wa kanuni kutokana na matokeo ya utafiti huu, (2021)

Mchoro (4.2.1) unadhihirisha kanuni ya Muungano inayorejelea mahusiano ya utawala wa viambajengo ambapo sentensi imeundwa na viambajengo viwili vya [KN na KT]. KN yaelekea kubeba dhima ya sentensi na viambajengo vinavyojitokeza vinatokana na KN. Katika utawala, yaelekea kuwa KN inatawaliwa na kategoria ya nomino [N] kama neno kuu na KT kutawaliwa na kategoria ya kitenzi [T] kama neno kuu. Katika mchakato yaelekea KN imejengwa na [T] na KN hata hivyo KT haitawali KN bali inatawala T. Aidha, KN imeundwa kwa [N] na KT. Hata hivyo, KN imetawaliwa na nomino. Mwisho KT imeundwa kwa T na N hata hivyo KT inaonekana kutawaliwa na T na N. T na N ni kategoria tofauti moja ikiwa ni kitenzi na nyingine nomino. Kwa jumla utatambua kuwa katika Luganda, sentensi hii inaonyesha mahusiano ya kimpangilio ya kategoria ya maneno yanayojenga sentensi. Kategoria hizi zimeonyesha mahusiano ya moja kwa moja kimuktadha kujenga sentensi sahihi yenye dhima ya mawasiliano. Mahusiano ya kikategoria yanayojitokeza yanatokana na viambajengo vya maneno. Mahusiano haya ni baina ya KN na KT ambapo nomino imetawala viambishi vipatanishi vya kitenzi katika KT. Hata hivyo, hakuna uhusiano unaojitokeza kati ya maneno [mukatale kugula ekalamu]. Vifundo ukomo vilivyoainisha kutokana na uambajengo wa kategoria ya maneno kuunda sentensi, unaonyesha uhusiano wa

KN na KT ambapo viambishi vilivyopachikwa katika kitenzi vinadhihirisha uhusiano wa kiupatanishi wa kisarufi kati ya nomino na kitenzi.

Kwa kurejelea mihimili ya ubia na upatanifu wa Nadharia ya Umilikifu na Unganifu ya Philipo & Kuyenga (2017), Massamba na wenzake, (2003), Namugala , (2014), Baertlein & Ssekitto, (2014), Mgullu (1999), ilidhihirika Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika kupanga mofu kuunda maneno na tungo ila zinatofautiana katika maumbo yanayowakilisha miundo sarufi ya viambishi au mofu za ngeli kuwakilisha idadi na ngeli kwa umoja na wingi kuwakilisha sifa za kisarufi. Kiswahili kimetumia kiambishi kimoja kuwakilisha muundo wa kisarufi wa ngeli na idadi ya kisarufi ya umoja, huku Luganda ikitumia viambishi viwili vya vibainishi ngeli na viambishi ngeli kubainisha sifa za sarufi muundo wa nomino kuwakilisha sifa za kisarufi za ngeli na idadi ya umoja na wingi. Kwa mfano; [O-mw-ana na m-toto] Luganda imetumia kibainishi ngeli {o-} kikifuatwa na kiambishi ngeli {mu-} na mwisho mzizi wa nomino katika kirai nomino, huku Kiswahili ikitumia kiambishi {m-} kuwakilisha muundo wa kisarufi wa nomino kuwakilisha idadi ya umoja na wingi katika ngeli ya kwanza katika kirai nomino tofauti na Luganda. Aidha, katika Luganda vipashio au seti za sifa zingine za kisarufi huchukua mpangilo au miundo ya kisarufi tofauti na Kiswahili hasa kuzingatia utaratibu wa kuambisha njeo katika vitenzi. Matokeo haya yanashabihiana na sifa za sarufi bia ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo

Matokeo haya yanaendana na maelezo ya Besha (1996), Kiyinikibi, (2021), Habwe & Karanja (2004), walionyesha kuwa, sifa kuu za uchambuzi wa sentensi ni kubaini mfuatano wa maneno katika sentensi, uainishaji wa maneno katika makundi, uhusiano wa maneno yanayojenga sentensi, na uhusiano kati ya sentensi. Sentensi huundwa kwa sehemu kuu mbili za kirai nomino na kirai kitenzi. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilibainika kuwa kanuni ya sarufi miundo licha ya kuwa inadhihirisha uwiano baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na vigezo vya uhusiano wa neno kuu na shamirisho, urejeo nyuma wa vipashio na mpangilio wa vipashio katika utungo, Kanuni ya sarufi miundo ni kanuni ambayo inajihusisha na upangaji wa vipashio vidogo katika kuunda maneno au mpangilio wa maneno baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kuunda virai, vishazi au sentensi hutofautiana.

5.1.1.4 Kanuni ya umiliki na usabaki wa viambajengo

Kanuni ya umiliki na usabaki ni kanuni ya sarufi miundo virai ambayo huonyesha uhusiano wa viambajengo katika tungo. Kanuni hii inashikilia kuwa: vifundo huunda kiambajengo kama na kama tu viambajengo hivyo vitakuwa ni jozi za vifundo vinavyomilikiwa kikamilifu na kifundo kikuu (Chomsky, 1957:1967). Aidha, katika utaratibu wa kuunganisha KN na KT, vitenzi huambishwa kwa maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino kuwakilisha sifa za kisarufi za mofosintaksia kuwakilisha nafsi, ngeli na idadi, ya umoja na wingi wa kiima na kitenzi. Umiliki ni uhusiano wa kisintaksia wa neno moja kutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo. Kisabaki ni umbo linalotumika kurejelea neno lililotajwa awali au litakalotajwa baadaye (Lusekelo, 2017). Kwa mujibu wa kanuni hii umiliki na usabiki hudhihirika kupitia kwa viambishi ngeli vya nomino na vitenzi ambapo kwa msingi wa kanuni ya ufungami, kiambishi ngeli huwa ni anafora huku nomino ikiwa ni kisabaki. (Mathooko, 2004, Haegeman, 1994, Ambuyo, 2007, Businge, 2014).


Kanuni hii hujihusisha na uchanganuzi wa virai vinavyojitokeza katika utungo ambapo kirai nomino husabiki kirai tenzi na jinsi sentensi inavyomiliki na kutawala kirai nomino na kirai tenzi. Kirai ni kipashio cha kimofosintaksia chenye neno moja au zaidi kisichokuwa na mahusiano ya kiima kiarifu (Kihore, Massamba & Msanjila, 2003). Mahusiano ya kiimakiarifu ni mahusiano yanayoonyesha anayetenda tendo (kiima) na tendo linalotendwa (kiarifu). Kanuni hii imeelezwa na wanaisimu kama vile Philipo & Kuyenga, 2017, Karanja & Habwe, 2003 na Kihore, Massamba & Msanjila, (2003) kama kanuni ya muundo virai. inachunguza muundo wa lugha unaotokana na sauti, silabi, neno, kirai na tungo kutoka kiwango au daraja ya juu hadi chini. Kila sentensi hujengwa na vipashio ambavyo hubeba habari zote za kisarufi zinazoonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya neno kuu na maneno mengine katika tungo (Chomsky 1993, 1995). Umiliki ni uhusiano wa kisarufi (kisintaksia) wa neno moja kutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo (TUKI, 1990) kama katika Data Na. (5.10) kutokana na kazi za Philipo & Kuyenga (2017), Massamba na wenzake, (2003), Namugala, (2014), Baertlein & Ssekitto, (2014), Mgullu (1999) kudhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya sarufi miundo. (5.10)

- a) *O-mw-ana a-genze mukatale kugula ekalamu a-genze mukatale kugula ekalamu*
- b) *M-toto a-meenda sokoni kununua kalamu a-me-enda sokoni kununua kalamu*
- c) *Omugati gugudde wanzi gu-gudde wansi*
- d) *M-kate u-me-anguka chini u-me-anguka chini*

Asili: Data za utafiti kutokana na Namugala, (2014), Baertlein & Ssekitto, (2014).

Utafiti huu ulitambua kujitokeza kwa kanuni hii katika Luganda na Kiswahili sanifu ambapo muundo msingi wa sentensi hujengwa kwa viambajengo viwili ambavyo ni kirai nomino [KN) na kirai tenzi [KT]. Matokeo haya yanaendana na sifa za sarufi bia ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Kwa mujibu wa viambajengo hivi, neno kuu katika KN ni nomino na katika KT ni kitenzi. Kwa kuzingatia kanuni hii ya umiliki na usabiki wa viambajengo, virai hivi vinahusiana kisarufi vinapotumika katika utungo. Virai huwekwa pamoja ili kujenga kipashio kikuu cha kimofosintaksia yaani sentensi. Matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili ni ya mhimili wa sarufi bia kwa mtazamo wa msingi wa maumbo ya nje na ndani ya viambishi vya umiliki na usabiki wa viambajengo. Mahusiano haya ya kimofosintaksia ni yale yanayotokana na kuwa katika upatanifu, kipengele kimoja hukitegemea kingine (upatanifu wa kiarifu hutegemea mahusiano ya kiima) kwa baadhi au sifa zote za kimofosintaksia kama inavyojitokeza katika data (5.10) kutokana na matokeo ya utafiti huu katika mchoro (M5.2)

Mchoro M5.2: Uchanganuzi kutumia mchoro wa matawi



Asili: Kutokana na Kihore & Massamaba, (2001) na (2003)


Mchoro huu unaonyesha kuwa Sentensi (S) huundwa kwa jozi za KN na KT, na KN imeundwa na jozi za Nomino (N) na Kivumishi (V). KT, imejengwa kwa jozi za T1, kitenzi cha kwanza na KN na mwisho KN ikaundwa kwa Kitenzi cha pili T2 na Nomino. viambajengo hivi ni huru ila vinahusiana kujenga kiambajengo kikubwa ambacho ni sentensi [S]. Mahusiano yanayojitokeza ni yale yanayojitokeza katika nomino na maneno mengine

katika virai vinavyohusika katika utungo. Kwa mujibu wa Egara (2016) uhusiano huo wa kiuambajengo wa sentensi unadhihirika kupitia viambishi ambavyo athari zake zinatokana na kiambishi cha jina la ngeli ya nomino. Pia, viambishi hivi kwa msingi wa kanuni ya ufungami lazima vidhihirishe upatanisho na ngeli ya nomino ambapo kiambishi ngeli huwa ni anafora huku nomino ikiwa ni kisabaki. Upatanishi huu hudhihirika kupitia kategoria ya kitenzi. Kwa hiyo, S humiliki vifundo KN na KT. Pia, KN humiliki kategoria iliyopo chini yake na KT kumiliki viambajengo vilivyoko chini yake. Uhusiano uliopo kati ya KN na KT ni wa neno kuu kutokana na uambajengo wa maneno chini yake kutoka kushoto kuelekea kulia ambapo neno kuu katika utungo ni wa KN. Kiuwakilishi maumbo ni kuwa;

S → KN → KT → uhusiano wa Umilikifu

Kwa kuzingatia mihimili ya Ubia na Upatanifu wa nadharia ya Umilikifu na unganifu, utafiti huu ulibaini Luganda na Kiswahili sanifu kutumia kanuni hii kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Kanuni ya umiliki na usabaki unaojitokeza katika Luganda na Kiswahili sanifu ni ule unaotawaliwa na urejeleo nyuma wa kutegemea makundi nomino (ngeli nomino) katika sentensi. Umiliki na usabaki katika Kiswahili ulibainika kudhihirika kupitia viambishi ambavyo athari zake zinatokana na kiambishi cha jina la ngeli ya nomino. Mahusiano ya umiliki na usabaki (upatanishi) wa ngeli kisarufi na kiidadi huathiri vijenzi vingine katika kiwango cha sintaksia kupitia kwa upatanisho wa viambishi ngeli. Hali hii inatokana na kuwa, Lugha nyingi za Kibantu ambazo ni lugha ambishibainishi, ni lazima kitenzi kipatane na nomino kiima kuhusu nafsi na idadi kimatumizi. Vilevile, vivumishi hupatana na nomino au kiima kuhusu idadi. Neno kuu katika kirai nomino (KN) hupatana kisarufi na vivumishi vyake kuhusu vipengele kama vile idadi na nafsi na kadhalika (Shaban, 2015; Philipo, 2012). Upatanishi huu hudhihirika kupitia kategoria ya kitenzi, vivumishi, viwakilishi nafsi, vikanushi na kategoria zingine za kisarufi katika utungo. Mfano wa data Na.(4.1, Uk. 73), (4.2, Uk. 77), (4.3, Uk 79) na (4.4, Uk. 83) (4.6, Uk. 90) katika sura ya nne inadhihirisha uwiano na tofauti za mofimu patanishi katika Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika mchoro (M5.3) kutokana na matokeo ya utafiti huu.

Mchoro M5.3: Kanuni ya umiliki na usabaki kwa njia ya matawi



Asili: Mchoro kutokana na matokeo ya utafiti huu, (2021)

Kwa kuzingatia sentensi hizi, viambishi vilivyokolezwa katika sentensi, vimetumika kwa kuzingatia urejeleo nyuma unaozingatia maumbo au viambishi ngeli vya kimofolojia vya nomino na viambishi ngeli vya upatanishi wa kisarufi ambavyo vimepachikwa nyuma ya vivumishi na vitenzi kuwakilisha sifa za kimofosintaksia za kisarufi zikiwakilisha idadi ya hali ya umoja na wingi na jinsi ya kisarufi. Hali hii inatokana na kijenzi cha sifa za sarufi bia za lugha inayoamini kuwa umilikifu ambajengo ni uhusiano wa miundo ya kisarufi unaotokana na vipashio kuvitangulia na kuvimiliki vingine na ambavyo hutumiwa kueleza uhusiano wa kianafora katika sentensi.

Viambishi hivi kwa msingi wa kanuni ya ufungami vimedhihirisha umiliki (upatanishi) na ngeli ya nomino ambapo kiambishi ngeli huwa ni anafora huku nomino ikiwa ni kisabaki. Aidha, uhusiano mwingine baina ya Luganda na Kiswahili ni kuwa, Luganda na Kiswahili sanifu huchunguza mahusiano ya kirai nomino na virai vingine kama virai vitenzi, vivumishi, vionyeshi na kadhalika katika utungo kutegemea ngeli. Uhusiano unaohusika hujitokeza ndani mwa nomino na virai. Katika utaratibu wa kuunganisha KN na KT, vitenzi huambishwa kwa maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino kuwakilisha sifa za kisarufi za mofosintaksia kuwakilisha ngeli na idadi, nafsi au ya umoja na wingi wa kiima na kitenzi. Mahusiano haya ya kimofosintaksia ni yale yanayotokana na kuwa katika upatanifu, kipengele kimoja hukitegemea kingine (upatanifu wa kiarifu hutegemea mahusiano ya kiima) kwa baadhi au sifa zote za kimofosintaksia. Kwa mujibu wa kanuni ya muundo virai ya kikategoria na kileksioni, utafiti huu umetambua kanuni nyingineyo ya:

5.1.1.4.1 Kanuni ya uambishaji amilifu

Kwa mujibu wa utafiti huu, hii ndiyo daraja muhimu inayotokana na uambishaji wa viambishi kwenye mizizi ya maneno, kujenga kategoria za maneno ambayo huwekwa katika virai kujenga muundo wa virai nomino na virai tenzi katika utungo. Aidha, uambishaji huu hujenga sentensi sahihi za lugha ya Luganda na Kiswahili sanifu tofauti na kanuni za kategoria zilizotolewa na Philipo & Kuyenga (2017) na Vitale (1981) na kanuni ya msamiati (Katamba, 1993). Kanuni hii inatokana na kigezo cha umuundo wa kanuni za uundaji maneno na nomino ambayo ni ya kimofolojia. Kwa hivyo, katika uchanganuzi wa sentensi, daraja hii ndiyo ya mwisho baada ya kuchambua viambajengo vya sentensi, kategoria za maneno na uainishaji wa maneno. Kwa kuongezea, kanuni hii hutumika kueleza vijenzi vya maneno na uhusiano wa maneno unaojenga ngeli nomino za kategoria za neno kuu na maneno mengine katika utungo, kuonyesha uhusiano wa neno kuu na maneno mengine katika utungo. Viambishi vinavyojitokeza ni viambajengo vya kimofosintaksia vya maneno ambayo yanabeba sifa za kisarufi za upatanisho wa maneno katika tungo. Kwa mfano sentensi katika mfano wa mchoro Na.(5.4) inadhihirisha ujitokezaji wa kanuni ya muundo virai ya uambishaji amilifu katika Luganda na Kiswahili sanifu katika sentensi ifuatavyo.

Hivyo, Luganda na Kiswahili sanifu huwiana na kutofautiana kuhusu vile upatanifu baina ya nomino na vivumishi vyake unavyodhihirika. Katika Luganda, upatanisho wa kisarufi huzingatia kwamba vibainishi na viambishi vinavyopachikwa mwanzoni mwa nomino katika sentensi huathiriwa na ngeli ya nomino husika, huku Kiswahili kikiongozwa na viambishi awali vya nomino kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na muktadha wa kimatumizi wa nomino husika katika utungo. Kiwiano, data za maktabani zilidhihirisha kuwa uteuzi wa nomino hutawala upatanishi wa kisarufi wa maneno mengine kama vile vitenzi, vivumishi, viwakilishi na hata vikanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu na maumbo ya upatanishi hutofautiana kutokana na uainishaji wa nomino katika ngeli moja hadi nyingine kutegemea pia lugha kama katika mifano ya data za (4.2, Uk. 73), (4.3, Uk. 79), (4.4, Uk. 83). Kwa mujibu wa data hizo viambishi vya kimofolojia vilivyokolezwa katika nomino ndivyo vinavyotawala upatanishi wa kisarufi wa vitenzi, vivumishi, vionyeshi ambavyo kwayo vipo karibu sana na nomino kama neno kuu katika utungo. Matumizi ya viambishi hivi vinaendana na kijenzi cha mihimili wa sifa za sarufi bia za lugha inayoamini kuwa umilikifu ambajengo ni uhusiano wa miundo ya kisarufi unaotokana na vipashio kuvitangulia na kuvimiliki vingine na ambavyo hutumiwa kueleza uhusiano wa kianafora katika sentensi.

Data hizi zilibainisha uwiano wa mihimili ya Ubia na Upatanishi wa kuwa, upatanishi wa kisarufi katika tungo za Luganda na Kiswahili huzingatia kwamba, viambishi vinavyowekwa mwanzoni mwa vitenzi katika sentensi huathiriwa na mofolojia ya nomino katika ngeli husika ili kujenga viambishi vya kisintaksia. Aidha, viambishi mwanzoni mwa vivumishi vya sifa katika sentensi huathiriwa na ngeli ya nomino husika ambapo viambishi ngeli vinavyokaririwa katika nomino ndivyo vinavyopachikwa mwanzoni mwa vivumishi vya sifa husika kutegemea ngeli nomino. Upatanisho huo hutofautiana kutoka ngeli moja hadi nyingine na maumbo ya nomino katika ngeli kutoka lugha moja na hadi nyingine. Kipashio cha kimofosintaksia kwenye mzizi wa nomino hugeuka na kuwa kipatanishi cha nomino kwenye mzizi ama wa kitenzi au kivumishi katika mazingira ambamo viambajengo hivyo hupatana kwa ngeli na idadi. Kanuni hii ya kimofosintaksia inafafanua mifanyiko ya kimofosintaksia inayochochewa na kategoria ya kimofosintaksia ya ngeli kuwakilisha idadi ya umoja na wingi.

5.1.1.4.2 Kanuni ya upatanishi wa kisarufi wa viambishi yambwa

Uchanganuzi wa data za mapitio ya maandishi Habwe & Karanja, (2004), Oichoe, (2005) na Egara (2016), Rose, (2009) na Kiyinikibi, (2021) ilibainika pia kuwa kanuni ya umiliki na

usabaki vilevile ulibainika kujitokeza katika viambishi yambwa ambao utafiti huu uliita kanuni ya upatanishi wa kisarufi wa viambishi yambwa. Yambwa tendo hudhihirisha athari ya kile kinachotendwa moja kwa moja na yambwa hupata manufaa ya kitendo. Egara (2016) anaeleza yambwa kuwa kitendwa au kitendewa katika muundo wa kishazi huru. Kulingana na fasili yake Egara (keshatajwa), yambwa hurejelea kirai nomino au kirai bainishi ambacho huja baada ya kiarifu. Katika maelezo yake, alibainisha aina mbili kuu za yambwa ambazo ni yambwa msingi au yambwa upili ambavyo hutokea katika kishazi huru.

Utafiti huu uligundua kiuwiana na kutofautiana kwa kanuni ya upatanishi wa viambishi yambwa baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kiwiano, utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia yambwa kama kipashio cha kimofosintaksia chenye uamilifu wa kisarufi katika kirai tenzi (KT). Uamilifu uliojitokeza ni ule wa matumizi ya mofimu za upatanishi kuonyesha uhusiano unaorejelea nomino tendwa na tendewa katika KT. Mofimu yambwa ni kiambishi kipatanishi cha nomino katika kirai tenzi. Mofimu hizi hupachikwa katika kirai tenzi kutegemea nomino kama neno kuu. Hii ina maana kuwa viambishi yambwa vinavyopachikwa kwenye KT hutofautiana kutokana na uainishaji wa nomino katika ngeli mbalimbali. Aidha, katika matumizi, kiambishi hiki huweza kutumia viambishi ngeli au viwakilishi nafsi kuwakilisha nomino tendwa au nomino tendewa. Viambishi yambwa ni mofimu (mofimu ya upatanishi wa kiima, mofimu ya upatanishi wa yambwa, Mofimu ya Njeo) ambayo hubeba sifa zote za kuonyesha uhusiano ambajengo wa neno kuu na maneno mengine (upatanishi kati ya vipashio) katika tungo (Kiyinikibi, 2021); Bochnak, 2013); Oichoe 2005; Chomsky 1993, 1995) kama inavyojitokeza katika data Na.(5.11) ya data ya yambwa kutokana na Egara (2016):

| Kiswahili | Luganda |
|--|--------------------------------------|
| A-LLNL-PIG-A | ya-n-kub-a |
| <i>Kip nafsi3.Ngeli1 umoja –wkt uliopita-kiptanishi</i> | <i>kiambishi yambwa- piga</i> |
| WA-LI-TU-PIG-A | Ba-a-tu-kub-a |
| <i>Kip nafsi3/Ngeli 2 Wingi –wkt uliopita-kiptanishi</i> | <i>kiambishi yambwa- piga</i> |
| A-LI-M-PELEK-A | ya-mu-twala |
| <i>Kip nafsi3/Ngeli 1 umoja –wkt uliopita-kiptanishi</i> | <i>kiambishi yambwa ng11- peleka</i> |
| WA-LI-WA-PELEK-A. | Ba-a-ba-twala |
| <i>Kip nafsi3/ngeli 2 wingi –wkt uliopita-kiptanishi</i> | <i>kiambishi yambwa- peleka</i> |

Asili: Kutokana na mapitio ya maandishi ya Oichoe, (2005) na Egara, (2016)

Mifano hii inaonyesha viambajengo katika KT. Viambajengo hivi vimeundwa na mofimu za idadi ya nomino katika ngeli, njeo, upatanishi, nafsi nk. Mifano hii inadhihirisha upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya kwanza (1). Upatanishi huu umechukua mofimu yambwa mbili. Mofimu yambwa ya nafsi na ngeli ya 1 na 2 ya upatanishi ngeli ya [a-wa] tendwa na yambwa tendewa. Kanuni inayojitokeza katika upatanishi huu ni pale yambwa tendwa hutangulia yambwa tendewa katika KT. Matumizi haya ya viambajengo yanaendana na msingi wa mihimili wa sarufi bia ambao huegemea katika upatanifu wa kisarufi ambao neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo na uchunguzi wa lugha kwa msingi wa umbo ndani na umbo nje.

Kwa kurejelea mihimili ya Ubia na Upatanishi ya Nadharia ya Umilikifu na Unganifu, utafiti huu ulibaini uwiano na tofauti ya matumizi ya viambishi yambwa katika virai. Uwiano na tofauti ulijitokeza kutokana na kanuni ya utawala inayofafanua uhusiano baina ya vijenzi sanjari vya kisintaksia. Kwa mujibu wa utafiti huu, uhusiano uliojitokeza ni ule uhusiano baina ya kichwa cha kirai na shamirisho. Kanuni ya utawala ilirejelea uhusiano wa kijenzi kimoja (mtawala) kikiwa na kingine mtawaliwa. Kanuni hii iliongoza utafiti huu kubainisha matumizi ya yambwa kutokana na kanuni ya umuundo wa viarifu na dhima ambapo ilitambulika kuwa vipatanishi vya virai nomino hufuata kitenzi kujenga yambwa (Egara, 2016; Chomsky 2000 na 2001). Upatanishi ulijitokeza kupitia kwa uhusiano baina ya vipatanishi na kategoria ya kitenzi katika vishazi au tungo. Kanuni ya anafora na usabaki ya nadharia ya ufungami ilijitokeza katika kuelezea upatanishi wa viambishi patanishi vya yambwa ambapo uhusiano baina ya anafora na kisabaki chake ulielezwa. Kupitia kwa kanuni hii, mahusiano ya yambwa na matumizi ya uwakilishi wa yambwa katika vishazi ulirejelewa.

Matokeo haya yanashadidiwa na yale ya utafiti wa Oduor na Wenzake, (2017) ambaye katika utafiti wake alibainisha kuwa uhamishaji wa sarufi ya Kiluo huathiri upatanishi wa kisarufi katika Kiswahili kwa sababu kanuni za lugha hizi mbili ni tofauti hasa katika kanuni ya uambishaji kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu. Matokeo yake yanaungwa mkono na yale ya Egara, (2016) aliyefafanua kuwa uhusiano kati ya yambwa na mofimu wakilisho yambwa hulingana na uhusiano wa kisabiki na anafora. Aidha kwa mujibu wa Kiyinikibi, 2021 na Namugala, (2014), tofauti iliyojitokeza baina ya upatanishi wa Luganda na Kiswahili sanifu ni ule wa nafasi ya utokeaji wa vipatanishi yambwa na tofauti za maumbo ya mofimu ya upatanishi wa yambwa iliyotokana na maumbo tofauti baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Matumizi haya yalidhibitishwa na Riedel (2009) anayedai kuwa wakilisho yambwa

zote katika Kibantu ni za madhumuni ya upatanisho wa kisarufi. Kanuni za matumizi ya yambwa hizi ni kuwa mofimu hizo hutangulia kitenzi. Aidha, mofimu hizi huchukua nafasi karibu na mzizi wa kitenzi. Hali hii inadhihirishwa na Egara (2016) anayefafanua kuwa hatua ya kubainisha kategoria za maneno ina umuhimu katika utafiti wa mofosintaksia ya yambwa kwa sababu yambwa hubainishwa kulingana na kategoria yake ya kisarufi. Aidha, yambwa ni kijenzi cha kishazi kinachowakilishwa kwa kirai nomino au kirai bainishi na dhima yake hutawaliwa na kiarifu Uwiano na tofauti hizi zilidhirisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia, kila lugha ilionyesha upekee wake katika matumizi ya kanuni kudhihirisha kuwa, ingawa lugha hizi ni za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zenye kudhihirisha upekee wa sifa za kimofosintaksia.

5.1.1.5 Athari ya kimofosintaksia ya Kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji

Kanuni za kifonolojia ni kanuni zinazohusika na matamshi ya mofimu zinazojenga maneno (Chomi, 2003, Habwe & Karanja, 2004). Kanuni hizi huhusika zaidi na mabadiliko ya matamshi ya mofimu kutokana na mkabiliano wa mofimu. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilitambulika kuwa lugha ya Kiswahili hudondosha baadhi ya viambishi ngeli wakati wa kuandika nomino katika ngeli ya kwanza na tatu umoja yenye alomofu, [M, Mu na Mw]. Kwa mujibu wa kanuni hii, irabu [u] ya kiambishi ngeli [mu] hudondoshwa katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti halisi kama [t, r, p] na kadhalika. Mabadiliko haya yanatokana na kanuni ya udondoshaji inayoshikilia kuwa: irabu ya kiambishi [mu] hudondoshwa ikifuatiwa na konsonanti halisi kama ilivyo katika data Na.(5.12) ya data kutokana na Mukuthuria, (2004), Chomi, (2003), Otiende, (2013) na Ontieri, (2016) kuhusu athari za kifonolojia katika mofolojia na sintaksia ya maneno ya Kiswahili, yalidhihirisha uwiano na tofauti baina ya Luganda na Kiswahili sanifu (5.12):

| <i>Umoja</i> | | <i>Wingi</i> |
|-------------------|------------------|------------------|
| <i>Mu-toto</i> | <i>M-toto</i> | <i>Watoto</i> |
| <i>Mu-sichana</i> | <i>M-sichana</i> | <i>Wasichana</i> |
| <i>Mu-vulana</i> | <i>M-vulana</i> | <i>Wavulana</i> |
| <i>Mu-ti</i> | <i>M-ti</i> | <i>Miti</i> |
| <i>Mu-kate</i> | <i>M-kate</i> | <i>Mikate</i> |

Asili: Data kutokana na Mukuthuria, (2004;120) na Ontieri, (2016:8)

Kiambishi awali [mu] ni umbo la ndani la kimofolojia la ngeli ya kwanza na tatu. Umbo hili hutumika katika uainishaji wa ngeli nomino kimofolojia. Hata hivyo wakati wa mazungumzo na maandishi, umbo hili huathirika na sauti ya konsonanti inayoifuata na kujenga umbo la nje

la [m] ambalo hutumika katika kuandika viambishi ngeli vya nomino ya ngeli ya kwanza na tatu. Mabadiliko ya maumbo haya yanatokana na kanuni ya utawala na ufungami inayodhihirisha mahusiano ya miundo ya nje, ndani, fonetiki na maumbo mantiki. Kwa mujibu wa Chomsky, (1981) na Okumu, (2006), muundo wa nje unatokana na muundo wa ndani huku umbo mantiki ukitokana na muundo wa nje kupitia ugeuzaji mmoja.

Utafiti huu uligundua kuwiana na kutofautiana katika matumizi ya kanuni hii. Kwanza kabisa, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili hupata na athari za mabadiliko ya kifonolojia ya fonimu katika matumizi. Hata hivyo, michakato yake licha kuwa huenda ikawa na mwingiliano baina ya lugha hizi mbili, Tofauti inayojitokeza kati ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa kanuni hii ya udondoshaji wa irabu katika ngeli ya kwanza na tatu huwa haifanyi kazi katika Luganda. Aidha, katika Luganda, viambishi ngeli vyake huweza kuongezwa vibainishi vya ngeli nyuma ya viambishi ngeli na maumbo yake hubakia jinsi yalivyo katika matamshi na maandishi kama ilivyo katika data Na. (5.13) kutokana na Katamba, (1993) na na Baertlein & Ssekitto, (2014) na Mgullu, (1999) (5.13):

Uainishaji wa vibainishi

O-mu-ntu

O-mu-wala

U-mu-lenzi

O-mu-ti

O-mu-kati

Uainishaji bila vibainishi

mu-ntu

Mu-wala

Mu-lenzi

Mu-ti

Mu-kati

Asili: Katamba, Leah na Ssehuya (2015: 13-15) Kim, B. M., na Lee, H. A. (2019:1863)

Kwa mujibu wa mifano hii, ni wazi kuwa mabadiliko ya kifonolojia ya sauti ya viambishi ngeli vya kimofolojia vya ngeli ya kwanza na tatu kwa umoja na wingi havijaathirika na mfuatano wa konsonanti na hivyo kubakiza sifa zake katika neno. Hali hii inadhihirisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja zinazohusiana katika matumizi ya kanuni za kimofosintaksia, kila lugha hudhihirisha upekee wake ambao usipozingatiwa katika matumizi, huweza kupotosha usanifu baina yake. Matokeo haya yanafanana na matokeo ya utafiti wa Otiende (keshatajwa) ambaye alibainisha athari za kimofonolojia ya Ekegusii katika ngeli za Kiswahili na ya utafiti wa Mukuthuria, (2004) kuhusu kuathiriana kwa Kimeru na Kiswahili sanifu. Aidha, licha ya tafiti hizo kushadidia athari za L1 katika L2, utafiti huu ulichanganua kanuni ambayo ilisababisha athari za matumizi baina ya Luganda na Kiswahili na kutambua kuwa kanuni hii huwiana na kutofautiana katika matumizi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu licha ya kuwa lugha zote ni za nasaba moja.

5.1.1.6 Kanuni ya kisarufi ya uwakilishi dhima na matumizi ya vibainishi na viambishi

Kanuni ya uwakilishi dhima na kanuni ya kisarufi ya vibainishi na viambishi ni kanuni mbili ambazo hushikilia kuwa; viambajengo huwa katika sehemu tofauti za neno na katika muktadha wa utungo na vinaunganishwa na sheria fulani ambazo husababisha umilikifu na uunganishaji wa viambajengo hivyo kuwakilisha dhima ya idadi na jinsi ya kisarufi ya umoja na wingi kimofosintaksia (Ambuyo 2007; Baertlein & Ssekitto 2014; Egara 2016; Chomsky 2000;2001; Philipo 2017). Kwa mujibu wa kanuni hii, kimuundo matumizi ya vibainishi na viambishi nomino katika utungo lazima vibebe dhima za kisarufi za nomino katika utungo kimofosintaksia. Kwa mujibu wa kanuni hii, vibainishi na viambishi ngeli vinapotumika, lazima maumbo yake yaonyeshe seti za kisarufi (dhima) za idadi, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira, na jinsi ya nomino katika utungo. Matumizi haya lazima yazingatie maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya maumbo kamili ya ngeli ambamo nomino kuu huainishwa. Kibainishi kisipotumika, neno au nomino hiyo huweza kujitosheleza kama sentensi sahili yenye kiima na yambwa (Baertlein & Ssekitto, 2014). Kulingana na Mulei, Ambuyo & Amukowa (2021), kila lugha huainisha ngeli zake kutumia maumbo wakilishi ya dhima za kisarufi. Maumbo haya yakikiukwa, dhima ya uambishaji wa nomino husika hupotoka na hivyo usanifu wa Lugha pia kupotoka kwa sababu dhima ya kueleza seti za kisarufi za matumizi ya vibainishi na viambishi husika katika kategoria za kisarufi katika tungo zimekiukwa. Kanuni hii huongozwa na kanuni ya viambajengo vya nomino katika utungo na kanuni ya dhima ya viambajengo katika tungo. Matumizi ya nomino lazima yazingatie mofolojia na sintaksia ya vibainishi na viambishi ngeli ambamo nomino hiyo huainishwa kama katika data (5.14) ya data ya vibainishi na viambishi ngeli baina ya Luganda na Kiswahili kutokana na Baertlein & Ssekitto, (2014), Mulei na wenzake (2021): (5.14):

- | | | |
|---|--|--|
| a) <i>Omulenzi</i> Mvulana | <i>abalanzi</i> wavulana | [idadi ya umoja na wingi ngeli ya 1 na 2] |
| b) <i>Akalenzi</i> Kavulana | <i>obulenzi</i> buvulana | [dhima ya udogo/udunishaji] [kudhalalisha] |
| c) <i>Mulenzi</i> [ni mvulana] | <i>omulenzi</i> [mvulana] | [udhihirishaji wa nomino moja kwa moja] |
| d) <i>Taata afunye omulenzi omunenne.</i> Baba amepata mvulana mnene | <i>Bataata bafunye abalanzi abanene.</i> | [jinsi ya kisarufi] Kina baba wamepata wavulana wanene |
| e) <i>Ng'eenda kulia</i> Ninaandaa kula chakula | <i>emmere.</i> | <i>Tugenda kulya emere.</i> [kuwakilisha Nafsi] Tunaenda kula chakula |

Asili: Kutokana na Namugala, (2014) na Baertlein & Ssekitto, (2014)

Mifano (a) inadhihirisha seti ya kisarufi ya nomino kwa kuwakilisha umoja na wingi wa nomino kimofosintaksia. Uwakilishi huu umetokana na vibainishi vya ngeli ya 1 na 2 [o-mu na -a-ba]. Matumizi ya vibainishi katika nomino za (b) zimedhihirisha dhima ya vibainishi ya udunishaji wa nomino kwa umoja na wingi kimofosintaksia kama inavyoelezwa na Namugala (2014). Nomino (c) ambayo haikuwekewa kibainishi ni nomino tata ambayo siyo dhahiri na kwa sababu hiyo imejitosheleza kama sentensi sahili [Ni mvulalna] ila nomino hii inapowekewa kibainishi inadhihirisha moja kwa moja nomino inayotajwa kwa umoja au wingi.

Data (d) inadhihirisha kanuni ya kimofosintaksia ya matumizi ya vibainishi ambavyo vinajenga upatanishi wa kisarufi wa nomino inayotajwa katika tungo na maneno yanayojenga utungo. Maneno haya yametumika kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine [kitenzi na kivumishi) kimofosintaksia. Maneno haya ni [a-funy-e] na [o-mu-nene]. Data (e) kinadhihirisha uwakilishi wa nafsi na pia upatanishi wa kisarufi wa matumizi ya vibainishi nafsi vya umoja na wingi [N na Tu]. Kwa utaratibu au mpangilio, vibainishi vimewekwa nyuma ya viambishi ngeli vikibeba seti za kisarufi katika nomino na utungo. Aidha, maana ya vibainishi imetumika kimuktadha hasa katika mpangilio wa sentensi kwa njia ya urejeleo nyuma wa kutaja nomino kama vile [o-mu-lenzi o-mu-nene]. Mwisho imedhihirika kuwa nomino na maneno mengine ya kategoria za kisarufi lazima iambishwe vibainishi hasa inapotumika ikiwana dhima ya kubeba seti za kisarufi za lugha husika. Matumizi haya yanadhihirisha uhusiano milikifu wa vibainishi na viambishi ngeli pamoja na uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo hasa katika Luganda.

Kwa kuzingatia nafasi ya utokeaji na uambishaji wa vibainishi na viambishi ngeli, ilibainika kuwa kanuni ya kidarajia ya viambajengo vinavyojenga neno na virai au vishazi ilijitokeza baina ya Luganda na Kiswahili. Kwa mujibu wa kanuni hii ambayo ilijitokeza katika matumizi ya vibainishi na viambishi, Luganda ilidhihirisha kuambisha viambishi vibainishi kabla ya viambishi ngeli vya nomino ambavyo hupachikwa kwenye mzizi au shina la neno. Kimofosintaksia, viambishi vibainishi katika Luganda sanifu hutumika kwa njia ya kubadilishana nafasi kuwakilisha dhima ya ngeli na idadi ya umoja au wingi kimofolojia na kisintaksia. Kwa mujibu wa kanuni hii, vibainishi nomino katika Luganda hutumika kutegemea maumbo ya ngeli nomino husika ambapo kila kibainishi hurejelea maana dhahiri na isiyodhahiri kutegemea muktadha au mantiki za matumizi.

Pia, viambishi vibainishi vya ngeli hutumika kwa njia ya mbadilishano ambapo kibainishi kimoja chaweza kutumika kubainisha umoja katika ngeli fulani na vilevile kibainishi hicho hicho kikatumika katika ngeli nyingine kubainisha wingi wa nomino katika ngeli nyingine. Kanuni hizi huongozwa na kanuni ya viambajengo vya nomino katika utungo. Kanuni ambayo hushikilia kuwa viambajengo huwa katika sehemu tofauti za neno na katika muktadha wa utungo na vinaunganishwa na sheria fulani ambazo husababisha umilikifu na uunganishaji wa viambajengo hivyo kuwakilisha idadi na jinsi ya kisarufi ya umoja na wingi kimofosintaksia. Katika Luganda, Vibainishi hutumika katika ngeli nomino tofauti na katika utungo kwa njia ya mbadilishano kuwakilisha seti za kisarufi za kuwakilisha, ngeli, idadi ya umoja na wingi, dhima, upatanishi wa kisarufi na jinsi ya kisarufi. Kwa kuzingatia nafasi ya utokeaji wa vibainishi, katika Luganda vibainishi vimewekwa kabla ya kiambishi ngeli kuwakilisha dhima moja ya kuwakilisha ngeli na idadi ya nomino kwa wingi na umoja.

Uchanganuzi wa data za Baertlein & Ssekitto, (2014), Mulei Ambuyo & Amukowa (2021) na Philipo (2017) kuhusu kanuni hizi, ulibaini Luganda sanifu kutumia vibainishi na viambishi ngeli kubainisha dhima za ngeli, idadi ya umoja na wingi pamoja na upatanishi wa kisarufi wa nomino kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa tungo. Ilibainika pia kuwa, matumizi ya vibainishi na viambishi ngeli bila kuzingatia mofolojia na sintaksia katika utungo, huathiri dhima za idadi, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira, na jinsi. Kwa kuzingatia mihimili ya ubia na upatanifu ya nadharia ya umilikifu na unganifu, utafiti huu ulibaini kuwa, ingawa nomino ndiyo neno kuu inayotumika kubainisha viambishi ngeli vinavyopachikwa kwenye maneno ya kategoria za kisarufi kama vivumishi, vitenzi, viwakilishi nafsi, vikanushi na kadhalika kuwakilisha uhusiano wa kimofosintaksia wa nomino na viambajengo vya sentensi (Rugemalira 2007; Radford, 2004).

Kiswahili hutumia viambishi vya ngeli katika kuwakilisha uhusiano huo wa kimofosintaksia tofauti na Luganda inayotumia vyote viwili. Hali hii inadhibitishwa na Lusekelo (2017) anayeeleza kuwa, Kiswahili ni lugha ambayo hutumia viambishi ngeli badala ya vibainishi ngeli kama ilivyo katika Luganda. Matumizi ya vibainishi ngeli katika lugha ya Kiswahili sanifu ni kapa au dhahania na hukuzwa na kanuni ya mahusiano ya kiutawala ya neno kuu ambayo hushikilia kuwa sifa za kisarufi za maneno yanayotawaliwa lazima yawe karibu na neno kuu linaloyatawala ili kupokea sifa za kisarufi za kimofosintaksia katika tungo. Hii ina maana kuwa, nomino katika Kiswahili huchukua vibainishi kimkutadha na hujitokeza katika mawasiliano ya mmilisi wa lugha bila kudhihirisha alama ya kiodhografia kuwakilisha maana

dhahiri na isiyodhahiri ya nomino. Katika Kiswahili, nomino zisizoambikwa viambishi ngeli huweza kubainishwa na viambishi kapa kutegemea muktadha wa matumizi ya nomino hiyo kama inavyojitokeza katika mifano (4.2, Uk. 73, 4.3, Uk. 79 na 4.4, Uk. 83) ya data zinazodhihirisha dhima za kisarufi za idadi ya umoja na wingi kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu.

Matokeo haya yanashadidiwa na Egara, (2016) na Ambuyo (2007) ambao katika maelezo yao viambishi vya kimofolojia ambavyo huwekwa mwanzoni mwa nomino huathiri utokeaji wa viambishi vya kisintaksia katika tungo vikishughulikia hasa upatanisho wa kisarufi wa vitenzi na maneno mengine katika tungo. Maelezo haya yanaungwa mkono na Richard Nordquist, (June, 2020) anayeeleza juu ya upatanisho wa kisarufi wa kutambua *umoja au wingi wa kitenzi au maneno mengine katika utungo hutegemea nomino kama neno kuu kuonyesha dhima ya uhusiano wa maneno na maana ya tungo. wakiunga mkono.* Lusekelo, (2013), Ambuyo, (2007) na Contini-Morava, (2000) nao wanaeleza kuwa katika upatanishi wa neno kuu, viambishi vya nomino na viambishi vipatanishi vya kiima hupatana kisintaksia na vipashio vya kisarufi vya kisintaksia vya ngeli, viwakilishi nafsi, jinsi ya kisarufi na idadi ya umoja na wingi kubeba dhima ya kimofosintaksia.

Tofauti na ufafanuzi wa wataalamu hawa utafiti huu uligundua kuwa kanuni hizi ni mojawapo wa kanuni ambazo hutumika katika Luganda na Kiswahili sanifu kuchanganua sifa za kisintaksia za vipashio vinavyojenga tungo. Tofauti inayojitokeza kati ya Luganda na Kiswahili sanifu ni ya uwakilishi dhima wa kimaumbo. Luganda ilidhihirisha kutumia vibainishi [a-, o- na e-] kukumusha nomino na inapoondoa vibainishi hivi katika kivumishi, huwa inafanya kazi ya uarifu au kiangama, hali ambayo ni tofauti na Kiswahili ambacho viambishi vyake vinavyoambikwa vikiondolewa mzizi unasimama bila kufanya kazi ya kisarufi, kukumusha na kuarifu juu ya nomino (Abudonia, 2014). Mathalan, Utafiti huu ulitambua kuwa vibainishi vyote hivi vilitumika kutegemea ngeli nomino na katika Kiswahili viliwakilishwa au vilijitokeza kidhahania vikisitiriwa katika viambishi ngeli vya nomino tajwa. Aidha, kwa mujibu wa utafiti huu, vibainishi vya Luganda vilitofautiana na vibainishi vya Kiswahili kimofolojia. Data (5.15) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za vibainishi na viambishi ngeli kuwakilisha dhima katika Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na matokeo ya utafiti huu (2021):

Luganda

Kiswahili sanifu

a) *A-ba-yizi ba-no bazannya o-mu-piira Wanafunzi hawa wanacheza mpira*

b) *O-mu-ddusi o-mu afunye zaabu Mwanariadha mmoja ameshinda dhahabu*

Asili: Kutokana na matokeo ya utafiti huu (2021)

Kwa mujibu wa sentensi hizi, sentensi za kwanza zinadhihirisha vibainishi vya ngeli ambapo Kiswahili imetumia [wa] kama kiambishi kibainishi cha ngeli ya pili katika nomino [wanafunzi] huku Luganda ikiwa imetumia kibainishi dhahiri [a-] cha ngeli na kiambishi ngeli ya pili [ba]. Katika data (b), Kiswahili kimetumia [mw-] kama kiambishi cha ngeli ya nomino ya kwanza, huku Luganda ikitumia kibainishi pamoja na kiambishi ngeli [o] na [mu]. Kimuundo, vibainishi hivi hutokea mwanzoni, na kufuatwa na kiambishi ngeli katika Luganda. Kwa kuzingatia utaratibu huo, ni wazi kuwa vibainishi vinavyowakilisha ngeli katika Kiswahili ni dhahania. Havijitokezi moja kwa moja bali kiambishi ngeli ndicho kinachobeba dhima hiyo ya kibainishi cha Kiswahili kama ilivyo katika Luganda.

5.1.1.7 Kanuni ya ukuu na darajia za vijenzi vya maumbo ya maneno na utokeaji wake

Neno kuu huwakilishwa na elementi za kategoria za vijenzi vya neno lenyewe. Vipashio hivyo na muundo wake huibuka kisintaksia. Kwa mfano vibainishi na viambishi awali vya neno vinavyopachikwa kwenye mzizi wa neno katika Luganda na Kiswahili ndivyo vinavyotoa taarifa za kisarufi za neno kuu kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi na vipatanishi vya kisintaksia vya neno vya neno kuu (VanPatten & Williams, (2015) na Lieber, 1981 na Droste 1989).

Kwa mujibu wa maelezo haya, sifa za neno kuu ni sifa za kimofosintaksia zinazotambulisha aina (kategoria) za neno au neno kuu katika utungo wa sentensi, ngeli ambamo neno hilo hujitokeza kutokana na vijenzi vya neno husika. Kwa mfano; [Mtu] ni neno lenye vijenzi viwili, [m] kiambishi awali cha ngeli ya kwanza ya idadi ya kwanza yenye sifa za kisarufi za umoja na [tu] ni mzizi ambapo wingi wake unatokana na elementi ya kiambishi awali [M] ambacho hubadilika na kuwa [wa]. Kiambishi ngeli hiki huwakilisha sifa za idadi na kisintaksia za wingi wa neno kuu ambalo ni nomino. Mofu hizi za nomino ni elementi zinazotambulisha kategoria ya neno kutokana na kuunganisha vijenzi vya viambishi na mzizi katika mpangilio maalumu. Kwa hivyo, katika ujenzi wa maumbo ya nomino za Kiswahili na Luganda ilitambulika kuwa vibainishi na viambishi awali hutokea mwanzoni vikifuatwa na kategoria za kisarufi za matumizi ya neno na mzizi kuwakilisha sifa za kimofosintaksia za

neni kuu pamoja na kudhihirisha neno kuu katika utungo (Van Der Wal & Namyalo, 2016; Hyman & Katamba, 1993; Mgullu, 1999).

Matokeo ya data ya mapitio ya maandishi ulibaini uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya ukuu na darajia za vijenzi vya maumbo ya maneno na utokeaji wake kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Tofauti ni kuwa Luganda hutangulia vibanishi kisintaksia, kufuatwa na viambishi ngeli vya kategoria ya neno, sifa zinginezo za kisarufi kama vile njeo kufuata, kisha mzizi wa neno kuu na kimalizio ambacho hutoa sifa fulani za kisarufi za kategoria ya neno. Kiswahili hutanguliwa na viambishi ngeli vya kategoria ya neno kuwakilisha idadi na ngeli ikifuatwa na sifa nyinginezo za kisarufi kama ilivyo katika Luganda, kisha mzizi na kimalizio (Namugala, 2014; Van Der Wal & Namyalo, 2016; Mgullu, 199; Habwe & Karanja, 2007). Hali hii inadhihirisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zenye mifumo ya kipekee inayotofautiana na lugha nyinginezo ambamo lugha hiyo huainishwa. Aidha uhamishaji wa kanuni za Luganda katika Kiswahili huenda ukaathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Data (5.16) inaonyesha uwiano na tofauti za matumia ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

- a) *O-mu-ntu* *a-ba-ntu (Luganda)* M-tu wa-tu (Kiswahili)
 [Kb-Kng1-Mz *Kb-Kng2-Mz (Lug)* *Kng1-Mz* *Kng2-Mz](Kis)*
- b) *Ya-* *zany-a* *(Luganda)*
 [Kb+Njeo (wakati uliopita)+ Kng1+ Nafsi3-Mz-Kiambishi tamati cha kitenzi]
- c) *Ba-a-zany-a (Luganda)*
 [Kng2 -Kb2+Njeo (wakati uliopita)+ Kng1+ Nafsi3-Mz-Kiambishi tamati cha kitenzi]
- d) *a-li-chez-a* (Kiswahili)
 [Kiwakilishi nafsi1+ Kng1- Njeo(wakati uliopita)-Mz- kiambishi tamati cha kitenzi]
- e) *Wa-li-chez-a (Kiswahili)*
 [Kiwakilishi nafsi1+ Kng2- Njeo(wakati uliopita)-Mz- kiambishi tamati cha kitenzi]

Kwa mujibu wa kirai cha (b), sifa za kisarufi za kishazi zimejitokeza katika muktadha au vijenzi vya kishazi ‘*alicheza* na *walicheza*’ kuwakilisha sifa za kisarufi za idadi, kuwakilisha kirai kitenzi kama neno kuu (*chez-a*), uwakilishi wa nafsi [a], njeo ya wakati uliopita [-li-], mzizi wa kitenzi [*chez-*] na kiambishi cha kitenzi cha Kibantu [-a]. Sifa hizo hizo zimetumika katika Luganda hata hivyo sifa za kisarufi za kiambishi [ya] zikawa na sifa za kisarufi zaidi tofauti na za Kiswahili ambapo [ya] imewakilisha nafsi, njeo ya wakati uliopita na idadi ya kisarufi na ngeli ya kwanza. Katika wingi mpangilio unabadilika pale ambapo kiambishi

ngeli cha pili kinatangulia, kikifuatwa na njeo inayowakilishwa na [-a] mabadiliko ya kimaumbo yanayotokana na mifanyiko ya kifonolojia za Luganda. sifa hizi zote zimejitokeza kimofosintaksia na kutofautiana kiujenzi kutokana na sifa za kimofosintaksia za Lugha husika kiutaratibu hasa kuwakilisha neno kuu katika maumbo ya maneno husika katika utungo.

5.1.2 Uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya aina za vivumishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu

Mbwillow (2017), anaeleza kuwa kivumishi ni neno linaloeleza zaidi kuhusu nomino, kiwakilishi na au kivumishi kingine katika tungo. Fasili hii inaonyesha kuwa vivumishi ni kipashio cha kimofosintaksia ambacho hutumika pamoja na nomino kama viambajengo vya virai nomino. Vivumishi ni mojawapo wa vipashio vya kimofosintaksia katika Luganda na Kiswahili. Ni maneno ya kimofosintaksia yanayotoa maelezo zaidi kuhusu nomino kama neno kuu katika tungo virai nomino, vishazi nomino na vishazi vivumishi (vishazi virejeshi na vishazi vihusishi). Vivumishi vya Luganda na Kiswahili hutofautiana kimaumbo na kimuundo hasa katika nafasi ya utokeaji na dhima. Matokeo ya uchanganuzi wa vitabu vya kisarufi na upekuzi wa maandishi mbalimbali ulidhihirisha kuwepo kwa uwiano na tofauti katika kanuni za matumizi ya aina mbalimbali ya vivumishi kama inavyojadiliwa ifuatavyo.

5.1.2.1 Vivumishi vimilikishi

Mgullu (1999) anaeleza kuwa vivumishi vimilikishi ni aina ya vivumishi ambavyo hueleza jinsi nomino inavyomilikiwa. Okumu (2006) anafafanua kuwa vivumishi vinavyoonyesha dhana ya kuwa na au kumiliki. Vivumishi vimilikishi ni vivumishi vinavyoelezea juu ya mmilikaji wa vitu, mali, mahali, viumbe na hata binadamu. Kanuni kadhaa zimedhihirika katika matumizi ya vimilikishi katika Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.2.1.1 Kanuni ya mofolojia ya uambishaji viambishi kwenye vivumishi

Kanuni ya uambishaji hudai kuwa: Uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi (uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu. Kanuni hii ni ya jumla ambayo huzingatiwa katika matumizi ya vivumishi vimilikishi. Kwa mujibu wa mihimili ya Ubia na Upatanishi wa nadharia ya Umilikifu na Unganifu, uchanganuzi wa data za Mbwillow, (2017), Lusekelo, (2017), Abodunia, (2017) na Namugala, (2014) na Kiyinikibi, (2021) ulibaini Luganda na Kiswahili sanifu kutumia kanuni ya uambishaji wa viambishi ngeli ambavyo hubeba sifa za

kimofosintaksia kwenye mizizi ya vivumishi vimilikishi kutegemea viambishi awali vya nomino. Muundo wa vivumishi vya Luganda na Kiswahili huwakilishwa na viambishi awali vya ngeli (jinsia ya Kisarufi) na idadi ya umoja na wingi pamoja na mizizi inayobeba sifa za kileksika za vimilikishi sita kwa umoja na wingi. Mizizi hii hutumika kulingana na nafsi tatu kwa umoja na wingi kama ilivyoielezwa na Kiyinikibi, (2021) na Mbwillow, (2017) na Kisakwah (2014). Hata hivyo, maumbo ya mizizi ya vimilikishi hutofautiana na maumbo ya viambishi ngeli vinavyopachikwa kuwiana na kutofautiana kutokana na ngeli ambamo nomino huainishwa kutegemea lugha husika. Jedwali (4.8, Uk 92; 4.9, Uk, 95 na 4.10, Uk. 98) kutokana na Rose (2009) na Mgullu (1999) inadhihirisha uwiano na tofauti za mizizi ya kileksika na viambishi vya vimilikishi vya Luganda na Kiswahili sanifu katika sura ya nne. Kwa mujibu wa majedwali haya, kanuni ya uambishaji vivumishi katika Luganda na Kiswahili sanifu hudai kuwa vivumishi vimilikishi huambishwa kiambishi patanishi cha msingi awali cha ngeli nomino ya neno kuu katika virai nomino kutegemea nafsi ya mmilikaji wa nomino inayotajwa katika mazungumzo au maandishi (kiyinikibi, 2021, Rose (2009) na Mgullu, 1999). Ukiukaji wa kuzingatia nafsi, na viambishi awali vya ngeli vya nomino inayohusika hupotosha usanifu wa tungo kwa kuwa sarufi na ujumbe lengwa wa kuwasilishwa utakuwa umepotoshwa.

Uchanganuzi wa matokeo ya uchanganuzi wa Kiyinikibi, (2021), Abudonia, (2014), Rose (2009) na Mgullu, (1999), utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za Kibantu ambazo hutumia vimilikishi kuzingatia nafsi tatu, kwa umoja na wingi. Kimuundo vimilikishi katika lugha hizi vimeundwa kwa viambishi awali vya nomino vinavyobeba maana ya kileksika na kisarufi na mizizi yenye kubeba maana ya kileksika iliyositiri maana au maudhui ya umilikaji. Vimilikishi hivi hubadilika kimaumbo katika tungo kutokana na maumbo tofauti ya viambishi awali vya ngeli nomino inayokumushwa na nafsi ya umilikaji. Viambishi awali vya ngeli nomino vinavyoambishwa kwenye mizizi ya vivumishi ni vya upatanishi ambavyo ni tofauti na vivumishi awali vya kimofolojia vinavyoweza kuambishwa kwenye vivumishi vingine kama vile vya sifa na kategoria zingine za kisarufi kama vitenzi kama katika mifano ya data Jedwali (4.8, Uk. 92; 4.9, Uk. 95 na 4.10, Uk. 98) kutokana na kutokana na Rose (2009) na Mgullu (1999) inadhihirisha uwiano na tofauti za viambishi vipatanishi baina ya luganda na Kiswahili sanifu.

Tofauti ya kikanuni inayojitokeza kati ya Luganda na Kiswahili ni mizizi ambayo kimaumbo ni tofauti na Kiswahili sanifu, viambishi ngeli vinavyopachikwa kwenye mizizi hutegemea

mpangilio na uwakilishaji wa maumbo ya konsonanti na irabu iliyo tofauti na Kiswahili sanifu. Katika uambishaji, Luganda hutumia viambishi viwili yaani vibainishi ngeli ambavyo ni vokali [a,o na e] huku Kiswahili sanifu kikitumia kiambishi awali cha ngeli kuwakilisha idadi ya umoja na wingi. Hali hii ilidhihirisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja zenye kanuni za kuzingatiwa, lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye upekee wa matumizi ya kanuni za kimofosintaksia katika matumizi zinazotumika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya nomino na maneno mengine katika tungo kama katika mifano ya data Jedwali (4.8, Uk. 92; 4.9, Uk. 95 na 4.10, Uk. 98) kutokana na Rose (2009) na Mgullu (1999) inadhihirisha uwiano na tofauti za mizizi ya kileksika ya vimilikishi vya Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.2.1.2 Kanuni ya kifonolojia

Kanuni hii inashikilia kuwa: Kiambishi kipatanishi cha msingi kikianza na ama konsonanti au irabu, huweza kusabababisha mabadiliko au kuathiri fonimu ambayo inapachikwa kwenye mizizi kama kiambishi kipatanishi cha msingi (KPM). Kanuni hii imetokana na maelezo ya kanuni ya kimofonolojia (Chomi 2003; Mgullu, 1999). Kanuni hii imewasilishwa katika mfumo ufuatao wa data Na. (5.17) kama taratibu zinazosababisha mabadiliko ya fonimu ya KPM kutokana na (Chomi 2003; Katamba, 2003):

Kanuni ya kimofolojia ya fonimu za KPM ya viambishi awali katika vivumishi vimilikishi

| | | | | |
|----------|---|----------------|--------|----------|
| a | + | e | —————→ | e |
| i | + | e | —————→ | e |
| u | + | [irabu] | —————→ | w |
| i | + | [irabu] | —————→ | y |
| u | + | a | —————→ | a |
| u | + | o | —————→ | o |
| a | + | a | —————→ | a |
| a | + | u | —————→ | u |
| i | + | a | —————→ | a |
| a | + | i | —————→ | e |
| i | + | i | —————→ | i |
| i | + | u | —————→ | u |
| a | + | o | —————→ | o |

i + o → o
 n + l → nd [nazali kuathiri konsonanti anadamizi]

K → i → a → ch

Nazali + konsonanti → fonimu nazali [kanuni ya unazali kutokan na konsonanti]

[n, m, b] + konsonanti fonimu nazali

Asili: Data kutokana na Chomi (2003) na Katamba, (2003)

Data za mapitio ya maandishi ya Katamba, (2003), Chomi, (200) Hyman & Katamba, (2012) kuhusiana na kanuni ya kifonolojia ilidhihirisha Ubia na Upatanifu wa matumizi ya kanuni hii katika Luganda na Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi. Uchanganuzi ulidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya vimilikishi. Uambishaji wa vivumishi vimilikishi kwa viambishi vipatanishi vya msingi [KPM] baina ya Luganda na Kiswahili sanifu husababisha mabadiliko ya viambishi msingi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vimilikishi. Uchanganuzi wa maandishi ulitambua kuwa kanuni za kifonolojia zilijitokeza katika viambishi patanishi vya msingi katika mianza ya KPM kuanza na ama konsonanti au irabu. Kanuni hizi husababisha uyeyushaji wa fonimu, udondoshaji wa fonimu, muunganiko wa sauti, uundaji wa fonimu mpya na kadhalika kama inavyojitokeza katika data (5.18) kutokana na Chomi, (2003) na Hyman & Katamba (2012):

- a) *Muyizi [wa] –[ange] anasoma bulungi. Abayizi [ba]- [affe] basoma bulungi.*
 Mwanafunzi [wa]-angu anasoma vizuri. Wanafunzi [wa]-[etu] wanasoma vizuri.
- b) *Omufumbi wo afumba emmere. Abafumbi [ba]-[ammwe] bafumba emmere.*
 Mpishi [wa]-[ako] anapika chakula. Wapishi [wa]-enu] wanapika chakula.
- c) *Omuzimbi we asaba omusennyu. Abazimbi [ba]-[aabwe] basaba omusennyu.*
 Fundi wa]-[ake] anaomba changarawe. Mafundi [wa]-[ao] wanaomba changarawe.

Asili: Data za matokeo kutokana na Chomi, (2003) na Hyman & Katamba (2012).

Mifano (5.18) ya data hizi zilidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya fonolojia ya vivumishi vimilikishi vya Luganda na Kiswahili katika nafsi ya kwanza hadi tatu katika ngeli ya kwanza na pili. Kivumishi cha kwanza kimedhihirisha kanuni ya udondoshaji wa irabu moja [-a-] na badala ya kuandika au kutamka {waange na waangu} na kiwakilishi cha vivumishi vimilikishi katika nafsi ya kwanza imetumia {wange na wangu} hii inatokana na kanuni hii ya udondoshaji fonimu moja kati ya {a na a} imedondoshwa na kubakisha moja [a] kwa umoja. Kwa kurejelea mihimili ya Ubia na Upatanishi, Kanuni ya fonolojia ya wingi katika nafsi ya kwanza umoja, ngeli ya pili inatofautiana kati ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Sentensi ya (a) kwa wingi inadhihirisha kanuni ya udondoshaji fonimu kama ilivyo katika sentensi ya nafsi ya kwanza umoja [a+a] na kubaki na [a]. Katika Kiswahili, fonimu e + a huungana na kujenga fonimu [e]. Kanuni hii ni kanuni ya kifonolojia ya muungano wa fonimu [a+e], [e] (Chomi, 2003; Katamba 2003). Jedwali (5.1) linadhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na Chomi, (2003), Hyman & Katamba (2012), Leah & Sseguya, 2014. Sababu za udododoshaji na mabadiliko ya kimofofolojia ni ya kiisimu za lugha husika zinazorahisisha matamshi.

Jedwali 5.1: Kanuni ambazo zimejitokeza katika sentensi (a-c)

| Umoja | Kanuni | Wingi | Kanuni |
|-------------------------|---------------------------|--------------------------|--|
| a)[wa]-[ange]- Wange | udondoshaji fonimu – a | [ba]- [affe]- baffe | Udondoshaji fonimu-a |
| [wa]-[angu]- wangu | udondoshaji fonimu – a | [wa]-[etu]-wetu | muungano wa fonimu [a na e] na kupata [e] |
| b) W-o | - | [ba]-[ammwe] – bammwe | Udondoshaji fonimu-a |
| [wa]-[ako] | Udondoshaji fonimu | [wa]-enu]- wenu | muungano wa fonimu [a na e] na kupata [e] |
| c) W-e | - | [ba]-[aabwe] baabwe | Odondoshaji fonimu – a |
| wa]-[ake] | udondoshaji fonimu | [wa]-[ao] | Udondoshaji fonimu – a |

Asili: Data ya maktabani kutokana na Chomi, (2003), Hyman na Katamba


Uchanganuzi baina ya Luganda na Kiswahili ulidhihirisha tofauti ambayo ilijitokeza katika baadhi ya KPM cha vivumishi vimilikishi huweza kupata mabadiliko ya kimofofonolojia na mengine kutokubali kuathirika kutokana na mfumo wa mofolojia ya muundo wa vivumishi katika Luganda. Hata hivyo, katika Kiswahili, KPM karibu zote huathirika na kanuni ya mbalimbali za kifonolojia katika maandishi na mazungumzo kimofofonolojia kama ilivyofafanuliwa na Leah & Sseguya, (2014), Hyman & Katamba, (2012).

5.1.2.1.3 Kanuni ya umiliki na usabaki

Kanuni hii huzingatia kuwa: vifundo huunda kiambajengo kama na kama tu viambajengo hivyo vitakuwa ni jozi za vifundo vinavyomilikiwa kikamilifu na kifundo kikuu (Chomsky, 1957:1967). Uchanganuzi wa data za upekuzi wa kazi za Shabani, (2015), Kiyinikibi, (2021) ulibaini kuwa umiliki na usabaki unaojitokeza katika Luganda na Kiswahili sanifu ni ule unaotawaliwa na urejeleo nyuma wa kutegemea makundi nomino (ngeli nomino) katika sentensi kuwakilisha upatanishi wa kisarufi na kujenga kanuni ya neno kuu katika kirai nomino (KN) kupatana kisarufi na vivumishi vyake kuhusu vipengele kama vile ngeli, idadi

na nafsi kwa umoja na wingi Mchoro ufuatao unadhihirisha matumizi ya kanuni hii kwa mujibu wa utafiti huu kutokana na Shabani (2015), Abudonia, (2014) na Kiyinikibi, (2021).

Mchoro (M5.5) unaowakilisha kanuni ya umiliki na usabaki



Asili: Data kutokana na matokeo ya utafiti huu, (2021).

Tawi hili la KN linaonyesha umiliki wa kivumishi {wange} na nomino {omwana}. Kwa upande mwingine, kivumishi {wangu} husabaki nomino {mtoto} ambapo uhusiano unaojitokeza ni wa kijoji. Uhusiano huu unajitokeza katika utungo wa kimofosintaksia wa kirai nomino. Umiliki na usabaki wa nomino na kivumishi unajitokeza katika viambishi awali vya ngeli nomino vinavyobeba sifa za kimofosintaksia za ngeli, nafsi na idadi kwa umoja na wingi.

Tofauti ya matumizi ya kanuni hii ni ule uwakilishi wa viambishi ambavyo ni vipatanishi vya msingi vinavyojenga sifa za kimofosintaksia na mizizi inayoambishwa kwa mujibu wa nafsi na ngeli. Viambishi vya ngeli, nafsi na mizizi ya vivumishi hutofautiana kimaumbo kutegemea nomino inayotajwa katika kundi nomino na tofauti kama hii inaweza kuathiri usanifu wa matumizi ya Kiswahili sanifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data Na. (5.19) wa data kutokana na Kiyinikibi (2021) na Leah & Sseguya (2015) inadhihirisha uwiano wa matumizi na tofauti za kanuni hii katika Luganda na Kiswahili. (5.19)

Luganda

Kiswahili

- a) *Embuzi ya-nge erya kasooli* **Mbuzi wangu anakula mahindi**
- b) *Mu lukiiko mw-ange mw'ateeseza.* Mkutanoni **mw-angu** ambamo anashiriki
- c) *Mu lukiiko lw-ange mw'ateeseza* Mkutanoni **mw-angu** anamoshiriki
- d) *Emicungwa egiyiise gyange.* Michungwa ambayo imemwangika ni **ya-ngu**

Asili: data kutokana na Kiyinikibi (2021) na Leah & Sseguya (2015)

Mfano wa (a) unadhihirisha matumizi ya nomino moja na kimilikishi chake katika Luganda na Kiswahili, {*Embuzi ya-nge na mbuzi wa-ngu*} kimuundo tungo, data hii imezingatia

kanuni ya umiliki na usabaki bali tofauti inayojitokeza ni kuwa, licha ya kuwa ‘embuzi (mbuzi) ni nomino katika viumbe hai, Luganda imeainisha nomino hii katika ngeli ya 9 na 10 kimofolojia huku uamilifu wake ukijitokeza kisintaksia (en-zi), huku Kiswahili kikiainisha ngeli hii katika ngeli ya 1 na 2 (a-wa) kisemantiki. Uainishaji huu ukawa unajenga maumbo tofauti yanayoambishwa kwenye maneno mengine kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa neno kuu na maneno mengi kuwakilisha usabaki na umilikaji ambapo Luganda hutumia viambishi {i-zi} huku Kiswahili kikitumia {a-wa} katika umoja na wingi. Hali hii ikawa inadhihirisha kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja zinazotumia vivumishi vimilikishi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu, lugha hizi ni mbili tofauti zenye upekee wake katika matumizi ambapo uhamishaji wa maumbo wakilishi ya usabaki na umilikaji kutoka Luganda hadi Kiswahili huenda ukaathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashadidiwa na Kiyinikibi, (2021) na Philipo & Kuyenga, (2017) ambao kwa mujibu wa kanuni hii wanadhihirisha kuwa, vivumishi hutumika katika Luganda na Kiswahili sanifu kama maneno ya kuarifu zaidi juu ya nomino au vishazi nomino na vivumishi. Uhusiano huu ni wa kijozi ambapo neno kuu katika kirai nomino humiliki neno linalofuata {kimilikishi} na neno linalofuata nomino katika KN {kimilikishi} likasabaki neno kuu {nomino au kivumishi} ambalo linatangulia. Walidhihirisha uwiano wa kanuni ya umilikaji na usabaki kusetiriwa katika viambishi msingi awali vya upatanishi wa kisarufi {vyenye sifa za kimofosintaksia} kuwakilisha ngeli, idadi na nafsi kwa umoja na wingi katika Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na ufafanuzi wa awali kuwa licha ya kuwepo kwa uwiano, wa matumizi ya kanuni ya umiliki na usabaki, matumizi yake hutofautiana baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na upekee wa Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa neno kuu na maneno mengine katika tungo.

5.1.2.1.4 Kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai

Data za upekuzi wa kazi za Rijkhoff, (2002) na Abudonia, (2014) kuhusiana na kanuni hii ilibaini kuwa, kanuni ya ukuu na darajia ya **utokeaji wa vipashio katika tungo** hufafanua utaratibu wa matumizi ya maneno katika tungo virai kutegemea hadhi ya maneno husika kimofosintaksia. Kwa mujibu wa kanuni hii, mpangilio au utokeaji wa vivumishi pamoja na neno kuu katika tungo huzingatia utaratibu maalumu. Iligunduliwa kuwa vivumishi vimilikishi katika KN baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutokea baada ya nomino au

neni kuu katika tungo virai. Kanuni hii iliendelezwa na kanuni ya ubainishaji wa nafasi tokeaji wa elementi kuu katika tungo ambayo huchunguza ukuu wa elementi muhimu na nafasi ya utokeaji wake katika KN kimofosintaksia (Rijkhoff, 2002). Kanuni hii inashikilia kuwa: Nomino kuu au neno kuu katika utungo huwakilishwa au huzingirwa na vibainishi au kirejeleo nomino (kiambishi nomino), kivumishi cha nomino na uhusika milikishi (Kivumishi na uhusika wa nomino). Kanuni hii huamini kuwa: Neno kuu katika utungo huchagua kuathiri maneno mengine kutegemea mazingira ambamo nomino au neno kuu tajwa hutokea. Kulingana na kanuni hii, nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo. Kanuni hii ndiyo iliyokuwa ya mshiko sana katika utafiti huu wa vimilikishi. Kwa mujibu wa kanuni hii, vivumishi (vimilikishi na vionyeshi) huchukua nafasi karibu na nomino kama neno kuu katika tungo virai hasa katika Lugha za Kibantu (Rijkhoff, 1986).

Kwa kurejelea mihimili ya Ubia na Upatanifu wa Nadharia ya Umilikifu na Unganifu, data za usomaji wa kazi za Katamba, (2003), Kiyinikibi, (2021), Dixon, (2010), Philipo & Kuyenga, (2017) na Mbwillow, (2017) kuhusiana na kanuni hii, utafiti huu ulibainisha Luganda na Kiswahili sanifu kutumia kanuni hizi ambazo zilichunguza ukuu wa utokeaji wa elementi na ukaribu au nafasi ya utokeaji wa elementi hizo katika tungo. Kwa kuchunguza elementi kuu katika tungo, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huzingatia ukuu wa utokeaji wa kategoria za maneno katika tungo kwa kuzingatia kanuni ya muundo virai. Kwa mujibu wa lugha hizi, sentensi huundwa kwa KN na KT ambapo uhusiano kati yake unatokana na neno kuu. Neno kuu ni neno lililobebea hadhi ya ukuu au ujumbe wa kirai. Neno hili hutangulia vivumishi wakati wa matumizi.

Uchanganuzi wa matumizi ya kanuni hii ulibainisha uwiano wa vivumishi kutokea karibu na baada ya nomino au neno kuu. Kuhusu utokeaji wa vivumishi vimilikishi, ilifahamika kuwa matumizi yake huweza kuja baada ya nomino kama neno kuu ila ikitokea na vivumishi vingine vinavyosisitiza ujumbe, utokeaji wake ni wa kimuktadha unaotegemea dhima ya kategoria inayobeba ujumbe kwa mujibu wa msemaji au mwandishi. Data (5.20) ya data hii inadhihrisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai baina ya Luganda na Kiswahili kutokana na Abudonia, 2014 na Dixon, 2010. (5.20).

a) *Omuyizi wange ono ayise ebibuuzo.*

Mwanafunzi **wangu huyu** amepita mitihani.

b) *Omuyizi oli wange ayise ebibuuzo.* Mwanafunzi **yule wangu** amepita mitihani.

c) *Ekitabo kino kirungi.* Vitabu hivi vizuri.

d) *Ebitabo byange byonna* Vitabu **vyangu vyote.**

e) *Obulamu bwange bulungi.* Maisha **yangu** mazuri.

f) *Abaana bange bombi balungi.* Watoto **wangu** wawili wazuri.

Asili: Kutokana na Leah na Ssuguya, (2015) na Abudonia, (2014)

Kwa kutumia mihimili ya Ubia na Upatanifu, Mifano hii imedhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo, imebainishwa kuwa utaratibu wa kutumia vimilikishi na vivumishi vingine katika KN umetokana na nomino {Omuyizi} kuwa neno kuu {kiima}. Hali ambayo inasababisha utaratibu wa vivumishi kutokea baada ya nomino au neno kuu kuonyesha uhusiano milikifu na Unganifu wa neno kuu na vimilikishi kama ilivyoelezwa na Rijkhoff, (1986). Aidha, uwiano mwingine unaojitokeza ni kuwa matumizi ya vivumishi vimilikishi katika Luganda na Kiswahili sanifu hutegemea dhima au ujumbe wa msemaji. Msemaji au mwandishi anaweza kuanza na kimilikishi au vivumishi vingine kutegemea hadhi au ukuu wa kivumishi kinachohusika katika KN. Kwa mfano data katika (a-b) kimilikishi kilisisitiza ujumbe na katika (c) kionyeshi kikasisitiza kikifuatwa na kimilikishi (Abudonia 2014; Ssekiryango 2006).

Tofauti ya kanuni hii ni kuwa licha ya kuwa vimilikishi hutokea baada ya nomino kama neno kuu, muktadha wa matumizi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana. Muktadha wa matumizi ya vimilikishi na vivumishi vingine kimfuatano katika Luganda hutofautiana katika ukuu wa aina ya kivumishi kinachotumika pamoja na kimilikishi na miktadha mbalimbali. Aidha, tofauti nyingine ambayo ilidhihirika katika uchanganuzi matumizi ya vivumishi katika Luganda na Kiswahili ni ya kiprakmatiki. Hata hivyo, Luganda mara nyingi huweza hata kubadilisha muundo wa kivumishi kutangulia nomino kutegemea muktadha na umilisi wa lugha. Kwa mujibu wa utafiti huu, dhima kuu katika Luganda ni kuwasiliana pasi kujali baadhi ya kanuni za kisarufi wa kimuktadha wa kutumia vivumishi. Mfano wa data (5.20) unadhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya vimilikishi.

Matokea ya matumizi ya kanuni hii katika Luganda na Kiswahili yanashadidiwa na matokeo ya utafiti wa Lusekelo, (2017) na Rugemalira (2007) kuhusu utokeaji wa vivumishi na vionyeshi katika tungo {KN} kuwa wa kimuktadha kutegema neno lililo na hadhi ya juu. Aidha, Abudonia, (2014) naye anaeleza kuwa matumizi ya vivumishi katika KN hutawaliwa na kanuni ya kipragmatiki na hadhi ya Kivumishi kipi husheheni dhima au ujumbe wa sentensi hata ingawa kanuni ya jumla ni kuwa kivumishi huja baada ya nomino kuu katika KN katika Luganda. hali ambayo vilevile hujitokeza katika Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa, licha ya unasaba wa Luganda na Kiswahili sanifu, matumizi ya kanuni hii yalidhihirisha kuwiana na kutofautiana. Matokeo haya yalidhihirisha kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye upekee wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia.

5.1.2.2 Uwiano na tofauti za kanuni za vivumishi vya a-Unganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu

Kwa mujibu wa Obara (2014), [-a] unganifu ni kiambishi tamati kinachoambatishwa kwenye viambishi vya ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa. Kisakwah, (2014), Habwe & Karanja, (2004) wanafafanua kuwa, kivumishi cha [-a] unganifu kuwa aina ya kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno. Kwa mujibu wa utafiti huu, [-a] unganifu ni aina ya kivumishi kinachotokana na mzizi husishi [-a] kinachotumika kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika utungo chenye dhima ya kimofosintaksia ya kuelezea zaidi juu ya aina, daraja, umilikaji na hali ya nomino husika katika tungo. Kimofosintaksia kivumishi hiki lazima kiunganishwe na mofu zinazowakilisha aina ya ngeli nomino inayohusika kiupatanisho kinapotumika ili kuonyesha uhusiano wa nomino na kategoria ya maneno mengine, kutoa taarifa zaidi za nomino kidaraja, umilikaji, hali/aina ya nomino au kiwakilishi chake katika utungo.

Kwa mujibu wa Obara (2014), Kisakwah, (2014) Oduor na wenzake (2017), mtumiaji asiyezingatia kanuni ya kuteua viambishi vya msingi patanishi vinavyofaa wakati wa kutumia kivumishi hiki huwa amekiuka kanuni ya sarufi na hivyo hupotosha usanifu wa lugha husika. Kila lugha huwa na maumbo yanayoshabihiana na kutofautiana katika matumizi ya vipashio vya kisarufi kama vile kivumishi cha {-a} unganifu. Luganda na Lugha ya Kiswahili sanifu hutumia kanuni mbalimbali kudhihirisha matumizi ya kivumishi cha {-a} unganifu. Utafiti huu uliweza kubainisha kanuni zifuatazo kama zinavyotumika na wamilisi wa Luganda na Kiswahili sanifu na kueleza uwiano na tofauti za matumizi ya {-a} unganishi.

5.1.2.2.1 Kanuni ya kisintaksia ya umilikishi au upatanishi wa kisarufi

Matokeo ya maandishi ya Habwe & Karanja, 2004; Oduor na Wenzake, (2017) maktabani ulibaini kuwa, kanuni ya umilikishi ni kanuni ambayo hudhihirisha uhusiano wa viambajengo vya kisarufi katika tungo. Kanuni hii hudhihirisha uhusiano baina ya neno kuu au neno tawala na shamirishi katika tungo virai au vishazi. Kanuni ya kisintaksia hujitokeza pale ambapo maneno katika sentensi au kishazi hufungamanishwa ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Umiliki ni uhusiano wa kisintaksia wa neno moja kutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo virai au vishazi. Kanuni hii hudai kuwa umilikishi wa vivumishi vya [a-] unganifu hutokana na mzizi au kihusishi tamati {-a} unaoambatishwa kwenye viambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno.

Kanuni nyingine kimofosintaksia ni kuwa: Kirai nomino huathiri maumbo ya matumizi ya kivumishi cha {-a} unganifu. Mzizi {-a} huchukua maumbo tofauti ya kisintaksia kutegemea nomino kuu katika tungo kirai nomino au vishazi vinavyovumishwa. Kanuni hizi zinatetewa na Chomi, (2003) anayedai kuwa nomino kuu hutawala vivumishi kwa kuakisiwa katika miundo ya maneno ya kategoria husika. Mifano ya data (4.11, Uk. 97) kutokana na Abudonia, (2014), Kiyinikibi, (2021) inadhihirisha mifano ya data ya uwiano na tofauti za matumizi ya {-a} unganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu katika tungo. Viambishi patanishi tofauti vya msingi vimeambatishwa kwenye mzizi {-a} kudhihirisha uhusiano kati ya nomino na maneno mengine katika tungo. Viambishi vilivyotumika ni vya kisintaksia ambavyo vinaonyesha uhusiano wa nomino na kivumishi husika. Katika KN, kivumishi {-a} unganifu kimejitokeza kama kiambajengo shirikishi cha kundi husishi kinachofanya kazi kama kivumishi kwa njia ya urejeleo mbele na nyuma wa kueleza zaidi juu ya nomino *mtoto* na Juma. Kuwa *Juma ana mtoto* (nomino tawala au umilikaji) na *mtoto* anayetajwa ni wa *Juma* (nomino tawaliwa- kisabaki).

Matokeo ya uchanganuzi wa Rose, (2009) Asiimwe, (2016), Obara, (2014) na Kisakwah, (2014) yalibainisha kuwa Luganda na Kiswahili hushabihiana katika kutumia kivumishi {-a} unganifu. Lugha hizi zote zilidhihirisha kutumia kivumishi {-a} unganifu kwa kuambatanisha viambishi patanishi msingi vya nomino kutegemea ngeli nomino inayohusika kuonyesha umilikaji, aina au hali na daraja ya nomino inayotajwa katika tungo. Tofauti iliyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni ya mofu za viambishi vya upatanishi msingi zinazoambatishwa kwenye mzizi tamati {-a}. Mofu hizi hutofautiana kutokana na mfumo au

mpangilio na maumbo ya viambishi patanishi tofauti vya ngeli kimofosintaksia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kama invayojitokeza katika Jedwali (4.11, Uk. 102) linadhihirisha uwiano na tofauti za vivumishi vipatanishi vya a-unganifu vya Luganda na Kiswahili kutokana na Rose (2009) Asimwe (2016) kuhusu viambishi vipatanishi vya –a unganifu katika sura ya nne. Kwa kurejelea matokeo ya maelezo na ufafanuzi wa kanuni ya wanaisimu hawa kuhusiana na kanuni hii, utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana na kutofautiana katika kutumia kanuni za umiliki na usabaki wakati wa kutumia vivumishi vya {-a} unganifu. Umiliki na usabaki ulijitokeza katika uambishaji wa viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) kwenye mzizi [-a] kuunda vivumishi vya [-a] unganifu kutegema nomino kuu. Uambishaji huu ulidhihirisha upatanishi wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi husika ambapo kiambishi ngeli kiliwakillisha anafora huku nomino ikiwa ni kisabaki.

Mchakato wa uambishaji ulisababisha kanuni ya kimofosintaksia ya uambishaji ya: Neno kuu katika kirai nomino (KN) hupatana kisarufi na vivumishi vyake kuhusu vipengele kama vile ngeli, nafsi na ya umoja na wingi wa neno kuu katika tungo virai na vishazi kupitia kwa viambishi patanishi vya msingi (VPM) vya neno kuu. Tofauti ya matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa licha ya lugha hizi kuwiana katika matumizi ya kanuni ya umiliki na usabaki, lugha hizi za Kibantu hutofautiana katika uwakilishi wa viambishi vipatanishi vya msingi, na mabadiliko ya kimofofnolija uliojitokeza katika uundaji wa VPM vya {-a} unganifu ambavyo ni vipatanishi vya msingi vinavyojenga sifa za kimofosintaksia za umiliki na usabaki baina ya nomino na kivumishi husika. Tofauti nyingine ni ya muundo wa matumizi ambapo Luganda iliathiri kivumishi {-a} na kusababishi mzizi mbadala {-e} wa {-a} unganifu. Tofauti hii ilijitokeza pale ambapo {-a} unaganifu iliunganika na nomino inayomiliki nomino kianafora pamoja na uwakilishaji wa vibaisho vya ngeli vilivyopachikwa nyuma ya viambishi awali vya ngeli nomino. Kama inavyojitokeza katika mfano wa data za awali Na. (4.12, Uk. 100) ilidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kivumishi cha ‘-a unganishi’ kati ya Luganda na Kiswahili (Baertlein & Ssekitto, 2014; Habwe & Karanja, 2004). Kuhusu muundo wa nomino huweza kuathiri a-unganifu kimuundo na kimofolojia na kusababisha a-unganifu ambayo imedondoshwa.

Matokeo haya yanashabihiana na kanuni ya Chomsky, (1957:1967) anayefafanua kanuni ya jumla ya umiliki na usabaki ya kuwa; vifundo huunda kiambajengo kama tu viambajengo hivyo vitakuwa ni jozi za vifundo vinavyomilikiwa kikamilifu na kifundo kikuu (Chomsky,

1957:1967). Mathalan, Mathooko (1994) na Ambuyo (2007) wanafafanua kuwa: Neno kuu katika kirai huyamiliki maneno mengine yote katika tungo kutokana na uhusiano uambajengo unaodhihirisha sifa za kimofosintaksia katika tungo virai. Kulingana na maelezo ya Aidha, matokeo ya utafiti huu yanalingana na ufafanuzi wa Obara (2014) anayeeleza kuwa, ‘-a’ unganifu ni kiambishi tamati kinachoambatishwa kwenye viambishi vya ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa. Mwanafunzi anapokitumia kiambishi hiki hana budi kuteua kiambishi cha ngeli kinacholeta uwiano wa upatanisho. Mwanafunzi akitumia kiambishi kisichofaa atakuwa amevunja kanuni za kisarufi (Obara, 2014:55).

Kwa mujibu wa matokeo ya kanuni hii, utafiti huu umefafanua utokeaji wa kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Imedhihirika kuwa, licha ya Luganda na Kiswahili kushabihiana katika matumizi ya kanuni hii ya vipashio vya kimofosintaksia, lugha hizi hutofautiana kutokana na sifa za kipekee zinazomilikiwa na lugha mahususi kimofosintaksia kuonyesha ubia na upatanifu wa nomino na maneno mengine katika tungo.

5.1.2.2.2 Kanuni ya kimofolojia ya uambishaji viambishi katika mzizi wa kivumishi

Kanuni hii hudai kuwa: Vivumishi {-a} unganifu huambishwa kiambishi patanishi cha msingi awali cha ngeli nomino ya neno kuu kwa ajili ya kuleta upatanishi unaofaa kati ya nomino na maneno mengine katika tungo virai au vishazi. Vilevile kanuni hii inadai kuwa: Kila nomino inayotumiwa huwa na vambishi patanishi vya msingi vinavyotofautiana kutokana na mfumo pamoja na maumbo ya kisintaksia ya ngeli nomino na kivumishi chake (Kiyinikibi, 2021; Katamba, 2003; Leah na Sseguya, 2014; Chomi, 2003). Ukiukaji wa kuambatisha viambishi vya kiupatanishi usiofaa huweza kupotosha uhusiano wa nomino na vivumishi na hivyo kupotosha usanifu wa matumizi ya lugha husika. Kanuni hii inatokana na kanuni ya jumla ya uambishaji inayodai kuwa: Uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu (Obara, 2014, Kisakwah, 2014 na Chomi, 2003).

Matokeo ya uchanganuzi wa maandishi ya Philipo (2012), Kiyinikibi, (2021) Katamba, (2003); Leah & Sseguya, (2014); Chomi, (2003) kuhusu uambishaji wa viambishi katika mizizi ya vivumishi kama inavyojitokeza katika mfano (4.11, Uk. 97) na jedwali Na. (4.11, Uk. 102), utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana na kutofautiana kimofolojia na kisintaksia hasa katika kuambatanisha mzizi wa kivumishi cha {-a} unganifu kinachowakilishwa na kiambishi tamati {-a} kutegemea maumbo ya viambishi

vipatanishi msingi vya ngeli husika. Aidha, kivumishi cha {-a} unganifu kimofolojia huundwa kwa kiambishi cha upatanishi msingi cha ngeli nomino na mzizi {-a}. Viambishi vya upatanishi wa ngeli huambatanishwa kwenye mzizi {-a} kuunda vivumishi kwa ajili ya kuleta maana. Katika kundi nomino, {-a} unganifu hutumika kuonyesha uhusiano wa kiupatanifu baina ya nomino na maneno mengine katika tungo virai na vishazi.

Uwiano na tofauti za matumizi ya matumizi ya kanuni hii umejitokeza katika maumbo ya uambishaji wa viambishi vipatanishi vya msingi kwenye kivumishi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya nomino na maneno mengine katika tungo. Uwiano na tofauti hizi ni kama zinavyojitokeza katika Jedwali (4.11, Uk 102) linadhihirisha uwiano na tofauti za vivumishi vipatanishi vya a-unganifu vya Luganda na Kiswahili kutokana na Rose (2009) Asimwe (2016) kuhusu viambishi vipatanishi vya {-a} unganifu na mifano ya data katika mifano ya (4.11, Uk. 97 na Jedwali 4.11, Uk. 102) kutokana na Abudonia, (2014), Leah & Sseguya, (2015), Kiyinikibi, (2021), Baertlein & Ssekitto, (2014), Mdee, Njogu, & Shafi, A. (2019) katika Kamusi ya Karne ya 21, (2019).

Kulingana na mifano hiyo, matumizi ya viambishi vipatanishi kwenye mzizi wa {-a} unganifu baina ya Luganda na Kiswahili ulishabihiana kwa kuwa lugha zote zilizidhamiria kudhihirisha upatanisho wa kisarufi wa nomino na maneno mengine katika tungo. Tofauti iliyojitokeza ni kuwa, japo lugha zote mbili zina mfumo unaoshabihiana wa kuambisha viambishi vipatanishi kwenye mzizi {-a}, maneno mengi yenye maana sawa na baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ya hupatikana katika ngeli tofauti na hivyo kuchukua viambishi tofauti kiupatanishi. Aidha, tofauti iliyojitokeza ni kuwa katika Luganda, nomino huweza kuathiri a-unganifu kimuundo na kimofolojia na kusababisha {-a} unganifu ambayo imedondoshwa na badala yake kiambishi tamati -a kubadilika na kuwa {-e}. Tofauti hii hujitokeza hasa kutokana na kibainishi na hali ya kuashiria mahali inayomiliki nomino kama inavyojitokeza katika mifano ya Na. (4.12, Uk. 100).

Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Obara, (2014) ambaye anaeleza kuwa;

Kwa kawaida {-a} unganifu hutumiwa na kiambishi cha ngeli pamoja na nomino kuunda kivumishi. Vivumishi hivi huundwa kwa kiambishi {-a} ambacho ni cha tamati kinachoambatishwa kwenye viambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno (Obara, 2014: 56).

Anaendelea kuonyesha kuwa ukiukaji wa kuambatanisha viambishi kifaacho kwenye {-a} unganifu, upatanifu wa kisarufi huwa umepotoka. Kisakwah (2014) akimuunga mkono Obara (keshatajwa), katika maelezo ya muundo na matumizi ya kivumishi {-a} na kushabihiana kwa matumizi yake na lugha za Kibantu, Anaeleza kuwa, “Kiunganifu {-a} ni aina ya kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno.”

Aidha, katika utafiti wake alibaini kuwa Kisuba na Kiswahili hutumia kiunganifu {-a} kwa namna inayoshabihiana na hujitokeza kama kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta upatanishi wa kisarufi baina ya nomino na maneno mengine katika tungo. Utafiti huu ulichanganua kanuni ya uambishaji na jinsi inavyojitokeza katika Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo yalibanisha kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili hutumia kanuni hii, kuna kushabihiana na kutofautiana kwa muundo na maumbo ya kimofosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu.

5.1.2.2.3 Kanuni ya kimofonolojia ya uambishaji wa KPM

Kanuni hii inadai kuwa: Kuna mabadiliko ya kimofonolojia mbalimbali yanayotokea katika uambishaji viambishi vipatanishi vya msingi kwenye kivumishi [-a] unganifu. Mabadiliko haya hutokana na umbo la kiambishi patanishi msingi ambalo hutegemea viambishi awali vya ngeli nomino vya upatanishi. Viambishi hivi huathiriana kutokana na mfuatano au utokeaji wake katika mazingira ya fonimu irabu na konsonanti katika mfumo wa matumizi ya viambishi patanishi msingi mwanzoni mwa mzizi hasa katika mazungumzo na maandishi (Katamba, 1993:2003; Chomi, 2003 na Mgullu, 1999).

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni za Kibantu za kimofolojia kutokana na Habwe & Karanja, (2004), Massamba na wengine, (2003), Katamba (1993:2003) na Chomi, (2003) yalitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana katika kutumia kanuni hii ya kimofonolojia ya uambishaji wa viambishi vipataishi vya msingi vya vivumishi. Aidha, kwa mujibu wa utafiti huu Luganda na Kiswahili sanifu zilizidhihirisha athari au mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia wakati wa uambishaji wa viambishi vipatanishi kwenye mzizi [-a] unganifu. Luganda na Kiswahili sanifu zilizidhihirisha kanuni ya uyeyushaji, udondoshaji na muungano wa fonimu irabu na kujenga viambishi vya msingi patanishi vilivyoambishwa kwenye mzizi wa kivumishi cha [-a] unganifu. Jedwali lifuatalo Na. (5.2) linadhihirisha data za uwiano na tofauti za kimofonolojia ambayo hutokea katika tungo kuwakilisha uhusiano

milikifu na unganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kwa mujibu wa Habwe & Karanja, 2004, Massamba na wengine, 2003, Katamba 1993:2003 na Chomi, 2003).

Jedwali 5.2: Kanuni za kimofonolojia za kivumishi cha [-a] unganifu za Luganda

| Ngeli | KPM Lug | KPM Kis | Mzizi | Kivumishi [-a] unganifu Luganda | Kivumishi [-a] unganifu Kiswahili | Kanuni za Luganda | Kanuni za Kiswahili |
|-------|---------|---------|-------|---------------------------------|-----------------------------------|---------------------|---------------------|
| 1 | A | u-a-yu | -a | Wa | wa | Muungano | Muungano |
| 2 | ba | wa | -a | Wa | wa | Udondoshaji | Udondoshaji |
| 3 | Gu | U | -a | Gwa | wa | Muungano | Muungano/uyeyushaji |
| 4 | Gi | I | -a | Ya | ya | Uyeyushaji | Uyeyushaji |
| 5 | Li | li | -a | Lya | la | Uyeyushaji/u | Udondoshaji |
| 6 | Ga | ya | -a | Ga | ya | Uyeyushaji | Uyeyushaji |
| 7 | Ki | ki | -a | Kya | cha | Uyeyushaji | - |
| 8 | Bi | vi | -a | Bya | vya | Udondoshaji | - |
| 9 | Ka | I | -a | Ka | ya | Udondoshaji | Uyeyushaji |
| 10 | Bu | zi | -a | Bwa | za | Muungano | Muungano |
| 11 | Lu | U | -a | Lwa | wa | Muungano | Muungano/uyeyushaji |
| 12 | Zi | zi | -a | Za | za | Muungano | - |
| 13 | Gu | - | -a | Gwa | - | Muungano | - |
| 14 | Ga | - | -a | Ga | - | Udondoshaji | - |
| 15 | Ku | ku | -a | Kwa | kwa | Muungano/uyeyushaji | Muungano/uyeyushaji |
| 16 | Ga | pa | -a | Ga | pa | Udondoshaji | Udondoshaji |
| 17 | Tu | ku | -a | Twa | kwa | Muungano | Muungano uyeyushaji |
| 18 | -mu | mu | - | Mwa | mwa | - | Uyeyushaji/muungano |

Asili: Data kutokana na Uchanganuzi matini maktabani na mijarabu nyanjani (2021)

Jedwali hili linadhihirisha kanuni za mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea katika uundaji wa vivumishi vya {-a} unganifu katika Luganda sanifu. Imedhihirika kuwa vivumishi vya {-a} unganifu huundwa kwa kuambisha viambishi vya upatanisho wa kisarufi au viambishi vya kisintaksia vya Luganda ambavyo hupitia mchakato wa kanuni za muungano, uyeyushaji na udondoshaji wa fonimu kuunda vivumishi vya {-a} unganifu. Baada ya mchakato wa ujenzi wa vivumishi vya {-a} unganifu, ilitambulika kuwa kila ngeli au nomino ilitumia kivumishi tofati na nomino zingine katika tungo kutokana na maumbo tofauti ya viambishi vipatanishi vilivyoambatishwa kwenye mzizi {-a} wa kivumishi unganifu. Tofauti iliyojitokeza kati ya Luganda na Kiswahili ni kuwa athari za kimofosintaksia zilitofautiana kutoka ngeli moja na nyingine kati ya Kiswahili na Luganda sanifu. Kwa mfano katika jedwali, ngeli ya (5-7) ambapo Luganda ilitumia viambishi vipatanishi msingi tofauti na Kiswahili sanifu. Luganda ilitumia kya, bya na lya huku Kiswahili ikitumia [la, vya na la] mtawaliwa. Hali hii

inatokana na kuwa kanuni ya kifonolojia ya uyeyushaji ilitumika katika Luganda, huku Kiswahili sanifu kikitumia kanuni ya kifonolojia ya muungano na udondoshaji kuunda VPM . Hali hii ilitokana na kanuni za kifonolojia tofauti kati ya Luganda na Kiswahili ingawa zote ni lugha za kibantu ambazo huathirika na mabadiliko haya ya kifonolojia. Matokeo haya yanaendana na maelezo ya Mgullu, (1999), Chomi (2003) ambao wanadhihirisha athari au mabadiliko ya kifonolojia yanayojitokeza katika lugha za Kibantu. Wanaeleza kuwa;

Kiambishi kipatanishi cha msingi kikianza na ama konsonanti au irabu, huweza kusabababisha mabadiliko au kuathiri fonimu ambayo inapachikwa kwenye mizizi kama kiambishi kipatanishi cha mssingi (KPM).

Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na maelezo ya Mgullu, (1999), Katamba (1993) na Chomi, (2003). Kama yalivyojitokeza katika utafiti wa Ontieri (2016) aliyetambua kuwa, Lugha ya Kiswahili ina mfumo wa kifonolojia ambao una upekee unapolinganishwa na lugha nyinginezo. Ingawa hii ni lugha ya Kibantu, kunadhihirika tofauti anuwai tunapolinganisha muundo wa lugha hii na lugha nyingine za Kibantu katika kiwango cha kifonolojia. Tofauti hizi ndizo zinazosababisha athari za kifonolojia ambazo zinadhihirika katika matumizi ya Kiswahili na wazawa wa jamii mbalimbali za Kibantu (Ontieri 2016:1).

Aidha, matokeo ya Otiende, (2013) katika utafiti wake kuhusu athari za kimofonolojia za Kiolusuba na Kiswahili zinadhihirisha kuwa athari za mofonolojia ya L1 katika matumizi ya Kiswahili husababishwa na sauti za Kiswahili zisizopatikana katika L2 na miundo tofauti ya baadhi ya maneno. Anaeleza kuwa, Kiswahili kina mfumo wa sauti mahususi ambao unastahili kufuatwa ili kukitumia kwa usahihi. Kila lugha huwa na miundo ya maneno inayoruhusiwa kama vile sauti zipi zinazoweza kufuatana na zipi katika mazingira fulani. Iwapo mtumiaji wa lugha ya Kiswahili atazihamisha sauti za lugha yake ya kwanza, ataivuruga Kiswahili na hivyo kukitumia vibaya (Otiende, 2013)

Tofauti na matokeo ya wataalamu hawa (washatajwa), Utafiti huu ulichanganua kanuni za kimofosintaksia za Luganda na Kiswahili na kutambua kuwa, Licha ya Luganda na Kiswahili kushabihiana katika matumizi ya kanuni ya kimofonolojia ya uambishaji, lugha hizi za nasaba moja zilidhihirisha kutofautiana hasa katika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu ya kipashio cha kivumishi cha –a unganifu katika tungo.

5.1.2.2.4 Kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa neno kuu na maneno mengine katika tungo

Heine (1976) anaeleza kuwa lugha zote za Kibantu hufuata utaratibu wa kiima kufuata kitenzi katika KN; Yambwa kufuata kitenzi; vikumushi vya nomino kama vile vivumishi vya idadi, vimilikishi, vionyeshi na virai virejeshi huja baada ya nomino; vivumishi vimilikishi hufuata vivumishi vinginevyo vinavyotokea katika tungo ambapo virai, vishazi na vielezi hutokea baada ya vitenzi na vivumishi. Uchanganuzi wa data za upekuzi wa kazi za Haine, (1976) Sseguya, (2015); Habwe & Karanja, (2004) na Abudonia (2014) na Dixon, (2010) ulidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa neno kuu na maneno mengine katika tungo baina ya Luganda na Kiswahili. Ilibainika kuwa, vivumishi vya [-a] unganifu hutokea baada na karibu na neno kuu katika KN. Hata hivyo utokeaji wake ni huru bali sio funge. Kivumishi hiki kilitokea baada ya neno kuu au nomino kama neno kuu na karibu sana na neno kuu kutegemea muktadha, dhima ya maneno mengine na hadhi ya vivumishi au maneno mengine katika tungo. Aidha, matumizi ya kivumishi cha [-a] unganifu kilitumika mtawaliwa kutegemea uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo virai, vishazi na vishazi, darajia na hali ya umilikaji wa dhana au nomino husika kuelezea juu ya umilikaji, aina na daraja ya nomino au dhana iliyozungumziwa. Hali ambayo ilionyesha ubia wa sarufi ya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyodhihirishwa katika data a. (5.21) kutokana na Asiimwe (2016). (5.21)

- | | |
|---|------------------------------------|
| a) <i>Ekinabiro [kya] bakyaala kikyafu.</i> | Bafu la wanawake ni chafu. |
| b) <i>Omulenzi omulungi [wa] Kabaka.</i> | Mvulana mzuri [wa] Kabaka. |
| c) <i>Omwana oyo [wa] ssomero lyaffe.</i> | Mtoto huyo [wa] shule yetu. |

Asili: Data za utafiti nyanjani, 2020

kwa kutumia mihimili ya ubia na upatanifu, Mifano hii inadhihirisha kuwa ingawa vivumishi vya [-a] unganifu hutokea baada ya nomino, ukaribu wake na nomino kama neno kuu kuwa ni wa kimahusiano bali sio wa nafasi ya utokeaji. Kwa mfano katika sentensi (a) imetokea baada ya nomino [ekinabiro]. Katika kishazi cha (b) imetokea baada ya kivumishi cha sifa na kimetokea karibu na baada ya kutajwa kwa kivumishi na baada ya nomino kama neno kuu. Kwa jumla imedhihirishwa kuwa kivumishi cha [-a] unganifu hutokea baada ya neno kuu au nomino kama neno kuu katika KN na inapotokea pamoja na vivumishi vingine, hutegemea muktadha na dhima yake katika KN.

Mathalani, uchanganuzi wa data ulidhihirisha tofauti za Kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa neno kuu na maneno mengine katika tungo baina ya Luganda na Kiswahili

sanifu. Tofauti iliyojitokeza ni kuwa ingawa kanuni za matumizi ya vivumishi vya [-a] unganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana kiutaratibu katika nafasi, ukaribu wa utokeaji na neno kuu pamoja na dhima ya kueleza aina, umilikaji na daraja ya mahusiano ya nomino na maneno mengine katika tungo, viunganishi vipatanishi vya msingi vilivyoambatishwa kwenye mzizi [-a] hutofautiana kati ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na idadi ya ngeli nomino, mfumo wa uainishaji wa nomino na maumbo ya kudhihirisha vivumishi vya [-a] unganifu kwa kila nomino inayohusika. Hali hii inatokana na mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea wakati wa kuambisha viambishi patanishi vya msingi kwenye mzizi [-a] kama inavyojitokeza katika Jedwali (4.11, Uk. 102) linalodhihirisha uwiano na tofauti za vivumishi vipatanishi vya a-unganifu vya Luganda na Kiswahili kutokana na Rose (2009) Sendanda & Asimwe (2016) kuhusu viambishi vipatanishi vya –a unganifu. Kwa mujibu wa jedwali hilo, vivumishi vya a-unganifu vya Luganda na Kiswahili sanifu vinatofautiana kulingana na viambishi vipatanishi awali vya ngeli nomino inayotajwa. Ngeli ya kwanza umoja inadhihirisha uwiano wa kiambishi kipatanishi cha umoja na kutofautiana na kiambishi cha upatanisho cha wingi. Vilevile imetambulika kuwa viambishi vipatanishi vya a-unganifu ya ngeli ya tano vinawiana. Hata hivyo, inafaa ikumbukwe kuwa ngeli hii inatofautiana na ngeli ya Kiswahili kwani majina yanayotajwa katika ngeli hii katika Luganda ni ya wanyama tofauti na majina ya ngeli hii inayohusiana na vitu hasa vinavyotengenezwa na binadamu katika Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Heine, (1976) na maelezo ya Dixon, (2010) na Abudonia, (2014) pamoja na Leah & Sseguya (2015) kuhusu utokeaji wa vivumishi ambavyo kulingana nao hutokea baada ya neno kuu. Kwa mtazamo wa maelezo ya wataalamu hawa, utafiti huu ilibaini kuwa lugha zote za Kibantu huzingatia utaratibu maalumu wa vivumishi kutokea baada ya nomino katika KN. Utata ni kuwa mitazamo yao haikubainisha kivumishi cha [-a] unganifu hutokea karibu na baada ya kategoria gani ya vivumishi. Ufafanuzi wa wataalamu hawa ulichangia kutafiti juu ya utokeaji wa vivumishi vya [-a] unganifu kutegemea kanuni ya ukaribu na utaratibu wa utokeaji wake katika KN baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.2.3 Uwiano na tofauti wa kanuni za matumizi ya Vivumishi Vionyeshi

Vivumishi vionyeshi ni aina ya vivumishi vinavyotumika kudhihirisha nomino kutegemea nafasi alipo mzungumzaji. Ni viashiria vinavyotumika kudhihirisha mahali kilipo kitu, viumbe au mahali kwa kuzingatia ujirani au umbali wa mtoaji kauli (Mgullu, 1999; Chomi,

2003; Mirikau, 2008). Habwe & Karanja (2004), wanafafanua kuwa vionyeshi hutumiwa katika tungo kuashiria wazi kinachozungumziwa (nomino tendaji) kutegemea nafsi tatu ya karibu, mbali kidogo na mbali sana. Vivumishi vionyeshi hutumika kwa kuzingatia kanuni za kimfosintaksia kujenga dhana vinginevyo tungo itakayotokea haitakuwa sahihi kisarufi. Zifuatazo ni miongoni mwa kanuni ambazo zinaongoza matumizi ya vivumishi viongozi kama ilivyojitokeza katika upekuzi wa maandishi mbalimbali.

5.1.2.3.1 Kanuni ya nafsi na ngeli nomino

Kanuni inayohusika katika matumizi ya vionyeshi inashikilia kuwa: Nomino huvumishwa kulingana na nafasi ilipo hasa kuzingatia ujirani na umbali wake na mtoaji kauli. Mathalan, nomino pia huvumishwa kutegemea kundi nomino ambamo inatokea. Utambuzi wa nafasi ya nomino na ngeli inamoainishwa nomino inayovumishwa humwezesha mzungumzaji na mwandishi kutambua na kutumia viwakilishi vya ngeli na nafasi kwa usahihi pasi kuvunja usanifu wake. Kwa mujibu wa kanuni hii, pronomino au viwakilishi nafsi na ngeli vinavyotumika lazima vidhihirishe upatanisho wa kisarufi wa nomino inayovumishwa. Kanuni ya nafsi na ngeli hutokana na kanuni kuwa vivumishi hutawaliwa na nomino kupitia kwa viambishi nomino vinavyodhihirisha sifa za kimfosintaksia vya kudhihirisha sifa za kisarufi za nafsi na idadi ya umoja na wingi. Kuhusu ngeli, viambishi awali vya ngeli nomino ndivyo vinavyoathiri upatanishi wa kisarufi wa matumizi ya viambishi vipatanishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya vionyeshi. Hii ina maana kuwa viambishi awali vya nomino ndivyo vinavyoamua aina ya viambishi vipatanishi vya msingi vinavyopachikwa kwenye vivumishi vionyeshi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi (Ngamau, 2004 na Egara 2006)

Kwa kuzingatia kanuni hii ya jumla ambayo hushikilia vionyeshi kutumika kulingana na ngeli nomino na ujirani na umbali wa nomino inayokumushwa, matokeo ya uchanganuzi wa upekuzi wa maandishi ya Obara (2014, Abudonia, (2014), Dixon, (2010) na Kisakwah, (2014), yalidhihirisha Luganda na Kiswahili sanifu kushabihiana katika matumizi ya vivumishi vionyeshi kuzingatia kanuni hii ya nafsi ya kwanza karibu sana; nafsi ya pili- mbali kidogo na nafsi ya tatu mbali sana pamoja na matumizi ya kiambishi kipatanishi cha msingi (KPM) cha ngeli ambacho huambishwa kwenye mzizi wa kionyeshi kama inavyojitokeza katika data Na. (5.22) kutokana na Kiyinikibi, (2021), Leah & Sseguya (2015), Obara, (2014), Dixon, (2010).

- | | |
|--|---|
| a) <i>Omwana ono/oyo/oli atawanya nnyo</i> | <i>Abaana aba/abo/bali/ batawanya nnyo</i> |
| Mtoto huyu/huyo/yule anasumbua | Watoto hawa/hao/wale wanasumbua |
| b) <i>Omukati guno/ogwo/guli kuwooma</i> | <i>Emikati gino/egyo/gili giwooma</i> |
| Mkate huu/huo/ule ni tamu | Mikate hii/hiyo/ile ni tamu |
| c) <i>Eriiso lino/elyo/lili lilaba bulungi</i> | <i>Amaaso gano/ago/ gali galaba bulungi</i> |
| Jichi hili/hilo/lile linaona vizuri | Macho haya/hayo/yale yanaona vizuri |

Asili: Data kutokana na Kiyinikibi, (2021)

Vishazi hivi vinadhihirisha kanuni ya nafsi na ngeli. Vionyeshi vilivyokolezwa (a-b), vinadhihirisha kutumika kutegemea ngeli kwa umoja na wingi pamoja na viashiria vilivyotumika katika nafasi tatu kuonyesha ujirani, umbali na umbali sana wa nomino inayokumushwa. Matumizi ya nomino na vionyeshi husika umezingatia upatanishi wa kisarufi wa kimofosintaksia ambapo nomino zimezingatia kanuni ya kimofolojia ambapo zimewakilishwa na maumbo ya kimofolojia ya viambishi awali vya nomino. Vionyeshi na vitenzi katika tungo virai vimewakilishwa na maumbo ya viambishi vipatanishi vya msingi vya kisintaksia ambavyo vilitumika kuonyesha au uwiano wa nomino inayovumishwa na vionyeshi husika. Data ya matokeo haya yanaendana na mihimili wa sarufi bia ambao hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo, yaani kuna vigezo vinavyozitofautisha lugha. utofauti unataokana na msingi wa umbo nje na nadani wa vionyeshi ambavyo hutumika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu.

Tofauti ya matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa Luganda hutumia vionyeshi vya mbali kidogo na mbali sana kwa nia ya kubadilishana kutegemea muktadha wa mawasiliano na umbali wa nomino inayokumushwa. Vilevile, katika Luganda baadhi ya nomino ambazo si za ngeli ya 1 na 2, hujikuta kutumia vionyeshi vya ngeli ya 1 na 2 kama inavyojitokeza katika data Na (5.23):

| | |
|--------------------------------|-----------------------|
| <i>Caayi ono talina sukari</i> | Chai hii haina sukari |
| <i>ffene oyo awooma</i> | Fenesi hilo ni tamu |

Aidha, Luganda vilevile huweza kudondosha nomino na kutumia vionyeshi kuwakilisha nomino katika mawasiliano. Hali ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu kama katika mifano (5.24) kutokana na Rose (2009) na Leah & Sseguya, (2015):

| | |
|-----------------------------------|--|
| <i>On'ani ayogela?</i> | nani anaongea? |
| <i>Oli'agambye ntino agwagala</i> | Yule amesema kuwa anakutaka/anakupenda |


Matokeo ya matumizi haya yanatokana na maelezo ya Iori, (2015) anayefafanua kuwa: Kivumishi kionyeshi huja baada ya neno kuu na hutangulia vivumishi vingine katika tungo

kulingana na nadharia tete kuwa ujumbe muhimu katika tungo hutokea kushoto mwa tungo virai [KN] hasa katika lugha zinazofuata utaratibu wa kuanza na kiima, kitenzi na kumaliza na shamirisho zake. Luganda na Kiswahili sanifu ikiwa miongoni mwa lugha ambishi bainishi zinazozingatia utaratibu huu wa mofosintaksia [KN na KT]. Aidha, Hannah Gibson, Rozenn Guérois and Lutz Marten (2018) wanaeleza kuwa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya lugha za Kibantu, licha ya kuonyesha ubia, vinatofautiana katika matumizi. Utafiti huu uligundua kuwa licha ya uwiano katika matumizi ya kanuni hii, Luganda na Kiswahili zilidhihirisha upekee wake katika matumizi ya vionyeshi kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi.

5.1.2.3.2 Kanuni ya kimofosintaksia ya maumbo ya vivumishi vionyeshi

Kanuni ya mofolojia ya vionyeshi inashikilia kuwa: Vivumishi vionyeshi ni vitatu ambavyo huwakilishwa na mofu (maumbo) ya kipekee inayotofautisha nomino moja na nyingine kisarufi kutegemea ujirani na umbali wake baina ya mzungumzaji na nomino inayokumushwa. Mofu zinazohusika ni mofu za kisarufi zinazodhihirisha upatanishi wa kisarufi, mizizi ya uundaji, nafsi, ngeli na idadi ya umoja na wingi. Kanuni hii inatokana na ufafanuzi wa vivumishi vionyeshi na wanaisimu kama vile Ashton (1982), Kapinga, (1983) Mohamed (2001), Chomi (2003), Habwe & Karanja (2004), Leah & Sseguya (2015) na Philipo, (2017).

Utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana katika matumizi ya vivumishi vionyeshi. Kimofosintaksia, Luganda na Kiswahili sanifu ilidhihirisha kutumia vivumishi vitatu ambavyo viliwakilishwa na mofu za kubainisha kionyeshi kimoja na kingine kutegemea nafasi tatu ya mzungumzaji na vipatanishi vya ngeli nomino kwa umoja na wingi. Vionyeshi hivi vina miundo yake ya kimofosintaksia inayotofautisha kiashiria kimoja na kingine kutegemea ngeli za nomino na upatanishi wa kisarufi wa nomino inayozungumziwa. Vionyeshi vya Luganda na Kiswahili vina maumbo ya kimofolojia inayotofautisha kiashiria cha ujirani, karibu na mbali kutegemea nafasi ya mzungumzaji na ngeli za nomino kiupatanishi (kisintaksia). Kila kionyeshi kinachokumushwa kiliwakilishwa na mofu za kisarufi zinazotofautisha kiashiria kimoja na kingine kulingana na ngeli nomino inayotajwa katika utungo na nafasi au mahali alipo mzungumzaji. Jedwali (4.12, Uk. 106) kutokana na Kisakwah, (2014); Obara, (2014) na Katamba, (2003), Leah & Sseguya (2015) pamoja na mchoro (M5.6) unaodhihirish uwiano na tofauti katika matumizi ya kanunu ya kimofosintaksia ya maumbo ya vivumishi vionyeshi kama inavyojitokeza katika mchoro (M5.6).



Asili: Kutokana na matokeo ya utafiti huu, (2021)

Kanuni ya mofosintaksia ya vionyeshi katika Luganda na Kiswahili sanifu huwakilishwa na maumbo ya Nafsi ya nomino [NfsN], mzizi [Mz], kiambishi kipatanishi cha msingi cha ngeli za nomino kuu [KPM Ng] irabu ya kiambishi kipatanishi cha nomino inayokumushwa [irabu-KPM] katika utungo. Kimofolojia vionyeshi vya Kiswahili ni vitatu vinavyowakilishwa na mizizi ya [h] na [-le]. Mzizi [h-] ni mzizi wa vivumishi vionyeshi vya ujirani na mbali kidogo na mzizi [-le] ni mzizi wa kivumishi kionyeshi cha mbali sana. Kivumishi cha vionyeshi vya nafsi ya kwanza na pili [h-], huambishwa irabu ya viambishi vipatanishi vya ngeli nomino na mzizi [-le] huambikwa viambishi vya upatanishi vya nomino (viambishi vya kisintaksia vya nomino). Aidha, kutofautisha vionyeshi vya ujirani na karibu au vivumishi vya urejeshi, kiambishi kirejeshi [-o] huwekwa mwishoni mwa viambishi irabu na VPM vya ngeli nomino katika muundo wa viwakilishi vya vivumishi vya mbali kidogo au karibu.

Kimpangilio, viambishi vya vivumishi vya ujirani na urejeshi, huwekwa mbele ya mzizi huku, vile vya nafsi ya kwanza vikiwekwa nyuma ya mzizi [-le]. Mathalan, utafiti huu ulitambua darajia ya mpangilio wa vionyeshi vya mbali hutofautiana na ule wa vivumishi vionyeshi vya ujirani na karibu ambapo, mzizi huja baada ya viambishi vipatanishi vya msingi vya ngeli nomino inayokumushwa. Viambishi vipatanishi vinavyoambishwa kwenye mzizi hutegemea nafasi ya nomino (mahali ilipo nomino) na viambishi vipatanishi msingi ambavyo vinatawaliwa na nomino. VPM hivi huonyesha uhusiano baina ya nomino inayokumushwa na vionyeshi kutegemea mahali ilipo nomino na mzungumzaji (Ngamau, 2004).

Tofauti ya matumizi ya kanuni hii, ni ya kimofolojia na kisintakisa baina ya maumbo ya vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu vina umbo na muundo unaotegemea nafasi ya mzungumzaji na msikilizaji ya kudhihirisha nomino iliyo karibu, mbali kidogo na mbali sana kulingana na ngeli za nomino. Hata hivyo, Luganda huwakilishwa na viashiria vya aina yake tofauti na Kiswahili sanifu kimaumbo na kimuundo kutokana na maumbo na muundo wa vionyeshi husika katika kila nafasi tatu kutegemea ngeli inayokumushwa. Tofauti hizi ni za kimofosintaksia, kimuundo, kimpangilio na utaratibu wa

uundaji wa vionyeshi husika. Data Na.(5.25) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya kimofosintaksia ya maumbo ya vionyeshi kutokana na Rose (2009) na Leah & Sseguya (2015) na Obara, (2014):

a) *Omutesitesi o-no ayagala kugenda waka.* *Abatesitesi bano bagala kugenda waka.*

| | | | |
|--------------|------------------|----------------|------------------|
| <i>O-</i> | <i>no</i> | <i>ba-</i> | <i>no</i> |
| <i>KbNg1</i> | <i>Mz nfsi 1</i> | <i>KPM Ng2</i> | <i>Mz nfsi 1</i> |

Msemaji **huyu** anataka kwenda nyumbani. Wasemaji **hawa** wanataka kwenda nyumbani.

| | | | | | | |
|------------------|--------------|-----------------|----------------|-----------|-----------------------|----------------|
| <i>h</i> | <i>-u</i> | <i>-yu</i> | <i>h-</i> | <i>a-</i> | <i>wa</i> | |
| <i>Mz nfsi 1</i> | <i>Irabu</i> | <i>-KPM Ng1</i> | <i>KPM Ng1</i> | <i>Mz</i> | <i>Irabu -KPM Ng1</i> | <i>KPM Ng2</i> |

b) *Omuchungwa ogwo gulabika bulungi.* *Emichungwa egyo gilabika bulungi.*

| | | | | | |
|----------------|----------------|---------------------|----------------|----------------|---------------------|
| <i>O-</i> | <i>gu-</i> | <i>o</i> | <i>e</i> | <i>gi</i> | <i>o</i> |
| <i>KbNgi 3</i> | <i>KPM Ng3</i> | <i>Mzizi nfsi 2</i> | <i>KbNgi 4</i> | <i>KPM Ng3</i> | <i>Mzizi nfsi 2</i> |

Mchungwa **huo** unapendeza. Michungwa **hiyo** inapendeza.

| | | | | | |
|---------------|--------------------------|-----------------------|----------------------|----------------------|------------------|
| <i>h-</i> | <i>u-</i> | <i>o</i> | <i>h-</i> | <i>i-</i> | <i>-o</i> |
| <i>Mz+KPM</i> | <i>- [irabu-KPM Ng3]</i> | <i>- Kmb Rej Nfs3</i> | <i>kirejeshi Mz-</i> | <i>irabu-KPM Ng3</i> | <i>kirejeshi</i> |

c) *Ekitabo kiri kirungi* *Ebitabo biri birungi*

| | | |
|-------------------------|--------------|-------------------|
| <i>Ki- ri</i> | <i>Bi-</i> | <i>ri</i> |
| <i>KNg7- Mz nafsi 3</i> | <i>KNg8-</i> | <i>Mz nafsi 3</i> |

Kitabu **Kile** ni kizuru vitabu **vile** ni vizuru

| | | |
|-------------------------|--------------|-------------------|
| <i>Ki- le</i> | <i>vi</i> | <i>le</i> |
| <i>KNg7- Mz nafsi 3</i> | <i>KNg8-</i> | <i>Mz nafsi 3</i> |

Asili: Data Kutokana na Leah & Sseguya, (2015)

Mifano (5.25) inadhihirisha uwiano na tofauti za maumbo ya kimofosintaksia ya vionyeshi vya Luganda na Kiswahili. Vionyeshi hivi vyote vimetumika kutegemea nafasi au mahali ilipo nomino inayokumushwa na mzungumzaji. Vionyeshi hivi ni vitatu vinavyodhihirisha ujirani, ukaribu na umbali wa nomino kutoka ngeli tofauti za [a-ba/ a-wa, gu-gi/u-I na ki-bi/ki-vi]. Hata hivyo imedhihirisha tofauti ya maumbo ya Mizizi, viambishi patanishi vya msingi, irabu za uwakilishi ngeli nomino kutokana na mfumo wa uainishaji wa ngeli kimofosintaksia kama inavyojitokeza katika mifano ya hapo juu. Maumbo na muundo huu wa viashiria umetawaliwa na nomino kuu pamoja na nafsi kwa umoja na wingi.

Matokeo ya uwiano na tofauti za kimaumbo ya kanuni hii yanashabihiana na matokeo ya Scottman (1970) ambaye katika utafiti wake kuhusu vikwazo vya upataji wa Kiswahili kama lugha ya pili miongoni mwa jamii za Baganda wanaopatikana nchini Uganda aligundua kuwa. matatizo ya upatanishi wa kisarufi ulijitokeza zaidi katika jamii ya Baganda hasa katika vionyeshi vya nafsi tatu, udondoshaji wa mofimu za nafsi na matumizi ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili visivyo sahihi katika matumizi.

5.1.2.3.3 Kanuni ya kimofonolojia ya vionyeshi

Kanuni ya kimofonolojia ua kanuni ya fonolojia ya vionyeshi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu inashikilia kuwa: uundaji wa vivumishi vionyeshi vya lugha za Kibantu huathirika na mabadiliko ya kimofonolojia ya fonimu kati ya viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) na fonimu inayotangulia mzizi. Vilevile, kanuni hii hushikilia kuwa: Kiambishi kipatanishi cha msingi kikianza ama na konsonanti au irabu, huweza kusabababisha mabadiliko au kuathiri fonimu jirani ambayo inapachikwa kwenye mizizi kama KPM (Chomi, 2003; Habwe & Karanja, 2004; Hyman & Katamba, 2012). Viambishi patanishi vya msingi [VPM] vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vionyeshi huathiriana kutokana na mfuatano au utokeaji wake katika mazingira ya fonimu irabu na konsonanti katika mfumo wa matumizi kimazungumzo na kimaandishi.

Kwa mujibu wa kanuni hii, Luganda na Kiswahili sanifu zilidhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya kimofonolojia katika uundaji wa vionyeshi vitatu vya ujirani/karibu, virejeshi na mbali sana. Mabadiliko yaliyojitokeza yalitokana na aina ya umbo jirani la irabu ya kipatanishi ngeli [irabu- KPM], kiambishi patanishi msingi [KPM] cha ngeli ambamo nomino kumushwa inainishwa na kirejeshi. Mabadiliko haya ndiyo yaliyotofautisha kionyeshi kimoja na kingine kati ya vitatu, kionyeshi cha nomino moja na nyingine na nafasi moja na nyingine ya nomino kuu. Hii ni kutokana na kuwa uambishaji wa VPM kwenye mzizi husababisha fonimu wakilishi ya kionyeshi kubadilika na kusaidia kubainisha kionyeshi kimoja na kingine, nomino na mahali ilipo kutegemea mzungumzaji. Kwa mujibu wa kanuni hii, Luganda na Kiswahili sanifu zilidhihirisha kanuni ya kifonolojia hasa katika uundaji wa vionyeshi virejeshi au vionyeshi vya mbali kidogo kwa umoja na wingi. Jedwali (5.4) na (5.5) linadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni hii ya kifonolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na Sharo, 2009), Leah & Sseguya, (2015), Katamba, (1993:2003) na Baertlein & Ssekitto, (2014), Chomi, (2003) na Mgullu, (1999).

Jedwali 5.3: Kanuni ya kifonolojia ya vivumishi vionyeshi rejeshi katika Luganda

| Ngeli | Mzizi KbNgKPM | KPM Ng | Mofu rej-o | Kanuni | Kionyeshi |
|-------|------------------|-----------|------------|--|-----------|
| a/yo | o | yu | o | [u-o] udondoshaji /u/ | oyo |
| a-ba | a | ba | o | [a-o] udondoshaji /a/ | abo |
| gu | o | Gu | o | [u-o] muunganiko na uongezaji /o/ | Ogwo |
| gi | e | Gi | o | [i+o]=/y/ + o uyeyeshaji/ uongezaji | Egyo |
| li | e | Li | o | [l-r] + [i-o] mpishano huru + uongezaji fonimu rej /-o/ | Eryo |
| ga | a | Ga | o | [a-o] udondoshaji /a/ | Ago |
| ki | e | Ki | o | [k+i]=/y/ +[o] uyeyushaji (irabu kuwa nusu irabu) + uongezaji /o/ | Ekyo |
| bi | e | Bi | o | [b+i]=/y/+o uyeyushaji (irabu kuwa nusu irabu) + uongezaji /o/ | Ebyo |
| ka | a | Ka | o | [a-o] udondoshaji /a/ uyeyushaji na uongezaji /o/ | Ako |
| bu | o | Bu | o | [u-o] muungano [w]+ kuongeza kirejeshi [o] | Obwo |
| lu | o | Lu | o | [u-o] uongezaji + uongezaji [o] | Olwo |
| zi | e | Zi | o | [i-o] udondoshaji /i/ | Ezo |
| gu | o | Gu | o | [u-o] muungano + uongezaji kirejeshi [o] | Ogwo |
| ga | a | Ga | o | [a-o] udondoshaji /a/ | Ago |
| ku | o | Ku | o | [u-o] muungano + uongezaji kirejeshi [o] | Okwo |
| ga | a | Ga | o | [a-o] udondoshaji /a/ | Ago |
| tu | | Tu | o | [u-o] muungano + uongezaji kirejeshi [o] | Otwo |

Asili: Data Kutokana na Baertlein & Ssekitto, (2014), Katamba, (1993:2003)

Jedwali 5.4: Kanuni ya kifonolojia ya vivumishi vionyeshi rejeshi vya Kiswahili sanifu

| Ngeli | Mzizi | i-KPM | KPM | mofu rej-o | Kanuni | kionyeshi |
|-------|-------|-------|-----|------------|---|-----------|
| a/yu | h | u | Yu | o | [u-o] udondoshaji | Huyo |
| wa | h | a | Wa | o | [a-o] udondoshaji | Hao |
| u | h | u | U | o | [a-o]udondoshaji /a/ | Huo |
| i | h | i | I | o | [i+o] + o=/y/ +o uyeyeshaji na uongezaji fonimu /y/ | Hiyo |
| li | h | i | Li | o | [i-o] udondoshaji /i/ | Hilo |
| ya | h | a | Ya | o | [a-o]udondoshaji /a/ | Hayo |
| ki | h | i | Ki | o | [k+i]-/tʃ/ + o ukakaishaji na uongezaji /o/ rej | Hicho |
| vi | h | i | Vi | o | [v+i]=/vy/+o] ukakaishaji na uongezaji /o/ rej | Hivyo |
| i | h | i | I | o | [i-o] +o = /y/o (vokali kuwa nusu irabu) Uyeyushaji na uongezaji /o/ | Hiyo |
| zi | h | i | Zi | o | [i-o] udondoshaji /i/ | Hizo |
| u | h | u | U | o | [u-i] udondoshaji /u/ | Huo |
| zi | h | i | Zi | o | [i-o] udondoshaji /i/ | Hizo |
| u | h | u | U | o | [u-o] udondoshaji /u/ | Huo |
| ya | h | a | Ya | o | [a-o] udondoshaji /a/ | Hayo |
| ku | h | u | Ku | o | [u-o] udondoshaji /u/ | Huko |
| pa | h | a | Pa | o | [a-a] udondoshaji /a/ | |
| ku | h | u | Ku | o | [u-o] udondoshaji /u/ | Huko |
| mu | h | u | Mu | o | [u-o] udondoshaji /u/ | Humu |

Asili: Data kutokana na uchanganyuzi wa Chomi, 2003; Habwe & Karanja, (2004) na Mgullu, (1999)

Majedwali haya (5.3 na 5.4) yanadhihirisha mshabihiano uliopo wa matumizi ya vionyeshi kuathirika na kanuni ya fonolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Mifano hii inadhihirisha pia tofauti zinazojitokeza katika maumbo na baadhi ya kanuni zinazoathiri kila fonimu inayotumika katika vivumishi vionyeshi. Kanuni zilizokolezwa katika Luganda, zinadhihirisha kushabihiana na zilizobaki zinadhihirisha tofauti ambayo hujitokeza wakati wa matumizi ya kanuni ya kifonolojia baina ya yake na Kiswahili sanifu.

Tofauti nyingine iliyojitokeza ni kuwa Luganda hukumbwa na mabadiliko ya kifonolojia katika vionyeshi vya urejeshi. Vionyeshi vya ujirani na mbali havionyeshi athari ya kifonolojia kinyume na Kiswahili sanifu ambayo ilionyesha matumizi ya kanuni hii katika vivumishi vya ujirani ambapo kanuni ya kifonolojia ya ukaakaishaji ulijitokeza katika ngeli ya 7 na 8, udondoshaji wa fonimu katika ngeli ya 5 na 6 zilijitokeza. Vivumishi vya mbali havikuweza kudhihirisha utokeaji wa kanuni ya kifonolojia katika Luganda na Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Mgullu, (1999), Habwe & Karanja, (2004), Mbwillow, (2017), Philipo, (2012) wanaeleza kuwa, vivumishi vionyeshi ni vitatu. Vionyeshi hivi vimeundwa kwa kuongeza viambishi vipatanishi kwenye mizizi maalumu. Uambishaji huu hutokea kabla au baada ya mzizi. Katika uundaji wa vionyeshi hivi vitatu vya ujirani, karibu na mbali, mabadiliko mbalimbali ya kimofonolojia hutokea. Mabadiliko haya ndiyo yanayotofautisha kisheria matumizi ya kiambishi cha ngeli moja na nyingine, kutegemea nafasi ya nomino na mahali alipo mzungumzaji. Matokeo ya utafiti huu yanashadidiwa na yale ya Owino (2016) ambaye anedhihirisha kuwa;

“Mifanyiko japo huweza kufafanuliwa katika lugha zote, kwa jumla si jumuishi. Mfanyiko kama vile udondoshaji huweza kudhihirika kwa njia tofauti baina ya lugha mbili au zaidi kwa kulinganishwa. Mifanyiko hii ina upekee wake kutegemea lugha husika.”

Matokeo ya utafiti huu yanashabihiana na ufafanuzi wa Owino (2016) kwani kuna uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya kimofolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Hali ambayo inaendana na mihimili ya sarufi bia na upatanifu wa nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981).

5.1.2.3.4 Kanuni ya utaratibu wa kidarajia ya utokeaji wa vionyeshi katika tungo.

Kanuni hii inashikilia kuwa: Vivumishi huchukua nafasi karibu na nomino kama neno kuu katika tungo virai hasa katika Lugha za Kibantu (Rijkhoff, 1986). Aidha, Lusekelo, (2017) anaeleza kuwa vivumishi vionyeshi katika lugha za Kibantu hasa Kiswahili huweza kuanza na vionyeshi ambavyo huchukuwa nafasi ya kuwa viwakilishi vya nomino. Anatoa mfano wa ‘wale watoto wawili’ ambapo [wale] ni kionyeshi cha mbali ambacho kimechukua nafasi ya nomino kama neno kuu ikifuatwa na nomino na kivumishi cha idadi. Katika hali kama hii, inadhihirisha kuwa “kivumishi kikitangulia katika nomino, huwa si kivumishi bali huwa kiwakilishi cha nomino [pronomino] kwa sababu katika sentensi hii, kivumishi kimetokea mwishoni [wawili]. Baada ya Kuhitimisha ufafanuzi wake, alieleza kuwa utaratibu wa matumizi ya vivumishi vionyeshi na vivumishi vingine katika Lugha ya Kiswahili sanifu hutawaliwa na kanuni ya kimuktadha kutegemea ujumbe wa mzungumzaji na ukuu wa elementi au kivumishi kionyeshi katika KN. Data za Ndomba, (2006), Rugemalira, (2007) na Iori, (2015), Heine, (1976) Mojaipelo (2007) na Abudonia, (2014) zilidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni hii kuzingatia mihimili ya ubia na upatanishi wa kisarufi baina ya Luganda na Kiswahili. Iligunduliwa kuwa vivumishi vingi katika Lugha ya Kiswahili na Luganda sanifu hutokea kutokana na ukuu na hadhi ambayo kivumishi fulani hubeba katika

KN. Vivumishi vyote katika Kiswahili na Luganda sanifu ulitokea baada ya nomino kuu na sifa za kisarufi za utokeaji wake ulitokana na neno kuu. Hata hivyo, utokeaji wake ulitokana na muktadha au kanuni ya pragmatiki yaani kutegema dhima, hadhi na ujumbe unaowasilishwa. Data Na. (5.26) inadhihirisha data za uwiano na tofauti za kanuni ya utaratibu wa kidarajia ya utokeaji wa vionyeshi katika tungo kutokana na matokeo ya utafiti huu, (2021):

- | | |
|---|--|
| a) Ono omwana mulungi | Bano abaana balungi |
| <i>Kio N V</i> | <i>Kio N V</i> |
| b) Huyu mtoto mzuri | Hawa watoto wazuri |
| <i>Kio N V</i> | <i>Kio N V</i> |
| c) Omwana ono mulungi | Abaana bano balungi |
| <i>N Kio V</i> | <i>N Kio V</i> |
| d) Mtoto huyu mzuri | Watoto hawa wazuri |
| <i>N Kio V</i> | <i>N Kio V</i> |
| e) Omusomesa wange alezze emmotoka eyo | Abasomesa waffe balezze mmotoka ezo |
| <i>N V T N Kio</i> | <i>N V T N Kio</i> |
| f) Mwalimu wangu alileta gari hilo | Walimu wetu walileta magari hayo |
| <i>N V T N Kio</i> | <i>N V T N Kio</i> |

Asili: Data kutokana na data za Lusekelo, (2017) na Kiyinikibi, (2021)

Vishazi hivi vinaonyesha matumizi ya vionyeshi katika nafasi tatu ya utokeaji. Mwanzoni, kati na mwishoni. Vishazi (a-b) vimetanguliza kionyeshi kabla ya nomino, (c-d) vionyeshi vimetoka baada ya nomino kuu na (e-f) kionyeshi kikatoka mwishoni lakini baada ya nomino kuu ya kwanza na pili. Utokeaji au utaratibu huu, ulidhihirisha kuwa matumizi ya vionyeshi katika Luganda na Kiswahili sanifu hutegemea muktadha wa dhima, ukuu na ujumbe unaowasilishwa.

Tofauti iliyojitokeza ya kidarajia ya utokeaji wa vionyeshi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa kila lugha ina viashiria vyake ambavyo vinatumika kulingana na upatanisho wa kisarufi wa ngeli za nomino kianafora. Sentensi (a-b) zilizoanza na kionyeshi ni sentensi ambayo muktadha wake ni wa kimaana wenye sifa za kimofosintaksia wa kufafanua zaidi juu ya sifa za nomino na sio kuashiria mahali ilipo. Hii inatokana na kuwa ufafanuzi zaidi wa nomino ni wa kivumishi cha sifa [mulungu/mzuri] na udhihirishaji wa mahali ilipo unajitokeza baadaye kianafora. Kumaanisha kuwa dhima ilikuwa ni ya kueleza sifa na baadaye kuashiria nomino kulingana na sifa zake. Matumizi ya viwakilishi vionyeshi hupitia

mchakato ambao huathirika na mabadiliko ya kifonolojia ambayo hutofautiana kutokana na kuwa kila lugha hufuata mfumo wa kifonolojia wa matumizi ya fonimu za lugha. Data Na. (5.27) inadhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni za utaratibu wa kidarajia ya utokeaji wa vionyeshi katika tungo kutokana na Chomi, (2003), Habwe & Karanja, (2004), Allen (2014):

Kiswahili sanifu

| Ng | mzizi | irabu-Kp | KPM | Kio |
|-----------|----------|----------|-----------|-------------|
| <i>u</i> | <i>h</i> | <i>u</i> | <i>u</i> | <i>huu</i> |
| <i>i</i> | <i>h</i> | <i>i</i> | <i>i</i> | <i>hii</i> |
| <i>li</i> | <i>h</i> | <i>i</i> | <i>li</i> | <i>hilo</i> |
| <i>ya</i> | <i>h</i> | <i>a</i> | <i>ya</i> | <i>haya</i> |

Asili: Chomi, (2003), Habwe & Karanja, (2004),

Luganda sanifu

| <i>Ngeli</i> | <i>KbNgKPM</i> | <i>KPM Ng</i> | <i>Mzizi</i> |
|--------------|----------------|---------------|--------------|
| <i>gu</i> | <i>o</i> | <i>gu</i> | <i>no</i> |
| <i>gi</i> | <i>e</i> | <i>gi</i> | <i>no</i> |
| <i>li</i> | <i>e</i> | <i>li</i> | <i>li</i> |
| <i>ga</i> | <i>a</i> | <i>ga</i> | <i>li</i> |

Asili: Data kutokana na Allen (2014), Abudonia, (2014).

Sentensi hii ina vivumishi vya ujirani au karibu [*guno/huu* na *gino/hii*] baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Mchakato wa uundaji wa vivumishi hivi unafanana (uambishaji wa vipatanishi ngeli) ila vionyeshi husika vinatofautiana kutokana na kila lugha kuwakilishwa na viwakilishi vyake, mpangilio wa uambishaji, uambishaji wa viambishi patanishi msingi kwenye mizizi na mabadiliko ya kifonolojia kutokana na kuathiriana kwa fonimu irabu na konsonanti katika mazingira ya fonimu ya mwanzo ya mzizi wa kionyeshi. Pia Luganda hutumia viambishi ngeli (Ngeli), vibainishi patanishi vya ngeli (KbNgKPM), viambishi patanishi msingi vya ngeli nomino (KPM Ng) na mzizi (Mz). Vibainishi hutumika zaidi katika kionyeshi cha mbali. Tofauti na Kiswahili sanifu ambayo hutumia viambishi vya upatanishi vya ngeli (Ng), mzizi, irabu ya kiambishi kipatanishi (irabu-Kp) na kiambishi patanishi msingi (KPM).

Matokeo ya matumizi ya kanuni hii yameelezwa pia katika kazi za Ndomba (2006), Rugemalira (2007) na Iori (2015) wanaofafanua kuwa: Kanuni ya utaratibu wa kidarajia ya utokeaji wa kategoria za maneno katika lugha nyingi za Kibantu hushikilia vivumishi


vionyeshi na vimilikishi kuchukua nafasi karibu na nomino kuu (neni kuu) katika tungo virai. Abudonia (2014) anaunga mkono maelezo ya wataalamu hawa akieleza kuwa Luganda sanifu huzingatia utaratibu wa kivumishi kufuata nomino kuu katika KN. Utokeaji wake hutawaliwa na kanuni ya kipragmatiki ya kubainisha kategoria ya kivumishi kipi kifuata kipi kulingana na hadhi (ukuu wa kivumishi) ya kivumishi husika katika KN. Utafiti huu ulibaini uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Licha ya kuwiana katika nafasi ya vionyeshi, maumbo wakilishi ya vionyeshi kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu ulitofautiana.

5.1.2.3.5 Kanuni ya umilikishi au upatanishi wa kisarufi wa Vivumishi Vionyeshi

Kanuni hii inadai kuwa upatanifu wa kisarufi katika utungo hutawaliwa na vipashio vya kimfosintaksia na vipashio hivyo huathiriana ambapo kipashio cha kwanza hutegemea sana kipashio cha pili ili kuleta maana (Chomsky, 1957; 1965). Aidha, Chomi (2003) anafafanua kuwa nomino kuu hutawala vivumishi kwa kuakisiwa katika miundo ya maneno ya kategoria husika.

Uchanganuzi wa data za upekuzi na usomaji wa Ichoe, (2005), Chomsky, (1957; 1965). Ngamau, (2004) na Egara, (2016), Chomi (2003) ulibaini kuwa matumizi ya viambishi vipatanishi vya kimofolojia na kisintaksia katika uundaji wa viambishi vipatanishi vya msingi vilivyopachikwa kwenye mizizi ya vionyeshi kutegemea kundi nomino ambamo nomino husika huainishwa. Viambishi hivyo hudhihirisha uhusiano wa KN na KT ambapo KN huwakilisha maumbo ya nomino ambayo huathiri maumbo ya maneno mengine katika tungo. Viambishi vinavyotumika katika KN ni maumbo ya kimofolojia na maumbo yanayojitokeza katika KT ni maumbo ya upatanishi wa kisarufi yanayoonyesha uhusiano wa viambajengo au kategoria za maneno katika tungo. Vionyeshi vingi viliathirika na maumbo ya kisintaksia yaliyojitokeza katika vitenzi kimrejeosabaki au kutegema nomino kuu katika tungo. Kila kiashiria kimechukua kiambishi ngeli cha upatanishi wa nomino inayozungumziwa (Ngamau, 2004 na Egara, 2016) kama inavyojitokeza katika data za mchoro (M5.7).

Kanuni ya umiliki baina ya Luganda na Kiswahili sanifu



Kanuni ya upatanishi wa kisarufi katika Luganda inadhihirika kupitia kwa muundo wa vionyeshi. Kionyeshi hiki kimeundwa na kiambishi patanishi cha nomino [ga] ambacho kimeambishwa mwanzoni mwa mzizi {no}. Kiambishi hiki cha upatanishi kimejitokeza katika vitenzi kudhihirisha upatanisho wa kisarufi. Maumbo yaliyopachikwa mwanzoni mwa vitenzi ndiyo maumbo yaliyokaririwa katika kionyeshi kudhihirisha upatanishi wa kisarufi katika KN na KT. Maumbo haya yamejitokeza kianafora kuwakilisha nomino {amaaso} inayosababisha maumbo ya upatanishi wa kisarufi wa vionyeshi katika KN na KT. Aidha, Luganda ilitumia vibainishi ngeli pamoja na viambishi vya kisintaksia vya nomino kudhihirisha upatanisho wa kisarufi wa vionyeshi katika tungo. Viambishi vibainishi na vipatanishi hutangulia na kufuatwa na mizizi ya vionyeshi kama ilivyokolezwa katika mifano (5.28) ifuatayo kutokana na matokeo ya utafiti huu:

Eliso {li-no, e-ly-o, li-li} {Umoja} Amaaso {ga-no, a-go, ga-li} {Wingi}(Luganda)

Jicho hili, hilo, lile

macho {haya, hayo, yale} (Kiswahili)

Katika Kiswahili, {ya} ni umbo la kimfosintaksia la kategoria za maneno ambayo huunda nomino na kionyeshi. Umbo hili limetumika kiupatanishi kuwakilisha nomino [matunda] ikidhihirisha sifa za kisarufi za ngeli na idadi ya umoja na wingi. Kiambishi [ma] cha kimofolojia cha nomino [matunda] kimewakilishwa na kiambishi cha upatanishi wa kisarufi wa nomino {ya}. Kiambishi hiki kiliwakilisha nomino {matunda} kilichotajwa awali (anafora). Uhusiano huu wa kiambishi kiwakilishi cha nomino awali kilitumika katika kitenzi kudhihirisha urejeleo nyuma wa maumbo yanayowakilisha upatanishi wa kisarufi katika tungo. Hali hii ni hali inayodhihirisha kanuni ya upatanishi wa kisarufi ambapo mahusiano ya utawala wa viambajengo ulijitokeza kianafora na kikatafora. Nomino kama neno kuu katika KN imemiliki kionyeshi kupitia kwa umbo la viambishi vipatanishi msingi vilivyopachikwa kwenye kionyeshi. Na uundaji wa kionyeshi umetokana na maumbo ya kimfosintaksia ya nomino na kipatanishi chake katika KT.

Kikanuni, utafiti huu uligundua kanuni ya umiliki wa vionyeshi iliyoshikilia kuwa: Upatanishi wa kisarufi wa matumizi ya vionyeshi (katika Luganda na Kiswahili sanifu) hutokana na viambishi vya upatanishi wa kisarufi au umiliki wa kuambisha mwanzoni mwa vitenzi katika KT ndiyo yanayokaririwa katika maumbo ya vionyeshi yanayopachikwa ama mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa vionyeshi. Viambishi hivyo au maumbo hayo hutokana na nomino kama neno kuu hasa kutokana na kundi ambamo nomino hiyo huainishwa kimofolojia na kisintakisa. Kanuni hii inajitokeza kimrejeosabaki ambapo viambishi vipatanishi vya msingi vinavyowekwa kwenye kionyeshi hujitokeza kianafora na

kitafora. Aidha Viambischi vipatanishi vya msini (VPM) huweza kupita mchakato wa kifonolojia ambapo baadhi huweza kuathirika katika mazingira ya utokeaji wa irabu na konsonanti kutokana na fonimu za mwanzoni mwa mizizi.

Tofauti inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili kuhusu kanuni hii ni ule mchakato wa uambishaji. Luganda huambisha maumbo ya kiupatanishi mwanzoni kutumia viambishi vibainishi na viambishi vipatanishi vya kisarufi katika uundaji wa vionyeshe vitatu vya karibu mbali na mbali sana kutegemea mahali alipo mzungumzaji. Nafasi ya pili ndiyo inayotumia sana vibainishi pamoja na viambishi vipatanishi vya ngeli kisintaksia. Vilevile, ni nafsi hii pekee inayopata na mabadiliko ya kifonolojia katika uundaji wa vionyeshi virejeshi (nafasi ya pili) mizizi ya vivumishi vya Luganda na [-no, -o na -li] mizizi hii huambishwa viambishi vipatanishi vya msingi na vibainishi ngeli mwanzoni. Luganda inatumia kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino inayozungumziwa na mzizi wake [-no] ambao huwekwa baada ya kiambishi ngeli cha upatanishi ijapokuwa ngeli ya kwanza ambayo hutumia viambishi tofauti vya [ono na oyo] karibu na mbali sana. Kiswahili hutumia mizizi {h-} kikifuatwa na irabu ya upatanishi kutegemea kipatanishi cha nomino tajwa na kipatanishi cha nomino inayozungumziwa. (vipatanishi vya ngeli) ambapo viambishi hupachikwa baada ya mzizi katika nafsi ya kwanza na pili na kabla ya mzizi katika nafsi ya tatu umoja na wingi. Mzizi wa nafsi ya tatu ni {-le} ambao huchukua viambisshi vipatanishi vya nomino vinavyopachikwa kwenye vitazi. Kila kiashiria (mzizi) huchukua kiambishi ngeli cha upatanishi wa nomino inayozungumziwa. Viashiria vya karibu vya Kiswahili vimeundwa kwa mzizi wa kivumishi {h-}, kikifuatwa na irabu ya upatanishi kutegemea kipatanishi cha nomino tajwa na kipatanishi cha nomino inayozungumziwa (vipatanishi vya ngeli). Luganda inatumia kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino inayozungumziwa na mzizi wake {-no} ambao huwekwa baada ya kiambishi ngeli cha upatanishi ijapokuwa ngeli ya kwanza ambayo hutumia viambishi tofauti vya {ono na oyo} karibu na mbali sana.

Matokeo haya yanaelezwa pia na Sylvain, (2020), Oduor, Inyani & Kobia (2013). walioeleza kuwa Viashiria hutumika kulingana na nomino kuu katika utungo viambishi vinavyojitokeza katika mizizi ya viashiria hubeba sifa za kisarufi za kisintakisa. Hii ina maana kuwa viambishi hivi ni viambishi patanishi vinavyotumika katika KN na KT kuonyesha uwiano tofauti kati ya nomino na vivumishi. Kila nomino huwa na viambishi vipatanishi vyake vinavyoonyesha uhusiano wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo. Aidha, wataalamu hawa (washatajwa) wanadai kuwa, lugha mbili za Kibantu

zinapotofautiana kwa viashiria vya kimofimu, bila shaka kuathiriana hudhihirika. Hii ina maana kuwa matumizi ya viashiria vifaavyo hutokana na matumizi ya viambishi vipatanishi mwafaka. Ukiukaji wa kuambisha viambishi vipatanishi visivyofaa huweza kauthiri usanifu lugha husika. Aidha, Oichoe (2005), anaungana na wataalamu, akieleza kuwa, “*Vivumishi pia huwa na upatanishi na nomino zinazovumishwa navyo.*” (Oichoe, 2005:58). Anaendelea kusema kuwa, “*Katika lugha ya Kiswahili, vionyeshi hivi huundwa kutokana na mzizi ha- hi - na hu- kisha unafuatwa na viambishi vya upatanishi vya nomino kuambatana na ngeli*” (Oichoe, 2005:61). Matokeo ya utafiti huu yalitambua kuwiana na kutofautiana kwa matumizi ya kanuni hii licha ya kuwa lugha hizi ni za nasaba moja.

5.1.2.4 Uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya Vivumishi vya Sifa

Vivumishi vya sifa ni maneno ambayo hutumika kutoa au kufafanua sifa za jinsi nomino inavyoonekana. Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha ambazo hutumia vivumishi vya sifa kuelezwa zaidi juu ya nomino kwa kuonyesha hulka au jinsi au mwonekano wa nomino tajwa katika mazungumzo na maandishi yao. Sheria mbalimbali huhusika katika kuzingatia usanifu wa matumizi ya vivumishi vya sifa kimofosintaksia kuelezea zaidi hulka au sifa fulani za nomino zinazokumushwa (Mgullu, 1999; Habwe & Karanja, 2004).

5.1.2.4.1 Kanuni za Kimofosintaksia ya vivumishi vya sifa


Kanuni hii inashikilia kuwa: Kila lugha huwa na maumbo ya kipekee yanayotumika kuunda vipashio vya kisarufi vya lugha kuwakilisha usahihi wake kimatumizi. Maneno ya lugha huundwa kwa vipande vidogo vidogo vinavyowekwa pamoja kwa mpangilio na utaratibu maalumu kujenga maana ya msingi ya maneno ya lugha (Massamba na wenzake, 1993). Matokeo ya uchanganuzi wa upekuzi wa maandishi ya Habwe & Karanja, (2004), Oichoe, (2005), Dixon, (2010) na Leah & Ssuguya, (2015) ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hudhihirisha matumizi ya kanuni ya kimosintaksia ya vivumishi vya sifa. Ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ilitumia kanuni hii kwa kuzingatia Mofolojia ya uambishaji wa viambishi patanishi vya msingi kwenye mizizi ya visifa ambao ulizingatia sifa za kisarufi za upatanishi wa kisarufi wa nomino kama neno kuu. Upatanishi huu wa kisarufi ulidhihirika kimofolojia na kisintaksia. Maumbo ya viambishi vilivyoambishwa kwenye mzizi wa vivumishi vilifanana na viambishi awali vilivyoambishwa kwenye mizizi ambishi ya vivumishi vya sifa ila vivumishi vya mkopo. Viambishi hivi vilidhihirisha sifa za kisarufi za ngeli nomino, upatanishi wa kisarufi na idadi ya umoja na wingi ambayo ilionyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi katika tungo.

Kwa hiyo kanuni ya vivumishi ya kimofosintaksia ni ile inayozingatia matumizi ya viambishi patanishi vya msingi kwenye mizizi ya kivumishi cha sifa kifaacho kulingana na ngeli nomino na idadi kudhihirisha upatanishi wa kisarufi kati ya jozi ya nomino na kivumishi. Kanuni ya kimofolojia inayohusika katika Luganda na Kiswahili sanifu ni ile inayoshikilia kuwa: Viambishi vinavyopachikwa kwenye mzizi wa kivumishi lazima vipatane au kufanana na viambishi vya kiima au nomino kuu katika KN. Kiambishi hiki huwekwa kabla ya mzizi kudhihirisha sifa za kisarufi wakati wa matumizi ili kuzingatia usarufi wa matumizi ya vivumishi vya sifa. Mifano katika Jedwali (4.13, Uk. 110) inadhihirisha data ya uwiano na tofauti ya matumizi ya mzizi wa kileksika wa kivumishi cha sifa baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, data (5.29) ya data kutokana na matokeo ya utafiti kutokana na data za maktabani yalidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya kimofosintaksia katika Luganda na Kiswahili sanifu. (5.29):

- | | |
|---|-------------------------------------|
| a) <i>Omwana omulungi amanyi okusoma</i> | Mtoto mzuri anajua kusoma |
| b) <i>Abaana abalungi bamanyi okusoma</i> | Watoto wazuri wanajua kusoma |
| c) <i>Ekitabo ekirungi kibuzze</i> | Kitabu kizuri kimepotwa |
| d) <i>Ebitabo ebirungi bibuzze</i> | Vitabu vizuri vimepotea |

Data kutokana na Abodunia (2014) na Chesswas (1967)

Mchoro (M5.8) wa kanuni za kimofosintaksia za vivumishi vionyeshi katika mchoroti



Mifano ya mchoro (M5.8), data katika jedwali (4.13, Uk. 110) na mifano katika data (5.29) inadhihirisha viambishi vya kimofolojia vya uundaji wa vivumishi vya sifa katika Luganda na Kiswahili sanifu kukubaliana na nomino zinazokumushwa. Miundo ya viambishi awali vya ngeli nomino hufanana na viambishi awali vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vivumishi vya sifa katika KN. Mizizi ya vivumishi vya sifa havibadiliki. Kisintaksia viambishi vinavyoambishwa kwenye maneno mengine katika KT huathirika na nomino kuu inayokumushwa. Kwa hiyo viambishi vipatanishi vya ngeli nomino husika huambikwa nyuma ya nomino kuwakilisha sifa za kivumishi na kimofosintaksia za nomino



inayokumushwa kimrejeosabiki. Mifano ya data (5.30) unadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni kwa mujibu wa uchanganuzi wa utafiti huu, (2021):

Kanuni za kimofosintaksia za vivumishi vya sifa



Anafora

katafora



Anafora -umiliki

katafora- utawala

Tofauti inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili ni kuwa hata ingawa vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli kiupatanifu, mfumo wa mpangilio wa nomino wa Luganda na Kiswahili kiasili unatofautiana na Kiswahili hivyo kila lugha kudhihirisha viambishi vinavyotofautiana kimofosintaksia. Pia viambishi vinavyotumika huathiriana kifonolojia na kujenga viambishi vipatanishi vya msingi vinavyotofautiana na VPM vya Kiswahili sanifu kutokana na michakato tofauti inayotumika wakati fonimu zinapotokea katika mazingira ya vokali na konsonanti ya mizizi. Kwa mfano, Luganda ilidhihirisha kutumia vibainishi na viambishi vipatanishi vya msingi tofauti na Kiswahili sanifu kilichotumia viambishi vipatanishi msingi peke yake.

Matokeo haya yanaona na ya Oichoe, (2005) anayefafanua kuwa: Vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli vya upatanishi wa kisarufi vinavyohusiana na sifa ya nomino iliyotajwa. Aidha, Kisakwah (2014) na Rose, (2009) katika kueleza juu ya vivumishi vya Luganda walidhihirisha kuwa, kimofosintaksia, Luganda na Kiswahili huambisha maumbo ya viambishi awali vya nomino kwenye mizizi inayobeba maana ya kileksika ya vivumishi vya sifa. Walieleza kuwa maumbo hayo hutoa taarifa zaidi za kisarufi za nomino inayotajwa kuonyesha uhusiano wa kumiliki na kutawala maneno mengine katika tungo. Tofauti na utafiti wa Kisakwah (2014) uliotambua tofauti ya kanuni ya kimofosintaksia ya uambishaji wa viambishi baina ya Kisuba na Kiswahili, utafiti huu uligundua kuwa viambishi vinavyoambikwa kwenye mizizi ya vivumishi hutofautiana kutokana na tofauti za maumbo ya ngeli pamoja na athari za kifonolojia ambazo hutokea katika lugha kati ya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyothibitishwa na Nurse na Philippon, (2014) na Katamba, (2003).

5.1.2.4.2 Kanuni ya kofonolojia

Kwa mujibu wa Kim (1999), Chomi (2003), Habwe & Karanja (2004) na Katamba (1993) Kanuni ya kimofonolojia au kanuni ya fonolojia ya vivumishi vya sifa inashikilia kuwa: uundaji wa vivumishi vionyeshi vya lugha za Kibantu huathirika na mabadiliko ya kimofonolojia ya fonimu kati ya VPM na fonimu inayotangulia mzizi. Vilevile, kanuni hii hushikilia kuwa: Kiambishi kipatanishi cha msingi kikianza ama na konsonanti au irabu, huweza kusabababisha mabadiliko au kuathiri fonimu jirani ambayo inapachikwa kwenye mizizi kama KPM . Viambishi patanishi vya msingi [VPM] vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vionyeshi huathiriana kutokana na mfuatano au utokeaji wake katika mazingira ya fonimu irabu na konsonanti katika mfumo wa matumizi kimazungumzo na kimaandishi. Kwa hiyo, matumizi ya vivumishi vya sifa lazima uzingatie mabadiliko ya kimofonolojia yanayojitokeza baina ya VPM na mizizi ya visifa ili maandishi na mazungumzo yadhahirishe usanifu wake. Matumizi ya visifa pasi kuzingatia fonolojia sahihi ya fonimu kimazungumzo na kimaandishi hupotosha usahihi au usanifu wa lugha inayohusika.

Kupitia kwa uchanganuzi wa data za maktabani za Chomi (2003), Katamba (1993), Kim (1999), Otiende (2013), Ontieri (2016), Leah & Sseguya (2015) na Baertlein & Ssekitto (2014) na Hyman & Katamba (2012), utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hudhahirisha matumizi ya kanuni hii kwa kuhakikisha kuwa maandishi na mazungumzo yanayotumika yanafuata fonolojia ya lugha zao. Matumizi haya hujitokeza katika maandishi na mazungumzo kwa kuhakikisha kuwa viambishi patanishi vya msingi vinavyotumika wakati wa uambishaji vinafuata mchakato wa kifonolojia unaofaa kwa kila nomino na ngeli nomino. Wazungumzaji na waandishi huhimizwa Kutumia viambishi awali vya nomino (kimofolojia) kama viambishi vipatanishi msingi vya vivumishi vya sifa katika sehemu ya kwanza ya KN bila kuingiza viambishi vya kisintaksia kwenye mizizi ya visifa. Viambishi vya kisintaksia vilijitokeza katika KT kuonyesha uhusiano uliopo kati ya KN na KT kujenga mofosintaksia sahihi ya matumizi ya vivumishi vya sifa ili kukidhi matilaba ya kanuni. Data Na. (5.31) ilidhahirisha baadhi ya kanuni za kimofonolojia ambazo zilizingatiwa katika Mchakato wa Luganda na Kiswahili sanifu:

Luganda sanifu

Omuntu omuerufu

Omupiira mueru

Ekitabo akieru

Enyumba zilungi

omuntu omwerufu

omupiira mweru

ekitabo ekyeru

enyumba ndungi

Kiswahili Sanifu

Muungano na uyeyushaji

Muungano na uyeyushaji [/u/-u-w]

Uyeyushaji/muungano /-i/- e /y/

Udondoshaji wa KPM na l -nd

Esaati empya *esaati empya* Udondoshaji wa n na kutumia /m/ katika
Mazingira ya /b na p/ hubadilika na kuwa /m/

Asili: Data za utafiti Kutokana Leah & Sseguya, (2015) na Katamba, (1993).

Kiswahili sanifu

| <i>Ngeli</i> | <i>KPM</i> | <i>Mz</i> | <i>V</i> | <i>kanuni</i> |
|------------------|------------|-----------------|--------------------------|-----------------------------|
| <i>A/m/mu/mw</i> | <i>m</i> | <i>-embamba</i> | <i>Muembamba</i> | <i>Uongezaji/uyeyushaji</i> |
| <i>wa</i> - | <i>wa</i> | <i>-embamba</i> | <i>Waembamba</i> | <i>Udondoshaji</i> |
| <i>m</i> | <i>m</i> | <i>-ekundu</i> | <i>Mekundu-mwekundu</i> | <i>Uyeyushaji</i> |
| <i>mi</i> - | <i>mi</i> | <i>-ekundu</i> | <i>Miekundu-mwekundu</i> | - |
| <i>li/Ji</i> | <i>ji</i> | <i>-eusi</i> | <i>Jieusi-jeusi</i> | <i>Udondoshaji</i> |
| <i>ya/ma</i> | <i>ma</i> | <i>-eupe</i> | <i>Meupe-meupe</i> | <i>Udondoshaji</i> |
| <i>ki</i> | <i>ki</i> | <i>-eupe</i> | <i>Kieupe-cheupe</i> | <i>Uyeyushaji</i> |
| <i>vi</i> | <i>vi</i> | <i>-eupe</i> | <i>vieupe- Vyeuoe</i> | <i>uyeyushaji</i> |

Asili: Data za Utafiti huu kutokana na Chomi (2003), Hyman & Katamba, (2012)

kwa mujibu wa mifano ya data (5.31), imedhihirika kuwa vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu hupitia michakato mbalimbali ya matumizi ya viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) wakati wa kutumia vivumishi vya sifa. Sharti ni kuwa lazima VPM vinavyotumika au kuambishwa kwenye mizizi ya vivumishi vya sifa kufuata fonolojia inayofuata na ni muhimu kila mtumiaji kuhakikisha kuwa anatambua mabadiliko ya kifonolojia yanayojitokeza ili kujenga fonolojia na maandishi ya Luganda au Kiswahili sanifu. Aidha, kulingana na mifano, imedhihirika kuwa baadhi ya kanuni za kimofonolojia zina mwingiliano mkubwa baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Luganda hutofautiana na Kiswahilikwa kutumia fonimu za vibainishi ngeli awali ambavyo husababisha au kuathiri mazingira ya utokeaji wa viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) vinavyoambishwa kwenye mizizi ya vivumishi vya sifa. Pia, imebainika kuwepo kwa tofauti za uambishaji viambishi awali vya vivumishi kwenye mizizi. Kwa mfano umbo la kimofolojia la /r/ linapoambikwa kwenye mzizi wa sifa – *lungi* hutumika badala ya foni /l/ baada ya kutokea kwa sauti /e/ na /i/ kama ilivyo katika ngeli ya 2 wingi, 3 na 4 kwa umoja. Mabadiliko mengine ya kifonolojia ni yale yaliyotokea katika ngeli ya tatu ambapo umbo la sauti /l/ hubadilika na badala yake pakatumika sauti/dd/ huku katika ngeli ya 8 na 9 sauti /l/ ya mzizi –lungi ikabadilishwa na umbo la kifonolojia /n/. Data Na.(5.32) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

- | | |
|--|---|
| a) <i>E- ttaayi e-no [e- n- lungi] e- gw- edde</i> | <i>Ettaayi eno ennungi egudde</i> |
| b) Tai hii nzuri imeanguka | Tai hii nzuri imeanguka |
| c) <i>Ekitabo ak(ie)ru</i> | <i>ekitabo e(kye)ru uyeyushaji/muungano /-i/- e /y/</i> |
| d) <i>Enyumba zilungi</i> | <i>enyumba ndungi udondoshaji wa KPM na l-nd</i> |
| e) <i>Eriiso erieru nungi</i> | <i>Eliiso eryeru ndungi</i> |
| f) Jicho Jekundu | Jicho Jekundu |

Asili: Data kutokana na Kiyinikibi (2021)

Matokeo haya yanashabihiana na matokeo ya utafiti wa Mayaka, (2012) ambaye katika utafiti wake, wa ‘Athari ya Mifanyiko ya Kimofonolojia kwa Upatanisho wa Kisarufi katika Kiswahili Sanifu’, alitambua athari za mifanyiko ya kimofonolojia ya ; usilimisho, uchopekaji, kuimarika na kudhoofika kwa fonimu ya Ekegusii katika upatanisho wa kisarufi wa nomino za ngeli ya JI-MA na KI-VI pamoja na N-N. Utafiti wake ulieleza sheria zilizohusiana na mabadiliko haya katika Kiswahili ili kudhibiti muundo asilia wa Kiswahili ya konsonanti vokali, konsonanti vokali (KVKV) pale ambapo irabu zaidi ya mbili zinapofuatana. Mathalan Utafiti huu lieleza kanuni za kifonolojia za Luganda na Kiswahili sanifu na kutambua kuwepo kwa uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni hii baiana ya Luganda na Kiswahili, licha ya kuwa lugha za nasaba moja. Aidha, Owino, (2016) anatambua kuwa “*kila lugha ina mifanyiko ya kipekee kutegema lugha. anasema kuwa. .Mfanyiko kama vile udondoshaji huweza kudhihirika kwa njia tofauti baina ya lugha mbili au zaidi kwa kulinganishwa. Mifanyiko hii ina upekee wake kutegemea lugha husika.*” Hali inayothibitisha kuwa kila lugha huwa na kanuni ya kifonolojia ambayo hutumika kwa njia ya kipekee kudhihirisha uhusiano milikifu na unganishi kama ilivyo Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.2.4.3 Kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa vivumishi vya sifa

Kanuni hii inashikilia kuwa: Vivumishi huchukua nafasi karibu na nomino kama neno kuu katika tungo virai hasa katika Lugha za Kibantu (Rijkhoff, 1986). Pia, kanuni hii inadai kuwa: Nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo. Abudonia, (2014) alifafanua kuwa Luganda sanifu huzingatia utaratibu wa kivumishi kufuata nomino kuu katika KN. Kwa mujibu wa maelezo yake, utokeaji wake hutawaliwa na kanuni ya kipramatiki, ukuu, hadhi na ujumbe wa kubainisha kategoria ya kivumishi ambayo ni lazima ifuate nomino kama neno kuu katika tungo. Data Na.(5.33) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa vivumishi vya sifa

- | | |
|---|---|
| a) <i>Omwana omugezi ayiise ebigezo</i> | Mtoto mwerevu amepita mitihani |
| b) <i>Emmotoka ye eyo ennungi</i> | Gari lake lile nzuri. |
| c) <i>Maama yafumbye emmere ennungi</i> | Mama alipika chakula kizuri/tamu |
| d) <i>Ettaayi eno ennungi egudde</i> | Tai hii nzuri imeanguka |
| e) <i>Nfumbidde maama wange emmere eno nnungi</i> | |
| | Nimempikia mamangu chakula hiki Kizuri |
| f) <i>Abaami bakola mu bibuga ebinene e-bi-lilaanye amazzi.</i> | |

Wanaume wanafanya kazi katika miji **mikubwa** iliyojirani na maji

Asili: Data kutokana na Kiyinikibi (2021) na Abudonia (2014)

Kwa mujibu wa data hii, imebainika kuwa kivumishi cha sifa kimetokea baada ya nomino kuu katika kishazi (a) kukumusha nomino [Omwana/Mtoto]. Katika Kishazi cha (b), kivumishi kimechukua nafasi ya pili karibu mwisho. Hata hivyo, kimefuata kanuni kuwa vivumishi hutokea baada ya nomino. Katika hali hii, kivumishi cha sifa kimetokea baada ya kimilikishi, kikifuatwa na kioneshi kisha kikajitikeza kama kielezi kinachobeba dhima ya kivumishi. Katika data ya (c), kivumishi kimetokea mwishoni kikisifu cahakula [Emmere/chakula] kilichopikwa na mama katika KN ya KT.

Utafiti huu ulibaini kuwa matumizi ya vivumishi vya sifa katika lugha na Kiswahili hushabihiana. Sharti ni kuwa lazima vivumishi vitokee baada ya nomino katika KN kuelezea zaidi juu ya nomino inayotajwa. Hata hivyo utokeaji wake unategemea hadhi, ukuu wa aina ya kivumishi ambacho huenda kikatangulia kisifa, na ujumbe unaobebwa katika tungo. Labda kwa kutumia kanuni swalivu, tunaweza kujiuliza kinachovumishwa katika tungo. Kwa mfano, tukichukua mfano wa (c) swali litakuwa je, chakula kilichopikwa na mama ni tamu. Swali litakuwa [kweli mama alipika chakulia tamu au chakulia kilichopikwa na mama ni kitamu. Ukiukaji wa kutotambua dhima ya utokeaji wa kivumishi cha sifa kutegema hadhi, ukuu wa utokeaji, muktadha, kanuni swalivu ya ujumbe muhimu, huenda ukapotosha usanifu wa lugha hasa kwa kukiweka kisifa hiki pasipohitajika. Kwa mfano [mzuri mtoto anakimbia] badala ya [mtoto mzuri anakimbia].

Tofauti iliyojitokeza katika matumizi ni muundo ya viambishi vipatanisshi vya msingi (VPM) vya Luganda ambavyo kwavyo hutofautiana na VPM vya Kiswahili sanifu kutokana na tofauti za maumbo ya ya Kiswahili, mabadiliko ya kifonolojia ya Luganda kutofautiana na ya Kiswahili sanifu na matumizi ya vibainishi ambavyo katika Luganda husaidia katika kubainisha aina ya kiambishi ngeli cha upatanishi wa kisarufi wa nomino kumushwa.

Matokeo haya yanashabihiana na ufafanuzi wa Lusekelo, (2017) wa vivumishi katika tungo {KN} kutokea kimuktadha kutegema neno lililo na hadhi ya juu. Ufafanuzi wake unafanana na wa Abudonia, (2014) ambaye anaeleza kuwa matumizi ya vivumishi katika KN hutawaliwa na kanuni ya kipragmatiki na hadhi ya kivumishi kipi husheheni dhima au ujumbe wa sentensi hata ingawa kanuni ya jumla ni kuwa kivumishi huja baada ya nomino kuu katika KN katika Luganda. Licha ya ufafanuzi wa wataalamu hawa kuelezea juu ya utokeaji wa vivumishi kimuktadha, Utafiti huu ulifafanua kanuni ya utaratibu wa kidarajia na utokeaji wa vivumishi vya sifa na kubaini kuwa utokeaji wa vivumishi vya sifa katika tungo huwiana na kutofautiana kimuktadha, kipragmatiki na kihadhi kimatumizi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi katika tungo.

5.1.2.4.4 Kanuni ya upatanishi wa kisarufi

Kanuni hii inashikilia kuwa neno kuu ndilo linalotawala matumizi ya kivumishi katika kundi nomino ambapo nomino ni kitawala na kivumishi ni kitawaliwa (Chomsky, 1957; 1965; 1995). Kimofosintaksia ngeli na idadi ndiyo inayoamua umbo la nomino na vivumishi, maana yake na sifa zake. Nomino inapokuwa na uamilifu wa kisintaksia, muundo mzima wa kisintaksia unaathirika kutokana na maneno kushikamanishwa kwa viambishi vya nomino kuu (Chomi, 2003). Kimatumizi, kanuni ya upatanishi wa kisarufi inadai kuwa wakati wa kukumusha nomino, Lazima nomino iakisiwe katika muundo wa kivumishi katika tungo vinginevyo tungo itakayojitokeza haitakuwa sahihi kisarufi. Muundo wa vivumishi huakisiwa na viambishi patanishi msingi vya nomino. Kulingana na Chomi (2003), Viambishi patanifu vinavyopachikwa mwanzoni mwa mzizi wa kivumishi lazima vionyeshi uhusiano wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi katika KN. Kanuni hii ilitumika na Oduor, Inyani na Kobia (2017) pamoja na Gromova, (2008) wanaoeleza kuwa, viambishi awali vya nomino na vya vivumishi, kwa kiasi kikubwa huwa havitofautiani kimaumbo bali huwa vinaandamana na viambishi vya umbo nomino. Hii ina maana kuwa katika tungo virai, nomino hutawala vivumishi kimuundo. Utawala wenyewe ukiwa umesitiriwa katika muundo wa vivumishi. Kimofolojia, kivumishi huundwa kwa kiambishi patanishi msingi pamoja na mzizi wa kivumishi. Viambishi patanishi hivi hurejelea ngeli nomino kimofolojia ambazo huambikwa kwenye mizizi ya nomino na vivumishi katika tungo virai.

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni hii kwa mujibu wa Baertlein & Ssekitto, (2014), Namugala, (2014), Ngamau, (2004), Lusekelo, (2017), Ambuyo, (2007), Kiyinikibi, (2021) ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana na kutofautiana katika matumizi ya

vivumishi vya sifa. Matumizi yake huzingatia uhusiano wa nomino kuu na kivumishi cha sifa kinachohusika. Upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na vivumishi huzingatia uambishaji wa VPM kimofosintaksia ambapo viambishi awali vya ngeli nomino huwekwa mwanzoni mwa kivumishi cha sifa na kiambishi cha upatanishi cha nomino kwenye kitenzi kuwakilisha uhusiano kati ya nomino inayokumushwa na vitenzi katika tungo. Kwa mujibu wa kanuni hii, kila nomino ya Luganda na Kiswahili ilipokea viambishi awali vya msingi vya nomino na viambishi vipatanishi tofauti kulingana na uainishaji ambamo nomino kumushwa huainishwa.

Aidha, ilitambulika kuwa Viambishi awali vya ngeli nomino na vibainishi ngeli vilivyokaririwa kwenye nomino ndivyo vilivyokaririwa katika mizizi ya vivumishi vya sifa kuzingatia mabadiliko ya kimofonolojia husika kama viambishi nomino kudhihirisha upatanishi wa kisarufi kati ya nomino na vivumishi katika tungo virai nomino (KN). Viambishi vinavyobebwa na vivumishi kwa hivyo hubeba sifa za maumbo ya kimofolojia ya ngeli nomino katika kirai momino. Aidha, upatanisho wa kisarufi huzingatia muundo wa maneno ambayo sentensi huathiriwa na ngeli ya nomino husika kujenga upatanishi wa kisarufi kupita kwa viambishi patanishi kama unavyojitokeza katika data (5.34) ya data inayodhihirisha matumizi ya VPM kuwakilisha uatanifu wa nomino na vivumishi katika tungo. mifano hii imedhihirsah uwiano na tofauti za vibainishi (Kb), viambishi ngeli (Kng), mizizi (mz) na vipatanishi vya msingi vya ngeli (KptKng). Data Na.(5.34) inabainisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya upatanishi wa kisarufi:

- a) *[E-ki]-tabo [e-ki]-lungi [E-bi]-tabo ebirungi ki-letebwa*
Kb-Kng7-Mz Kb-Kng7-Mz Kb-Kng8-Mz Kb-Kng8-Mz KptKng7 na 8-
- b) Ki-tabu ki-zuri ki-meletwa vi-tabu vi-zuri vi-meletwa
Kng7-Mz- Kng7-MzV Kng7-meletwa Kng8-Mz Kng8-MzV Kpt7/8
- c) *O-mw-ana o-mu-gezi a-yiise ebigezo M-toto mw-erevu amepita mitihani*
Kb-Kng1-Mz Kb-Kng1-Mz KptKng1 Kng1-Mz Kng2-Mz KptKng1

Asili: Matokeo ya utafiti kutokana na Abudonia, (2014) na Kiyinikibi (2021)

Tofauti iliyojitokeza ni kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha tofauti ambazo huzingatia fonolojia na othografia yake. Kwa hiyo, mabadiliko ya kimofolojia yaliyojitokeza katika uundaji wa VPM vya uambishaji kwenye vivumishi vya sifa ulitofautiana kifonolojia. Aidha, mpangilio wa ngeli na maumbo ya kimofolojia ya viwakilishi vya viambishi vipatanishi vya ngeli kutoka ngeli moja na nyingine ulidhihirisha tofauti. Ilitambulika kuwa Luganda hutumia vibainishi awali vya ngeli nomino pamoja na viambishi awali vya nomino na viambishi vipatanishi vya kisarufi katika tungo zao huku Kiswahili ikizingatia matumizi ya

viambishi awali vya ngeli na viambish vipatanishi kukumushwa nomino katika tungo. kwa mfano sentens (a-c) inadhihirisha matumizi ya mzizi [*lungi/zuri*] ambao haubadiliki kimaana bali maumbo yake ya uwakilishi wa dhana no tofauti. Pia, viambishi ambavyo vimeambikwa kwenye mzizi [*lungi/zuri*] umadhihirishwa kutofautiana kutokana na kila nomino kuwakilishwa na viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) na viambishi vipatanishi vya kisarufi tofauti kutoka ngeli ambamo nomino husika huainishwa. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha ya nasaba moja, hizi ni lugha mbili tofauti zinazotofautiana katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya vivumishi.

5.1.2.5 Uwiano na tofauti ya kanuni za matumizi ya Vivumishi vya Idadi isiyodhahiri

Vivumishi vya idadi isiyodhahiri ni vivumishi ambavyo hutaja kiasi fulani cha idadi kwa ujumla bila kutumia idadi kamili (Mgullu 1999; Habwe & Karanja 2004; Kisakwah 2014). Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha ambazo zina vivumishi vya idadi isiyodhihirika. Utafiti huu uliegemea uwiano na tofauti ya kanuni za matumizi ya vivumishi vya idadi vya Luganda na Kiswahili ili kuweza kutathimini jinsi vinavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya uchanganuzi wa data za usomaji na upekuzi wa maandishi mbalimbali ulibaini kuwa, matumizi ya vivumishi hivi hutegemea kanuni ambazo huhusika kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Hata hivyo, kila kivumishi cha idadi kilidhihirisha kanuni za kipekee. Aidha, utafiti ulibaini uwiano na tofauti ya matumizi ya kanuni za matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri mbalimbali vya {-*ngi/-ingi*, -*tono/chache na dodo*, -*lala/-ingine na – onna/-ote*}. Rejelea Jedwali (4.14, Uk. 111) la uwiano na tofauti za mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri vya Luganda na Kiswahili Sanifu.

5.1.2.5.1 Kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa vivumishi


Kanuni ya matumizi ya vivumishi hivi inashikilia kuwa: Matumizi ya vivumishi vya idadi lazima yazingatie viambishi awali vya nomino. Viambisho hivi ni vile ambavyo pia ni vipatanishi msingi vya nomino vinavyoambishwa kabla ya mizizi ya vivumishi vinavyobeba maana ya kileksika ya kivumishi kinachokumusha nomino katika KN. ijapokuwa vivumishi vya mkopo vsivyi vya asili ya Kibantu. Ukiukaji wa kimatumizi usiozingatia muundo wa vivumishi wa uambishaji viambishi awali vya nomino na viambishi vipatanishi msingi vya nomino, huweza kudhoofisha usanifu wa lugha husika. Hali inatokana na kuwa, maumbo ya vivumishi vinavyoambishwa hufuata kanuni ya kimosintaksia ya uambishaji inayodai kuwa: Uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi

(uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu. Kimofosintaksia, muundo wa vivumishi huchukua maumbo sawa ya viambishi ngeli vya nomino kimofolojia kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi na nomino au kirai nomino kuathiri umbo la vivumishi (Oduor na Wenzake, 2017).

Aidha, kanuni hii inatetewa na Lusekelo, (2017) anayetambua kuwa: Neno kuu katika utungo huchagua kuathiri maneno mengine kutegemea mazingira ambamo nomino tajwa hutokea. Kulingana na kanuni hii, nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai kupitia kwa vibainishi na viambishi nomino vyake vinavyodhihirisha upatanishi wa kisarufi. Rejelea jedwali (4.15, Uk.113) lenye kuonyesha data za uwiano na tofauti za mizizi na viambishi awali vipatanishi vinavyowekwa kwenye mizizi ya vivumishi vya idadi isiyo kamili baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Mifano ya jedwali (4.15, Uk. 113) ilibainika kuwa vivumishi vya idadi isiyodhahiri huzingatia uambishaji wa viambishi awali vya nomino ambavyo pia ni vipatanishi msingi vya nomino vinavyoambishwa kabla ya mizizi ya vivumishi vinavyobeba maana ya kileksika ya kivumishi kinachokumusha nomino katika tungo. uambishaji huu huzingatia ngeli ambamo nomino kuu huainishwa. Viambishi vinavyoambishwa huwa ni vya wingi wa idadi ambavyo huwa na maana ya kileksika ya ujumla wa nomino inayokumushwa bila kutaja hesabu au takwimu kamili. Hii ina maana kuwa kila nomino huwa na viambishi tofauti na viambishi vingine na kuna vile ambavyo kutegemea nomino, huchukua viambishi kapa vinavyodhihirika kidhahania wakati wa matumizi. Aidha viambishi hivi huweza pia kupitia mchakato wa kimofonolojia katika ujenzi wa viambishi vipatanishi vya msingi vinavyoambikwa kwenye mizizi wa kileksika wa kivumishi kinachokumushwa. Matumihi zhaya yanadhihirisha ubia na upatanifu wa kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi katika tungo kati ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Tofauti iliyojitokeza katika matumizi ya kanuni hii ni ile ya kanuni ya kimofolojia ya matumizi ya viambishi awali vya upatanishi vya wingi wa nomino na mizizi ya kivumishi husika unaotegemea ngeli nomino inayokumushwa. Kanuni hii inashikilia kuwa: KPM kikiambishwa kabla ya mizizi wa kileksika wa kivumishi cha idadi isiyodhahiri huunda kivumishi cha idadi kisichodhahiri ambacho kimepitia mabadiliko ya kifonolojia kama inavyojitoeza katika mchoro (M5.9) wa sentensi inayofafanua akanuni.



Matokeo haya yanaendana na maelezo ya Kisakwah, (2014) ambaye anaeleza juu ya muundo wa vivumishi vya idadi. Katika maelezo yake, anasema kuwa, “Ni muhimu kuzingatiwa kuwa, vivumishi vina sehemu kuu mbili yaani kiambishi awali ambacho pia ni kipatanishi cha nomino kinachowekwa kabla ya mzizi wa kivumishi.” (Kisakwah, 2014: 42). Ufafanuzi ambao unatolewa na Balagadde na Premchand (2016).

5.1.2.5.2 Kanuni ya darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai

Kanuni ya darajia ya ukuu wa utokeaji wa vipashio katika tungo hushikilia kuwa: Mpangilio au utokeaji wa vivumishi pamoja na neno kuu katika tungo huzingatia utaratibu maalumu. Nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo (Lusekelo, 2017). Kanuni hii inadhihirisha kuwa mizizi ya vivumishi vya idadi visivyodhahiri vinaweza kutumika kwa pamoja na viambishi ngeli au vibainishi vya nomino na viambishi vya uhusika vya nomino inayokumushwa ambayo hutokea karibu na neno kuu au nomino kama neno kuu. Kwa mujibu wa kanuni hii, kuna darajia zinazozingatiwa katika upangaji wa vipashio katika tungo. Darajia hizo hubainisha element muhimu katika tungo. Kwa mujibu wa kanuni hii, Vivumishi huchukua nafasi karibu na nomino kama neno kuu katika tungo virai hasa katika lugha za Kibantu. hii inatokana na kuwa nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo kama inavyoelezwa na Rijkhoff, (1986), Lusekelo, (2013) na Mwamzandi, (2018), Rose, (2009) na Abudonia, (2014). Aidha, ilibainika kuwa vivumishi vya idadi vya Luganda na Kiswahili sanifu hujitokeza katika KN ambapo neno kuu ni nomino na Kivumishi chake ni kivumishi cha idadi isiyodhahiri. Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana na kutofautiana katika matumizi ya kanuni hii ambapo kivumishi cha idadi hutokea baada na karibu sana na neno kuu linalokumushwa kwa idadi isiyodhahiri katika KN. Utokeaji wake katika tungo kutegemea muktadha au ujumbe wa mwandishi au mzungumzaji kuhusu nomino inayokumushwa.

Uchanganuzi wa upekuzi wa maandishi ya Rijkhoff, (1986), Rose, (2009) na Abudonia, (2014), ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huawiana na kutofautiana katika kupangilia vivumishi vya idadi katika tungo. Iligunduliwa kuwa Vivumishi vya idadi vya

Luganda na Kiswahili sanifu hujitokeza katika KN ambapo neno kuu ni nomino na Kivumishi chake ni kivumishi cha idadi isiyodhahiri. Katika utaratibu wa upangaji wa vivumishi, ilidhihirishwa kuwa lugha hizi huambisha viambishi vya idadi isiyodhahiri mwanzoni mwa mizizi ya kileksika ya vivumishi visivyodhahiri baada na karibu na neno kuu au nomino kuu katika tungo virai. Kuzingatia utaratibu wa maneno katika muundo virai, Luganda na Kiswahili sanifu huzingatia utaratibu wa vivumishi vya idadi isiyodhahiri kutokea baada na karibu na nomino inayokumushwa kudhihirisha idadi husika. Kwa Ilibainika kuwa utokeaji wa vivumishi vya idadi isiyodhahiri hutawaliwa na kanuni ya kipramatiki, ukuu, hadhi na ujumbe unaosisitizwa katika tungo. Kwa mujibu wa utaratibu huu, ukiukaji wa kutozingatia utaratibu wa uambishaji unaofaa na kivumishi cha idadi kutokea baada na karibu na nomino kuu huweza kupotosha maana na hata usanifu wa matumizi ya vivumishi husika katika tungo.

Kwa hiyo, kanuni ambayo ni bayana ni ile inayozingatia kuwa vivumishi vya idadi huchukua nafasi karibu na neno kuu au nomino kuu na utokeaji wake lazima utegemee muktadha, hadhi, ukuu na ujumbe unaosisitizwa. Data (5.35) ya data kutokana na Abudonia, (2014), Dixon, (2010), Rijkhoff, (1986) na Rose, (2009) inadhihirisha uwiano na tofauti za kidarajia za utokeaji wa vivumishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. (5.35)

Luganda

a) *Abayizi ba-angi baayiise ebigezo.*

N V T N

**Abayizi baayiise ebigezo bangi.*

N T N V

b) *Abazimbi banenne ba-lala bazimba.*

N V V T

**Abazimbi ba-lala banenne bazimba etoyi. Wajenzi we-ngine wanene wanajenga choo.*

N V V T N

c) *Maama yafumbye emmere entono.*

N T N V

**Maama yafumbye entono emmere.*

N T V N

d) *Emiti gya taata gyonna kimezze.*

N V N V T

**Emiti gyona gya taata kimezze.*

Kiswahili sanifu

Wanafunzi **we-angi** walipita mitihani.

N V T N

Wanafunzi walipita mitihani we-angi

N T N V

Wajenzi wanene **we-ngine** wanajenga.

N V V T

**Wajenzi we-ngine wanene wanajenga choo.*

N V V T N

Mama alipika chakula **ki-cache/kidogo**

N T N V

Mama alipika **ki-cache/kidogo** chakula*

N T V N

Miti ya baba yote imemea

N U N V T

Miti **yote** ya baba imemea*

Asili: Data kutokana na Abudonia, (2014) na Rijkhoff, (1986)

Mifano (5.35) ya data [a-d] inadhihirisha kanuni ya uambishaji wa viambishi vipatanishi vya msingi kwenye mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri ambapo viambishi VPM vimewekwa mwanzoni mwa mzizi tena baada na karibu ya nomino kuu katika tungo. pia Utaratibu huu unadhihirisha kanuni ya kivumishi cha idadi isiyodhahiri kutokea baada na karibu na nomino kuu. Hata hivyo, matumizi yake ni ya kimuktadha na mabyo yanategemea dhima au ujumbe wa tungo ambapo katika (a) imetokea baada na karibu na nomino kuu, katika (b) imetokea baada ya kivumishi cha sifa cha nomino kuu, kishazi cha (c) Hakikumushi nomino kuu bali kinazungumzia juu ya chakula wala sio mama kama neno kuu, na katika (d), kivumishi cha idadi kimetokea baada ya kivumishi cha [-a] unganifu.

Tofauti zinazojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili ni kuwa miktadha ya utaratibu wa utokeaji wa vivumishi vya idadi kukumusha idadi hutofautiana. Mpangilio au utaratibu wa Luganda huenda ukawa haupotoshi maana na ujumbe pamoja na usanifu wa lugha, huku Kiswahili kikipotosha na kinyume. Kwa mfano, kishazi cha (a) ingawa ni sahihi kimazungumzo, hakikumushi nomino kuu moja kwa moja kwa sababu imewekwa baada ya nomino [Mitihani] katika KN ya KT. Ili kuelewa maana au ujumbe lazima utumie kanuni nyingine ya swali ili utambue kuwa kivumishi hicho hakikumushi [mitihani] bali wanafunzi. Kishazi cha (b) hakina utata mwingi kwani kimebadilishana tu nafsi na kivumishi cha sifa na hivyo usanifu wake unatokana na ukuu wa kukumusha nomino husika. kishazi cha (c) kinaonekana kupotosha usanifu wakati wa kupangilia vivumishi [Chache] kwa hiyo hii ina maana kuwa ingawa utokeaji wa vivumishi ni wa kimuktadha lazima ujumbe na dhima ya tungo izingatiwe hasa ukitazama muundo wa kishazi cha pili. Mwisho, kishazi cha (d) kinadhihirisha tofauti ya muktadha wa matumizi ya vivumishi vya idadi. Katika Luganda virai vyote hivi ni sanifu hata ingawa vimebadilishana nafasi. Hata hivyo, katika Kiswahili, ufasiri wa moja kwa moja umepotosha dhima na maana ya kirai cha kwanza. Hata hivyo kiutaratibu, kirai cha pili ni sanifu kwa sababu ya kuzingatia kanuni ya utokeaji baada ya nomino kuu.

Tofauti nyingineyo inayojitokeza ni kuwa, Luganda wakati mwingi hupachika vibainishi nyumba ya vivumishi vya idadi hasa kwa kutaja vivumishi vya idadi na katika tungo baadhi ya vivumishi vya idadi havichukui vibainishi bali viambishi awali vya msingi ambavyo ni VPM vya nomino inayokumushwa. Kiswahili hutumia viambishi awali vya nomino ambavyo

pia ni VPM kimofosintaksia kuzingatia maumbo ya nomino na upatanishi wake kama sharti. Ukiukaji wa matumizi ya VPM vinavyofaa na katika utaratibu na nafasi unayofaa, huweza kupotosha usanifu wake. Kwa mujibu wa data za mifano hii, ilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huzingatia kanuni ya kivumishi cha idadi isiyodhahiri kutokea baada na karibu sana na neno kuu [nomino] katika KN. Hata hivyo, hutofautiana katika maumbo wakilishi ya viidadi ambavyo huambishwa kwenye mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri.

5.1.2.5.3 Kanuni ya uambishaji wa vivumishi vya idadi isiyodhahiri katika tungo.

Kanuni hii hushikilia kuwa: Nomino kuu au neno kuu katika utungo huwakilishwa au huzingirwa na vibainishi au kirejeleo nomino (kiambishi nomino), kivumishi cha nomino na uhusika milikishi (Kivumishi na uhusika wa nomino). Kulingana na kanuni hii, Neno kuu katika utungo huchagua kuathirika kwa maneno mengine katika tungo kutegemea mazingira ambamo nomino tajwa hutokea. Hali hii hushikilia nomino kama neno kuu kutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo.

Matokeo ya uchanganuzi wa ufafanuzi wa Mgullu, (1999), Kisakwah (2014), Obara, (2014), Namugala, (2014), Kiyinikibi, (2021), Abudonia, (2014), ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana na kutofautiana katika uambishaji wa vivumishi vya idadi isiyodhahiri. Lugha hizi huambisha viambishi vipatanishi vya msingi kwenye mizizi ya kileksika ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri ambayo hutotokea karibu n nomino kuu. Aidha, kulingana na kanuni hii, viambishi vipatanishi hivi huwekwa mwanzoni mwa mzizi wa kivumishi kutegemea viambishi awali vya msingi na viambishi vipatanishi vya nomino husika kuwakilisha idadi husika ila katika baadhi ya vivumishi vya mkopo ambavyo haviambishi ila hujitokeza kidhahania kuwakilisha idadi husika kwa njia ya ukapa [φ].

Data katika jedwali Na. (4.14, Uk. 111) la mumbo ya mizizi ya vivumishi visivyo vya idadi kamili, Jedwali Na. (4.15, Uk. 113) la viambishi awali vipatanishi vinavyowekwa kwenye mizizi ya vivumishi vya idadi isiyokamili na data za matumizi ya jedwali Na (4.16, Uk. 119) inadhihirisha uwiano na tofauti ya mizizi na maumbo ya mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri bbaina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data hii inadhihirisha uwiano wa uambishaji wa VPM kwenye mizizi ya vivumishi kutokana na kanuni ya neno kuu katika utungo kuchagua kuathiri maneno mengine (Vivumishi vya idadi isiyodhahiri) kutegemea mazingira ambamo nomino tajwa hutokea, neno kuu kutawala maneno mengine (vivumishi

vya idadi isiyodhahiri) yanayotokea kwa karibu sana na nomino kuu katika tungo virai pamoja na nomino kuu kuwakilishwa na vibainishi au kirejeleo nomino (kiambishi nomino), kivumishi cha nomino na uhusika milikishi.

Tofauti inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni ile ya kanuni za matuzi ambapo baadhi maneno katika Luganda hutumia vibainishi pamoja na viambishi ngeli kudhidhirisha idadi ya nomino inayokumushwa. Kiswahili huwakilishwa na viambishi awali vya nomino ambavyo pia ni VPM vya nomino kuu inayokumushwa katika KN. Aidha, baadhi ya athari za kifonolojia zinazojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana kulingana na viambishi awali vya ngeli nomino ambavyo pia ni viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) pamoja na sifa za kifonolojia zinazotofautisha Luganda na Kiswahili sanifu kama lugha za kipekee hata ingawa ni lugha za kibantu kama ilivyo katika mifano ya [a na e]. Uambishaji wa vivumishi kwa viambishi vipatanishi vya msingi [VPM] baina ya Luganda na Kiswahili sanifu husababisha mabadiliko ya viambishi msingi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vimilikishi kutegemea ngeli nomino ambamo nomino inayotajwa huainishwa. Hii ina maana kuwa mizizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri huambishwa kwa VPM kwa ajili ya kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya kivumishi na nomino inayokumushwa kama ilivyodhihirika kutokana na maelezo ya Kisakwah (2014) kuwa; *Vivumishi vina sehemu kuu mbili yaani kiambishi awali ambacho pia ni kipatanishi cha nomino kinachowekwa kabla ya mzizi wa kivumishi. viambishi hivyo aghalabu huwa ni kipatanishi cha wingi cha nomino na hutumika kabla ya mzizi wa vivumishi.*

5.1.3 Uwiano na tofauti ya kanuni za matumizi ya viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu Kimofosintaksia

Viwakilishi vinapotumika, nomino zinazowakilishwa na viwakilishi hivyo huwa hazitajwi (Mgullu, 1999). Viwakilishi huwa ni maneno yoyote yanayosimama badala ya majina ili kujulisha kitu kinachohusika na maonyesho, ulizo au kitenzi kinachoarifu tukio fulani, bila kutaja jina la kitu tajwa. Viwakilishi hivi ni viwakilishi nafsi, viwakilishi vimilikishi, vionyeshi, viulizi, viwakilishi vya sifa, visisitizi, viwakilishi vya idadi na virejeshi (Kisakwah, 2014a, Oichoe, 2005 na Habwe & Karanja, 2004). Utafiti huu ulichunguza viwakilishi nafsi kwa kueleza muundo wake kati ya Luganda na Kiswahili, kanuni za matumizi yake na jinsi matumizi ya Luganda inavyoathiri matumizi yake katika Kiswahili sanifu. Matumizi ya viwakilishi hivi vya nafsi hutumika kulingana na kanuni mbalimbali za

kisarufi au za kimofosintaksia. Ukiukaji wa kanuni hizi huweza kupotosha usanifu wa lugha ya Kiswahili. Aidha, katika utafiti huu, kanuni zifuatazo zilibainishwa kutokana na usomaji na upekuzi wa kazi za sarufi ya Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.3.1 Kanuni ya umiliki na usabiki

Kila kiwakilishi nafsi kina kiambishi cha upatanishi wa kisarufi ambacho huambishwa mwanzoni mwa vitenzi. Kiambishi hiki hutokea au kuwekwa mwanzoni mwa kitenzi kurejelea nomino tendaji au kiima na yambwa iliyotajwa kuepukana na marudio (Egara, 2016). Kwa mujibu wa matumizi ya kanuni hii, nomino hurejelewa kianafora kama nomino kapa ambayo hujidhihirisha katika ubongo wa msikilizaji au msemaji. Maumbo haya yanapotumika hurejelea nomino tajwa awali katika mawasiliano. Katika kanuni ya umiliki na usabiki, viambishi vya nafsi lazima vitumike kulingana na nafsi ya nomino inayorejelewa katika kiima/KN na kujitokeza katika KT kama anafora na kisabiki chake kwa njia ya muungano wa maumbo (viwakilishi) ya nafsi na wakati ambao huwekwa kabla ya mzizi wa vitenzi. Viambishi hivi lazima vidhihirishe uhusiano wa kisarufi kati ya nomino tajwa (kuu) na maneno mengine katika tungo. Kwa mujibu wa Wani (2010, na Oduor na Wenzake, 2017), lazima kiwakilishi kikubaliane na kisabiki chake katika jinsia na idadi. Hii ina maana kwamba nomino iliyo katika umoja lazima iwakilishwe na kiwakilishi katika umoja. Vivyo hivyo, ikiwa nomino inarejelea jinsia ya kike, ibainike katika sentensi kwamba kiwakilishi nomino kinarejelea jinsia ya kike.


Kwa kurejelea kanuni hii, mapitio ya vitabu vya kisarufi na tafiti za Mgullu, (1999), Habwe & Karanja, (2004), Matasi & Furaha, (2016), Baertlein & Ssekitto (2014), Leah & Sseguya, (2015) Luganda na Kiswahili sanifu huwakilishwa na viwakilishi vya nafsi vitatu ambapo vyote hutumika kuwakilisha kiima (nafsi huru) na yambwa (nafsi tegemezi). Viwakilishi hivi vimegawanyika katika makundi mawili. Viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsu tegemezi. Kwa kuzingatia kanuni ya umiliki, imebainika kuwa kila kiwakilishi cha nafsi huru kina kiambishi cha upatanishi (tegemezi) kinachoambikwa kwenye vitenzi katika tungo. Data (5.36) ya data kutokana na Matasi & Furaha, (2016), Kiyinikibi, (2021), Kisakwah, (2014a), Oichoe, (2005) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu:

- | | |
|--------------------------------|-----------------------------|
| a) <i>Nze nsamba omupiira</i> | <i>Ffe tusamba omupiira</i> |
| Mimi ninacheza mpira | Sisi tunacheza mpira |
| b) <i>Ggwe osamba omupiira</i> | <i>Mwe musamba omupiira</i> |

- Wewe unacheza mpira Nyinyi mnacheza mpira.
 c) Ye asamba omupiira Bbo basamba omupiira
 Yeye anacheza mpiira Wao wanacheza mpira


Asili: Data Kutokana na Matasi na Furaha, (2016), Kiyinikibi, (2021)

Data Na. (5.36) ilidhihirisha viambishi viwakilishi viwili. Viwakilishi vinavyotangulia ni huru vinavyotumika kuwakilisha kiima na vya pili vilivyoambatishwa kwenye njeo na kitenzi kuwakilisha yambwa. Viambishi hivi vyote kwa mujibu wa kanuni hii vinafaa vitumike pamoja na kitendo. Kwa hiyo, viambishi vyote lazima viungane na kitenzi kuelezea juu ya nomino kuu iliyotajwa awali kiurejeshi (anafora) ambapo nomino inayozungumziwa ni kisabaki cha nafsi iliyoungana na kitenzi kuelezea juu ya kitendo kifanywacho kutegemea wakati kama inavyojitokeza katika mchoro (M5.10) kutokana na matokeo ya utafiti huu.



Asili: Mchoro kutokana na utafiti huu, (2021)

Kimfosintaksia, kanuni hii inaweza kuwakilishwa pia njia ya matawi kama katika (M5.10)




Asili: Mchoro kutokana na utafiti huu, (2021)

Kimfosintaksia virai hivi vya Luganda na Kiswahili sanifu vimeundwa kwa KN na KT. Kirai huru huwakilishwa na kirai tegemezi katika tungo kudhihirisha upatanifu wa kisarufi (umiliki) unaotokana na kanuni ya muungano wa nafsi na kitenzi kinachofanyika kulingana na wakati. Upatanishi huu umewakilishwa na maumbo ya viambishi [mimi na ni]. [Mimi] ni kiwakilishi cha nafsi huru kinachodhihirisha umoja wa nomino tendaji. Kiwakilishi nafsi huru kinaweza kutumika peke yake kuwakilisha upatanifu wa idadi na ngeli ya umoja na wingi wa nomino. Kikiondolewa katika kirai chenye kiwakilishi nafsi huru, pengo la usanifu

wa maandishi na mazungumzo hupotoshwa. Virai [*Nze samba omupiira*] na [*Mimi nacheza mpira*] hudhihirisha upungufu wa kimatumizi ambapo kwa mfano [N] ya nafsi ya Luganda husaidia kujenga nafasi na njeo ikiondolewa, usanifu hupotoshwa. Kimazungumzo, kirai cha Kiswahili angalau kina dhihirisha mtendaji na kiima hata ingawa kiwakilishi nafsi tegemezi kimeondolewa. Hii ni kwa sababu kanuni ya maswali ikitumika kuuliza mtendaji nomino inaweza kutajwa na sentensi kupata usanifu kama vile [*Mchezaji nacheza mpira*] hata hivyo lazima kiwakilishi cha ngeli kitumike ili usanifu udhihirike. Kwa mujibu wa mchoro (5.2.10), [*mimi*] ni kisabaki cha [*ni*] na [*ni*] ni kiambishi anafora cha [*mimi*] ambayo ni kapa, hali hii inadhihirisha upatanishi wa nomino na viwakilishi vyake.

Kiambishi cha pili cha umilikaji nomino ni [*ni-*] ambacho hutokana na muungano wa njeo na kitenzi kuzalisha kirai patanishi kinachowakilisha upatanishi wa kitenzi na nomino tajwa kiurejeshi. Kwa mujibu wa kanuni hii, imedhihirishwa kuwa maumbo ya nafsi ya Luganda na Kiswahili sanifu huungana na njeo pamoja na vitenzi kuzalisha virai vipatanishi kurejelea nomino kuu kianafora na kiusabaki. Ukiukaji wa kanuni hii huzalisha mazungumzo na maandishi yasiyosanifu. Mchoro (5.11) kutokana na matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha muhtasari wa kanuni hii ya umiliki na usabaki. Mchoro (M5.11):



Asili: Kutokana na data za utafiti huu, (2021)

Kanuni hii vile vile huzungumzia juu ya upatanishi wa kisarufi wa virai yambwa ambapo huambikwa karibu na kitenzi baada ya kiambishi cha njeo. Viambishi vinavyotumika ni viambishi vya kiima vinavyotegemea ngeli. Vipatanishi hivi ni vipatanishi vinavyowakilisha nafsi yambwa ambavyo hutumika kulingana na nomino kuu. Viambishi hivi vya upatanishi hutumika kianafora na kiusabaki kuwakilisha viwakilishi huru ambapo kishazi huru humiliki au hutawala kiambishi nafsi yambwa, huku kiwakilishi yambwa kikisabiki kiwakilishi huru. Jedwali (5.8) linawasilisha uwiano na tofauti za upatanishi wa kisarufi wa yambwa baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, Mifano ya vishazi (5.37) vilidhihirisha data ya uwiano na tofauti za matumizi ya vipatanishi vya kanuni ya umiliki na usabaki baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data (5.37) na Jedwali Na (5.5) ya data kutokana na matokeo ya utafiti huu

yanadhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya vipatanishi kati ya Luganda na Kiswahili sanifu na utaratibu wa utokeaji wake. (5.37)

| | | | |
|------------------|-----------------|-------------------|-------------------------|
| <i>Yankubye</i> | [<i>nzee</i>] | <i>Batukubye</i> | [<i>ffe</i>] |
| <i>Alinipiga</i> | [<i>mimi</i>] | <i>Walitupiga</i> | [<i>sisi</i>] |
| <i>Yakutumye</i> | [<i>ggwe</i>] | <i>Babatumye</i> | [<i>mwe</i>] |
| <i>Alikutuma</i> | [<i>wewe</i>] | <i>Waliwatuma</i> | [<i>nyinyi</i>] |
| <i>Yamulabye</i> | [<i>ye</i>] | <i>Babalabye</i> | [<i>bba/abo/bali</i>] |
| <i>Alimwona</i> | [<i>yeye</i>] | <i>Waliwaona</i> | [<i>wao</i>] |

Jedwali 5.5: Uwiano na tofauti za viwakilishi vipatanishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu

| Viwakilishi na vipatanishi kwa umoja | | | Viwakilishi na vipatanishi kwa wingi | |
|--------------------------------------|--------------------|--------------------------------|--------------------------------------|----------------|
| Viwakilishi nafsi huru (Umoja) | Vipatanishi yambwa | Viwakilishi nafsi huru (wingi) | Vipatanishi yambwa | |
| Mimi | -ni- | Sisi | -tu- | Kiswahili |
| <i>Nze</i> | -n- | <i>Ffe</i> | -tu- | <i>Luganda</i> |
| Wewe | -ku- | Nyinyi | -wa- | Kiswahili |
| <i>Ggwe</i> | -mu- | <i>Mmwe</i> | -ba- | <i>Luganda</i> |
| Yeye | -m- | Wao | -wa- | Kiswahili |
| <i>Ye</i> | -m- | <i>Bba</i> | -ba- | <i>Luganda</i> |

Asili: Kutakana na Mulei (2014) na Matasi na Furaha (2016)

Mifano ya Jedwali 5.5 na mifano (5.37) ya data inadhihirisha umiliki na usabaki wa viambishi yambwa baina ya kiima yaani nomino kuu inayowakilishwa na nafsi huru kwa njia ya ukapa, vipatanishi vya nafsi ya kwanza pili na tatu ikiwakilishwa na ngeli ya kwanza kisintakisa kwa umoja na wingi. Kiambishi [a na ya] ni cha nafsi ya tatu na kiwakilishi cha upatanisho wa kisarufi wa ngeli nomino ya kwanza. Kiwakilishi hiki kupitia kwa kanuni ya swali inairejelea nomino tendewa, tendi na tendwa kuzingatia nafsi tatu kuu. Upatanisho wa nomino tendi, tendwa na tendewa umewakilishwa na vipatanishi vilivyopachikwa nyuma ya kitenzi baada ya njeo kutokana na nomino kuu ambayo imewakilishwa na [a-wa] katika Kiswahili na [a-ba] katika Luganda. Kwa mfano katika kishazi [a-li-mw-ona], [a] ni nomino

inayozungumziwa ambayo ipo mbali ikiwakilishwa na [yeye]. [Yeye] ni nomino dhahania ama kapa inayotambulika na mzungumzaji kutegemea nafsi na ngeli husika.

Matokeo ya utafiti huu yanashadidiwa na yale ya Kisakwah, (2014), Obara, (2014), na Oduor na Wenzake, (2017) ambao walibainisha tofauti za upatanishi baina ya lugha za Kibantu za Kisuba na Kidholuo ambapo viambishi vipatanishi katika lugha hizi ilidhihirika kutofautiana na ya lugha ya Kiswahili sanifu kutokana na upekee wa lugha hizi kiisimu na Kiswahili sanifu. Aidha, utafiti wa Rugemalira (2005) ulidhihirisha uwiano wa mofu nafsi katika lugha za Kibantu za Runyambo na Kipemba. Utafiti huu ulibaini kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, matumizi ya viwakilishi nafsi huwiana na kutofautiana kimaumbo kutokana na kanuni ya umiliki na usabaki.

5.1.3.2 Kanuni ya urejeshi

Urejeshi katika viwakilishi nafsi hutokea katika vitenzi pale ambapo nomino tendaji hurejelewa kuonyesha mtenda, mtendwa na mtendewa tendo (kiima na yambwa). Viambishi vinavyowakilisha nomino iliyotenda tendo, mtendwa na mtendewa hutumika kurejelea nomino iliyotenda kitendo bila kurudia kuitaja tena (Chomi, 2003). Aidha, Oduor, Kobia & Inyani, (2017) wanaelezea kuwa ujirejeaji ni mchakato wa kimofonolojia ambapo kipashio katika kiarifu hurejelea tena kiima hali ambapo majukumu mawili hudhihirika katika tungo moja. Thompson na mwenzake (2001) wanaeleza ya kuwa kanuni ya urejeshi wa nomino hutokea kwa kuzingatia viwakilishi vya nafsi na ngeli za nomino ambapo viambishi vya urejeshi huwekwa baada ya njeo na kabla ya kitendo vikichukua maumbo yake kutokana na ama kiima husika au nafsi. Jedwali (5.6) na mifano (5.38) linabainisha uwiano na tofauti za matumizi ya viwakilishi vya nafsi na ngeli rejeshi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Jedwali 5.6: Viwakilishi vya nafsi na ngeli rejeshi

| Kiwakilishi nafsi | Kiambishi kirejeshi yambwa | Ngeli | Kiambishi kirejeshi |
|--------------------------|-----------------------------------|---------------------|----------------------------|
| | Kiswahili sanifu | | |
| Mimi - Sisi | -ni- -tu- | Ngeli ya 1-2 | m-wa |
| Wewe - Nyinyi | -ku- -wa-/ | Ngeli ya 3-4 | u-i |
| Yeye - wao | -m- -wa- | Ngeli ya 5-6 | li- ya |
| | Luganda sanifu | | |
| <i>Nze - Ffe</i> | <i>-n- -tu-</i> | <i>Ngeli ya 1-2</i> | <i>a-ba</i> |
| <i>Ggwe - Mwe</i> | <i>-ku- -ba-</i> | <i>Ngeli ya 3-4</i> | <i>gu-gi</i> |
| <i>Ye - bba</i> | <i>-mu- -ba-</i> | <i>Ngeli ya 5-6</i> | <i>li-ga</i> |

Asili: Data kutokana na Thomson na Schleicher (2001) na Mugerwa (2005)

Data ya jedwali (5.6) inadhihirisha matumizi ya viambishi virejeshi vinavyorejelea mtenda, mtendwa na mtendewa kitendo. Virejeshi hivi hutokea baada ya njeo na kabla ya kitenzi husika kutegemea nafsi na ngeli za nomino kuwakilisha idadi na ngeli kwa umoja na wingi. Kimofosintaksia viwakilishi nafsi huzingatia mpangilio maalumu ambapo hata kikiambikwa viambishi vinginevyo viambishi hivi huwa haviathiriki kwa sababu vinabeba kiima na yambwa ya tungo. Viambishi hivi huundwa kwa kiambishi cha kiima [kwk], kikifuata kiambishi cha njeo [Knj], kiwakilishi kirejeshi ama cha nafsi au ngeli nomino [Knfs/Kng] kisha shina au mzizi wa kitenzi [MzT] (Thompson & Schleicher 2001).

Luganda na Kiswahili sanifu hutumia viwakilishi nafsi kama kipashio cha kimofosintaksia chenye uamilifu wa kisarufi katika KT kwa njia ya ujirejeleaji na urejeshi kuwakilisha yambwa na kiima. Yambwa ni nomino inayowakilishwa na mofimu za nafsi na ngeli nomino kudhihirisha mtenda, mtendwa na mtendewa tendo. Mofimu zinazotumika hutangulia kitenzi kuzingatia upatanishi wa kisarufi na huchukua nafasi karibu na mzizi wa kitenzi kuwakilisha nomino. Mofimu yambwa ni kiambishi kipatanishi cha nomino katika kirai tenzi. Mofimu hizi hupachikwa katika kirai tenzi kutegemea nomino kama neno kuu. Hii ina maana kuwa viambishi yambwa vinavyopachikwa kwenye KT hutofautiana kutokana na uainishaji wa nomino katika ngeli mbalimbali. Mifano ya data Na.(5.38) inadhihirisha mpangilio au nafasi ya utokeaji wa viambishi virejeshi na matumizi a kanuni rejeshi.

ALI-NI-PIGA

Kip nafsi3/Ngeli1 umoja –wkt uliopita-kipatanishi kiambishi yambwa- piga

WALI-TU-PIGA

Kip nafsi3/Ngeli 2 Wingi –wkt uliopita-kipatanishi kiambishi yambwa- piga

ULI-JI-LIPIA


Kip nafsi3/Ngeli 1 umoja –wkt uliopita-kipatanishi kiambishi yambwa ng1- peleka

WALI-WA-PELEKA.

Kip nafsi3/ngeli 2 wingi –wkt uliopita-kipatanishi kiambishi yambwa- peleka

Asili: Thompson & Schleicher 2001).

Mchoro 5.12: Matawi yanayodhihirisha kanuni ya kimofosintaksia ya urejeshi wa viwakilishi nafsi.



Tanbihi: KB (Kibainishi) Knfs (Kiambishi nafsi), Kng1 (kiambishi cha ngeli ya kwanza, NJ-Njeo).

Asili: Data kutokana na utafiti huu, (2021)

Mifano (5.38) na mchoro (5.12) inadhahirisha kanuni ya kimfosintaksia ya urejeshi wa viwakilishi nafsi ambavyo vinafanya dhima ya yambwa na kiima. Viambishi virejeshi vimetokea baada ya njeo na kabla ya mzizi wa kitenzi kurejelea nomino tendwa, tendewa na tendwa. Kiambishi kirejeshi katika Luganda na Kiswahili ni [m] hata hivyo utaratibu wa matumizi ya njeo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu unadhahirisha kutofautiana. Tofauti hii huenda ikapotosha usanifu matumizi ya viwakilishi hata kama muundo wake na nafasi ya utokeaji pamoja na kuzingatia upatanishi wa kisarufi utakuwa umezingatiwa. Kiswahili kimetumia kiambishi cha nafsi ya tatu [a] huku Luganda ikitumia [y na a] kuwakilisha nafsi na ngeli nomino tajwa pamoja na wakati uliopita muda mrefu uliopita.

Tofauti inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kuhusu kanuni ya urejeshi ni kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia maumbo ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza ambavyo vinafanana na kubeba dhima sawa ya kurejelea nomino kwa umoja na wingi, umbo la nafsi ya pili [ku] umoja na alamofu ya M ya Kiswahili ambayo ni [mu] katika nafsi ya tatu kwa umoja. maumbo mengine yanatofautiana kama vile maumbo ya nafsi ya pili na tatu kwa wingi. Aidha, mabadiliko ya kimofolojia yanayoathiri matumizi ya kanuni hii pamoja na uambishaji njeo hutofautiana kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, mwanafunzi ambaye L1 ni Luganda anafaa kuwa makini anapotumia viwakilishi nafsi ili usanifu usipotoshe kwa kuzingatia matumizi mwafaka ya viwakilishi nafsi, ngeli, utaratibu wa uambishaji na muundo wa viwakilishi kuhakikisha upatanifu wa kisarufi wa viwakilishi husika. Tofauti kama hizi huenda zikaathiri matumizi ya Kiswahili sanifu hasa kutokana na mwiingiliano na ukuruba uliopo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulitambua viwakilishi virejeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu na katika uchanganuzi, ilibainika kuwa

matumizi ya kanuni ya urejeshi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu huwiana na kutofautiana hasa katika maumbo na muktadha katika matumizi ya virejeshi.

5.1.3.3 Kanuni ya muungano wa viwakilishi na maneno mengine

Kanuni hii inashikilia kuwa: Viwakilishi nafsi ni mofimu maluum ambazo huunganika na maneno mengine kuunda tungo. Mofimu hizi hutumika kuwakilisha kiima na yambwa katika tungo na hudhihirika katika tungo kwa kuungana na viambishi vingevyo kama viambishi vya wakati ambavyo hudhihirika katika vitenzi. Kanuni hii ya muungano pia hurejelea utaratibu na nafasi ya utokeaji wa viwakilishi husika katika tungo.

Kupitia kwa uchanganuzi wa Oichoe, (2005), Egara, (2016), Leah & Ssuguya, (2015), utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha ambazo hudhihirisha matumizi ya kanuni ya muungano ambapo viwakilishi nafsi vimeungana na njeo pamoja na vitenzi kwa njia ya uambishaji wa viambishi husika kujenga utungo kuwakilisha kiima na yambwa katika muungano. Kwa mujibu wa matumizi haya, viwakilishi vya nafsi hutawala viambishi vya njeo na vitenzi. Katika muktadha huu, viambishi hutokea mwanzoni, vikifuatwa na njeo au wakati, vikifuatwa na mzizi ya vitenzi na kiishio. Hali hii hutokea kama viwakilishi vya nafsi vinavyotumika sio viwakilishi virejeshi vya nomino tenda, tendwa na tendewa. Viwakilishi virejeshi vinapotumika, viwakilishi vya ngeli nomino hutumika kuwakilisha nomino kuu, vikifuatwa na njeo, viwakilishi virejeshi vikifuata na kisha mzizi wa kitenzi na kiishio chake. Ukiulaji wa kuzingatia kanuni hii ya uambishaji husababisha viambishi husika vya kategoria za maneno kukosa mantiki na hivyo kupotosha maana au usanifu wa lugha kama ilivyofafanuliwa na (Thompson & Schleicher 2001). Data Na. (5.39) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za muungano na nafasi za utokeaji wa viwakilishi nafsi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

a) *A-samb-a omupiira*

Ba-samb-a omupiira

Knfs2 umoja- Mz- Knj wakati uliopo –a Knfs2 wingi- Mz- Knj wakati uliopo -a

U-na-chez-a mpira

Mnacheza mpira.

Knfs2 umoja- Knj iliyopo-Mz-a

Knfs2 umoja- Knj iliyopo-Mz-a

b) *A-n-dab-ye*

Ba-tu-lab-y-e

Knfs3-Kkirej 1- Mz- hali me

Knfs3-Kkirej 1- Mz- hali me

A-me-ni-ona

A-me-tu-ona

Knfs3/Kng1-hali timilifu- Kirej1-ona

Knfs3/Kng2-hali timilifu- Kirej1-ona

c) *A-mu-lab-ye*

ya-ba-lab-ye

Knfs3-Kkirej 1- Mz- hali me

Knfs3-Kkirej 1- Mz- hali me

a-me-**mw**-on-a

Knfs3/Kng1-hali timilifu- Kirej1-ona

a-me-**wa**-ona

Knfs3/Kng2-hali timilifu- Kirej1-ona

Asili: Data kutokana na Leah & Sseguya (2015)

Tofauti inayojitokeza ni ya matumizi ya aina ya viwakilishi nafsi. Katika muunganiko wa viambishi, utafiti huu uligundua kuwa viwakilishi nafsi vya nomino hutokea mwanzoni vikifuatwa na kategoria ya njeo na vitenzi, vile vile, matumizi ya viwakilishi nafsi virejeshi yalidhihirisha muunganiko wa viwakilishi vya ngeli za nomino, njeo, virejeshi na kisha vitenzi. Hata hivyo matumizi haya huadhirika na mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea kutokana na fonimu irabu au konsonanti kuathiriana na kusababisha mabadiliko ya fonimu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Mabadiliko haya hutofautiana kutokana na kanuni pamoja na maumbo ya fonimu na alofoni zake. Kwa hiyo tofauti za maumbo ya viwakilishi nafsi na mabadiliko ya kifonolojia ni miongoni mwa tofauti ambazo huenda yakaathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali ambayo utafiti huu unatarajia kutathimini baadaye katika lengo la tatu.

Katika Luganda, wakati mfupi uliopita wa tendo (hali timilifu –me-) huundwa kutokana na mizizi ya maneno. Baadhi ya mizizi ya maneno inayoishia na silabi [-ba, -ma, -pa, au –na], huweza kuchukua kiwakilishi cha njeo [-ye] ambapo kiishia /-a/ hubadilika na kuwa [ye]. Kwa hiyo [ye] ndicho kiambishi cha wakati mfupi uliopita wa kutendeka kwa tendo (hali timilifu –me-) na ambao huwekwa mwishoni mwa kitenzi. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambapo kiwakilishi nafsi cha tatu (3) [a] na kiambishi cha ngeli 1 kimetangulia, kikafuatwa na njeo, kiambishi kirejeshi cha nafsi ya 3 kikatoka nyuma ya kitenzi. Aidha katika mfano wa (a) kitenzi ni {laba} ambapo kiambishi kiwakilishi {n} kimesababisha mabadiliko ya kifonolojia ya fonimu /l/ kuwa /d/ kama inavyodhihirishwa katika data (5.40) kutokana na data ya utafiti huu.

a) A-**n**-dab-ye

Knfs3-Kkirej 1- Mz- hali me

A-me-**ni**-ona

Knfs3/Kng1-hali timilifu- Kirej1-ona

b) A-**mu**-lab-y-e

Knfs3/Kng1-Kkirej 1- Mz- hali me

a-me-**mw**-on-a

Knfs3/Kng1-hali timilifu- Kirej1-ona

Ba-**tu**-lab-y-e

Knfs3/Kng2-Kkirej 1- Mz- hali me

Wa-me-**tu**-ona

Knfs3/Kng2-hali timilifu- Kirej1-ona

ba-**ba**-lab-y-e

Knfs3/Kng2-Kkirej 1- Mz- hali me

wa-me-**wa**-ona

Knfs3/Kng2-hali timilifu- Kirej1-ona

Matokeo haya yanafanana na maelezo ya Oichoe (2005), Matasi & Furaha (2016), Kiyinikibi, (2021) ambao wanashadidia juu ya muungano viwakilishi nafsi, njeo pamoja na vitenzi kwa njia ya uambishaji wa viambishi husika kujenga utungo kuwakilisha kiima na yambwa ambayo kwayo hudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Aidha, Hafsa, (2016) katika utafiti wake wa mofu nafsi za Kiswahili na Kipemba, aligundua kuwepo kwa tofauti kubwa za mofu nafsi baina ya Kiswahili na kipembe. Matokeo haya yanashadidia kuwa licha ya lugha kuwa katika nasaba moja, maumbo ya mofu nafsi ambayo ni ya viwakilishi nafsi hutofautina kati ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Hali ambayo ilidhihirika katika utafiti huu ambapo ilibanika kuwa licha ya Luganda na kiswahili kuwa lugha za nasaba moja, matumizi ya kanuni ya muungano wa viwakilishi nafsi huwiana na kutofautiana katika maumbo na taratibu.

5.1.3.4 Kanuni ya uambishaji

Viwakilishi vya nafsi ni maneno ambayo hutumiwa badala ya majina ya watu au nomino. Maneno haya hutumiwa kuashiria nafsi tatu umoja na wingi yakiwakilishwa na maumbo mbalimbali ya viambishi ambayo huambikwa kwenye mizizi ya vitenzi katika KN na KT kurejelea nafsi husika (Mgullu, 1999, Chomi, 2003, Massamba, 2004 na Mbwillow, 2017). Kanuni hii inashikilia kuwa kila lugha huwa na maumbo ya kipekee yanayotumika kuunda vipashio vya kisarufi vya lugha kuwakilisha usahihi wake kimatumizi. Vilevile kanuni hii hudai kuwa uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi (uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu (Kisakwah, 2014), Leah & Sseguya, (2014), Namugala, (2014), Massamba & Kihore (2003). Kila nomino huwakilishwa na maumbo ya viambishi dhahiri na kapa ambayo huambikwa kwenye kategoria za maneno katika tungo kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa nomino kuu. Thompson na mwenzake (2001) wanadai kuwa, karibia vitenzi vingi vilivyofanyiwa uambikaji, lazima kuwe na viambishi viwakilishi vya nafsi/kiima na njeo. Hata kama uambikaji huo si kubwa, mara nyingi viambishi hivyo lazima viwepo.

Kwa mujibu wa uchanganuzi wa mapitio ya maandishi ya Chomi, (2003), Massamba, (2004) na Mbwillow, (2017). Leah & Sseguya, (2015), Mgullu, (1999), Namugala, (2014), utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili hutumia maumbo mbalimbali ya viambishi kuwakilisha nomino kuu katika tungo. Maumbo haya ni maumbo dhahiri ambayo huwakilisha nafsi ya kwanza, pili na tatu kwa umoja na wingi. Maumbo haya hutumika

kuwakilisha nomino ambayo ni kapa au dhahania inayokisiwa kutenda, kutendwa au kutendewa tendo. Aidha, maumbo haya huambikwa mwanzoni mwa vitenzi kuwakilisha nomino kuu katika KT yakiwa na dhima ya kelezua juu ya kiima na yambwa. Data Na. (5.41) kutokana na data ya utafiti inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za uambishaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

| | |
|-------------------------------|---------------------------------------|
| Umoja | Wingi |
| c) <i>Nkulabye mu'kibiina</i> | Tukulabye mu'bibina (Luganda) |
| Nilikuona darasani | Tulikuona darasani (Kiswahili) |
| d) <i>Osamba omupiira</i> | Musamba omupiira (Luganda) |
| Unacheza mpira | Mnacheza mpira (Kiswahili) |
| e) <i>Asamba omupiira</i> | Basamba omupiira (Luganda) |
| Anacheza mpiira | Wanacheza mpira (Kiswahili) |
| f) <i>Yantabye</i> | yatulabye (Luganda) |
| Aliniona | Alituona (Kiswahili) |
| g) <i>Yakulabye</i> | yamulabye (Luganda) |
| Alikuona | alimwona (Kiswahili) |
| h) <i>yamulabye</i> | yabalabye (Luganda) |
| Alimwona | Aliwaona (Kiswahili) |

Asili: Data kutokana na Leah & Sseguya (2015)

Mofimu zilizokolezwa zinadhihirisha kanuni ya uambishaji wa viwakilishi vya nafsi tegemezi. Viambishi hivi ni viambishi vinavyotumika badala ya nomino ambavyo huwekwa mwanzoni mwa kitenzi, vikifuatwa na njeo kisha kitenzi. Aidha, kwa njia ya urejeshi, viambishi hivi huambikwa baada ya njeo na kabla ya mzizi kuwakilisha nomino kuu inayorejelewa kama kiima au yambwa tenda, tendwa na tendewa. Kanuni hii inashikilia kuwa lazima utaratibu wa uambishaji wa viwakilishi hivi uzingatiwe ili kuhifadhi usanifu wa lugha. Matumizi ya viwakilishi hivi lazima uzingatie muktadha na kila nafsi iwakilishwe na kiambishi chake bayana kinachopachikwa katika kitenzi pasi kuvurugwa.

Tofauti iliyobainika kimatumizi ni kuwa Luganda na Kiswahili sanifu kama lugha mbili tofauti, hutumia viambishi viwakilishi vya kipekee kimaumbo ambavyo hutumika kuwakilisha nomino husika. Kwa mfano, Luganda hutumia mofimu [n, o, a na tu, mu, ba] pamoja na viwakilishi nafsi virejeshi [n, ku, mu na tu, mu, ba]. Kiswahili hutumia [ni, ku, m] na [tu, wa, wa]. Aidha, matumizi ya viwakilishi hivi huathirika na mabadiliko ya kifonolojia ambayo hutofautiana. Matumizi ya viambishi hivi viwakilishi yasipotumika kwa umakini

kuzingatia utaratibu wa uambishaji huenda yakaathiri usanifu wa lugha baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. hali ambayo utafiti huu unachunguza kutathimini athari za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. matokeo ya utafiti huu yanaendana na maelezo ya Rose, (2009), Leah & Sseguya, Namugala (2014), Mgullu, (1999), Massamba na Wenzakae, (2003) na Oichoe ambao walitambua kanuni ya uambishaji wa maneno katika Luganda na Kiswahili hasa, viwakilishi nafsi katika tungo kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu.

5.1.3.5 Kanuni ya kimofolojia (kimaumbo) ya viwakilishi nafsi

Kanuni hii hushikilia kuwa; viwakilishi ni maumbo ambayo hukaa badala ya majina ya watu. Maumbo haya ni maumbo huru (halisi) na maumbo tegemezi ambayo huwakisiwa na viambishi tofauti. Maumbo haya hutofautiana kimatuzi ila huwakilisha dhana moja ya kuwakilisha nomino tendi (kiima) na tendwa (yambwa). Kulingana na kanuni hii, ukiukaji wa kimatuzi wa viambishi hivi huweza kupotosha usanifu wa lugha (Mgullu, 1999; Chomi, 2003; Oichoe, 2005; Leah & Sseguya, 2015).

Kwa mujibu wa data kutokana na Leah & Sseguya, (2015), Katamba, (2003), Oichoe, (2005), Thompson & Schleicher, (2001). na Matasi & Furaha (2016), Kisakwah, (2014) kanuni hii, ilibaini kuwa Luganda na Kiswahili hutumia maumbo tofauti kusisitiza utendaji wa vitendo na kuwakilisha utendaji milikishi wa nomino husika. Maumbo huru ya viwakilishi nafsi vinapotumika pamoja na vitenzi, viambishi halisi au huru hudondoshwa na badala yake viambishi tegemezi kutumika. Pia, viambishi hivi vyote vinaweza kutumika katika sentensi kiupatanifu kusisitiza ujumbe/ kiima. Ukiukaji wa matumizi ya maumbo haya hutofautisha dhima ya uwakilishi nafsi. Mfano ya data Na.(5.42) wa matumizi ya viwakilishi nafsi katika tungo inadhihirisha uwiano na tofauti za kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Nze nsamba omupiira Ffe tusaamba emipiira Nsamba omupiira Tusamba emipiira
Mimi ninacheza mpira **Sisi** tunacheza mpira **Ninacheza** mpira **Tunacheza** mpira
Ggwe Osamba omupiira Mwe msamba omupiira Osamba omupiira Msamba
emipiira
Wewe unacheza mpiira **Nyinyi** mnacheza mpiira **Unacheza** mpiira **Mnacheza** mpira
Ye asamba omupiira Bba asamba omupiira Asamba omupiira Basaamba emipiira
Yeye anacheza mpira **Wao wanacheza mpira** **Anachezampira** **Wanacheza** mpira

Asili: Data kutpokana na Matasi & Furaha, (2016) na Sseguya, (2015).

Kwa mujibu wa kanuni hii, Luganda na Kiswahili zimewakilishwa na maumbo ya viwakilishi huru na viwakilishi tegemezi ambavyo lazima watumiaji kuzingatia pasi kwenda kinyume ili

kulinda usanifu wa lugha husika. Kwa kurejelea jedwali (5.5) na (5.6) la uwiano na tofauti za viwakilishi vipatanishi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu katika sura ya hii, kuhusu maumbo huru na tegemezi ya viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu, ni dhahiri kwamba kuna uwiano na tofauti baina ya maumbo ya viwakilishi vya nafsi kimofolojia na kisintaksia kuhusiana na viambishi awali vya mtenda vya nafsi ya kwanza, pili na tatu umoja na wingi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Aidha, Viwakilishi vya nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu huchukua nafasi ya kwanza kimuundo katika utungo kuwakilisha nomino. viwakilishi nafsi huru hutangulia katika tungo vikifuatwa na viwakilishi nafsi funge kutegemea muktadha wa sentensi. Luganda na Kiswahili sanifu pia hutumia viwakilishi vya nafsi virejeshi ambavyo hutokea baada na nyuma ya mzizi wa kitenzi na kutumika kurejelea nomino kwa kauli mbalimbali za utendaji. Tofauti hizi zinatokana na matumizi ya maumbo tofauti yanayotumika kuwakilisha kiima na yambwa. Kimofolojia, kuna viambishi huru ambavyo hujitokeza kama mofimu huru yenye maana inayojitosheleza na kisintaksia kuna viambishi vya upatanishi wa kisarufi ambavyo hutumika pamoja na viwakilishi huru kwa njia ya anafora kuisitiza nafsi ya kwanza milikishi.

Uwiano unaojitokeza ni kuwa kimofosintaksia, Luganda na Kiswahili sanifu hutumia maumbo ya viwakilishi nafsi tegemezi [tu] kuwakilisha viambishi vya nafsi ya kwanza wingi na [a] kuwakilisha maumbo ya viambishi viwakilishi vya nafsi ya tatu umoja. Aidha, uwiano mwingine unaojitokeza ni ule wa matumizi ya maumbo ya [mu] na [m]. Maumbo haya ni ya nafsi ya pili ambapo [mu] ni alomofu ya [m] ya Kiswahili sanifu ambapo zote zimetumika kuwakilisha nafsi ya pili wingi. Kwa hiyo katika matumizi, maumbo haya yanafanana hata ingawa yanatofautiana kifonolojia. Tofauti ambayo ni dhahiri ni ile ya maumbo ya nafasi ya tatu. Maumbo haya yanatofautiana hata ingawa yanafanya kazi sawa ya kuwakilisha nafsi ya tatu wingi. Luganda hutumia umbo [ba] na Kiswahili kutumia umbo la [wa] katika Kiswahili sanifu. Maumbo haya yanatofautiana.

Matokeo haya yamejadiliwa na Taher, (2021), Habwe & Karanja, (2004), Massamba na wenzake (2003) na Katamba, (2003) wanadhihirisha uwiano na tofauti za Luganda na Kiswahili kutumia maumbo tofauti kuisitiza utendaji wa vitendo na kuwakilisha utendaji milikishi wa nomino husika katika tungo. Aidha kulingana na wataalamu hawa, maumbo huru ya viwakilishi nafsi vinapotumika pamoja na vitenzi, viambishi halisi au huru hudondoshwa na badala yake viambishi tegemezi kutumika. Aidha, viwakilishi hivi vyote au

maumbo haya hutumika katika sentensi Pia, kiupatanifu kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo kwa ajli ya kusisitiza ujumbe. Mathalan, Kwa kuzingatia maumbo ya kimofolojia ya viwakilishi huru, imebainika kuwa maumbo ya nafsi ya kwanza na pili ya Luganda na Kiswahili yanatofautiana na nafsi ya tatu kuoyesha kukaribiana. Licha ya uwiano huo, ilibainika kuwa Luganda ilidodosha silabi ya pili [ye] na kutumia umbo [ye] kuwakilisha nafsi ya tatu umoja huku Kiswahili ikitumia umbo [yeye]. Kimatumizi, maumbo haya yasipotumika kikamilifu, huenda yakapotosha usanifu wa Kiswahili sanifu hasa pale ambapo tofauti inajitokeza kimatamshi na kimaandishi.

5.1.4 Uwiano na tofauti za kanuni za Vikanusho kimofosintaksia

Ukanushaji ni kauli, hali au tendo la kukataa jambo fulani. Kukataa au kupinga tendo yakini lililoelezwa katika kitenzi. Ukanushaji huongozwa na kanuni maalumu na kila lugha hudhihirisha kanuni zake. Ukiukaji wa kuzingatia kanuni mwafaka huweza kupotosha usanifu wa lugha husika kisarufi na hata kisemantiki. Utafiti huu ulichunguza kanuni za ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu na kufafanua uwiano na tofauti zilizojitokeza katika kila kategoria ya kisarufi. Utafiti huu ulichunguza kanuni za ukanushaji wa vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli na viwakilishi vyake, viwakilishi nafsi, nyakati na hali kama inavyofafanuliwa na wataalamu wa kiisimu wa Luganda na Kiswahi sanifu pamoja na matumizi kama inavyotolewa na wanafunzia wa Kiswahili sanifu ambao L1 ni Luganda.

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni katika vitabu vya kisarufi vilivyoidhinishwa na vya ziada, tasnifu, makala ya utafiti, na upekuzi wa maandishi maktabani ulibaini kuwa, ukanushaji katika Luganda na Kiswahili sanifu, hufuata vipashio vya kisarufi maalumu. Kila kategoria ya kisarufi inayoathiri ukanushaji hujitokeza na kanuni ambazo ni za kipekee. Kwa kuzingatia mihimili ya ubia na upatanifu ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky, (1981) ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili huwiana na kutofatiana katika kanuni za ukanushaji kama inavyochanganuliwa hapa chini.

5.1.4.1 Uwiano na tofauti ya kanuni za Ukanushaji wa Ngeli za Luganda na Kiswahili

ukanushaji katika Lugha nyingi za Kibantu hufuata vipashio vya kisarufi maalumu. Vipashio hivi ndivyo vinavyojenga usarufi wa lugha. Uwiano na tofauti za ukanushaji ni muhimu ujiegemeze katika vipashio vya kisarufi ambavyo vinajenga tendo linalotendeka. Tendo hubeba dhima ya kisemantiki ya tungo. Kwa hivyo ni kitendo kinachobeba vikanushi. Kulingana na Lupogo, (2021), Polome (1967) alibainisha baadhi ya vipashio vinavyowekwa

kwenye vitenzi na miongoni mwanzo ni viwakilishi vya ngeli. Viwakilishi vya ngeli ni maumbo wakilishi ya ngeli za nomino. Kwa hiyo, utafiti huu ulichunguza ukanushaji kwa kuegemea juu ya ngeli za nomino. Katika uchambuzi, utafiti huu ulibaini kanuni zifuatazo zilizodhihirisha uwiano na tofauti ya ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.4.1.1 Kanuni ya uambishaji (uongezaji) vikanushi kifonolojia

Kanuni ya ukanushaji wa nomino huzingatia ngeli za nomino. Sheria inayohusika katika ukanushaji wa nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu ni ya kuongeza maumbo kanushi kwenye viambishi awali vya ngeli ambavyo pia ni viambishi vipatanishi vya ngeli husika. Matokeo ya uchanganuzi wa data kutokana na, Matasi na Furaha (2016), Habwe & Karanja, (2004), Baertlein & Ssekitto (2014), Lupogo, (2021) yalidhihirisha uwiano wa Luganda na Kiswahili sanifu kutumia kanuni hii kwa kuongeza vikanushi mwanzoni mwa viambishi awali vya ngeli ambavyo pia ni viambishi vya upatanishi wa nomino kiidadi kuwakilisha kauli ya ukanushaji. Maumbo kanushi yaliyoongezwa katika Luganda yalikuwa maumbo ya kifonolojia ya viambishi awali vya ngeli kuanza na konsonanti au vokali. Maumbo hayo yalikiwa [te-] na (t-) Kiswahili kiliwakilishwa na maumbo [ha] na [hu] (Hyman (2018). Kisheria ni kuwa katika Luganda, [te-] huongezwa kwenye viambishi awali vya ngeli ambavyo pia ni viambishi vipatanishi vya ngeli husika ikiwa kiambishi awali cha nomino kinachohusika kinaanza na konsonanti. Aidha, kiambishi kiwakilishi cha nomino kikianza na vokali, lazima kikanushi [t-] kiongezwe kabla ya kiambishi cha ngeli husika. Katika Kiswahili umbo [ha] au [hu] huwekwa nyuma ya viambishi vipatanishi vya msingi vya ngeli kwa umoja na wingi. Ukiukaji wa kanuni hii ya uambishaji wa viambishi vikanushi kuzingatia maumbo ya kifonolojia ya VPM katika tungo, huweza kupotosha usanifu wa lugha husika.

Utafiti huu pia ulibaini tofauti katika matumizi ya kanuni ya uambishaji vikanushi baina ya Luganda na Kiswahili. Kwa mujibu wa matokeo, ilibainika kuwa; Luganda hutegemea fonimu konsonanti na irabu unaojitokeza katika vitenzi kama viambishi vipatanishi viwakilishi vya nomino tendaji. Ukanushaji huu ni wa kuongeza kikanushi [t-] kwenye kiambishi ngeli awali kilichoambishwa kwenye kitenzi kinachoanza na irabu au vokali na kuongeza kikanushi [te-] nyumba ya kiambishi kipatanishi cha nomino tendaji katika tungo. Kiswahili hutumia viwakilishi vikanushi [ha] na alomofu yake [hu] ambavyo huambikwa nyuma ya kiambishi kipatanishi cha nomino kiidadi (umoja na wingi) kimofosintaksia kudhihirisha kauli ya ukanushaji.

Tofauti hii ni ya kimaumbo ambapo Luganda huzingatia maumbo ya kifonolojia inayotokea mwanzoni mwa vitenzi kisintaksia ilhali Kiswahili sanifu huzingatia mofimu za ukanusho kama inavyodhihirishwa katika maeleze ya uwiano na tofauti za ukanushaji wa Luganda na Kiswahili katika data za jedwali (4.18, Uk. 124). Data inayojitokeza inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya uambishaji wa viambishi vikanushi kifonolojia na kimofolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kanuni ya kifonolojia ilitumika na Luganda ambapo fonimu [t- na te-] iliambishwa kabla ya kiambishi awali cha nomino katika ngeli ambacho pia ni kiambishi kipatanishi cha msingi cha nomino katika ngeli katika tungo, huku Kiswahili kikitegemea mofimu au mofu kanushi ya [ha] kudhihirisha ukanushaji kimofosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa viambajengo katika tungo.

Matokeo haya yanashadidiwa na Lupogo, (2020), Mulei, (2020) na Mulei, (2020) na Taher, (2013;2021), Chisia, (2012) ambao wanadhihirisha mfumo wa lugha hizi mbili za Luganda na Kiswahili kuongeza viambishi vikanushi nyuma ya vitenzi na nyuma ya viambishi vipatanishi vya msingi vya ngeli katika nomino. Aidha, Hyman (2018) anaeleza kuwa katika ukanushaji wa Luganda kunadhihirika matumizi ya kikanushi {te} ambacho huwekwa nyuma ya konsonanti na t- ambacho huwekwa nyuma ya irabu. Anasema kuwa : “...we see from the plural forms that the negative prefix is tè- before a consonant. Second, the (surface) realization of the negative prefix is t- before a vowel ”(Hyman, 2018: 3). Aidha anaungwa Mkono na Mulei (2020) katika athari za ukopaji wa ukanushaji na Lupogo (2020) ambao wanakubaliana kuwa vikanushi vya Luganda huwekwa mwanzoni mwa maneno yanayokanushwa. Aidha kwa makubaliano na maoni ya Mulei (2020), Lupogo, (2021) anaeleza kuwa;

Maumbo ya ukanushi katika lugha ya Kiswahili yanayotajwa na wataalamu mbalimbali ni yale yanayoambikwa katika maneno hususani vitenzi kama vile ha (halii), si (siendi), ja (hawajalima), ku (hakutuelewa), kuto/to (kuto fika kwake), sipo/si (wasipotuona) na I (siibi) (Lupogo, 2020: 9).

Aidha kwa mujibu wa data za utafiti huu, ilibainika kuwa maumbo ya ukanushaji baina ya Kiswahili na Luganda ni maumbo ambayo huambikwa katika vitenzi na hujitokeza mwanzoni kama sehemu ya viambishi awali kudhihirish sifa za uhusiano milikifu na unganifu ya maneno katika tungo kueleza hali ya kisarufi. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha uwiano na tofauti baina ya kanuni ya uambishaji katika ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili. Matokeo yaliyojitokeza ni kuwa Luganda na Kiswahili iliwiana katika uambishaji na nafasi ya utokeaji wa maumbo wakilishi ya ukanushaji na kutofautina katika maumbo ambapo ukiukaji wa

kanuni za uongezaji au uambishaji huweza kuathiri uhusiano milikifu na unganifu baina ya maneno katika tungo.

5.1.4.1.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa viambishi vikanushi

Kupitia kwa uchanganuzi wa kazi za Lupogo, (2020: 2021), Mulei, (2014: 2020), Kihore, Msanjila na Massamba (2003), Mgullu, (1999), Leah & Sseguya, (2015), na Ngonyani, (2001). Utafiti huu ulibaini kuwa uambishaji wa mofimu au viambishi vikanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu hutokea mwanzoni kabla au nyuma ya kitenzi katika muundo wa kirai kitenzi. Mofimu hizi hutokea mwanzoni au kabla ya kitenzi, nyuma ya kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino tendaji. Kulingana na data za utafiti huu maktabani kutokana na Mgullu (1999), kila ngeli katika lugha hizi huwakilishwa na mofimu ya ukanushi ambayo hutokea nyuma ya kiwakilishi kipatanishi cha nomino au kiwakilishi yambwa rejeshi ya nomino kuu katika tungo tenzi. Ukiukaji wa kuambisha vikanushi kutegemea ngeli nomino, nafasi na nyakati huweza kuvuruga usanifu wa lugha husika, mantiki na maana ya usemi au maandishi.

Tofauti iliyojitokeza ni kuwa mazingira ya utokeaji wa vikanushi vya Luganda vilizingatia maumbo ya kifonolojia ya viambishi awali vya upatanishi wa nomino vinavyotokea kabla ya vitenzi kama VPM vya ngeli nomino. Kwa mujibu wa kanuni hii, uambishaji ulitegemea kama viambishi vilivyotokea vilikuwa konsonanti au irabu. Luganda iliongeza [t-] kama kiambishi ngeli kilianza na irabu na [te-] kama kiambishi ngeli kilianza na konsonanti. Kiswahili kilijali zaidi nafasi ya uambishaji nyuma ya viambishi awali vya ngeli ambavyo pia ni viambishi vipatanishi vya ngeli nomino husika. Kiswahili kilitumia kikanushi [ha] kilichoambishwa kabla ya kiambishi kipatanishi awali cha nomino tendaji. Wakati mwingine, kiambishi hiki kiliathiriana kimofonolojia na viambishi vipatanishi vya msingi na badala yake alomu [hu] kutumika kama kikanushi. Kwa mfano katika ngeli za U-I, U-Zi, U-Ya na U ambapo kanuni ya kimofonolojia ya udondoshaji wa fonimu /a/ hutokea na badala yake [hu] kutumika badala ya [hau] kama inavyojitokeza katika data (5.43) ya data kutokana na utafiti huu (2021). (5.43)

Omuyizi agamba ntino bakuyita (Luganda)

Omuyizi t- a- gamba ntino bakuyita
KKn- KnjKngl- T

Mwanafunzi anasema kwamba unaitwa (Kiswahili)

Mwanafunzi ha- ja – sema unaitwa

| | | | | |
|--|-------------------|----------------------|-------------------|--|
| | <i>KmKknNg-</i> | <i>KmKknj-</i> | <i>T</i> | |
| | <i>Abayizi</i> | <i>bageze</i> | <i>mubibiina</i> | <i>(Luganda)</i> |
| | <i>abayizi</i> | <i>te-</i> | <i>ba-</i> | <i>genze mubibiina</i> |
| | <i>KmKkn-</i> | <i>Kn2-</i> | <i>KmKknj-T</i> | |
| | <i>Wanafunzi</i> | <i>wameenda</i> | <i>darasani</i> | <i>(Kiswahili)</i> |
| | <i>wanafunzi</i> | <i>ha-</i> | <i>wa-</i> | <i>ja-</i> <i>enda madarasani</i> |
| | <i>KmKkn-Kn2-</i> | <i>KmKknj-</i> | <i>T</i> | |

Kiambishi kikanushi [KmKkn] Kiambishi ngeli [Kng] Kiambishi kikanushi cha njeo [kmKknj] Kikanushi [ha] kimewekwa nyuma ya kiambishi cha upatanishi cha ngeli nomino mwanzoni kuwakilisha kauli kanushi katika lugha ya Kiswahili sanifu. Aidha, alomofu [hu-] hutumika katika kukanusha viambishi vipatanishi vya ngeli ambavyo huwakilishwa na kiambishi cha upatanishi ngeli kwa umoja kinachoanza na [u-] hasa katika ngeli za [u-i, u-zi, u-u na u-ya] ambapo kiambishi kipatanishi cha umoja [u] kinaambishwa kikanushi [hu] + [u] na kudondosha fonimu /u/ ya pili na hivyo kuwa na kikanushi [hu-] ambacho ni alomofu ya kikanushi [ha-] kinachotumika kuwakilisha kauli kanushi. Luganda ilidhihirisha kuongeza fonimu kanushi [t] kwenye viambishi awali au vibainishi vya upatanishi wa kisarufi unaonza na vokali na [te] mwanzoni mwa kiambishi kipatanishi cha ngeli kinachotanguliwa na konsonanti kama viwakilisha awali vya upatanishi wa nomino. Kwa jumla lugha hizi mbili huzingatia kuweka mofimu kanushi nyuma ya vitenzi na viambishi vipatanishi vya nomino na njeo katika KT.

Matokeo ya kanuni hii yanashadidiwa na Lupogo, (2021) na Hyman, (2018) pamoja na Mulei, (2020) wanaofafanua nafasi ya utokeaji wa vikanushi. Wanafafanua kuwa ukanushaji katika Luganda na Kiswahili ni ule wa kuambisha vikanushi mwanzoni au nyuma ya vitenzi kama sehemu ya viambishi awali. Aidha Lupogo (2021) katika maelezo yake ya kuanisha maumbo ya vikanushi katika Kiswahili, anavitambua na kusema kuwa; *Maumbo hayo huambikwa katika vitenzi na hujitokeza mwanzoni kama sehemu ya viambishi awali* (Lupogo, 2021:2). Maelezo haya yanaungwa mkono na Hyman, (2018) ambaye anaelezea nafasi ya utokeaji wa vikanushi vya Luganda [te-] na [t-]. Katika maelezo yake, Luganda huongeza kikanushi [t-] kwenye kiambishi ngeli awali kilichoambishwa kwenye kitenzi kinachoanza na irabu au vokali na kikanushi [te-] kuongezwa nyumba ya kiambishi kipatanishi cha nomino tendaji katika tungo.

5.1.4.1.3 Kanuni ya kimofonolojia

Kanuni hii hushikilia kuwa fonimu irabu na konsonanti zinapotokea katika ujirani wa fonimu fulani huweza kuathiriana na kusababisha mabadiliko ya fonimu inayotumika katika maandishi au mazungumzo. Kwa mujibu wa uchanganuzi wa maandishi ya Hyman, (2018), Katamba, (2003), Leah & Sseguya, (2015) na Mgullu, (1999), utafiti huu uligundua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiana katika matumizi ya kanuni ya kimofonolojia. Ilibainika kuwa maumbo kanushi ya Kiswahili huathirika na kanuni hii wakati wa kukanusha tungo zilizotumia nomino zinazotoka katika ngeli za U-I, U-Zi, na U-U. Katika kanuni hii, irabu [a] ya kikanushi [hu] iliungana na kipatanishi cha ngeli [u] cha umoja na kusababisha mvutano na udondoshaji wa fonimu ya kikanushi [a] na kubakisha fonimu /u/ ya kiwakilishi cha nomino. Kwa hivyo, kikanushi cha umoja katika ngeli hizi huwa [hu] badala ya [hau] kama inavyoelezwa katika mifano (5.44) ya data kutokana na utafiti huu (2021)

- | | | |
|---------------------------------------|---------------------------|-----------------------------------|
| a) Mkate ulinunuliwa | Mikate ilinunuliwa | |
| <i>Mkate h[-a-u]kununuliwa</i> | <i>Mkate hukununuliwa</i> | <i>Mikate haikununuliwa</i> |
| b) Uzi ulikatika | Nyuzi zilikatika | |
| <i>Uzi h[-a-u]kukatika</i> | <i>Uzi hukukatika</i> | <i>Nyuzi hazikukatika</i> |
| c) Unga ulimwagika ukazoleka | | Unga ulimwagika ukazoleka |
| <i>Unga h[a-u]kumwagika ukazoleka</i> | | <i>Unga hukumwagika ukazoleka</i> |

Asili: Data kutokana na Sakwa na wenzake (2013)

Tofauti iliopo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa Luganda haidhihirishi matumizi ya kanuni hii bali kanuni ya kifonolojia ya kuambisha viambishi vikanushi [t-] kwenye viambishi vipatanishi vya ngeli vinavyoanza na irabu na [te-] kwenye viambishi vipatanishi vya nomino vinavyoanza na konsonanti.

Matokeo haya yanashabihiana na ufafanuzi wa Mulei, (2014), Ngonyani, (2001) na Chomi, (2003) na Massamba na Wenzake (2003) ambao wanadhihirisha utokeaji wa kanuni ya kimofonolojia wa viambishi vikanushi kupatwa na mabadiliko ya kimofonolojia katika mazingira anuai. Mathalani, Massamba na wenzake (2003) akinukuliwa na Makini, (2015) akikubaliana na wataalamu hawa (washatajwa) anasema kuwa; *Katika kiwango cha kifonolojia mofimu mbili zinapokutanishwa kuna mambo mawili yanayoweza kutokea. Ama kugotana huku kunaweza kuleta mabadiliko katika kimoja kati ya vipande sauti vinavyohusika au kutakuwa hakuna badiliko lolote.* Vilevile, Lupogo (2021) anashadia kanuni hii akisema kuwa; “...kuna vitenzi vyenye maumbo ya ukanushi ambayo yanaweza kujitokeza katika sura mbili, sura hizo ni [ha] na [hu]....” (Lupogo, 2021:103).

Hyman (2018) naye anadhihirisha kanuni ya kimofolojia kujitokeza katika Luganda. Katika ufafanuzi wake, ilidhihirika kuwa ukanushaji katika Luganda huathirika na kanuni ya kimofonolojia wakati wa uambishaji wa vikanushi vya Luganda kwenye mfuatano wa vokali ambazo huenda ikasababisha athari za udondoshaji, uongezaji, muunganiko, uyeyushaji na kujenga matamshi sahihi isiyikiuka usarufi. Matokeo haya yanadhihirisha kuwepo kwa uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni hii, ya uambishaji ambapo maumbo ya uambishaji yazipofuata sheria ya upatanifu, uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo hukosa usanifu. Utafiti huu umethiirisha ubia na upatanifu ambao kila lugha inadhihirisha matumizi ya kanuni moja ila katika upatanifu, lugha hizi zinatofautiana katika maumbo. Hali ambayo inadhihirisha lugha hizi kuwa lugha mbili tofauti zenye upekee wake kimofosintaksia.

5.1.4.1.4 Kanuni ya upatanishi wa mofimu kanushi na KPM cha nomino

Mofimu za ukanushaji katika Luganda na Kiswahili hujitokeza katika muundo wa kirai tenzi [KT] kama kiambishi awali kinachoambishwa kwenye kitenzi. Luganda hutumia mofimu kanushi [t- na te-] na Kiswahili sanifu kutumia kikanushi [ha]. Matumizi na utokeaji wa mofimu hizi hutegemea viambishi vipatanishi vya ngeli nomino vinavyoambikwa kwenye vitenzi kama viwakilishi vya nomino tendaji. Pia, matumizi ya vikanushi hivi hutegemea maumbo ya kifonolojia ya viambishi vipatanishi vya ngeli nomino tajwa.

Kwa mujibu wa data kutokana na Mayaka, (2012), Makini, (2015), Owino, (2016), Leah & Sseguya, (2015) na kwa kushirikisha mihimili ya ubia na upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na upatanifu, utafiti huu ilibaini kuwa kifonolojia, Luganda huongeza fonimu kanushi [t] kwenye viambishi awali au viambishi vya upatanishi wa kisarufi vinavyoanza na vokali na mofimu [te] mwanzoni mwa kiambishi kipatanishi cha ngeli kinachotangukiwa na konsonanti kama viwakilishi awali vya upatanishi wa nomino. Aidha, Kiswahili sanifu huathirika na kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji wa fonimu /a/ ya kikanushi [ha] na badala yake kutumia fonimu inayowakilisha nomino (kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino) za U-I, U-Zi na U-U kwa umoja. Kimofolojia, viambishi vikanushi huambikwa nyuma ya kiambishi kipatanishi cha nomino kilichoambikwa kwenye KT. Kanuni ya uambishaji wa viambishi hivi ni wa kiupatanifu, ukiukaji wa kutotumia viambishi kwa utaratibu unaofaa wa maumbo, nafasi yake ya utokeaji na kuzingatia mabadiliko ya kimofolojia huweza kuathiri mofosintaksia ya kipashio na kupotosha uhusiano wa viambajengo wa kuonyesha uhusiano milikifu na

5.1.4.1.5 Kanuni ya mofolojia ya vikanushi na utokeaji wake katika tungo

Kanuni hii inazingatia uambishaji wa mofu kanushi mwafaka katika vipashio mbalimbali za sentensi au viambajengo kutegemea mofu kanushi zinazotambulika katika lugha mahususi. Kwa mujibu wa kanuni hii kama inavyofafanuliwa na Ngonyani (2001) na Hyman (2018), Leah & Sseguya, (2015) Luganda huwakilishwa na vikanushi vya aina tatu, vikanushi vya kutumia mofu [si] nyuma ya vivumishi na nafsi ya kwanza umoja, mofu [t-] ya viambishi vipatanishi vinavyoanza na irabu katika vitenzi na mofu [te-] ya viambishi vipatanishi vya nomino vinavyoanza na konsonanti. Kiswahili sanifu huwakilishwa na mofu [si] ya kukanusha kiambajengo kisicho kitenzi na kikanushi [ha-] kinachotokea katika muundo wa kitenzi au KT kama inavyojitokeza katika data ya (4.18, Uk. 115), data ya Na.(4.20, Uk. 118) ambayo inadhihirisha mofu kanushi [si-, t- na te] za Luganda sanifu na mofu [si- na ha-] zinazotumika katika Kiswahili sanifu] kutokana na data ya utafiti.

Matokeo ya uchanganuzi wa data kutokana na Ngonyani, (2001), Baertlein & Ssekitto (2014) na Immanuel, (2019) ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiana na kutofautiana katika matumizi ya kanuni hii. Luganda hutumia vikanushi [t-] na [te-] kwenye sentensi za amri pamoja na sentensi za maelezo peke yake kuzingatia kanuni ya fonolojia ya maumbo ya viambishi ngeli vinavyoanza na irabu na konsonanti mtawaliwa. Kiswahili sanifu hutumia kikanushi [si-] kwenye sentensi za amri katika ngeli mbalimbali na mofu [ha-] pamoja na alamofu [hu] katika viambishi vipatanishi vya ngeli nomino za umoja katika ngeli za ngeli za U-Zi, U-U na U-I kwenye sentensi za maelezo. Matokeo haya yanaendana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ambapo ilibainika kuweppo kwa wiano na tofauti katika matumizi ya kanuni kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu. Aidha ilibainika kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti licha ya kuwa lugha za nasaba moja.

Kwa kuzingatia kanuni hii ya mofolojia ya vikanushi na utokeaji wake kama ilivyoelezwa na Leah & Seugaya (2015), Ngonyani, (2001), Mgullu, (1999) Utafiti huu ulibaini pia kuwa Kiswahili hutumia kikanushi [si-] katika ngeli mbalimbali kwenye sentensi za amri au maombi pasi sentensi za maelezo. Kwa mujibu wa kanuni hii, mofu [si-] inapotumika, lazima itokee baada ya kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino, nyuma na karibu na kitenzi kwa umoja na wingi. Ukiukaji wa kutambua nafasi ya kikanushi hiki, hupotosha usanifu wa sentensi za amri au maombi na ambayo pia ni kinyume na kanuni ya kukanusha sentensi za maelezo. Kinyume na Kiswahili sanifu, Luganda sanifu ilionyesha kuwa kikanushi [si-] hakitumiki kwenye ngeli bali kwenye vivumishi na nafsi ya kwanza umoja. badala yake.

Katika ukanushaji wa sentenzi za maombi au amri za ngeli mbalimbali, wao hutumia mofu [t-] ya viambishi awali vya ngeli vinavyoanza na irabu na mofu kanushi [te-] kwenye viambishi vipatanishi vya ngeli nomino za sentensi za maelezo na amri au maombi kama inavyojitokeza katika data Na.(5.46) inayoonyesha uwiano na tofauti katika matumizi kutokana na data za utafiti:

| | | |
|------------------------------|--------------------------------|-------------------------------|
| <i>Omuyizi ayitibwe</i> | <i>Omuyizi tayitibwa</i> | <i>ngeli ya [a-ba/a-wa]</i> |
| Mwanafunzi aitwe | mwanafunzi asiitwe. | |
| <i>Omugati gusalibwe</i> | <i>omugati tegusalibwa</i> | <i>Ngeli ya [gu-gi/u-i]</i> |
| Mkate ukatwe | Mkate usikatwe | |
| <i>Esigiri ekumibwe</i> | <i>esigiri tekumibwa</i> | <i>Ngeli ya [e-zi/li-ya]</i> |
| Jiko liwashwe | Jiko lisiwashwe | |
| <i>Ebitanda bilongozebwe</i> | <i>ebitanda tebilongosebwa</i> | <i>Ngeli ya [ki-bi/ki-vi]</i> |
| Vitanda vitengenezwe | Vitanda visitengenezwe | |

Chanzo: Data kutokokana na Leah & Sseguya (2015) na Chesswas (1967)

Kwa mujibu wa kanuni hii ilibainika kuwa kwa kuzingatia kanuni ya mofolojia ya mofu kanushi na utokeaji wake, Kiswahili sanifu hutumia mofu kanushi [si-] ambayo huwekwa baada ya kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino huku Luganda ikitumia mofu kanushi [t- na -te] ambazo zilitokea mwanzoni mwa sentensi za amri au maombi na kubadilisha kiambishi tamati /e/ kuwa /a/ kuwakilisha amri. Tofauti kama hizi ndizo huweza kuleta athari za matumizi ya Kiswahili sanifu ikiwa mwanafunzi atajikuta akitumia kanuni za L1 katika Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashadidiwa na maelezo ya Palome, (1967), Lupogo, (2021) ambao walidhihirisha kuwa kila kikanushi hutumika katika mukutadha wake na hutokea ktaika mazingira maalumu kikiwa na dhima ya kisarufi kinachobeba katika tungo. Palome alibainisa nafasi mbili, mwanzoni na tamati ya utokeaji wa vikanusho katika Kiswahili. Lupogo anabainisha nafasi ya utokeaji wa viambishi vikanushi anuai katika tungo. Anaeleza kuwa; “...ukanushi unajitokeza katika nafasi nne nadani ya vitenzi vya Kiswahili...” (Lupogo, 2021: 88). Aidha katika Luganda Hyman(2018) alionnyesha mwanzoni, kati na mwisho.

Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa nafasi ya utokeaji hutegemea kipashio na kikanusho. Katika ukanushaji wa ngeli katika nomino, ukanushaji hutokea mwanzoni ukiambishwa nyuma ya kiambishi ngeli, kati ukitokea katika nafasi ya njeo na tatu mwishoni hasa katika ukanushaji wa wakati uliopo.

5.1.4.2 Uwiano na tofauti ya Ukanushaji wa Vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu

Kila lugha huwa na maumbo ya kipekee ya vivumishi. Vivumishi hivyo huwakilishwa na maumbo maalumu ambayo hutumika kutegemea kanuni zinazoipambanua na kutofautisha lugha moja na nyingine. Uchanganuzi wa matokeo ya mapitio ya maandishi, tasnifu, vitabu vya kisarufi vilivyoidhinishwa na serikali na vitabu vya ziada pamoja na mapito ya kazi mtandaoni na katika maktaba ya umma, shuleni, na chuoni pamoja na magazeti, utafiti huu ulidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za ukanushaji wa vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyofafanuliwa hapa chini.

5.1.4.2.1 Kanuni ya Kimapokezi masharti ya uongezaji vikanushi nyuma ya vivumishi

Matokeo ya uchanganuzi wa Hyman, (2018), Mgullu, (1999), Leah & Sseguya (2015), Lupogo, (2021) Ngonyani, (2001), Kihore, Massamba & Msanjila (2012) ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili hutumia kanuni ya kimapokezi masharti ya uongezaji vikanusho nyuma ya vivumishi. Ilidhihirika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kiambishi kikanushi cha nafsi ya kwanza [si] kukanusha vivumishi katika tungo. Kwa mujibu wa kanuni hii, mofimu kanushi [si] huambikwa au huwekwa nyuma ya kivumishi baada ya nomino kukanusha sifa au kivumishi kinachokumusha nomino tajwa kama inavyodhihirika katika data (4.21, Uk. 121) kutokana na Leah & Sseguya (2015). Data hii ilidhihirisha matumizi ya kikanushi [si-].

Aidha, utafiti huu pia ulibaini kuwa Luganda ina kanuni ya kimapokeo na ambayo ni sharti ya kutumia mofu kanushi za [t] na [te-] hasa kukanusha vivumishi vinavyojitokeza pamoja na vitenzi. Kwa mujibu wa kanuni hii ya kimapokeo, ikiwa kivumishi kimewakilishwa na kitenzi, kanuni ya kuongeza [te-] au [t-] nyuma ya kitenzi hutumika kutegemea ikiwa fonimu inayotangulia ni irabu au konsonanti. Kiswahili hutumia kikanushi [ha] kudhihirisha ukanushaji wa vitenzi vya nomino iliyokumushwa pamoja na [hu] inayotumika kwa ngeli za U-I, U-Zi na U-U kutokana na mabadiliko ya kifonolojia pamoja na kujali kuambisha viambishi awali vya vipatanishi vya ngeli nomino na kudondosha fonimu /a/ iliopo kwenye kikanushi halisi [ha] kama inavyodhihirika katika data (4.19, Uk. 117) kutokana na Leah & Sseguya (2015) na Hyman (2018) ambayo inadhihirisha uwiano na tofauti za mofu kanushi katika Luganda na Kiswahili kidhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maumbo katika tungo.

Vilevile, Kwa kuzingatia vivumishi vya nafsi vinavyotokana na ngeli husika, utafiti huu uligundua kuwa, kanuni hii hushikilia kuongeza kikanushi [t-] mwanzoni mwa viwakilishi

vya nafsi kwa sababu vinaanza na irabu ila kiwakilishi nafsi cha kwanza ambapo kiwakilishi [siri] hutumika. Kwa hiyo, kanuni ni kuwa katika nafsi ya kwanza kuna kuongeza [siri] nyuma ya kivumishi, nafsi ya pili, [toli] na nafsi ya tatu [tali] kwa umoja. Katika wingi, nafsi ya kwanza hutumia [tetuli], nafsi ya pili, [temuli] na nafsi ya tatu, [tebali]. Kuzingatia kanuni ya kuongeza [t-] kwenye viwakilishi nafsi vinavyoanza na vokali na [te] kwa vile vinavyoanza na konsonanti kama inavyodhihirika katika data Na. (4.17, Uk. 114) kutokana na Leah & Sseguya (2015). Tofauti inayojitokeza ni ya maumbo ya vikanushi vya Luganda na ambavyo hujali sana kukanusha vivumishi kutegemea ikiwa fonimu inayotangulia kivumishi ni konzonanti au irabu. Aidha kwa kuzingatia ukanushaji wa vivumishi vya nafsi, Kiswahili hutumia kikanushi [si-] huku Luganda ikizingatia kanuni ya kuongeza vikanushi [t-] na [te-] kwenye viwakilishi vinavyoanza na konzonanti [te-] au irabu [t-].

Matokeo ya matumizi ya kanuni hii yalishadidiwa na Ssentumbwe, ByeongMan2 Kim & Hyunah Lee (2019) na pamoja na Mulei, (2020) ambao wanafafanua kuwa ukanushaji katika Luganda na Kiswahili ni ule wa kuambisha vikanushi mwanzoni au nyuma ya vitenzi kama sehemu ya viambishi awali. Matokeo haya yalidhihirisha uwiano na tofauti ya matumizi ya vikanushi katika nafasi mbalimbali kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa vipashio katika tungo. Aidha, licha ya kuwa lugha hizi zilidhihirisha kufanana katika matumizi ya kanuni na baadhi ya maumbo, kila lugha ilidhihirisha upekee wake ambao ulibainisha kuwa licha ya kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti kimofosintaksia.

5.1.4.2.2 Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa vikanushi katika vivumishi.

Kanuni hii hushikilia kuwa mofu kanushi huambishwa katika nafasi mbalimbali kudhihirisha ukanushaji wa sentensi na ukanushaji wa viambajengo. Kwa mujibu wa kanuni hii, mofu kanushi hutokea baada ya nomino kuu, nyuma na karibu na kivumishi cha nomino kuu (Mgullu, 1999 na Habwe & Karanja 2004, Kitsao, 2015). Matokeo ya wataalamu hawa, ilibaini kuwa Kiswahili na Luganda sanifu huambisha kikanushi [si] baina ya nomino na kivumishi ambapo, kikanushi hutokea baada ya nomino kuu, nyuma na karibu na kivumishi cha nomino kuu. Utafiti huu ulibaini pia kuwa, Luganda na Kiswahili sanifu huambiasha vikanushi mwanzoni mwa vitenzi hasa vivumishi ambavyo vimeambatana na vitenzi. Tofauti ya nafasi ya utokeaji ni kuwa Luganda hujali zaidi kanuni ya [t-] na [te-] wakati wa kukanusha vivumishi vilivyowakilishwa na vitenzi. Kwa kuzingatia vikanushi vya vivumishi vya nafsi, Kiswahili sanifu hushikilia kanuni ya kikanushi [si-] kuwekwa baina ya kiwakilishi cha nafsi na kivumishi ambapo kinatokea baada ya nafsi nyumba ya kivumishi cha nafasi.

Luganda huweka vikanushi vyake nyuma ya viwakilishi nafsi kutegemea kanuni ya matumizi ya [t- na te-] ya irabu na konsonanti mtawaliwa kama katika data Na. (5.47)

Luganda sanifu

Kiswahili sanifu

- a) *Abasajja a-ba-ta-a-leeta migugu.* Wanaume ambao **ha-wa-ku-leta** mizigo.
b) *Emigugu abasajja gye-ba-ta-a-leeta.* Mizigo ambayo **ha-i-ku-letwa** na wanaume.
c) *Mwana y'a-ta-soma kitabo.* Ni mtoto ambaye **ha-kusoma** kitabu
d) *Maama agambye nti asobola obu-ta-ja.* Mama amesema kuwa anaweza **ku-to-kuja**
e) *Obu-ta-laba ngo* **ku-to-ona chui.**
f) *Omusajja mulungi.* Mwanamume **mzuri**
Omusaja si mulungi Mwanamume **si** mzuri
g) *Caayi mulungi.* Chai **nzuri.**
Caayi si mulungi. Chai **si** nzuri.

Asili: Data kutokana na Hyman na Katamba (1999) na Leah na Sseguya, (2015)

Kwa mujibu wa kanuni hii, Luganda na Kiswahili zilidhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya nafasi ya utokeaji wa vikanushi kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu. Aidha, kwa kuzingatia mihimili ya sarufi bia na upatanifu, Luganda na Kiswahili licha ya kuwa lugha za nasaba moja, zilidhihirisha kuwa lugha mbili tofauti zenye maumbo yake ya kutumia katika ukanushaji kudhihirisha uhusiano wa kisarufi wa maneno katika tungo.

Kanuni hii inaelezwa na Lupogo, (2021) na Hyman, (2018) pamoja na Mulei, (2014) Ngonayani, (2001) ambao walifafanua juu ya uambishaji wa viambishi vikanushi mwanzoni nz nyuma ya maneno yanayokumushwa. Aidha, Hyman, (2018) anathibitisha nafasi ya utokeaji wa vikanushi vya Luganda [te-] na [t-] ambayo huambishwa nyumba ya kiambishi kipatanishi cha nomino tendaji katika tungo. Leah & Sseguya (2015) anakubaliana na Hyman, (2018) akieleza kuwa katika Luganda maumbo ya ukanushaji hutokea mwanzoni mwa vitenzi na katika vivumishi, kikanushi si uwekwa nyuma ya kivumishi. Anaeleza kuwa;

“....in Luganda a simple ‘si’ can be placed in front of the adjective: ‘omusajja si mulungi’, ‘omuyizi si mugezi’, ‘omusumesa si mutufu’ ‘caayi si mulungi’ ‘engatto si nene’ ‘eryenvu si dene’. When the adjective is expressed through a verb, the normal way of negating a verb is used: Emmere tewooma, caayi tayokya, ovaceddo takulwa, emicungwa tegikalubwa, enviri tezigonda.....” (Leah na Sseguya, 2015: 31).

5.1.4.3 Uwiano na tofauti ya kanuni za Ukanushaji wa Viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili

Kwa mujibu wa Mgullu (1999) na Waihiga (1999) viwakilishi vya nafsi ni maneno huru na ambata ambayo hutumika au kusimamia nomino ya viumbe wenye uhai. Oichoe (2005) anaeleza kuwa viwakilishi nafsi ni maneno huru na funge ambayo hufanya kazi kama nomino. Viwakilishi vya nafsi hutumika badala au huchukua nafasi ya nomino pale ambapo nomino haipo. Viwakilishi hivi vikiwa huru yaani, maneno kamili yenye kubeba maana ya kileksika huwa haviambishwi. Kila lugha huwakilishwa na maumbo ya kipekee ya vipashio vya kisarufi. Maumbo haya hutumika kiyakinishi na kikanushi kuzingatia kanuni za lugha husika. Uchunguzi wa uwiano na tofauti ya kanuni za ukanushaji wa viwakilishi nafsi ulibainisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za viwakilishi nafsi kimofosintaksia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatansishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981).

5.1.4.3.1 Kanuni ya upatanishi nafsi

Mofu za ukanushaji wa nafsi kimofosintaksia ni mofu ambayo huzingatia vipatanishi vya nafsi. Kila kiwakilishi cha nafsi tegemezi huwakilishwa na viambishi vikanushi vinavyoambikwa katika nafasi ya viwakilishi nafsi yakinishi, kabla ya vitenzi. Muundo wa ukanushaji wa viwakilishi nafsi katika tungo za Luganda na Kiswahili sanifu hutokana na uambishaji wa vipatanishi vya nafsi ambavyo huwekwa kwenye shina au mizizi ya vitenzi vinavyobeba maana au dhamira fulani kulingana na wakati au hali. Aidha, ukanushaji wa utungo wenye vipatanishi vya kisarufi vya nafsi hutokea au kubadilika kulingana na viambishi awali vya shina au mizizi wa kitenzi (Hyman 2018, Mgullu, 1999).

Matokeo ya uchambuzi kutokana na Kamoga, (1968), Hyman, (2018) na Leah na Sseguya, (2015), Utafiti huu ulibaini kuwa, mizizi wa kitenzi cha Luganda unaoanza na konsonanti kwa umoja [N-] hubadilika na kuwa [Si] na katika matumizi ya kiambishi [s-] hutumika. Kwa mfano; [Ngeenda] hubadilika na kuwa; [Sigeenda]. Aidha, [t-] hupatana na mizizi ya vitenzi vinavyoanza na vokali. Kwa mfano, nafsi ya pili [O-] huongezwa [t-] hupatana na [o] na kuunda kikanushi [to] kinachoambikwa nyuma ya kitenzi husika. Katika nafsi ya tatu, kiwakilishi nafsi [a] nacho kwa sababu ni irabu, hupatana na mfu kanushi [t-] ambayo huwekwa nyuma ya kitenzi na kuwa [ta] kanuni hii ni ya viambishi vipatanishi vikanushi vya nafsi ya 1, 2 na 3 kwa umoja. Uchanganuzi wa data ulibaini kuwa viwakilishi vya nafsi ya kwanza pili na tatu kwa wingi katika Luganda huanza na konsonanti. Kwa hivyo, mofu

kanushi [te-] hupatana na viwakilishi vya nafsi kwa kuiambisha nyuma ya kononanti ya nafsi ya 1, 2 na 3 [tu, mu na ba] na kuunda viwakilishi vikanushi [tetu-, temu, na teba-] kudhihirisa uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo. Ukiukaji wa kanuni hii huadhiri upatanishi wa kisarufi wa maneno katika tungo.

Kwa muhibu wa data kutokana na Mbwilow, (2017), Lusekelo, (2017), Mgullu, (1999), Habwe & Karanja (2004), Utafiti huu ulibaini kuwa kanuni hii ya upatanishi wa viwakilishi nafsi na mofu kanushi ulidhihirika pia katika Kiswahili sanifu ambapo vikanushi vya nafsi ya 1, 2 na 3 kwa umoja na wingi viliambikwa kwenye nafsi kuwakilisha kauli kanushi. Mofu kanushi [si] ilitumika badala ya [ni], [hu] kutumika badala ya kiwakilish [u] na [ha] hutumika katika nafsi ya tatu. Hii ina maana kuwa mofu kanushi patanishi za Kiswahili sanifu za nafsi ya 1, 2 na 3 huwakilishwa na mofu kanushi [si, hu, na ha] na wingi ukawa unatumia mofu [ha] inayopachikwa nyuma ya kiwakilishi nafsi cha wingi [tu. m na wa] na kupata vikanushi kuwa [hatu, ham na hawa]. Aidha, uambishaji wa vipatanishi hivi kuwakilisha hali kanushi pia hutegemea dhamira, hali, njeo na uwakilishi wa nafsi kwa umoja na wingi kama inavyojitokeza katika data ya jedwali Na. (5.7) kutokana na Leah na Sseguya, (2017) na Habwe & Karanja (2004):

Jedwali 5.7: Kanuni ya upatansihwa wa kisarufi wa viambishi vikanushi baina ya Luganda na Kiswahili

| <i>Nafsi</i> | | <i>Vikanushi</i> | | <i>Vikanushi</i> |
|--------------|---------------|---------------------------|------------------------|------------------------------|
| 1 | <i>Nsamba</i> | <i>Sisamba/ tetusamba</i> | <i>Neetaga/twetaga</i> | <i>Seetaga/Tetwetaaga</i> |
| | Ninacheza | Sichezi/ hatuchezi | Ninataka/tunataka | Sitaki/ hatutaki |
| 2 | <i>Osamba</i> | <i>Tosamba/ temusamba</i> | <i>Wetaga/ mwetaga</i> | <i>Teweetaaga/temwetaaga</i> |
| | Unacheza | Huchezi/ hatuchezi | Unataka/mnataka | Hutaki/ hamtaki |
| 3 | <i>Asamba</i> | <i>Tasamba/tebasamba</i> | <i>Yetaga/ betaga</i> | <i>Teyeetaaga/tebeetaaga</i> |
| | Anacheza | Hachezi/ hawachezi | Anataka/ hawataki | Hataki/ hawataki |

Asili: Data kutokana na Leah na Sseguya, (2015) na Mgullu, (1999)

Tofauti ya kanuni hii ya upatanishi ni kuwa Kiswahili sanifu huambisha viambishi vipatanishi vikanushi [si na ha] kwa umoja na wingi ambapo nafsi ya pili umoja [u] huathirika na mabadiliko ya kimofofolojia ya udondoshaji wa fonimu /a/ katika kikanushi [ha] na kutumia /u/ ya nafsi ya pili kuwakilisha hali kanushi ya nafsi ya pili ambayo ni [hu]. Luganda imetumia mofu [si-] kama ilivyo Kiswahili sanifu badala ya [te-n] (Hyman, 2018). Vinginevyo Luganda hutumia mofu kanushi [t-] na [te-] kifonolojia kutegemea ikiwa

kiwakilishi nafsi kinaanza na irabu au konsonanti. Kwa mujibu wa matokeo ya uambishaji, Luganda ilidhihirisha kuongeza mofu kanushi patanishi [t-] kwenye kiwakilishi nafsi kinachoanza na irabu na [te-] kwenye kiwakilishi nafsi kinachoanza na konsonanti na ambayo huathiri pia matamshi na maandishi ya viwakilishi katika matumizi. Data Na. (5.48) kutokana Hyman, (2018) inadhihirisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni:

a) Wakati uliopo

| | |
|------------------|---------------------|
| <i>Siyimba</i> | <i>Te-tu-yimb-a</i> |
| Si- imb-i | Ha- tu-imb-i |
| <i>To-yimb-a</i> | <i>Te-mu-yimb-a</i> |
| Hu- imb-i | Ha- mw-imb-i |
| <i>Ta-yimb-a</i> | <i>Te-ba-yimb-a</i> |
| Ha- imb-i | Ha- wa-imb-i |

b) Wakati Uliopita

c) Wakati Ujao

| | | | |
|---------------------|------------------------|----------------------|------------------------|
| <i>Sa-a-yimb-a</i> | <i>Te-twa-a-yimb-a</i> | <i>Si-li-imb-a</i> | <i>Te-tu-li-imb-a</i> |
| Si- ku-imb-a | ha- tu-ku-imb-a | si- ta-imb-a | ha- tu-ta-imb-a |
| <i>Te-wa-yimb-a</i> | <i>Te-mw-a-a-imb-a</i> | <i>To-li-imb-a</i> | <i>Te-mu-li-imb-a</i> |
| Hu- ku-imb-a | Ha- m-ku-imb-a | Hu- ta-imb-a | Ha- m-ta-imb-a |
| <i>Te-ya-yimb-a</i> | <i>Te-ba-a-yimb-a</i> | <i>Ta-li-i-imb-a</i> | <i>Te-ba-li-imb-a</i> |
| Ha- ku-imb-a | Ha- wa-ku-imb-a | Ha- ta-imb-a | Ha- wa-ta-imb-a |

Asili: Data Kutokana na data ya Hyman, (2018) na Leah & Sseguya (2015).

Data (5.48) inadhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwakilishwa na maumbo au mofu yakinishi na kanushi inayowakilisha nafsi ya kwanza, pili au tatu. Kila nafsi imewakilishwa na kiwakilishi kipatanishi cha kiwakilishi nafsi kwa umoja na wingi. Kinachojitokeza ni kuwa mofu [te-] hupatana na kiambishi kipatanishi awali cha nafsi kinachoanza na konsonanti na [t-] kupatana na kiambishi kiwakilishi kipatanishi cha nafsi kinachoanza na vokali. Mofu hizi za upatanishi katika Luganda imebainika kutoathiri swala la njeo na hali. Tofauti inayojitokeza ni kuwa Luganda ina viwakilishi nafsi vipatanishi vya aina yake kama ilivyo Kiswahili sanifu. Kiswahili kinatofautiana na Luganda kikanuni ambapo Kiswahili huongeza viambishi au mofu ya ukanushaji [ha] au alomofu yake [hu] nyuma ya viwakilishi vipatanishi vya nafsi kimofosintaksia, huku Luganda ikizingatia aina ya viambishi viwakilishi vya nafsi kuwa ama irabu au konsonanti. Aidha, ukanushaji katika Kiswahili huathirika zaidi na dhamira, hali, viwakilishi nafsi na wakati kinyume na Luganda ambayo hujali zaidi utokeaji wa mofu patanishi kutegemea ama irabu au konsonanti. Matokeo haya yanaendana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya kisarufi ambayo

huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo haya yanaungwa mkono na stump (2017), Hyman, (2018), Leah & Sseguya, (2015) ambao walidhihirisha upatanishi wa kisarufi wa viwakilishi nafsi kwa kutegemea nafasi ya utaokeaji na mazingira ya tokeaji wa viwakilishi mwanzoni mwa irabu ama konsonanti. Obara, (2014) anakubaliana na Hyman (keshatajwa) kuhusiana na upatanishi wa kisarufi, Kulingana naye viambishi viwakilishi vya viwakilishi vinavyoambikwe kwenye vitenzi, ndivyo vinavyodhihirisha kanuni ya upatanifu. Anasema kuwa:

*Upatanisho pia huashiriwa na viambishi vya nafsi. Viwakilishi vya nafsi hubainishwa katika ngeli ya kwanza na ya pili. Kuna nafsi tatu katika lugha ya Kiswahili sanifu, nafsi hizi zina viambishi tofauti... Nafsi ya kwanza huwakilishwa na kiwakilishi **mimi** katika hali ya umoja na **sisi** katika hali ya wingi. Viambishi vinavyowakilisha nafsi hii katika umoja na wingi ni **ni-** na **tu-**. Nafsi ya pili huwakilishwa na kiwakilishi **wewe** katika umoja na **ninyi / nyinyi** katika wingi. Viambishi viwakilishi vya nafsi hii ni **u-** na **m-** katika hali ya umoja na wingi mtawalia. Viwakilishi **yeye** na **wao** huwakilisha nafsi ya tatu. Viambishi hivi ndivyo huashiria upatanisho wa kisarufi (Obara, 2014: 49-50).*

Kutokana na Maelezo haya, ilidhihirika wazi kuwa Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana katika matumizi ya kanuni ya upatanisho kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya nomino na maneno mengine katika tungo.

5.1.4.3.2 Kanuni ya kifonolojia ya maumbo ya viambishi nafsi na mofu kanushi

Kanuni hii inazingatia sheria zinazotawala uambishaji wa mofu kanushi katika viwakilishi nafsi kutegemea fonimu irabu na konsonanti na jinsi mofu hizo zinavyoathiriana na kusababisha mabadiliko mbalimbali wakati wa kujenga muundo wa sentensi na viambajengo kanushi kimazungumzo na kimaandishi. Kanuni hii hutegemea mabadiliko mbalimbali ya kimofonolojia inayojitokeza katika matumizi ya viwakilishi nafsi kimazungumzo na kimaandishi (Chomi 2003; Habwe & Karanja, 2004; Mgullu 1999; Massamba 2003 na Hafsa 2016).

Matokeo ya uchanganuzi wa data kutokana na Chomi, (2003); Habwe & Karanja, (2004); Mgullu, (1999); Massamba. (2003) na Hafsa, (2016) kulidhihirisha kuwiana na kutofautina

kwa matumizi ya kanuni ya kimofonolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.. Kwa kuzingatia kanuni hii kwa mujibu wa mihimili ya ubia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hupata na athari za kimofonolojia inayotokana na utokeaji wa fonimu irabu na konsonanti katika mazingira mbalimbali. Udondoaji wa data za orodha ya uchunzaji kuhusu maumbo ya kifonolojia ya viambishi nafsi, ilibainika kuwa Luganda huambisha mofu kanushi [t-] kwenye mizizi au viwakilishi vinavyoanza na irabu na kuambisha mofu kanushi [te-] kwenye viwakilishi nafsi vinavyoanza na konsonanti. Data Na. (5.49) kutokana na Katamba, 1993:2003), inadhihirisha uwiano na tofauti za athari za kimofonolojia ambayo hujitokeza wakati wa kutumia kanuni ya kimofonolojia:

| <i>Umoja</i> | <i>Wingi</i> |
|---|--|
| <i>Saasoma</i> | <i>te-t-[u-a]-som-a [u+a=wa] +a [Tetwaasoma]</i> |
| <i>Te-[u-a]-som-a[u+a=wa]</i> | <i>[Tewasoma] te-m[u-a]-som-a [u+a=wa]-a</i> |
| <i>Tewasoma</i> | <i>Temwaasoma</i> |
| <i>T[e-a]-som-a [e+a=ya]+a [Teyasoma]</i> | <i>Tebaasoma</i> |
| <i>Teyasoma</i> | |

Asili: Data kutokana na uchanganuzi wa Mugerwa (2005)

Data Na. (5.49) inadhihirisha kuwa nafsi ya kwanza imetumia fonimu irabu [a] kuwakilisha wakati wa kutendeka kwa jambo. Hata hivyo, fonimu hii ambayo ni kiwakilishi cha njeo kimerefushwa kwa sababu kikanushi [si na a]. Badala ya kusema [siasoma] kanuni ya udondoshaji na uimarikaji wa fonimu wakilishi ya njeo hrefushwa na kuwa [saasoma]. Vinginevyo, Muundo wa viwakilishi nafsi vya 2 na 3 umoja, vinadhihirisha mabadiliko ya kimofonolojia ambapo fonimu /o/ na /e/ ilipitia kanuni ya uyeyushaji na kulazimisha fonimu hii kubadilika kuunda fonimu [wa] ya nafsi ya pili. Nafsi ya tatu vilevile iliathirika na katika mazingira ya fonimu /e/ na /a/, kubadilika na kuunda fonimu [ya] ya nafsi ya tatu. Vikanushi [t-] vya irabu na [te-] ya konsonanti iliambishwa na kujenga kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji wa viwakilishi nafsi katika Luganda ambapo, ukiukaji wa kanuni hii huweza kupotosha usanifu wa lugha kimofosintaksia.

Tofauti inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa, inagawa kanuni hii hujitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu, mabadiliko yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu ni finyu sana. Mabadiliko hayo yemejitokeza katika nafsi ya pili ambapo mofu [hu] hutumika badala ya mofu kanushi [ha] inayoathirika na mabadiliko ya kimofolojia ya kanuni ya muungano wa kiwakilishi nafsi [u] na [a] ya kikanushi [ha]. Fonimu [a]

hudondoshwa na badala yake [u] hutumika na kubadilisha muundo wa fonimu kanushi [ha] kuwa [hu] ambayo kwayo bado ni alamofu ya [ha-]. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilidhihirishwa kuwa mbadiliko ya kimofolojia yanayojitokeza katika Kiswahili sanifu hutofautiana kwa sababu mabadiliko mengi yanayotokea ni ya kimuktadha au kialofoni inayowakilisha mofimu moja na ambayo kwayo, hujitokeza katika maandishi na kudhihirika katika mazungumzo. Ilibainika pia kuwa kanuni za ukanushaji wa Kiswahili ni dhahiri inayotumia mofu kanushi [si] ya nafsi ya kwanza na [ha] ambayo hutokea mwanzoni mwa nafsi na kitenzi kinachokanushwa.

Matokeo haya yanashabihiana na matokeo ya Otiende, (2013) na Obara, (2014) ambao waligundua mwingiliano wa viwakilishi katika matumizi ya kanuni ya kimofonolojia. Otiende (2013) alidhihirisha tofauti baina ya mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kiolusuba ambayo huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Huku Obara (2014) akimuunga mkono kwa kusema kuwa: *Tunapochunguza fonolojia ya Ekegusii na Kiswahili Sanifu tunagundua kuwa lugha hizimbili zinaingiliana pakubwa sana. Kuingiliana huku husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo* (Obara, 2014: 37-38).

Matokeo haya yanaendana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya kisarufi ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Data ya utafiti huu ilibaini uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya kimofonolojia hasa katika maumbo na mazingira ya utokeaji wa mabadiliko ya kimofonolojia ambayo huathiri maumbo yanayoonyesha upatanishi wa Kisarufi wa nomino na maneno mengine katika tungo.

5.1.4.3.3 Kanuni ya maumbo wakilishi ya vikanushi

Kanuni hii hushikilia kuwa kila kiwakilishi nafsi huwakilishwa na mofu kanushi dhahiri ambazo hutumika kutegemea dhima, wakati, hali na nafsi husika. ukiukaji wa kutozingatia maumbo mwafaka na kutumia maumbo yasio sanifishwa katika lugha bainifu huweza kupotosha usanifu wa lugha husika (Mulei, 2014: 2020; Lupogo, 2020:2021 na Mgullu, 1999).

Matokeo ya data za upekuzi wa maandishi ya Ngonyani, (2001) na Mgullu, (1999), Hyman, (2018) na Kamoga, (1968), utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwakilishwa na maumbo ya vikanushi ambayo matumizi yake huingiliana na kutofautiana. Aidha, Kupitia kwa mijadala ya wanafunzi kutokana na matokeo ya mijarabu, ilitambulika kuwa Luganda huwakilishwa na mofu kanushi [t- na te-] pamoja na mofu [si]. Mofu kanushi hizi hutumika kulingana na nafsi husika na huongezwa nyuma ya viwakilishi nafsi tegemezi. Kiswahili nacho hutumia vikanushi [si- na ha-]. Kapinga (1983) na Chomi (2003), wanadhihirisha kuwa Kiswahili kina alomofu kuu mbili [si- na ha-]. Kikanushi [ha] kina alomofu [si-, ha-, na –to- na sipo] Kiswahili Kupitia kwa mofu hizi, vikanushi vya viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu katika nafsi tatu ni vifuatavyo kwa umoja na wingi. Data ya jedwali Na.(4.17, Uk. 122) inaonyesha uwiano na tofauti za mofu za ukanushaji wa vipatanishi vya nafsi kwa umoja na wingi kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo haya yanawiana mhimili wa upatanishi wa nadharia ya ya Umilikifu na unganishi ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo.

Kwa mujibu wa data katika jedwali Na. (4.17, Uk. 122), ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kikanushi [si-] kwa nafsi ya kwanza umoja. aidha, ilibainika kuwa nafasi ya utokeaji wa viambishi vikanushi vya Luganda na Kiswahili vilishabihiana katika hali fulani, kulidhihirishwa tofauti ya maumbo yaliyotokana na mabadiliko ya kanuni ya kimofonolojia. Utafiti huu ulibaini pia kuwa, hata ingawa maumbo ya viwakilishi nafsi vya kwanza wingi, na nafsi ya tatu vinashabihiana, Luganda na Kiswahili sanifu ilidhihirisha tofauti za matumizi ya vikanushi hivi kimofosintaksia ambapo Luganda iliongeza kikanushi [t-] kwenye mizizi inayoanza na irabu na [te] kwenye mianzo ya viwakilishi nafsi vilivyoanza na konsonanti. Kiswahili kilidhihirisha kudondosha kiwakilishi cha nafsi ya kwanza [ni-] na badala yake kutumia kikanushi [si]. Aidha, Kiswahili kuliambisha kikanushi [ha] kwenye kitenzi chenye kiambishi patanishi kiima isipokuwa nafsi ya kwanza [ni-]. Iligunduliwa kuwa ukiukaji wa kutotumia maumbo yaliyosanifisha, kwa kufuata utaratibu unaofaa na katika lugha husika huweza kupotosha usanifu wa lugha husika.

Matokeo haya yanashabihiana na yale ya Lupogo, (2020) katika utafiti wake linganishi wa vikanushi baina ya Kiingereza na Kiswahili sanifu. Alibainisha maumbo tisa ya Kiswahili. Katika uafanuzi wake anasema kuwa; “*Maumbo ya ukanushi katika lugha hizi mbili (luganda*

na Kiswahili) yanatofautiana kwa namna Fulani na yanafanana kwa namna nyingine” (Lupogo, 2021). Kwa upande mwingine, Hyman, 2018, naye alibanisha vikanushi [si-], [t-] na [te] matokeo yanayoshadidiwa na Leah & Sseguya ambao waliongeza maumbo mengineyo ya ukanushaji [Obuta-] ambayo huwekwa nyuma ya kitenzi, [-naba-] ambayo hutokea mbele ya vikanushi {te} na [t-] na Kikanushi si kinachowekwa nyuma ya kivumishi cha sifa.

Utafiti huu ulidhihirisha utokeaji wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya kisarufi ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Hali hii ilitokana na kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili huwiana katika kudhihirisha utokeaji wa matumizi ya kanuni hii, lugha hizi zinadhihirisha upekee wa kuwa lugha mbili tofauti ya maumbo wakilishi na utaratibu unaowiana na kutofautiana kimatumizi.

5.1.4.3.4 Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa mofu kanushi

Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa mofu kanushi katika viwakilishi nafsi ni ile inayoshikilia kuwa vikanushi katika viwakilishi nafsi hutokea mwanzoni nyuma ya viambishi vipatanishi vya nafsi na nyuma ya kitenzi kinachokanushwa au kategoria zingine za maneno. Uchanganuzi wa data kutokana na Leah & Sseguya, (2015), Hyman (2018), na Ngonyani (2001) nafasi ya matumizi ya maumbo ya vikanushi katika viwakilishi nafsi, udondoaji wa data ulibaini uwiano na tofauti katika ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data Na (5.50) kutokana na Hyman, (2018) na Ngonyani, (2001) ulidhihirisha uwiano na tofauti ya matumizi ya kanuni ya nafasi ya utokeaji wa mofu kanushi.

- | | |
|---|--|
| a) Mimi si mrefu <i>Knfs1 -Kkn-V</i> | sisi [si] warefu <i>Knfs1 -Kkn-V</i> |
| b) Hu-ta-imb-a <i>KKn/Knfsi-Nj(ta)-Mz-a</i> | Ha-tu-ta-imb-a <i>KKn-Knfsi-Nj(ta)-Mz-a</i> |
| c) Te-ya-yimb-a <i>KKn/Knfsi-Nj(li)-Mz-a</i> | Te-ba-a-yimb-a <i>KKn-Knfsi-Nj(li)-Mz-a</i> |
| Ha -ku-imb-a <i>KKn/Knfsi-Nj(li)-Mz-a</i> | Ha -wa-ku-imb-a <i>KKn-Knfsi-Nj(li)-Mz-a</i> |

Asili: Data kutokana na Leah na Sseguya, (2015), Hyman, (2018), Hannah, (1975)

kanuni hii kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa viwakilishi vya nafsi na maneno mengine katika tungo kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na unganifu ya Chomsky, (1981).

5.1.4.4 Uwiano na tofauti ya ukanushaji wa Njeo na Hali katika Luganda na Kiswahili

Kwa mujibu wa nadharia ya Reichenbach (1947) kama inavyoelezwa na Swaleh, (2017), njeo ni maneno ambayo huonyesha uhusiano wa wakati wa usemi na wakati wa utekelezaji wa tendo. Kila lugha huwa na maumbo wakilishi pamoja na kanuni za matumizi ya njeo na hali katika hali yakinishi na kanushi. Uchunguzi wa vitabu vya kisarufi, tasnifu, makala na mitandao mbalimbali kuhusu uwiano na tofauti za ukanushaji wa njeo na hali katika Luganda ulidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni mbalimbali za ukanushaji kama inavyofafanuliwa hapa chini.

5.1.4.4.1 Kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi za njeo na hali

Kanuni hii inashikilia kuwa, katika ukanushaji wa njeo na hali, ni muhimu mzungumzaji na mwandishi kutambua mofu au maumbo yanayowakilisha nyakati pamoja na kutambua ikiwa maumbo hayo yanawakilishwa na maumbo kanushi au la. Utambuzi wa maumbo kanushi ya njeo na hali humsaidia mtumiaji lugha kuyatumia vikamilifu bila kuenda kinyume kuhifadhi usanifu wa lugha tumizi kimaandishi na kimazungumzo.

Kwa mujibu wa Lupogo, (2021), Hyman (2018), Leah & Sseguya, (2015) na Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za Kibantu ambazo zinadhihirisha matumizi ya njeo na hali ikiwakilishwa na maumbo yakinishi na kanushi mbalimbali. Udonzoaji wa kanuni ya kimofolojia ya maumbo kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi kutoka kwa data za usomaji wa vitebu teule na maandishi ya wataalamu (washatajwa), utafiti huu ulibaini kuwepo kwa uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi. Uwiano na tofauti ulidhihirisha katika maumbo ya njeo na hali yakinishi na kanushi Data ya Jedwali Na.(4.18, Uk. 124) inadhihirisha uwiano na tofauti za kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. ukiukaji wa matumizi ya maumbo haya kwa utaratibu unaozingatiwa, uhusiano milikifu na unganifu wa vipashio katika tungo hupotosha usanifu wa kuonyesha uhusiano milikifu na unganishi wa tungo.

Aidha, utafiti ulibaini kuwa Kiswahili sanifu kilikanusha kauli kutegemea viwakilishi nafsi, hali, nyakati na ngeli. Kila nyakati na hali iliwakilishwa na maumbo kanushi ila wakati ujao muda mrefu. Kwa upande mwingine, data kutokana na Kiyinikibi, (2021), Leah & Sseguya,

na Hyman (2018) ilidhihirika kuwa Luganda sanifu haikudhihirisha maumbo ya vikanushi vya njeo na hali kama ilivyo katika Kiswahili sanifu. Luganda huwakilishwa na maumbo ya nyakati na, hata hivyo, nyakati hizi na hali haziathirika wakati wa ukanushaji. Luganda ilizingatia zaidi kutumia mofu za kifonolojia za kuambisha vikanushi vya jumla [t-] nyuma ya viwakilishi nomino vinavyoanza na irabu na [te-] ya kuanza na konsonanti. Njia mbadala iliyotumika ilikuwa ni ya kutumia baadhi ya fonimu na mofimu kanushi kuwakilisha ukanushaji wa kauli katika wakati maalumu kama inavyojitokeza katika mfano wa data katika jedwali Na (4.18, Uk 124).

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni hii kutokana na Hyman, (2003), Ngonyani, (2001) Lupogo, (2021), Leah na Sseguya, (2015) ulidhihirisha kuwa maumbo ya njeo na hali yakinishi na kanushi katika Luganda yanatofautiana na ya Kiswahili sanifu. Ilitambulika kuwa maumbo ya njeo na hali za Luganda ni zaidi ukilinganisha na mofu au maumbo ya Kiswahili sanifu. Kwa mfano, wakati uliopo hali timilifu [-me-] katika Luganda huwakilishwa na mofu nyambuzi [-zze, -a- na -ye] ambazo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi elekezi. Mofu [-li,-ba na -ye] na [li-ba na -a] za wakati ujao ambazo huwekwa baada ya kiambishi kipatanishi na kiambishi tamati na mofu [-naa, -ba na -YE] na [-naa, -ba na -a] za hali ya wakati uliopita. Mofu hizi za njeo na hali hazikudhihirisha utokeaji wa maumbo ya mofu kanushi wakati wa matumizi bali ukanushaji ulijitokeza tu katika vitenzi kwa kutegemeza fonimu kanushi [si] ya nafasi ya kwanza umoja, [t-] ya kukanusha viambishi vya vitenzi, nafsi au ngeli vinavyoanza na vokali na [te-] ya konsonanti.

Ukanushaji katika Luganda haudhihirishi maumbo kanushi ya vikanushi kama ilivyo katika Kiswahili sanifu. Kiswahili huwakilishwa na njeo na hali ambazo pia yana maumbo mbadala yanayotumika katika nafasi ya njeo wakati wa ukanushaji. Kwa mujibu wa utafiti huu ilibainika kuwa Kiswahili sanifu hudondosha nyakati na hali na badala yake kutumia mofu wakilishi kanushi ya njeo na hali wakati wa kukanusha kauli au tungo. Luganda hujali sana uambishaji wa vikanushi [t- na te-] kwenye mwanzoni mwa viambishi viwakilishi au vipatanishi vya nomino ambayo huambikwa kwenye mizizi ya vitenzi kuwakilisha ukanushaji huku njeo ikibakisha hadhi yake katika nafasi zake.

Matokeo haya yanashadidiwa na Swaleh (2017), Lupogo, 2021, Mulei, 2020 na Hyman, (2018) ambao wanafafanua maumbo yakinishi na maumbo kanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu. Lupogo, (2021) alibainisha maumbo tisa ya vikanushi naye Hyman, (2018) naye alibainisha vikanushi vitatu, katika Luganda ambavyo ni {si, t- n ate] huku Rose, (2009)

na Leah na Sseguya, (2015) wakibainisha mofu za ukanushaji wa njeo na hali. Swaleh, (2017) anashadidia matumizi ya kanauni hii anapoeleza kuwa: “*Mofimu tatu ndizo zinazohusika zaidi katika kuleta ukanushi katika Kiswahili, ambazo ni ha-, -si- na -to...Kuna mofimu nyingine zinazoongezewa kwenye ukanushi ambazo ni mofimu za kukanusha njeo au hali kama ya -i, -ja- na ku katika Kiswahili Sanifu*” (Swaleh, 2017:49). Tofauti na matokeo ya utafiti wa Swaleh, 2017 ambaye alitambua uwiano na tofauti za maumbo ya Kiswahili na Kitikuu, Kulingana na maelezo ya wataalamu haya, Matokeo ya utafiti huu yalibainisha uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi za njeo na hali baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Hali ambayo ilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili licha ya kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti katika kutumia maumbo wakilishi na utaratibu wa ukanushaji kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo kimofosintaksia.

5.1.4.4.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi katika nyakati na hali

Kanuni hii hushikilia kuwa kila lugha huwa na darajia ya utokeaji wa vikanushi katika tungo virai ambao lazima uzingatiwe wakati wa kutumia lugha kimazungumzo na kimaandishi pasi kizingatiwa, usanifu wa lugha hupotoshwa. Darajia hizi ni nafasi ambapo mofu kanushi huambishwa kwenye sentensi au viambajengo kuwakilisha dhima au dhamira kanushi. Aidha, kanuni hii pia hushikilia kuwa utokeaji wa mofu kanushi katika tungo hutegemea nafasi ya viambishi awali au viwakilishi vya nomino kuu, dhamira (aina ya ukanushaji), idadi, njeo na hali (Ngonyani, 2001, Mulei, 2014 na Hyman, 2018).

Matokeo ya data kutokana na Mdee, (1996), Leah & Sseguya (2015), Ngonyani, (2001), na Hyman, (2018) ilidhihirika kuwiana na kutofautiana kwa darajia za utokeaji wa vikanushi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu katika tungo kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo. Data Na.(4.17, Uk. 114) katika mifano ya ukanushi wa kiwakilishi kanushi na mifano. Aidha Data za Na.(4.17, Uk. 114 na 4.18, Uk. 115) zinazidi kuonyesha uwiano na tofauti za kidarajia za ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Aidha, uchanganuzi wa data za Mgullu (1999) ilibaini kuwa ukanushaji wa njeo na hali katika Luganda na Kiswahili sanifu hutanguliwa na vikanushi, ukifuatwa na viambishi viwakilishi vya nomino ambavyo huaambikwa kwenye vitenzi vinavyokanushwa kuwakilisha idadi ya umoja na wingi. Aidha, baada ya viambishi viwakilishi vya neno kuu, hufuatwa viambishi vikanushi vya nyakati na hali mbalimbali katika Kiswahili sanifu huku Luganda

ikiweka mofu za njeo na hali kabla ya kiambishi kipatansihi na baada ya mzizi [Mz] wa kitenzi kinachokanushwa. Utaratibu huu ni utaratibu ambao unaendana na mihimili ya usarufi bia na upatanishi ya nadharia ya Umilikifu na unganifu. Utaratibu huu unapokiukwa, uhusiano wa kimofosintaksia wa lugha hupotoshwa.

Tofauti inayojitokeza ni kuwa ukanushaji katika lugha ya Kiswahili sanifu huzingatia sana maumbo wakilishi ya mofu kanushi za njeo na hali katika ukanushaji wa sentensi. Mofu kanushi hizi hutokea katika mazingira ya njeo na hali baada ya kiambishi kipatanishi cha nomino kuu [Kkp] nyuma na karibu sana na shina au mzizi [Mz] wa kitenzi kinachokanushwa. Vile vile, utafiti huu uligundua kuwa ukanushaji au mofu ya ukanushaji katika Kiswahili kilitokea mwishoni mwa vitenzi hasa katika ukanushaji wa tungo katika wakati uliopo ambapo kiambishi tamati [-a] kiliweza kudondosha na badala yake kikanushi [-i] kutumia huku kiambishi cha wakati uliopo [-na-] kikedondoshwa na mwisho, matumizi ya kikanushi [si] katika sentensi rejeshi ambapo kikanushi hiki hutokea baada ya kiambishi kipatanishi msingi cha nomino kuu.

Pia, data za Leah na Ssuguya (2015), ulibaini kuwa ukanushaji wa tungo rejeshi katika Kiswahili ulishabihiana na na kutofautiana wa Luganda sanifu ambao ulidhihirisha nafasi tofauti ya utokeaji wa mofu kanushi za njeo na hali katika tungo. Data Na. (5.52) kutokana na Leah na Ssuguya (2015), inadhihirisha uwiano na tofauti za ukanushaji

a) *Abayizi abaakola obulungi bawebwe kisiimo*

Wanafunzi wanaofanya vyema watuzwe

b) *Abayizi [a-ba-ta-kola] bulungi tebawebwa akisiimo*

. Wanafunzi [wa-si-o-fanya] vyemwa wasituzwe

c) *Omukazi y-a-fumba emmere nnungi. Omukazi te-ya-fumba emmere*

Mwanamke Alipika chakula kizuri **Ha-ku-pika** chakula kizuri

d) Mwanamke ambaye **a-li-pika** chakula Mwanamke ambaye **ha-ku-pika** chakula

e) Mwanamke aliyepika chakula kizuri Mwanamke ambaye **ha-ku-pika** chakula

f) *Omusajja eyampadde ebisumuluzo yagenze. Mwanamme aliyenipa ufunguo*

ameenda Omusajja eyampadde ebisumuluzo te-yagenze

Mwanamme alijenipa ufunguo **ha-ja-enda**

Asili: Data kutokana na Leaha na Sseguya, (2015)

Data hii ilibainisha kuwa, mtumiaji akitumia -o' rejeshi, kiambishi cha njeo na hali hudondoshwa ila ikitumika na [amba-] njeo hutokea baada ya kikanushi cha Kkp nyuma na

karibu sana na mzizi wa kitenzi. Tofauti inayojitokeza ni kuwa; ingawa Kiswahili hutumia mofu kanushi za njeo zinazotokea baada ya kikanushi [ha-], Luganda hutumia njeo na hali halisi kwa sababu haina mofu kanushi inayotumika badala ya mofu ya njeo husika na ambayo hutokea baada ya mofu kanushi za jumla [t- na te-].

Kwa mujibu wa data za Matasi na Furaha (2016) na Ngonyani (2001) utafiti huu vile vile ulidhihirisha tofauti kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Ilibainika kuwa; ingawa viambishi vikanushi katika lugha hizi mbili hutokea mwanzoni, nyuma ya Kiambishi kipatanishi cha msingi na baada ya kiambishi kipatanishi cha msingi katika tungo rejeshi, ukanushaji katika Luganda uliathirika zaidi na kanuni za kifonolojia ya kutumia vikanushi [t- na te-] ikiwa kiambishi kipatanishi cha msingi vinavyofuata kikanushi ni irabu au konsonanti. Aidha, mabadiliko ya kimofolojia na toni ya baadhi ya sauti yalitiliwa mkazo au kufupisha kutegemea kanuni hii ya uambishaji vikanushi [t- na te-] kama katika data (5.53) kutokana na matokeo ya utafiti huu (2021).

| | |
|--------------------------------------|---------------------------------|
| a) <i>Nsamba</i> (wakati uliopo) | <i>Sisamba</i> |
| Ninacheza | Sichezi |
| b) <i>Nsambye</i> (hali timilifu) | <i>Sisambye</i> |
| Nimecheza | Sijacheza |
| c) <i>Nasambye</i> (wakati uliopita) | S-aa-samb-ye |
| Nilicheza | Sikucheza |
| d) <i>Joshua akuyita mugende</i> | <i>Joshua anakuita mwende</i> |
| <i>Joshua t-a-kuyita genda</i> | <i>Joshua ha-ku-it-i kwenda</i> |

Asili: Data kutokana na Ngonyani, (2001) na Leah na Sseguya, (2015).

Matokeo haya yanafanuliwa na Lupogo, (2021) anayezungumzia juu ya utokeaji wa vikanushi katika nafasi mwanzoni, katikati na mwishoni katika Kiswahili. Naye Hyman (2018) na Leah na Sseguya, (2015) wanaonyesha utokeaji wa ukanushaji mwanzoni mwa, kabla ya viambishi vipatanishi. Matokeo ya utafiti huu yanashabihiana na ufafanuzi wa wataalamu hawa. Utafiti huu ulibainisha uwiano na tofauti za kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. aidha utafiti huu ulibaini kuwa ukiukaji wa kanuini ya kidarajia ni uvunjaji wa utaratibu wa kisarufi wa kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo.

5.1.4.4.3 Kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji wa nyakati na njeo

Kanuni hii hushikilia kuwa baadhi ya fonimu zikikaribiana na fonimu fulani kama ni irabu au konsonanti, ujirani huo husababisha mabadiliko ya fonimu mbalimbali yanayojitokeza katika maandishi au mazungumzo. Uchanganuzi wa data za Chomi, (2003), Habwe & Karanja, (2004), Mgullu, (1999) Massamba, (2003) uligundua kuwa kanuni ya kifonolojia ilidhihirishwa katika ukanushaji wa njeo na hali katika Luganda na Kiswahili sanifu. hata hivyo, matumizi ya kanuni hii uliwiana na kutofautina kama katika data Na.(5.54) kutokana na Ssekiryango Leah na Sseguya, (2015) na Hyman, (2018) na Human na Katamba, (2010), inadhihirisha uwiano na tofauti za athari za kimofonolojia ambayo hujitokeza wakati wa kutumia kanuni ya kimofonolojia.

| | | | |
|--------------------|------------------------|-------------------------|---------------------------------------|
| <i>Baasambye</i> | <i>te-ba-samb-ye</i> | | <i>udondoshaji wa [a] yakinishi</i> |
| Wamecheza | hawajacheza | - | |
| <i>y-aa-samb-a</i> | <i>Te-y-a-samb-a</i> | <i>[te-a-asamba]</i> | <i>uyeyushaji na Udondoshaji</i> |
| alicheza | hakucheza | - | |
| <i>Nnsamba</i> | <i>Sa-a-samba</i> | <i>[sinasamba]</i> | <i>udondoshaji n [siasamba] mkazo</i> |
| Ninacheza | Sichezi | - | |
| <i>Twaasamba</i> | <i>te-tw-aa-samb-a</i> | <i>[tetu-oasamba]</i> | <i>uyeyushaji</i> |
| Tulicheza | Hatukucheza | - | |
| <i>Yasaamba</i> | <i>te-y-a-a-samb-a</i> | <i>[te-oasamba]</i> | <i>uyeyushaji</i> |
| Alicheza | Hakucheza | - | |
| <i>Mwasaamba</i> | <i>te-mw-a-asamb-a</i> | <i>[te-mu-oasaamba]</i> | <i>uyeyushaji</i> |
| Mlicheza | Hamkucheza | - | |
| <i>Wasaamba</i> | <i>te-w-a-a-samb-a</i> | <i>[teoasaamba]</i> | <i>uyeyushaji</i> |
| Ulicheza | Hukucheza | - | |

Asili: Data kutokana na Leah na Sseguya, 2015; Katamba, 2003

Kwa mujibu wa data hii, ukanushaji katika Luganda ulidhihirisha mabadiliko ya kifonolojia ambayo yalitokea katika viambishi awali vya vitenzi na ambavyo pia viliathiri viwakilishi vya njeo na hali katika mchakato wa ukanushaji. Kile ambacho kinafaa kuzingatiwa ni kwa mabadiliko yaliyotokea ni ya kimofonolojia tu ila viambishi vya njeo vilibakisha hadhi yake ya kifonimu bila kubadilika kimaumbo tofauti na inavyjitokeza katika Kiswahili sanifu. Matokeo ya data yalibainisha kanuni ya kimofonolojia iliyoathiri ukanushaji wa nafsi na njeo pamoja na hali baina ya Luganda na Kiswahili. kuwa, ukanushaji katika Luganda uliathirika na maswala ya kifonolojia. Kwa mfano, ilibainika kuwa katika wakati uliopita, kikanushi cha [Nnima] badala ya kuwa [si-a-lim-a], kiambishi cha wakati uliopo [-a-]

kinarefushwa kwa sababu ya maumbo ya kikanushi [si] na kiambishi cha wakati [a] kuathiriana na kusababisha mabadiliko ya fonimu kutokana na ujirani wa [Konsonanti Irabu (KI) +Irabu (I)]. Ujirani huu husababisha kiambishi cha njeo kutiliwa mkazo au kurefushwa wakati wa mazungumzo na maandishi na kuwa [saa-lim-a] ambapo mvutano wa sauti unaathiri sauti dhaifu [i] na kusababisha toni ya juu ya sauti irabu [aa] zinazofuatana kuonyesha ukanushaji na wakati.

Utafiti huu ulitambua pia Luganda huathirika zaidi na kanuni hii kuliko Kiswahili sanifu kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo. Kwa mfano Kiswahili huathirika na kanuni hii hasa katika nafsi ya pili tegemezi ambayo hutumia kiambishi [u] pamoja na viambishi vipatanishi vya nomino vinavyotumia kiambishi [u] hasa kuwakilisha idadi ya ngeli nomino katika nafsi ya kwanza. Aidha, kikanushi si hutumika pamoja na kiambishi njeo [a] kuwakilisha wakati uliopo kama inavyofafanuliwa na (Swaleh, 2017; Chomi, 2003).

Kwa upande mwingine, Leah na Sseguya, 2015; Katamba, 1993) waliweza kudhihirisha kuwa Luganda huathirika katika nafsi tatu wakati wa kutumia nafsi na njeo. Luganda ilidhihirisha kanuni ya uyeyushaji wa fonimu inayowakilisha nafsi ya pili na tatu. Katika kanuni hii ujirani wa irabu /o-a-/ ulisababisha kiambishi nafsi [w] na /e-a-/ kuyeyushwa na kusababisha kiwakilishi nafsi [y] ambacho kwayo kiliambishwa viambishi vikanushi pamoja na njeo na hali kudhihirisha hali yakinishi na kanushi. Matokeo haya yalidhihirisha usarufi bia na upatanishi wa nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981) ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo ya utafiti huu yanashadidiwa na Otiende, (2013) na Obara, (2014) ambao waligundua mwingiliano wa viwakilishi katika matumizi ya kanuni ya kimofonolojia. Aidha, Lupogo, (2021) na Swaleh, (2017) ambao walidhihirisha utokeaji wa kanuni ya kimofonolojia katika kikanushi [ha-]. Kwa kuelezea zaidi, Swaleh anathibitisha utokeaji wa kanuni hi katika Kiswahili kuwa:

“kiambishi {hu-} kimetumika badala ya {ha-} kwa sababu ya mabadiliko ya kimofonolojia ambapo {ha-} ya ukanushi ikifuatwa na {u}, basi kunatokea udondoshi wa vokali ya kwanza ambayo ni {a}.

/ha-u-som-i/ → [hu-som-i]

Sheria: /a/ → [∅] / -/u/....” (Swaleh.2017: 52)

Kwa mujibu wa matokeo ya maelezo haya, utafiti huu ulibaini kuwa kuna uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ambayo hutokea katika mazingira tofauti kutokana na upekee wa lugha ya Kiswahili na Luganda katika kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu baina ya viamabjengo katika tungo. Aidha ilibainika kuwa, licha ya lugha hizi kuwiana, zinatofautiana katika matumizi ya kanuni hii kuwakilishi uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo kimofosintaksia.

5.1.4.4 Kanuni ya muktadha na dhima ya utokeaji wa vikanushi

Kanuni hii huchunguza muundo ndani na muundo nje wa dhana inayokanushwa. Kanuni hii hushikilia kuwa ukanushaji hujitoteza kulingana na muktadha pamoja na dhamira au dhima ya kupasha ujumbe au kuwasiliana. Mtumiaji lugha yeyote anapotekeleza ukanushaji, lazima atambua dhima na muktadha wa dhana inayokanushwa ili kupasha kwa ajili ya kupotosha ujumbe au kuwasiliana bila utata. Aidha, kanuni hii inashikilia kuwa aina ya ukanushaji huweza kudhihirisha maana au ujumbe kutegemea muktadha na dhima ya ukanushaji. Ukiukaji wa kanuni hii hupotosha maana ya ukanushaji katika mawasiliano na hata usanifu wa lugha husika kauli (Habwe & Karanja, 2004).

Matokeo ya uchunguzi wa Habwe & Karanja (2004); Pak (2017); Leah & Sseguya (2015) na Lupogo (2021) ulidhihirisha kuwa ukanushaji wa sentensi katika Luganda na Kiswahili sanifu huwa tata kwa sababu hujidhihirisha ikiwa na maana zaidi ya moja na hivyo ni muhimu kutambua muktadha wake wa matumizi. Matokeo ya matumizi ya kanuni hii kwa mujibu wa mihimili ya usarufi bia na upatanishi ya Chomsky, (1981) ilibainisha uwiano na tofauti katika ukanushaji kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo. Data Na. (5.55) kutokana na Pak, (2007) na Leah na Sseguya, (2015) inadhihirisha uwiano na tofauti ya muundo ndani na wa nje katika ukanushaji katika Luganda na Kiswahili sanifu.

a) *Maama wange ye'muntu agaba emmere nyingi.*

Maama wange **agaba emmere nyingi.**

Mama yangu ni mtu anayegawa chakula kingi.

Mama yangu hugawa chakula kingi.

b) *Maama wange ye'muntu atagaba emmere nyingi.*

Maama wange **tagaba emmere nyingi.**

Mama yangu ni mtu asiyegawa chakula kingi. Mama yangu hagawi chakula kingi.

Asili: Data kutokana na Pak, (2007)

Kwa mujibu wa mifano hii, sentensi ya kwanza inazungumzia juu ya sifa za ukarimu wa mtu ambaye ni mamake msemaji kwa njia ya urejeshaji huku sentensi ya pili, ikielezea hali ya mazoea ya jinsi mamake msemaji anavyofanya kazi yake ya kugawa chakula. Kwa hivyo, viambishi vikanushi vimebadilisha nafasi yake kutokana na muktadha wa kisemantiki wa sentensi na dhima ya sentensi kutegemea ujumbe unaowasilishwa kwa wasikilizaji na wasomaji. Kimofosintaksia, nafasi ya matumizi ya vikanushi katika utungo katika Luganda hutofautiana kimuktadha na Kiswahili sanifu kuwakilisha dhima, Kiswahili hukanusha vipatanishi nomino, viwakilishi vya njeo na hali kwa njia ya mbadilishano katika utungo huku, Luganda ikibadilisha na kuweka viambishi vikanushi baada ya vipatanishi hata ingawa ukanushaji wao wote huzingatia muktadha na dhima. Kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya kabubi hii kunabainisha kuwa, licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha za nasaba moja, kikanuni lugha hizi zinatofautiana kwa msingi wa data ya lugha hizo kuwa lugha mbili tofauti zenye kanuni za kipekee ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Kazi ya Lupogo, (2021) inaupa utafiti huu msisitizo kwani unadai kuwepo kwa muundo wa nje na ndani ambao unasitiriwa katika vikanusho katika Kiswahili. Aidha, matokeo ya utafiti wake yanaungwa mkono na Pak, (2017) na Leah & Sseguya (2015) ambao wanadhihirisha dhima ya ukanushaji ambao hutokana na dhima ya ukanushaji kutegemea muktadha na vikanushi vinavyohusika. Swale anaeleza dhamira za vikanusho mbalimbali katika ukanushaji wa lugha ya Kitikuu na Kiswahili sanifu. Kutokana na maelezo haya, utafiti huu ulibainisha kanuni ya muktadha na dhima ya utokeaji wa vikanushi. Matokeo ya uchanganuzi yalidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni ya muktadha na dhima /dhamira katika ukanushaji ambapo kila kikanushi, kilitokea katika mazingira maalumu ikiwa na dhima au dhamira ya kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

5.1.4.4.5 Kanuni ya uambishaji/uongezaji wa mofu kanushi

Kanuni hii hushikilia kuwa uambishaji wa viambishi katika tungo huzingatia mpangilio maalumu. Mpangilio unaokubalika na ambao ni lazima uzingatiwe ni ule wa kutumia viambishi mwafaka vinavyopatana na maneno mengine katika nafasi inayofaa kujenga dhana inayokubalika kisarufi. Kwa mujibu wa kanuni hii, uambishaji wa viambishi nafsi, njeo na ngeli kwenye vitenzi huathiri mofu kanushi ambazo huambikwa kwenye kategoria hizi za

maneno kujenga sarufi inayokubalika. Kupotoka kutumia kanuni ya uambishaji isiyokubalika kisarufi huweza kupotosha aina ya vikanushi vinavyostahili kuambishwa kwenye vitenzi na hivyo kupotosha usanifu wa lugha.

Uchanganuzi wa kazi za Chomi, (2003) na Leah na Sseguya, (2015), Lupogo, (2021), Kihore, Massamba & Msanjila, (2003:2012) Kiyinikibi, (2013) ulidhihirisha uwiano na tofauti za uongezaji wa viambishi vikanushi katika nafsi mbalimbali ya utokeaji wa vikanushi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data Na (5.56) inadhihirisha uwiano na tofauti ya matumizi ya kanuni ya uambishaji kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu kutokana na Hyman, (2018), Ngonyani (2001. (5.56).

- | | |
|---|---|
| a) <i>Sisoma ekitabo kyo 'luswayiri</i> | <i>Seetaaga kusoma ekitabo kyo 'luswayiri</i> |
| Si-som-i kitabo cha Kiswahili | Si-tak-i kusoma kitabo cha Kiswahili |
| b) <i>Togenda Ku ssomero</i> | <i>Towetaaga kugenda ku ssomero</i> |
| Hu-end-i shuleni leo | Hamw-end-i shuleni leo |
| c) <i>Temugenda ku ssomero leero</i> | <i>Temwetaaga genda ku ssomero leero</i> |
| Ham –end-i shuleni leo | Ham-fa-i kwenda shuleni leo |
| d) <i>Tasoma Oluganda bulungi</i> | <i>teyeetaga okusoma Oluganda bulungi</i> |
| Ha-som-i Luganda vizuri | Ha-fa-i kusoma Luganda Vizuri |

Asili: Data Kutokana na Hyman na Katamba (2010), Hyman, (2018)

Utafiti huu ulitambua kuwa uambishaji wa nafsi na njeo ya wakati uliopo kwenye vitenzi vya Luganda huzingatia mpangilio wa kiambishi kipatanishi cha nafsi, mzizi wa kitenzi na kiambishi tamati cha wakati uliopo (Kkp-Mz- [-a]Knj) ambacho kwayo husababisha athari za kifonolojia za fonimu za nafsi ya kwanza, pili na tatu ambazo hubadilika na kuwa [n-, w- na y-] kwa umoja na [tu-, mu-, b] kwa wingi. Hali hii huathiri mofu ya ukanushaji inayojitokeza katika nafsi kutegemea uambishaji wa viambishi nafsi, vitenzi na njeo ya kuongeza [t- au te-] kutegemea fonimu irabu na konsonanti inayotangulia katika kitenzi mtawaliwa. Kiswahili sanifu nacho huongeza mofu kanushi [ha-] kwenye kitenzi chochote chenye viambishi vipatanishi vya kiima isipokuwa [ni-].

Katika uambishaji wa viambishi nafsi na njeo katika vitenzi, ilibainika kuwa Luganda hutumia viambishi vikanushi tofauti kutegemea fonimu inayojitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi. Vile vile viambishi vya wakati vilivyotumika katika tungo havibadiliki. Tofauti na Kiswahili sanifu inayoongeza kikanushi [ha-] kwenye viambishi vipatanishi vya nomino kuu katika tungo, Luganda hujali sana kuambisha mofu za jumla za ukanushaji za [si-] za nafsi ya

kwanza, [te-] kwenye viambishi vya vitenzi vinavyoanza na konsonanti na [t-] ya viambishi vinavyoanza na irabu. Kiswahili sanifu hutumia mofu kanushi ambazo huambishwa katika nafasi ya kiwakilishi cha njeo au hali kinachotokea kati ya kiambishi kipatanishi cha msingi na mzizi wa kitenzi na kiambishi tamati cha wakati cha wakati uliopo. Kwa hiyo uambishaji wa Kiswahili hutokea mwanzoni, kati na mwishoni. Huku Luganda ikitumia nafasi moja ya mwanzo mwa vitenzi vinavyokanushwa kutegemea fonimu irabu na konsonanti.

Kwa mujibu wa Lupogo (2021), Ngonyani (2001) na Mulei (2020), utafiti huu uligundua kuwa kanuni ya uongezaji au uambishaji katika Luganda na Kiswahili sanifu huhusiana na matumizi ya vikanushi vinavyoambikwa kwenye mizizi ya vitenzi na kategoria za njeo katika tungo. Kwa mujibu wa kanuni hii, ilibainika kuwa Kiswahili hutumia viambishi vikanushi vya njeo na hali katika tungo badala ya viwakilishi vya njeo halisi. Matumizi haya hutokea katika nafasi ya njeo kwa njia ya mbadilishano. Tofauti inayojitokeza ni kuwa Luganda huambisha vikanushi [si-] ya nafsi ya kwanza na vikanushi [t-] vya irabu na [te-] ya konsonanti. Viambishi vya njeo hubakisha hadhi na nafasi yake bila kubadilika au kuongezwa kama inavyodhihirishwa na Rose, (2009), Leah na Sseguya, (2015), Kamoga, (1968). Aidha, wataalamu hawa wanadhihirisha kuwa Luganda hutumia kiambishi –na- kuwakilisha wakati uliopo hali timilifu [-me-] ambacho huwekwa kwenye kitenzi, katika kukanusha hali ya [-me-]. Silabi hii, huongezwa kwenye kikanushi [-naba] ambacho huongezwa baada ya kikanushi [si-] cha nafsi ya kwanza, [te-] ya konsonanti na [t-] ya irabu ikikifuatwa na ku- ya kitenzi jina. Kama inavyodhihirishwa katika Mifano (5.57) ya data kutokana na utafiti huu (5.57)

| | | | |
|---------------|---------------------------------|-----------------|-----------------------|
| <i>Nkoye</i> | <i>sinaba kukowa</i> | <i>tukooye</i> | <i>tetunaba koowa</i> |
| Nimechoka | <i>bado kuchoka</i> (sijachoka) | tumechoka | hatujachoka |
| <i>Olidde</i> | <i>tonaba kulya</i> | <i>mulidde</i> | <i>temunaba kulya</i> |
| Umekula | <i>bado kula</i> (sijakula) | mmekula | hatujakula |
| <i>Azze</i> | <i>tanaba kujja</i> | <i>bazze</i> | <i>tebanaba kujja</i> |
| Amekuja | <i>bado kuja</i> (hajaja) | <i>wamekuja</i> | hawajaja |

Asili: Data kutokana na Leah & Sseguya (2015)

Kwa kuongezea, ilibainika pia kuwa uongezaji mwingine unaojitokeza katika Luganda sanifu ni ule wa kukanusha hali timilifu ambapo [-nna-] huongezwa kwenye kitenzi kikanusho kinachotokea kabala kikanushi [si-] kati ya kiambishi nafsi na mzizi wa kitenzi, [te-] ya konsonanti na [t-] ya irabu kama inavyojitokeza katika mifano (5.58) ya data kutokana na matokeo ya utafiti (2021):

| | | | |
|-----------------|--------------------|------------------|---------------------|
| <i>Nyiimbye</i> | <i>Sinnayimba</i> | <i>Tuyimbye</i> | <i>Tetunayimba</i> |
| <i>Nimeimba</i> | <i>Sijaimba</i> | <i>Tumeimba</i> | <i>Hatujaimba</i> |
| <i>Ofumbye</i> | <i>Sinnafumba</i> | <i>Muffumbye</i> | <i>Ietunafumba</i> |
| <i>Umepika</i> | <i>Hujapika</i> | <i>Mmepika</i> | <i>Hamjapika</i> |
| <i>Ayisewo</i> | <i>Tannayitawo</i> | <i>Bayisewo</i> | <i>Tebanayitawo</i> |
| <i>Ampita</i> | <i>Hajapita</i> | <i>Wampita</i> | <i>hawajapita</i> |

Asili: Data kutokana na Leah & Sseguya (2015)

Mathalani kulingana na Leah na Sseguya, (2015), ilibainika kuwa Mofu [obu-] hutumika katika Luganda kuunda nomino inayokanusha kitenzi. Kiambishi hiki hutokea mbele ya kikanushi nafsi cha tatu umoja cha nomino inayokanushwa. Uongezaji wa kiambishi hiki husababisha kitenzi kukanushwa katika hali ya kuendelea. Mfano (5.58) wa data kutokana na Leah na Sseguya, (2015) unadhihirisha matumizi ya kanuni hii katika Luganda tofauti na Kiswahili sanifu: (5.58)

| | |
|-----------------------|-------------------------|
| <i>Kulya mmere</i> | <i>Obutalya emmere</i> |
| <i>Kula chakula</i> | <i>kutokula chakula</i> |
| <i>Kulima emmere</i> | <i>obutalima emmere</i> |
| <i>Kulima chakula</i> | <i>kutolima chakula</i> |

Asili: Data data kutokana na Leah na Sseguya, (2015).

Matokeo haya yanaendana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi nadharia ya umilikifu na unganifu ambayo ilidhihirsha kuwa Luganda na Kiswahili licha ya kuwa na kanuni moja ya uongezaji wa wa viambishi katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu, lugha hizi ni lugha mbili tofauti yenye kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo. Aidha, matokeo haya yanafanuliwa na Kiyinikibi, (2021) ambaye anadhihirsha kuwa Kiswahili huambisha vikanushi vyake mwanzoni kabla ya KPM , katikati mahali pa njeo na mwishoni mwa kitenzi hasa katika wakati uliopo. Maelezo yake yanashabihiana na ya Hyman (2018) na Leah na Ssguya ambao wanadonyesha uambishaji wa vikanushi vya luganda mwanzoni mwa kitenzi kinachokumushwa.

5.1.4.4.6 Kanuni ya udondoshaji wa mofu ya nafsi ya I na kihusishi [ni] katika kauli yakinishi

Kanuni hii hushikilia kuwa baadhi ya vipashio vya kisarufi katika tungo virai hudondoshwa na badala yake kutumika mofu mbadala kudhihirisha hali kanushi ya vitenzi. Udondoshaji huu hutokea kwenye vitenzi vyenye kiambishi kipatanishi cha nafsi ya kwanza (Mgullu, 1999; Chomi, 2003, Ngonyani, 2001 na Habwe & Karanja, 2004). Kwa mujibu wa waaalamu

hawa (washatajwa), utafiti huu ulibaini kushabihiana kwa matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Luganda na Kiswahili hudhihirisha matumizi ya kanuni hii ya kudondosha kipatanishi cha nafsi ya kwanza [n] ya Luganda na [Ni-] ya Kiswahili na katika nafasi yake au katika mazingira yake mofu kanushi [si-] kutumika kama inavyojitokeza katika data Na. (5.59) kutokana na Leah & Sseguya na Rose (2009), Mulei, (2020), Lupogo, (2021), Habwe & Karanja, (2004) kuhusu udondoshaji wa mofu kanushi

| | | | |
|-----------------|---------------------|-----------------|------------------------|
| <i>N-yimba</i> | <i>[Si-yimbi]</i> | <i>Tuyimba</i> | <i>tetuyimba</i> |
| <i>Ninaimba</i> | <i>[si-o-imb-i]</i> | <i>Tunaimba</i> | <i>[ha-tu-o-imb-i]</i> |

Mfano (5.60) unadhihirisha kudondoshwa kwa kipatanishi cha nafsi ya kwanza [n] ya Luganda na [ni-] ya Kiswahili na badala yake mofu kanushi [si-] kutumika. Vilevile, imedhihirika kuwa kiambishi cha njeo ya wakati uliopo [-na-] cha Kiswahili hudondoshwa na badala yake ukanushaji kutokea mwishoni mwa kitenzi ambapo kiishio [-a] hupokea mofu kanushi [-i]. Tofauti inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni kuwa Luganda hutumia kanuni hii bila kudondosha njeo na hali, huku Kiswahili kikizingatia kudondosha na kutumia mofu mbadala kuwakilisha hali kanushi ya njeo na hali.

5.1.4.4.7 Kanuni ya kubadilisha viwakilishi vya njeo na hali

Kanuni hii hushikilia kuwa kila njeo na hali huwakilishwa na mofu kadhaa ambazo wakati wa kukanusha mofu hizi hudondosha na badala yake mofu kanushi wakilishi ya njeo na hali kutumika. Ukiukaji wa kutumia mofu kanushi tofauti na mofu kanushi inayohusika katika ukanushaji wa njeo na hali hupotosha usanifu wa lugha husika. Swaleh, (2017), Lupogo, (2021), Ngonyani (2001), Mulei, (2020) na Hyman, (2018), ilibainika kuwa kanuni hii haijitokezi katika Luganda bali imesheheni ukanushaji wa vitenzi katika Kiswahili sanifu. Kila njeo imewakilishwa na kikanushi chake ambacho hutumika katika mazingira sawa na ya njeo yakinishi ila katika njeo ya wakati uliopo ambapo kiwakilishi kikanushi hutokea mwishoni mwa kitenzi. Rejelea jedwali (4.17, Uk.122 na 4.18 Uk. 124) yanayodhihirisha maumbo ya njeo na hali ya ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na Mulei, (2014: 2020), Ngonyani, (2001), Lupogo, (2021), Habwe & Karanja, (2004), Kyagaba (1996) (1999) na Leah na Sseguya, (2015).

Tofauti inayojitokeza baina ya kanuni ya mabadiliko ya njeo na hali baina ya Kiswahili na Luganda sanifu ni kuwa, Luganda hujali sana kutumia kanuni za kuambisha vikanushi [si-t-na te-] kutegemea nafsi ya kwanza na fonimu irabu na konsonanti mtawaliwa ila njeo na nyakati hubakisha hadhi zake na utokeaji wake. Ukanushaji katika Kiswahili sanifu

hutegemea sana njeo na hali ambapo kila njeo na hali huwakilishwa na mofu kanushi ila katika wakati ujao [-ta-] Habwe & Karanja, 2004, Lear na Sseguya, 2015, Ngonyani, 2001 na Rose, 2009). Matokeo haya yamejadiliwa na Mulei (2014: 2020), Lupogo (2020:2021) na Swaleh, (2017) ambao wanadhihirisha udondoshaji wa maumbo ya nafsi ya kwanza [ni], kutumia kikanushi {si}, kudondosha njeo yakinishi na badala yake kutumia mofu kanushi ya njeo na hali. Aidha, Hyman (2018), Kamoga na Kiyinikibi, (2021) wanashadidiwa matumizi ya kanuni katika Luganda. Kutokana na ugunduzi huu, utafiti huu uliweza kutambua kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti ambazo hudhihirisha utokeaji wa kanuni ya udondoshaji wa viwakilishi njeo na badala yake kutumia vikanushi kudhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo.

5.2 Hitimisho

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni ulidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kila kipashio kilidhihirisha kanuni ya kipekee inayotumika kuonyesha uhusiano milikifu na Unganifu ya neno kuu na maneno mengine katika tungo. Kanuni za kimofosintaksia za ngeli za nomino, vivumishi, viwakilishi na vikanusho zilichanganuliwa. Kila kipashio kilidhihirisha upekee wa matumizi ya kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino na mofolojia ya uambishaji, uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kimofosintaksia, sarufi miundo, umiliki na usabaki wa viambajengo, uambishaji amilifu, upatanishi wa kisarufi wa viambishi yambwa, kifonolojia ya udondoshaji, kisarufi ya uwakilishi dhima na matumizi ya vibainishi na viambishi na kanuni ya ukuu na darajia za vijenzi vya maumbo ya maneno na utokeaji miongoni mwa kanuni kadhaa za vipashio vilivyohusika katika utafiti vilichanganuliwa. Uchanganuzi wa kanuni ulibaini kuwa kanuni ndio nguzo ya pekee inayoweza kufafanua uhusiano wa vipashio vya kimofosintaksia katika muktadha wa tungo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa kanuni hizi, uchanganuzi wa kanuni za Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni kadhaa zinazofafanua matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia ambazo hutegemea, muundo au sifa za kipashio, maumbo ya kipashio, mpangilio au nafasi ya utokeaji wa kipashio, upatanishi wa kisarufi wa kipashio, mabadiliko ya kimofonolojia, uwakilishi maumbo ya kipashio na dhima ya matumizi ya kipashio katika tungo. Kwa mujibu wa uchanganuzi, ilibainika kuwa kila kipashio cha kimofosintaksia cha Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni zinazofafanua mifanyiko au matumizi yake. Hata hivyo, kanuni hizi ziliwiana na kutofautiana kutoka kipashio kimoja na kingine na kutoka lugha moja na nyingine.

SURA YA SITA

KANUNI ZA MIFANYIKO YA KIMOFOSINTAKSIA YA LUGANDA NA ATHARI ZAKE KATIKA MATUMIZI YA KISWAHILI SANIFU

6.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili matokeo ya data kuhusu madhumuni ya tatu ya kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Data zilikusanywa maktabani na nyanjani. Nyanjani, data zilikusanywa kutumia mijarabu ya kisarufi iliondaliwa kwa ajili ya kujibiwa na wanafunzi kimaandishi. Vile vile data ilikusanywa nyanjani kutumia mijadala kutokana na matokeo ya mijarabu darasani ambapo wanafunzi waliongozwa kujadiliana kuhusu matumizi ya vipashio vya mofosintaksia kutokana na matokeo ya majibu ya mijarabu ya mazoezi ya kisarufi. Kifaa cha kudondoa data chenye sifa za kimofosintaksia kilitumika kutathimini kanuni za Luganda, mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia na athari za matumizi ya kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Uwasilishaji na mijadala ya matokeo yaliwasilishwa kutumia njia ya maelezo kwa mujibu wa madhumuni ikiongozwa na mihimili ya ubia na upatanifu ya Nadharia ya Umilikifu na Uganifu ya Chomsky, (1981) inayoshikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo.

Tathimini ya kanuni za matumizi ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na maandishi na mazungumzo ya wanafunzi yalidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli katika nomino (nomino katika ngeli), vivumishi, viwakilishi na vikanushi. Kufanana na kutofautiana kwa kanuni za vipashio vya mofosintaksia vya Luganda katika matumizi kulisababisha athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama inavyojadiliwa hapa chini.

6.1.1 Mwingiliano na athari za kanuni za ngeli nomino za Luganda katika matumizi ya Kiswahili

Matokeo ya uchanganuzi wa data za maktabani na nyanjani kuhusu mwingiliano na athari za kanuni za ngeli nomino katika matumizi zilibainisha kuwa, licha ya kuwa matumizi ya kanuni za ngeli za Kiswahili sanifu huzingatia utaratibu wa kupanga nomino kuonyesha upatanishi wa kisarufi wa nomino na maneno mengine ya kategoria ya kisarufi kimofolojia na kisintaksia, wanafunzi ambao L1 ni Luganda hujikuta wakitumia kanuni mbalimbali za matumizi ya ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili kuonyesha mahusiano ya nomino husika na maneno

mengine ya kategoria ya kisarufi (vipashio vya kisarufi) na viambajengo vingine katika utungo. Matumizi haya yalipotosha sifa kamili za matumizi ya ngeli za Kiswahili sanifu katika tungo kama inavyojadiliwa hapa chini.

6.1.1.1 Kanuni ya Kimofosintaksia ya Uundaji wa Nomino

Data za utafiti kutokana na mijadala ya wanafunzi kuhusu uundaji wa nomino, ulidhihirisha kwamba Luganda na Kiswahili sanifu huunda nomino zake kwa kuwekea viambishi mbalimbali kwenye mizizi ya nomino kutumia kanuni ya kimofolojia ya uundaji wa nomino. Kanuni hii inashikilia kuwa: Nomino huundwa kutokana na kupachika viambishi mbalimbali vyenye sifa za kiuamilifu za mofolojia na sintaksia kwenye mizizi ya maneno katika tungo. Mifano ya data katika Jedwali (4.2, Uk. 76) ulidhihirisha utokeaji wa kanuni baina ya Luganda na Kiswahili kutokana na data za maktabani.

Kwa kutumia mjarabu ya kisarufi, wanafunzi waliulizwa kutumia jozi za ngeli za Kiswahili kimofolojia na kisintaksia, kutunga sentensi za Kiswahili kwa umoja na wingi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Kwa kuzingatia mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya Chomsky, (1981), matokeo yalidhihirisha mwingiliano wa maumbo ya Luganda kujitokeza katika matumizi ya Kiswahili sanifu na athari za ukopaji na uhamishaji wa maumbo wakilishi nomino katika ngeli ya Luganda kimofolojia na kisintaksia kuonyesha uhusiano wa neno na maneno mengine katika tungo. Mwingiliano huu ulitokana na kuwa maumbo na taratibu za mpangilio wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu unaotumiwa kuonyesha uhusiano wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo hutofautiana hata ingawa baadhi ya maumbo yanayotumika yanafanana. Matokeo haya yanaendana na msingi wa uchunguzi wa muundo ndani na nje wa maumbo ya Lugha mbili za Luganda na Kiswahili kwa mujibu wa mihimili wa sarufi bia wa nadharia ya umilikfu na Unganifu ya Chomsky (1981). Data Na. (6.1) ilidhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino katika ngeli.

Na. (6.1a)

| <i>Athari za mwingiliano</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> | <i>Ngeli</i> |
|------------------------------|-----------------------------|--------------------------------|
| <i>Mutoto muzuri</i> | M toto m zuri | <i>m-wa [mu-ba ya Luganda]</i> |
| <i>Omwana Omulungi</i> | | |
| <i>Muwalimu murefu</i> | M walimu mrefu | <i>m-wa [mu-ba ya Luganda]</i> |
| <i>Omusomesa omuwanvu</i> | | |
| <i>Mupolisi/wapolisi</i> | Polisi | <i>m-wa [mu-ba ya Luganda]</i> |

Mudaktari/wadaktari Daktari *m-wa* [mu-ba ya Luganda]

Na. (6.1b)

Muti mukubwa Mti mkubwa *m-mi* [mu-mi ya Luganda]

Omuti munene

Mukati/mugati mutamu Mkate mtamu *m-mi* [mu-mi ya Luganda]

Omugaati

Muguu kubwa Mguu mkubwa *m-mi* [gu-ga ya Luganda]

Okugulu kunene

Na. (6.1c)

Vitabu byangu Vitabu vyangu *ki-vi* [ki-bi ya Luganda]

Ebitabo byange

Kiatu yangu Kiatu **changu** *Ki-vi* [ki-bi ya Luganda]

Viatu zangu Viatu **vyangu** *ki-vi* [ki-bi ya Luganda]

Engaato zange

Na. (6.1d)

Maji mangi/maingi Maji **mengi** *ji-ma* [ma ya Luganda]

*Amazzi **Mangi***

Mayai mangi/maingi Mayai **mengi** *ji-ma* [ma ya Luganda]

Amaggi mangi

Sikio kupana Sikio pana (*semantiki [ku] ya sikio [okutu ku...]*) [ku-ma ya Luganda]

Okutu kunene

Asili: Data kutokana na mjarabu wa kisarufi wa wanafunzi wa Kiswahili

Data Na.(6.1) inadhahirisha, mwingiliano na athari za matumizi ya kanuni za kimofosintaksia za uundaji wa nomino za Luganda katika Kiswahili, wanafunzi walikopa au kuhamisha maumbo wakilishi ya nomino katika ngeli ya Luganda kimofolojia na kisintakisa. Matumizi haya yalitokana na mwingiliano na tofauti za maumbo ya kimofosintaksia. Miundo hii ya matumizi ya viambishi hutofautiana. Tofauti zinazojitokeza ni za kimaumbo za nje na ndani. Maumbo haya hutumika kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi wa nomino kimofolojia na Kisintakisa. Viambishi vya Luganda vilivyotumika katika tungo za Kiswahili kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi viliathiri mofosintaksia ya Kiswahili sanifu. Maumbo yaliyotumika yalikuwa na tofauti ingawa yalikaaribiana kufanana au kufanana kimatamshi au kifonimu na ya Kiswahili hata hivyo hayakuwakilisha maumbo kamili ya kimofolojia na kisintaksia ya Kiswahili sanifu. Licha ya matumizi haya kuonyesha matumizi ya mhimili wa upatanifu unaofafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo

huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika, kanuni hii idhihirisha kutofautiana kidogo kati ya Luganda na Kiswahili hivyo kusababisha athari za mwingiliano kwa mujibu wa mhimili wa sarufi bia. Data katika jedwali Na (6.1) inadhihirisha mwingiliano wa maumbo yaliyohamishwa kutoka Luganda katika matumizi ya Kiswahili ambayo yalijitokeza katika tungo za wanafunzi kama inavyojitokeza katika ngeli za Luganda na Kiswahili za 1

Jedwali 6.1: Viambishi awali vya ngeli vya Luganda vilivyoathiri muundo wa nomino za Kiswahili sanifu na maneno mengine katika tungo

| <i>Ngeli</i> | <i>Mofosintaksia ya viambishi awali vya nomino Vya Luganda</i> | <i>Athari za Mwingiliano wa viambishi awali vya Luganda katika Kiswahili</i> |
|--------------|--|--|
| 1 | <i>m-</i> | <i>mu-</i> (<i>mutoto, muwalimu, muallimu</i>) |
| 3 | <i>m-</i> | <i>mu-</i> (<i>muti, mulango, muchungwa</i>) (<i>omuti, omulyango, omucungwa</i>) |
| 4 | <i>mi-</i> | <i>mi-</i> (<i>miyembe, miyembe, mikopo</i>) (<i>omuyembe, emiyembe, ebikopo</i>) |
| 5 | <i>li-</i> | <i>li-</i> (<i>liso, licho, lino</i>) (<i>riiso, riinnyo</i>) |
| 6 | <i>ma-</i> | <i>ma-</i> (<i>mambuzi, mang'ombe, maino</i>) |
| 7 | <i>ki-</i> | <i>ki-</i> (<i>kyifuniko, kikyiko, kyikarayi</i>) |
| 9 | <i>n-</i> | <i>n-</i> (<i>mbuzi zinakula, kuku zimeletwa</i>) (<i>embuzi zirya, enkoko zireteddwa</i>) |
| 10 | <i>n-</i> | <i>n-</i> (<i>mbuzi zinakula, kuku zinaletwa</i>) (<i>embuzi zilikulya, enkoko bazireeta</i>) |
| 15 | <i>ku-</i> | <i>Ku-</i> (<i>kunyumba, kushule, kusokoni</i>) |
| 18 | <i>mu-</i> | <i>mu-</i> (<i>munyumba, mudarasa, mujikoni</i>) (<i>Munnyumba, Mukibiina, Mufumbiro</i>) |

Asili: Data Kutokana na mjarabu ya tungo za wanafunzi nyanjani

Jedwali hili linadhihirisha kuwa nomino za Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana kimuundo kutokana na maumbo awali yanayopachikwa kwenye mizizi ya maneno ya kileksika kuwakilisha ngeli, jinsia ya kisarufi (dhima) na idadi ya umoja na wingi. Maumbo ya ngeli za [1,3,4,5,6,7,8,9,10,11,15,18] kimofolojia yalidhihirisha kufanana au kukaribiana kufanana kuzingatia viashiria au viambishi awali vya nomino kuu vilivyopachikwa kwenye vivumishi vya Kiswahili sanifu. Kutokana na kufanana, wasailiwa waliweza kuhamisha maumbo hayo na kuyatumia hata ingawa nomino zilizotumika zilitoka katika ngeli tofauti na lugha tofauti kiuanishaji. Vilevile, walitumia uainishaji wa kisemantiki kufasiri nomino na kutumia viambishi vya kisarufi vya Luganda na kupachika viambishi awali vya ngeli kwenye vivumishi badala ya viambishi kamili vya Kiswahili sanifu. Wanafunzi walihamisha viambishi awali vya nomino na vya upatanishi wa kisarufi, kuchanganya maumbo ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Athari hii ilitokana na kanuni ya muundo na matumizi ya ngeli katika Luganda. Athari za mwingiliano wa matumizi ya ngeli kimofolojia

na kisintaksia yalijitokeza katika maneno yaliyochukua viambishi awali vya nomino kuu kuwakilisha utawala na umilikifu wa nomino kama neno kuu katika kundi nomino (KN). Muundo huu ulijitokeza katika tungo zenye nomino na vivumishi vya sifa na vitenzi kama ilivyojitokeza katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi.

Matokeo haya yanashabihiana na ya Oduor, Inyani & Kobia, (2017), Odeo & Maina, (2008) ambao wanaeleza kuwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili huathiriwa na lugha ya kwanza, hasa inapotokea kwamba mfumo na miundo wa lugha ya asili hutofautiana na ule wa Kiswahili sanifu. Kutokana na utafiti huu, ilibainika kwamba Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za Kibantu ambazo zilidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za uundaji na maumbo ya matumizi ya kipashio cha kimofosintaksia cha ngeli. Matokeo haya yalidhihirisha vilevile kuwa, licha ya Luganda na Kiswahili kutumia kanuni hii, matumizi yake hutofautiana kutokana na upekee baina ya maumbo ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo haya yanashabihiana na mapitio ya maandishi ya Kihore & wenzie, (2001) wanaosema kwamba sifa za upatanifu wa kisarufi kutokana na matumizi ya ngeli nomino sio wa Kiswahili pekee bali ni wa lugha zote za Kibantu. Kwa hivyo, pale lugha mbili za Kibantu zinapotofautiana kwa viashiria vya kimofimu, bila shaka kuathiriana kutakuwepo.

Tathimini ya matumizi ya kanuni hii maktabani ilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia viambishi amilifu vinavyoambishwa mwanzoni mwa mizizi ya nomino kuwakilisha ngeli, idadi ya umoja na wingi (mofolojia) pamoja na upatanishi wa kisarufi unaodhihirisha mahusiano ya neno kuu katika utungo na maneno mengine kisintaksia. Matumizi ya viambishi hivi vilitokana na kanuni au msingi wa uainishaji wa ngeli nomino kimofolojia na matumizi ya maneno mengine kisarufi (kisintaksia). Viambishi hivi vilibeba sifa au taarifa za nomino kimofosintaksia kimatumizi. Mfano wa data Na.(6.2) unadhihirisha uambishaji husika.

Luganda

a) *Ente ereeteddwa kussomero*

b) *Ente zireeteddwa kussomero*

c) *Omuti gugudde ne gumenya enyumba*

d) *Emiti gigudde ne gimenya amayumba*

Kiswahili sanifu

Ngo'mbe ameletwa shuleni

Ngo'mbe wameletwa shuleni

Mti ulianguka na kuvunja nyumba

Miti ilianguaka na kuvunja nyumba

Asili: Data za upatanishi wa kisarufi kutokana na Kiyinikibi, (2021:23) Maktabani

Data hii ilidhihirika kuwa maumbo ya nje na ndani na taratibu za uundaji wa nomino na mpangilio wa ngeli za Luganda na Kiswahili kuwakilisha idadi ya umoja na wingi kimofosintaksia hufanana na kutofautiana kama ilivyodhibitishwa katika maelezo ya Mulei, Amukowa & Ambuyo (2021) na Namugala, (2014), Chomi, (2003), Kiyinikibi, (2021), Namugala, (2014) na Mukuria, (1987), Besha (1996), Mgullu, (1999), Habwe & Karanja, (2004) maktabani. Mofu za kimofolojia za nomino hudhihirisha uamilifu wake katika maneno mengine kudhihirisha umilikifu na unganifu wa maumbo patanifu katika tungo kimofosintaksia. Kufanana na kutofautiana huku kunatokana na msingi wa mihimili wa sarufi bia wa uchunguzi wa maumbo ya ndani na nje. Licha ya kuwa matumizi ya maumbo haya ni ya upatanifu unaofafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika, tofauti inayojitokeza inadhihirisha usarufi bia wa zinazotumika katika lugha zote, kutofautiana kidogo katika msingi wa data ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashadidiwa na Jerro, (2018) Hyman na Katamba (1991: 1993) na Katamba (2003) ambao walidhihirisha ukosefu wa vibainishi vya ngeli katika maumbo ya kimofolojia ya ngeli kinyume na jinsi inavyodhihirishwa katika Luganda kimofonolojia. Aidha, walitambua uchache wa idadi za ngeli za Kiswahili ikilinganishwa na ngeli za Luganda mkabala wa ngeli za Proto-Bantu. Wanaeleza kuwa:

“As for the phonological shape of the morphemes, Swahili lacks the pre-prefix that is found in Luganda and Rwanda. At a first glance, this could be argued to be an instance of phonological reduction in Swahili.” (Jerro, 2018:11).

Kuhusu umbo la kifonolojia la mofimu, Kiswahili hakina kiambishi awali ambacho kinapatikana katika Luganda na Kinyarwanda. Kwa mara ya kwanza inaweza kufikirika kuwa mfanyiko wa kifonolojia wa kudondoa sauti (TY).

Matokeo ya mjadala kuhusu kubainisha kanuni ya kimofolojia na kisintaksia ya uundaji wa nomino ilidhihirisha ufahamu wa wanafunzi kutambua kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino katika Luganda na Kiswahili. Wanafunzi waliweza kubaini kuwa nomino za Luganda na Kiswahili sanifu huundwa kwa viambishi mbalimbali ambavyo huainisha nomino katika vikundi kimofolojia na kisintaksia. Mtafiti alipowauliza wanafunzi kujadili jinsi nomino za Luganda zinavyoundwa kimofosintaksia, Mwanafunzi 34 alieleza kuwa:

“Nomino za Luganda na Kiswahili zina viambishi ambavyo huwekwa nyuma ya mzizi wa nomino kuonyesha kikundi cha nomino ambayo inatajwa kimofolojia na maumbo ya upatanishi ambayo huwekwa kwa vitenzi na maneno mengine katika sentensi.”

Aidha, wanafunzi alipoulizwa kueleza uwiano na tofauti za nomino za Luganda na Kiswahili, Mwanafunzi 22 alieleza kuwa:

Baadhi ya maumbo ya nomino za ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu yanafanana na mengine kutofautiana.

Katika mijadala, ilibainika kuwa licha ya wanafunzi kubaini kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa nomino katika Luganda na Kiswahili, wanafunzi 12 walidhihirisha kutotambua baadhi ya maumbo na mpangilio wa ngeli za Luganda na Kiswahili. Aidha, wanafunzi 31 walikuwa na uwezo wa kutambua ngeli nomino za Luganda na Kiswahili ila hawakutambua utaratibu na maumbo ya kimofosintaksia ya baadhi ya nomino hadi wanapotumia katika tungo. Wanafunzi 11 walidhihirisha ufahamu wa kutambua uwiano na tofauti za maumbo ya kimofosintaksia na mchakato wa uundaji wa nomino na uainishaji wake katika Luganda na Kiswahili. Aidha, data katika Jedwali (4.2, Uk. 76) liliweza kubainisha kufanana na kutofautina kwa maumbo ya kimofosintaksia ya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu licha ya kuwa lugha hizi zote ni lugha za Kibantu.

Maelezo ya Katamba, (2006), Jerro, (2018), Katamba & Hyman, (2001:1991:1993) ambao wanakubali kuwa Luganda ni lugha nasibu yenye mifumo ya kipekee ya fonolojia, mofolojia na sintaksia inayotofautiana na lugha zingine za Kibantu kama ilivyo Kiswahili sanifu. Hali ambayo ilidhihirika katika utafiti huu. Nomino za Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana kimuundo kutokana na maumbo awali yanayopachikwa kwenye mizizi ya maneno ya kileksika kuwakilisha ngeli, jinsia ya kisarufi (dhima) na idadi ya umoja na wingi.

6.1.1.2 Kanuni ya sarufi maumbo / mofolojia ya uambishaji maneno

Kanuni hii inashikilia kuwa, kila lugha huwa na maumbo ya kipekee yanayotumika kuunda vipashio vya kisarufi vya lugha kuwakilisha usahihi wake kimatumizi. Pia, kanuni hii inaendelea kushikilia kuwa uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi (uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno kutokana na nomino kama neno kuu. Data na. (5.1 Uk. 131) inadhihirisha mwingiliano na athari za matumizi ya kanuni yamofolojia ya uambishaji maneno kisarufi. data (5.1) ilidhihirisha kuwa Luganda hutumia vibainishi na viambishi ngeli kutenda kazi moja ya kutambulisha ngeli nomino na idadi ya

umoja na wingi huku Kiswahili kikitumia viambishi ngeli nomino pekee. Hata hivyo, vibainishi hivi na viambishi ngeli huambisha mwanzoni, vikifuatwa na viambishi vinginevyo vinavyowakilisha sifa za kisarufi. Data hii ina hii inaendana na mihimili ya usarufi bia na upatanifu wa matumizi ya kanuni hii kwa mujibu wa nadharia ya Umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981).

Kwa kurejelea data ya maktabani kuzingatia kanuni ya mofolojia ya uambishaji wa maneno, utendakazi wa kanuni hii, ilibaini kuwepo kwa mwingiliano wa utaratibu wa kuongeza mofu za kisarufi kwenye mizizi ya maneno kujenga maana fulani za kisarufi za maneno husika bila kuunda maneno mapya au bila kubadilisha aina za nomino, maneno na aina za maneno, taratibu zinazohusika katika uundaji wa maneno na matumizi ya maneno katika utungo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu (Katamba 2003, Massamba na wenzake 2001:2003 na Kiyinikibi, 2021). Pia, ilibainika kuwepo kwa mwingiliano wa kiuamilifu wa matumizi ya maneno baina ya Luganda na Kiswahili sanifu katika tungo kujenga maana za kisarufi kuelezea dhana, idadi ya umoja na wingi na jinsi ya maneno katika utungo. Aidha, kwa sababu uamilifu wa lugha hujitokeza katika mazungumzo na maandishi, uchanganuzi wa mpangilio na taratibu za kutumia vitamkwa, mizizi, viambishi na mifanyiko ya uambishaji na unyambulishaji katika uundaji wa maneno na tungo virai kuwakilisha ngeli husika na idadi ya umoja na wingi vile vile ulidhihirisha uwiano na tofauti kati ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Massamba na Wenzake, (2003) wanaoeleza kuwa, nomino huundwa kwa viambishi awali vya unominishaji ambavyo hutumika kuwakilisha maana ya kisarufi katika utungo. Viambishi vya nomino huweza kuwakilishwa na maumbo dhahiri na kapa. Viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi huwakilisha maana za kisarufi. Majina yanayoainishwa huzingatia maumbo yaliyo na upatanishi wa kisarufi wa maneno mengine ulio sawa kiurejeshi.

Matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya kubainisha maumbo ya kisarufi ya uambishaji maneno katika tungo ilibaini mwingiliano na athari za matumizi ya kanuni ya mofolojia ya uambishaji maneno kisarufi. Kwa kurejelea maumbo ya nomino katika Luganda na Kiswahili, wanafunzi waliulizwa kubainisha uwiano na tofauti za maumbo ya nomino katika Luganda na Kiswahili kutumia jedwali. Matokeo yalibainisha mwingiliano wa maumbo na tofauti za maumbo ya kimofolojia ya uambishaji wa maneno kisarufi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika Jedwali Na (6.2):

Jedwali 6.2: Maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya ngeli nomino na mwingiliano wake.

| <i>Ngeli</i> | <i>Maumbo ya Luganda kimofolojia</i> | <i>Maumbo ya Luganda kisintaksia</i> | <i>Maumbo ya Kiswahili kimofolojia</i> | <i>Maumbo ya Kiswahili kisintaksia</i> | <i>Mwingiliano</i> |
|--------------|--------------------------------------|--------------------------------------|--|--|---------------------------|
| 1 | (o)mu- | a- | m(u)- | a- | [Mu-a]→[m-a] |
| 2 | (a)ba- | ba- | wa- | wa- | - |
| 3 | (o) mu- | gu- | m(u)- | u- | [mu]→[m] |
| 4 | (e)mi- | gi- | mi- | i- | [mi]↔[mi] |
| 5 | Li; (e)ri- | li- | ji-∅ | li- | [li-umoja] [li- wingi] |
| 6 | (a)ma- | ga- | ma- | ya- | [ma] ↔[ma] |
| 7 | (e)ki- | ki- | ki- | ki- | [ki] ↔ [ki] |
| 8 | (e)bi- | bi- | vi- | vi- | - |
| 9 | (e)n- | e- | n- | i- | [n-] ↔ ∅/n] |
| 10 | (e)n- | zi- | n- | zi- | [n] ↔ [zi] |
| 11 | (o)lu- | en- | u- | u- | - |
| 12 | (a)ka- | ka- | n- | zi- | [ka-] [∅] |
| 13 | (o)tu- | tu- | - | - | [tu-] [∅] |
| 14 | (o)bu- | bu- | - | - | [bu] [∅] |
| 15 | (o)ku- | ku- | ku- | ku- | [ku] ↔ [ku] |
| 16 | wa- | wa- | pa- | pa- | - |
| 17 | ku- | ku- | ku- | ku- | [ku] ↔ [ku] |
| 18 | mu- | Mu- | mu- | mu- | [mu-] ↔ [mu-] |
| 20 | (o)gu- | gu- | | | |
| 22 | (a)ga- | ga- | | | |
| 23 | E | | | | |

Chanzo: Data kutokana na Abudonia (2015) na Mgullu, (1999)

Data ya Jedwali (6.2) inadhihirisha kuwepo kwa maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya Luganda na Kiswahili ambayo hufanana ingawa yanatumia nomino za aina tofauti kisemantiki. Maumbo haya yalisababisha athari za mwingiliano wa kimofosintaksia unaojitokeza katika matumizi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo ya kifaa cha kudondoa data chenye maumbo ya kimofosintaksia yalidhihirisha kuwa; kutokana na mfanano wa kimofolojia na sintaksia ya maumbo yanayowakilisha viambishi awali vya nomino na maumbo yaliyoonekana kuwa alomofu ya viambishi husika, wanafunzi ambao L1 ni Luganda walijikuta wakitumia viambishi vya Luganda kimofolojia na kisintaksia katika tungo virai vya Kiswahili hasa walipopata ugumu wa kuelewa viambishi mwafaka. Matumizi haya yalitokana na Luganda na Kiswahili sanifu kuainisha nomino zake kwa kuzingatia msingi huu wa kanuni ya kimofolojia ya uambishaji wa maneno katika tungo.

Kwa kutumia kifaa cha kudondoa data kutoka kwa mjarabu wa kutunga sentensi na kubainisha maumbo ya uambishaji wa maneno, utafiti huu uligundua athari za Mwingiliano wa ukopaji na uhamishaji maumbo. Wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikopa na kuhamisha viambishi vya Luganda kimofosintaksia katika tungo za Kiswahili hasa walipopata ugumu wa kuelewa viambishi mwafaka kutokana na msingi wa kimofolojia na kisintaksia wa uambishaji wa maneno katika tungo. wanafunzi walikosa kufahamu kuwa licha ya Kufanana kwa maumbo ya Luganda yanayoonyesha uhusiano wa kimiundo wa sheria za kiupatanishi, maumbo hayo ya Luganda hutofautiana na ya Luganda katika maumbo ya msingi ya nje na ndani kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya nadharia ya Chomsky (1981). Data Na. (6.3) kutokana na Mjarabu wa kisarufi wa kutunga sentensi ulidhihirisha mwingiliano na athari kutokana na kanuni hii: (6.3)

Athari za Luganda kwa Kiswahili

Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

- | | |
|--|-----------------------------------|
| a) <i>Ng'ombe zimeletwa nyumbani</i> [n-zi] <i>Ente zireeteddwa ewaka</i> | Ng'ombe wameletwa nyumbani [Ø-wa] |
| b) <i>Mbuzi zinakula mahindi</i> [n-zi] <i>Embuzi ziryaka kasooli</i> | Mbuzi wanakula majani. [Ø-wa] |
| c) <i>Paka zimekamata panya</i> [n-zi] <i>Ekapa zikute emmese</i> | Paka wamewakamata panya [Ø-wa] |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi

Wanafunzi waliathiri Kiswahili sanifu kwa kubeba viambishi vipatanishi vya ngeli ya 10 ya Luganda katika matumizi ya nomino katika ngeli ya 1 na 2. Uhamishaji huu ulitokana na uhamishaji wa nomino na maumbo ya kimofolojia ya nomino katika ngeli ya 10 hadi ngeli ya 1 na 2 kisemantiki kudhihirisha umilikifu na Unganifu wa vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hudhihirika katika mofu za kisintaksia za vipashio. Uhamishaji huu ulibadilisha maumbo ya upatanishi wa nomino za ngeli ya [m-wa/a-wa] hasa kwa nomino za viumbe hai ya wanyama ambayo hayabadiliki kimaumbo. Viambishi vipatanishi vya nomino za majina ya Kiswahili ya viumbe hai kama wanyama yalitumia viambishi awali vipatanishi vya nomino kutoka katika ngeli ya 10 ambayo ni ngeli ya majina ya wanyama katika Luganda.

Kwa mujibu wa ngeli hii, majina ya ngeli hii yamo katika wingi na hujumuisha majina ya wanyama kama mbwa, paka, kuku na kadhalika. Majina haya huchukua mofu dhahania ya wingi ila maumbo ya upatanishi ndiyo yanayojitokeza katika tungo kuwakilisha kanuni ya umilikifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Matumizi ya kanuni hii

yalidhihirishwa kwa kutumia kiambishi awali kipatanishi [zi] badala ya kipatanishi cha Kiswahili sanifu [wa] kama katika (a na b). Uhamishaji huu wa maumbo ya nomino ya ngeli ya 10 ya Luganda na kuyaambisha katika nomino za ngeli ya Kiswahili yaliathiri usanifu wa Kiswahili sanifu.

Aidha, wanafunzi walitumia maumbo ya awali ya mofolojia na maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Data Na (6.4) inadhahirisha athari za mwingiliano katika tungo za wanafunzi. (6.4)

Athari za Luganda kwa Kiswahili Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

| | | | |
|--------------------------------|----------------|---------------------------------|------------------|
| <i>Macho gananiuma/ganauma</i> | <i>[ma-ga]</i> | Macha yananiuma /yanauma | [Ø/ji-ma] |
| <i>[li-ma]</i> | | | [li-ya] |
| <i>[li-ga]</i> | | | |
| <i>Erriso linuuma</i> | | | |
| <i>Amaaso ganuma</i> | | | |

Wanafunzi walitumia viambishi awali vipatanishi vya nomino ngeli vya wingi wa ngeli ya 6 [li-ga] katika matumizi ya nomino ambazo zilijitokeza katika nomino hii kwa sababu kiupatanishi wao hutumia kiambishi kipatanishi cha kisintaksia [ga]. Matumizi haya yaliathiri usarufi na usanifu wa kimofosintaksia wa kanuni ya kimofolojia ya uambishaji ya Kiswahili sanifu.

Mwingiliano na athari nyingine uliyojitokeza katika tungo ni ya kuhamisha na kujumlisha matumizi ya maumbo ya Luganda na Kiswahili kinyume chake bilia kutambua kuhusu utofauti wa maumbo ya kiupatanishi ya lugha na utofauti wa sheria na kanuni za matumizi ya maumbo msingi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na Unganifu ya Chomsky (1981) kama inavyojitokeza katika data Na.(6.5):

Athari za Luganda kwa Kiswahili Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

| | | |
|------------------------------------|----------------|-------------------------|
| a) <i>Mupolisi alikuja hapa</i> | <i>[mu-a]</i> | Ø-polisi alikuja hapa |
| <i>Omupoolisi yaze wano</i> | | |
| b) <i>Wapolisi walikuja hapa</i> | <i>[wa-wa]</i> | Mapolisi walikuja hapa |
| c) <i>Waaskari wamekamata mutu</i> | <i>[wa-wa]</i> | Maaskari wamemshika mtu |
| <i>Abaserikali bakute omuntu</i> | | |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi nyanjani

Wanafunzi walitumia majina ya ngeli ya kwanza na pili ya wafanyakazi ambayo hubeba idadi ya umoja kapa na wingi kuchukua kiambishi awali [ma-] kuzingatia muundo wa uambishaji wa Luganda. Wengine waliambisha kiambishi cha wingi [wa-] mwanzoni kuwakilisha wingi wa nomino husika na hivyo kuathiri usanifu wa matumizi ya nomino hizi kimofosintaksia. Maumbo haya ya kimofolojia ambayo uamilifu wake hujitokeza katika sintaksia ya Luganda yalitumika katika Kiswahili na hivyo kuathiri mofosintaksia ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu.

Kwa kuongezea, athari za uhamishaji wa maumbo ya umoja na wingi ya upatanishi wa kisarufi ya Luganda katika Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika Data Na. (6.6)

| <i>Athari za Luganda kwa Kiswahili</i> | | <i>Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu</i> | |
|--|---------|--|--------|
| a) <i>Mukate gumeisha jokoni</i> | [mu-gu] | Mkate umekwisha jikoni | [m- u] |
| b) <i>Miti gimekatwa</i> | [mi-gi] | Miti imekatwa | [mi-i] |
| <i>Emiti gisaliddwa</i> | | | |
| c) <i>Mugulu gunaluma</i> | [mu-gu] | Mguu unauma/ unaniuma | [m-u] |
| <i>Okugulu gunnuma</i> | | | |
| d) <i>Maguu gananiuma</i> | [ma-ga] | Miguu inaniuma | [mi-i] |
| <i>Amagulu gannuma</i> | | | |

Asili: uchanganuzi wa data za mijarabu ya kisarufi

Mwingiliano wa kutumia maumbo ya kimofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya nomino za Kiswahili kudhihirisha umilikifu na unganifu uliathiri usanifu wa Kiswahili sanifu. Wanafunzi walitumia maumbo ya kimofosintaksia ya viambishi vipatanishi vya nomino kwa umoja na wingi. Matumizi haya yalizingatia maumbo ya awali ya mofolojia na maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu na kuathiri usahihi wa matumizi ya mofu mwafaka za kisintaksia za Kiswahili sanifu.

Aidha, wanafunzi walitumia mbinu ya ujumlishaji wa kutumia viambishi vya wingi vya Kiswahili katika kupachika kwenye nomino za wingi na kutumia maumbo ya viambishi vya kipatanishi cha kisarufi katika matumizi ya Kiswahili hasa katika mazungumzo na maandishi. Matumizi haya yalitokana na kanuni ya ujumlishaji wa kanuni pamoja na kanuni ya uhamishaji wa maumbo ya viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya Luganda na kuviambisha katika maneno mengine ya Kiswahili kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa tungo katika Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na (6.7) kutokana na mijarabu ya kisarufi: (6.7)

.Athari za Luganda kwa Kiswahili**Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu**

- | | | | |
|---|----------------|---------------------------|----------------|
| a) Wamikate <i>gimeletwa</i> Emigaati <i>gireteddwa</i> | <i>[wa-gi]</i> | Mikate imeletwa | <i>[mi-i]</i> |
| b) Wamutoto <i>banayimba</i> <i>Abaana bayiimba</i> | <i>wa-ba]</i> | Wanafunzi wanaimba | <i>[wa-wa]</i> |
| c) Kiongozi <i>kinaongeya</i> | <i>[ki-ki]</i> | Kiongozi anaongea | <i>[ki-wa]</i> |
| d) Kifaru <i>kinakimbia</i> <i>Kifaru Kidduka</i> | <i>[ki-ki]</i> | Kifavu anakimbia | <i>[ki-a]</i> |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya Kisarufi

Wanafunzi ambao L1 ni Luganda walitumia mbinu ya ujumlishaji kutumia viambishi vya Kiswahili visivyo sahihi na uhamishaji wa viambishi vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yaliathiri usanifu wa kanuni za matumizi ya ngeli nomino katika Kiswahili sanifu. Ujumlishaji mwingi ulijitokeza katika ngeli ya 1 na 2 [m-wa/m-wa] pamoja na 3 na 4 [m-mi/u-i] za Kiswahili sanifu. Matumizi haya ya mofu kwa kutozingatia mofu sahihi za kimofolojia mbazo uamilifu wake hujitokeza katika sintaksia uliathiri upatanishi wa kisarufi wa tungo za Kiswahili kimofosintaksia. Matumizi haya yalitokana na umilisi alionao mtumiaji wa lugha husika. Matokeo ya matumizi haya yalitokana na utofauti wa sheria za kiasili za Luganda na Kiswahili sanifu. Hali ambayo inaendana na mihimili wa sarufi bia wa nadharia ya Chomsky (1981) unaeleza kuwa huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo, yaani kuna vigezo vinavyozitofautisha lugha.

Aidha katika kutumia viambishi awali na virejeshi, wanafunzi walidhihirisha matumizi ya viambishi vya wingi vya ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data (6.8) kutokana na mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi katika tungo.

- | | |
|--|--|
| a) Wapolisi walibakamata <i>waizi</i> <i>[wa-ba]</i> <i>[/a/-i-e/]</i> Abapoliisi <i>babakwaata ababbi</i> <i>[Ma,-ba- na e-]</i> | Mapolisi waliwakamata wezi |
| b) Wadaktari <i>balitibu sisi</i> <i>[wa-ba]</i> <i>Abasawo batujjanjabye</i> | Madaktari walitutibu <i>[wa-tu]</i> |
| c) Leta vintu <i>mubiingize</i> ndani <i>[mu-, bi]</i> <i>Mureete abintu mubiyingize munda</i> | Leta vitu m-viingize ndani <i>[m-vi]</i> |

Data hii inadhihirisha wanafunzi kutumia viambishi vya ngeli katika tungo ni matumizi ya viambishi awali vipatanishi virejeshi vya nomino katika tungo. Viambishi hivi viliwekwa

nyuma ya kitenzi kuwakilisha nomino kuu. Hata hivyo viambishi vilivyotumika vilikuwa viambishi vya maumbo ya kimofosintaksia ya Luganda. Wanafunzi walitumia kiambishi ngeli cha ngeli ya pili [ba-] kama ilivyo katika [d na e]. Wanafunzi hawa pia walikosa kutambua kanuni ya kimofonolojia inayotokea katika maneno yanayoathirika na uambishaji wa viambishi vipatanishi kama vile [waizi] ambapo fonimi irabu [a-i] huunganika na kuunda fonimu mpya /-e-/ kama katika [a]. kwa mfano katika a) *walibakamata* badala ya waliwakamata; *mubiingize* badala ya *mviingize* katika (c) na mwisho udondoshaji wa viambishi virejeshi vya Kiswahili sanifu. Hali hii inatokana na kanuni ya matumizi na maumbo ya viambishi awali vipatanishi katika tungo za Luganda. Matumizi haya ya mofimu za kimofosintaksia za Luganda yaliathiri kanuni ya matumizi ya ngeli nomino katika Kiswahili sanifu kutokana na kuepukana na kutumia sifa bainifu za viambishi virejeshi, kutozingatia kanuni za kimofonolojia, udondoshaji wa viambishi virejeshi nafsi na kuhamisha maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yalikiuka kanuni ya umilikifu na Unganifu wa mofimu za kimofosintaksia za Luganda na Kiswahili sanifu. ukiukaji huu ulisababisha athari za mwingiliano wa mofu za kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Kwa mujibu wa data za utafiti huu kuhusu msingi wa uainishaji wa ngeli, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huanisha nomino zake kwa kuzingatia msingi wa kanuni ya kimofolojia ya uambishaji wa maneno katika tungo. Nomino katika Luganda na Kiswahili sanifu ziliainishwa na kutumiwa kutokana na sifa za kimofolojia za nomino kuu. Kutokana na mwingiliano wa kanuni hii, wanafunzi wa Kiswahili sanifu ambao L1 ni Luganda waliweza kutumia maumbo ya kofonolojia ya Luganda. Aidha, kwa kutumia viambishi vya umoja au wingi, kuhamisha viambishi vya kundi nomino moja na kuvitumia katika ngeli nyingine, kutozingatia mifanyiko ya kimofonolojia, kutumia viambishi virejeshi vya nomino vya Luganda badala ya viambishi virejeshi vya Kiswahili na kujumlisha kanuni ya umoja kwa kutumia viambishi vya Kiswahili visivyofaa katika nomino kuu katika tungo. Hivyo kuathiri usanifu wa Kiswahili sanifu kitahajia, kimaendelezo, kiidadi na kiupatanishi wa kisarufi (jinsi ya kisarufi). Hali hii ilitokana na tofauti za kimaumbo za viambishi awali msingi vya ngeli nomino kwa umoja na wingi, viambishi awali vya upatanishi wa kisarufi wa nomino kuu kisintaksia, kanuni tofauti za mifanyiko, na utaratibu wa mpangilio wa ngeli nomino za Luganda na Kiswahili sanifu kisintaksia. Athari hii ya kimaumbo inaendana na mihimili ya usarufi bia na upatanishi ambayo inashikilia kuwa kanuni zilezile za kimofosintaksia

hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo.

Matokeo haya yanashabihiana na yale ya Obara, (2014) ambaye katika utafiti wake alitambua mwingiliano na athari za kanuni ya kimofolojia ya uambishaji wa maneno katika ngeli baina ya Egekusii na Kiswahili sanifu. Katika utafiti wake alitambua kuwa katika uainishaji wa ngeli kimofolojia, maneno mengi ya Egekusii ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili huainishwa katika ngeli tofauti. Hata hivyo, wazungumzaji wa Egekusii hufanya makosa ya kuhamisha kanuni za uambishaji wa L1 katika Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu ulidhihirisha athari za mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya kimofolojia ya uambishaji wa nomino baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kazi ya Kirabi (2015) ambayo inakubaliana na Selinker, (1969) akielezea kuwa miongoni mwa mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo inachanganua matatizo katika matumizi ya lugha, uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza husababisha ukiukaji wa kanuni za lugha ya pili na kusababisha lugha kadirifu isiyo sanifu. Utafiti huu ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, hata hivyo uhamishaji wa maumbo umechangia pakubwa katika ukiukaji wa kanuni za matumizi ya lugha ya Kiswahili kutokana na upekee wa lugha hizi mbi li tofauti.

Kuhususia na mjadala wa athari za matumizi ya maumbo za nomino, wakijibu swali la kwanini wanafunzi hujipata wakitumia maumbo ya Luganda au kujumlisha maumbo katika matumizi ya Kiswahili sanifu, Mwanafunzi 7 alieleza kuwa;

“....Wakati mwingine ni vigumu kutambua maumbo kamili. Kwa sababu baadhi ya maumbo ya Luganda hufanana na ya Kiswahili, wanafunzi huamua kukopa na kutumia maumbo ya Luganda katika Kiswahili sanifu”.

Wanafunzi walieleza kuwa uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya nomino ndiyo yaliyoathiri mofosintaksia ya tungo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, walieleza kuwa, athari za matumizi ya maumbo ya Luganda katika Kiswahili hutokana na mpangilio tofauti wa ngeli na aina za maneno au nomino inayotumika katika tungo kuwakilisha idadi ya umoja na wingi. Aidha, matokeo yalibainisha kuwa tofauti hizi ndizo zilizoathiri jinsi ya upatanishi wa kisarufi wa nomino kimrejeosabaki kuwakilisha umilikifu na ufungamanisho wa neno kuu katika virai husika kama ilivyoelezwa na mwanafunzi 48, aliyeungwa mkono na mwanafunzi 12, 19 na 47. Alieleza kuwa;

“....Mwalimu ni kwa sababu ya mfanano wa sifa za ngeli za Luganda. wanafunzi hubahatisha na kutumia maumbo yanayoweza kuendana na neno ama sentensi.”

Aidha, mwanafunzi wa 23, alifahamisha utafiti huu kuwa,

“...wakati mwingine wanafunzi wanahamisha au kufasiri maana au ya nomino au sentensi kutoka Kiswahili hadi Luganda na hivyo kutumia maumbo ambayo yanaendana na maumbo ya matumizi ya Luganda.

Matokeo haya yanadhihirisha uwiano na tofauti za lugha za nasaba moja kutokana na mihimili ya usarufi bia na upatanifu wa nadharia ya Umilikifu na ufungamanisho (Chomsky, 1981) ambayo hudhihirisha hali ya vipashio fulani vya kisarufi kutawala na kumiliki vipashio vingine katika tungo. Matokeo yalidhihirisha wanafunzi kuhamisha, kuchanganya, kubadilisha, kuongeza na kujumlisha kanuni za kimofosintaksia za matumizi ya ngeli katika maandishi na mazungumzo ya Kiswahili sanifu.

6.1.1.3 Kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofosintaksia (Kanuni ya Urejeshi)

Data ya makatabani kutokana na Kiyinikibi (2013: 2021), Namugala (2014), Besha (1996) na Kirabi, (2015) ilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hudhihirisha mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofosinraksia. Kanuni hii inashikilia kuwa: Uambishaji unaohusika katika maneno katika utungo kimofosintaksia lazima ubebe sifa za kimofosintaksia kutegemea vibainishi awali au viambishi awali vinavyopachikwa kwenye maneno na aina za maneno katika tungo. Kulingana na kanuni hii, nomino zote zilizo na viambishi awali vya umoja na wingi vinavyofanana huwekwa katika kundi moja ambalo huitwa ngeli. Pia, viambishi ambavyo havina maumbo ya umoja au wingi au kinyume kuwekwa katika kundi lake (Mgulu, 1999; Kiyinikibi, 2021; Habwe & Karanja, 2004; Katamba, 2003 na Besha, 1996). Data katika majedwali Na (4.1 Uk. 71; 4.2 Uk. 76; 4.5 Uk. 84; 4.7 Uk. 89) na Na.5.4, Uk. 191) na inabainisha uhusiano wa viambishi vya mofolojia na sintaksia vinavyopachikwa kwenye maneno na aina za maneno katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino kutawala maneno mengine katika tungo.

Aidha, Matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya kutambua matumizi ya kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofosintaksia, wanafunzi walipoulizwa kupigia mistari maumbo ya viambishi vya ngeli vinavyoonyesha sifa za kisarufi zinazodhihirisha maumbo ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika tungo kutoka katika tungo za sentensi. Wanafunzi waliweza kutambua maumbo ya nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu katika sentensi walizotunga. Hata hivyo ilibainika

mwingiliano na athari za maumbo ya uainishaji wa Luganda katika maumbo yaliyobainishwa na wanafunzi. Kwa kutumia data za majedwali ya ngeli kutoka katokana na Leah & Sseguya (2015) na Sakwa, T., Masaba, V. Kajoka, J. na Gashengeshi, A. (2013), wanafunzi waliulizwa kutambua uwiano na tofauti katika viambishi vya uainishaji wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, kutokana na Uainishaji wa nomino katika ngeli, wanafunzi waliulizwa kubainisha mwingiliano wa uainishaji wa ngeli katika Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo ya data katika jedwali Na.(6.1) ilidhihirisha kufanana kwa maumbo ya uainishaji na maumbo ya uainishaji na Jedwali Na. (6.2) mwingiliano wa uainishaji na maumbo ya uainishaji ambayo ilidhihirisha mihimili ya ubia na upatanifu wa matumizi ya kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofosintaksia.

Matokeo ya uchanganuzi wa athari za mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofosintaksia kwa kutumia kifaa cha kudondoa data na mwongozo wa wenye sifa za kimofosintaksia kutokana na orodhahakiki ya matokeo ya kutunga sentensi kutumia viambishi ngeli kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo, utafiti huu uligundua athari za ukopaji na uhamishaji wa maumbo ya viambishi vya ngeli, ujumlishaji wa kanuni ya uambishaji viambishi ngeli kama inavyojitokeza katika data Na.(6.9) kutokana na kutunga sentensi kuonyesha sifa za kimofosintaksia za nomino na maneno mengine katika tungo.

- a) *Mbuzi emepelekwa malishoni kula nyasi Mbuzi amepelekwa malishoni [en-a]*
Embuzi etwaliddwa mukisaawe kulya abusubi
- b) *Mbuzi imepelekwa malishoni kula nyasi Mbuzi amepelekwa malishoni [i-a]*
- c) *Mbuzi zimepelekwa malishoni kula nyasi Mbuzi wamepelekwa malishoni [zi-wa]*
- d) *Embuzi zitwaliddwa kutale okulya omuddoi*

Asili: Data kutokana na mijarabu nyanjani

Data Na (6.9) ilidhihirisha athari za ukopaji na uhamishaji wa maumbo ya kimofosintaksia za uainishaji wa viambishi vya ngeli vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi 43/54 ambao L1 ni Luganda walitumia kanuni za uainishaji wa nomino za majina ya wanyama ambayo yameainishwa katika ngeli 10 za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Wanafunzi 4 walijumlisha kanuni ya uambishaji na 6 walionyesha usahihi katika matumizi ya kanuni hii ya uainishaji.

Matumizi haya yalikiuka mhimili wa upatanishi wa nadharia ya umilikifu na unganifu wa nomino kutawala maneno mengine katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu na

maneno mengine katika tungo. hali hii ilitokana na kuwa majina ya wanyama katika Luganda hayachukui viambishi awali vya umoja ila huchukua maumbo ya upatanishi wa kisarufi kuwakilisha idadi ya wingi. Maumbo haya hubakia katika maumbo yake ya umoja ya [N], [en], [em] kuwakilisha idadi ya umoja. Maumbo haya ya ngeli ya tisa hutumia sauti nazali [N], [en], [em] na majina yanayotumia konsonanti mbili kwa ajili ya kutilia mkazo sauti.

Majina haya yanapowekwa katika wingi huchukua kiambishi kipatanishi [zi-]. Kwa kutumia kanuni hii ya ngeli ya 9 na 10, wanafunzi ambao L1 ni Luganda walihamisha maumbo ya ngeli ya 9 na 10 ya Luganda katika matumizi ya nomino za majina ya viumbe wanyama ambayo yameainishwa katika ngeli ya 1 na 2 ya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yaliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kwa sababu upatanishi wa sarufi wa nomino hizi na maneno mengine katika tungo yalipotoshwa na kuharibu sifa za Kiswahili sanifu ya kudhihirisha umilikifu na unganifu wa nomino kutawala maumbo ya maneno mengine katika tungo.

Mwingiliano na athari nyingine iliyojitokeza ni ile ya kuhamisha viambishi vipatanishi vya ngeli za Luganda katika matumizi ya nomino ambamo nomino hizo zimeainishwa. Hali hii ilifanywa kwa kuzingatia maumbo na viambishi vipatanishi vya uainishaji. Matokeo ya matumizi Na. (6.10) ya wanafunzi katika mijarabu ilibaini kuwa, kimatumizi wanafunzi walihamisha maana ya nomino kutoka Kiswahili hadi Luganda au kufasiri au kutafsiri nomino na kuianisha na ngeli za Luganda. Kutokana na mkakati huu wa matumizi ya nomino. Wanafunzi walitumia viambishi awali vipatanishi vya nomino ngeli vya wingi wa ngeli za Luganda katika matumizi ya nomino za Kiswahili sanifu ambazo zimeainishwa katika jozi moja na Luganda. Data Na. (6.10) inadhihirisha athari za mwingiliano kutokana na mijarabu ya wanafunzi.

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili Maumbo ya Kiswahili

a) *Macho gananiuma/ganauma* [ma-ga] **Macho yananiuma /yanauma** [Ø/ji-ma]

Amaaso gaannuma

[li-ma]

[li-ya]

[li-ga]

b) *Mkate gumeretwa* Mkate **umeletwa** [gu-u]

Omugaati gureteddwa

c) *Mikate gimeletwa* Mikate **imeletwa** [gi-i]

Emigaati gireteddwa

Asili: Data kutokana na mijarabu ya Kisarufi ya wanafunzi

Matokeo ya matumizi Na. (6.10) ya wanafunzi katika mijarabu ilibaini kuwa, kimatumizi wanafunzi waliamisha maumbo ya viambishi vya uainishaji wa nomino katika ngeli kimofosintaksia kutoka Luganda hadi Kiswahili sanifu. Umbo la nomino [*macho*] ni umbo la ngeli ya 6 ya Luganda ambayo hupatikana katika jozi la ngeli ya 5 na 6 ya [*li-ma*] ambamo nomino hii imeanishwa kimofolojia. Kisemantiki, nomino [*macho*] ni [*maaso*] katika Luganda na umoja wake ni [*liiso/jicho*]. Kisintaksia, nomino hii imeanishwa katika ngeli ya [*li-ga*]. Kwa hiyo, matumizi ya nomino hii katika tungo za Luganda kimofosintaksia hutumia kiambishi awali kipatanishi cha nomino kuu [*ga*] kudhihirisha umilikifu na unganifu wa mofu za kimofolojia ambazo uamilifu wake hujitokeza katika sintaksia. Kutokana na kanuni hii ya kimofokisintaksia, wanafunzi waliamisha umbo la upatanishi wa kisarufi [*ga*] la Luganda na kulitumia katika umbo la kiupatanishi wa kisarufi wa nomino [*macho*] katika Kiswahili sanifu. Hali hii ilijitokeza hasa mwanafunzi aliposhindwa kutambua viambishi vipatanishi vya nomino na mahali ambamo nomino hiyo imeainishwa. Katika (b na c) wanafunzi wamehamisha viambishi awali vya upatanishi wa kisarufi wa ngeli ya 3 na 4 ambamo nomino hizi zimeanishwa kwa mujibu wa ujozi wa ngeli ya Luganda na Kiswahili. Matumizi haya ya viambishi vipatanishi vya Luganda [*gu-gi*] badala ya viambishi vipatanishi vya Kiswahili sanifu [*u-i*] vimeathiri sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu kimaendelezo na kiupatanishi kutegemea uainishaji wa ngeli za Kiswahili sanifu kisintaksia.

Matumizi ya nomino bila kuzingatia uainishaji wa kimofosintaksia wa viambishi ngeli ambamo nomino husika zimeanishwa kuwakilisha upatanishi wa kisarufi, idadi ya umoja na wingi na ngeli katika utungo kianafora na katafora uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali hii ilitokana na kuwa viambishi vyote vinavyotumiwa katika umbo nomino hutawala viambishi vyote vinavyotumiwa katika tungo kama viwakilishi jirejee. Kwa hiyo matumizi yasipozingatia maumbo na utaratibu wa mpangilio ambamo nomino imeainishwa, mpangilio wa umantiki wa maumbo ya mofu za ngeli na idadi au jinsia, kimofolojia na kisintaksia kuwakilisha idadi ya umoja na wingi pamoja na usarufi hupotoka.

Uainishaji wa ngeli huhusika na upangaji wa ngeli nomino zilizo na mianzo tofauti pamoja kwa kufuata mantiki ya upatanisho wa kisarufi. kwa hiyo matumizi yasio sahihi huwa hayaonyeshi uainishaji ngeli za nomino pamoja na mahusiano ya viambishi nomino na maneno mengine katika tungo. Matokeo haya yanaendana na Mhimili ya sifa za sarufi bia na upatanishi ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya

lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Aidha utafiti huu ulitambua kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuonyesha kufanana katika matumizi ya kanuni ya uainishaji wa viambishi vya ngeli nomino, kuna tofauti za kimaumbo na za kimpangilio ambao unajitokeza na kudhihirisha kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye vipashio vya kimofosintaksia tofauti.

Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kuhusu jinsi kanuni ya uainishaji wa viambishi ngeli unavyoingiliana na kuathiri matumizi ya vipashio, utafiti huu ulitambua kuwa matumizi ya nomino katika tungo hutegemea nomino kama neno kuu ambalo huathiri uhusiano wa kimofosintaksia wa nomino na maneno mengine katika tungo. Hata hivyo, Licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja zinazotumia kanuni hii ya uainishaji wa maumbo ya viambishi vya ngeli kubeba sifa za kimofosintaksia, lugha hizi ni lugha mbili zinazodhihirisha tofauti za kimaumbo na kimpangilio katika matumizi ya kanuni hii. Hali ambayo husababisha athari za mwingiliano wa matumizi ya maumbo ya viambishi vya uainishaji wa ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu. Wanafunzi wakijadili juu ya sababu ya wanafunzi kutumia maumbo ya viambishi vya uainishaji wa nomino ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo, Mwanafunzi 37 alieleza kuwa;

“Mara nyingi ukitumia viambishi vya ngeli ambavyo havionyeshi uhusiano unaathiri sarufi ya lugha. kwa hiyo, wanafunzi huhamisha maumbo ya Luganda kwa kiswahili kwa sabab wanayafahamu vyema kuliko ya Kiswahili sanifu.

Aidha, mwanafunzi 5 alifafanua kuwa;

“kufanana kwa maumbo na maana ya nomino husababisha mwanafunzi kutumia maumbo ya uainishaji wa nomino katika nge ya Luganda katika Kiswahili sanifu.”

Mwanafunzi 50 naye katika kufafanua sababu za athari za mwingiliano wa kanuni hii naeleza kuwa,

“Maumbo ya uainishaji wa ngeli ni mgumu na unasumbua, sisi tulitumia mfumo wa uainishaji wa mofolojia katika kujifunza ngeli lakini sasa mfumo wa kimofosintaksia. Mwanafunzi anastahili kujua nomino na maumbo yake, kisha atambua maumbo ya kisintaksia yanayohusiana na nomino. Kwa hiyo, mwanafunzi hutafsiri nomino ya Kiswahili kwa Luganda au kutumia maumbo ya kuainisha nomino ngeli za Luganda zinazokaribiana na za Kiswahili katika Kiswahili sanifu.”

Katika mijadala, wanafunzi walieleza kuwa,

“Wanafunzi walihamisha maumbo ya kimofolojia na ya kisintaksia ya Luganda katika tungo za Kiswahili sanifu. Umbo la (a) ni umbo la kimofolojia la ngeli ya 9 katika Luganda na umbo la [i] katika (b) ni umbo la kifonolojia baina ya Luganda na Kiswahili kimaandishi ambapo wanafunzi badala kuandika /e/ wao huandika /i/ au kinyume na mwisho umbo [zi/ ni umbo la kisintaksia la nomino za wanyama katika ngeli ya 10.”

Walipoulizwa kutaja athari za mwingiliano, matokeo ya mijadala ilibaini kwamba, kutokana na uainishaji wa ngeli kimaumbo, wanafunzi waliweza kuathiri Kiswahili sanifu kwa kuhamisha viambishi vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali hii iliathiri usanifu wa Kiswahili sanifu kimatamshi na hata kisarufi.

Aidha, mijadala ya wanafunzi kuhusiana na kutambua maumbo ya uainishaji wa ngeli za nimno za Luganda na Kiswahili zinazolingiana na kufanana, wanafunzi waliweza kutambua maumbo katika data ya jedwali Na.(6.1, Uk. 266) na Na.(6.3 Uk. 338). Waliweza kubaini kuwepo kwa ukuruba mkubwa wa kimaumbo hata ingawa aina za nomino zinazohusika hutofautiana. Pia, ilitambulika kuwa ngeli hufanana au kukaribiana kufanana. Kijoji, ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu zimepangwa katika jozi ambapo ngeli kutoka 1 hadi 10 ni jozi ambazo zinafanua uainishaji wa nomino kimaumbo kwa umoja na wingi. Wanafunzi waliweza pia kutambua kuwa Luganda ina zaidi ya jozi ya 13 na 14 ambayo Kiswahili hakitumii. Matokeo ya tathimini ya mijadala wa wanafunzi ilibainisha kuwa kufanana na kutofautiana kwa viambishi vya kuainisha ngeli nomino baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ndio iliyokuwa nguzo iliyosababisha athari za mwingiliano kwa vipashio vya mofosintaksia katika Kiswahili sanifu kama ilivyondhihirishwa kutokana na kazi za Mulei, Amukowa & Ambuyo (2021), Katamba (2003), Namugala (2014), Assimwe (2016), Mgullu (1999) na Kirabi (2015).

Barno, (2013), Chebet, (2016), Egara, (2016) na Chepkwony, (2012) katika tafiti zao walidhihirisha kuwa uwiano na tofauti za matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu kimofosintaksia husababisha mwingiliano katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Suala ambalo limejitokeza katika utafiti huu. aidha, matokeo haya yanashabihiana na maelezo ya Habwe & Karanja, (2004) na Mgullu, (1999) kuwa ukiukaji wa kutumia viambishi visivyoiweka nomino katika kundi ambamo nomino imeanishwa huweza kuharibu usanifu au usahihi wa matumizi ya nomino husika. Aidha, Kisakwah, (2014) na Obara, (2014) wanaeleza juu ya athari za kanuni za uainishaji wa viambishi ngeli

katika maneno kubeba sifa za kimofosintaksia ambapo wanafunzi walifanya makosa ya kisarufi katika tungo kwa kuhamisha maumbo ya uainishaji wa nomino zinazofanana za lugha ya kwanza katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Aidha, utafiti huu ulitathmini na kueleza mwingiliano wa kanuni na athari katika uhamishaji wa matumizi ya kanuni hii baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Utafiti huu uligundua kuwa kanuni ya uainishaji na uambishaji wa viambishi ngeli ambavyo hubebe sifa za kimofosintaksia za maneno ya kisarufi yenye sifa za upatanisho wa kisarufi zinazotokana na nomino kama neno kuu baina ya Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana. Ilibainika kuwa Uwiano na tofauti za kanuni hii ya uainishaji wa viambishi ngeli katika maneno kubeba sifa za kimofintaksia ulikiukwa katika matumizi miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Ukiukaji wa matumizi ulisababisha uhamishaji wa viambishi vya uainishaji wa nomino vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. uhamishaji huu ulisababisha athari za mofosintaksia katika Kiswahili sanifu ambapo uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo hukuzingatiwa.

6.1.1.4. Kanuni ya sarufi miundo

Kanuni hii inashikilia kuwa mpangilio wa maumbo ya kimofolojia katika kategoria ya maneno huathiri vipashio na umbo linalofuata katika muundo wa utungo. Vile vile kanuni hii inadai kuwa upatanifu wa kisarufi katika utungo hutawaliwa na vipashio vya kimofosintaksia na vipashio hivyo huathiriana ambapo kipashio cha kwanza hutegemea sana kipashio cha pili ili kuleta maana. Upatanifu ni uhusiano wa kisarufi ambapo neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo (TUKI, 1990). Kanuni ya sarufi miundo ni Kanuni ya upatanifu ambayo hutegemea nomino kama neno kuu.

Kanuni hii ni Maneno yaliyo karibu na neno kuu katika tungo huweza kubainisha uhusiano wa ngeli, nafsi na idadi ya umoja na wingi wa maneno mengine katika tungo. Upatanishi huu ni ule wa karibu na neno kuu. Kanuni hii ilielezwa na Nordquist (2020). Kanuni hii ni ya kisintaksia ambapo neno kuu (Nomino) hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo kuwakilisha ngeli, idadi na upatanishi wa kisarufi. Uhusiano wa neno kuu katika tungo ni uhusiano wa kimofosintaksia ambao hutegemea viambishi vya uainishaji wa neno kuu kuathiri maneno mengine katika tungo. Uhusiano huu ni wa umilikifu wa karibu na neno. Data Na. (5.9, Uk. 145) inadhihirisha matumizi ya kanuni ya sarufi miundo ambayo kwayo inadhihirisha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo.

Matokeo ya uchanganuzi wa maandishi ya wanafunzi katika mijarabu ya kisarufi kuonyesha miundo ya kisarufi ya kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na maneno mengine katika sentensi ulidhihirisha mwingiliano na athari za matumizi ya kanuni ya sarufi miundo. Maumbo yaliyotumika na wanafunzi katika tungo hayakuonyesha mahusiano ya kuathiri maneno mengine kinafora na kitafora wala kuonyesha nomino kuu kutawala maneno mengine katika tungo au kuathiriana kimrejeo sabaki kama inavyojitokeza katika data (6.11):

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili Maumbo sanifu ya Kiswahili

- a) *Ng'ombe zimeletwa nyumbani [n-zi]* *Ng'ombe wameletwa nyumbani [Ø-wa]*
- b) *Paka zimekamata panya [n-zi]* *Paka wamekamata panya [Ø-wa]*
- c) *Meno gananiuma [ma-ga]* *Meno yananiuma [ma-ya]*
- d) *Muti gumevunjika [mu-gu]* *Mti umeanguka [M-u]*
(*Omuti gumenyese*)
- e) *Miti gimeanguka [mi-gi]* *miti imeanguka [mi-i]* (*emiti giggudde*)
- f) *Kiongozi kinaongeya [ki-ki]* *Kiongozi anaongea [ki-wa]*
- g) *Kifaru kinakimbia [ki-ki]* *Kifavu anakimbia [ki-a]*
- h) *Mupolisi alikuja hapa [mu-a]* *Ø-polisi alikuja hapa*
- i) *Wapolisi walikuja hapa [wa-wa]* *Ø-polisi walikuja hapa*
- j) *Musirikale amekamata muntu [mu-a/ba]* *Askari amekamata mtu*
Omusirikale akutte omuntu
- k) *Waaskari wamekamata mutu [wa-wa]* *Ø-askari wamemshika mtu*

Asili: Data kutokana mijarabu ya kisarufi

Data Na. (6.11) ilibainisha athari za mwingiliano katika ngeli za 1 na 2, 3 na 4, ngeli ya 5 na 6, ngeli ya 7 na 8 na ngeli ya 9 na 10. Data [a, b, f na g] zinadhihirisha uhamishaji viambishi vya ngeli za 9 na 10 [en-zi] na 7 na 8 [Ki-bi] ya Luganda katika matumizi ya nomino za Kiswahili bila kuzingatia kanuni ya usemantiki iliyotumika kuzianisha nomino hizi katika Kiswahili sanifu ambapo [a na b] ni ngeli ya [i-zi] kiupatanishi na kimofolojia *ng'ombe* huchukua umbo dhahania la [Ø] na wingi wake kuchukua [i-]. Data za tungo [c, d, e, h, j] zimehamisha maumbo ya upatanshi wa kisarufi ya Luganda kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa Kiswahili sanifu. Mwisho, viambishi vya [k na i-] zimetumika kwa kutumia kanuni ya ujumlishaji wa maumbo ya Luganda na Kiswahili sanifu. Hata hivyo, ujumlishaji huu ulitokana na maumbo ya Luganda ya wingi hasa umbo [ba] lililolinganishwa na Kiswahili sanifu. Matumizi haya yalitokana na ukuruba wa maumbo ya vipatanishi vya Kisarufi vya Luganda na Kiswahili sanifu kuwakilisha uhusiano wa nomino kuu na maneno

mengine katika tungo virai kianafora na kiatafora Matumizi ya viambishi hivi bila kuzingatia sifa za uambishaji wa viambishi vipatanishi vya kisarufi vya Kiswahili sanifu katika virai nomino uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu upatanishi wa kisarufi wa kisintaksia wa neno kuu kutawala maumbo ya kimofolojia ya maneno mengine kutegemea maumbo ya kimofosintaksia ya Kiswahili sanifu na ukaribu wa maneno mengine katika tungo hayakuzingatiwa.

Athari za mwingiliano mwingine uliodhihirika katika mijarabu ya tungo za wanafunzi katika kutumia nomino katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu ni ule wa kuchanganya, kuhamisha, kudondosha, kufananisha maumbo ya viambishi yambwa katika Kundi tenzi kuwakilisha upatanifu wa kisarufi. ya Luganda na Kiswahili sanifu na kutumia katika tungo za Kiswahili sanifu. Data Na. (6.12).

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

- a) Paka *zimemkamata panya* [Ø] Paka **wamewakamata panya** [-wa-]
- b) Waaskari *wameshikaa mutu* [Ø] Ø-askari **wamemshika mtu** [-m-]
- c) **Macho ganauma mimi** [Ø] **Macho yanauma** [-tu-]
- d) Wapolisi *walibakamata waizi* [-ba-] Ø-polisi **waliwakamata wezi** [-wa-]
- e) Wadaktari *balitibu sisi* [Ø] Ø-daktari **walitutibu** [-tu-]
Abasawo bajjanjabye ffe
- f) Leta vitu *mubiingize ndani* [mu-, -bi-] Leta vitu **m-viingize ndani** [m-vi-]

[Ø]- Kudondosha kwa kiambishi yambwa katika KT

Asili: Data kutokana mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi

Data Na. (6.12) inadhihirisha athari za mwingiliano wa upatanishi wa kisarufi wa matumizi ya viambishi yambwa katika KT kuwakilisha upatanishi wa kisarufi. Yambwa ni nomino na huweza pia kuwakilishwa na mofimu za kuwakilisha idadi ya umoja na wingi wa nomino katika tungo. Luganda na Kiswahili sanifu hutumia yambwa kama kipashio cha kimofosintaksia chenye uamilifu wa kisarufi katika KT. Uamilifu wake hujitokeza katika matumizi ya mofimu za upatanishi kuonyesha uhusiano unaorejelea nomino tendwa na tendewa katika KT. Kanuni za matumizi ya viambishi yambwa ni kuwa mofimu hizo huchukua nafasi karibu na mzizi wa kitenzi. Mofimu yambwa zenyewe ni viambishi vipatanishi vya nomino vinavyopachikwa katika kirai tenzi kutegemea nomino kama neno kuu. Viambishi yambwa vinavyopachikwa kwenye KT, hutofautiana kutokana na uainishaji wa nomino katika ngeli mbalimbali. Aidha, katika matumizi, kiambishi hiki huweza kutumia

viambishi ngeli au viwakilishi nafsi kuwakilisha nomino tendwa au nomino tendewa kama ilivyofafanuliwa na (Riedel, 2009, Egara (2016).

Matokeo ya mijarabu ya kisarufi, wanafunzi walitambua kuwa wanafunzi 7/54 ndio waliotumia kanuni hii kwa usahihi, huku wanafunzi 47/54 wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda licha ya kutumia maumbo ya upatanishi wa kisarufi ya Luganda kuwakilisha upatanishi wa tungo za Kiswahili kimofosintaksia, walidondosha viambishi yambwa vipatanishi na kuongeza mwishoni kiwakilishi nafsi ya nomino tendaji au tendwa. Vilevile wanafunzi hawa walihamishi viambishi yambwa vya upatanishi wa kisarufi wa Luganda moja kwa moja katika KT za Kiswahili sanifu. Matokeo haya yanashadidiwa na maelezo ya Mukuthuria, (2004) na Ontieri, (2016) wanaoeleza kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye kanuni na miundo ya kiisimu ambayo ina ukuruba na lugha nyinginezo za Kibantu. Ukuruba baina ya lugha mbili tofauti zenye mtagusano wa muda mrefu, husababisha mwathiriano wa lugha husika kuchukua baadhi ya sifa za vipashio vya kiisimu vya fonolojia, mofolojia na sintaksia kutoka lugha nyingine na kuingiza katika matumizi ya lugha yake. Obara, (2014) na Kisakwah, (2014) ambao walionyesha hali ya uhamishaji wa kanuni za matumizi ya vipashio vya lugha ya kwanza kwa Kiswahili sanifu.

Matokeo ya kanuni hii yanaendana na kanuni ya utawala ambayo huchunguza uhusiano uliopo baina ya neno kuu na maneno mengine katika utungo. Kwa mujibu wa mapitio ya Egara, (2016) na Shabani, (2015), Kanuni hii hushikilia kwamba, maneno katika sentensi lazima yakubaliane na ngeli ambamo nomino husika imeanishwa. Aidha kanuni hii inaendana na nadharia ya utafiti huu ambayo huongozwa na masharti kama ilivyoelezwa na Chomsky, (1981) na Shabani, (2015) wanaoeleza kuwa, elementi inayotawala maneno mengine lazime iwe neno kuu ambalo hutokea kushoto au kulia kutegemea mpangilio wa lugha inayohusika; Pia ili elementi itawale katika tungo, lazima pawe na uhusiano wa moja kwa moja na elementi inayofuata na isiingiliwe na elementi ya tatu; aidha, elementi hutawala elementi nyingine kama tu, elementi zote (yaani tawala na tawaliwa) zinachipukia katika fundo moja na elementi ya kwanza ikiwa ndio neno kuu na kihusishi ndiyo elementi ya pekee inayoweza kutatiza elementi moja kuitawala nyingine.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kushabihiana katika mpangilio wa vipashio kuonyesha uhusiano wa maumbo kujenga utungo ambao ni wa upatanishi wa kisarufi, uhusiano wa vipashio vya mofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu kutofautiana. Matumizi ya kanuni hii miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao

L1 ni Luganda yalidhihirisha athari za mwingiliano wa matumizi ya kipashio cha ngeli cha kimofosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu na kuathiri Kiswahili sanifu. Athari hizi zinatokana na kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha mbili tofauti licha ya kuwa ni lugha za nasaba moja. Matumizi haya hayakukidhi sifa za miundo ya kimofosintaksia ya Kiswahili sanifu ila yalipotumika yaliathiri Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu maumbo yaliyopachikwa kwenye nomino na maneno mengine hayakuonyesha uhusiano wala athari ya umbo la kwanza kuathiri umbo la pili la maneno mengine au kuathiriana kianafora na kiatafora.

6.1.1.5 Kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji

Sauti za lugha zinapotumika katika neno au tungo, mara nyingi huweza kuathiriana na kusababisha msuko wa sauti zinazolingiliana. Kanuni za kifonolojia ni kanuni zinazohusika na matamshi ya mofimu zinazojenga maneno. Kanuni hizi huhusika zaidi na mabadiliko ya matamshi ya mofimu kutokana na ujirani wa mofimu. Ngeli za Luganda na Kiswahili zimeundwa kwa maumbo ya kimofonolojia ambayo matumizi yake yasipozingatiwa kimaandishi na kimazungumzo, sifa za kimofosintaksia za lugha husika huathirika na kupoteza usanifu wake. Kanuni hii inashikilia kuwa: irabu ya kiambishi [mu] hudodoshwa ikifuatiwa na konsonanti halisi kama inavyojitokeza katika data Na. (6.13)

| | <i>Umoja</i> | <i>Wingi</i> |
|----|-------------------------------------|--------------|
| a) | <i>Mu-tu</i> M -toto | Watoto |
| b) | <i>Mu-sichana</i> M -sichana | Wasichana |
| c) | <i>Mu-vulana</i> M -vulana | Wavulana |

Asili: Data kutokana na Mukuthuria, (2004;120) na Ontieri, (2016:8)

| <i>Uainishaji wa vibainishi</i> | <i>Uainishaji bila vibainishi</i> |
|---------------------------------|-----------------------------------|
| a) <i>O-mu-ntu</i> | <i>mu-ntu</i> |
| b) <i>O-mu-wala</i> | <i>Mu-wala</i> |
| c) <i>U-mu-lenzi</i> | <i>Mu-lenzi</i> |

Asili: Katamba, (1993: 2003); Chomi, (2003), Mgullu, (1999)

Mifano ya data hii kutoka maktabani inadhibitishwa na wataalamu Mukuthuria, (2004), Chomi, (2003), Otiende, (2013) na Ontieri, (2016) na mifano ya data Na. (5.13, Uk. 158) kutokana na Katamba, (1993) na Baertlein & Ssekitto, (2014), Mgullu, (1999) na Mutale. & Muwanga, (2009) kuhusu athari za kifonolojia katika mofolojia na sintaksia ya maneno ya Kiswahili na Luganda. Matokeo haya yanadhihirisha ukiukaji wa matumizi ya mofu za

kimofosintaksia ya Kiswahili kudhihirisha umilikifu na Unganifu wa nomino na maneno mengine katika tungo.

Matakeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi katika tungo ulitambua kuwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda waliamisha matamshi ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili, kubadilisha sauti kwa mujibu wa L1, kushindwa kutambua kanuni za kimofosintaksia zinazoongoza baadhi ya maneno na kuyatumia jinsi yalivyo katika tungo za kimofosintaksia za Kiswahili sanifu. Hali hii ilipotosha usahihi wa matumizi ya Kiswahili sanifu kwa sababu sauti zenyewe zilikiukwa kimaandishi na kimatamshi kama inavyojitokeza katika data Na. (6.14).

Matamshi na maandishi

a) Watoto w-[a-i]-ngi walikuja darasani. Watoto w-[e]-ngi walikuja darasani.

b) Mayai m-[a-i]-ngi yameoza. Mayai M-[e]-ngi yameoza.

Ubadilishanaji sauti badala ya [wa]

c) Wapolisi walibakamata w-[a-i]-zi. [-ba-] Mapolisi wali-[wa]-kamata w-[e]-zi [-wa-]

d) Leta vitu [mu]-[bi]-ingize ndani.[mu-, -bi-] Leta vitu [m]-[vi]-ingize ndani [m-vi-]

Kubadilisha matamshi ya viambishi; mofimu [ki-] na kutumia [ch] na [cha] kuandikwa kama [kya], [che] kuandikwa kama [kye]

e) [Kya]-kula chimeiva chilete a]-kula kimeiva kilete [ky-ch]

f) [Chi]-kombe [kye]-usi [chi]-mepasuka [Ki]-kombe [che]usi [ki]-mepasuka.

Kukiuka kanuni ya kudondosha fonimu [-u] inayofuatwa na konsonanti

g) [Mu]-kate [mu]-zuri. MKate [m]-zuri.

h) M [-u]-walimu muzuri. [Mw]-alimu [m]-zuri.

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi

Data Na. (6.13) ilidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya kimofonolojia kwa kuandika na kutumia mofimu ya viambishi vipatanishi vya kimofosintaksia vya Luganda katika tungo za Kiswahili sanifu. Vivumishi vingi vilipokea ukiukaji wa kanuni za kimofosintaksia kama vile katika [a, b, c, na f]. Katika ubadilishanaji wa sauti, wanafunzi 5/54 walidhihirisha matumizi sahihi ya viambishi vipatanishi vya kimofosintaksia. Wanafunzi 49/54 waliamisha mofimu za viambishi vinavyoakaribiana kimaumbo, kimatamshi na kiuainishaji ya Luganda na kuitumia katika Kiswahili sanifu kama katika mfano wa [c-h]. Matumizi haya yalionyesha ukiukaji wa matumizi ya maumbo sahihi na matamshi sahihi ya viambishi vya ngeli nomino ambavyo vimejegwa kimofonolojia kuwakilisha idadi ya umoja na wingi wa nomino

kuegemea sifa za Kiswahili sanifu. Ukiukaji huu ulisababisha athari za kimfosintaksia za tahajia na maendeleo yanayoonyesha matumizi mabaya ya Kiswahili sanifu.

Matokeo ya mijadala ya utokeaji wa ukiukaji wa kanuni ya kimofonolojia ya udondoshaji katika matumizi ya nomino katika ngeli kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino kutawala maneno mengine katika tungo ulidhihirisha athari za mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya kimofonolojia. Matokeo yalithibitisha uhamishaji wa maumbo kama yanavyotamkwa na kuandikwa kutolka Luganda katika matumizi ya Kiswahili. Matokeo haya yalidhibitishwa na mwanafunzi 25 ambaye alieleza kuwa;

Wanafunzi wangi husoma maneno yanayoanza na kiambishi awali {ki} utawasikia wakisema {chi} na unapowaelekeza kuandika maneno hayo huenda wakayaandika kama {kyi} kama katika kikombe ambapo utawasikia wakiandika kama {kyikombe}.

Aidha, mwanafunzi 14 alikubaliana na ufafanuzi wa mwanafunzi 25 akieleza kuwa:

“Kwa sababu matamshi ya Kiswahili yanafanana na yale ya Luganda, sisi hutumia sauti za Luganda katika Kiswahili kwa sababu ya kushindwa kutambua kanuni za kimfosintaksia zinazoongoza baadhi ya maneno yenye sifa za tungo za kimfosintaksia za Kiswahili sanifu.”

Matokeo haya yanashadidiwa na Otiende, (2013) ambaye anaeleza kuwa kuna tofauti kubwa baina ya mifumo wa fonimu za Kiswahili na Kiolusuba huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kiolusuba. Otiende (2013) akikubaliana na Hyman (1975) anaeleza kuwa kila lugha huwa na muundo wake wa silabi ambazo huundwa kwa kuleta pamoja fonimu katika mazingira fulani ili kupata ruwaza inayoweza kutamkika. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwepo kwa mabadiliko ya fonimu za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Wanafunzi walitumia ruwaza za Luganda katika maandishi na mazungumzo ya Kiswahili sanifu na kuathiri mofosintaksia ya Kiswahili sanifu. Athari za mwingiliano huu ulitokana na tofauti za kisarufi baina ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha mbili tofauti.

6.1.1.6 Kanuni ya uwakilishaji dhima wa matumizi ya nomino katika tungo

Dhima ya ngeli nomino katika tungo huwakilishwa na viambishi vipatanishi vya mofolojia na sintaksia vinavyoambishwa kwenye maneno mengine katika tungo kutegemea nomino kuu. Kanuni ya uwakilishi dhima inashikilia kuwa: Viambishi vyote vinavyopachikwa kwenye kategoria ya maneno ya kisarufi lazima viwakilishe dhima ya kimfosintaksia kiuamilifu na kimuktadha ya idadi ya umoja na wingi, jinsia ya kisarufi hasa kwa kudhihirisha umoja na

wingi wa nomino inayotumika katika muundo wa kirai nomino na kirai tenzi na shamirisho zake katika muundo wa ndani wa sentensi kuwakilisha maana kamili ya tungo. Data Na. (5.14, Uk. 159) kutokana na Mulei na Wenzake, (2021) na Baertlein & Ssekitto, (2014) inadhihirisha utokeaji wa kanuni hii katika Luganda na Kiswahili sanifu.

Uchanganuzi wa matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi kuhusiana na dhima ya kisarufi ya ngeli nomino katika tungo, ilibaini mwingiliano na athari za matumizi ya kanuni ya uwakilishi dhima wa matumizi ya nomino katika tungo. Utafiti huu ulitambua kuwa, licha Luganda sanifu kuwa na ngeli zake zilizoainishwa kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki kama ilivyo katika Kiswahili, wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 walikiuka kanuni hii kwa kukopa na kuhamisha maumbo ya uwakilishi ngeli wa Luganda katika nafasi ya maumbo ya kimofolojia na kisintaksia kuwakilisha dhima ya idadi ya umoja na wingi, jinsia ya kisarufi ya upatanishi wa kisarufi wa kuonyesha mahusiano ya neno kuu na maneno mengine katika tungo na hata kupotosha maana kamili ya kisarufi ya tungo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu. Data Na (6.15) kutokana na mijarabu ya kutunga sentensi kwa umoja na wingi ulidhihirisha athari za mwingiliano.

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili

a) *Kiongozi chetu kinaongea muzuri.*

[ch-we, ki-a, mu-vi]

b) *Viongozi vyetu vinaongea muzuri.*

[vy-we, vi-wa, mu-vi]

c) *Kifarur kinacheza na mutoto yake.*

[ki-a, mutoto-ndama, y-w]

d) *Maji gamekyemuka.*

[ga-ya]

Amazzi gakyemuse

e) *Gari emeanguka*

[en-li, ø-li]

Emotoka egudde

f) *Magari zimeanguka*

[zi-ya]

Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

Kiongozi wetu anaongea vizuri.

Viongozi wetu wanaongea vizuri.

Kifarur anacheza na ndama wake.

Maji yamechemka.

Gari limeanguka

Magari yameanguka

Asili: Data za mijarabu ya kisarufi

Uchanganuzi wa matokeo ya ulibainisha wanafunzi (54) wakiwa na tatizo la matumizi ya ngeli nomino kuwakilisha dhima ya uwakilishi wa viambishi vilivyotumika kuonyesha

uhusiano milikifu na unganifu wa idadi na wingi. Wanafunzi (11) walionyesha ukomavu katika matumizi kutokana na misingi ya Kiswahili. Data Na. (6.14, Uk. 290) inadhihirisha ukiukaji wa uainishaji wa ngeli za Kiswahili sanifu kimaana. Wanafunzi walihamisha maumbo ya viambishi vya nomino kuu ya ngeli za Luganda mkabala wa kisemantiki hasa katika [a- f] bila kutambua kuwa nomino husika ni nomino zilizoainishwa katika kategoria mbalimbali za kisemantiki na kutumika katika tungo kimofosintaksia kuwakilisha idadi ya umoja na wingi, jinsia ya kisarufi ya uhusiano wa nomino kuu na maneno mengeni katika tungo. Wanafunzi walitumia nomino za ngeli za 9 na kumi ya wanayama na vitu katika nafasi ya maumbo ya kimofosintaksia ya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yalikiuka sifa kamili ya matumizi ya viambishi vipatanishi kuwakilisha dhima husika na hivyo kusababisha athari za kimaendelezo na kimaana ya tungo za Kiswahili sanifu. Aidha, matumizi haya yaliathiri kanuni ya kisarufi ya matumizi ya viambishi kwa kuwa viambishi nomino vilivyotumika katika utungo havikubeba taarifa za kisarufi za nomino katika utungo kimofosintaksia za kuonyesha seti za kisarufi za idadi ya umoja na wingi wa nomino kuu, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira, na jinsi ya nomino katika utungo.

Matokeo haya yanaendana na upekuzi wa maandishi ya Kihm, (2005) ambaye anaeleza kuwa matumizi ya nomino yasiozingatia dhima ya ngeli nomino hupotosha sifa kamilifu za nomino iliyotumika kama neno kuu katika tungo, idadi yake, uhusiano wake na maneno mengine katika tungo na maana ya tungo husika. Aidha, Mukuthuria, (2004) anathibitisha jinsi wazungumzaji wa L1 wanavyohamisha viambishi vya ngeli kutoka lugha mama (L1) katika Kiswahili sanifu na kusababisha athari za mwingiliano katika matumizi. Upekuzi wa kazi ya Nurse, Spear, na Spear (1985) nao walitambua kuwa mfumo wa ngeli za majina katika lugha za Kibantu hasa katika uundaji wa msamiati na upachikaji wa maumbo ya umoja na wingi na upatanishi wa kisarufi unahusiana katika uambishaji wa viambishi..

Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kuhusiana na tungo na uwakilishi wa dhima, wakijadiliana kuhusu jinsi uwakilishi dhima wa matumizi ya nomino katika tungo unavyojitokeza, Ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili hutumia maumbo mbalimbali yanayoambishwa kwenye kategoria mbalimbali kuwakilisha dhima ya kisarufi kama ilivyothibitishwa na Mwanafunzi 9 aliyeleza kuwa;

“Luganda na Kiswahili hutumia viambishi ambavyo huwekwa kwenye nomino na maneno mengine kama vitenzi na vivumishi kuwakilishi dhima ya kimofosintaksia ya nomino na maneno mengine katika tungo.”

Aidha, mwanafunzi (35) alifahamisha kuwa;

“Matumizi ya viambishi hivi ni muhimu kwa sababu vinapotumika kwa usahihi vinajenga uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo na visivyotumika vyema vinapotosha dhima ya kisarufi ya kutambua idadi, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira, na jinsi ya nomino katika utungo.”

Kanuni ya uwakilishi dhima na kanuni ya kisarufi ya vibainishi na viambishi ni kanuni mbili ambazo hushikilia kuwa; viambajengo huwa katika sehemu tofauti za neno na katika muktadha wa utungo na vinaunganishwa na sheria fulani ambazo husababisha umilikifu na unganishaji wa viambajengo hivyo kuwakilisha dhima ya idadi na jinsi ya kisarufi ya umoja na wingi kimofosintaksia. Aidha, Kwa mujibu wa kanuni hii, vibainishi na viambishi ngeli kama vinavyojitokeza katika Luganda vinapotumika, maumbo yake yanonyeshe seti za kisarufi (dhima) za idadi, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira, na jinsi ya nomino katika utungo. Matumizi haya lazima yazingatie maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya maumbo kamili ya ngeli ambamo nomino kuu huainishwa. Kibainishi kisipotumika, neno au nomino hiyo huweza kujitosheleza kama sentensi sahili yenye kiima na yambwa (Baertlein & Ssekitto, 2014). Katika utafiti huu ilibainika kuwa wanafunzi ambao L1 walipotosha dhima ya uambishaji wa maneno kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa nomino. Wanafunzi walilhamisha, kujumlisha na kutumia maumbo kwa njia ya mbadilishano wa viambishi vya ngeli nomino vya Luganda katika Kiswahili kuwakilisha dhima ya kisarufi.

6.1.2 Mwingiliano wa kanuni za vivumishi vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili

Vivumishi ni kipashio cha kimofosintaksia kinachotumika kukumusha nomino katika KN. Kipashio hiki hutumika kwa kuzingatia utaratibu maalumu katika Luganda na Kiswahili sanifu. Taratibu hizi ndizo zinazowaongoza wamilisi wa lugha kutumia vivumishi mwafaka bila kuvunja sifa za kisarufi za kimofosintaksia. Mbwilow (2017), anaeleza kuwa maneno ya lugha asilia ya binadamu huwa na mpangilio ulio maalumu ambao hufuata kanuni na taratibu zinazowaongoza watumiaji wa lugha hiyo katika mawasiliano. Utafiti huu ulichunguza kanuni hizo za matumizi ya vivumishi na wanafunzi wa Kiswahili na ambao L1 ni Luganda kwa madhumuni ya kutambua mwingiliano wa kanuni za matumizi ya kanuni za vivumishi vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kwa kuzingatia vigezo vya muundo na maumbo ya vivumishi, mpangilio, dhima, mahali pa utokeaji, mahusiano ya vivumishi na maneno makuu katika tungo na urejeleo wa vivumishi katika tungo, utafiti huu ulidhihirisha mwingiliano wa kanuni za matumizi ya vivumishi vya Kiswahili zifuatazo katika Kiswahili sanifu.

6.1.2.1 Kanuni ya kimofolojia ya uambishaji VPM vya ngeli za nomino

Kanuni ya uambishaji hudai kuwa: Uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu. Kimofosintaksia, muundo wa vivumishi katika KN huchukua maumbo sawa ya viambishi ngeli vya nomino kimofolojia kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi na maumbo ya nomino katika tungo za kirai nomino huathiri maumbo yaa vivumishi (Oduor na Wenzake 2017). Uchanganuzi wa Upekuzi wa maandishi ya Abudonia, (2014), Balagadde, (2016), Mbwillow, (2017) na Philipo, (2012), uligundua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kanuni hii katika kuambisha vivumishi mbalimbali katika matumizi. Hata hivyo, ingawa matumizi ya vivumishi katika lugha hizi mbili huzingatia uambishaji wa viambishi awali vya ngeli na idadi ya umoja na wingi kwenye mizizi inayobeba sifa za kileksika za vivumishi, maumbo ya uambishaji hutofautiana. Utofauti huu ulidhihirisha mwingiliano wa matumizi ya vivumishi mbalimbali vya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulidhihirisha mwingiliano unaotokana na uambishaji kwa kutegemea aina mbalimbali za vivumishi kama ifuatavyo:

6.1.2.1.1 Athari za Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vimilikishi

Vivumishi vimilikishi ni aina ya vivumishi ambavyo hueleza jinsi nomino inavyomilikiwa. Vivumishi hivi huelezea hali ya kuwa na au kumiliki kwa nomino (Okumu, 2006 na Mgullu, 1999). Aina hii ya vivumishi ni miongoni mwa kipashio muhimu cha kimofosintaksia kinachotumika katika KN. Matokeo ya upekuzi wa maandishi ya Namugala, (2014), Mgullu, (1999), Peterson, R. (2017) Kihore na wenzake, (2004) na Habwe & Karanja, (2004), ulibaini kuwa Luganda na Kiswahili hutumia mizizi sita inayobeba sifa za kileksika za vimilikishi inayotumika kulingana na nafsi tatu kwa umoja na wingi kama inavyorejelewa katika jedwali Na. (4.12, Uk. 106) na (5.1, Uk. 170) kutokana na orodhahakiki ya kazi za maktabani ya Kyagaba (1996; 2015) na Habwe & Karanja (2004).

Matokeo ya uchanganuzi wa data za mijarabu ya kisarufi kwa kuzingatia mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1984), utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walihamisha maumbo ya viambishi awali vya Luganda na kuyapachika katika mizizi ya vivumishi vimilikishi vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na.(6.16) kutokana na mijarabu ya kisarufi ya matumizi ya vimilikishi katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu wa nomino na vivumishi katika tungo.

- a) *Ngeli ya [n-zi na m-wa]* [y- na z-] → [w- na w-]
Ng'ombe yangu/ yako/ yake Zangu/ zako/ zake Ng'ombe wangu /wako/ wake
Ente yange/yiyo/yiye zange/zizo/zize
Ng'ombe yetu/ yenu/ yao Zetu/ zenu/ zao Ng'ombe wetu wenu wao
Ente yaffe/yamwe/yaabwe zaffe/zammwe/zaabwe
- b) *Ngeli ya [mu-mi- na m-mi]* [gy- na z-] → [w- na y-]
Mupira gwangu ngwako gwake Gyangu, gyako gyake Mpira wangu wako wake
Omupiira gwaange/gwo/gwe
Mipira yangu yako yake Zangu zako, zao Mipira yangu yako yake
Mipira yetu yenu yao Zetu zenu zao Mipira yetu yenu yao
Kyatu yangu yako yake Kyangu kyako kyake Kiatu changu chako chake
Engaato yange yiyo/yiye zange/zizo/zize
Viatu zangu zako zake Zetu zenu zao Viatu vyangu vyenu vyao
Engaato zange/zizo/zize zaffe/zammwe/zaabwe
- c) *Ngeli ya [ki-bi na ki-vi]* [ky- na by-] → [ch- na vy-]
Kitabo kyangu kyako kyake Kyetu kyenu kyao Kitabu changu chako chake
Ekitabo kyange kikyo kikye kyafe kyamwe kyaabo
Vitabo byangu, byako byake Byetu byenu byao Vitabu yetu vyenu vyao
Ebitabo byange bibyo bibye byaffe byabyo, byaabwe
- d) *Ngeli ya [en-zi na ø/ji-ma]* [y- na z-] → [l- na y-]
Gari yangu yako yake Yetu yenu yao Gari langu, lako lake
Emmotoka yange yiyo yiye yaffe yammwe yaabwe
Magari yangu yako yake Yangu zako zake Magari yetu yenu yao
Magari Yetu yenu yao Zetu zenu zao
Emmotoka yaffe yammwe yaabwe zaffe zammwe zaabwe

Asili: Kutokana na data za mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Data Na (6.17) inadhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni za uambishaji wa viambishi awali nomino vya upatanishi kwenye mizizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu. Wanafunzi walihamisha maumbo awali ya ngeli nomino yanayoambishwa kwenye vimilikishi vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu wa uhamishaji ulijitokeza katika Ngeli za [n-zi na m-wa], Ngeli za [mu-mi na m-mi], Ngeli za [ki-bi na ki-vi] na Ngeli za [en-zi na ji-ma] za Luganda na Kiswahili sanifu mtawaliwa. Mwingiliano huu ulijitokeza katika kuwakilisha umiliki wa nomino kwa wingi na umoja.

Mijadala ya wanafunzi kuhusu uhamishaji na ufasiri wa maumbo ya Luganda na kuyatumia katika Kiswahili, matokeo ya mjadala ilibaini kuwa wanafunzi ambao L1 walifasiri maumbo ya Luganda na kuyahamisha katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Walipoulizwa sababu yao kutumia maumbo ya Luganda badala ya Kiswahili; Mwanafunzi 51 alieleza kuwa;

“Maumbo ya viambishi vya Luganda hukaribiana kufanana na vile vya Kiswahili kwa hiyo mimi nikishindwa kutambua umbo sahihi, ninafasiri umbo la Luganda na kuitumia katika Kiswahili.”

Aida mwanafunzi 28 akiunga mkono mchango wa mwanafunzi 51, alieleza kuwa’

“Wanafunzi huchukulia kuwa kwa ujumla, sheria za maumbo ya Luganda ambayo yanarandana na ya Kiswahili sanifu yalikuwa sahihi. Kwa hiyo mimi ninaona kutumia maumbo ya Luganda ni sawa na ya Kiswahili hata kama inatofautiana kidogo.”

Matokeo ya mijadala hii ilibaini kuwa utegemezi wa uwiano wa kisarufi wa vimilikishi vya Luganda na Kiswahili, uliathiri matumizi ya vimilikishi vya Kiswahili. Luganda na Kiswahili zilikuwa lugha mbili tofauti licha ya kuwa kanuni za matumizi ya vimilikishi ulikuwa na ukuruba. Matokeo haya yanaendana na mihimili ya sarufi bia ambayo hushikilia kuwa kanuni zilizile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Kwa hiyo, licha ya kufanana kwa maumbo ya uambishaji na kanuni ya uambishaji pamoja na utaratibu wa kutumia vimilikishi katika tungo za Luganda na Kiswahili sanifu, athari za uhamishaji uliathiri maumbo ya vivumishi katika tungo kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu wa vivumishi vya Kiswahili sanifu.

Kyagaba, (1996), (2014), Obara, (2014), Kisakwah, (2014) walieleza kuwa, kimuundo vimilikishi katika Luganda na Kiswahili sanifu vimeundwa kwa viambishi awali vya nomino vinavyobeba maaan ya kileksika na kisarufi na mizizi yenye kubeba maana ya kileksika iliyosetiri maana au maudhui ya umilikaji. Vimilikishi hivi hubadilika kimaumbo katika tungo kutegemea maumbo tofauti ya viambishi awali vya ngeli nomino inayokumushwa na nafsi ya umilikaji. Viambishi hivi hutegema nomino kuu kwani maumbo yake huathiri maumbo ya vivumishi kwa sababu maumbo yanayokaririwa katika nomino kuu ndiyo yanayokaririwa kwenye vivumishi. Hata hivyo, matokeo ya matumizi ya viilikishi ya wanafunzi ambao L1 ni Luganda, ilikiuka kanuni hii na kutumia viambishi ngeli vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu kwa kuhamisha na kufasiri matumizi na maumbo yake kutoka Luganda katika kiswahili sanifu na hivyo kupotosha

uwiano wa kisarufi wa Kiswahili sanifu. Hali hii ilitokana na tofauti ya maumbo ya uainishaji wa ngeli nomino kimofolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

6.1.2.1.2 Athari za Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya –a unganishi

[-a] unganifu ni vivumishi vilivyoundwa kwa kiambishi tamati [-a] kinachoambishwa viambishi vipatanishi vya ngeli nomino mwanzoni kufafanua uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo. Kivumishi hiki kimeundwa kwa kuambatanisha kiambishi kipatanishi cha msingi [KPM] awali cha ngeli nomino na mzizi wenyewe [-a]. Kimofosintaksia, kivumishi hiki hutumika kutegemea ngeli za nomino au kihusishi chake kisintaksia kwa ajili ya kuleta maana mbalimbali kuhusu nomino inayotajwa (Chomi 2003; Habwe & Karanja 2004; Mirikau 2008; Obara 2012 na Kisakwah, 2014).

Kanuni ya matumizi ya kivumishi cha [-a] unganifu hushikilia kuwa: Vivumishi [-a] unganifu huambishwa kiambishi patanishi cha msingi awali cha ngeli nomino ya neno kuu kwa ajili ya kuleta upatanishi unaofaa kati ya nomino na maneno mengine katika tungo virai au vishazi. Kila nomino huwa na viambishi patanishi vya msingi vinavyotofautiana kutokana na mfumo pamoja na maumbo ya kimofosintaksia ya ngeli nomino na kivumishi chake. Ukiukaji wa kuambatisha viambishi vya kiupatanishi usiofaa huweza kupotosha uhusiano wa nomino na vivumishi na hivyo kupotosha usanifu wa matumizi ya lugha husika kama inavyorejelewa katika Jedwali Na. (4.15, Uk. 113) kutokana na ya orodhahakiki ya data ya maktabani.

Uchanganuzi wa matini ya kipashio cha {-a} unganifu kutokana na Nsimbi, Walusimbi, Mpalanyi na Mukasa (2015), Mgullu (1999) Namugala (2014), Obara, (2014), Kyagaba, (1996) na Philipo, (2017) ulidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushabihiana kimofolojia na kisintaksia katika kuambatanisha mzizi wa kivumishi cha [-a] unganifu kinachowakilishwa na kiambishi tamati [-a] kutegemea maumbo ya viambishi vipatanishi msingi vya ngeli husika. Hata hivyo, tofauti za maumbo ya viambishi vipatanishi vya msingi vya ngeli nomino vinavyoambatanishwa kwenye mzizi huu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana kutoka na tofauti za mpangilio wa ngeli na maumbo wakilishi ya nomino kimaumbo (Rejelea Jedwali 4.15 Uk 113).

Matokeo ya mjarabu ya kisarufi ya kutunga sentensi kuonyesha matumizi sahihi ya kivumishi cha –a unganifu miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda ulibainisha athari za mwingiliano wa kuhamisha, kujumlisha na kutumia maumbo ya viambishi

vipatanishi vya msingi vya ngeli za Luganda kudhihirisha upatanishi wa kisarufi baina ya nomino kuu na vivumishi husika katika virai kudhihirisha dhima, ngeli za idadi ya umoja na wingi. Hali hii iliweze kupotosha usanifu wa matumizi ya Kiswahili sanifu kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo kwa mujibu wa kanuni ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981). Data Na.(6.17) kutokana na mijarabu aya kisarufi ya kutunga sentensi kutumia {-a} unganifu kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na Upatanifu ulidhihirisha athari za mwingliliano.

a) Ngeli ya [N-zi-(e-zi) na m-wa (a-wa)]

| | |
|---------------------------------------|--------------------------------------|
| <i>Kondoo ya Kasibante imepoteya</i> | Kondoo wa Kasibante amepotea |
| <i>Endiga ya Kasibante ebuzze</i> | |
| <i>Kondoo za Kasibante zimepoteya</i> | <i>Kondoo wa</i> Kasibante wamepotea |
| <i>Endinga za Kasibante Zibuzze</i> | |

b) Ngeli za [mu-mi-(gu-gi) na m-mi-(u-i)]

| | |
|---------------------------------------|--------------------------------------|
| <i>Mupira gwa gari kumepasuka</i> | Mpira wa gari umepasuka |
| <i>Omupiira gw'emotooka kuyabise</i> | |
| <i>Myoyo gy'a watu ni mubaya sana</i> | Mioyo ya watu ni mibaya sana. |
| <i>Emyoyo gy'a bantu mibi nnyo</i> | |

c) Ngeli ya li-ma (li-ga) na ø/Ji-ma (li-ya)

| | |
|-----------------------------------|-----------------------------------|
| <i>Jicho lya mutoto limevimba</i> | Jicho la mtoto limevimba |
| <i>Eriiso ly'omwana liziimbye</i> | |
| <i>Macho ga mutoto gamevimba</i> | Macho ya watoto yamevimba. |
| <i>Amaaso g'omwana gazimbye</i> | |

d) Ngeli ya [ki-bi na ki-vi]

| | |
|---------------------------------------|-------------------------------------|
| <i>Kigiko kya Sulait gimeanguka</i> | Kijiko cha Sulait Kimeanguka |
| <i>Ekigiko kya Sulait kigudde</i> | |
| <i>Bintu bya jokoni ni bikyafu</i> | Vitu vya jikoni ni vichafu |
| <i>Ebintu by'omufumbiro biddugala</i> | |

e) Ngeli ya [lu-en(lu-zi) na u-n(u-zi)]

| | |
|-----------------------------------|--------------------------------|
| <i>Ulimi lwa nyoka lunatisha</i> | Ulimi wa nyoka unatisha |
| <i>Olulimi lw'amusota lutiisa</i> | |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi nyanjani

data Na. (6.17) kutokana na mijarabu ya Kisarufi ilidhihirisha ukopaji na uhamishaji wa kanuni ya mofolojia ya uambis haji wa viambishi vya msingi vya ngeli nomino. Matokeo ya uchunguzi wa matokeo kwa mujibu wa mihimili ya ubia na upatanishi, utafiti huu ulibainisha

athari za mwingiliano wa kuambisha viambishi ngeli vipatanishi vya msingi kwenye mzizi wa –a unganifu kudhihirisha uhusiano wa vipashioa vya kisarufi baina ya nomino kuu na maneno mengine katika tungo. Wanafunzi walipopatwa na ugumu wa kutambua kivumishi cha –a unganifu, waliamisha vipatanishi kutoka Luganda katika Ngeli za li-ma (li-ga) na Ji-ma (li-ya) na Ngeli za [N-zi-(e-zi) na m-wa (a-wa)] za Kiswahili na Luganda kimfuatano.

Uchanganuzi wa data za sentensi zilizoandikwa na wanafunzi kwa kutumia kifaa cha kudondoa data chenye sifa za kimofosintaksia za matumizi ya –a unganifu utafiti huu uligundua kuwa, wanafunzi wakitumia mikakati ya umilisi wa ngeli nomino na matumizi ya –a unganifu ya Luganda zaidi katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Mikakati hii ilisababisha athari za kuhamisha, kubadilisha na kujumlisha viambishi vipatanishi vya msingi vya a- unganishi vya Luganda katika mazungumzo na maandishi yao. Matumizi ya aina hii yaliathiri Kiswahili sanifu kwani katika matumizi wanafunzi walitumia viambishi visivyo na hivyo kusababisha athari za kitahajia na kimaendelezo, makosa ya upatanifu wa kisarufi baina ya nomino kuu na maneno mengine katika tungo. Hali hii ilikiuka kanuni ya utawala na umilikifu kwa sababu ya kukiukwa kwa masharti ya matumizi ya –a unganifu katika Kiswahili sanifu.

Hii ni kwa sababu kivumishi cha –a unganifu hutumika kuonyesha uhusiano wa nomino na maneno mengine katika utungo chenye dhima ya kimofosintaksia ya kuelezea zaidi juu ya aina, daraja, umilikaji na hali ya nomino husika katika tungo. Kimofosintaksia kivumishi hiki lazima kiunganishwe na mofu zinazowakilisha aina ya ngeli nomino inayohusika iupatanisho kinapotumika ili kuonyesha uhusiano wa nomino na kategoria ya maneno mengine, kutoa taarifa zaidi za nomino kidaraja, umilikaji, hali/aina ya nomino au kiwakilishi chake katika utungo. Kwa hiyo, mtumiaji yeyote asiyezingatia kanuni ya kuteua viambishi vya msingi patanishi vinavyofaa wakati wa kutumia kivumishi hiki huwa amekiuka kanuni ya sarufi na hivyo hupotosha usanifu wa lugha husika.

Matokeo haya ya matumizi ya yanashadidiwa na Kirabi, (2015) anayeleza baadhi ya makosa ya kimofosintaksia yanyofanywa na wanafunzi kutokana na kuhamisha kanuni ya L1 kwa L2. Miongoni mwa makosa anayotaja ni yale ya matumizi mabaya ya -a unganifu kwa kuhamisha –a unganifu ya ngeli ya L1 kwa L2. Anatoa mifano ya, “matumizi yasiyofaa ya –a unganifu kwa mfano: *Michungwa za jirani, moyo ya mtoto, kuna mkutano ya walimu* (Kirabi, 2015: 72). Matokeo haya yanungwa mkono Kisakwah (2014) ambaye anadhihirisha ukiukaji wa

matumizi ya kivumishi cha {-a} unganifu ambayo kwayo ilipotosha upatanifu wa kisarufi wa nomino na maneno mengine katika tungo.

6.1.2.1.3 Athari za Mwingiliano wa kanuni Katika matumizi ya vivumishi vionyeshi

Kanuni ya mofolojia ya vionyeshi inashikilia kuwa: Vivumishi vionyeshi ni vitatu ambavyo huwakilishwa na mofu (maumbo) ya kipekee inayoitofautisha nomino moja na nyingine kisarufi kutegemea ujirani na umbali wake baina ya mzungumzaji na nomino inayokumushwa. Mofu zinazohusika ni mofu za kisarufi zinazodhihirisha upatanishi wa kisarufi, mizizi ya uundaji, nafsi, ngeli na idadi ya umoja na wingi. Data Na. (5.22, Uk. 185) ya data kutokana na Kiyinikibi, (2021), Leah & Sseguya (2015) na Kyagaba (1996), na Data Na.(5.25, Uk. 188) kutokana na data ya maktabani ya (Ashton 1982; Kyagaba (1996); Habwe & Karanja 2004; Leah & Sseguya 2015 na Philipo 2017) Inatoa ithibati ya uwiano na tofauti za maumbo wakilishi ya vionyeshi baina ya Luganda a Kiswahili sanifu.

Matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi ya kutunga sentensi kutumia vivumishi vionyeshi, utafiti huu ulibainisha kuwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda wakihamisha viambishi vipatanishi awali vya msingi vya Luganda katika matumizi ya vionyeshi vya Kiswahili katika tungo. Matumizi haya yalijitokeza katika baadhi ya ngeli nomino ambazo hazikuonyesha uwiano wa kimaumbo ya kimofosintaksia ya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na.(6:18).

a) *Ngeli za n-zi (e-zi) na M-wa (a-wa)*

Paka hii enapenda kucheza

Paka huyu anapenda kucheza

kapa eno eyagala nnyo okuzannya

Mbuzi hizi, zile zinakula sana

Punzi hawa wanakula sana

Embuzi zino, zili zilya nnyo

b) *Ngeli ya mu-mi (gu-gi) na mu-mi(u-i)*

Nipatiye mugaati gule/ guli

Nipe mkate huo/ule

Leeta omugaati guno/guli

Hugwo mukeka ni gwange

Mkeka huo ni wangu

Ogwo omugaati gwange

c) *Ngeli ya [ki-bi na ki-vi]*

Bikopo hibi, bile binapendeza

Vikombe hivi vinapendeza

Ebikopo bino, bili birungi

Viatu hibyo ni bya nani?

Viatu hivyo ni vya nani

Viatu zile zinapendeza

Viatu hivyo vinapendeza

Nilimpatia zile vintu ulimpa

Nilimpa vitu vile ulivyonipa

d) Ngeli za [li-ma (li-ga) na ji-ma (li-ya)]

Maandazi huyo mutamu sana

Maandazi hayo ni matamu sana

Magari hizi, hizo, zile zimeanguka *Magari haya/ hayo/yale yameanguka*

Emmotoka zino, ezo, zili

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi ya kutunga sentensi

Kutokana na data ya mijarabu ya wanafunzi, iligunduliwa kuwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda walijumlisha matumizi ya viambishi vya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu, kuhamisha viambishi vipatanishi vya Luganda na kubadilisha maumbo ya viambishi vipatanishi vya ngeli nomino ambavyo vilistahili kuambishwa kwenye mizizi ya vionyeshi vya Kiswahili sanifu. Walitumia viambishi visivyodhihirisha uhusiano wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa nomino na vionyeshi kwa umoja na wingi. wanafunzi walieleza kuwa, nafsi zote tatu ziliathirika sana hasa katika jozi za ngeli nomino ambazo zilikaribiana na kutofautiana na viambishi husika kama vile ngeli ya 1 na pili ya Kiswahili ikiathirika na maumbo ya ngeli ya 9 na 10 ya Luganda, ngeli ya 3 na 4 ya Kiswahili ikiathirika na ya Luganda, ngeli ya 5 na 6 ikiingiliana na kuathiri matumizi ya ngeli ya Kiswahili na ngeli ya 7 na 8 ikingiliana na kuathiri ngeli ya Kiswahili sanifu.

Data ya uchanganuzi wa mijadala ya wanafunzi ilidhihirisha kuwa mwingiliano huu uliathiri usanifu wa matumizi ya vionyeshi vya kiswahili na kusababisha Kiswahili kupotosha usanifu wake kimazungumzo na kimaandishi. Hali hii ilitokana na kukiuka utaratibu wa kutumia viambishi vipatanishi vinavyoambishwa kwenye mzizi hutegemea nafasi ya nomino (mahali ilipo nomino) na viambishi vipatanishi msingi ambavyo vinatawaliwa na nomino. Viambishi vipatanishi msingi ambavyo huonyesha uhusiano baina ya nomino inayokumushwa na vionyeshi kutegemea mahali ilipo nomino na mzungumzaji kama ilivyoielezwa na Ngamau, (2004) Obara, (2014), Kisakwah, (2014) Kirabi, (2015) katika utafiti wao.

6.1.2.1.4 Athari za Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya sifa

Vivumishi vya sifa huundwa kwa kiambishi patanishi cha msingi na mizizi. Vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli vya upatanishi wa kisarufi vinavyohusiana na sifa ya nomino iliyotajwa kila mara vinapotumika Oichoe, (2005). Kwa mujibu wa kanuni hii, neno kuu ndilo linalotawala matumizi ya kivumishi katika kundi nomino ambapo nomino ni

kitawala na kivumishi ni kitawaliwa kama inavyojitokeza katika data Na. (5.27, Uk. 194) kutokana na kifaa cha udondoaji data chenye sifa za kimfosintaksia za matumizi ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data hii inadhihirisha kuwa viambishi vipatanishi msingi inavyokaririwa kwenye nomino kuu ndivyo vinavyokaririwa katika vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu ijapokuwa vivumishi vya sifa vya mkopo. Kimfosintaksia vivumishi vya sifa lazima viambishwe viambishi ambavyo huzingatia sifa za kisarufi za upatanishi wa kisarufi baina ya nomino kuu na kivumishi cha sifa chenyewe kama neno au kategoria ya kimfosintaksia katika tungo.

Matokeo ya tathimini ya mijarabu ya kisarufi iliyofanywa miongoni mwa wanafunzi, utafiti huu ilidhihirisha athari za mwingiliano wa matumizi ya viambishi vipatanishi vya msingi vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa mihimili ya usarufi bia na upatanifu wa nadharia ya umilikifu na unganifu, utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi walihamisha, kuchanganya, kubadilisha na kujumlisha viambishi vya Luganda na vya Kiswahili katika matumizi ya vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu kama katika data Na. (6.19) kutokana na mijarabu ya kisarufi ya kutunga sentensi kuonyesha uambishaji wa vivumishi vya sifa katika tungo.

| | Nomino | | Vivumishi vya sifa | | | |
|--------------------|---------------|---------------|---------------------------|----------------|----------------|--|
| a) <i>Ng'ombe</i> | <i>muzuri</i> | <i>mubaya</i> | <i>murefu</i> | <i>muweusi</i> | <i>mukubwa</i> | |
| b) <i>Mupishi</i> | <i>muzuri</i> | <i>mubaya</i> | <i>murefu</i> | <i>muweusi</i> | <i>mukubwa</i> | |
| c) <i>Kitanda</i> | <i>muziri</i> | <i>mubaya</i> | <i>murefu</i> | <i>muweusi</i> | <i>mukubwa</i> | |
| d) <i>Chunguwa</i> | <i>muzuri</i> | <i>mubaya</i> | - | <i>muweusi</i> | - | |
| e) <i>Kalamu</i> | <i>muzuri</i> | <i>mubaya</i> | <i>murefu</i> | <i>muweusi</i> | - | |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi katika tungo nyanjani

Kwa mujibu wa data Na. (6.19), wanafunzi walishindwa kutambua kiambishi kipatanishi cha msingi na kanuni inayohusika katika matumizi ya vivumishi, [-zuri, -baya, -refu, -eusi] na vivumishi vya sifa vinginevyo kwa mkabala wa uainishaji. Badala yake walijumlisha na kutumia kiambishi cha ngeli ya kwanza umoja na wingi [mu-]. Matumizi haya yaliathiri usanifu wa matumizi wa kipashio hiki cha kimfosintaksia kwa kutumia viambishi vya nomino visivyofaa kwenye mizizi ya vivumishi vya sifa kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu.

Kiswahili hutumia kiambishi [m-] kwenye mizizi ya nomino za viumbe hai ambavyo hupatikana katika ngeli ya 1 na 2. Pia, kiambishi hiki hutumika katika ngeli ya 3 umoja. Hata hivyo, wanafunzi ambao L1 ni Luganda walitumia kiambishi hiki na kuongeza irabu [u]

mbele yake na kutumia katika kukumusha nomino ambazo si hisivu na nomino katika ngeli ya 3 kwa umoja katika matumizi yao. Hali ya kuongeza irabu katika mazingira ambamo haistahili kujitokeza ilikiuka kanuni ya muundo wa silabi wa Kiswahili sanifu ambao huzingatia kuwa konsonanti ya king'ong'o /m/ hufuatwa na konsonanti halisi kama vile vipasuo, vikwamizo, vipasuo-kwamizo, vitambaza, na vimadede moja kwa moja (Besha 1996, .Habwe & Karanja, 2012 na Mukuria, 1987).

Aidha, wanafunzi waliambisha vivumishi vya sifa vya mkopo kama vile katika mifano ya data Na.(6.20) kutokana na mijarabu ya kisarufi wa wanafunzi.

| Luganda | Kiswahili |
|----------------------------|-----------------|
| <i>Mutoto mujasiri</i> | Mtoto jasiri |
| <i>Musilikali mushujaa</i> | Askari shujaa |
| <i>Muzungu mukarimu</i> | Muzungu mkarimu |
| <i>Mhusika musugu</i> | Mhusika sugu |
| <i>Chumba kinadhifu</i> | Chumba nadhifu |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi, (2021).

Kwa mujibu wa matumizi ya Kiswahili sanifu, vivumishi hivi ni vivumishi ambavyo haviambishwi viambishi vya nomino kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu baina ya nomino na vivumishi katika tungo.

Mwingiliano mwingine wa kifonolojia uliojitokeza ni ule wa kubadilisha sauti na kutumia nyingine ambayo ni tofauti ingawa ina ukuruba wa sifa za kifonetiki (uhawilisho wa sauti) kama inavyojitokeza katika data Na. (6.21) kutokana na mijarabu ya wanafunzi nyanjani:

| <i>Athari za mwingiliano</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|------------------------------|-------------------------|
| <i>Bitu bizuri</i> | Viti vizuri |
| <i>Watoto bazuri</i> | Watoto wazuri |
| <i>Watu babaya</i> | Watu wabaya |
| <i>Bifuniko bikubwa</i> | Vifuniko vikubwa |
| <i>Bitanda birefu</i> | vitanda virefu |
| <i>Bitanda biwanvu</i> | |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi nyanjani.

Data Na. (6.21) inadhahirisha udondoshaji wa fonimu konsonanti za Kiswahili sanifu /v/ na /w/ za viambishi vipatanishi vya ngeli za Kiswahili sanifu na badala yake kutumia fonimu /b/ ya Luganda sanifu. Mabadilishano ya fonimu hizi yanaonyesha mwingiliano wa Luganda

katika matumizi ya Vivumishi vya sifa katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano wa aina hii katika matumizi ya Kiswahili yalitokana na kuwa; hata ingawa vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli kiupatanifu, mfumo wa mpangilio wa nomino wa Luganda na Kiswahili kiasili unatofautiana na Kiswahili hivyo kila lugha kudhihirisha viambishi vinavyotofautiana kimofosintaksia. Matokeo haya yanaendana na mhimili wa sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981) kwa msingi wa maumbo ya nje na ndani ya nomino kuonyesha tofauti kidogo inayojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Pia, viambishi vinavyotumika huathiriana kifonolojia na kujenga viambishi vipatanishi vya msingi vinavyotofautina na VPM vya Kiswahili sanifu kutokana na michakato tofauti inayotumika wakati fonimu zinapotokea katika mazingira ya vokali na konsonanti ya mizizi.

Wanafunzi walidondosha sauti ya Kiswahili ya kipatanishi cha kisarufi katika ngeli za [1 na 2 [-a-wa] na [7 na 8- [ki-vi] na kutumia fonimu ya [chi-bi]. Katika kufanya hivyo, silabi [ki] ya Kiswahili ambayo pia inatumika katika Luganda kama kiambishi awali cha ngeli nomino kiwakilishi cha umoja kilitamkika kama [chi]. Kwa hiyo konsonanti /k/ ilidondoshwa na badala yake /ch/ kutumika. Vilevile kiambishi awali cha wingi cha Kiswahili cha ngeli ya 8 wingi [vi] kilidondoshwa na badala yake fonimu konsonanti /v/ ikadondoshwa na /b/ kutumika. Ubadilishanaji huu ulikiuka kanuni ya matumizi ya fonimu konsonanti inayotokea katika mazingira ya ujirani na fonimu irabu /i/ na kupotosha matamshi na maandishi ya Kiswahili sanifu. Sauti za konsonanti za Kiswahili zilizoathiriwa zaidi ni zile ambazo hazipatikani katika mfumo wa kifonolojia wa lahaja ya Luganda.

Matokeo ya matumizi ya kanuni hii yanashadidiwa na Kirabi (2015); Obara (2014); Kisakwah (2014) na Lukamika (2015) ambao katika utafiti wao walibainisha ukiukaji wa maumbo patanishi ya nomino yanayokaririwa katika vivumishi vya sifa vya Kiswahili. Aidha, katika kuelezea usahihi wa matumizi ya kanuni hii, Obara (keshatajwa) anaeleza kuwa; Vivumishi hutumika pamoja na nomino kama viambajengo vya kikundi nomino. Vivumishi hivi kimuundo, huathiriwa na aina ya nomino inayohusika. Viambishi vipatanishi hivyo huonyesha upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi. Ikiwa mwanafunzi hatateua vipatanishi sahihi atakuwa amefanya kosa la kisarufi. Ila katika matokeo yake anaeleza kuwa: Kuna aina tofauti tofauti za vivumishi, makosa ya uambishaji usiofaa yalifanywa katika aina hizi tofauti.

Maelezo haya yanathibitisha matumizi ya kanuni na kuonyesha jinsi wanafunzi walivyoathirika na matumizi kutokana na mwingiliano wa wa vivumishi vya sifa na Kiswahili sanifu. Kutokana na matokeo haya, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huwiano na kutofautiana katika matumizi ya kanuni za matumizi ya vivumishi vya sifa baina ya Luganda na Kiswahili, licha ya kuwa lugha za nasaba moja.

6.1.2.1.5 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya Idadi isiyodhahiri

Vivumishi vya idadi isiyodhahiri ni vivumishi ambavyo hutaja kiasi fulani cha idadi kwa ujumla bila kutumia idadi kamili (Mgullu 1999; Habwe & Karanja, 2004; Kisakwah 2014). Utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia vivumishi vya idadi isiyodhahiri katika tungo za kimofosintaksia. Utafiti huu ulichunguza vivumishi vya idadi isiyodhahiri vinne vya [-ngi/ingi, tono/ chache/dogo, lala/ -ingine, onna/-ote] baina ya Luganda na Kiswahili sanifu mtawaliwa kama inavyojitokeza katika jedwali Na. (4.14, Uk. 111).

Kimofosintaksia, vivumishi hivi vya idadi isiyodhahiri vya Luganda na Kiswahili sanifu vimeundwa kwa sehemu kuu mbili kimofosintaksia. Kanuni ya matumizi ya vivumishi visivyo vya idadi hushikilia kuwa: vivumishi vya idadi isiyokamili vinapotumika katika tungo, lazima viambishi awali vya nomino ambavyo pia ni vipatanishi msingi vya nomino vizingatiwe. Vivumishi vipatanishi hivi huambishwa kabla ya mizizi ya vivumishi vinavyobeba maana ya kileksika ya idadi inayokumusha nomino katika KN, ijapokuwa vivumishi vilivyokopwa ambavyo huwa haviambishwi. Hii ni kwa sababu neno kuu katika utungo huchagua kuathiri maneno mengine kutegemea mazingira ambamo nomino tajwa hutokea. Ukiukaji wa kimatumizi usiozingatia muundo wa vivumishi wa uambishaji viambishi awali vya nomino na viambishi vipatanishi msingi vya nomino huweza kudhoofisha usanifu wa lugha husika.

Matokeo ya mijarabu ya kisarufi kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya kisarufi ulibaini athari za mwingiliano wa kanuni ya matumizi ya vivumishi vya Idadi isiyodhahiri miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi walihamishi na kujumlisha matumizi ya viambishi awali ambavyo pia ni viambishi vipatanishi vya msingi vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya idadi isiyokamili vya Kiswahili sanifu. Data Na.(6.22) ya data kutokana matokeo ya mijarabu ilidhihirisha athari za mwingiliano wa uambishaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Matumizi ya [-ngi na ingi]

Luganda

Kiswahili Sanifu

- | | |
|---|---|
| a) Watu <i>mingi/bengine</i> wamekuja kulala | Watu <i>wengi/wengine</i> wamekuja kulala |
| b) Chakula <i>mingi/mingine</i> imepikwa | Chakula <i>Kingi/kingine</i> kimepikwa |
| c) Maji <i>mingi/maingine</i> inamwagika | Maji <i>mengi/mengine</i> yanamwagika |
| d) Maji <i>maangi/maingi/mangine/maingine</i> | Maji <i>mengi/ mengine</i> |
| e) Viberiti <i>bingi/ bingine</i> | Viberiti <i>vingi/ vingine</i> |
| f) Ugonjwa <i>mingi/mingine</i> | Ugonjwa <i>mwingi/mwingine</i> |

Asili: Data kutokana mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi

Mwingiliano uliojitokeza hapa ni wa kujumlisha kiambishi kipatanishi awali cha msingi cha ngeli na kutumia kiambishi [mi] bila kuzingatia viambishi awali vya ngeli sahihi na kuhamisha viambishi vipatanishi vya ngeli ya 7 na 8 kwa wingi katika ngeli za [a-wa na ki-vi]. Aidha, wanafunzi waliambisha kwenye mzizi [-ingi na -ingine] wa kivumishi cha idadi isiyodhahiri kiambishi [mi-]. Walijumlisha kanuni hii kwa kutumia kivumishi [mingi] kwa kila nomino kuu bila kuzingatia utaratibu na maumbo awali ya nomino kuu katika tungo. Hali hii ya kuambishi kiambishi kisichoonyesha uhusiano baina ya nonimo na kivumishi kulidhihirisha ukosefu wa ufasaha na kusababisha athari za kisarufi za upatanishi wa kisarufi baina ya nomino kuu na kivumishi.

Mwingiliano mwingine uliojitokeza ni wa kutumia viambishi vya kimuktadha bila kujali maumbo ya kuambishi kwenye vivumishi vya idadi isiyo kamili ya mzizi [-ingine] pamoja na kudondosha maumbo ya nomino kuu kama katika data Na (6.23) kutokana na data za mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani.

Matumizi ya lala na -ingine

Luganda

Kiswahili sanifu

- | | |
|---|---|
| a) Watu <i>waingine wanakuja</i> | Watu <i>wengine wanakuja</i> |
| b) Bintu <i>bingine binasumbua</i> | Vitu <i>vingine husumbua</i> |
| c) <i>Kalamu ingine</i> | <i>Kalamu nyengine</i> |
| d) <i>Nyumba ingine</i> | <i>Nyumbe nyingine</i> |
| e) <i>Tunayenda kucheza mchezo ingine</i> | <i>Tunaenda kucheza mchezo mwingine</i> |
| f) <i>Gari ingine inakuja</i> | <i>Gari linguine linakuja</i> |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi kutoka nyanjani

Data hii inadhihirisha ujumlishaji na udondoshaji wa kanuni ya uambishaji wa mizizi ya uambishaji kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa vivumishi vya idadi isiyo kamili. Mwingiliano mwingine uliojitokeza katika mijarabu ya kisarufi ni wa wanafunzi kudondosha viambishi vipatanishi vya ngeli ambavyo vilistahili kuambishwa kwenye mizizi ya kivumishi [-ingine] hasa katika (c hadi f). Pia, wanafunzi walidondosha kiambishi cha ngeli sahihi cha ngeli ya 7 na 8 na kutumia kiambishi cha wingi cha ngeli ya 8 ya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu.

Aidha, ilibainika kuwa wanafunzi walihamisha viambishi vya kisarufi vya upatanishi wa Luganda katika kuambisha kwenye mizizi ya nomino kuu ya Kiswahili kama inavyojitokeza katika data Na.(6.24) kutokana na data za mijarabu nyanjani.

Matumizi ya -tono/Chache

Luganda

- a) *Ng'ombe muchache/n-chache*
- b) *Nisaidie kalamu yako kadogo*

Kiswahili

- Ng'ombe chache.
- Nisaidie na kalamu yako kidogo.

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi

Matokeo ya haya yalibainisha kuwa wanafunzi walihamisha kiambishi kipatanishi cha ngeli ya Luganda ya [n-] kwa umoja na kuongeza kiambishi cha ngeli chenye asili ya Luganda katika kiambishi [chache] ambacho kwa mujibu wa kanuni ya kimfosintaksia hakistahili kuambishwa katika (a) na kutumia kiambishi cha ngeli ya udunishaji wa vitu ya [ka-bu] katika kirai cha (b). Matumizi haya yalidhihirisha mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya vivumishi vya idadi vya Kiswahili sanifu kama ilivyodhihirika kutokana na mijarabu ya kisarufi ilidhihirisha athari za mwingiliano baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

Pia, wanafunzi walidondosha kiambishi cha ngeli sahihi cha ngeli ya 7 na 8 na kutumia kiambishi cha wingi cha ngeli ya 8 ya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu kama katika (b) kama inavyojitokeza katika mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi kama katika data Na.(6.25)

Matumizi ya Onna na ote

Luganda

- a) *Watu yote nasimama*
- b) *Amekula chakula yangu yote*
- c) *Magari zote zimeenda*
- d) *Wanafunzi wawote/boote*
- e) *Penda yeye na moyo gwako gwote*

Kiswahili Sanifu

- Watu wote wamesimama
- Amekula chakula changu chote
- Magari yoye yameenda
- Wanafunzi wote
- Mpende kwa moyo wako wote

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi, (2021)

Katika kutumia kiambishi cha idadi ya jumla [-ote], matokeo yalidhihirisha wanafunzi wakijumlisha kanuni na kuhamisha viambishi vipatanishi vya ngeli ya Luganda katika matumizi ya kivumishi [-ote] kama katika mfano wa (e), (b) na (c). Pia, wanafunzi walijumlisha kanuni ya kuongeza viambishi vipatanishi vya wingi kwenye kiambishi [-ote/ kwa mfano katika (d) ama kutumia kiambishi awali cha wingi cha ngeli ya 1 na 2 cha Luganda [ba-].

Matokeo haya ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi ilibainisha kuwa, uambishaji uliofanywa na wanafunzi ambao L1 ni Luganda haukuzingatia ngeli ambamo nomino kuu iliainishwa. Wanafunzi walitumia viambishi vinavyoambishwa bila kujali athari yake. Kikanuni, viambishi vya wingi wa idadi ambavyo huwa na maana ya kileksika ya ujumla wa nomino inayokumushwa bila kutaja hesabu au takwimu kamili ndivyo vinavyotumika. Kwa mujibu wa matokeo haya, ilibainika kuwa kila nomino huwa na viambishi tofauti na viambishi vingine vya nomino zinazohusika katika tungo. Hata hivyo, wanafunzi walijikuta wakitumia kiambishi kimoja katika zaidi ya nomino tofauti, kutozingatia kanuni ya kimofonolojia, kudondosha viambishi vya Kiswahili na kutumia vya Luganda na kujumlisha kanuni.

Matokeo haya yanashadidiwa na Massamba (1986) aliyegundua kuwa wanafunzi walihamisha viambishi mbalimbali kutoka lugha za kwanza na kuviingiza katika Kiswahili sanifu na hivyo kusababisha makosa ya kimofolojia na yale ya kimuundo. Alitetewa na Munyua, (2002) ambaye alitambua kuwa athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi ambayo huchangia matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili katika viwango vyote vya lugha. Aidha, Nyanda (2015) alikubaliana wataalaamu hawa (washatajwa) ambapo katika utafiti wake aligundua kuwa mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha mwathiriano wa lugha jirani. Naye Mulei na Wenzake, (2021) ambao wanaeleza kuwa;

Mwingiliano wa maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya Luganda na Kiswahili ulisababisha uhamishaji maumbo ya ngeli za Luganda kimofosintaksia katika matumizi ya Kiswahili sanifu ambapo maumbo yanayopachikwa kwenye mzizi wa nomino kuwakilisha idadi ya umoja na wingi yanatofautiana hata ingawa watumiaji huyatazama kama alomofu ya mofimu moja.

Utafiti huu ulitambua kuwa, Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, hata hivyo hizi ni lugha mbili tofauti ambazo zina uwiano na tofauti katika matumizi ya kanuni ya

kimofolojia ya uambishaji VPM vya msingi vya ngeli ambao uliathiri matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu.

6.1.2.2 Kanuni ya kifonolojia

Kanuni ya uambishaji wa vivumishi vimilikishi kwa kuambisha viambishi vipatanishi vya msingi [KPM] husababisha mabadiliko ya viambishi msingi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vimilikishi. Miongoni mwa kanuni za kifonolojia zinazoathiri viambishi patanishi vya msingi ni mianzo ya KPM kuanza na ama konsonanti au irabu. Kanuni hizi husababisha uyeyushaji wa fonimu, udondoshaji wa fonimu, muunganiko wa sauti, uundaji wa fonimu mpya na kadhalika. Kanuni hii inashikilia kuwa: Kiambishi kipatanishi cha msingi kikianza ama na konsonanti au irabu, huweza kusabababisha mabadiliko ya fonimu ambayo inapachikwa kwenye mizizi kama KPM (Kiambishi patanishi msingi) (Chomi, 2003; Mgullu, 1999 na Otiende, 2013). Data Na. (6.26) ilidhihirisha utokeaji wa kanuni ya kifonolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

a) *Muyizi [wa] –[ange] anasoma bulungi. Abayizi [ba]- [affe] basoma bulungi.*

Mwanafunzi [wa]-angu anasoma vizuri. Wanafunzi [wa]-[etu] wanasoma vizuri.

b) *Omuzimbi we asaba omusennyu. Abazimbi [ba]-[aabwe] basaba omusennyu.*

Fundi wa]-[ake] anaomba changarawe. Mafundi [wa]-[ao] wanaomba changarawe.

Asili: Data za matokeo kutokana na Chomi, (2003) na Hyman na Katamba (2012).

Data (5.18) Uchanganuzi baina ya Luganda na Kiswahili ulidhihirisha tofauti ambayo ilijitokeza katika baadhi ya KPM cha vivumishi vimilikishi huweza kupata mabadiliko ya kimofonolojia na mengine kutokubali kuathirika kutokana na mfumo wa mofolojia ya muundo wa vivumishi katika Luganda. Hata hivyo, katika Kiswahili, KPM karibu zote huathirika na kanuni ya mbalimbali za kifonolojia katika maandishi na mazungumzo kimofonolojia kama ilivyofafanuliwa na Leah & Sseguya, (2015), Hyman na Katamba, (2012). Tofauti hizi ndizo zilizoathiri matumizi ya kanuni ya kifonolojia ya Luganda katika Kiswahili sanifu na kuathiri usahihi katika Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda.

6.1.2.2.1 Mwingiliano wa kanuni ya kimofolojia katika matumizi ya vivumishi vimilikishi

Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kuhusu athari za mwingiliano kutokana na matokeo ya mijarabu ya wanafunzi ulibainisha kuwa, wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda walikosa kubaini matumizi sahihi ya kanuni ya kimofolojia ya kudondosha baadhi ya fonimu

katika vimilikishi. Matokeo ya mijadala ya kutataka kujua jinsi walivyokiuka matumizi ya kanuni hii na kuathiri Kiswahili sanifu mwanafunzi 4 alieleza kuwa;

“Wanafunzi waliambisha viambishi vipatanishi kwenye mizizi kimaandishi kama kanuni inavyodai bila kuzingatika kanuni ya kimofolojia inayojitokeza katika michakato ya uambishaji”.

Matokeo ya tathimini ya matumizi ya kanuni ya kifonolojia na jinsi inavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu ilidhihirisah uwiano na tofauti za matumizi ya vimilikishi katika Luganda na Kiswahili sanifu. Data Na. (5.17, Uk. 167), Jedwali Na.(5.4, Uk. 191) na mifano ya data Na. (5.18, Uk. 168) na jedwali Na. (5.2, Uk. 180) ilidhihirisha uwiano na utokeaji wa kanuni ya kifonolojia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Utokeani wa kanuni hii katika matumizi inadhihirisha utokeaji wa mihimili ya sarufi bia na upatanifu ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Uchanganuzi wa tathimini ya jinsi kanuni ya kifonolojia ya Luganda na jinsi inavyoathiri matumizi ya vimilikishi kwa muibu wa mihimili ya usarufi na upatanishi utafiti huu ulibaini kuwa uambishaji wa vivumishi vimilikishi kwa viambishi vipatanishi vya msingi [KPM] baina ya Luganda na Kiswahili sanifu husababisha mabadiliko ya viambishi msingi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vimilikishi. Hata hivyo, uchanganuzi wa matumizi ya vimilikishi katika tungo za Kiswahili kwa kutumia kifaa cha kudondoa data chenye sifa za kifonolojia zilidhihirisha kuwa wanafunzi ambao L1 walihamisha kanuni za kimofonolojia, fonimu na vimilikishi vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu kama inavyodhihirika katika maandishi ya mijarabu ya kisarufi katika mfano (6.27):

| Luganda | Kiswahili |
|--|---------------------------------------|
| a) <i>Mbuzi zangu/zange zimepoteya</i> | Mbuzi wangu wamepotea |
| b) <i>Jiko lyange/lyangu/lyangu limewaka</i> | Jiko langu limewaka |
| c) <i>Kitabo kyangu/kyako/kyake kinapendeza</i> | Kitabu changu chako chake kinapendeza |
| d) <i>Kitabo kyangu/kyako/kyake kinapendeza</i> | [Kie-kye-che] |
| e) <i>Vikombe viangu/viako/viake/ vimeng'ara</i> | Vikombe vyangu/ viako/ viake |
| f) <i>Vigiko vyetu/vyenu/vyawo vimetumika</i> | Vijiko vyetu/vyeunu/ vyao vimetumika |

Asili: Data Kutokana na a mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani

Data Na.(6.27) inadhihirisha ukiukaji wa kanuni za udondoshaji wa fonimu inayotokea katika kiambishi cha ngeli kama katika [a na b]. Mfano wa (b) unoanyesha kutotambua kanuni ya udondoshaji wa fonimu ya KPM na badala yake kutumia kanuni ya kimofolojia ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Katika mfano wa [c], wanafunzi walitumia kanuni ya komofolojia ya Luganda katika uambishaji wa vivumishi vilimikishi vya Kiswahili sanifu ya fonimu /i/ na /e/ kuunganika na kuunda fonimu /y/. Waliokosa kutambua kanuni ya komofolojia katika Luganda na Kiswahili sanifu walitumia hali ya ujumlishaji wa kuambisha VPM bila kuzingatia kanuni ya udondoshaji na mvutano wa fonimu kuunda fonimu mpya.

Data [c] unaonyesha wanafunzi kushindwa kutambua kanuni ya ukakaishaji wa fonimu katika Kiswahili sanifu na kutumia kanuni ya ukakaishaji katika Luganda katika vimilikishi vya Kiswahili sanifu. Hali hii inatokana na kuwa: Lugha za Kibantu hudhihirisha kanuni ya kimofolojia ya ukakaishaji wa fonimu mbalimbali. Tofauti ya ukakaishaji huu wa Luganda na Kiswahili sanifu ndio ulioathiri ukiukaji wa kanuni hii na kuhamisha kanuni ya Kiswahili ambapo ukaakaishaji hutokea pale sauti isiyo ya kaakaagumu hubadilika na kuwa mojawapo ya sauti za kaakaagumu. Fonimu /i/ huyeyushwa na kuwa nusu irabu /j/. Nusu irabu hiyo hudondoshwa huku sauti ya kipasuo /k/ ikidhoofika na kuwa [t]. Katika Luganda, udhoofishaji hautokei bali fonimu /i/ hubadilika na kuwa /j/ na kunda [ki] kuwa [ky] ambayo hupachikwa kwenye mzizi wa kimilikishi.

6.1.2.2.2 Mwingiliano na athari katika matumizi ya vivumishi –a unganifu

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni ya kimofolojia ulidhihirisha kuwa wa kanuni ya kimofolojia ulijitokeza katika vivumishi vya –a unganifu. mijadala ulibaini kanuni hii kudhihirika katika ngeli ya 7 na 8 na 5 na 6 ya Luganda na Kiswahili sanifu [ki-bi/ki-vi] na [li-ma/li-ya] mtawaliwa, ngeli ya U-ya, i-zi, ya-ya kama inavyojitokeza katika Data Na. (6.28).

Luganda

*Kijiko **kya** Sulait gimeanguka*

*Ekijiiko **kya** Sulait kigudde*

*Bintu **bya** jokoni ni bikyafu*

Ebintu by'omufmbiro bikyafu

*Ndizi **lya** [lia-lya-la] mutoto*

Kiswahili Sanifu

*Kijiko **cha** Sulait kimeanguka*

*Vitu **vya** jikoni ni vichafu*

*Ndizi **la** mtoto*

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi

Matokeo ya uchanganuzi kutokana na mijadala ya wanafunzi Katika mifano hii ulidhihirisha kuwa wanafunzi walikiuka matumizi ya kanuni ya ukaakaishaji wa fonimu katika mfano wa [a] na udondoshji wa irabu ya kiambishi kipatanishi /i/ katika [c]. Walihamisha viambishi vipatanishi vya L1 vilivyopitia kanuni ya kimofolojia ya L1 katika matumizi ya vivumishi viunganishi vya [-a] vya Kiswahili sanifu kama katika [a -c]. Hali hii ilionyesha mwingiliano wa kanuni ya kifonolojia ya L1 katika matumizi ya vivumishi viunagishi vya [-a] kinyume na jinsi ilivyo katika Kiswahili sanifu na kuathiri usanifu wake. Matokeo haya yanashabihiana na mihimili ya sarufi bia na upatanifu ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Mulei, Ambuyo & Amukowa (2021) walioeleza kuwa; Wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda walihamisha matamshi ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili, kubadilisha sauti kwa mujibu wa L1, kushindwa kutambua kanuni za kifonolojia zinazoongoza baadhi ya maneno na kuyatumia jinsi yalivyo katika tungo za kimofosintaksia za Kiswahili sanifu na kuungwa mkono na Chomi, (2003), Owino, (2016) na Massamba katika tafiti zao za awali. Maelezo haya yalithibitisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, matumizi ya kanuni ya kanuni ya kimofolojia, huwiana na kutofautiana katika matumizi ya -a unganifu ya Luganda na Kiswahili sanifu. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili hudhihirisha uwiano wa matumizi ya kanuni ya kifonolojia, hata hivyo hutofautiana katika michakato na maumbo ya matumizi kuonyesha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zenye kanuni za kifonolojia za matumizi ya kanuni za kifonolojia yaliyo ya kipekee.

6.1.2.2.3 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vionyeshi

Matokeo ya uchanganuzi wa kanuni ya kimofolojia katika mijadala ya wanafunzi wa jinsi matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, ilibainika kuwa mwingiliano wa kanuni ya kanuni ya kimofolojia hujitokeza katika matamshi na maandishi ya vionyeshi vya ngeli ya 7 na 8 ya [ki-bi/ki-vi] ya Luganda na Kiswahili sanifu. Data Na.(6.29) kutokana na mijadala ya wanafunzi:

Luganda

- a) *Kitanda hichi ni kyangu*
- b) *Kitabo hikyo china picha Muzuri*
- c) *Viti hibi binaenda ofisini*
- d) *Bitabu hibyo bipeleke darasani*

Kiswahili Sanifu

- Kitanda hiki ni changu
- Kitabu hicho kina picha nzuri
- Viti hivi vinaenda ofisini
- Vitabu hivyo vipeleke darasani

Asili: Data ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunz

Mijadala ya kueleza jinsi kanuni za kifonolojia inavyojitokeza na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, ilibainika kuwa; Katika matamshi, wanafunzi hutumia kanuni ya ukaakaishaji wa kutumia kiambishi ngeli [ki] na kuitamka kama [chi]. Aidha, katika maandishi ya tungo za mijarabu kwa umoja na wingi, utafiti huu ulitambua mwingiliano wa kionyeshi cha nafsi ya pili na kile cha Luganda kimaandishi badala ya [hi-cho], [cho] iliandikwa kama [kyo] na hivyo kionyeshi kuandikwa kama [hikyo] ambacho hakikuathiri kionyesho cha Kiswahili sanifu kimatamshi/kimazungumzo [hicho].

Matumizi ya vionyeshi vya Kiswahili kimazungumzo na kimaandishi yaliathirika na kanuni ya kifonolojia ya uyeyushaji ya Luganda katika maandishi ambapo [kio] inaandikwa kama [kyo] na kanuni ya mabadiliko ya kanuni ya ukaakaishaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kimatamshi ambapo sauti isiyo ya kaakaa gumu inatamkwa kama sauti ya kaakaa gumu ya [ki] kutamkwa kama [chi]. Mbali na kanuni hii ya kimofolojia, pia, utafiti huu ulibaini uhamishaji wa fonimu za Luganda katika matumizi ya vivumishi vionyeshi ambapo viambishi ngeli vya Luganda vya ngeli ya 8 wingi [bi] ilitumika badala ya [vi] ya Kiswahili sanifu [c na d]. Matumizi haya yaliathiri usanifu wa matumizi ya Kiswahili kwa sababu fonolojia ya Kiswahili ilikiukwa kimaandishi na kimatamshi na kujenga Kiswahili kisicho sanifu kimatamshi na kimaandishi. Hali hii ilitokana na ukosefu wa mazoea ya kutumia Kiswahili sanifu, kukosa kutambua kanuni za kifonolojia za lugha ya Kiswahili pamoja na athari za L1 katika matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda.

Matokeo ya utafiti huu yalielezwa na Chomi, (2003), Mgullu, (1999) na Habwe & Karanja, (2004) kuhusiana na kanuni ya kimofonolojia. Aidha, Owino (2016) anashadidia kuwa: Katika uchanganuzi wa kimofonolojia, ruwaza za kifonolojia na za kimofolojia huweza kuingiliana wakati wa kufafanua mabadiliko kwenye maumbo ya maneno mbalimbali. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa, licha ya Luganda na Kiswahili kutumia kanuni moja ya

kifonolojia, ligha hizi ni lugha mbili tofauti zinazotofautiana katika baadhi ya utaratibu na maumbo ya kifonolojia pamoja na mazingira ya utokeaji wa michakato wa kifonolojia.

6.1.2.2.4 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya sifa

Kanuni ya matumizi ya vivumishi vya sifa inashikilia kuwa: Matumizi ya visifa katika tungo ya kimofosintaksia lazima vizingatie kanuni ya kimofonolojia wakati wa uambishaji wa viambishi vipatanishi kwenye mizizi ya visifa husika katika tungo. Hali hii ilitokana na kuwa kiambishi kipatanishi cha msingi kinachoambishwa kwenye mzizi kikianza ama na konsonanti au irabu, huweza kuathiri fonimu jirani inayopachikwa kwenye mizizi na kusababisha aidha kudondoshwa, uundaji wa fonimu mpya na mabadiliko mengineyo (chomi, 2003), Hyman & Katamba (2010) na Kiyinikibi, (2021). Data Na. (5.1, Uk. 131) na (4.2, Uk. 77 na 4.3, Uk. 79) kutokana na data ya maktabani kupitia kwa kifaa cha kudondoa data inadhihirisha uwiano na tofauti ya utokeaji wa kanuni ya kifonolojia katika matumizi ya vivumishi vya sifa.

Viambishi patanishi vya msingi [VPM] vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu huathiriana kutokana na mfuatano au utokeaji wake katika mazingira ya fonimu irabu na konsonanti katika mfumo wa matumizi kimazungumzo na kimaandishi. Hata hivyo, matokeo ya utafiti huu kutokana na mijarabu ya kisarufi kwa kuzingatia mihimili ya usarufi bia na upatanishi ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika, utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikiuka kanuni ya kifonolojia ya vimilikishi. Data Na, (6.30) kutokana na mijarabu ya matumizi ya kivumishi –*zuri* kilidhihirisha athari za ujumlishaji wa kanuni ya kifonolojia katika matumizi ya vuvumishi.

Luganda

Mutoto muzuri

Kitanda muzuri

Mchungwa muzuri

Ugonjwa mbaya

Daktari muzuri

Kiswahili Sanifu

Mtoto mzuri

Kitanda kizuri

Mchungwa mzuri

Ugonjwa mbaya

Daktari mzuri

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanishi matokeo haya yalidhihirisha athari za kujumlisha kanuni ya Luganda na Kiswahili sanifu, wanafunzi kushindwa kutambua mabadiliko ya kimofonolojia yanayohusika na kuandika vivumishi vya sifa jinsi vilivyo katika Luganda na wengine kuhamisha moja kwa moja kanuni ya kimofonolojia ya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu

Mjadala wa wanafunzi wa kutambua jinsi mwingiliano wa kifonolojia ulivyojitokeza na kuathiri uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi katika tungo, Uchangaunzi wa mijadala ulibaini kuwa athari za mwingiliano ulitokana na kuongeza fonimu [u] kwenye viambishi vya ngeli ya 1 na 3 kwa umoja. Uongezaji wa fonimu hii ulikiuka kanuni ya Kiswahili sanifu inayotumia kiambishi [m-] kwenye mizizi ya nomino za viumbe hai ambavyo hupatikana katika ngeli ya 1 na katika ngeli ya 3 umoja ya viumbe visivyo hai. Hali ya kuongeza irabu katika mazingira ambamo haistahili kujitokeza ilikiuka kanuni ya muundo wa silabi wa Kiswahili sanifu ambao huzingatia kuwa konsonanti ya king'ong'o /m/ hufuatwa na konsonanti halisi kama vile vipasuo, vikwamizo, vipasuo-kwamizo, vitambaza, na vimadede moja kwa moja. Tofauti za mfumo wa silabi wa Luganda na Kiswahili sanifu ndio uliosababisha mwingiliano huu, na ukiukaji wa kanuni ya kimofonolojia ya Kiswahili sanifu. hali hii ilibainisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zinaposhirikisha kanuni ya kifonolojia ya matumizi ya vivumishi vya sifa kimofosintaksia.

Matokeo haya yanashabihiana na yale ya Mukuthuria (2004:120) ambaye aligundua kuwa kiambishi cha ngeli cha awali {m} hubadilishwa kimofonolojia kwa kuongeza irabu /u/ mbele yake. Anaendelea kuonyesha athari za kimofonolojia anaposema kuwa;

“Athari hii inasababishwa na mfanyiko wa kifonolojia wa uchopekaji wa irabu /u/ kuvunja mkabiliano wa king'ong'o /m/ na konsonanti halisi za Kiswahili.”

Mukuthuria (2004:120)

Utafiti huu ulitambua uwiano na tofauti za Luganda na Kiswahili sanifu na kubainisha kuwa, licha ya kuwa lugha hizi ni sa nasaba moja, huwiana na kutofautiana katika matumizi ya kanuni ya kimofosintaksia ya kifonolojia.

6.1.2.2.5 Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri

Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi kuhusiana na matumizi ya kanuni ya kimofonolojia uliojitokeza katika mijarabu ya utafiti ilibaini kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikanganywa na kanuni ya kifonolojia ya

Kiswahili. Kutokana na utata huu, wanafunzi waliamua kutumia kanuni za kifonolojia za Luganda katika matumizi ya vivumishi visvyo vya idadi dhahiri. Katika matumizi, ilibainika kuwa, wanafunzi walijumlisha kanuni na kuambisha viambishi awali vya msingi bila kujali kanuni za udondoshaji, uyeyushaji, ukaakaishaji wa fonimu na muungano wa fonimu kuunda fonimu mpya kama inavyojitokeza kaatika Data Na. (6.31) kutokana na mijarabu ya kisarufi nyanjani.

Matumizi ya [-ngi na ingi]

Luganda

Kiswahili sanifu

- | | |
|--|--|
| a) Bageni b[a-i]ngi/b-[e]-ngine banakula | Wageni wengi/wengine wanakula |
| b) Chakula [m]-ingi/[m]-ngine imepikwa | Chakula Kingi/kingine kimepikwa |
| c) Maji [m]-ingi/ m-[ai]-ngine inamwagika | Maji mengi/mengine yanamwagika |
| d) Maji ma-[a]-ingi/m-[ai]-ngi/mangine/maingine | Maji mengi/ mengine |
| e) Viberiti [b]-ingi/ [b]-ngine | Viberiti vingi/ vngine |

Asili: Data kutokana mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Mwingiliano wa kifonolojia unaojitokeza hapa ni ule wa kudondosha fonimu konsonanti za Kiswahili sanifu na kutumia fonimu za Luganda katika kuambisha viambishi awali vya upatanishi wa kisarufi wa vivumishi vya idadi isiyokamili ya Kiswahili sanifu. Kwa mfano katika (a) wanafunzi walitumia fonimu /b/ badala ya /w/, katika (b) wakatumia /m/ badala ya /k/ na katika (e) wakatumia fonimu /b/ badala ya /v/.

Matokeo ya mwingiliano mwingine uliojitokeza katika matumizi ya [ingi- na ingine] ni kutumia utaratibu wa kifonoloji wa Luganda katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano katika (a) walitumia kivumishi [pengine] kutokana na fonimu /a na i/ kuungana na kuunda fonimu mpya /e/. hata hivyo ilipotokea katika Kiswahili, walishindwa kutumia kanuni hii na kujumlisha matumizi kama ilivyo katika (c na d) kama walivyoshindwa kudodosha irabu /a/ katika /d/. Athari nyingine ambayo ilijitokeza ni ya matumizi ya vivumishi vya idadi isiyokamili vya [lala na -ingine], [lala na -ingine], [Onna na -ote] ambayo ilidhihirisha athari za kofonolojia za ujumlishaji wa kanuni, ukopaji na uhamishaji kanuni na udondoshaji kama ilivyoelezwa katika kanuni ya kimofolojia ya uambishaji viambishi vipatanishi vya msingi vya idadi isiyokamili dhahiri ya data Na (6.24 Uk. 308; 6.25, Uk. 308; 6.27, Uk. 311) na 6.29, Uk. 314)

Matokeo haya yanashadidiwa na Owino, (2016), Otiende, (2013), Kyagaba (2015) na Mutale na Muwanga (2009) Katamba, (1991, 1993; 2003) ambao wanatambua mifanyiko mbalimbali

inayojitokeza katika lugha za Luganda na Kiswahili. Utafiti hii ulibanisha kuwa kanuni ya kimfosintaksia ya kifonolojia hujitokeza katika maandishi na mazungumzo ya Luganda na Kiswahili. Hata hivyo, licha ya kuwa lugha hizi ni za nasaba moja, matumizi ya kanuni hii huwiana na kutofautiana katika matumizi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu.

6.1.2.3 Kanuni ya umiliki na usabaki

Kanuni inazingatia kuwa: vifundo huunda kiambajengo kama na kama tu viambajengo hivyo vitakuwa ni jozi za vifundo vinavyomilikiwa kikamilifu na kifundo kikuu (Chomsky, 1957:1967). Neno kuu katika kirai huyamiliki maneno mengine yote katika tungo kutokana na uhusiano uambajengo unaodhihirisha sifa za kimfosintaksia katika tungo virai (Ambuyo, 2007). Mathalan, nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo (Lusekelo, 2017 na Mwamzandi, 2018). Data Na.(6.32) kutokana na data za kifaa cha udondoaji data kutoka maktabani inadhihirisha mwingiliano wa utokeaji wa kanuni hii ya umiliki na usabaki baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

- a) *Omuzanyi omulungi* *Abazannyi abalungi* [ngeli o(mu)-a(ba)]
- b) *Mchezaji mzuri.* *Wachezaji wazuri* [Ngeli ya M-Wa]
- c) *Ekitabo ekilungi kilinde* *Ebitabo ebirungi bilinde* [Ngeli ya e(ki)- e(bi)]
- d) *Kitabu kizuri kitunze.* *Vitabu vizuri vitunze* [Ngeli ya Ki-Vi]
- e) *Ennyumba ennungi* *Ennyumba ennyungi* [Ngeli ya en-en]

Asili: Data za utafiti kutoka kwa data za Abudonia, (2014)

Matokeo ya kazi za Kyagaba (1996:2015); Lusekelo (2017) na Obara, (2014), Mwamzandi, (2018) ilidhihirisha kuwa kimatumizi, viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya kileksika ya vivumishi humiliki au hutawala mzizi kuwakilisha nomino inayokumushwa kwa wingi wake au ujumla wake. Hata hivyo, kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanisho ya nadharia ya umilikifu na unganifu (1981), huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Matokeo ya jinsi mwingiliano huu wa kanuni ya umiliki na usabaki unavyoathiri matumizi ya Kiswahili umejadiliwa kama ifuatavyo:

| <i>Luganda</i> | <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> |
|--|---------------------------------|--------------------------|
| a) <i>Mupira gwangu ngwako gwake</i> [<i>Gyangu/ gyako/ gyake</i>] | | Mpira wangu wako wake |
| b) <i>Mipira yangu yako yake</i> | [<i>Zangu/ zako/ zao</i>] | Mipira yangu yako yake |
| c) <i>Mipira yetu yenu yao</i> | [<i>Zetu/ zenu/ zao</i>] | Mipira yetu yenu yao |
| d) <i>Kyatu yangu yako yake</i> | [<i>Kyangu/ kyako /kyake</i>] | Kiatu changu chako chake |
| e) <i>Viatu zangu zako zake</i> | [<i>Zetu/ zenu/ zao</i>] | Viatu vyangu vyenu vyao |
| 3. Ngeli ya [ki-bi na ki-vi] | [<i>ky- na by-</i>] | →[<i>ch- na vy-</i>] |

| <i>Luganda</i> | <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> |
|---------------------------------------|-------------------------|---------------------------|
| a) <i>Kitabo kyangu kyako kyake</i> | <i>Kyetu kyenu kyao</i> | Kitabu changu chako chake |
| b) <i>Vitabu byangu, byako byake</i> | <i>Byetu byenu byao</i> | Vitabu vyetu vyenu vyao. |
| 4. Ngeli ya [en-zi na ø/ji-ma] | [<i>y- na z-</i>] | →[<i>l- na y-</i>] |

| <i>Luganda</i> | <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> |
|----------------------------------|------------------------|-----------------------|
| a) <i>Gari yangu yako yake</i> | <i>Yetu yenu yao</i> | Gari langu, lako lake |
| b) <i>Magari yangu yako yake</i> | <i>Yangu zako zake</i> | Magari yetu yenu yao |
| c) <i>Magari Yetu yenu yao</i> | <i>Zetu zenu zao</i> | |

Data Na. (6.33) ya matumizi ya viambishi patanishi [ya- na z-] katika (a) na (b) badala ya [w- na w-] ya Kiswahili katika data (1) ilitokana na uhamishaji, udondoshaji wa VPM vya Kiswahili sanifu, kubadilisha VPM kwa kuvihamisha katika ngeli ya 9 na 10 ya Luganda. Wanafunzi walitumia VPM vya Luganda badala ya VPM vya Kiswahili sanifu. Katika kufanya hivyo, walihamisha VPM vya Luganda na kuvitumia katika vimilikishi vya Kiswahili sanifu kama katika (1-4). Wanafunzi walibadilisha fonimu ya wingi, kukiuka kanuni ya ukaakaishaji ya Kiswahili sanifu na kutumia VPM vya Luganda katika matumizi ya vimilikishi vya Kiswahili. katika kufanya hivyo umiliki na usabaki wa nomino na vimilikishi ulivyojikita katika VPM ukapotoshwa. Hali hii iliathiri usanifu wa matumizi ya Kiswahili sanifu kama katika mifano ya (3). Mwingiliano mwingine uliojitokeza ni ule wa ujumlishaji wa matumizi ya VPM na kuchanganya VPM vya Luganda na Kiswahili katika tungo kama inavyorejelewa katika mifano yote ya (1,2,3 na 4). Mwingiliano huu wa kutotumia VPM mwafaka uliathiri mofosintaksia ya matumizi ya vimilikishi vya Kiswahili sanifu. 6.2.2.3.1.

Matokeo haya yanadhibitisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zenye uwiano wa matumizi ya kanuni za umilikifu na usabaki, na ambazo hutofautiana katika maumbo na utaratibu kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanifu ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote,

ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

6.2.2.3.2 Umiliki na usabaki wa nomino na vivumishi vionyeshi

Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kuhusiana na matumizi ya vionyeshi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wake na maneno mengine katika tungo ulidhihirisha mwingiliano wa kanuni ya umiliki na suabaki wa nomino na vivumishi katika matumizi ya VPM vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Katika kufafanua athari za mwingiliano matokeo yalibainisha athari za ujumlishaji viambishi vya ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu, kuhamisha viambishi vipatanishi vya Luganda na kubadilisha maumbo ya viambishi vipatanishi vya ngeli nomino ambavyo vilistahili kuambishwa kwenye mizizi ya vionyeshi vya Kiswahili sanifu. Uchanaganuzi wa matokeo ya mijadala wa jinsi mwingiliano ulivyoathiri matumiaji katika Kiswahili ulibaini kuwa nafsi zote tatu za vionyeshi ziliathirika sana hasa katika jozi za ngeli nomino ambazo zilikaribiana na kutofautiana na viambishi husika kama vile ngeli ya 1 na 2 ya Kiswahili iliathiriwa na maumbo ya ngeli ya 9 na 10 ya Luganda, ngeli ya 3 na 4 ya Kiswahili ikiathirika na ya Luganda, ngeli ya 5 na 6 ikiingiliana na kuathiri matumizi ya ngeli ya Kiswahili na ngeli ya 7 na 8 ikingiliana na kuathiri ngeli ya Kiswahili sanifu.

Wanafunzi walidhihirisha matumizi ya viambishi visivyodhihirisha uhusiano wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa nomino na vionyeshi kwa umoja na wingi. Matokeo haya yanadhibitishwa na wanafunzi ambao katika kujibu swali la jinsi na athari zinazojitokeza katika matumizi ya vionyeshi, mwanafunzi 33 alieleza kuwa;

“Kulingana na mimi, nimeona wanafunzi wakitumia vionyeshi vya Luganda, maumbo ya vipatanishi ya umoja na wingi vya Luganda katika tungo za vionyeshi vya Kiswahili kuonyesha uhusiano wa vionyeshi na maneno mengine”

Aidha, mwanafunzi huyu anaungwa mkono na mwanafunzi 20 ambaye anaeleza kuwa:

“Athari ambayo alishuhudia katika matumizi ya vionyeshi ni ya wanafunzi ya Luganda ambayo sio sahihi katika Kiswahili. Kwangu wanafunzi hao hawajui hata matumizi ya vionyeshi vya Luganda na Kiswahili.”

Matokeo haya ya mjadala yalithibitisha mwingiliano wa matumizi ya vionyeshi vya Luganda ambao uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kutokana na upekee wa kanuni ya umiliki na

usabaki ya matumizi ya vionyeshi kuonyesha uhusaino wa nomino na vionyeshi katika tungo. Hali hii ilidhihirisha kuwa Licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zinazotaofautiana katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia.

Aidha, mwingiliano huu ulitokana na mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya nadharia ya umilikifu na unganifu ambao hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Matokeo ya mijarabu ya wanafunzi kuhusiana na kutumia vivumishi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vionyeshi katika tungo ulidhihirisha utokeaji huu wa mihimili ya ubia na upatanifu. Matokeo ya mijarabu ya wanafunzi kutokana na data za mijarabu ilidhihirisha hali ya ukiukaji wa utaratibu wa kutumia viambishi vipatanishi vinavyoambishwa kwenye mzizi hutegemea nafasi ya nomino (mahali ilipo nomino) na viambishi vipatanishi msingi ambavyo vinatawaliwa na nomino kwa mujibu wa mihimili wa sarufi bia na upatanishi wa kuzingatia sheria na kanuni za matumizi ya maumbo msingi ya nje na ndani. Viambishi vipatanishi msingi ambavyo huonyesha uhusiano baina ya nomino inayokumushwa na vionyeshi kutegemea mahali ilipo nomino na mzungumzaji kama inavyojitokeza katika Data Na.(6.34):

Luganda

1. Ngeli za n-zi (e-zi) na M-wa (a-wa)

- a) *Paka hii enapenda kucheza*
- b) *Mbuzi hizi/ zile zinakula sana*

2. Ngeli ya mu-mi (gu-gi) na mu-mi(u-i)

- a) *Mlima hugu/ gule guna kima*
- b) *Nipatiye mugati gule/ guli*
- c) *Hugwo mukeka ni gwange*

3. Ngeli ya [ki-bi na ki-vi]

- a) *Bikopo hibi/bile binapendeza*
- b) *Viatu hibyo ni bya nani?*
- c) *Viatu zile zinapendeza*
- d) *Nilimpatia zile vitu ulimpa*

4. Ngeli za [li-ma (li-ga) na ji-ma (li-ya)]

- a) *Mandazi huyo mutamu sana*
- b) *Magari hizi/hizo/zile zimeanguka*

Kiswahili Sanifu

Paka hawa wanapenda kucheza

Punzi hawa wanakula sana

Mlima huu/ule una kima

Nipe mkate huo/u

Mkeka huo ni wangu

Vikombe hivi vinapendeza

Viatu hivyo ni vya nani

Viatu hivyo vinapendeza

Nilimpa vitu vile ulivyonipa

Maandazi hayo ni matamu sana

Magari haya/ hayo/yale yameanguka

Asili: Data kutokana na mijarabu ya kisarufi nyanjani.

Matokeo haya yanashadidiwa na Obara, (2014) na Kisakwah (2014) katika utafiti wao walibainisha makosa ya upatanishi wa kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili kinyume na kuwa kivumishi hiki huambishwa VPM kuleta upatanishi wa kisarufi husika. Kwa mfano Obara (2014) anaeleza kuwa: Mwanafunzi anapoteua kiambishi kipatanishi kisichofaa huwa amefanya kosa la kisarufi. Ili mwanafunzi aweze kutunga sentensi sahihi zinazofuata kanuni za kisarufi za Kiswahili Sanifu sharti atue kiambishi kipatanishi kinachowiana na maneno mengine katika sentensi.

Utafiti huu unakubaliana na matokeo ya utafiti kuwa wanafunzi walifanya makosa na kusababisha athari za mwingiliano wa kanuni za Luganda katika Kiswahili sanifu kwa kutumia viambishi vipatanishi visivyofaa wakati wa kutumia vivumishi vionyeshi.

6.2.2.3.3 Umiliki na usabaki wa nomino na vivumishi vya –a unganifu

Kila nomino huwa na vambishi patanishi vya msingi vinavyotofautiana kutokana na mfumo pamoja na maumbo ya kimofosintaksia ya ngeli nomino na kivumishi chake. Ukiukaji wa kuambatisha viambishi vya kiupatanishi usiofaa huweza kupotosha uhusiano wa nomino na vivumishi na hivyo kupotosha usanifu wa matumizi ya lugha husika (Obara, 2014; Kisakwah, 2014; Kirabi, 2015; Oduor, Inyani na Kobia, 2017) kama katika Data Na. (5.20 Uk. 173) Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kutokana na matokeo ya mijarabu ya wanafunzi kuhusiana na matumizi ya kivumishi cha –a unganishi miongoni mwa wanafunzi, wakijibu swali la kueleza jinsi mwingiliano wa kanuni ya umilikifu na unganifu inavyojitokeza katika matumizi ya vionyeshi vya Kiswahili, ilibainika kuwa athari za mwingiliano wa matumizi ya –a unaganishi ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Wakijadiliana juu ya matokeo ya mijarabu ya data Na. (6.33, Uk. 319), katika maelezo ya kutambua athari zilizobainika katika mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi, mwanafunzi 8 alieleza kuwa:

“Wanafunzi walihamisha –a unganifu, kubadilisha viunganishi mwafaka vya Kiswahili sanifu na kutumia vya –a unganifu ya Luganda katika Kiswahili sanifu.”

Uchanganuzi wa mijadala ulitambua kuwa kutokana na mshabihiano wa kimofolojia na kisintaksia katika kuambatanisha mzizi wa kivumishi cha [-a] unganifu kinachowakilishwa na kiambishi tamati [-a], wanafunzi walihamisha, kujumlisha na kubadilisha maumbo ya viambishi vipatanishi msingi vya ngeli husika ya Luganda na Kutumia VPM vya Luganda. Aidha, Tofauti za maumbo maumbo ya viambishi awali vipatanishi vya msingi vya ngeli nomino vinavyoambatanishwa kwenye mzizi huu baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana, ulisababisha mwingiliano wa kimatumizi wa kivumishi cha –a unganifu na

kuathiri matumizi bora ya vivumishi vya -a unganifu vya Kiswahili sanifu kama inavyojadiliwa katika data Na. (6.35A-E)

A. Ngeli ya [N-zi-(e-zi) na m-wa (a-wa na Ki-vi)]

| Luganda | Kiswahili |
|--|--------------------------------------|
| a) Kondoo ya Kasibante imepoteya | Kondoo wa Kasibante amepotea |
| b) Kondoo za Kasibante zimepoteya | Kondoo wa Kasibante wamepotea |
| c) Viongozi vya shule yetu | Viongozo wa shule yetu |

Asili: Data kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani

Katika mijadala ilibainikiwa kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walihamisha –a unganifu ya ngeli ya 9 na 10 na kuitumia katika ngeli ya 1 na 2 hasa wakisikia majina ya wanyama kwa sababu ngeli ya 9 na 10 ya Luganda ni ya wanyama na vitu vinginevyo, pia wanafunzi walishindwa kutambua uainishaji wa kisemantiki wa nomino za wanyama na binadamu na kujipata wanahamisha –a unganifu ya ngeli ya 9 na kumi na 7 na 8 katika matumizi ya a-unganishi ya ngeli ya 1 na 2.

B. Ngeli za [mu-mi-(gu-gi) na m-mi-(u-i)]

| Luganda | Kiswahili |
|---|--------------------------------------|
| a) Mupira gwa gari kumepasuka | Mpira wa gari umepasuka |
| b) Mioyo gya watu ni mubaya sana | Mioyo ya watu ni mibaya sana. |

Asili: Data kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani

Wanafunzi walihamisha moja kwa moja VPM vya –a unganifu ya ngeli ya 3 na 4 na kuitumia katika Kiswahili sanifu. Hali ambayo ilikiuka kanuni mwafaka ya kutumia VPM vinavyokubalika na hivyo kuathiri matumizi ya –a unganifu ya Kiswahili sanifu.

C. Ngeli ya li-ma (li-ga) na ø/Ji-ma (li-ya)

| Luganda | Kiswahili |
|--------------------------------------|-----------------------------------|
| a) Jicho lya mutoto limevimba | Jicho la mtoto limevimba |
| b) Macho ga mutoto gamevimba | Macho ya watoto yamevimba. |
| c) Machungwa ga Kenya matamu | Machungwa ya Kenya ni matamu |

Asili: Data kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani

Wanafunzi walishindwa kudondosha irabu katika kiambishi ngeli na badala yake wakaingiza kanuni ya uyeyushaji kama inavyofanywa katika Luganda na kutumia kivumishi cha –a unganifu [lya] kisicho sanifu katika Kiswahili sanifu. Vilevile walihamisha moja kwa moja –

a unganifu ya Luganda na kuitumia katika Kiswahili sanifu. Hali ambayo ilikiuka kanuni mwafaka ya kimfosintaksia ya kuonyesha uhusiano nomino kuu na maneno mengine katika tungo.

D. Ngeli ya [ki-bi na ki-vi]

Luganda

Kiswahili

- | | |
|--|---------------------------------------|
| a) <i>Kigiko kya Sulait gimeanguka</i> | Kijiko cha Sulait Kimeanguka |
| b) <i>Bitu bya jokoni ni bichafu</i> | Vitu vya jikoni ni vichafu |
| c) <i>Vijana bya shule yetu iko wazuri</i> | Vijani wa shule yetu ni wazuri |

Asili: Data kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani

Mwingiliano mwingine uliojitokeza ni ule wa kutumia vivumishi vya –a unganifu moja kwa moja katika -a unganifu ya Kiswahili sanifu. Aidha, wanafunzi walishindwa kutambua kanuni ya kubadilisha fonimu isiyoya kaakaa gumu ya [kya] na ya kiswahili [cha]. Katika kutumia –a unganifu ya Luganda walikiuka kanuni ya ukaakishaji ambayo hutumika katika Kiswahili na vilevile kutumia fonimu /b/ badala ya /v/ hata ingawa kivumishi chenyewe ni cha ujumlishaji kanuni. Matumizi haya ya vivumishi vya –a unganifu vya Luganda katika Kiswahili sanifu uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

E. Ngeli ya [lu-en(lu-zi) na u-n(u-zi)]

- | | |
|--|-------------------------------------|
| a) <i>Ulimi lwa nyoka lunatisha</i> | Ulimi wa nyoka unatisha |
| b) <i>Lugha lwa mwalimu ni ngumu</i> | Lugha ya mwalimu ni ngumu |
| c) <i>Muimbo lwa Chameleon unapendwa</i> | Wimbo wa Chameleon unapendwa |

Asili: Data kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi nyanjani

Data hii vilevile unadhihirisha uhamishaji wa moja kwa moja wa vivumishi vya –a unganifu vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya –a unganifu vya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yalikiuka matumizi bora ya vivumishi vya –a unganifu na hivyo kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kimaandishi na kimazungumzo. Matumizi ya aina hii yaliathiri Kiswahili sanifu kwani katika matumizi wanafunzi walitumia viambishi visivyo na hivyo kusababisha athari za kitahajia na kimaendelezo, makaosa ya upatanifu wa kisaru baina ya nomino kuu na maneno mengine katika tungo. Hali hii ilikiuka kanuni ya utawala na unilikifu kwa sababu ya kikikukwa kwa masharti ya matumizi ya Kiswahili sanifu.

Matokeo haya yanashadidiwa na Ngamau, (2004), Mwamzandi, (2018), Kirabi, (2015), Lukamika, (2015), Chomi (2003), Mirikau, (2008) Habwe & Karanja (2004) na Obara (2014) ambao wanaeleza kuwa Vivumishi vionyeshi ni vitatu ambavyo huwakilishwa na mofu (maumbo) Vivumishi vionyeshi ni aina ya vivumishi vinavyotumika kudhihirisha nomino

kutegemea nafasi alipo mzungumzaji. Maelezo yao yanaungwa mkono na Leah & Sseguya (2015) na Philipo, (2017) ambao wanafafanua kuwa Mofu zinazohusika ni mofu za kisarufi zinazodhihirisha upatanishi wa kisarufi, mizizi ya uundaji, nafsi, ngeli na idadi ya umoja na wingi. Utafiti huu ulibaini uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni ya umiliki na usabaki baiana ya Luganda na Kiswahili sanifu licha ya kuwa lugha hizi ni za nasaba moja. Ilibainisha kuwa matumizi ya viambishi vipatanishi vya kimofolojia na kisintaksia katika uundaji wa viambishi vipatanishi vya msingi vilivyopachikwa kwenye mizizi ya vionyeshi kutegemea kundi nomino ambamo nomino husika huainishwa vilitofautiana katika kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu.

6.2.2.3.4 Umiliki na usabaki wa nomino na vivumishi vya sifa

Vivumishi vya sifa huundwa kwa kiambishi patanishi cha msingi na mizizi. Kimofosintaksia vivumishi vya sifa lazima viambikwe viambishi ambavyo huzingatia sifa za kisarufi za upatanishi wa kisarufi baina ya nomino kuu na kivumishi cha sifa chenyewe kama neno au kategoria ya kimofosintaksia katika tungo (Chomi, 2003; Kiyinikibi 2021; Mgullu 1999).

Matokeo ya mijarabu ya kisarufi kutokana matumizi ya vivumishi vya sifa iligundua kuwa kanuni ya umiliki na usabaki ilikiukwa na wanafunzi ambao L1 Luganda. Uchanganuzi wa athari za mwingiliano zilibainisha kuwa wanafunzi walihamisha, kuchanganya, kubadilisha na kujumlisha viambishi vipatanishi vya Luganda kimofolojia na kisintaksia na kuvitumia katika vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu viambishi vilivyopachikwa kwenye mzizi wa kivumishi havikupatana kisarufi na viambishi vya kiima au nomino kuu katika KN kama katika data Na.(6.36)

| <i>Luganda</i> | <i>Kiswahili Sanifu</i> |
|---|---|
| g) Watu <i>mingi/bengine</i> wamekuja kulala | Watu <i>wengi/wengine</i> wamekuja kulala |
| h) Chakula <i>mingi/mingine</i> imepikwa | Chakula <i>Kingi/kingine</i> kimepikwa |
| i) Maji <i>mingi/maingine</i> inamwagika | Maji <i>mengi/mengine</i> yanamwagika |
| j) Maji <i>maangi/maingi/mangine/maingine</i> | Maji <i>mengi/ mengine</i> |
| k) Viberiti <i>bingi/ bingine</i> | Viberiti <i>vingi/ vingine</i> |
| l) Ugonjwa <i>mingi/mingine</i> | Ugonjwa <i>mwingi/mwingine</i> |

Asili: Data kutokana mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi

Kwa mujibu wa mihimili ya mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilkifu na unganifu, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili licha ya kuwa lugha za nasaba moja zinaotumia kanuni ya umiliki na usabaki, zinadhihirisha tofauti katika matumizi ya kanuni

hii. Hii inatokana na kauli kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Data hii ilibainisha kuwa Kiswahili hutumia kiambishi [m-] kwenye mizizi ya nomino za viumbe hai ambavyo hupatikana katika ngeli ya 1 na 2. Pia, kiambishi hiki hutumika katika ngeli ya 3 umoja. Hata hivyo wanafunzi ambao L1 ni Luganda walitumia kiambishi hiki na kuongeza irabu [u] mbele yake na kutumia katika kukumusha nomino ambazo si hisivu na nomino katika ngeli ya 3 kwa umoja katika matumizi yao. Hiki ni kiambishi awali cha nomino katika ngeli ya kwanza umoja. Mwingiliano mwingine ulikuwa wa ujumlishaji wa kuambisha vivumishi vya sifa vya mkopo ambavyo hata Luganda huwa hawaambishi viambishi vipatanishi vya msingi kama inavyojitokeza katika Data Na.(6.37) kutokana na mijarabu ya wanafunzi.

Matumizi ya lala na –ingine

Luganda

- g) *Watu waingine wanakuja*
- h) *Bintu bingine binasumbua*
- i) *Kalamu ingine*
- j) *Nyumba ingine*
- k) *Tunayenda kucheza mchezo ingine*
- l) *Gari ingine inakuja*

Kiswahili sanifu

- Watu wengine wanakuja
- Vitu vingine husumbua
- Kalamu nyengine
- Nyumbe nyingine
- Tunaenda kucheza mchezo mwingine
- gari linguine linakuja*

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi kutoka nyanjani

Mwingiliano mwingine ulijitokeza katika ngeli ya 7 na 8 ambapo wanafunzi walibadilisha kiambishi patanishi cha ngeli ya 8 ya Kiswahili sanifu [vi] na kutumia KPM cha Luganda [ba-] katika mazungumzo na maandishi. Hali hii ilidhihirisha uhamishaji wa maumbo ya VPM kutoka Luganda hadi Kiswahili sanifu. Hali hii iliathiri usanifu wa matumizi ya vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi Na.(6.37).

Mwingiliano wa aina hii katika matumizi ya Kiswahili yalitokana na kuwa; hata ingawa vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli kiupatanifu, mfumo wa mpangilio wa nomino wa Luganda na Kiswahili kiasili unatofautiana na Kiswahili hivyo kila lugha kudhihirisha viambishi vinavyotofautiana kimofosintaksia. Pia, viambishi vinavyotumika huathiriana kifonolojia na kujenga viambishi vipatanishi vya msingi vinavyotofautina na

VPM vya Kiswahili sanifu kutokana na michakato tofauti inayotumika wakati fonimu zinapotokea katika mazingira ya vokali na konsonanti ya mizizi.

Matokeo haya yalikiuka maelezo ya Oichoe, (2005), Mukuthuria (2004), Mbwillow, (2017) ambao wanadhihirisha kuwa; Vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli vya upatanishi wa kisarufi vinavyohusiana na sifa ya nomino iliyotajwa kila mara vinapotumika. Hii ina maana kuwa viambishi vipatanishi msingi vinavyokaririwa kwenye nomino kuu ndivyo vinavyokaririwa katika vivumishi vya sifa vya Kiswahili sanifu ijapokuwa vivumishi vya sifa vya mkopo. Matumizi ya kivumishi hiki yalikiuka kanuni ya kimofosintaksia ya vivumishi vya sifa ambavyo lazima viambikwe viambishi ambavyo huzingatia sifa za kisarufi za upatanishi wa kisarufi baina ya nomino kuu na kivumishi cha sifa chenyewe kama neno au kategoria ya kimofosintaksia katika tungo.

6.2.2.3.5 Umiliki na usabaki wa nomino na vivumishi vya idadi isiyodhahiri

Kimofosintaksia, vivumishi vya idadi isiyodhahiri vya Luganda na Kiswahili sanifu vimeundwa kwa kiambishi awali ambacho pia ni kipatanishi cha wingi wa nomino kinachowekwa kabla ya mzizi wa kivumishi na mizizi ya vivumishi ambavyo hubeba maana ya kileksika ya kivumishi cha idadi ya nomino inayotajwa Uchunguzi wa utafiti huu ulibaini kuwepo kwa mwingiliano wa kanuni wa kuhamisha VPM vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Idadi isiyodhahiri kama katika data Na.(6.38 Uk. 328).

Matumizi ya Onna na ote

Luganda

- a) *Watu yote nasimama*
- b) *Amekula chakula yangu yote*
- c) *Magari zote zimeenda*
- d) *Wanafunzi wawote/boote*
- e) *Penda yeye na moyo gwako gwote*

Kiswahili Sanifu

- Watu wote wamesimama
- Amekula chakula changu chote
- Magari yoye yameenda
- Wanafunzi wote
- Mpende kwa moyo wako wote

Asili: Data kutokana na mjarabu ya kisarufi ya wanafunzi, (2021)

Uchanganuzi wa data ya mjarabu ya kisarufi ya wanafunzi ambao L1 ni Luganda ilibainisha utokeaji wa athari za wanafunzi kuhamishi, kujumlisha kanuni, kubadilisha VPM vya Kiswahili, kutozingatia kanuni ya kifonolojia wakati wa uambishaji viambishi na kutumia viambishi vya Luganda moja kwa moja katika vivumishi vya idadi isiyodhahiri vya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yalikosa kuonyesha utawala na ufungami wa nomino kuu na vivumishi vya idadi isiyokamili pamoja na maneno mengine katika tungo. Hali hii ilaithiri

sarufi ya Kiswahili sanifu na kujenga lugha kadri isiyo ya kiswahili sanifu kwa sababu ya kuchanganya VPM vya Kiswahili na Luganda sanifu katika matumizi ya vivumishi vya idadi isiyokamili.

Katika mijadala ya wanafunzi wakijibi swali la kueleza jinsi mwingiliano wa kanuni ya umiliki na usabaki inavyoathizi matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri kutokana na (6.38, Uk. 328) ilidhihirisha kuwa wanafunzi waliambisha kwenye mzizi [-ingi na -ingine] wa kivumishi cha idadi isiyodhahiri kiambishi [mi-]. Mwanafunzi 23 akijibu swali hili alieleza kuwa:

“Wanafunzi wengi hujumlisha kanuni hii kwa kutumia kivumishi [mingi] kwa kila nomino kuu bila kuzingatia utaratibu na maumbo awali ya nomino kuu katika tungo.”

Kulingana na mwanafunzi 17;

“Hali hii ya kuambishi kiambishi kisichonyesha uhusiano baina ya nomimo na kivumishi kulidhihirisha ukosefu wa ufasaha na kusababisha athari za kisarufi za upatanishi wa kisarufi baina ya nomino kuu na kivumishi.”

Mathalani, wanafunzi waliutumia mzizi [-ingine] bila kuambisha viambishi awali vya upatanishi wa kisarufi. Matumizi haya yanadhihirisha mwingiliano wa kutumia viambishi vya kimuktadha kwa njia ya ujumlishaji, udondoshaji na kuhamisha VPM vya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo kamili ya Kiswahili sanifu.

Athari nyingine iliyojitokeza kulingana na data Na (6.38, Uk. 328) ni ya wanafunzi kuhamisha kiambishi kipatanishi cha ngeli ya Luganda ya [n-] kwa umoja na kuongeza kiambishi cha ngeli chenye asili ya Luganda katika kiambishi [chache] ambacho kwa mujibu wa kanuni ya kimofosintaksia hakistahili kuambishwa katika (a) na kutumia kiambishi cha ngeli ya udunishaji wa vitu ya [ka-bu] katika kirai cha (b). Matumizi haya yalidhihirisha mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya vivumishi vya idadi vya Kiswahili sanifu.

Mijadala ya wanafunzi wakijibu jinsi athari ilivyojitokeza katika matokeo ya mijarabu ya wanafunzi kutokana na kifaa cha orodhahakiki chenye sifa ya kimofosintaksia ya matumizi ya vivumishi vya idadi isiyo dhahiri, mwanafunzi 2 akijadili mfano wa data (c hadi f).” alieleza kuwa:

“Wanafunzi walidondosha viambishi vipatanishi vya ngeli ambavyo vilistahili kuambishwa kwenye mizizi ya kivumishi [-ingine].”

Pia, mwanafunzi 25 akijadili data (b) alieleza kuwa;

“Wanafunzi walidondosha kiambishi cha ngeli sahihi cha ngeli ya 7 na 8 na kutumia kiambishi cha wingi cha ngeli ya 8 ya Luganda katika matumizi ya vivumishi vya Kiswahili sanifu.”

Matokeo haya yalionyesha jinsi Luganda na Kiswahili sanifu ilivyo lugha mbili tofauti licha ya kuwa lugha za nasaba moja kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky, (1981). Katika kujadili matokeo ya mijarabu ya kisarufi Na.(6.26, Uk. 310) cha kutumia kiambishi cha idadi ya jumla [-ote], ilibainika kuwa wanafunzi walijumlisha kanuni na kuhamisha viambishi vipatanishi vya ngeli ya Luganda katika matumizi ya kivumishi [-ote] kama katika mfano wa (e), (b) na (c). Pia, wanafunzi walijumlisha kanuni ya kuongeza viambishi vipatanishi vya wingi kwenye kiambishi [-ote/ kwa mfano katika (d) ama kutumia kiambishi awali cha wingi cha ngeli ya 1 na 2 cha Luganda [ba-]. Matokeo yaliyojitokeza yalidhihirisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha za nasaba moja zilizotumia kanuni moja wa umiliki na usabaki, lugha hizi zilidhihirisha tofauti katika matumizi ya kanuni hii. Utafiti huu ulibaini kuwa mwingiliano wa matumizi ya kanuni hii ulisababisha athari katika matumizi ya Kiswahili sanifu. mwingiliano ulitokana na kufanana kwa matumizi ya kanuni na uambishaji wa maumbo wakilishi ya viambishi vya kuonyesha uhusiano wa maneno kumiliki na kusabaki maneno mengine katika tungo. Aitha tofauti ilikuwa ya kimaumbo ambayo iliathiri usanifu wa matumizi ya Kiswahili sanifu.

6.1.2.4 Kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji wa vivumishi katika tungo virai

Kanuni hii hushikilia kuwa: Neno kuu katika utungo huchagua kuathiri maneno mengine kutegemea mazingira ambamo nomino au neno kuu tajwa hutokea. Kulingana na kanuni hii, nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo kama inavyojitokeza katika data ya maktabani Na.(5.20, Uk. 173).

Matokeo ya data za maktabani wa lugha za Kibantu kulingana na Rijkhoff, (1986), Kiyinikibi (2013:2021) na Abudonia (2014), ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kanuni hii katika utaratibu wa kupanga vipashio vya kimofosintaksia katika tungo. Aidha, ilibainika kuwa katika Luganda na Kiswahili sanifu, nomino hutokea mwanzoni mwa tungo kama neno kuu ikifuatwa na vivumishi. Ukuu wa utokeaji wa vivumishi na maneno mengine katika tungo hufuatwa kanuni ya muundo virai ambao huonyesha uhusiano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo. Neno kuu ni neno linalobeba hadhi ya ukuu au ujumbe

wa kirai ambalo hutangulia vivumishi wakati wa matumizi. Utokeaji wa vivumishi katika tungo hutokana na dhima ya vivumishi ya kueleza zaidi juu ya nomino na vitenzi au maneno mengine katika tungo virai kama ilivyoelezwa na Abudonia, (2014).

Pia, ilibainika kuwa vivumishi hutokea karibu na baada ya nomino au neno kuu ila ikitokea na vivumishi vingine vinavyosisitiza ujumbe, utokeaji wake ni wa kimuktadha (kipragmatiki), unaotegemea dhima ya kategoria inayobeba ujumbe kwa mujibu wa msemaji au mwandishi (Abodunia, 2014). Katika uchunguzi wa kutambua utokeaji wa aina mbalimbali za vivumishi vinavyotumika katika maandishi na mazungumzo, utafiti huu uligundua kuwa vivumishi vyote hutokea baada ya neno kuu mbalo ni nomino katika KN, ila kutanguliwa kwa aina fulani ya kivumishi kutangulia kivumishi kingine kulitokana na dhima, ujumbe, muktadha na dhamira ya mzungumzaji au mwandishi. Matokeo haya yanadhihirsha kuwepo kwa uwiano wa matumizi ya vivumishi katika Luganda na Kiswahili. Licha ya kuwepo kwa mwingiliano, mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya ya nadharia ya umilikifu na unganifu huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo ya data za mijarabu kwa mujibu wa mihimili ya ubia na ulibaini kuwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda walitumia sana matumizi ya vivumishi kipragmatiki na kuhamisha miktadha ya matumizi ya Luganda katika Kiswahili hasa kwa vivumishi kutangulia neno kuu katika tungo virai. Mwingiliano huu ulijitokeza zaidi katika matumizi ya nomino kuu na vivumishi vionyeshi kama inavyojitokeza katika data Na. (6.39).

Luganda

- a) *Chai hii si nzuri*
- b) *Mtoto huyu anasubua sana*
- c) *Mwalimu huyo anatufunza*
- d) *Daktari yule ananijua*
- e) *Ktabu hiki kinauzwa*

Kiswahili sanifu

- Huyo*** chai si muzuri
- Huyu*** mtoto husumbua
- Huyo*** mwalimu nafundisha sisi
- Huyo*** mudaktari najua mimi
- Hiki*** kitabu kinauzwa

Asili: Data kutokana na, mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi (2021)

Matumizi haya yalijitokeza kusisitiza namna vivumishi vionyeshi vinavyotumika katika Luganda sanifu. Matumizi haya ni kinyume na Kiswahili ambacho kionyeshi kikitangulia

nomino kuu basi kionyeshi hicho hufanya kazi ya kiwakilishi cha nomino husika (Lusekelo, 2017). Katika Luganda miundo yote miwili hufanya kazi moja ya dhima ya kuwasiliana na hutegemea muktadha. Wanafunzi walikiuka kanuni ya vivumishi kuchukua nafasi karibu na nomino kama neno kuu katika tungo virai hasa katika Lugha za Kibantu (Rijkhoff, 1986). Kanuni inayodai kuwa: Nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo. Aidha, matumizi hayo ya wanafunzi wa Luganda katika matumizi ya nomino na vivumishi yalikiuka utaratibu wa lugha za Kibantu ulioelezwa na Heine (1976) ya kuwa lugha zote za Kibantu hufuata utaratibu wa kiima kufuata kitenzi katika KN; Yambwa kufuata kitenzi; vikumushi vya nomino kama vile vivumishi vya idadi, vimilikishi, vionyeshi na virai virejeshi huja baada ya nomino; vivumishi vimilikishi hufuata vivumishi vinginevyo vinavyotokea katika tungo virai na vishazi na vielezi kutokea baada ya vitenzi na vivumishi.

Matokeo ya mijadala kutokana na mijarabu ya kisarufi kuhusu matumizi ya vivumishi ilibaini kuwa katika Luganda hutokea kutokana na ukuu na hadhi inayobebwa na kivumishi katika KN kama inavyojitokeza katika data (6.40) kutokana na mijadala ya wanafunzi.

- a) **Ono** omwana mulungi **Bano** abaana balungi [*dhima ya kuonyesha*]
W N V W N V
Huyu mtoto mzuri **Hawa** watoto wazuri [*dhima ya kiwakilishi*]
W N V W N V
- b) Omwana **ono** mulungi Abaana **bano** balungi [*dhima ya kuonyesha*]
N V (kio) V N V(Kio) V
Mtoto **huyu** mzuri Watoto **hawa** wazuri [*dhima ya kuonyesha*]
N KV V N V(kio) V
- c) Omusomesa **wange** alezze emmotoka **eyo** Abasomesa **waffe** balezze mmotoka **ezo**
N V T N V(vio) N V T N V(Kio)
[*Dhima ya umilikishi na onyeshi*]
Mwalimu **wangu** alileta gari **hilo** Walimu **wetu** walileta magari **hayo**
N V T N Kio N V T N Kio
[*Dhima ya kimilikishi tendaji*]
- d) Omwana **omugezi** ayiise ebigezo Abaana **abagezi** bayiise ebigezo
Mtoto **mwerevu** amepita mitihani Wanafunzi **werevu** wamepita mitihani
- e) Omwana **wange** oyo muwanvu nnyo. Abaana **bange** abo bawanvu [*dhima ya kimo*]

Mtoto wangu huyo ni mrefu sana. Watoto wangu hao ni warefu sana. [dhima ya umilikaji na kimo].

Data hii ilidhihirisha kuwa vivumishi vyote vilitokea baada ya nomino kuu na sifa za kisarufi za utokeaji wake ulitokana na neno kuu. Hata hivyo, utokeaji wake ulitokana na muktadha au kanuni ya pragmatiki yaani kutegema dhima, hadhi na ujumbe unaowasilishwa. Ufasiri wa dhima ya tungo kutegemea muktadha wa Luganda uliathiri matumizi ya vionyeshi vya Kiswahili sanifu na kusababisha mwingiliano wa kanuni za matumizi ya vivumishi vya Luganda katika Kiswahili sanifu kama inavyodhihirishwa. Matokeo haya yanakubaliana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungamanisho ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

6.1.3 Mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili Sanifu

Kwa mujibu wa Oichoe, (2005), Viwakilishi nafsi ni maneno huru na funge ambayo hufanya kazi kama nomino. Matokeo ya uchunguzi wa kazi za Oichoe, (2005), Kisakwah, (2014), Obara, (2014), Rose, (2009) na Leah & Sseguya, (2015), Matasi & Furaha, (2016) yalidhihirisha kuwa viwakilishi vya nafsi vya Luganda na Kiswahili vimegawanywa kuzingatia nafsi kuu tatu. Viwakilishi hivi nafsi vimegawanyika katika idadi ya umoja na wingi vikifanya dhima muhimu ya kusisitiza nomino tendaji. Licha ya kuwa viwakilishi vya nafsi huru na funge vya Luganda na Kiswahili sanifu huzingatia utaratibu wa kutegemea nafsi tatu ya umoja na wingi, maumbo ya viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu huwiana na kutofautiana. Uchanganuzi wa sheria na miundo ya matumizi ya viwakilishi nafsi kutokana na mihimili ya ubia na upatanishi ilibainisha uwiano na kutofautiana kwa kanuni ya kimofosintaksia ya matumizi ya viwakilishi nafsi.

6.1.3.1 Kanuni ya umiliki na usabiki

Kwa mujibu wa matumizi ya kanuni hii, nomino hurejelewa kianafora kama nomino kapa ambayo hujidhihirisha katika ubongo wa msikilizaji au msemaji. Maumbo haya yanapotumika hurejelea nomino tajwa awali katika mawasiliano. Vilevile, kanuni hii ya umiliki na usabiki, hushikilia kuwa viambishi vya nafsi lazima vitumike kulingana na nafsi ya nomino inayorejelewa katika kiima/KN na hujitokeza katika KT kama anafora na kisabiki

chake kwa njia ya muungano wa maumbo (viwakilishi) ya nafsi na wakati ambao huwekwa kabla ya mzizi wa vitenzi. Viambishi hivi lazima vidhihirishe uhusiano wa kisarufi kati ya nomino tajwa (kuu) na maneno mengine katika tungo.

Data ya mjarabu ya kisarufi ya wanafunzi ilibaini kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili hutumia kanuni moja ya uambishaji wa viwakilishi nafsi kwenye vitenzi, tofauti za kimaumbo zilisababisha athari za mwingiliano wa kanuni ya umiliki na usabaki miongoni mwa maandishi na mazungumzo ya wanafunzi kama inavyojitokeza katika data Na. (6.41)

1. Udondoshaji wa silabi ya nafsi [mi, we na ye]

Luganda

Kiswahili Sanifu

a) *Mi naona wewe njiani*

Mimi ninakuona njiani

b) *We aliona mimi wapi*

Uliniona wapi? Wewe uliniona wapi?

c) *Ye aliomba pesa mingi*

Aliomba pesa nyingi Yeye aliomba pesa nyingi

Asili: Data za mjarabu ya wanafunzi nyanjani

Mijadala ya matokeo ya mjarabu ya kisarufi (6.41) ya kutambua athari za mwingiliano, utafiti huu ilidhihirisha athari za uhamishaji wa kanuni, ufasiri wa matumizi ya viwakilishi vya nafsi vya Luganda na udondoshaji wa maumbo ya viwakilishi katika Kiswahili sanifu.

Mwanafunzi 16 akijadili mwingiliano wa kudondosha viwakilishi vya nafsi huru vya nafsi ya kwanza, pili na tatu na jinsi inavyoathiri matumizi ya Kiswahili, alieleza kuwa, wanafunzi ambao L1 hutumia viwakilishi nafsi kwa njia ya uhamishaji wa kanuni. Iitambulika kuwa;

“Wanafunzi hutafsiri viwakilishi vya nafsi na jinsi vinavyotumika katika Luganda ambavyo vina silabi moja tu yaani [nzze], [gwe] na [ye] na kuihamisha katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika maandishi na mazungumzo. Wanafunzi walitumia viwakilishi [mi] badala ya [mimi]; [we] badala ya [wewe] na [ye] badala ya [yeye].”

aidha, Katika matumizi haya, ilibainika kuwa silabi ya pili ya viwakilishi huru ilidondoshwa kufuatwa utaratibu wa matumizi ya Luganda badala ya Kiswahili sanifu. Wanafunzi walikosa kutumia vyema viwakilishi nafsi yambwa au virejeshi na badala yake wakatamia viwakilishi nafsi huru kama ilivyo katika mifano ya a) na b). Matumizi haya yalikiuka kanuni ya umiliki na usabaki kwa sababu, kiwakilishi cha kiima huru kimedondosha silabi na kiwakilishi cha kumilikiwa na kisabaki kudondoshwa kama ilivyo katika mfano wa a). Katika mfano wa b), kiwakilishi nafsi cha kumilikiwa na kisabaki [kiwakilishi huru cha pili] kilichotumika ni kiwakilishi nafsi cha tatu umoja. Kimewekwa katika nafsi tofauti kwani [a] huambishwa katika nafsi ya tatu kama kimilikiwa cha nomino kuu ya nafsi ya tatu.

Matokeo ya Mijadala kuhusu udondoshaji ilibaini dodondoshaji mwingine uliojitokeza ni katika viwakilishi nafsi huru katika tungo. katika data Na. (6.42).

2. Kudondosha njeo ya wakati uliopo na kiwakilishi nafsi ya kwanza

- a) *Mimi [-] nacheza mpira* **Mimi ninacheza**
- b) *Mimi [-]-nasema na wewe* **Mimi ninasema nawe**
- c) *Mi naona wewe njiani* **Mimi ninakuona njiani**

Asili: Data za mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Udondoshaji huu ulitokana na kufananisha kiwakilishi nafsi cha Luganda [n] na Kiwakilishi nafsi cha Kiswahili sanifu [ni-]. Mwanafunzi 3 akijibu jinsi udondoshaji ulivyojitokeza, alieleza kuwa;

“Wanafunzi walidondosha kiwakilishi cha nafsi na kuwacha kiwakilishi cha njeo [-na-] kuwakilisha nafsi ya kwanza. Vilevile, kiwakilishi hiki cha njeo kilidondosha irabu [-a] ambayo ni kiwakilishi cha nafsi ya tatu mtendaji na kuambisha kitenzi [cheza] ambacho katika Luganda ni [zanya].”

Kwa kurejelea maelezo ya mwanafunzi 3, utafiti huu ulibaini kuwa katika mfano a) wanafunzi walidondosha viwakilishi nafsi na viwakilishi njeo na kutumia kwa kuzingatia muundo wa Luganda [nze n-zannya] badala ya [ni-na- cheza]. Mfano wa pili (a) nao ulionyesha udondoshaji wa kiambishi kiwakilishi cha kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja. Matumizi haya yalikiuka kanuni ya umiliki na usababi ambapo viwakilishi nafsi huru humiliki viambishi vipatanishi ambavyo pia ni viwakilishi nafsi tegemezi.

Athari nyingine iliyojitokeza ni ile ya kutafsiri, kudondosha na kuchanganya viwakilishi nafsi kama katika mfano wa data (6.43)

1. Kutafsiri, kudondosha na kuchanganya viwakilishi nafsi

- a) *We aliona mimi wapi?* **Uliniona wapi?** **Wewe uliniona wapi?**
- b) *Ye- aliomba pesa mingi* **Aliomba pesa nyingi** **Yeye aliomba pesa nyingi**
- c) *We onacheza mupila* **Wewe unacheza mpira** **Unacheza mpira**

Asili: Data za mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Aidha, matokeo ya Mfano wa data [c] ulidhihirisha utafsiri na udondoshaji wa silabi ya kiwakilishi huru cha pili na tatu kwa kuzingatia muundo wa Luganda na kutumia kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya tatu [-a-] cha umoja ambacho hakitumiki kiusanifu katika mfano wa (a). Mthalan badala ya kuambisha kiambishi kirejeshi yambwa cha nafsi ya kwanza [-ni-] nyuma ya kitenzi baada ya kiwakilishi cha njeo, kiwakilishi huru cha nafsi ya kwanza umoja kilitumika. Katika mfano wa tatu [3], wanafunzi vilevile walidondosha silabi ya kiwakilishi huru cha nafsi ya pili umoja ambapo badala ya kutumia [wewe], walitumia silabi [we]

kimuundo kukilinganisha na cha Luganda [gwe]. Aidha badala ya kutumia kiwakilishi cha nafsi ya pili umoja cha Kiswahili sanifu [u], walitumia kiambishi cha nafsi ya pili [o] cha umoja ambacho ni cha Luganda sanifu. Matumizi haya yaliathiri usanifu wa matumizi ya viwakilishi nafsi kwa kuwa wanafunzi walichanganya viambishi viwakilishi vya Luganda katika matumizi ya viwakilishi katika tungo za kimofosintaksia za vya Kiswahili sanifu na kukiuka kanuni ya kanuni ya umiliki na usabaki kamakatika data Na.(6.44)

2. Kuhamisha viwakilishi huru vya L1 kwa L2

| <i>Athari za mwingiliano</i> | <i>Kiswahili Sanifu</i> | |
|---------------------------------|------------------------------|---------------------------------|
| a) <i>We aliona mimi wapi</i> | <i>Uliniona wapi?</i> | <i>Wewe uliniona wapi?</i> |
| b) <i>Ye aliomba pesa mingi</i> | <i>Aliomba pesa nyingi</i> | <i>Yeye aliomba pesa nyingi</i> |
| c) <i>Mwalimu oliita mimi</i> | <i>Je, mwalimu uliniita?</i> | |
| d) <i>Gwe onasema nini?</i> | <i>Wewe unasema nini?</i> | |
| e) <i>Ye acheza mupila</i> | <i>Wao banacheza mupila.</i> | |

Asili: Data za mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Mwingiliano wa [d] ulidhihirisha udondoshaji wa silabi ya pili ya kiwakilishi huru ambacho ni kisabaki cha kiwakilishi nafsi tegemezi kudhihirisha umiliki na usabaki kama katika [a, b na e]. Aidha, wanafunzi walihamisha viwakilishi vya nafsi ya tatu kwa umoja visivyo katika nafsi ya pili na hata kudondosha kiwakilishi cha njeo katika nafsi ya tatu kama ilvyo katika [e]. Wanafunzi vilevile wamehamisha viwakilishi huru vya Luganda hasa kiwakilishi cha nafsi ya pili [gwe] na [ye] ya nafsi ya tatu huru katika matumizi ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili sanifu kama katika data Na. (6.45)

3. Matumizi ya iko badala ya kiwakilishi [ni]

| <i>Mwingiliano 1</i> | <i>mwingiliano 2</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|-----------------------------|----------------------------|-------------------------|
| a) <i>Mimi iko jikoni</i> | <i>Mimi iko jikoni</i> | <i>Mimi nipo jikoni</i> |
| b) <i>We iko nalia sana</i> | <i>Wewe iko nalia sana</i> | <i>Wewe unalia sana</i> |
| c) <i>Ye iko nacheza</i> | <i>Yeye iko nacheza</i> | <i>yeye anacheza</i> |

Wanafunzi vilevile walitumia vibadala vinavyotumika katika Luganda na kuitafsiri katika Kiswahili sanifu na kutitumia katika tungo za Kiswahili sanifu. Katika matumizi haya, wanafunzi walitumia kiwakilishi nafsi cha mahali [iko] badala ya kutumia viwakilishi nafsi huru vya nafsi ya a, b na c umoja.

Kwa mujibu wa data hii ilidhihirishwa kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha za nasaba moja zenye mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya umiliki na usabaki wa viwakilishi nafsi, Lugha hizi ni lugha mbili tofauti kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungamanisho ambayo inashikilia kuwa kanuni zilezile za

kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Mhimili wa pili wa upatanifu ulihusika pia katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu a sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo haya yanashadidiwa na Oichoe, (2005), Kisakwah, (2014), Obara, (2014), Rose, (2009) na Leah & Sseguya, (2015), Matasi & Furaha, (2016) wanaobainisha kuwa kila kiwakilishi nafsi katika Luganda na Kiswahili kina kiambishi cha upatanishi wa kisarufi ambacho huambishwa mwanzoni mwa vitenzi. Kiambishi hiki hutokea au huwekwa mwanzoni mwa kitenzi kurejelea nomino tendaji au kiima na yambwa iliyotajwa kuepokana na marudio. Aidha, matokeo haya yalikiuka kanuni ya umiliki na usabaki kulingana na Wani (2010) na Oduor na Wenzake, (2017) wanaofafanua kuwa matumizi ya viwakilishi nafsi vinavyotumika, lazima kiwakilishi kikubaliane na kisabaki chake katika jinsia na idadi. Hii ina maana kwamba nomino iliyo katika umoja, lazima iwakilishwe na kiwakilishi katika umoja.

Tofauti na matokeo ya awali, utafiti huu uligundua kuwa licha ya kuwepo kwa mwingiliano wa kanuni na vipashio vya kimofosintaksia vya viwakilishi nafsi, maumbo ya viwakilishi yaliyotumika hayakuonyesha usabaki na umiliki kwa sababu maumbo hayo hayakuwa ya Kiswahili sanifu. Athari za Udondoshaji, uhamishaji na uchanganayaji wa maumbo ya viwakilishi huru na tegemezia katika virai yaliathiri usanifu wa Kiswahili sanifu kwani yalikiuka umb, muundo na nafasi ambapo ilitahili kutumika.

6.1.3.2 Kanuni ya urejeshi

Kanuni ya urejeshi wa nomino hutokea kwa kuzingatia viwakilishi vya nafsi na ngeli za nomino ambapo viambishi vya urejeshi huwekwa baada ya njeo na kabla ya kitendo vikichukua maumbo yake kutokana na ama kiima husika au nafsi (Rijkhoff 1986; Kyagaba 1996 na Abudonia 2014). Viwakilishi nafsi hutokea katika kundi tenzi kwa njia ya ujirejeleaji na urejeshi kuwakilisha yambwa na kiima. Virejeshi hivi hutokea baada ya njeo na kabla ya kitenzi husika kutegemea nafsi na ngeli za nomino kuwakilisha idadi na ngeli kwa umoja na wingi. Kimofosintaksia viwakilishi nafsi huzingatia mpangilio maalumu ambapo hata kikiambikwa viambishi vinginevyo viambishi hivi huwa haviathiriki kwa sababu vinabeba kiima na yambwa ya tungo kama inavyojitokeza katika data za jedwali (6.3):

Jedwali 6.3: Viwakilishi vya nafsi na ngeli rejeshi

| Kiwakilishi nafsi | Kiambishi kirejeshi yambwa | Ngeli | Kiambishi kirejeshi |
|-------------------|----------------------------|--------------|---------------------|
| | Kiswahili sanifu | | |
| Mimi - Sisi | -ni- -tu- | Ngeli ya 1-2 | m-wa |
| Wewe - Nyinyi | -ku- -wa-/ | Ngeli ya 3-4 | u-i |
| Yeye - wao | -m- -wa- | Ngeli ya 5-6 | li- ya |
| | Luganda sanifu | | |
| Nze - Ffe | -n- -tu- | Ngeli ya 1-2 | a-ba |
| Ggwe - Mwe | -ku- -ba- | Ngeli ya 3-4 | gu-gi |
| Ye - bba | -mu- -ba- | Ngeli ya 5-6 | li-ga |

Asili: Data kutokana na Kyagaba (1996) Sakwa na wenzake (2013)

Uchanganuzi wa data ya mijadala ya wanafunzi kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi kuhusu matumizi ya viwakilishi virejeshi vya Kiswahili sanifu na wanafunzi ambao L1 ni Luganda, utafiti huu ulidhihirisha athari za mwingiliano wa utaratibu, maumbo na kanuni za urejeshi wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Athari za mwingiliano uliojitokeza ulidhihirishwa katika data Na(6.46) ya data kutokana na matokeo mijarabu ya wanafunzi.

1. Uhamishaji wa viwakilishi nafsi ambavyo pia ni virejeshi vinavyowakilisha nafsi

- a) Askari alibakimbiza waizi Askari aliwakimbiza wezi
 b) Shangazi alimukimbiza mbuzi Shangazi alimkimbiza mbuzi

Mwanafunzi 18 akijadili juu ya jinsi mwingiliano wa matumizi ya Luganda inavyoathiri Kiswahili sanifu katika data Na. (6.46), alieleza kuwa,

“Wanafunzi walidhihirisha mwingiliano wa kanuni ya urejeshi kwa kuhamisha virejeshi vya nomino kuu vya Luganda katika Kiswahili sanifu. wanafunzi walitumia kwa mfano kiambishi kipatanishi cha nafsi ya pili [-ba-] na [-mu-] ambavyo pia ni viambishi virejeshi yambwa vinavyotumika kuwakilisha nomino kuu katika tungo.”

Athari za mwingiliano mwingine uliojitokeza katika mijarabu ni ile ya uchanganuzi na udondoshaji wa viwakilishi nafsi katika matumizi ya virejeshi nafsi yambwa vya Kiswahili sanifu kwa kutumia viambishi vipatanishi vya nafsi yambwa kuzingatia mkabala wa Luganda kama inavyojitokeza katika data Na. (6.47)

Mwingiliano wa Luganda

Matumizi ya Kiswahili sanifu

- | | | |
|--------------------------|---------------------|------------|
| a) Wewe alipiga mimi | wewe ulinipiga | Ulinipiga |
| b) Mimi niliomba yeye | Mimi nilimwomba | Nilimwomba |
| c) Ye anajua wewe | Yeye anakujua | Anakujua |
| d) Wanafunzi waliona wao | Wanafunzi waliwaona | |
| e) Mtoto alitoroka wewe | Mtoto alikutoroka | |
| f) Lubega alimuleta yeye | Lubega alimleta | |

Asili: data Kutokana na Mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Mwananafunzi 53 katika kujadili jinsi athari za uchanganyaji na udondoshaji wa viwakilishi nafsi zilivyoathiri matumizi ya Kiswahili, alieleza kuwa;

”Wanafunzi walitumia utaratibu wa viambishi vipatanishi vya nafsi yambwa kuzingatia mkabala wa Luganda. Wanafunzi ambao LI ni Luganda badala ya kuambisha kiwakilishi nafsi yambwa nyuma ya kitenzi, walidondosha kiambishi kiwakilishi yambwa cha umoja au wingi na kutumia kiwakilishi nafsi huru kama kirejeshi cha nafsi.”

Matumizi haya yanakiuka kanuni ya urejeshi ambapo kirai nomino au kirai bainishi kinachowakilisha yambwa katika Kiswahili lazima kitokee katika mazingira moja ya kisintaksia na wakilisho yambwa

Matokeo haya yalidhihirisha utokeaji wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungami ya Chomsky (1981) ambayo huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilidhihirika kuwa licha ya Luganda na Kiswahili sanifu kuwa lugha za nasaba moja yenye kanuni ya matumizi ya viwakilishi nafsi na viambishi vipatanishi vya yambwa nafsi, matumizi yake yalitofautiana kimaumbo na utaratibu unaofaa katika Kiswahili. Matumizi haya yaliathiri matumizi bora ya Kiswahili na kusababisha upatanishi wa kisarufi baina ya Kiima na yambwa. upotovu huu ulitokana na udodoshaji wa silabi ya kiwakilishi nafsi kiima na kipatanishi yambwa chake ambacho kilistahili kutokea nyuma ya kitenzi baada ya kiwakilishi njeo, pamoja na kubadilisha utaratibu wa kutumia kiwakilishi nafsi huru badala ya kiwakilishi kipatanishi yambwa nafsi cha umoja au wingi.

Mwingiliano mwingine ni ule wa matumizi ya viwakilishi nafsi huru kama virejeshi badala ya viwakilishi nafsi yambwa tegemezi kama katika data Na.(6.48) wa uhamishaji na matumizi ya viwakilishi nafsi huru badala ya yambwa rejeshi kutokana na mijarabu ya wanafunzi.

Athari za mwingiliano

a) **Mupishi** aliletaya **sisi** kyakula

b) **Mimi** nilifanyia wewe kazi

c) **Yeye** aliwomba msamaha kwa **wewe**

Kiswahili Sanifu

Mpishi alituletea chakula

Nilikufanyia kazi

Alikuomba msamah

| | |
|---|---------------------------------|
| d) <i>Mwalimu aliita yeye kwa ofisi</i> | <i>Mwalimu alimwita ofisini</i> |
| e) <i>Watoto wanasumbua sisi</i> | <i>Watoto wanatusumbua</i> |
| f) <i>Mpira ulipiga yeye</i> | <i>Mpira ulimpiga</i> |
| g) <i>Gari iligonga mimi</i> | <i>Gari lilinigonga</i> |
| h) <i>Baba atakuja kuona sisi</i> | <i>Baba atakuja kutuona</i> |

Kuhamisha viwakilishi virejeshi kutoka Luganda na kutumia viwakilishi huru kuwakilisha urejeshaji nomino, wanafunzi walitumia viambishi huru badala ya kutumia viambishi vipatanishi yambwa nafsi, virejeshi vya nomino tendewa kama ilivyo katika mfano wa (a) na kuhamisha moja kwa moja viambishi vipatanishi yambwa nafsi vinavyorejelea nomino tendewa ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Uhamishaji huu hukuzingatia maumbo au mofolojia kamili ya vipatanishi nafsi yambwa vya Kiswahili sanifu na badala yake kutumia vya Kiswahili sanifu kama ilivyo katika mifano ya [b na c].

Aidha, katika matokeo ya mijarabu ya wanafunzi, utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi walidhihirisha mwingiliano wa kutumia viwakilishi nafsi virejeshi vya Luganda pamoja na viwakilishi nafsi huru vya Kiswahili katika tungo kama ilivyojitokeza data (6.49)

| | |
|--|---------------------------------------|
| a) <i>Askari ali-[ba]-kimbiza nyinyi</i> | <i>Askari ali-[wa]-kimbiza</i> |
| b) <i>Shangazi ali-[mu]-kimbiza yeye</i> | <i>Shangaza ali-[m]-kimbiza mbuzi</i> |

Matumizi haya hayakudhihirisha vikamilifu kanuni ya urejeshi kwani maumbo *-[ba]- na -[mu]-* yaliyohamishwa kutoka Luganda hayakuwa ya Kiswahili na pili baada ya kutumia kiambishi kipatanishi yambwa, ambacho ni kiwakilishi cha nafsi tegemezi, hakuna haja ya kutumia viwakilishi nafsi huru.

Mwingiliano wa kutumia viambishi viwakilishi vya ngeli ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano mwingine ambao ulidhihirika katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi hasa katika mijarabu ya kisarufi yalikuwa ya kuhamisha viambishi vipatanishi vya ngeli ambavyo pia ni viwakilishi virejeshi vya nomino kuu katika Kiswahili sanifu kurejelea nomino kuu. Mwingiliano huu ulijitokeza katika nafsi ya pili na tatu kama katika mfano (6.50) kutokana na mazungumzo ya wanafunzi,

| | |
|--|--------------------------------------|
| a) <i>Askari ali-[ba]-kimbiza</i> | <i>Askari ali-[wa]-kimbiza</i> |
| b) <i>Shangazi ali-[mu]-kimbiza kuku</i> | <i>Shangaza ali-[m]-kimbiza kuku</i> |

Kwa kuhitimisha, ingawa matumizi ya viwakilishi yambwa na vibainishi vya kipronomino vinaweza kutokea kwa pamoja na kibainishi cha nafsi kiupatanishi, katika mazingira moja kulingana na sifa za idadi ya umoja na wingi, wanafunzi walishikilia ile kanuni ya kuongeza

viwakilishi virejeshi vya kiima huru baada ya kiwakilishi kirejeshi chenyewe kutajwa. Hali hii ilikwenda kinyume na kanuni ya urejeshi inayoshikilia kuwa kirai nomino au kirai bainishi kinachowakilisha yambwa lazima kitokee katika mazingira moja ya kisintaksia na wakilisho yambwa. Matokeo haya yalikiuka kanuni ya urejeshi kama ilivyofafanuliwa na Thompson & Schleicher (2001) kuwa viambishi hivi huundwa kwa kiambishi cha kiima [kwk], kikifuata kiambishi cha njeo [Knj], kiwakilishi kirejeshi ama cha nafsi au ngeli nomino [Knfs/Kng] kisha shina au mzizi wa kitenzi [MzT].

6.1.3.3 Kanuni ya muungano wa viwakilishi nafsi na maneno mengine

Kanuni hii inashikilia kuwa: Viwakilishi nafsi ni mofimu maalumu ambazo huunganika na maneno mengine kuunda tungo. Mofimu hizi hutumika kuwakilisha kiima na yambwa katika tungo na hudhihirika katika tungo kwa kuungana na viambishi vinginevyo kama viambishi vya wakati ambavyo hudhihirika katika vitenzi. Kanuni hii ya muungano pia hurejelea utaratibu na nafasi ya utokeaji wa viwakilishi husika katika tungo. Matokeo ya mijarabu ya wanafunzi kuhusu matumizi ya viwakilishi nafsi ulidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya muungano wa viwakilishi nafsi na maneno mengine katika tungo. wanafunzi walidhihirisha athari za mwingiliano wa kudondosha viambishi nafsi (*Knfsi*) vya kwanza hasa katika virai vya wakati uliopo kama katika data Na.(6.51) ya data kutokana na mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi:

a) *Mimi [-] nacheza mpira*

| | | | | |
|----------------|-------------------|-------------------|--------------|----------------|
| <i>Mimi</i> | <i>ni-</i> | <i>na-</i> | <i>chez-</i> | <i>a</i> |
| <i>Knfsi 1</i> | <i>KPM Knfsi1</i> | <i>- Knj[na]-</i> | <i>Mz-</i> | <i>Kiishio</i> |

b) *Mimi [-]-nasema na wewe*

| | | | | | |
|---------------|-------------------|--------------------|------------|----------------|-------------|
| <i>Mimi</i> | <i>ni-</i> | <i>na-</i> | <i>sem</i> | <i>-a</i> | <i>nawe</i> |
| <i>Knfsi1</i> | <i>KPM Knfsi1</i> | <i>- Knj [na]-</i> | <i>Mz-</i> | <i>Kiishio</i> | |

c) *Mi naona wewe njiani*

| | | | | | | |
|----------------|-------------------|-------------------|---------------|------------|----------------|---------------|
| <i>Mimi</i> | <i>ni-</i> | <i>na-</i> | <i>ku-</i> | <i>on-</i> | <i>a</i> | <i>njiani</i> |
| <i>Knfsi 1</i> | <i>KPM Knfsi1</i> | <i>- Knj [na]</i> | <i>Kirej-</i> | <i>Mz-</i> | <i>Kiishio</i> | |

Asili: Data kutokana na mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Data hii inadhihirisha Udondoshaji ambao uliharibu mpangilio au utaratibu maalumu unaojenga muunganiko wa vipashio vingene vinavyowekwa pamoja na viwakilishi nafsi kujenga umiliki na usabaki wa viwakilishi nafsi ambavyo pia hufanya kazi kama kiima au nomino kuu katika tungo kimofosintaksia.

Mwingiliano mwingine uliojitokeza ambao ulikiuka kanuni ya muungano wa viwakilishi na maneno mengine katika mjarabu ya kisrufi ni ule wa kuhamisha viambishi vipatanishi vya Luganda na kuvitumia kama viwakilishi vya nafsi vya Kiswahili. Uchanganyaji wa viwakilishi hivi ulipotosha usanifu wa matumizi ya viwakilishi kuzingatia kanuni ya muungano kujenga tungo za kimofosintaksia zenye maana. Hii ni kwa sababu viambishi vilivyotumika vilikosa kuunganika na vipashio vingine vya Kiswahili kujenga tungo sahihi kama inavyojitokeza katika data (6.52) kutokana na mjarabu ya wanafunzi:

| <i>Mwingiliano 1</i> | <i>Mwingiliano 2</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|------------------------------|----------------------------|-------------------------|
| a) <i>Mimi iko jokoni</i> | <i>Mimi iko jokoni</i> | Mimi nipo jikoni |
| b) <i>We iko nalia sana</i> | <i>Wewe iko nalia sana</i> | Wewe unalia sana |
| c) <i>Ye iko nacheza</i> | <i>Yeye iko nacheza</i> | Yeye anacheza |
| d) <i>Gwe onasema nini?</i> | <i>Wewe unasema nini?</i> | |
| e) <i>We onacheza mupila</i> | <i>Wewe unacheza mpira</i> | Unacheza mpira |

Wanafunzi waliingiza kbadala [ndi] ambacho kilitafsiriwa na kutumika na kile cha Kiswahili [iko]. Kibadala hiki kilitumika badala ya viwakilishi nafsi tegemezi vya Kiswahili sanifu kwa umoja na wingi kama ilivyo katika mifano ya [a-c]. Matumizi yake yalikosa kuzingatia utaratibu wa uambishaji wa viwakilishi vya nafsi kuunganika na vipashio vingine kujenga usanifu wa tungo kimofosintaksia. Katika mifano ya [d na e], wanafunzi walihamisha viwakilishi vya Luganda katika Kiswahili sanifu na kupotosha maumbo kamili na maana ya vipashio ambavyo vilistahili kuunganika na maneno mengine kujenga tungo sahihi. Kiwakilishi [gwe] kimetumika badala ya [wewe] na kiwakilishi nafsi tegemezi cha Luganda [o-] kutumika badala ya [u-] ya Kiswahili sanifu.

Mwingiliano mwingine uliojitokeza ni ule wa udondoshaji wa silabi ya pili ya viwakilishi vya nafsi huru kama katika data Na.(6.53) ya data kutokana mjarabu ya kisarufi ya waanafunzi:

| | | |
|---------------------------------|------------------------------|---------------------------------|
| a) <i>Mi naona wewe njiani</i> | <i>Mimi ninakuona njiani</i> | |
| b) <i>We aliona mimi wapi</i> | <i>Uliniona wapi?</i> | <i>Wewe uliniona wapi?</i> |
| c) <i>Ye aliomba pesa mingi</i> | <i>Aliomba pesa nyingi</i> | <i>Yeye aliomba pesa nyingi</i> |

Asili: Data kutokana na mjarabu ya wanafunzi nyanjani

Mwingiliano unaojitokeza ni ule wa kudondosha silabi ya pili ili kusawasisha silabi za viwakilishi nafsi vya Kiswahili na vya Luganda ambavyo hutamkwa na kuandikwa kwa silabi moja. Udondoshaji huu ulisababisha athari za kitahajia au kisarufi ambayo ilizuiya muunganiko wa viwakilishi nafsi kiima na viwakilishi vipatanishi ambavyo pia ni viambishi

vya nafsi tegemezi. Hii ni kwa sababu viwakilishi vya Kiswahili sanifu vina silabi mbili huku vile vilivyotumika vikiwa na silabi moja.

Matokeo haya yalidhihirisha utokeaji wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi wa nadharia ya umilikifu na ufungami ambayo hushikiliakuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Matokeo ya matumizi ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili ulikiuka kanuni ya muungano wa viwakilishi nafsi na maneno mengine katika tungo kama ilivyodhihirishwa na Oichoe, (2005), Egara, (2016) na Matasi na Furaha, (2016). Wanafunzi hawakuzingatia utaratibu mwafaka wa viambishi viwakilishi nafsi kutokea mwanzoni, vikifuatwa na njeo au wakati, vikifuatwa na mzizi ya vitenzi na kiishio. Katika kanuni hii ya muungano, Viwakilishi vya nafsi hutawala viambishi vya njeo na vitenzi. Aidha, Egara (2016) anadhihirisha ukiukaji wa matumizi ya viwakilishi nafsi akisema kuwa: Tilitambua kuwa mofosintaksia ya Kiswahili inaweza kuathiri wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu ulitambua kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuingiliana katika kanuni ya matumizi ya viwakilishi nafsi, lugha hizi ni mbili zinazotaofautiana katika matumizi ya kanuni hii kimosintaksia kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa maneno katika tungo.

6.1.3.4 Kanuni ya uambishaji

Kanuni hii inashikilia kuwa kila lugha huwa na maumbo ya kipekee yanayotumika kuunda vipashio vya kisarufi vya lugha kuwakilisha usahihi wake kimatumizi. Vile vile kanuni hii hudai kuwa uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi (uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu. Kila nomino huwakilishwa na maumbo ya viambishi dhahiri na kapa ambayo huambikwa kwenye kategoria za maneno katika tungo kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa nomino kuu.

Data ya mijadala ya wanafunzi kuhusiana na matokeo ya matumizi ya viwakilishi nafsi ilidhihirisha kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda waliathiri maumbo ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili kwa kutumia viambishi vya Luganda badala ya kutumia maumbo ya viwakilishi nafsi vya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na.(6.54).

| | | |
|-------------------------------|----------------------------------|-----------------------------|
| <i>Umoja</i> | <i>Wingi</i> | |
| <i>Nakuona darasani</i> | <i>Ninakuona darasani</i> | |
| <i>Nawomba maji ya kunywa</i> | <i>Ninaomba maji ya kunywa</i> | |
| <i>Mi napenda wewe</i> | <i>Mimi ninakupenda</i> | |
| <i>Nze nkwagala</i> | | |
| <i>Mi iko nyumbani</i> | <i>Mimi nipo nyumbani</i> | Nipo nyumbani |
| <i>Mi najua wewe</i> | <i>Mimi ninakujua</i> | Ninakujua |
| <i>Nze nkmanyi</i> | | |
| <i>We iko mubaya</i> | <i>Wewe ni mbaya</i> | Umbaya |
| <i>We onakimbia wapi?</i> | <i>Wewe onakimbia wapi?</i> | Unakimbia wapi? |
| <i>Ye adukila wa?</i> | | |
| <i>We nayimba muzuri sana</i> | <i>Wewe unayimba vizuri sana</i> | Unayimba vizuri sana |
| <i>Ye iko nayimba</i> | <i>Yeye anayimba</i> | Anayimba |
| <i>Ye nalima shamba</i> | <i>yeye analima shambani</i> | Analima shambani |

Mwanafunzi 39 akijibu jinsi matumizi ya viwakilishi nafsi ya wanafunzi katika matokeo ya mjarabu ya kisarufi ya tungo alieleza kuwa;

“Wanafunzi walidondosha silabi ya pili ya viwakilishi nafsi huru kwa madhumuni ya kusawazisha na viwakilishi nafsi vya Luganda ambavyo huwakilishwa na maumbo ya silabi moja.”

Kwa mujibu wa matokeo haya ilidhihirika athari za uhamishaji wa maumbo na utaratibu wa matumizi ya viwakilishi vya nafsi vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Matumizi haya yaliweza kupotosha upatanifu wa kisarufi na usarufi wa Kiswahili sanifu. Mofimu zilizokolezwa katika (6.35) zilizidhihirisha utaratibu wa uambishaji wa viwakilishi vya nafsi tegemezi na huru. Viambishi hivi ni viambishi vinavyotumika badala ya nomino ambavyo huwekwa mwanzoni mwa kitenzi, vikifuatwa na njeo kisha kitenzi. Mifano katika data (6.35) ilibanisha kuwa wanafunzi walikiuka kanuni ya uambishaji kwa kuhamisha viwakilishi vya nafsi vya Luganda katika Kiswahili sanifu, kudondosha silabi ya pili ya maumbo ya viwakilishi nafsi huru vya Kiswahili sanifu na kutumia viwakilishi vya nafsi huru kuwakilisha dhima ya yambwa rejeshi badala ya viambishi vipatanishi vya nafsi yambwa katika tungo.

Matumizi haya yalipotosha usahihi wa Kiswahili sanifu kimofosintaksia. Wanafunzi walikiuka matumizi ya kanuni inayoshikilia kuwa, katika matumizi ya viwakilishi nafsi, lazima utaratibu wa uambishaji wa viwakilishi nafsi uzingatie muktadha wa kila nafsi

kuwakilishwa na kiambishi chake bayana kinachopachikwa katika kitenzi pasi kuvurugwa. Matokeo haya yanashadidia utokeaji wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi wa nadharia ya Umiliki na usabaki. Kwa mujibu wa mihimili hii, Luganda na Kiswahili ilidhihirisha mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya uambishaji wa viwakilishi nafasi. Hata hivyo ilitofautiana katika matumizi kutokana na wanafunzi kuhamisha matumizi ya uambishaji wa Luganda katika Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha athari za mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya uambishaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi. Hali hii ilidhihirisha kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, lugha hizi huwiana na kutofautiana katika matumizi ya kanuni za uambishaji wa viwakilishi nafsi kimofosintaksia .

6.1.3.5 Kanuni ya nafasi ya utokeaji wa viwakilishi nafsi

Riedel (2009) anaeleza kuwa viwakilishi nafsi yambwa huweza kuwepo katika mazingira moja na vibaishi vya kipronomino. Hata hivyo, utafiti huu ulitambua kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikiuka katika kutumia kanuni ya utokeaji wa viwakilishi nafsi kuzingatia nafasi ya utokeaji wake katika Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na. (6.55):

| <i>Umoja</i> | <i>Wingi</i> |
|--|---|
| a) <i>Mwambia mimi ukweli</i> | <i>ambia sisi ukweli</i> |
| <i>Gamba nze amazima</i> | |
| <i>Niambie ukweli</i> | <i>Tuambie ukweli <i>Twambie ukweli</i></i> |
| <i>Ng'amba amazima</i> | |
| b) <i>Nachukua wewe nyumbani</i> | <i>Nachukuwa nyinyi nyumbani</i> |
| <i>Ntwala gwe ewaka</i> | |
| <i>Nak<u>u</u>chukua nyumbani</i> | <i>Naw<u>a</u>chukuwa nyumbani</i> |
| <i>Nkutwala ewaka</i> | |
| c) <i>Peleka yeye kwa mwalimu</i> | <i>Peleka wao kwa mwalimu</i> |
| <i>Mutwale wa musomesa</i> | |
| <i>Mpeleke kwa mwalimu</i> | <i>Wapeleke kwa mwalimu</i> |
| d) <i>Chukulia yeye chakula</i> | <i>Chukuliya wao chakula</i> |
| <i>Mchukulie chakula</i> | <i>Wachukulie chakula</i> |
| e) <i>Saidia mimi na kalamu</i> | <i>Saidia sisi kalamu</i> |
| <i>Nisaidie na kalamu</i> | <i>Tusaidie na kalamu</i> |

Data ya mijadala ya wanafunzi kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya Na. (6.55) kuhusiana na matumizi ya viwakilishi nafsi ilidhihirisha athari za kubadilisha nafasi ya muundo wa matumizi ya viwakilishi nafsi huru ambapo badala ya kutumia utaratibu wa kiwakilishi nafsi huru kutokea mwanzoni kuwakilisha nomino kuu au kiima, walikiweka mbele ya kitenzi na kupotosha utaratibu wa matumizi yake. Mtindo huu wa matumizi ya

lugha kati ilidhihirisha vilevile athari za uhamishaji wa kanuni ya matumizi ya viwakilishi nafsi huru walivyojifunza darasani na kutumia utaratibu wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Matumizi haya yalikiuka kanuni ya utaratibu wa utokeaji wa viwakilishi nafsi ambapo vilitumika katika nafsi ambayo haikustahili na pili badala ya kutumia viwakilishi yambwa tegemezi kuwakilisha nomino yambwa kwa kuiambisha katika kitenzi kuwakilisha kiima na yambwa kiupatanifu. Mwanafunzi akijadili jinsi mwingiliano wa kanuni hii unavyoathiri matumiai ya viwakilishi vya nafsi ya Kiswahili alieleza kuwa;

“Wanafunzi walibadilisha maumbo na kutumia viwakilishi nafsi huru katika mazingira yasiyokubalika katika Luganda na hata katika Kiswahili sanifu.”

Kwa mujibu wa kanuni hii, viwakilishi nafsi huru vilitokea mwanzoni mwa tungo vikiwakilisha nomino kuu. Viambishi hivi vilifuatwa na viwakilishi nafsi tegemezi ambavyo vilitumika kama viambishi vipatanishi vya nafsi vinavyomilikiwa na viwakilishi nafsi huru. Viambishi hivi viliunganika na kiwakilishi cha nje na nyuma ya mzizi wa kitenzi kukatokea kiwakilishi nafsi kirejeshi au kiwakilishi nafsi yambwa rejeshi ambacho hutumika kurejelea nomino tendewa au tendwa. Viwakilishi nafsi vyote vinavyotumika lazima vionyeshe upatanishi wa kisarufi kimofosintaksia. Kwa mfano viambishi virejeshi lazima vionyeshe upatanishi wa kisarufi na kiima kinachorejelewa na hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Utokeaji wa matokeo haya unadhihirisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuwa lugha za nasaba moja ambazo hudhihirisha matumizi ya kanuni moja ya kimofosintaksia ya nafasi ya utokeaji, kila lugha ilidhihirisha upekee wa matumizi ya kanuni. Hali hii inakubaliana na mihimili ya ubia na usarufi wa nadharia ya umilikifu na ufungami ya Chomsky ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo ya matumizi ya viwakilishi nafsi kutegemea nafasi ya utokeaji yalienda kinyume na kanuni kama inavyoshadidiwa na Egara (2016) ambaya anaeleza kuwa; “Mofimu wakilisho yambwa huchukua nafasi ya kabla ya mzizi wa kitenzi kwenye kiarifu.”

6.1.4 Mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya Vikanusho vya Kiswahili Sanifu

Ukanushaji ni kipashio cha kimofosintaksia cha kukataa au kupinga tendo yakini lililoelezwa katika kitenzi (Mgullu 1999, Lupogo 2021 na Mulei 2021). Ukanushaji huongozwa na kanuni maalumu na kila lugha hudhirisha kanuni zake. Ukiukaji wa kuzingatia kanuni mwafaka huweza kupotosha usanifu wa lugha husika kisarufi na hata kisemantiki. Matokeo ya data ya mijarabu ya wanafunzi ylidhirisha kanuni mbalimbali kuingiliana na kuathiri matumizi ya vikanusho vya Kiswahili sanifu katika vipasho vya ngeli katika nomino, vivumishi, viwakilishi nafsi na njeo na hali kama inavyotathiminiwa hapa chini.

6.1.4.1 Mwingiliano wa Kanuni za Luganda katika Ukanushaji wa Ngeli nomino za Kiswahili sanifu

Nomino ni muhimu sana katika sarufi ya lugha za Kibantu. Nomino katika Luganda na Kiswahili hutegemea kanuni ya uambishaji ambao hutokea mwanzoni (katika viambishi awali vya ngeli), kati na mwisho mwa nomino (Mgullu, 1999, Kyagaba, 1996). Ukanushaji katika Luganda na Kiswahili sanifu hufuata kanuni maalumu za uambishaji wa viambishi mbalimbali katika tungo kudhirisha hali yakinishi na kanushi. Lugha hizi mbili ni lugha ambishi bainishi. Kwa hiyo, utafiti ulichunguza kanuni za uambishaji wa viambishi mbalimbali ili kutambua mwingiliano na athari za matumizi ya kanuni za Luganda katika matumizi ya vikanusho vya Kiswahili sanifu. Data za maktabani na mijarabu ya kisarufi na mijadala kutokana na matokeo ya mijarabu ya wanafunzi ilitumika kubainisha mwingiliano wa kanuni na athari za mwingiliano wa kanuni kana inavyotathiminiwa hapa chini.

6.1.4.1.1 Kanuni ya uambishaji (uongezaji) wa maumbo ya vikanushi kifonolojia

Kimofosintaksia, ukanushaji wa ngeli katika Luganda sanifu huongozwa na uambishaji wa maumbo ya viambishi vikanushi nyuma ya kipatanishi cha kisarufi ambacho hutokea nyuma au mwanzoni mwa kiambishi awali cha nomino ambacho pia ni kiambishi kipatanishi cha ngeli (Kyagaba 1996:2015 na Mugerwa 2005). Kanuni hii vile vile hutumika katika Kiswahili sanifu ambapo maumbo ya vikanushi huwekwa kabla ya viambishi vya ngeli husika. Licha ya kanuni hii kushabihiana na kanuni ya uambishaji ya maumbo ya vikanushi kabla ya viambishi vya ngeli, tofauti za maumbo na sheria za Luganda na Kiswahili ulisababisha athari za mwingiliano wa matumizi ya maumbo ya Luganda katika ukanushaji wa ngeli za Kiswahili sanifu kimofosintaksia. Kama katika data Na.(4.17 Uk. 114; na 4.19, Uk. 117).

Data ya mijadala ya wanafunzi kuhusiana na kanuni ya uambishi ilibaini athari za mwingililiano wa kanuni za uambishaji wa Luganda katika Kiswahili sanifu. Katika maelezo ya mijadala, wakijadili jinsi mwingililiano wa kanuni ya uambishaji ilivyoathiri ukanushaji katika Kiswahili sanifu, mwanafunzi 44 alieleza kuwa;

“Maumbo yaliyoambishwa kabla ya viambishi ngeli vya Kiswahili sanifu yalikuwa maumbo ya Luganda ambayo yalizingatia utaratibu au sheria za kifonolojia ambapo kiambishi [t-] kiliwekwa nyuma ya viambishi ngeli vya Kiswahili sanifu.”

Kulingana na uchanganuzi kiambishi kilichotumika kiliathiri ngeli ya kwanza hasa kutokana na umbo la msingi la upatanishi wa kisarufi [-a]. Uambishaji huu ulitokana na kanuni ya Luganda kuwa umbo [t-] huambikwa kwenye viambishi vipatanishi vinavyoanza na irabu na [te-] kwenye viambishi vipatanishi vya msingi (VPM) vinavyoanza na konsonanti kama unavyojitokeza katika Data Na.(6.56) kutokana na mjarabu ya wanafunzi:

- | | |
|------------------------------------|---------------------------------------|
| a) <i>Mtoto anaenda shuleni</i> | <i>Mtoto [t]-aenda shuleni</i> |
| | <i>Omwana tagenda kusomero</i> |
| b) <i>Mwalimu alinunua kalamu</i> | <i>Mwalimu [t]-alinunua kalamu</i> |
| | <i>Omusomesa taguze kalaamu</i> |
| c) <i>Ng'ombe ataletwa nymbani</i> | <i>Ng'ombe [t]-aletwa nymbani</i> |
| | <i>Ente tejjakuleetebwa awaka</i> |
| d) <i>Shangazi ameondoka leo</i> | <i>Shangazi [t]-ameondoka leo</i> |
| | <i>Ssenga tajakugenda leero</i> |

Asili: data kutokana na mjarabu ya wanafunzi

Data Na. (6.56) ilidhihirisha kuwa wanafunzi walitumia kiambishi kikanushi cha Luganda [t-] ambacho huambikwa kabla ya kiambishi kipatanishi na kiambishi cha ngeli, kikizingatia sifa ya kifonolojia ya irabu badala ya kuzingatia kanuni ya uambishaji wa kikanushi [ha] kutegemea kanuni ya viambishi ngeli na njeo inayotumika katika tungo. Matumizi haya ya uambishaji yalikiuka kanuni na maumbo ya ukanushaji wa ngeli katika Kiswahili sanifu hasa katika ngeli za kisintkaksia zinazoanza na irabu kama vile ngeli ya [a-wa], ambapo ngeli ya kwanza iliathirika, ngeli ya 3 na 4, ngeli ya i-zi ambapo ngeli ya 9 iliathirika, ngeli ya u-zi ambapo ngeli ya 11 na ngeli ya U-ya ambapo ngeli ya U iliathirika. Kuathirika huku kulijitokeza kwa sababu ngeli hizi ziliwakilishwa na VPM ambavyo ni irabu kwa umoja na zingine kwa wingi.

Mwingiliano huu wa matumizi ya vikanushi vya Luganda, hasa wa kuambisha kikanushi [t-], cha Luganda sanifu iliathiri kanuni ya mabadiliko ya njeo na baadhi ya viambishi kutokana na kanuni ya Kiswahili sanifu. Kwa mfano, wanafunzi walidondosha kiambishi njeo cha wakati uliopita [-na-] na kiishio [-a] kuhifadhi hadhi yake tofauti na inavyofanywa katika Kiswahili sanifu. Katika mfano wa pili, wanafunzi walishindwa kutambua kanuni ya Kiswahili sanifu ya kubadilisha umbo la njeo ya wakati uliopita [-li-] na kutumia umbo kanushi [-ku-] katika mfano wa b). Katika mfano wa c), wanafunzi walidondosha kiwakishi njeo ya wakati ujao, hali ambayo ni kinyume na Kiswahili sanifu. Katika mfano wa d) wanafunzi walishindwa kutambua kikanushi [-ja-] cha wakati uliopo hali timilifu [-me-] pamoja na kutambua kuwa kikanushi kamili cha Kiswahili sanifu ambacho kilistahili kutumika ni [ha-] kama katika data Na. (6.57).

| Mwingiliano wa Luganda kati Kiswahili | Kiswahili sanifu |
|--|---|
| <i>Athari za Mwingiliano wa Luganda</i> | <i>Kiswahili</i> |
| a) <i>Mtoto [t]-aenda shuleni</i> | Mtoto [ha]-end- [i] shuleni |
| b) <i>Mwalimu [t]-alinunua kalamu</i> | Mwalimu [ha]- [ku] -nunua kalamu |
| c) <i>Ng'ombe [t]-aletwa nymbani</i> | Ng'ombe [ha]-taletwa nymbani |
| d) <i>Shangazi [t]-ameondoka leo</i> | Shangazi [ha]- [ja] -meondoka leo |

Asili: Data Kutokana na Mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Mifano (6.57) iliwiana na mihimili ya mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungami ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Matokeo haya kwa mujibu wa kanuni iliwiana kwa kuambisha viambishi, hata hivyo viambishi vilivyotumika vya Luganda vilikiuka kanuni ya ukanushaji ya Kiswahili ambayo kwayo kiambishi kikanushi [ha-] huwekwa nyuma ya kiambishi kipatanishi cha ngeli kuwakilishi kauli kanushi. Ukiukaji huu uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika tungo za kimofosintaksia kanushi. Hali hii ilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti licha ya kuwa na mwingiliano wa kanuni ya uambishaji wa maumbo ya ukanushaji.

Matokeo haya yalikiuka kanuni ya ukanushaji wa Kiswahili sanifu ya uambishaji wa vikanushi vinavyofaa kama ilivyoshadidiwa na Palome, (1967), Mgullu (1999), Habwe & Karanja (2004), Taher (2013), Kitsao (2015) ambao walidhihirisha ukanushaji wa ngeli za

nomino kwa kuweka kikanushi [ha-] nyuma ya kiambishi cha ngeli katika ukanushaji. Utafiti huu ulitambua uhamishaji wa maumbo na kanuni za uambishaji wa maumbo ya ukanushaji kutokamLuganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

6.1.4.1.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa viambishi vikanushi katika tungo

Kanuni hii hushikilia kuwa uambishaji wa mofimu au viambishi vikanushi katika Luganda hutokea mwanzoni kabla ya kiambishi awali cha nomino ambacho pia ni kiambishi kipatanshi cha msingi na baada ya kiambishi ngeli cha nomino hasa kwa viambishi virejeshi vya nomino. Kwa mujibu wa utafiti huu, kila ngeli huwakilishwa na mofimu ya ukanushi ambayo hutokea nyuma ya kiwakilishi kipatanishi cha nomino na kutokea mbele hasa katika tungo za kimfosintaksia zinazowakilishi yambwa rejeshi ya nomino kuu katika tungo tenzi kutofautisha nomino moja na nyingine katika tungo.

Matokeo ya data ya mijadala ilidhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa viambishi ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Ilibainika kuwa athari za mwingiliano uliojitokeza katika matumizi ya vikanushi vya Kiswahili sanifu uliotokana na maumbo ya kifonolojia ya viambishi awali vya upatanishi wa nomino vya Luganda vinavyotokea kabla ya vitenzi kama VPM vya ngeli nomino. Mijadala ya wanafunzi kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya data Na. (6.56, Uk. 348 na 6.57 Uk. 349) ilibaini kuwa, wanafunzi walihamisha maumbo ya viambishi vya msingi vya upatanifu vya Luganda hasa katika VPM vilivyoanza na irabu vya Kiswahili sanifu. Wanafunzi wakijadili jinsi mwingiliano wa kanuni hii ya Luganda jinsi ilivyoathiri ukanushaji wa Kiswahili sanifu. Mwanafunzi 26 akijibu swali la jinsi kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa viambishi vikanushi vya Luganda vilivyoathiri kiswahili sanifu, alieleza kuwa;

“Wanafunzi walihamisha kanuni ya Luganda ya kutumia vikanusho [t-] kwenye viambishi vipatanishi vya ngeli au vya awali vilivyojitokeza kwenye vitenzi kuanza na irabu au [te-] kwa viambishi awali vilivyoanza na konsonanti. Wanafunzi walihamisha matumizi ya maumbo ya vikanusho vya Luganda katika Kiswahili sanifu.”

Matokeo haya yalidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya kidarajia wa viambishi vya Luganda katika Kiswahili sanifu.

Matokeo ya tathimini ya athari za kanuni za darajia ya uambishaji wa vikanushi vile vile ulijitokeza katika yambwa rejeshi. Katika mwingiliano huu, wanafunzi waliongeza kiambishi kikanushi [-ta-] mbele ya KPM na nyuma ya kitenzi ambao kinyume na kanuni ya Kiswahili

sanifu uliozingatia kitenzi kinachofuata KT rejeshi pamoja na viwakilishi vya njeo vinavyohusika katika tungo. Data Na. (6.58)

- a) *Watoto waliofika wamepewa chakula* Watoto wa-[ta]-ofika wamepewa chakula
- b) *Walimu wanaocheza mpira wameshinda* Walimu wa-[ta]-ocheza mpira wameshinda
- c) *Kalamu atakayonunua ni yangu* Kalamu a-[ta]-yonunuwa ni yangu.
- d) *Kitabu kilicholetwa kiliraruka* Kitabu ki-[ta-]choletwa si kibaya
- e) *Mti uliokatwa umekauka* Mti u-[ta]-okatwa umekauka

Wanafunzi kwa kutumia kanuni au utaratibu wa ukanushaji wa yambwa rejeshi walitumia kikanusho [-ta-] kwa kukiweka baada ya kiwakilishi cha ngeli nomino nyuma ya kiambishi kipatanishi yambwa badala ya kutumia kanuni au utaratibu wa Kiswahili wa kukanisha utungo wenye yambwa rejeshi au utungo rejeshi. Matumizi haya yalipuuza dhima ya viwakilishi njeo na hali katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu na kukiuka utaratibu wa ukanushaji wa Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu wanafunzi walitumia kanuni ya Luganda katika ukanushaji wa tungo rejeshi za Kiswahili sanifu kama katika mifano (6.59) kutokana na matokeo ya utafiti huu.

- a) *Watoto wa-[ta]-o-fik-a wamepewa sare.* Watoto waliofika [**ha**]-wa-[**ja**]-pewa sare
wa- [ta]- o- fik- a [**ha**]-wa- [**ja**]- pew-a
KPM Ng2-Kkn-Kirej MzT- a *Kkn-KPM Ng2- Kkn [me] -MzT-a*
- b) *Walimu wa-[ta]-ocheza mpira wamelala.* Walimu wanaocheza mpira [**ha**]wa-[**ja**]-lala
wa- [ta]- o- chez-a [**ha**]- wa- [**ja**]- *lal-a*
KPM Ng2-Kkn-Kirej MzT-a *Kkn-KPM Ng2- Kkn [me] - MzT-a*
- c) *Kalamu a-[ta]-yonunuwa ni yangu.* Kalamu atakayonunua [**si**] yangu
a- [ta]- yo- nunuw-a atakayonunu-a[**si**]
KPM Ng2-Kkn-Kirej MzT- a *Kkn [ni]*
- d) *Kitabu kitacholetwa kiliraruka* Kitabu kilicholetw-a [**ha**]-ki-[**ku**]-raruka
Ki- [ta]-cho- letw-a [**ha**] -ki- [**ku**]- raruk- a
KPM Ng2-Kkn-Kirej MzT- a *Kkn-KPM Ng4- Kkn [li] -MzT-a*
- e) *Mti u-[ta]-o-katwa umekauka* Mti uliokatwa [**ha**]-u-[**ja**]-kauka
u- [ta]- o- katw-a [**ha**]-u- [**ja**]- *kauk-a*
KPM Ng2-Kkn-Kirej MzT- a *Kkn-KPM Ng2- Kkn [me] -MzT-a*

Tanabihi: [Kkp- kiambishi kipatanishi; Ng1/Ng2- ngeli ya kwanza na pili; MzT- mzizi wa kitenzi; Knj kiambishi cha njeo; KkpKrijNg1- kiambishi kirejeshi cha ngeli ya 1; Kb- kibainishi cha ngeli na Kkn- kiambishi kikanushi].

Matokeo haya ni tofauti na kanuni ya nafasi ya utokeaji wa viambishi kanushi kama ulivyofafanuliwa na Taher, (2013) na Lupogo, (2021) walioainisha viambishi ngeli na kudhihirisha kuwa vikanushi vya Kiswahili hutokea mwanzoni au katikati ya neno kutegemea kiwakilishi. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha ukiukaji licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja zinazodhihirisha kanuni ya uambishaji wa viambishi vikanushi kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino namaneno mengine katika tungo. Matokeo haya yanaendana na mihimili ya kanuni ya sarufi bia ya Nadharia ya Umilikifu na ufungami ya Chomsky (1981) ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

6.1.4.1.3 Kanuni ya upatanishi wa mofimu kanushi na KPM cha nomino

Mofimu za ukanushaji katika Luganda hujitokeza katika muundo wa kirai kitenzi [KT] kama kiambishi awali kinachoambishwa nyuma ya kiambishi kipatanishi cha ngeli nomino kilichoambishwa kwenye kitenzi (Kyagaba 1996; Matasi na Furaha, 2016; Habwe & Karanja 2004). Matumizi na utokeaji wa mofimu hizi Lazima yategemeo viambishi vipatanishi vya ngeli nomino vinavyoambikwa kwenye vitenzi kama viwakilishi vya nomino tendaji na maumbo ya kimofonolojia ya viambishi vipatanishi vya ngeli nomino tajwa. Maumbo ya kifonolojia yanatokana na kanuni ya Luganda kuambisha vikanushi kutegemea fonimu irabu na konsonanti inayoanza katika kiambishi awali cha upatanisho wa kisarufi cha nomino tendaji kama inavyojitokeza katika data Na. (5.60) kutokana na kifaa cha utondoaji data maktabani. 60

a) *Nze nsamba omupiira Ffe tusaamba emipiira Nsamba omupiira Tusamba emipiira*

b) *Mimi ninacheza mpira Sisi tunacheza mpira Ninacheza mpira Tunacheza mpira*

Asili: Data kutpokana na Matasi & Furaha, (2016) na Leah & Sseguya, (2015).

Matokeo ya data ya mijarabu ya wanafunzi kuhusu upatanishi wa mofimu kanushi kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981) ilidhihirisha kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikuwa wakizingatia kanuni ya upatanishi wa kisarufi wa Luganda katika matumizi au ukanushaji wa Kiswahili sanifu. Matokeo haya yanadhihirishwa katika data Na. (6.61)

| <i>Athari za Mwingiliano wa Luganda</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|---|--------------------------------|
| a) <i>Tonaenda shuleni mapema</i> <i>Togenga kusomero mangu</i> | Huendi shuleni mapemba sana |
| b) <i>Tonajua kupika chapati.</i> <i>Tomanyi kusiika capati</i> | Hujui kupika chapati |
| c) <i>Tonapenda kulia kila mara.</i> <i>Togenda kulya buli kiseera</i> | <i>Hupendi kulia kila mara</i> |

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Matokeo ya mijadala ya wanafunzi kuhusiana na jinsi mwingiliano na athari ilivyojitokeza uligundua kuwa, wanafunzi walitumia kikanushi [t-] kilichopatana na viambishi ngeli vilivyoanza na irabu na kuongeza kiambishi kikanushi [-ta-] cha yambwa rejeshi. Licha ya kuwa matumizi haya yalikuwa sahihi katika Luganda, wanafunzi waliyatumia katika ukanushaji wa tungo za kimofosintaksia za Kiswahili sanifu na kuacha matumizi sahihi ya upatanishi wa viambishi vikanushi vya Kiswahili sanifu vilivyozingatia uambishaji wa kikanushi [ha-] nyuma ya KPM , kukanusha maumbo ya njeo na hali na kuendeleza utaratibu wa kukanusha vitenzi vilivyotokea baada ya KT iliyo na kirejeshi. Rejelea data Na. (6.56, Uk. 348; 6.57, Uk. 349; 6.58, Uk. 351).

Matokeo haya yanaendana na mihimili ya Ubia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungami ya Chomsky (1981). Licha ya kuwa lugha hizi ziliingiana katika matumizi ya kanuni ya upatanishi, kulitokea tofauti katika utaratibu na maumbo ulioonyesha kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti hasa katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia. Kama ilivyoielezwa na wmanfunzi 10 akijadili jinsi mwingiliano ulivyosababisha athari, alieleza kuwa;

“Wanafunzi walikiuka kanuni ya upatanishi wa kisarufi ambapo mofimu kanushi za Luganda zilitumika badala ya maumbo kanushi ya Kiswahili sanifu.”

Matokeo haya yalidhihirisha kuwa licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nsaba moja, ni lugha mbili zinatofautiana katika matumizi ya kanuni za kimofosintaksia.

6.1.4.1.4 Kanuni ya mofolojia ya vikanushi na utokeaji wake katika tungo

Kanuni hii inazingatia uambishaji wa mofu kanushi mwafaka katika vipashio mbalimbali za sentensi au viambajengo kutegemea mofu kanushi zinazotambulika katika lugha mahususi. Kwa mujibu wa kanuni hii, Luganda huwakilishwa na vikanushi vitatu [t-] na [te-] ya fonimu irabu na konsonanti inayotangulia katika viambishi awali vipatanshi vya ngeli nomino

mtawaliwa na [-ta-] ya yambwa rejeshi ambayo hutokea baada ya VPM vya ngeli nomino (Kyagaba, 1996 na Leah & Sseguya, 2015). Kiswahili nacho huongozwa kikanushi [ha-/hu-] ambayo hutokea nyuma ya VPM vya ngeli nomino na vikanushi vya njeo na hali ambazo kila kiwakilishi njeo huwakilishwa na mofu kanushi. Data ya jedwali Na (4.18, Uk. 124) la maumbo ya kimofolojia ya ukanushajiwa Kiswahili sanifu liadhihirishwa mwingiliano wa matumizi ya kanuni hii. Matokeo ya data za mijadala ya wanafunzi kuhusu mwingiliano na athari za ukanushaji kuzingatia maumbo ulibani mwingiliano wa kanuni ya mofolojia ya maumbo ya kimofolojia ya vikanushi vya Luganda katika ukanushaji wa kauli za ngeli za Kiswahili sanifu. Wanafunzi wakijadiliana juu ya athari za mwingiliano uliojitokeza ktaika matokeo ya data Na. (5.62); Mwanafunzi 15 alieleza kuwa;

“Wanafunzi hawakuzingatia maumbo kanushi ya njeo na hali kama ilivyo katika Kiswahili sanifu. wao walihamisha maumbo ya ukaushaji wa Luganda na kanuni ya kutumia vikanusho [t- n ate] ya Luganda badala ya maumbo ya Kiswahili.”

Matumizi haya ya uhamishaji wa vikanusho na ujumlishaji wa viwakilishi vya njeo uliathiri usanifu wa Kiswahili sanifu na kupotosha dhima, na usarufi wa Kiswahili sanifu. Katika ujumlishaji wa ukanushaji, wanafunzi ambao L1 ni Luganda walidondosha au kutodondosha viwakilishi vya njeo na hali bila kutambua kuwa Kiswahili hudondosha viwakilishi vya njeo na kutumia vikanushi katika nafasi za njeo kama inavyojitokeza katika data za mijarabu Na.(5.62).

Athari za Mwingiliano wa Luganda katika Kiswahili Sanifu

- a) Mtoto [t]-aenda shuleni Mtoto [ha]- end-[i] shuleni [udondoshaji njeo]
- b) Mwalimu [t]-alinunua kalamu Mwalimu [ha]-[ku]-nunua kalamu [kutondosha]
- c) Ng’ombe [t]-aletwa nymbani Ng’ombe [ha]-[ta]-letwa nymbani [ujumlishaji]
- d) Shangazi [t]-ameondoka leo Shangazi [ha]-[ja]-meondoka leo [ujumlishaji]
- e) Kiboko [t]-aonekana muzuri Kiboko [ha]-[ta]-onekana vizuri

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Mwingiliano wa kuhamisha vikanushi vya Luganda na ujumlishaji wa matumizi ya viwakilishi njeo kufuata kanuni na utaratibu wa ukanushaji wa Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu kimofosintaksia uliozingatiwa ulikubaliana na mihimili ya ubia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungami ya Chomsky (1981) ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika

kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo haya yanashadidiwa na Immanuel (2019); Taher (2013); na Mulei, (2014:2020) na Hyman (2018) walidhiririsha vikanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu. kwa mujibu wa wataalamu hawa, Kiswahili huongozwa kikanushi [ha-/hu-] ambayo hutokea nyuma ya VPM vya ngeli nomino na vikanushi vya njeo na hali ambazo kila kiwakilishi njeo huwakilishwa na mofu kanushi. Luganda huwakilishwa na vikanushi vitatu [t-] na [te-] ya fonimu irabu na konsonanti inayotangulia katika viambishi awali vipatansihi vya ngeli nomino mtawaliwa na [-ta-] ya yambwa rejeshi ambayo hutokea baada ya VPM vya ngeli nomino. Rejelea jedwali la data Na.(4.17, Uk. 122) la maumbo ya kimofolojia ya ukanushaji wa Kiswahili sanifu

6.1.4.2 Kanuni za Ukanushaji wa Vivumishi vya Luganda sanifu

Ukanushaji wa vivumishi katika Luganda huzingatia maumbo ya vikanushi vitatu ambavyo ni [si, t- na te] vikanushi hivi hutumika kulingana na kanuni ya maumbo ya vikanushi vya Luganda vinavyoongozwa na fonimu irabu au konsonanti (Kyagaba, 1996; Mugerwa, 2005). Ukanushaji wa vivumishi vya Luganda pia huzingatia mizizi na uambishaji wa viambishi awali ambavyo hutokana na viambishi awali vya nomino ambavyo pia ni viambishi vipatanishi msingi vya nomino inayozungumziwa (Kiyinikibi 2021; Leah na Sseguya, 2015). Kwa kushirikisha mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya Chomsky (1981), upekuzi wa maandishi kutumia kifaa cha kudondoa data, mjarabu na mijadala, utafiti huu ulibaini mwingiliano wa kanuni zifuatazo katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu.

6.1.4.2.1 Kanuni ya kimapokezi masharti ya uongezaji vikanushi nyuma ya vivumishi

Kanuni hii inashikilia kuwa kikanushi [si] lazima kiwekwa kabla ya neno kuu lisilo kitenzi. Mara nyingi ukanushaji huu hujitokeza katika ukanushaji wa viambajengo mbapo ukitaka kukanusha kiambajengo kimoja lazima kikanushi kuwekwa kabla ya neno (kiambajengo] hicho bora neno au kiambajengo tajwa kisiwe kitenzi (Leah & Sseguya 2015; Kyagaba 1996). Kwa mujibu wa kanuni hii, mofimu kanushi [si] huambikwa au huwekwa nyuma ya kivumishi baada ya nomino kukanusha sifa au kivumishi kinachokumusha nomino tajwa. Ukanushaji wa kuzingatia ngeli unahifadhi kanuni ya kuambisha mofu za kifonolojia za [t-] na [te-] nyuma ya viambishi vipatanishi vya msingi vya ngeli nomino na kuambisha kiambisha [-ta-] katika tungo rejeshi kuwakilisha kauli kanushi ya viambishi yambwa rejeshi kama katika data ya majedwali Na. (4.17, Uk. 122 na 4.18 Uk 124).

Uchunguzi wa kikanushi [si-] kwa mujibu wa Hyman, (2018) kanuni hii ilishabihiana na ile ya Kiswahili sanifu ila kanuni ya uambishaji wa kiambishi [-ta-] kilichotokea baada ya viambishi vibainishi na viambishi vipatanishi vya ngeli nomino pamoja na maumbo yaliyoambikwa kabla au nyuma ya vikanushi vya Kiswahili sanifu kutofautiana na vya Kiswahili sanifu. Tofauti za utaratibu wa kuongeza kikanushi [-ta-] cha Luganda baada ya kiambishi kipatanishi cha msingi cha ngeli nomino kilisababisha mwingiliano wa matumizi ambapo wanafunzi walijipata wakitumia utaratibu huu katika ukanushaji wa tungo za kimfosintaksia za Kiswahili sanifu. Matumizi ya uhamishaji wa kanuni hii uliathiri ukanushaji wa njeo na hali na ukiukaji wa kanuni ya Kiswahili sanifu ya kukanusha vitenzi vinavyofuata KT lenye kiambishi kirejeshi katika tungo husika kuwakilisha kauli kanushi kama ilivyojitokeza katika data (6.58, Uk. 351) na (6.59, Uk 351).

Kiambishi kikanushi cha yambwa rejeshi kimetumika kimetumika baada ya kiambishi kipatanishi cha msingi cha ngeli nomino kinachoambikwa kwenye KT rejeshi badala ya kukanusha kitenzi kinachotokea baada ya Kundi tenzi lenye kirejeshi katika sentensi zote za [a-e]. Udondoshaji wa vambishi vya njeo na hali umezingatiwa badala ya kudondosha na kutumia viambishi kanushi vya njeo na hali kulingana na kanuni ya ukanushaji wa njeo za Kiswahili sanifu. Udondoshaji huu umetokea katika sentensi zote za [a-e]. Matumizi haya yalidhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni ya ukanushaji ya Luganda katika Kiswahili sanifu.

Data ya mijarabu ya wanafunzi ulibainisha athari za uhamishaji a ujumlishaji wa matumizi ya vikanushi vya Luganda katika Kiswahili sanifu kama unavyojitokeza katika data Na.(6.56, Uk. 348 na 6.57, Uk. 349). Matokeo haya yanashabihiana na mihimili ya nadharia ya umilikiu na unganifu ya Chomsky (1981) kwa kutumia kanuni ya kuambisha vikanushi vya Luganda nyuma ya kiambishi kipatanishi na kiambishi cha ngeli ya Luganda badala ya kutumia viambishi vya Kiswahili sanifu ambavyo hutokea katika vivumishi vinavyoambikwa viambishi vipatanishi vya msingi. Kulingana na matumizi haya, yalikiuka utaratibu na kanuni ya ukanushaji wa njeo na hali na kusababisha uhamishaji na ujumlishaji wa vikanushi vya Luganda katika Kiswahili sanifu ambapo njeo ilipuuzwa, kudondosha baadhi ya njeo bila kuibadilisha na kikanushi chake.

Kanuni hii inashadidiwa na Sharon, (2009) na Leah & Sseguya (2015) na kukinzana na kanuni ya Kiswahili ambayo ilidhihirsha kanuni za ukanushaji wa vivumishi kama ilivoelezwa na Habwe na Karanja (2004) na Hyman, (2018), Taher, (2013), Ngonyani, (2001)

na Mulei, (2014:2020). Matokeo yalidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili licha ya kuwa lugha za nasaba moja zenye kanuni zinazoingilina, kuna tofauti katika matumizi kuonyesha kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti kiisimu. Ni tofauti hizi zilizodhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni za ukanushaji kutokana na tofauti za kanuni ya maumbo ya ukanushaji baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.

6.1.4.2.2 Kanuni ya kuongeza maumbo kanushi ya kipekee kukanusha vivumishi

Kanuni hii hutumika katika vivumishi vya nafsi na ngeli. Kanuni hii hushikilia kuwa katika nafsi ya kwanza maumbo kanushi [siri] huongezwa nyuma ya kivumishi cha nafsi ya pili, [toli] na nafsi ya tatu [tali] kwa umoja. Katika wingi, nafsi ya kwanza hutumia [tetuli], nafsi ya pili, [temuli] na nafsi ya tatu, [tebali]. Kuzingatia kanuni ya kuongeza [t-] kwenye viwakilishi nafsi vinavyoanza na vokali na [te] kwa vile vinavyoanza na konsonanti (Leah & Sseguya 2015 Kyagaba 1996). Data ya mijarabu ya wanafuzi ilidhihirisha mwingiliano wa uhamishaji wa viambishi vikanushi vya nafsi vya Luganda katika ukanushaji wa vivumishi vya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na.(6.63).

| | | | |
|-----------------------------|---------------------------|-----------------------------|------------------------------|
| a) <i>Ndi mwana</i> | <i>Siri mwana</i> | <i>Tuli Baana</i> | <i>Tetuli baana</i> |
| b) <i>Mimi ni mtoto</i> | <i>Mimi sili mutoto</i> | <i>Sisi ni batoto</i> | <i>Sisi teli watoto</i> |
| c) <i>Mimi apana mutoto</i> | <i>Mimi si mtoto</i> | <i>Sisi ni watoto</i> | <i>Sisi apana watoto</i> |
| d) <i>Oli mwavu</i> | <i>Toli mwavu</i> | <i>Muli Baavu</i> | <i>temuli baavu</i> |
| e) <i>Wewe ni maskini</i> | <i>Wewe toli maskini</i> | <i>Nyinyi ni maskini</i> | <i>Nyinyi temuli maskini</i> |
| f) <i>Wewe si maskini</i> | <i>Wewe apana maskini</i> | <i>Nyinyi apana maskini</i> | <i>Nyinyi si Maskini</i> |
| g) <i>mwavu</i> | <i>ssi mwavu</i> | <i>Baavu</i> | <i>ssi baavu</i> |
| h) <i>Yeye ni maskini</i> | <i>Yeye tali maskini</i> | <i>Wao ni maskini</i> | <i>Wao tewali maskini</i> |

Asili: Data ya kutokana na mijarabu nyanjani

Kwa mujibu wa data ya mijadala ya wanafunzi kuhusiana na jinsi ukanushaji wa Luganda wa kuongeza maumbo kanushi ulivyoathiri Kiswahili sanifu. Ilibainika kuwa Mbali na kuwa wanafunzi walitambua kuwa kikanushi [si] huwekwa nyuma ya kivumishi cha nomino wanafunzi vile vile walihamisha maumbo kanushi ya Luganda katika Kiswahili sanifu. Aidha, walitumia kikanushi cha Kiswahili [Hapana] kwa mtindo wa Luganda ambapo pia hutumika kama kikanusho kwa kudondoa herufi awali ya ukanusho /h/. Wanafunzi wakijadiliana juu ya uhamishaji na udondoshaji wa fonimu /h/ ya kikanushi cha Kiswahili [hapana] kulidhihirisha kuchanganya vikanushi vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Aidha, wakijadili mwingiliano wa kanuni hii ya athari za uhamishaji, udondosaji na uchanganyaji wa

kanuni ya uambishaji maumbo ya vikanusho ya Luganda katika Kiswahili sanifu, kutokana na matokeo ya mijarabu ya wanafunzi, mwanafunzi 21 alidhihirisha kuwa;

“Wanafunzi badala ya kutumia maumbo sahihi na kikanushi (si) kukanusha vivumishi vya Kiswahili, walitumia maumbo ya siri, toli, tebali, temuli ya nafsi katika ukanushaji katika Luganda katika ukanushaji. Pia walichanganya vikaunushi vya Kiswahili na Luganda katika kukanusha kauli za Kiswahili sanifu.”

Matokeo haya ya kutumia maumbo ya Luganda katika Kiswahili sanifu yalidhihirisha utafauti wa kanuni za matumizi ya kanuni moja ya uambishaji wa vikanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu. Tofauti hii ilikubaliana na mihimili ya ubia na upatanishi ya nadharia ya Umilikifu na unganifu ya Chomsky (1981) ambayo hushikilia kuwa kanuni zile zile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Matokeo haya ya matumizi ya maumbo ya kikanushi inashadidiwa na Leah na Sseguya, (2015) ambayo vilevile yalielezwa na Habwe & Karanja, (2004), Hyman, (2018), Taher, (2021) na Mulei, (2014) kuhusiana na maumbo na utaratibu halisi wa ukanushaji katika Kiswahili. Kwa mujibu wa maelezo yao, Luganda na Kiswahili hudhihirisha kanuni ya uambishaji, hata hivyo maumbo yake na utaratibu huwiana na kutofautiana. Utafiti huu ulibaini mwingiliano wa kanuni ya Luganda ya kuhamisha, kudondoa na kuchanganya maumbo ya ukanushaji katika Kiswahili sanifi. Matumizi hayo yaliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu licha ya kuwa lugha hizi ni lugha za nasaba moja.

6.1.4.3 Mwingiliano wa kanuni za ukanushaji wa Viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu

Viwakilishi nafsi ni maneno ambayo huwakilishwa na viambishi huru na tegemezi. Kila lugha huwakilishwa na maumbo yake. Matokeo ya uchanganuzi wa mijadala, mijarabu na mazungumzo ya wanafunzi yalidhihirisha mwingiliano wa kanuni za ukanushaji wa viwakilishi nafsi vya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyotathiminiwa hapa chini:

6.1.4.3.1 Kanuni ya upatanishi nafsi

Kanuni hii ya kimofosintaksia ya upatanishi wa nafsi inahusika na maumbo au mofu zinazotumika katika ukanushaji wa viwakilishi nafsi. Kanuni hii hushikilia kuwa Mofu za ukanushaji wa nafsi kimofosintaksia ni viambishi vikanushi vinavyoambikwa katika nafasi ya

nyuma ya viwakilishi nafsi kurejelea kauli kanushi (Matasi & Furaha, 2016 na Kyagaba, 1996). Mofu kanushi zinazotumika huhusiana na mofu za viwakilishi vya nafsi vinavyodhihirisha sifa za kisarufi za idadi ya umoja na wingi. Muundo wa ukanushaji wa viwakilishi nafsi katika tungo za Luganda sanifu hutokana na uambishaji wa vipatanishi vya nafsi ambavyo huwekwa kwenye shina au mizizi ya vitenzi vinavyobeba maana au dhamira fulani kulingana na wakati au hali. Aidha, ukanushaji wa tungo yenye vipatanishi vya kisarufi vya nafsi hutokea au kubadilika kulingana na viambishi awali vya shina au mzizi wa kitenzi (Hyman, 2018).

Matokeo ya data ya mijarabu ya wanafunzi kuhusiana na matumizi ya kanuni ya ukanushaji ya upatanisho ya kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu ya viwakilishi nafsi ilidhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni ya Luganda katika Kiswahili sanifu katika nafsi ya kwanza pili na tatu kwa umoja na wingi kama inavyojitokeza katika data Na.(6.62, Uk. 354; 6.63, Uk. 357 na 6.64, Uk. 359). Kwa kurejelea mihimili ya upatanishi na upatanishi ya Chomsky (1981), utafiti huu ulibaini athari ya kutodondosha kiwakilishi cha wakati uliopo cha Kiswahili kama ilivyo katika mifano ya [a –c], athari za kujumlisha kanuni ya ukanushaji kwa kutumia kikanushi cha nafsi ya kwanza na kiambishi cha wakati uliopita [-li-] badala ya kubadilishana kwa kiambishi cha wakati na kikanusho [ku] kama inavyojitokeza katika data Na.(6.64):

1. Ukanushaji wa nafsi ya kwanza umoja wakati uliopita

| Athari za Mwingiliano wa Luganda | Kiswahili sanifu |
|---|--------------------------|
| a) <i>Sinapenda kucheza Kandanda</i> | Sipendi kucheza kandanda |
| b) <i>Sinayimba wimbo na mwalimu</i> | Siyimbi wimbo na mwalimu |
| c) <i>Silikuomba kalamu yake</i> | Sikuomba kalamu yake |
| d) <i>Silikimbia peke yangu</i> | Sikukimbia peke yangu |

Asili: Mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Data za mijadala ya matokeo ya mijarabu ya nafsi ya kwanza Na.(6.64) miongoni mwa wanafunzi wa jinsi matumizi ya kanuni ya upatanishi ya Luganda ilivyoingiliana na kuathiri Kiswahili ilidhihirika kuwa, wanafunzi walitumia utaratibu wa ukanushaji wa Luganda katika Kiswahili. Mwanafunzi 39 akijibu swali hili la jinsi kanuni ya Luganda ilivyoathiri kanuni ya ukanushaji wa Kiswahili, alieleza kuwa;

“Wanafunzi walitumia utaratibu wa kutodondosha viambishi vya wakati. Katika Luganda, viambishi vikanushi huwa havizingatiwi wakati wa ukanushaji. Hii ndiyo hali iliyoharibu sarufi ya Kiswahili.”

Matumizi haya yanaendana na kanuni ambayo inashikilia kuwa licha ya kuwa lugha za nasaba moja hudhihirisa uwiano wa kanuni, kuna tofauti ndogo ambayo huonyesha lugha husika kuwa lugha mbili tofauti. Matokeo ya nafsi hii yalidhihirisha Mwingiliano ambao uliathiri upatanishi wa kisarufi wa ukanushaji katika Kiswahili sanifu kwa sababu viambishi vilivyotumika havikupatana na utaratibu pamoja na maumbo ya ukanushaji ya Kiswahili sanifu. Mwingiliano mwingine ni ule uliojitokeza katika nafsi ya pili. Kwa mujibu wa data za mijarabu ya wanafunzi, utafiti uligundua kuwa wanafunzi ambao L1 walidhihirisha athari ya kutondosha kiambishi cha wakati uliopo [-na-] cha Kiswahili pamoja na kutumia (kuhamisha) viambishi vikanushi vya nafsi ya pili vya Luganda badala ya kutumia viambishi vipatanishi vya ukanushaji vya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na (6.65)

| 2. Ukanushaji wa nafsi ya pili Umoja | wakati uliopo |
|---|----------------------------|
| <i>Athari za Mwingiliano wa Luganda</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
| d) <i>Tonaenda shuleni mapema</i> | Huendi shuleni mapema sana |
| e) <i>Tonajua kupika chapati.</i> | Hujui kupika chapati |
| f) <i>Tonapenda kulia kila mara.</i> | Hupendi kulia kila mara |

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Data ya mijadala ya wanafunzi kuhusu jinsi athari za mwingiliano ulivyoathiri kiswahili sanifu, Wanafunzi wakijadili matokeo ya mijarabu Na.(6.65) walidhihirisha athari za uhamishaji wa kanuni ya Luganda na kushindwa kutumia kanuni ya Kiswahili ya kudodoshia viwakilishi wakati uliopo na uliopita kuongeza [h-] nyuma ya kiwakilishi nafsi [u-]. Mwanafunzi 54 akijadili jinsi mwingiliano wa kanuni ulivyoathiri upatanishi wa Kisarufi wa Kiswahili, alieleza kuwa;

“Wanafunzi walihamisha viambishi vikanushi pamoja na viwakilishi nafsi vya Luganda [t-] na [o-] mtawaliwa katika ukanushaji wa viwakilishi vya nafsi vya Kiswahili sanifu. Walitumia kikanushi na kiwakilishi nafsi [to] na kusahau kudondosha kiwakilishi cha wakati uliopo na kutumia kikanushi [-i] cha kiambishi cha Kibantu [-a] katika Kiswahili.”

Kwa mujibu wa data hii, matumizi haya yaliathiri Kiswahili sanifu kwa sababu wanafunzi walichanganya vikanushi vya Luganda na kanuni ya ukanushaji isiyokanusha wakati katika kukanusha viwakilishi vya nafsi ya pili vya Kiswahili sanifu. Katika ukanushaji wa nafsi ya tatu wakati ujao, data ya mijarabu ya wanafunzi ilidhihirisha ujumlishaji wa kanuni, kuchanganaya vikanushi vya njeo ya wakati uliopo na wakati ujao, kudondosha kiwakilishi cha njeo ya wakati ujao kinyume na kanuni ya Kiswahili ambayo huwa haidondoshi kama inavyojitokeza katika data Na. (6.66):

3. Ukanushaji wa nafasi ya tatu wakati ujao

| <i>Athari za Mwingiliano 1</i> | <i>Athari ya Mwingiliano 2</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|--------------------------------|--------------------------------|-------------------------|
| a) <i>Apendi kulima</i> | <i>Asinapenda kulima</i> | Hapendi kulima |
| b) <i>Aongei vizuri</i> | <i>Asinaongea vizuri</i> | Haongei vizuri |
| c) <i>Asileta chai tamu</i> | <i>Asilileta chai tamu</i> | Hakuleta chai tamu |
| d) <i>Asilitazama runinga</i> | <i>Asitazama runinga</i> | Hakutazama runinga |
| e) <i>Atacheza mpira kesho</i> | <i>Asitacheza mpira kesho</i> | Hatacheza mpira kesho |

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Uchanganuzi wa data za mijadala ya wanafunzi wa jinsi mwingiliano wa Luganda ulivyoathiri Kiswahili sanifu, ilidhihirika athari za udondoshaji wa kiambishi cha njeo [ta] pamoja na kikanushi [h-] na badala yake kiwakilishi cha nafsi ya tatu [a-] kutumika kama kikanushi. Vilevile walidondosha kimalizio [-a] cha kitenzi na kutumia kikanushi [-i] cha ukanushaji cha wakati uliopo kama inavyodhihirishwa katika mfano wa [a na b]. Mifano ya [c hadi e], wanafunzi walidondosha kikaunshi [h] na kutumia kikanushi [si-].

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanishi, matumizi haya yaliathiri sana tahajia, usanifu wa Kiswahili na kujenga ukanushaji uliokiuka kanuni za upatanishi wa vikanushi vya viwakilishi nafsi na viwakilishi njeo vya Kiswahili sanifu kutokana na tofauti ndogo zinazojitokeza katika kanuni ya upatanishi wa kisarufi.

Athari za mwingiliano mwingine ulijitokeza katika nafsi ya kwanza hali timilifu. Matokeo ya mijarabu yalidhihirisha uhamishaji na ujumlishaji wa kanuni ya kutumia kikanushi cha nafsi ya kwanza umoja [si-] na kushindwa kubadilisha hali ya me na kikanushi chake [-ja-] kama katika data Na. (6.67):

4. Ukanushaji wa nafsi ya ya kwanza hali timilifu

| <i>Athari za mwingiliano wa Luganda</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|---|-------------------------|
| a) <i>Simeona muwalimu</i> | Sijaona mwalimu |
| b) <i>Simelala nyumbani</i> | Sijalala nyumbani |
| c) <i>Simeondoka</i> | Sijaondoka |

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Data ya mijadala ya wanafunzi wa jinsi kanuni hii ilivyoa thiri matumizi ya kiswahili ilidhihirisha kuwa wanafunzi walitumia kikanushi [si-] pamoja na kiwakilishi cha wakati hali timilifu [-me-] badala ya kiambishi kikanushi [-ja-] cha Kiswahili sanifu. Mwanafunzi 6 akijaadili jinsi mwingiliano huu wa kanuni ya upatanishi inavyoathiri Kiswahili sanifu, alisema kuwa;

“Wanafunzi waliamisha kikanushi [si] cha Luganda ambacho pia hutumika katika Kiswahili, wakakosa kudondosha kiwakilishi cha hali ya [-me-] na katika nafasi yake kutumia kiambishi kikanushi [-ja-] cha Kiswahili.”

Data Na.(6.66) ya data kutokana na matokeo ya mijarabu ya kisarufi ya nafsi ya pili kwa kutumia kiifaa cha kudondoa data kutoka katika mijarabu ilidhihirisha athari za ujumlishaji wa kutumia kikanushi [si-] cha nafsi ya kwanza. Wanafunzi walidhihirisha athari za mwingiliano ambapo badala ya kuongeza mzizi wa kikanusho [h-] nyuma ya kiwakilishi nafsi ya pili [-u-] kinachotumika katika ukanushaji wa nafsi ya pili katika Kiswahili sanifu kama katika data Na. (6.68)

5. Ukanushaji wa nafsi ya ya pili hali timilifu

Athari za mwingiliano wa Luganda

- a) *Simeona nyumba*
- b) *Usimekula chakula*
- c) *Simepata kalamu*

Kiswahili sanifu

- Umeona nyumba
- Umekula chakula
- Umepata kalamu

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Mwingiliano uliojitokeza hapa ni ule wa kutumia kikanushi [si] kwa ujumla. Hali hii ilidhihirisha mwingiliano wa ujumlishaji wa kutumia vikanushi vya Luganda katika nafasi ambapo hakipaswi kutumika kama ilivyo katika mifano ya [a) na c)]. Uchanganuzi wa data za mijadala ya wanafunzi ulibaini athari za ujumlishaji kanuni na udondoshaji wa fonimu [h-] ambayo ilitahili kuwekwa nyuma ya kiwakilishi nafsi cha nafsi ya pili [-u-] kama ilivyo katika mfano wa [b]. Matumizi haya ya ujumlishaji, matumizi ya viwakilishi nafsi yakinishi badala ya viwakilishi nafsi kanushi vya nafsi ya pili na ujumlishaji wa kutumia kikanushi [si-] katika ukanushaji wa nafsi ya pili uliathiri tahajia na usarufi wa Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu wanafunzi walichanganya kanuni ya Luganda katika ukanushaji wa nafsi ya pili hali timilifu [-me-].

Data ya mijarabu vilevile ilitambua athari za mwingiliano wa matumizi ya vikanushi vya Luganda katika Kiswahili sanifu ambapo kikanushi kinachowekwa nyuma ya irabu [t-] kilitumika na kiwakilishi cha hali timilifu kutotondoshwa. Kama katika data Na (6.69)

Athari za Mwingiliano wa Luganda

- a) *Tameendesha gari*
- b) *Tameondoka mapema leo*
- c) *Tamejificha kitandani*

Kiswahili sanifu

- Hajaendesha gari
- Hajaondoka mapema leo
- Hajajificha kitandani

Asili: Data ya mijarabu ya wanafunzi

Matokeo haya ya matumizi ya viwakilishi vya nafsi na njeo ilikosa kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa vipashio katika tungo na hivyo kupotosha upatanishi wa kisarufi. Matumizi haya yalikubaliana na mihimili ya ubia na upatanishi ya nadhara ya umilikifu na

ufungami ya Chomsky (1981). Utaratibu huu ulikiuka mipaka ya kutoonyesha uhusiano wa kisarufi wa vikanushi vya nafsi ya tatu na hali timilifu ya [-me-] kama inavyotumika katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ulikiuka kanuni na kusababisha Kiswahili kisicho sanifu katika maazungumzo na maandishi ya wanafunzi.

Matokeo haya yanafanana na maelezo ya Hyman, (2018), Leah & Sseguya, (2015) kuhusu matumizi ya viwakilishi nafsi na ukanushaji wake. Aidha, matokeo yao yanatofautiana na ya utafiti huu ambao ulibainisha athari za mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya upataishi wa Luganda na Kiswahili sanifu kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi. Aidha kanuni hii licha ya kuwa inachembe ya utaratibu wa ukanushaji katika Kiswahili sanifu, matokeo ya matumizi yalikiuka kanuni ya ukanushaji wa Kiswahili ambao kila nafsi katika Kiswahili huwakilishwa na kiambishi kikanushi kama ilivyoelezwa na Hyman, (2018), Habwe & Karanja, (2004), Matasi & Furaha, (2016), Taher, (2013).

6.1.4.3.3 Kanuni ya maumbo wakilishi ya vikanushi

Kanuni hii hushikilia kuwa kila kiwakilishi nafsi huwakilishwa na mofu kanushi dhahiri ambazo hutumika kutegemea dhima, wakati, hali na nafsi husika. Ukiukaji wa kutozingatia maumbo mwafaka na kutumia maumbo yasio sahihi katika lugha bainifu huweza kupotosha usanifu wa lugha husika (Mgullu 1999 na Mulei, 2014). Data ya mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi yalidhihirisha athari za mwingiliano wa kutumia viambishi vikanushi vya Luganda katika nafsi ya vikanushi vya Kiswahili sanifu ambavyo havikutumika kama ilivyojitokeza katika mijarabu ya wanafunzi data Na. (6.62, Uk. 354; 6.63, Uk. 357; 6.64, Uk. 359; 6.65, Uk 360; 6.66, Uk. 361; 6.67, Uk. 361; 6.68, Uk. 362)

Mijadala ya wanafunzi kuhusiana na maumbo wakilishi ya vikanushi kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na unganifu ilitambua kuwa wanafunzi aambao L1 ni Luganda walitumia maumbo ya vikanushi vya Luganda sanifu [t-, ta, na si-] na kusahau kuwa Kiswahili hutumia maumbo ya [ha, hu, na si] ambayo hutumika katika ukanushaji wa nafsi kutegemea njeo. Mwanafunzi 1 akijadili jinsi mwingiliano wa maumbo ya Luganda yalivyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu, alieleza kuwa;

“Wanafunzi wa Kiswahili walipuuza ubadilishanaji wa viwakilishi vya njeo yakinishi na viwakilishi kanushi ambapo katika Kiswahili, kila njeo na hali huwakilishwa na mofu kanushi. Matumizi haya yalitokana na kuwa Katika Luganda viambishi vya njeo huwa havina maumbo kanushi kama ilivyo katika Kiswahili sanifu.”

Matumizi haya ya maumbo ya vikanushi na kutojali kukanusha viambishi vya njeo na hali ulisababisha upotofu wa matumizi ya Kiswahili sanifu kwa sababu tungo zilizojitokeza zilikuwa hazizingatii kanuni za ukanushaji wa Kiswahili sanifu. Ukiukaji wa matumizi ya maumbo ya vikanushi visivyo vya Kiswahili sanifu katika muktadha wa mazungumzo au maandishi ya Kiswahili sanifu ulitokana na matumizi ya maumbo kanushi kama ilivyoelezwa katika Jedwali (4.23).

Kutokana na mfano (4.18 Uk.115) wa maumbo ya ukanushi, wanafunzi walishindwa kutambua mabadiliko ya matumizi ya viambishi viwakilishi vya njeo na hali pamoja na vikanushi vya viwakilishi vya nafsi na kutumia vikanusho vya viwakilishi vya nafsi vya Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu. Wanafunzi walistahili kutambua mabadiliko hayo na kuyatumia pasi kuyakiuka. Kila njeo na hali katika Kiswahili huwakilishwa na kiambishi yakinishi na kanushi. Kwa mfano; njeo -li- ya wakati uliopita, huwakilishwa na umbo la [-ja-], [-na-] ya wakati uliopo hupotea kabisa na nafasi yake kusitiriwa katika nafsi inayohusika huku kiambishi tamati kikibadilika kutoka [-a] na kuwa [-i]. Wakati ujao [-ta-] hubakisha hdhi yake kama ilivyo katika wakati wa [-po- na -ki-]. Ukanushaji huu wa njeo hutanguliwa na vikanushi si-, hu- au ha- kutegemea nafsi yenyewe. Hali hii inadhihirisha kuwa vikanushi vya njeo na hali vinapoambatanishwa na njeo, hupelekea kutokea mabadiliko ya njeo na hali kama inavyojitokeza katika majedwali kama inavyojitokeza katika majedwali (6.4a-d) kutokana na matokeo ya utafiti kutokana na Kawale, (2015); Mdee, (1996) na Mulei, (2014).

Jedwali 6.4a: Maumbo ya wakati uliopita ya Kiswahili sanifu

| Nafsi | Yakinishi | Kanushi | Mabadiliko ya Nafsi | Mabadiliko njeo |
|-------|-----------|--------------------|---------------------|-----------------|
| 1 | Niliona | [si + ku]+ on-a | [Ni- → Si] | [-li- → -ku-] |
| 2 | Uliomba | [Ha + ku]+ omb-a | [U- → Hu] | [-li- → -ku-] |
| 3 | Aliogopa | [ha + ku] + ogop-a | [A- → Ha-] | [-li- → ku-] |

Asili: Data kutokana na Ngonyani, (2001); Mulei (2020); Matasi na Furaha (2016)

Jedwali 6.4b: Maumbo ya ukanushaji vya wakati uliopo vya Kiswahili sanifu

| Nafsi | Yakinishi | Kanushi | Mabadiliko ya Nafsi | Mabadiliko ya njeo |
|-------|-----------|-------------------|---------------------|--------------------|
| 1 | Ninasoma | [Si] + [ø] som+ a | [Ni- → Si] | [na → ø] [a → i] |
| 2 | Unalala | [Hu] + [ø] lal+ a | [U- → Hu] | [na → ø] [a → i] |
| 3 | Anaimba | [Ha] + [ø] imb+ a | [A- → Ha-] | [na → ø] [a → i] |

Asili: Data kutokana na Ngonyani, (2001); Mulei (2020); Matasi na Furaha (2016)

Jedwali 6.4c: Maumbo ya vikanushi vya hali timilifu [-me-]

| Nafsi | Yakinishi | Kanushi | Mabadiliko ya Nafsi | Mabadiliko ya njeo |
|-------|------------|-------------------------|---------------------|--------------------|
| 1 | Nimeondoka | [Si] + [-ja-] ondok+ a | [Ni- → Si] | [-me- → -ja-] |
| 2 | Umependeza | [Hu] + [-ja-] pendez+ a | [U- → Hu] | [-me- → -ja-] |
| 3 | Ameugua | [Ha] + [-ja-] ugu+ a | [A- → Ha-] | [-me- → -ja-] |

Asili: Data kutokana na Ngonyani, (2001); Mulei (2020); Matasi na Furaha (2016)

Jedwali 6.4d: Maumbo ya vikanusho vya wakati ujao

| Nafsi | Yakinishi | Kanushi | Mabadiliko ya Nafsi | Mabadiliko ya njeo |
|-------|-----------|-------------------------|---------------------|--------------------|
| 1 | Nitachota | [Si] + [-ta-] chot+ a | [Ni- → Si] | [-ta- → -ta-] |
| 2 | Utacheza | [Hu] + [-ta-] chez+ [i] | [U- → Hu] | [-ta- → -ta-] |
| 3 | Atasafiri | [Ha] + [-ta-] safir-i | [A- → Ha-] | [-ta- → -ta-] |

Asili: Data kutokana na Ngonyani, (2001); Mulei (2020); Matasi na Furaha (2016)

Matokeo ya utafiti huu yamelezwa na Kawale (2015), Mdee (1996), Mulei (2014) na kushadidiwa na Hyman (2018); Lupogo (2021); Matasi na Furaha (2016); Ngonyani (2001), na Leah & Sseguya (2015) ambao walieleza kanuni mwafaka katika ukanushaji wa nafsi. Licha ya ufafanuzi wa kanuni hii katika ukanushaji, matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa ingawa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja zenye uwiano za kanuni ya maumbo wakilishi ya vikanusho, ni lugha mbili tofauti. Matokeo haya yanaendana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadhari aya Chomsky 1981 ambayo hushikilia kuwa; kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

6.1.4.4 Mwingiliano wa Kanuni za ukanushaji wa Njeo na hali za Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu

Njeo na hali kimofosintaksia huwakilishwa na maumbo yakinishi na kanushi yanayoambishwa kabla ya vitenzi kutofautisha muda wa kutendeka kwa jambo na jinsi vitendo vinavyofanyika katika hali mbalimbali za wakati huu. Kila lugha huwa na maumbo na taratibu mbalimbali zinazotumika katika tungo kuwakilisha njeo na hali. Kiswahili ni lugha ambayo njeo na hali ni muhimu sana katika ukanushaji. Kila njeo na hali huwakilishwa na viambishi yakinishi na kanushi. Hali na taathira ya njeo na hali za Luganda kujitokeza katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu hauchawekwa bayana kimofosintaksia. Utafiti huu ulichunguza mwingiliano wa kanuni za ukanushaji wa njeo na hali za Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu na kubaini athari za kimofosintaksia zinazojitokeza. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kanuni mbalimbali zilizodhihirisha mwingiliano wa njeo na hali za Kiswahili sanifu. Kanuni zilizojitokeza zimetathiminiwa hapa chini kutokana na mijadala na mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi ambao L1 ni Luganda.

6.1.4.4.1 Kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi za njeo na hali

Njeo na hali katika Luganda sanifu huwakilishwa na maumbo mbalimbali yanayowakilisha wakati wa kutendeka kwa jambo zikiwemo mofu nyambuzi ambazo huwekwa mwishoni mwa vitenzi na mofu zingine kuwekwa kabla ya mizizi ya vitenzi. Mofu hizi za njeo na hali hazidhihirishi utokeaji wa mofu kanushi wakati wa matumizi bali ukanushaji hujitokeza tu katika vitenzi kwa kutegemeza fonimu kanushi [si] ya nafasi ya kwanza umoja, [t-] ya kukanusha viambishi vya vitenzi, nafsi au ngeli vinavyoanza na vokali na [te-] ya konsonanti. Data ya mijarabu ya wanafunzi nyanjani kuhusu kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi ya njeo nah hali kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi, ilidhihirisha mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi ya njeo na hali miongoni mwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda kama inavyojitokeza katika data Na.(6.70).

- a) [Si-li-kuomb-a] kalamu yake [Si-ku-omb-a] kalamu yake [Nafsi ya kwanza -li-]
Kkn[Kkp]-Knj-Mz-a Kkp[Kikanushi]-[Kkn[ku] cha njeo]-Mz-i
- b) [Si-na-chez-a] mpira [Si-chez-i] mpira [Nafsi ya kwanza -na-]
Kkn[Kkp]-Knj-Mz-a Kkp[Kikanushi]-[udondoshaji njeo]-Mz-i
- c) [T-a-me-ondok-a] mapema leo [Ha-ja-ondok-a] mapema leo [Nafsi ya tatu -me-]
Kkn-[Kkp[nafsi3Lug]-Knj-Mz-a Kkp[Kikanushi]-[Kkn[ku] cha njeo]-Mz-i
- g) Tonaenda shuleni mapema Huendi shuleni mapemba sana [Nafsi ya pili -na-]
Kkn-[Kkp[nafsi3 Lug]-Knj-Mz-a Kkp[Kikanushi]-[Kkn[ku] cha njeo]-Mz-i

Asili: Data za mijarabu ya wanafunzi nyanjani

Data za mijadala ya wanafunzi kuhusiana na matokeo ya mijarabu ya wanafunzi Na. (6.61) ilibainisha kuwa wanafunzi walitumia kanuni ya kimofolojia ambapo viambishi vya njeo vya Kiswahili havikudondoshwa bali waliambisha viambishi vikanushi [t-, te na si-] vya Luganda katika nafsi. Aidha, wanafunzi waliamisha kanuni ya ukanushaji wa Luganda ya kutumia viambishi njeo na hali vinavyofaa pamoja na maumbo ya vikanushi [si. Te- na t-] kimuktadha kuwakilisha hali yakinishi na kanushi. Matumizi haya yalikiuka kanuni ya Kiswahili sanifu ambapo kila umbo la njeo na hali huwakilishwa na umbo yakinishi na umbo kanushi.

Mwanafunzi 30 akijadili jinsi mwingiliano huu ulivyoathiri matumizi ya kanuni ya maumbo ya mofu knushi ya njeo na hali, alieleza kuwa;

“Wanafunzi waliongeza vikanushi [Kkn] vya Luganda [si] katika nafsi ya kwanza ambacho pia kiliwakilisha kiambishi kipatanishi cha nafsi ya kwanza umoja [N] ya Luganda, kuongeza kiambishi [-t] nyuma ya kiambishi kipatanishi [Kkp] cha nafsi ya pili [o] na kikanushi [t-] nyuma ya kiambishi kipatanishi cha nafsi ya tatu [a].”

Aidha akichangia mjadala huu, mwanafunzi 11 alieleza kuwa;

“Wanafunzi ambao L1 ni Luganda walitumia viwakilishi vya njeo na hali yakinishi badala ya kuvibadilisha na viambishi viwakilishi vya njeo na hali vya Kiswahili sanifu. Waliamisha kanuni za ukanushaji wa njeo na hali kutoka Luganda katika ukanushaji wa njeo na hali ya Kiswahili sanifu.”

Matokeo haya yanashadidia utokeaji wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Wanafunzi hawa walifuata kanuni ya Luganda ambayo ilikiuka kanuni ya ukanushaji wa Kiswahili sanifu na kusababisha uhamishaji wa maumbo ya vikanushi na utaratibu wa kutobadilisha maumbo yakinishi ya njeo na hali pamoja na maumbo kanushi ya njeo na hali. Mwingiliano wa kanuni ya maumbo ya ukanushaji wa Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili na kuathiri dhima, dhamira na maudhui ya tungo kimofosintaksia.

Ufafanuzi wa Habwe & Karanja (2004); Hyman (2018); Leah & Sseguya (2015) na Swaleh, (2017) kuhusu udhihirishaji wa maumbo ya kimofolojia ya vipashio vya mofosintaksia vya njeo na hali pamoja na utaratibu wa matumizi ya maumbo wakilishi yakinishi na kanushi ya Luganda na Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanashabihiana na utafiti wa Hafsa, (2016) ambaye katika utafiti wake ulibainisha kuwepo kwa uwiano na tofauti ya udhihirikaji wa

mofu nafsi na njeo baina ya lugha za Kibantu za Kipemba na Kiswahili sanifu. Tofauti na maelezo ya udhihirishaji wa mofu za njeo na hali na taratibu ya ukanushaji, utafiti huu ulibainisha athari za mwingiliano wa kanuni ya kimofolojia ya maumbo ya mofu kanushi za njeo na hali ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kanuni hii inaungwa mkono na Moh'd (2018) ambaye katika ufafanuzi wa kudhihirika kwa mabadiliko ya maumbo ya njeo na hali kutoka muundo wa ndani na nje, anasema kuwa; Kanuni za uyeyushaji, udondoshaji na tangamano la irabu ni za kimofonolojia.

6.1.4.4.2 Kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi katika nyakati na hali

Kanuni ya darajia ya utokeaji wa vikanushi hushikilia kuwa utokeaji wa mofu kanushi katika tungo hutegemea nafasi ya viambishi awali au viwakilishi vya nomino kuu, dhamira (aina ya ukanushaji), idadi ya umoja na wingi, njeo na hali (Hyman Larry, 2018; Leah na Sseguya, 2015 Mulei, 2014; na Ngonyani, 2001). Matokeo ya data za mijarabu za kuhusu tathimini ya kanuni za kidarajia za utokeaji wa vikanushi yalidhihirisha athari za mwingiliano wa kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi kama katika data Na. (6.71).

| | |
|---------------------------------------|-------------------------------------|
| a) [Si-na]-pend-[a] kucheza mpira | Sipechezi kucheza mpira |
| b) [Si-na]-imba wimbo na mwalimu | Siimbi wimbo na mwalimu |
| c) [T-o-na]-ju-[a] kupika chapati. | Hujui kupika chapati |
| d) [T-o-na]-penda kulia kila mara. | Hupendi kulia kila mara |
| e) [T-a-me]-ondoka mapema leo | Hajaondoka mapema leo |
| f) [T-a-me]-jificha kitandani | Hajajificha kitandani |
| g) [A-si-ta]-cheza mpira kesho | hatacheza mpira kesho |
| h) [A-si-na]-penda kulima | Hapendi kulima |
| i) [A-si-] leta chai tamu | hakuleta cha tamu |
| j) [a-si-li-] leta chungwa tamu | Hakuleta chungwa tamu |
| k) U-[si]-jui Kiswahili hapana ongeya | U-[sipo]-jua Kiswahili, usiiongee |
| l) U-[si]-jui kuimba muimbo utaanguka | U-[sipo]-jua kuimba wimbo utaanguka |

Uchanganuzi wa data za maktabani kwa mujibu wa mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya Chomsky (1981) ilidhihirisha kuwa ukanushaji wa njeo na hali katika Luganda sanifu hutanguliwa na vikanushi, ukifuatwa na viambishi viwakilishi vya nomino ambavyo huambikwa kwenye vitenzi vinavyokanushwa kuwakilisha idadi ya umoja na wingi. Tofauti na lugha zingine za Kibantu kama Kiswahili kilicho na mofu wakilishi kanushi ya njeo na hali isipokuwa wakati ujao, Luganda haina maumbo au mofu kanushi wakilishi ya njeo na hali bali hutumia maumbo ya kifonoloji ya kuambishi mofu kanushi ya irabu [t-]; mofu

kanushi ya konsonanti [te-] na mofu [si-] inayotumiwa katika nafasi ya [N] kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja yanayowekwa kabla au nyuma ya viwakilishi vya nomino na njeo katika tungo kuwakilishi dhana ya ukanushi wa tungo. Ukanushaji wa tungo za kimofosintaksia za sentensi rejeshi hutokea katika nafasi tofauti ya utokeaji wa mofu kanushi za njeo na hali katika tungo. Mofu kanushi hutokea nyuma ya kitenzi mbele ya kiambishi kiwakilishi cha nomino kutokana na kirejeshi kutokea katika nafasi hiyo.

Matokeo ya data za mijadala ya wanafunzi kuhusiana na kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa vikanushi katika nyakati na hali ulibainisha mwingiliano wa darajia ya utokeaji wa vikanushi kama inavyojitokeza katika data za mijarabu ya wanafunzi kama katika data Na. (6.62, Uk 354; 6.63, Uk. 357; 6.64, Uk. 359; 6.65, Uk 360; 6.66, Uk. 361; 6.67, Uk. 361; 6.68, Uk. 362). Mijadala ya matokeo ya data ilidhihirisha nafasi ya utokeaji wa kikanushi [si-] cha nafsi ya kwanza ambacho kimetumika kiusahihi kama katika Mifano ya [a na b] na kiambishi kinachofuata ambacho ni kiwakilishi cha njeo ya wakati uliopita kutumiwa visivyo. Kiambishi hiki hakistahili kutokea katika nafasi hii kwa sababu katika ukanushaji wa wakati uliopo, kiambishi hiki hudondoshwa na kiambishi tamati [-a] kubadilika na kuwa [i]. Viambishi [-na-] na [-a] vimetumika katika darajia na nafasi ambayo haistahili kutumika. Viambishi hivi vilistahili kutokea katika tungo yakinishi bali sio kanushi. Mwingiliano uliojitokeza kwa hivyo ni ule wa kudondosha viwakilishi vya nyakati na kiambishi tamati cha kibantu [-a] na katika nafasi yake kutumia kiambishi kikanushi [-i]. hali hii iliathiri tahajia kutoka na kuchanganya vikanushi na maumbo yakinishi ya Kiswahili sanifu

Mwingiliano uliojitokeza ni ule wa kutumia maumbo ya ukanushaji ya Luganda katika ukanushaji wa nafsi ya pili ya Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika mifano ya [c na d]. Hali hii ilitokana na kuchanganya umbo wakilishi la nafsi ya pili [o-] ya Luganda badala ya [u-] ya Kiswahili sanifu. Kutokana na uhamishaji wa kiwakilishi nafsi cha Luganda katika Kiswahili sanifu, wanafunzi vilevile walihamisha kikanushi cha irabu [t-] cha Luganda katika ukanushaji wa utungo wa kimofosintaksia wa Kiswahili sanifu katika nafsi ya pili. Pia, wanafunzi walishindwa kudondosha kiwakilishi cha wakati uliopo [-na-] na kuijumlisha katika tungo. Matumizi ya umbo nafsi [o-] na kikanushi cha Luganda cha irabu [t-] pamoja na kudondosha kiwakilishi cha njeo [-na-] na kubadilisha kiishio [-a] katika tungo kanushi ya kimofosintaksia, iliathiri usanifu wa tungo kanushi ya nafsi ya pili katika Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu kikanushi [t-] na kiwakilishi nafsi [o-] yalitokea katika nafsi ya viwakilishi

vikanushi [ha] na kiwakilishi nafsi ya pili [u]. Aidha, kiwakilishi njeo hakikustahili kutokea katika nafasi hiyo bali kudondoshwa na kiishi [-a] kubadilishana na kikanushi [-i].

Mwingiliano mwingine wa darajia na utokeaji wa vikanushi ulijitokeza katika mifano ya [e na f] ambayo ni nafsi ya tatu. Mijadala ya wanafunzi wakijadili tathimini ya athari za mwingilia ulibaini kuwa, wanafunzi walihamisha kikanushi cha Luganda [t-] na kukiweka katika nafsi ya kikanushi cha Kiswahili sanifu [-a]. Vile vile, wanafunzi walishindwa kudondosha kiambishi cha hali tumilifu [-me-] na kuibadilisha na kikanushi chake [-ja-]. Matumizi haya yalikiuka kanuni ya darajia na utokeaji wa vikanushi vya Kiswahili sanifu kwani walitumia vikanushi vya Luganda [t-]. Mwanafunzi 3 akijadili athari kutokana na mwingiliano wa kanuni alieleza kuwa;

“Katika Luganda, maumbo ya njeo na hali huwa hayana viwakilishi vikanushi. Kwa hiyo, wanafunzi walihamisha na kuchanganya maumbo na utaratibu wa Luganda katika ukanushaji wa nafsi ya tatu ya Kiswahili sanifu.”

Kwa mujibu wa mijadala ya wanafunzi; ilidhihirika kuwa wanafunzi walivunja kanuni ya kidarajia na nafasi ya utokeaji wa vikanusho kwa kutumia kikanushi [si-] cha nafsi ya kwanza katika nafasi amabyo hakikustahili kutokea kama katika mifano ya [f – i] ambayo ilitokea katika nafsi ya tatu wakati uliopita, uliopo na ujao. Aidha, viwakilishi vya njeo vilidhihirika kutumika lakini katika nafsi ambamo havikustahili kutokea. Vilevile kikanushi [ha-] kilidondoshwa na hivyo kufanya ukanushaji wote kuwa wa ujumlishaji ambao haukuzingatia kanuni ya ukanushaji wa Kiswahili sanifu. Uhamishaji wa kikanushi [si-] cha nafsi ya kwanza na kukiweka katika tungo za nafsi ya tatu kama kikanushi uliathiri utaratibu wote wa ukanushaji katika Kiswahili sanifu. Hali hii ilijenga mchanganyiko wa matumizi ya viwakilishi nafsi kanushi, kikanushi [si-] na viwakilishi vya njeo. Matumizi ya kikanushi [-si-] yalitokana na utaratibu wa Luganda kuweka vikanushi vyake baada ya kiambishi nafsi ay kiambishi kipatanishi cha msingi kinachowakilisha umoja na wingi wake.

Tathimini ya matumizi ilibaini viambishi vikanushi ambavyo vilistahili kutokea katika nafasi ya viwakilishi njeo na hali vikipuuzwa na badala yake viwakilishi vya njeo na hali yakinishi vikibakisha hadhi yake katika utaratibu wa ukanushaji ambao ulifanywa na wanafunzi ambao L1 ni Luganda. Matumizi haya ya wanafunzi katika tungo na mijadala yao uliharibu utaratibu wa ukanushaji ambao hujitokeza katika Kiswahili sanifu na hivyo kuathiri sarufi ya tungo za kimofosintaksia, upatanishi wa kisarufi, dhima na dhamira ya ukanushaji wa tungo. Ukiukaji huu ulitokana na Luganda kutokuwa na maumbo wakilishi ya ukanusho wa njeo na hali bali

viwakilishi [si-] ya nafsi ya kwanza, [t-] ya irabu na [te-] ya konsonanti. Matumizi haya yalikiuka darajia na nafasi ya utokeaji wa vikanushi vya Kiswahili sanifu na kuathiri usarufi wa Kiswahili sanifu kitahajia na kiupatanisho.

Swaleh, (2017), Mgullu, (1999), Masamba na Wenzake (2009), Habwe & Karanja, (2004) walibainisha mofimu kanushi za njeo na hali katika Kiswahili sanifu na utokeaji wake. Rose, (2009), Kiyinikibi, (2013: 2021), Leah & Sseguya nao walitambua mofu kanushi na kueleza nafasi za utokeaji wake katika Luganda. licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za nasaba moja, Utafiti huu ulidhihirisha kuwa nafasi ya utokeaji wa maumbo wakilishi ya ukanushaji katika Luganda na Kiswahili huwiana na kutofautiana. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha athari za mwingiliano wa matumizi ya kanuni ya kidarajia ya utokeaji wa Luganda katika matumizi ya ukanushaji wa njeo na hali katika Kiswahili sanifu. Athari hizi ziliathiri usanifu wa Kiswahili kudhihirisha uhusiano milikishi na unganifu wa viambajengo vya kimofosintaksia katika tungo za Kiswahili sanifu.

6.1.4.4.3 Kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji wa nyakati na njeo

Kanuni hii hushikilia kuwa baadhi ya fonimu zilikaribiana na fonimu fulani kama ni irabu au konsonanti, ujirani huo husababisha mabadiliko ya fonimu mbalimbali yanayojitokeza katika maandishi au mazungumzo (Chomi 2003; Habwe & Karanja, 2004). Data ya nyanjani kutokana na mjarabu ya kisarufi ilidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji wa fonimu irabu ambazo huathiriana wakati wa matumizi kama katika data Na. (6.72).

| <i>Hali yakinishi</i> | <i>Mwingiliano wa kifonolojia</i> | <i>Kiswahili sanifu</i> |
|--|--|-------------------------|
| a) Ulipotea njia | <i>Haulipotea njia</i> | Hukupotea njia |
| b) Unaugua | <i>Haunaugua</i> | Huungui |
| c) Utapika wali | <i>Hautapiga wali</i> | Hutapiga wali |
| d) Umefanya kosa | <i>Haumefanya kosa</i> | Hujafanya kosa |
| e) Apendi | <i>Haapendi</i> | Hapendi |
| f) Aongei | <i>Haaongei</i> | Haongei |
| g) <i>U-[si]-jui Kiswahili hapana ongeya</i> | <i>U-[sipo]-jua Kiswahili, usiiiongee</i> | |
| h) <i>U-[si]-juikuimba muimbo utaanguka</i> | <i>U-[sipo]-jua kuimba wimbo utaanguka</i> | |

Kwa kurejela kanuni ya kimofonolojia ya ukanushaji wa nyakati na njeo, tathimini ya matumizi ilibaini kuwa wanafunzi walikosa kudondosha kiambishi [-a] cha kikanushi [ha] na kubakisha kiwakilishi nafsi [u-] ambapo kikanushi katika nafsi ya pili kilistahili kuwa [hu-]

badala ya [hau-]. Kwa mujibu wa Kiswahili sanifu, udondoshaji huu hufanyika katika ukanushaji wa nafsi ya tatu ambapo kikanushi [hu-] hutumika badala ya kikanushi cha [h-a-u]. Matokeo haya yanakubaliana na mihimili ya kanuni ya Ubia na upatanishi ambayo hushikilia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo hasa katika kufafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.

Licha ya kuwa Luganda na Kiswahili hidhihirisha kanuni hii ya kimofosintaksia, Data ya mijarabu ya wanafunzi ilidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya kifonolojia ya Luganda ambayo kwayo fonimu /a/ ilitahili kudondoshwa katika mchakato wa ukanushaji wa nafsi ya pili na nafsi ya tatu katika maandishi. Aidha, wanafunzi waliongeza mofu ya njeo badala ya kuidondosha kulingana na kanuni ya Kiswahili na kuibadilisha na mofu kanushi ya njeo ya wakati wa [-me-] na [-li-]. Mwanafunzi 52 akichangia katika mjadala wa jinsi mwingiliano ulivyoathiri Kiswahili sanifu alieleza kuwa,

“Wanafunzi ambao LI walidondosha fonimu ya kikanusho [h-] cha Kiswahili pamoja na kiambishi cha wakati [-po-] ambavyo vilistahili kuongezwa kwenye kiwakilishi nafsi cha nafsi ya tatu na [-po-] kuwekwa mbele ya kikanushi [si-] kuwakilishai ukanushaji wa wakati wa [-po-] na hivyo kwenda kinyume na kanuni ya kifonolojia ya Kiswahili.”

Matokeo haya yanashadidiwa na Lupogo (2021), Mulei (2020) Massamba na wenzake (2009), Swaleh, (2017) ambao walidhihirisha udondoshaji wa {-a-} inayotokea katika kikanushi {h-a} na kutumia {-u-} katika ukanushaji. Swaleh (2017) anathibitisha kanuni hii kwa kuelezea kuwa:

“...kiambishi {hu-} kimetumika badala ya {ha-} kwa sababu ya mabadiliko ya kimofonolojia ambapo {ha-} ya ukanushi ikifuatwa na {u}, basi kunatokea udondoshi wa vokali ya kwanza ambayo ni {a}.”

6.1.4.4.4 Kanuni ya uambishaji/uongezaji wa mofu kanushi

Kanuni hii hushikilia kuwa uambishaji wa viambishi katika tungo huzingatia mpangilio maalumu. Mpangilio unaokubalika na ambao ni lazima uzingatiwe ni ule wa kutumia viambishi mwafaka vinavyopatana na maneno mengine katika nafasi inayofaa kujenga dhana inayokubalika kisarufi (Besha, 1996 na Kyagaba, 1996). Uambishaji wa viambishi nafsi, njeo na ngeli kwenye vitenzi huathiri mofu kanushi ambazo huambikwa kwenye kategoria hizi za

maneno kujenga sarufi inayokubalika. Kupotoka kutumia kanuni ya uambishaji isiyokubalika kisarufi huweza kupotosha aina ya vikanushi vinavyostahili kuambishwa kwenye vitenzi na hivyo kupotosha usanifu wa lugha (Chomi 2003 na Leah & Sseguya 2015).

Tathmini ya data za mijarabu ya wanafunzi ilibaini kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikiuka matumizi sahihi ya kanuni ya uongezaji wa mofu kanushi. wanafunzi waliambisha viambishi vikanushi vya Luganda katika ukanushaji wa njeo na hali za Kiswahili sanifu. Aidha, walitumia utaratibu wa ukanushaji wa Luganda katika ukanushaji wa Kiswahili sanifu kwa kuhamisha maumbo na utaratibu wa uambishaji wa vikanushi wa njeo na hali katika Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika data Na. (6.63 Uk. 358).

Mijadala ya data Na. (6.63) ya jinsi wanafunzi walivyohamisha viambishi vikanushi vya Luganda katika ukanushaji wa njeo na hali za Kiswahili sanifu. Mwanafunzi 24 akichangia mjadala huu ailieze kuwa;

“Wanafunzi walitumia utaratibu na ukanushaji wa Luganda katika kiswahili sanifu kwa kuhamisha maumbo na utaratibu wa uambishaji wa kuhamisha vikanushi [si-] na [t-]. Kudondosha fonimu [h] ya kikanusho cha Kiswahili [ha] na kuongeza viambishi viwakilishi vya njeo yakinishi badala ya kividondosha na kuvibadilisha na viambishi vya njeo na hali kanushi.”

Mwingiliano huu uliathiri upatanishi wa kisarufi wa viambishi kudhihirisha utawala na ufungamanisho wa viambishi vikanushi katika tungo, kupotoshwa kwa dhima na dhamira pamoja na tahajia ya kisarufi ya Kiswahili sanifu. Kwa kutumia kifaa cha udondoaji data kutokana na mijarabu ya wanafunzi, utafiti huu vilevile ulibaini kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda waliongeza vikanushi vya Luganda [sinnaba] ambayo kwa Kiswahili ni [bado] pamoja na [apana] kuongeza nyuma ya vitenzi kama vikanusho kama ilivyojitokeza katika data ya mijarabu Na. (6.73).

| | | | |
|-------------------------------|-----------|--------------------------|--------------------|
| <i>a) Mimi bado kuchoka</i> | Sijachoka | <i>Sisi bado kuchoka</i> | <i>Hatujachoka</i> |
| <i>b) Wewe bado bado kula</i> | Sijala | <i>Nyinyi bado kula</i> | Hatujala |
| <i>c) Yeye bado kuja</i> | Hajaja | <i>Wao bado kija</i> | Hawajaja |
| <i>d) Mimi apana jua</i> | sijui | <i>Sisi apana jua</i> | Hatujui |
| <i>e) Wewe apana lima</i> | Usilime | <i>Nyinyi apana lima</i> | Msilime |
| <i>f) Yeye apana cheza</i> | Hachezi | <i>wao apana cheza</i> | Hawachezi |

Matokeo ya mijadala kutokana na data hii ulidhihirisha uambishaji wa vikanushi vya kipekee ambavyo Luganda hutumia katika Kiswahili sanifu. Wanafunzi walitumia kiambishi –na-kuwakilisha wakati uliopo hali timilifu [-me-] ambacho huwekwa kwenye kitenzi, katika

kukanusha hali ya [-me-]. Silabi hii, huongezwa kwenye kikanushi [-naba] ambacho huongezwa baada ya kikanushi [si-] cha nafsi ya kwanza, [te-] ya konsonanti na [t-] ya irabu ikifuatwa na ku- ya kitenzi jina. Kwa kutumia utaratibu huu, wanafunzi walikanusha vitenzi vya hali timilifu kwa kuongeza kikanushi [bado] ambacho ni [*sinaba* na *tetunaba*] na kuongeza kikanushi [apana] kilichodondosha fonimu [h] katika kukanusha wakati uliopo. Matumizi haya yaliendana na mihimili ya sarufi bia na upatanishi ya nadharia ya umilikifu na ufungami ya Chomsky (1981). Hali ambayo ilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu licha ya kuwa lugha ya nasaba moja yenye matumizi ya kanuni moja, lugha hizi ni lugha mbili tofauti kutokana na ofauti ndogo ambazo hujitokeza katika matumizi ya kanuni moja za kimofosintaksia.

Matokeo haya yalikiuka kanuni ya maumbo wakilishi ya Kiswahili sanifu kama yalivyofafanuliwa na Lupogo, (2021), Mulei (2014 na 2020), Massamba na wenzake (2009), Swaleh, (2017), Mgullu, (2017), Habwe & Karanja (2004) ambao walifafanua maumbo ya njeo na hali na kudhihirisha nafasi ya utokeaji wake na matumizi yale kuwakilisha dhima yakinishi na kanushi. Swaleh (keshatajwa) anakubaliana na Beaudoin, (1999) ambaye anaeleza kuwa; “*Kuna mofimu nyingine zinazoongezewa kwenye ukanushi ambazo ni mofimu za kukanusha njeo au hali kama ya -i, -ja- na ku katika Kiswahili.*” Kwa kuongezea, Swaleh (2017) alitambua mofimu tatu za **ha-**, **-si-** na **-to** ambazo aliamini kuwa ndizo zinazohusika katika ukanushaji wa matendo yakini ya Kiswahili sanifu.

6.1.4.4.5 Kanuni ya udondoshaji wa mofu kanushi katika kauli yakinishi

Kanuni hii hushikilia kuwa baadhi ya vipashio vya kisarufi katika tungo virai hudondoshwa na badala yake kutumika mofu mbadala kudhihirisha hali kanushi ya vitenzi. Tathimini ya kanuni hii kutokana na kazi ya Leah & Sseguya (2015), Rose, (2009), Kamoga (1968) na Kiyinikibi (2013:2021) Luganda hudondosha kipatanishi cha nafsi ya kwanza [n] ya Luganda na katika nafasi yake mofu kanushi [si-] kutumika. Matokeo ya uchanganuzi wa mijarabu ya kisarufi na mijadala ya wanafunzi, ulibaini ukiukaji wa kanuni ya udondoshaji katika ukanushaji wa nafsi ya kwanza ya Kiswahili. Wanafunzi walidondosha kiwakilishi cha nafsi ya kwanza [ni-] kama inavyotekelezwa katika Luganda na kushindwa kudondosha kiwakilishi cha wakati uliopita na kiishio [-a] ambacho kilistahili kubadilishwa na kiambishi kanushi [-i]. Aidha kwa mujibu wa kanuni hii, viambishi vya njeo vya Kiswahili havikudondoshwa kutoka katika kauli yakinishi na kutumia viwakilishi vikanushi vya njeo na hali kama inavyojitokeza katika mifano (6.74).

- | | | |
|------------------------------------|----------------------------------|-----------------------|
| a) <i>Si-[na]-imb-[a]</i> | Siimb-i | [kutotondosha] |
| b) <i>Ha-[u-li]-cheza</i> | Hukucheza | |
| c) <i>Ha-u-li-ogopa kula</i> | Hukuogopa kula | |
| d) <i>Ha-u-li-potea njia</i> | Hukupotea njia | |
| e) <i>A-si-one nyoka atakuluma</i> | Usipomwona nyoka anaweza kukuuma | |

f) *Ni-si-kimbia mvuwa tanyeshe mimi Nisipokimbia mvua itaninyeshea [udondoshaji] [e-f]*

Kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia na upatanisho ya nadharia ya umilikifu na ufungami, Mifano ya [a-d], ilidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya udondoshaji wa viambishi njeo wakilishi vya Kiswahili na wa kubadilisha viambishi vya njeo kanushi na kiishio [-a] katika kirai cha wakati uliopita. Aidha, Mfano wa [e na f] unadhihirish uzingatifu wa kanuni ya udondoshaji. Hata hivyo udondoshaji uliofanywa haukuzingatia kanuni ya ukanushaji wa kiambishi cha wakati wa [-po-] ambao kiwakilishi hiki cha wakati huwa hakindondoshi kimatumizi kama ilivyo katika wakati wa [-ki- na -ta-]. Matumizi haya yalidhihirisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili kuingiliana katika matumizi ya kanuni ya udondoshaji wa mofu kanushi, lugha hizi hudhihirisha tofauti katika matumizi ya kanuni hii katika vpashio vya kimofosintaksia. Kwa hivyo, matumizi ya utaratibu wa udondoshaji wa viwakilishi njeo kutoka katika Luganda na kuungiza katika ukanushaji wa njeo na hali katika Kiswahili sanifu uliathiri upatanisho wa kisarufi katika ukanushaji na hivyo kupotosha dhima na dhamira ya tungo ya Kiswahili kimofosintaksia.

Matokeo haya yanashadidiwa na ufafanuzi wa Mgullu, 1999; Chomi, 2003, Ngonyani 2001 na Habwe & Karanja, (2004) kuhusu udondoshaji wa viambishi wakilishi vya njeo na kutumia maumbo yakinishi. Aidha, kulingana na wataalamu hawa, udondoshaji hutokea kwenye vitenzi vyenye kiambishi kipatanishi cha nafsi ya kwanza na njeo. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya udondoshaji na ubadilishanaji wa maumbo yakinishi na kanushi ya njeo na hali katika Kiswahili sanifu. Wanafunzi walitumia utaratibu wa Luganda katika ukanushaji wa tungo katika Kiswahili sanifu na kuathiri mofosintaksia ya viambajengo kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu katika tungo.

6.2 Hitimisho

Sura hii iliwasilisha matokeo ya madhumuni ya tatu ya kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Matokeo yalionyesha tathimini ya kanuni za vipashio vya ngeli katika nomino, viwakilishi nafsi,

vivumishi na vikanusho za uundaji wa nomino, kanuni ya sarufi maumbo, kanuni ya urejeshi, kanuni ya sarufi maumbo, kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji, uongezaji kanuni ya uwakilishi dhima wa matumizi ya nomino, kanuni ya vivumishi ya kimofolojia ya uambishaji, kanuni ya kifonolojia, kanuni ya umiliki na usabaki, kanuni ya ukuu na darajia ya utokeaji, kanuni ya muungano wa viwakilishi nafsi, kanuni ya uambishaji, kanuni ya upatanishi wa mofimu, kanuni ya mofolojia, kanuni ya kimapokezano masharti, kanuni ya uongezaji maumbo, maumbo wakilishi ya vikanusho za matumizi ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na maandishi na mazungumzo ya wanafunzi yalidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli katika nomino (nomino katika ngeli), vivumishi, viwakilishi na vikanushi. Kufanana na kutofautiana kwa kanuni za vipashio vya mofosintaksia vya Luganda katika matumizi kulisababisha athari za mwingiliano wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti ilibaini athari za uhamishaji wa kanuni na maumbo, ubadilishanaji, ujumlishaji, uchopekaji na uongezaji fonimu na maumbo kimofofolojia kama ilivyojadiliwa.

SURA YA SABA

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO UTAFITI

7.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari wa utafiti kwa ujumla, muhtasari wa mahitimisho ya matokeo yaliyopatikana maktabani na nyanjani, mapendekezo ya kiujumla na ya tafiti za baadaye, changamoto zilizokumba utafiti huu, na mchango wa utafiti huu kitaaluma.

7.2 Muhtasari wa matokeo

Matokeo ya utafiti huu ni kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye kanuni na miundo ya kiisimu ambayo ina ukuruba na lugha nyinginezo za Kibantu. Ukuruba wa vipashio na kanuni za kimofosintaksia za Luganda na Kiswahili sanifu ulidhihirisha athari za mwingiliano ambao ulisababisha matumizi ya Kiswahili yasio sanifu. Ilibainika kuwa, licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, lugha hizi huwiana na kutofautiana katika matumizi ya vipashio na kanuni za kimofosintaksia. Uwiano na tofauti ulidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha mbili tofauti licha ya kuwa ni lugha za nasaba moja. Kwa muhtasari, matokeo ya utafiti huu yamepangwa kulingana na madhumuni matatu ya utafiti.

7.3.1 Kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu

Vipashio vilivyoelezwa vilikuwa vinne vya mofosintaksia vya ngeli za nomino, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanushi katika Luganda na Kiswahili sanifu. Utafiti ulichunguza muundo wa ngeli, viwakilishi nafsi, vikanushi na vivumishi kama vinavyotumika katika Luganda na Kiswahili sanifu ili kutambua jinsi vinavyofafanana na kutofautiana.

Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa vipashio vya kimosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu hufanana na kutofautiana kimuundo (sifa), kidhima, nafasi ya utokeaji wa vipashio katika tungo kuonyesha uamilifu wake na vipashio vingine katika sentsensi. Kufanana na kutofautiana huku kulibainisha kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti zenye vipashio vya kimofosintaksia vinavyodhihirisha sifa za kiisimu zilizo za kipekee. Kwa sababu ya upekee huu, matumizi yake lazima yatumike kulingana kwa mujibu wa sifa za kimofosintaksia za vipashio. Ukiukaji wa kutozingatia sifa hizi huweza kuathiri matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu.

7.3.2 Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi

Uchanganuzi ulidhihirisha kwamba; matumizi ya kila kipashio cha kimofosintaksia katika Luganda na Kiswahili sanifu hujitokeza katika muktadha wa tungo kwa kuzingatia mfumo au utaratibu maalumu, na mabadiliko ya kimiundo au mfumo huweza kuathiri matumizi ya vipashio vingine katika tungo kimofosintaksia. Hali kadhalika, iligunduliwa kuwa mfumo au utaratibu ni nguzo ya kudhihirisha uhusiano wa kisarufi uliopo baina ya vipashio vya kimofosintaksia unaofafanua usanifu au usahihi katika matumizi ya lugha.

Aidha, matokeo yalibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni kadhaa zinazofafanua matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia ambazo hutegemea: muundo/sifa za kipashio, maumbo ya kipashio, mpangilio au nafasi ya utokeaji wa kipashio, upatanishi wa kisarufi wa kipashio, uwakilishi maumbo ya kipashio na dhima ya matumizi ya kipashio katika tungo. Kila kipashio cha kimofosintaksia cha Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni zinazofafanua mifanyiko au matumizi yake. Mathalani, matokeo ilidhihirika kuwepo kwa mshabihiano na tofauti za kanuni zinazofafanua matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu yaliyojitokeza katika mazungumzo na maandishi.

Utafiti huu ulibaini kuwa uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za mifanyiko iliyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ilitokana na utaratibu wa matumizi ya kipashio kudhihirisha muungano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo na suala la umiliki na usabaki baina ya neno kuu na maneno mengine katika tungo hutegemea muundo au sifa za kipashio, dhima na dhamira yake, nafasi/ukuu wa darajia na utokeaji wa kipashio katika tungo, uwakilishi/uambishaji maumbo, umilikifu/utawala wa kipashio katika tungo na mabadiliko ya kifonolojia katika ujenzi wa tungo za kimofosintaksia.

7.3.3 Tathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu

Tathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda yalidhihirisha kuwa Luganda ni lugha ya Kibantu ambayo huongozwa na kanuni au mfumo sanifu wa matumizi ya vipashio mbalimbali vya kimofosintaksia kama ilivyo lugha ya Kiswahili sanifu. Kanuni hizi ni taratibu zinazotawala matumizi ya viwango au vipashio vya kisarufi vya mofosintaksia katika kuunda kipashio kikubwa cha kisarufi. Kanuni hizi ni sanifu kwa sababu ni taratibu za lazima zilizowekwa kumwongoza mzungumzaji na mwandishi wa lugha. Kanuni za kimofosintaksia

ni zile zilizowekwa na wanaisimu kuhifadhi hadhi au sifa za lugha na ambazo hutumika kupima viwango vya umilisi wa mazungumzo na maandishi. Ukiukaji wa kaida hizi hudhihirisha ukosefu wa usanifu na urasmi wa matumizi ya lugha hii. Kwa mujibu wa utafiti huu, viapashio vya kimosintaksia vya ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho vya Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni ambazo hufanana na hutofautiana kutoka kipashio kimoja hadi kingine (kanuni leksia) katika matumizi.

Utafiti huu ulibaini kuwa, hata ingawa kila kipashio huongozwa na kaida fulani, matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia katika muundo wa sentensi huunganishwa na kutawaliwa na kanuni za kimofosintaksia ambapo kila lugha huwa na kanuni za kipekee zinazobainisha na kuitofautisha lugha moja na nyingine. Luganda na Kiswahili sanifu zina mifumo ya kimofolojia na kisintaksia za matumizi ya vipashio vya kisarufi zinazotofautiana, japo zote ni lugha za Kibantu. Tofauti hizi huzua athari za kanuni za kimofosintaksia za vipashio vya kisarufi vya ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Hali hii ilitokana na athari za aina moja za kitahajia za mofolojia na sintaksia zinazotokana na uhamishaji, ubadilishanaji, uchanganyaji, ukopaji wa kanuni za Luganda katika matumizi ya vipashio vya Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi ya wanafunzi uliojitokeza katika mijadala, mijarabu ya kisarufi ya wanafunzi.

Matokeo ya tathimini ya kanuni yalidhihirisha kuwa kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho vya Luganda huhusiana na kutofautiana kutegemea sifa bia, upatanisho wa kisarufi, na muungano wa kipashio kimoja na kingine katika tungo kutegemea neno kuu. Mahusiano na tofauti za matumizi ya kanuni hizi yaliongozwa na kanuni za sifa bia ambazo huhusiana na kutofautiana kutegemea muundo au sifa za kipashio, mofolojia na uwakilishi wa maumbo au uambishaji maumbo ya kipashio, ukuu, darajia na utokeaji wa kipashio, dhima ya kisarufi ya kipashio, dhamira ya kipashio, kanuni za muunganiko au umilikifu na usabaki (upatanisho wa kisarufi), mabadiliko ya mofofonolojia, kanuni ambazo hudhihirisha muungano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo na suala la umiliki na usabaki baina ya neno kuu na maneno mengine katika tungo. Kanuni za sarufi bia, muungano/ufungami na umilikifu zilisababisha mwingiliano wa matumizi ya kanuni za mofosintaksia za Luganda katika Kiswahili sanifu.

Aidha, iligunduliwa kwamba kuna athari za mwingiliano kadha za Luganda katika matumizi ya kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ulisababisha athari za kitahajia, kisarufi, uchanganyaji wa ndimi na matatizo ya kutafsiri

dhana za Kiswahili kwa misingi wa Luganda, ukopaji na uongezaji wa maumbo na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia, uhamishaji wa kanuni za Luganda katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu, uhamishaji wa dhamira na dhima za vipashio kutoka Luganda hadi Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi. Mwingiliano huu wa matumizi ya kanuni za vipashio vya kimofosintaksia ulitokana na mofolojia na sintaksia ya uundaji wa vipashio, uwakilishi dhima na dhamira ya kisarufi ya kipashio katika tungo, umilikifu na usabaki wa vipashio katika tungo, ukuu, darajia na mazingira ya utokeaji wa kipashio katika tungo na muungano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo. Kwa kuzingatia vipimo hivi, matokeo ya kutathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda yaliathiri matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda sanifu kutokana na kuhamisha, kukopa, kuchanganya, kutafsiri, kubadilishana kanuni, uundaji kanuni mpya kutokana na kanuni ya L1, kujumlisha kanuni, kudondosha kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu.

Ushahidi wa matokeo ya mwingiliano huu ulibainika kutokana na dosari nyingi za aina au hali moja za kimofolojia na kisintaksia zilizojitokeza katika mazungumzo na maandishi ya wanafunzi kutoka katika mijadala na mijarabu ya kisarufi. Utafiti ulibaini athari za kimofolojia na kisintaksia za uhamishaji wa maumbo kimofolojia, dhima na dhamira za kisarufi kimofosintaksia mabadiliko ya kimofofonolojia ya maumbo kimofolojia, tafsiri ya vipashio kutoka Luganda hadi Kiswahili sanifu, uchopekaji na uongezaji fonimu na maumbo kimofofolojia, ubadilishanaji wa maumbo wakilishi wa vipashio, ukopaji wa viambishi vipatanishi msingi (VPM) wakilishi, ujumlishaji wa matumizi ya maumbo na sifa za kipashio, hali ambayo iliathiri tahajia, dhima na dhamira (semantiki) ya kisarufi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho vya Kiswahili sanifu na hivyo kujenga lugha kadiriya isiyo Kiswahili sanifu.

7.4 Mahitimisho

Kwa kuzingatia mhimili wa sarufi bia na upatanifu, kama ulivyoelezwa na Chomsky 1981, utafiti huu ulibaini kuwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu hufafanana na kutofautiana kisarufi. Uwiano huu na tofauti hutokana na kauli kuwa msingi wa kanuni zinazotawala sarufi ya lugha ni uwiano wa kisarufi uliopo baina ya vipashio mbalimbali vinavyounda tungo. Mahitimisho ya utafiti huu yamewasilishwa kwa kuzingatia madhumini matatu ya utafiti huu. Utafiti huu unahitimisha kama ifuatavyo.

7.4.1 Kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu

Uchanganuzi wa matokeo ya kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu ulibaini kuwa vipashio vya kimosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu hufanana na kutofautiana kimuundo (sifa), dhima na dhamira ya kisarufi, nafasi ya utokeaji wa vipashio katika tungo na maumbo kimofolojia na kisintaksia, ukuu, darajia na mazingira ya utokeaji wa maumbo, uainishaji, umilikifu na usabaki wa vipashio katika tungo, na kanuni za matumizi ya vipashio husika. Aidha, tofauti za kimofosintaksia kati ya Luganda na Kiswahili sanifu pamoja na kanuni zinazoongoza matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wilayani Kampala. Matokeo haya yalidhihirisha kuwa. Luganda na Kiswahili ni lugha za Kibantu zenye vipashio vya kiisimu vinavyofanana na kutofautiana. Uwiano ni ule ukuruba uliopo baina ya lugha za Kibantu zenye mnasaba mmoja. Vilevile, ilibainika ukuruba na tofauti baina ya lugha mbili tofauti zenye mtagusano wa muda mrefu, husababisha mwathiriano wa lugha husika kuchukua baadhi ya sifa za vipashio vya kiisimu vya mofolojia na sintaksia kutoka lugha nyingine na kuingiza katika matumizi ya lugha yake.

7.4.2 Uchanganuzi wa kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi

Uchanganuzi wa kanuni ulibaini kuwa kanuni ndio nguzo ya pekee inayoweza kufafanua uhusiano wa vipashio vya kimofosintaksia katika muktadha wa tungo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kwa mujibu wa kanuni hizi, uchanganuzi wa kanuni za Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni kadhaa zinazofafanua matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia ambazo hutegemea, muundo au sifa za kipashio, maumbo ya kipashio, mpangilio au nafasi ya utokeaji wa kipashio, upatanishi wa kisarufi wa kipashio, mabadiliko ya kimofonolojia, uwakilishi maumbo ya kipashio na dhima ya matumizi ya kipashio katika tungo. Kwa mujibu wa uchanganuzi, ilibainika kuwa kila kipashio cha kimofosintaksia cha Luganda na Kiswahili sanifu huongozwa na kanuni zinazofafanua mifanyiko au matumizi yake. Hata hivyo, kanuni hizi ziliwiana na kutofautiana kutoka kipashio kimoja na kingine na kutoka lugha moja na nyingine.

Matokeo yalidhihirisha mshabihiano na tofauti za kanuni zinazofafanua matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, mshabihiano na tofauti za

mifanyiko iliyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu ni ya utaratibu wa matumizi ya kipashio kudhihirisha muungano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo. Kufanana na kutofautiana huku kulibainika kutegemea muundo au sifa za kipashio, dhima na dhamira yake, nafasi/ukuu wa darajia na utokeaji wa kipashio katika tungo, uwakilishi/uambishaji maumbo, umilikifu/utawala wa kipashio katika tungo na mabadiliko ya kifonolojia katika ujenzi wa tungo za kimofosintaksia. Matokeo haya kwa hivyo yalidhihirisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye kanuni na miundo ya kiisimu ambayo ina ukuruba na lugha nyinginezo za Kibantu. Ukuruba na tofauti baina ya lugha mbili tofauti zenye mtagusano wa muda mrefu kama inavyojitokeza baina ya Luganda na Kiswahili sanifu, husababisha mwathiriano wa lugha katika matumizi. Athari za mwathiriano huu ni ule wa lugha moja husika kuchukua baadhi ya sifa za vipashio vya kiisimu vya mofosintaksia kutoka lugha nyingine na kuingiza katika matumizi ya lugha yake kama ilivyojitokeza miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda.

7.4.3 Tathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu

Tathimini za kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda, imebainisha kwamba Luganda na Kiswahili sanifu zina mifumo ya kimofolojia na kisintaksia za matumizi ya vipashio vya kisarufi zinazowiana na kutofautiana, japo zote ni lugha za Kibantu. Tofauti za kanuni za Luganda na Kiswahili sanifu ndizo zinazozua mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia za vipashio vya kisarufi vya ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ndio ulioharibu kaida za matumizi sanifu ya vipashio kutokana na uhamishaji, ukopaji, ubadilishanaji wa kanuni za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, ujumlishaji wa kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu na uundaji wa kanuni mpya ambayo kwayo si sanifu katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu. Aidha, uchanganuzi wa matumizi ya kanuni ulibaini kwamba hata ingawa mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ulikuwa kikwazo kikuu katika usarufi wa Kiswahili sanifu, ulikuwa msingi na mkakati uliowaongoza wanafunzi katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Ukiukaji uliosababisha Kiswahili kisicho sanifu katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi.

Utafiti huu ulibaini kuwa mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu hutokana na ukuruba wa lugha baina ya Luganda na Kiswahili ambazo zote ni lugha za Kibantu. Uchanganuzi wa maandishi na mazungumzo

ya wanafunzi yalibaini kuwa baadhi ya kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda vilikuwa na mwingiliano ambao ulitumika na wanafunzi katika mazungumzo na maandishi. Mwingiliano huu ulijitokeza wanafunzi waliposhindwa kutambua kanuni ya matumizi sanifu ya kipashio kutokana na kanuni leksia ya kipashio cha kimofosintaksia cha Kiswahili sanifu katika tungo. Kwa sababu hiyo, wanafunzi waliamua kutumia kanuni leksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kwa ajili ya kupatanisha kipashio na maneno mengine katika tungo kutegemea neno kuu.

Tathimini ya kanuni za kimofosintaksia za Luganda zilibaini kwamba, tofauti za mifumo ya kimofolojia na Kisintaksia za Luganda na Kiswahili sanifu ndio iliyokuwa asili kuu ya mwingiliano ulioathiri matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu. Hali hii ilitokana na kuwa usarufi wowote ule katika lugha hizi hutegemea kanuni leksia, sintaksia na muungano wa vipashio vya kimofolojia na kisintaksia kama vile muundo na uambishaji viambishi kimofolojia, muunganiko wa vipashio kama viambajengo vya tungo za kimofosintaksia unaojenga uhusiano wa neno kuu na maneno mengine katika tungo. Ithibati ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia ilibaini kwamba, wanafunzi walitumia sifa za kisarufi za vipashio vya Luganda, kulinganisha na sifa za Kiswahili sanifu pamoja na kanuni leksia za Luganda katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu bila kutambua kuwa kila lugha ina upekee wa mifumo ya matumizi ya kipashio kutegemea kanuni leksia na kanuni unganifu ya kipsahio na viambajengo vingine katika tungo.

Tathimini ya kanuni katika matumizi yalidhihirisha kuwa, japo Luganda ilidhihirisha uwiano wa kanuni katika matumizi ya kipashio baina ya Luganda na Kiswahili sanifu, vipimo vya sifa za kimofosintaksia za matumizi ya vipashio ulitofautiana na kusababisha tofauti za kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Tofauti hizi ndizo zilizoathiri matumizi ya kanuni za Luganda katika vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu ambapo athari za kimofolojia na kisintaksia zilidhihirika katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi. Kwa mfano, wanafunzi walitumia kanuni ya uundaji nomino katika kipashio cha ngeli kwa kuzingatia kipimo cha uambishaji wa viambishi awali na vipatanishi vya msingi na kusahau mfumo wa mpangilo wa viambishi kisemantiki, kisintaksia, kijozi na kitakwimu. Kwa hiyo, wanafunzi walitumia nomino kwa kuzingatia maumbo na kusahau kanuni ya ujozi, semantiki, sintaksia na mofolojia ambayo kwayo kiuambishaji, Luganda huwakiliswa na maumbo ya nomino ambayo hutofautiana au kufanana ila takwimu na ujozi wake nomino hujitokeza katika ngeli tofauti kama ilivyo katika nomino za viumbe hai ambazo huambikwa viambishi

vya ngeli ya [ki-vi] ya ngeli ya [7 na 8] lakini kisemantiki majina haya hupatikana katika ngeli ya [1 na 2].

7.5 Mchango wa utafiti

Utafiti huu ulitoa mchango kwa taaluma ya isimu tumikizi na linganishi ya Kibantu na Kiswahili kwa kutambua mwingiliano wa miundo na kanuni ya mofosintaksia ya Luganda kudhihirisha jinsi inavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Uliweka wazi uwiano na tofauti za vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili, kuchanganua kanuni za matumizi ya vipashio vya Luganda na Kiswahili na kuonyesha jinsi uwiano na tofauti za vipashio husika na kanuni za matumizi ya vipashio vya Luganda huingiliana na kusababisha athari katika matumizi mwafaka ya lugha ya Kiswahili sanifu kimofosintaksia. Vilevile, utafiti huu uliendeleza na kuchangia mofosintaksia ya lugha za Kibantu kwa kubainisha miundo na kanuni za vipashio vya mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu, kuonyesha uhusiano na tofauti za lugha za nasaba moja na jinsi lugha hizo huingiliana na kusababisha athari katika matumizi ya vipashio na kanuni za kimofosintaksia. Halikadhalika, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kukuza na kuendeleza umilisi na matumizi ya Kiswahili sanifu nchini Uganda pamoja na lugha za Kibantu ambazo zina ukuruba na mtagusano pamoja na ukinzani wa muda mrefu baina yao (Luganda ikikinzana na Kiswahili). Aidha, utafiti huu utafahamisha jamii jinsi lugha za Kibantu huwiana na kutofautiana kimofolojia na kisintaksia (kimuundo) na kikanuni, kuingiliana na kusababisha athari katika matumizi kutokana na ukuruba, mtagusano na ukinzani baina yao kama lugha za nasaba moja.

Halikadhalika utafiti huu badala ya kuzungumzia juu ya ukiukaji wa matumizi ya kanuni na miundo ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi ambao wanajifunza L2, uliweka bayana hali na viwango vya mwingiliano wa vipashio na kanuni za kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kudhihirisha jinsi mofosintaksia ya Luganda inavyoingiliana na kuathiri mazungumzo na maandishi ya Kiswahili sanifu miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Kufanikiwa kwa utafiti huu kulitoa mchango wa maarifa ya Luganda na Kiswahili Sanifu katika ngazi za mofosintaksia kwa kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa vipashio vya mofolojia na jinsi vinavyopata uamilifu wake katika tungo kujenga uhusiano milikifu na unganifu ya vipashio vya kiisimu vya lugha mahususi.

Vile vile, utafiti huu uliweka misingi ya kuchunguza kuathiriana kwa lugha kunakopelekea kutokuwepo kwa matumizi sanifu ya lugha ya Kiswahili kutokana na mwingiliano wa

matumizi ya kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya (lugha za Kibantu) Luganda katika Kiswahili sanifu. Msingi ambao uliweka bayana athari za mwingiliano wa lugha za kienyeji katika matumizi ya Kiswahili sanifu nchini Uganda kutokana na kuwa athari za mwingiliano wa vipashio na kanuni za lugha za Kibantu kama vile Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu hakujafanyiwa utafiti wa kutosha kudhihirisha jinsi kufanana na kutofautiana kwa vipashio na kanuni za mifanyiko ya vipashio vya mofosintaksia vya Luganda huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu licha ya kuwa zote ni lugha za nasaba moja. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa licha ya Kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja ya Kibantu, ni lugha mbili tofauti kiisimu ambazo uchunguzi wake unaonyesha mchango wa lugha asili katika ujifunzaji na umilisi wa lugha ya pili.

7.6 Mapendekezo ya utafiti wa baadaye

Utafiti huu ulishughulikia swala la mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulieleza uwiano na tofauti ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu, kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kwa ajili ya kutathimini jinsi kanuni za mifanyiko za Luganda zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Data za utafiti huu zilitambua kuwa uwiano na tofauti za vipashio na kanuni za vipashio vya mofosintaksia huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu na kusababisha matumizi ya Kiswahili kisicho sanifu. Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa kufanana na kutofautiana kwa vipashio vya kimofosintaksia baina ya lugha ni muhimu sana katika kutambua umilisi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili sanifu. kwa hiyo, unapendekeza kuwa;

Kwanza, utafiti mwingine unaweza kufanywa kufananisha na kutofautish vipashio vya kimofosintaksia vinginevyo vya kiisimu kama vile vihusishi, viwakilishi, vielezi na vipashio vinginevyo, kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipashio baina ya lugha za asili na Kiswahili sanifu. Utafiti huu unaamini kuwa aina ya utafiti huu ukifanywa, utaweza kuweka misingi imara ya ukuzaji wa umilisi katika matumizi ya Kiswahili sanifu unaotokana na mchango wa lugha asili katika matumizi na ujifunzaji wa Kiswahili sanifu katika mazingira maalumu.

Pili, utafiti huu ulichunganganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi. Ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za Kibantu ambazo hudhihirisha mwingiliano wa matumizi ya kanuni za vipashio

vya kimofosintaksia. Utafiti huu unapendekeza tafiti zinginezo kufanywa kudhihirisha uchanganuzi wa vipashio vinginevyo ama kanuni zinginezo za kiisimu ambazo zinaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha zilizo na unasaba mmoja au kutofautiana kinasaba. Utafiti huu unaamini kuwa uchanganuzi kama huo ni muhimu katika kujenga umilisi katika matumizi ya lugha za mnasaba mmoja na zinazotofautiana.

Tatu, utafiti huu unapendekeza tafiti za baadaye kufanywa kuhusiana na tathimini ya kanuni za kiisimu za lugha asili au za Kigeni na jinsi zinavyoathiri ama kukuza matumizi ya Kiswahili sanifu ama kinyume. Tafiti za baadaye zinaweza kufanywa kuegemea mihimili na nadharia tofauti baina ya lugha tofauti na utafiti huu, kuchanganua mchango wa lugha asili katika ukuzaji wa umilisi wa Kiswahili sanifu. Tafiti hizi zitaweka misingi ya kuwaongoza watafiti kuelewa nadharia mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa katika mchakato wa ujifunzaji na ujenzi wa umilisi wa matumizi ya lugha.

7.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa mujibu wa madhumuni matatu. Muhutisari wa matokeo unadhihirisha kuwa licha ya Luganda na Kiswahili sanifu kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti zenye vipashio na kanuni za mifanyiko ya vipashio vya kimofosintaksia vinavyofanana na kutofautiana. Kufanana na kutofautiana huku kunasababaisha athari za mwingiliano wa vipashio na kanuni za kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Matumizi haya yanakifanya Kiswahili kinachozungumzwa na mwanafunzi ambaye L1 ni Luganda kukosa usahihi katika matumizi kwa sababu ya kuhamisha sifa za maumbo na kanuni za vipashio vya kimofosintaksia vya Ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanusho vya Kiswahili sanifu vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Sura hii imeangazia pia mchango wa utafiti huu katika taaluma ya isimu tumikizi na linganishi ya lugha za Kibantu zenye nasaba moja na kutoa mapendekezo ya tafiti zaidi za baadaye wa kuweka misingi imara ya ukuzaji wa umilisi katika matumizi ya Kiswahili sanifu unaotokana na mchango wa lugha asili katika matumizi na ujifunzaji wa Kiswahili sanifu katika mazingira maalumu.

MAREJELEO

- Adam, J., & Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies. Mzumbe Book Project*, 138.
- Abdallah, S. S. (2018). *Uwiano na Utofauti wa Kiisimu Kati ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Adewole, S.M. 1986. "A syntactic basis for noun classification in Kiswahili". *Kiswahili* 53, 37-49.
- Abudonia, R. A. (2014). The Syntax of Luganda Adjectives: Katika *Egyptian Journal of Linguistics and Translation*, 1(1), 35–44.
- Aikhenvald, A. Y. (2017). ‘A typology of noun categorization devices’, in Alexandra Y. Aikhenvald (ed.), *The Cambridge Handbook of Linguistic Typology*, (361- 404) Cambridge University Press.
- Aikhenvald, A. Y. (2006). *Classifiers and Noun Classes: semantics*. Elsevier.
- Aikhenvald, A.,Y. (2000). *Classifiers: A typology of noun categorization devices*. Oxford University Press.
- Allen, A. (2014). *Definiteness and specificity in Runyankore-Rukiga*. Unpublished PhD Thesis, Stellenbosch University.
- Amberber, M., & Collins, P. (2002). *Language universals and variation*. Greenwood Publishing Group.
- Ambuyo, B. A. (2011). *Uamilishi Dhima katika Sentensi za Luloogoli: Mtazamo wa sintaksia Finyizi*.
- Amidu, A., A. (2006). *Pronouns and Pronominalizations in Kiswahili grammar*. Rudiger Koppe.
- Anderson, S. R. (1992). *A-morphous morphology* (Vol. 62). Cambridge University Press.
- Asiimwe, A. (2019). The syntax of relative clause constructions in Runyankore-Rukiga: A typological perspective. *Stellenbosch Papers in Linguistics Plus*, 2019(58), 131-154.
- Asiimwe, C. (2016). Ulinganishi wa Ngeli za Nomino za Lugha za “Runyačitara” 1. *Kiswahili*, 81(1).
- Asiimwe, A. (2016). Investigating the connection between the demonstrative and the definite morpheme-a in Runyankore-Rukiga. *South African Journal of African Languages*, 36(1), 65-73.
- Ashton, E. O. (1947). *Swahili grammar*. London: Longman Group Ltd.
- Ashton, E.O., E.M.K. Mulira, E.G.M. Ndawula, & A.N. Tucker. 1954. *A Luganda*

- grammar*. Longmans Green & Co.
- Ashton, E.O. (1982). *Swahili Grammar (Including Intonation)*. London: Longman Green and Co. Ltd.
- Athumani, M. R. (2015). Athari za Kiisimu za Lugha ya Kiswahilikatika Lugha ya Kiyao. (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Baertlein, E & Ssekitto, M. (2014) "Luganda Nouns: Inflectional Morphology and Tests," *Linguistic Portfolios*: Vol. 3, Article 3.
- Baker, G. P., & Hacker, P. M. S. (2009). *Rules and Grammar*.
- Balagadde, R. S. (2016). The Structured Compact Tag-Set for Luganda. *International Journal on Natural Language Computing (IJNLC) Vol, 5*.
- Barney Glaser & Anselm Strauss (1967). *The discovery of grounded theory: strategies for qualitative research*. New York: Aldine de Gruyter,
- Barno, C . (2013). Muundo wa Kimofu-sintaksia wa Kitenzi cha Kinandi kwa Mtazamo wa Kiunzi cha Kanuni Finyu. *Nordic Journal of African Studies 22(4): 213-235.*, 4(22), 213-235.
- Basweti, O., N., (2005). A Morphosyntactic Analysis of Agreement In Ekegusii In The Minimalist Program. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Bavuai, A. I. (2017). *Muundo wa Kirai Nomino katika lahaja ya Kimakunduchi* (Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Bearth, T. (2003). Syntax. In Derek Nurse, Gérard Philippson (eds.) *The Bantu languages*, Routledge.,121-139.
- Beaudoin-Lietz, C. (1999). Formatives of Tense , Aspect, Mood and Negation in the Verbal Constuction of Standard Swahili. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Memorial Newfoundland.(Haijachapishwa).
- Behera, A. K. (2013). Etymological Analysis of English Words. *Journal AJHSS, 1(1)*.
- Bernander, R., Devos, M., & Gibson, H. (2018). The negative existential cycle in Bantu. *Unpublished manuscript. University of Helsinki, Royal Museum of Central Africa, University of Essex*.
- Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Macmillan Aidan Ltd.
- Besha, R., M. (1996). Misingi ya uainishaji ngeli - Besha.pdf. Kioo cha Lugha.
- Bochnak, M. R. (2013). *Cross-linguistic variation in the semantics of comparatives*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Chicago, Division of the Humanities, Department of Linguistics.

- Bochnak, M. R. (2013). The non-universal status of degrees: Evidence from Washo. *Katika Proceedings of NELS* (Vol. 42, pp. 79-92).
- Bhela, B. (1999). Native language interference in learning a second language : Exploratory case studies of native language interference with target language usage, *1*(1), 22–31.
- Black, C. A. (1999). A step-by-step introduction to the Government and Binding theory of syntax. *SIL-Mexico Branch and University of North Dakota*.
- Britain, G., Press, P., Keller, L., Cnrs, D. C., & Applique, R. (1992). Analytical Estimator of Measurement Variances in Data Error, *16*(3), 185–188.
- Brown, D. J.(2005). *Testing in Language Program*. New York: McGraw-Hill.
- Businge, J. (2014). *Uchanganuzi wa Kimofosintaksia wa Sentensi za Kitooro kwa Mkabala wa Nadharia ya Umilikifu na Unganifu*. Chuo Kikuu cha Uisilamu, Uganda.
- Bussmann, H. (2006). *Routledge dictionary of language and linguistics*. Routledge.
- Byamugisha, J., Town, C., Keet, C. M., Town, C., Derenzi, B., & Town, C. (2018). Pluralizing Nouns across Agglutinating Bantu Languages, 2633–2643.
- Carolyne, O., Simala, I. K., & John, K. M. (2017). Athari za Uhamishaji wa Sarufi ya Kiluo kwenye Upatanisho wa Sarufi ya Kiswahili. *Kiswahili*, 76(1).
- Chama cha Kiswahili Nchini Uganda. (2019).
- Chebet, C. S. (2016). *Morphosyntactic Analysis of Kinandi L1 Speaking Pupils' Kiswahili Essays as an Insight into Psycholinguistic Challenges of Second Language Acquisition* (Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Moi).
- Chege, N.J (2020) Pragmatiki ya kirai nomino katika sintaksia ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta – Haichajapishwa.
- Chapetón, C. M. (2008). Cross-linguistic influence in the writing of an Italian learner of English as a foreign language: An exploratory study. *Colombian Applied Linguistics Journal*, (10).
- Chepkwony, L. C. (2012). *Matatizo ya Kisarufi Miongoni mwa Wanafunzi wa Kipsigisi wanaojifunza Kiswahili sanifu: Mtazamo wa Lugha Kadirifu*. Chuo Kikuu Ca Kenyatta.
- Chepyegon, D. K., Khaemba, J., & Bartoo, P. (2021). The Morphosyntactic Features and Tense Aspect Marking in Samor of Baringo Kounty, kenya. A morpho-phonosyntactic Study. *International Journal of Linguistics*, 2(1), 11-35.
- Chesswas, J., D (1967). *The Essentials of Luganda*. Oxford University Press, UK.
- Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. E. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.
- Chisia, M. (2012). *Uchanganuzi Wa Kauli Katika Sentensi Elekezi Ya Kiswahili Sanifu-*

- Mtazamo Wa Nadharia Ya Ubanifu* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).
- Choge, S (2016). *Morphosyntactic Analysis of Kinandi L1 Speaking Pupils' Kiswahili Essays as an Insight into Psycholinguistic Challenges of Second Language Acquisition*. Tansifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Moi.
- Chomi, E. W. (2016). *Let Us Speak Kiswahili: A Manual for Teaching Kiswahili Conversation*, 3).
- Chomi (2003). *Kozi Tangulizi Katika Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Sebha, Libya... Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.
- Chomi, E. (2013) *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam; Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge, Mass.: M.I.T. Press, Pp. x + 251.
- Chomsky, Naom. (1982). *Some Concepts and Consequences of the Theory of Government and Binding*. *Book*.
- Chomsky, N. (1981). *Lectures on government and binding*. Dordrecht: Foris.-. 1986. Knowledge of language: Its nature, origin, and use. *New York: Praeger..(1993)" A Minimalist Program for Linguistic Theory"*. *Kenneth Hale and Samuel J. Keyser, Eds. The View from Building, 20*, 1–52.
- Chomsky, N., Lasnik, H., Jacobs, J., von Stechow, A., Sternefeld, W., & Vennemann, T. (1993). *Syntax: An international handbook of contemporary research*. Berlin: de Gruyter, 506-569.
- Chomsky, N. (1995). *Bare phrase structure. Government and Binding theory and the Minimalist Program*, edited by Gert Webelhuth, 71-132. Oxford: Blackwell.
- Chomsky, N. (1995), *The Minimalist Program*. 'A Minimalist Program for linguistic theory'. Cambridge MA MIT Press. 28: 167–2170.
- Cohen, N., & Arieli, T. (2011). *Field research in conflict environments: Methodological challenges and snowball sampling*. *Journal of Peace Research*, 48(4), 423–435.
- Collins, L., & White, J. (2015). *The quantity and quality of language practice in typical interactive pair/group tasks*. *TESL Canada Journal*, 31, 47.
- Comrie (1976); *Aspect 3–25* Cambridge: Cambridge University Press.
- Contini-Morava, E. (2000). *Noun class as Number in Swahili*. *Amsterdam studies in the Theory and History of Linguistic Science Series 4*, 3-30.
- Cook, V. J. & Newson, M. (1996). *Chomsky's Universal Grammar: An Introduction*, 2nd

edn. Blackwell.

- Corder, S. P. (1981). *Interlanguage and error analysis*. Oxford University Press.
- Corder, S. P. (1967). The significance of learner's errors.
- Corbett, Greville G. (2007). Gender and noun classes. Katika Timothy Shopen (ed.), *Language typology and syntactic description III: Grammatical categories and the lexicon.*, 241–279. Cambridge University Press.
- Crisma. P., Martem, L., & Sybesma, R. (2011). The Point of Bantu, Chinese and Romance nomina classification. *Revista di Linguistica*, 23(2) 251-299.
- Crystal, D. (2004). *The Cambridge encyclopedia of the English language*. Ernst Klett Sprachen.
- Crystal, D. (2011). *A dictionary of linguistics and phonetics* (Vol. 30). John Wiley & Sons.
- Crystal, D. (1980). *A first dictionary of linguistics and phonetics*. Westview Press.
- Cummins, J. (2000). *Language, power, and pedagogy: Bilingual children in the crossfire* (Vol. 23). Multilingual Matters.
- Demuth, K. 2000. Bantu noun class systems: Loan word and acquisition evidence of semantic productivity. Katika G. Senft (ed.), *Classification Systems*. Cambridge University Press. pp. 270-292.
- Diercks, M. J. K. (2010). *Agreement with subjects in Lubukusu* (Doctoral dissertation, Georgetown University).
- Dixon, R. M. W. (2010). *Where have all the adjectives gone?: and other essays in semantics and syntax* (Vol. 107). Walter de Gruyter.
- Dixon, Robert. (1982). *Where have all the adjectives gone?: and other essays in semantics and syntax*. Mouton Publishers.
- Downing, L. J. (2011). The prosody of ‘dislocation’ in selected Bantu languages. *Lingua*, 121(5), 772-786.
- Downing, S. Zerbian & L. Marten (eds.), *Papers in Bantu grammar and description*. ZASPiL 43. Berlin: ZAS.
- Droste, M. (1989). Event structures and domains. *Theoretical Computer Science*, 68(1), 37-47.
- Egara, M.B (2016) Mofosintaksia ya Yambwa katika Kishazi cha Kiswahili. [Tasnifu ya uzamili], Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Ellis, R. (1994) *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford: OUP.
- Ellis, R., & Shintani, N. (2013). *Exploring language pedagogy through second language acquisition research*. Routledge.

- Faki J., B. (2019). *Kirai nomino katika kipemba: uchanganuzi wa kimuundo* (doctoral dissertation, suza).
- Ferrari-Bridgers, F. (2008). A unified syntactic analysis of Italian and Luganda nouns. *The Bantu-Romance Connection*, 239-258.
- Frawley, W. J. (2003). *International Encyclopaedia of Linguistics*, Oxford University.
- Gaiza A, M. (2011). Module -2 Second Language Acquisition. *Texas A and M University – Kingsville*.
- Grinevald, C. (2000). A morphosyntactic typology of classifiers. In: Senft, G. (ed.), *Systems of Nominal Classification*. Cambridge: Cambridge University Press, pp. 50–92.
- Gromova, N. V. (2008). Maswali Machache ya Usanifishaji wa Kiswahili (Jingine au Lingine?). In *Swahili Forum* (Vol. 15, pp. 115-120).
- Gass, S., & Selinker, L. (2008). The role of the native language: an historical overview. *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. Taylor & Francis, 89–120.
- Gérard, A. S. (1981). *African Language Literatures: An introduction to the literary history of sub-Saharan Africa*. Longman London.
- Gibson, H., Mapunda, G., Marten, L., Shah, S., & Taji, J. (2020, June). Variation in double object marking in Swahili. In *Swahili-Forum* (Vol. 26, pp. 142-165). Universität Leipzig.
- Gibson, H., & Guérois, R. (2019). Variation in Bantu copula. *The grammar of copulas across languages*, 73, 213.
- Guérois, R., Gibson, H, Everdium & Marten, L. (2017). Parameters for Bantu morphosyntactic variation. Leverhulme project ‘Morphosyntactic variation in Bantu typology, contact and change. SOAS, University of London.
- Gichuru, M.T. (2010) Uchanganuzi wa nomino ambatani za Kiswahili Mtazamo wamofolojialeksia. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Greenberg, J. H. (1963). Some Universals of Grammar with Particular Reference to the Order of Meaningful Elements. *Universals of Language*, 2, 73–113.
- Guthrie, M. (1948). „The Classification of Bantu Languages", published for the International African Institute by the Oxford University Press.
- Guthrie, M. (1967). 1971. Comparative Bantu. *Farnborough, England: Gregg International Publishers, Ltd.*
- Guthrie, M. (2017). *The Classification of the Bantu Languages bound with Bantu Word Division*. Routledge.
- Guthrie, M. (1971). The western Bantu languages. *Current Trends in Linguistics*, 7, 357–366.

- Habwe J. & Karanja P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers Ltd.
- Haegeman, L., & Atkinson, M. (1994). *Introduction to Government and Binding Theory 11* (second edi). Blackwel Publishers Ltd.
- Hafsa, S.H. (2016). Ujidhihirishaji wa mofu zinazowakilisha nafsi na njeo katika Kiswahili: Tafiti Linganishi wa lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. [Tasnifu ya uzamili] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Hallberg, L. R. (2006). The “core category” of grounded theory: Making constant comparisons. *International journal of qualitative studies on health and well-being*, 1(3), 141-148.
- Hamad Khamis, & Juma. (2015). NGELI ZA NOMINO ZA KI-MICHEWENI. *Jarida La MULIKA Journal ., Juzuu la 3*.
- Hannah, X. (1975). morphosyntax in swahili.
- Hassan, H. S. (2016). *Ujidhihirishaji wa Mofu Nafsi na Njeo Katika Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu* (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Haule, F. (2014). Muundo wa Njeo za Lugha ya Kingoni. Tasnifu za Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijchapishwa.
- Heine, B. (1976). *A Typology of African Languages: Based on the Order of Meaningful Elements*. Dietrich Reimer.
- Hendrikse, A.P. & Poulos, G (1990). A continuum interpretation of the Bantu noun class system. Edited by Gowlett, D.F. 1992. African Linguistic Contributions. Pretoria: Via Afrika Limited.
- Hepburn-Gray, R. (2016, September). A survey of Niger-Congo noun class agreement systems. In *2nd International Congress “Towards Proto-Niger-Congo: Comparison and reconstruction”*. LLACAN (Vol. 1, No. 3).
- Hooper, J. (1976). Introduction to Genitive Phonology. Oxford: Oxford University Press.
- Hyman, L. (2018). The First Person Singular Subject Negative Portmanteau in Luganda and Lusoga. *Berkeley Papers in Formal Linguistics*, 1(1).
- Hyman, L. M., & Katamba, F. X. (2001). November, 2001 The Word in Luganda Larry M. Hyman. *Word Journal Of The International Linguistic Association*, (L)
- Hyman, L. M., & Katamba, F. X. (2010). Tone, syntax, and prosodic domains in Luganda. *ZAS Papers in Linguistics*, 53, 69-98.
- Hyman, L (1975) *Phonology: Theory and A nalysis*. Holt Rinehart and Row.
- Hyman, Larry M. & Francis X. Katamba (2010). "Tone, syntax, and prosodic domains in

- Luganda". *ZAS Papers in Linguistics* 53, pp. 69–98.
- Hyman, L. M., & Katamba, F. X. (1999). 12 *The syllable in Luganda phonology and morphology* (Vol. 45, p. 349). Walter de Gruyter.
- Hyman, L. M., & Katamba, F. X. (2012). 12 The syllable in Luganda phonology and morphology. In *The Syllable* (pp. 349-416). De Gruyter Mouton.
- Immanuel, N. (2019). An analysis of semantic and syntactic negation in Oshiwambo and English. *JULACE: Journal of the University of Namibia Language Centre*, 4(2), 30-40
- Iori, I. (2015). *What can the Research on Japanese Anaphoric Demonstratives Contribute to General Linguistics?* Hitotsubashi University.
- Jerro, K. (2018). Linguistic complexity : A case study from Swahili. *African linguistics on the prairie*, 3(2018), 3–19. <https://doi.org/10.5281/zenodo.1251708>
- Jilala, H. (2014). *Athari za kiutamaduni katika tafsiri mifano kutoka matini za Kitalii katika makumbusho za Tanzania* (Doctoral dissertation, University of Dar es Salaam).
- Jjingo, C., & Visser, M. (2017). The Ssenteza Kajubi Legacy: The Promotion of Teaching Kiswahili in Uganda. *Journal of Pan African Studies*, 10(9).
- Joy, M. S. (2012). Causes of syntactical errors in Kiswahili second language learning among western Kenya's Kiidakho first language speakers. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies*, 3(6), 921.
- Juma, H. K. (2017). Ngeli za Nomino za Ki-Micheweni. *Mulika Journal*, 35(1).
- Kamoga, F. K., & Stevick, E. W. (1968). *Luganda: basic course*. Foreign Service Institute.
- Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A. (2019). *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja*. Longhorn Publishers.
- Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kariuki (2012). *Makosa ya Kisintaksia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili za Wanafunzi wa Shule za Upili*. (Tasnifu ya Uzamili), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Karuku, S., na Tennant, G. (2016). Towards a Harmonized Curriculum in East Africa: A Comparative Perspective of the Intended Secondary School Mathematics Curriculum in Kenya, Rwanda, Tanzania and Uganda. In *Mathematics Education in East Africa* (pp. 9–25). Springer.
- Katamba, F., & Stonham, J. (2006). *Morphology*. NY.
- Katamba, F. X. (2006). *Uganda: The language situation*.
- Katamba, F. (2003). Nominal Morphology. In Derek Nurse, Gérard Philippson (eds.) *The Bantu languages*, Routledge., 103–120.

- Katamba, F. X. (1993). *Modern Linguistics: Morphology*. Palgrave Publishers. *Palgrave Publishers*.
- Kawale, F. R. (2015). *Ukanushi wa vishazi katika kiswahili sanifu* (Doctoral dissertation, University of Dar es Salaam).
- Kießling, R. 2013. On the origin of Niger-Congo nominal classification. *Katika Historical Linguistics 2011: Selected papers from the 20th International Conference on Historical Linguistics, 25-30 July 2011* (Vol. 326, p. 43). John Benjamins Publishing.
- Kihore, Yared M, Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA)*. *Sekondari Na Vyuo. Tanzania*.
- Kihore, Yared Magori, Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kihm, A. (2005). Noun class, gender, and the lexicon-syntax-morphology interfaces. *The Oxford handbook of comparative syntax*, 40, 459-512.
- Kim, H. S. (1999). Universal phonological processes in eastern Bantu: a theoretical analysis. *Linguistics*, 7, 199-225.
- Kirabi, J. M. (2015). *Makosa ya Kimofosintaksia katika Lugha ya Kimaongezi Dhidi ya Kanuni za Lugha ya Kiswahili*. *Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.
- Kisakwah, B. A. (2014a). *Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili sanifu na za Kisuba*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kitsao, R (2015). *Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za Wanafunzi wa shule za msingi na yanavyochangia Matokeo mabaya ya mitihani, kata ya ganze, kaunti Ya kilifi, Kenya*. *Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Pwani*.
- Kithuku, M. (2012). *Mofosintaksia ya ngeli ya 9/10 (N/N)*. *Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*.
- Kiyinikibi, N. (2011). *Ensulo y'olulimi Oluganda*. Kamprint.
- Kiyinikibi, N. (2012). *Gulama w'olulimi Oluganda*. Kamprint.
- Kiyinikibi, N.D (2013), *Ensulo Y'olulimi Oluganda. Eddaala II: The Fountain of Luganda II*. Mugulansigo print book, Uganda,
- Kiyinikibi, N. D. (2021). *The locative in Luganda: a syntax-interfaces approach* (Doctoral dissertation, Stellenbosch: Stellenbosch University).
- Kombe, L. E. (2016). *Uambatishaji wa Vishazi katika Lugha ya Kiswahili : Uchunguzi wa Madai ya De Vos na Riedel (2017)*. *Kioo cha lugha 16(1)*

- Kombe, L. E. (2020). Ufasiri wa Mahusiano ya Uwakati Baina ya Vishazi Ambatani katika Lugha ya Kiswahili. *JULACE: Journal of the University of Namibia Language Centre*, 5(1), 37-47.
- Kombo, D. K., & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis writing: an introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Komunte, B. S. (2000). The Impact Of Bantu Languages In English Language Learning Processes In Tanzania Secondary Schools.
- Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques*. New Age International.
- Krifka, M., et al (1995). Genericity: An Introduction. In: Carlson, G.N., Pelletier, F.J. (eds.) *The Generic Book*, pp. 1–124. The University of Chicago Press.
- Kuhl, P. K. (2004). Early language acquisition: cracking the speech code. *Nature reviews neuroscience*, 5(11), 831-843.
- Kumaravadelu, B. (2006). *Understanding language teaching From method to postmethod*, (Mahwah, NJ Lawrence Erlbaum).
- Lado, R. (1957). *Linguistics across cultures*. University of Michigan Press
- Leah, S na Sseguya, F.N. (2015). A Luganda grammar. Yiga Olu-ganda. Accessed on 9 February 2016 from <http://learn-luganda.com>.
- Levers, M. D. (2013). Philosophical Paradigms, Grounded Theory and Perspectives on the Emergence. *SAGE open*, 1-6. <https://doi.org/10.1177/2158244013517243>
- Lewis, M. P. (2009). *Ethnologue: Languages of the world*. SIL international.
- Lieber, R. (1981). Morphological conversion within a restrictive theory of the lexicon. *The scope of lexical rules*, 161-200.
- Lonyangapuo. (2009). *Kiswahili Morphosyntax: A Generative Approach*. Chuo Kikuu cha Egerton.
- Lukamika, M. (2015). *Matumizi ya Ngeli Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, nchini Kenya* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno).
- Lupogo, I. (2021). Ulinganishaji wa Maumbo na Miundo ya Ukanushi katika Lugha ya Kiswahili na Kiingereza. *Journal of Linguistics and Language in Education*, 14(2).
- Lusekelo, A. (2017). The Swahili noun phrase in its Sentential: Katika *Mkwawa Journal of Education and Development*, Juzuu 1, Issue 1,
- Lusekelo, A. (2013). DP-internal and V-external Agreement Patterns in Bantu: Re-statement

- of the Facts on Eastern Bantu Languages. Katika: *Journal of Linguistics and Language in Education* 7(1). 19-47.
- Lusesa, J. (2013). Athari ya lugha mama (Kisukuma) katika kujifunza lugha ya Kiswahili. *Muymursinah, John Academia Edu* (2015).
- Lyons, J. 1995. *Language and Linguistic: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Magesa, J. P. N. (2017). *Ulinganishi Changanuzi wa Mofu Njeo za Kikara na Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamili) Chuo Kikuu Huria, Tanzania.
- Maho, Jouni. 1999. *A comparative study of Bantu noun classes*. Gothenburg: Acta Universitatis Gothoburgensis.
- Majaliwa (2021), Ukubalifu wa vitamkwa na ruwaza ghairi za vitamkwa kutoka kiingereza na Kiarabu katika fonolojia ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania
- Makini, G, N,. (2015) udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika Lugha ya Ekegusii, [Tasnifu ya Uzamili], Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya
- Mangi, J. E. (2019). *Athari za Lugha ya Kinyaturu katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Mangwa, D. . (2005). *Athari za Egakusii katika Kiswahilina vinavyochangia matokeo mabaya ya mitihani ya Kiswahiliwa kitaifa wa Kiswahilikwa wanafunzi wa Kisii wilayani Kisii kusini*. Chuo Kikuu cha Egerton.
- Margaret, K. M. (1981). uchanganuzi ngeli Ya 9/10 (N/N): Uainishaji wa Kimofolojia. *European Journal of Biochemistry*, 118(Mimi), 599.
- Marshad, H. A. (1993). *Kiswahiliau Kiingereza?(Nchini Kenya): Utepuzi wa maongozi ya lugha nchini Kenya*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Marten, L., Kula, N. & Thwala, N. (2007). Parameters of morphosyntactic variation in Bantu, *Transactions of the Philological Society* 105(3): 253-338.
- Masanja, P. (2014). *Mofosintaksia ya ruwaza ya ukanushi katika vitenzi vya lugha ya kisukuma: lahaja ya Kimunasukuma* (Doctoral dissertation, University of Dar es Salaam).
- Masasa, J. I. (2017). *Kuchunguza Athari ya Lugha ya Kijita katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Masebo, J. naNyangwine, N. (2008). *Kiswahili1 kidato cha 3 na 4*. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine publishers.
- Masinde, E (2016). *Morphosyntactic Structure of Lutachoni Verb Phrase Kenyatta*

- University. Tasnifu ya Uzamili-Haichachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Hokororo, J. I. (1999). Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA): sekondari na vyuo. (*No Title*).
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tanzania.
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Hokororo, J. I. (2012). Misingi ya Fonolojia. Dar es Salaam: TATAKI.
- Matasi, B., H., na Furaha, C., (2016) Ulinganishaji wa Kimofosintaksia Baina ya Kiswahili na Kiarabu katika Viwakilishi-nafsi: *RUWAZA AFRICA. Journal of Contemporary Research in Humanities and Social Sciences. Juzuu la 4 (144-151)*.
- Mathooko, P. M. (2002). Kutoka lugha kienzo hadi lugha ya isimu: matatizo yanayotinga Kiswahilikama lugha ya kufunzia isimu vyuoni vikuu nchini Kenya 2 p. Mbatha Mathooko, 72, 125–134.
- Mathooko P.M (2004) *Morphology and Syntax*, Nairobi: Institute of Open and Distance Learning, Kenyatta University.
- Mayaka, J. G. (2012). “Athari ya Mifanyiko ya Kimofonolojia kwa Upatanisho wa Kisarufi katika Kiswahili Sanifu.” Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Egerton (Haijachapishwa).
- Mazrui, A. A., & Mazrui, A. M. (1995). *Swahili state and society: The political economy of an African language*. East African Publishers.
- Mbaabu, I. (2007). *Historia ya usanifishaji wa Kiswahili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mbaabu, I. (1995) Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili. Nairobi: Longhorn Kenya Ltd.
- Mbaabu, I (1992): *Sarufi ya Kiswahili*: Longman Kenya
- Mbwillow, S. N. (2017). Muundo wa Vitenzi, Vivumishi, Vibainishi, Numerali/Namba na Vielezi katika Kiswahili, 1–26.
- Mdee, J. (1996) Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo: Dar es Salaam DUP.
- Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.
- Meeussen, A.E. (1967) —Bantu Grammatical Reconstructionl. *Africana Linguistica*, Juz. III: 79-121.
- Meredith, D. G. (2003). Joyce P. Gall, Walter R. Borg. Educational Research An Introduction. New York: Longman.
- Mgullu, R. (1999). *Mtala wa Isimu. Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Ltd, Kenya.

- Mlacha, S. A. K. (1995). *Kiswahili katika kanda ya Afrika mashariki:(historia,matumizi na sera)*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mogere, G. N., & Wasike, M. (2018). Athari za Mafunzo-Kazini: Mfano Halisi wa Walimu wa Kiswahili Katika Shule za Upili Garissa. *Mulika Journal*, 1(1).
- Moh'd, B. N. (2018). *Kuchunguza Viambishi Njeo na Hali katika Lahaja ya Kitumbatu* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Mohamed, M. A. (2001) *Modern Swahili Grammar*. East Africa Educational Publishers.
- Mohamed, A M. (1988). *Sarufi mpya na mazoezi ya ziada*. Foundation Books Limited.
- Momanyi, W. K., Ambuyo, B. A., & Chimerah, R. M. (2019). Uchanganuzi wa Athari ya Mageuzi ya Maneno kwenye Muundo wa Sentensi ya Ekegusii.
- Monchamps, G. M. (1904). L 'Oeuvre Linguistique des Pères Blancs d 'Afrique. Imprimeur de l Académie Royale de Belgique.
- Morimoto, Y. (2006). Agreement properties and word order in comparative Bantu.' In L. Mojapelo, M. L. (2007). *Definiteness in Northern Sotho*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Stellenbosch.
- Mpangala, G. (2018). *Athari za Lugha ya Kimakonde Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamili- Haijchapishwa, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).
- Mudhune, E.S. 1994. 'A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Learners'. M.A. Thesis, Kenyatta University (Unpublished).
- Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Acts Press.
- Mukama, R. (1995). Gender stereotyping in African languages. *Theoretical Approaches to African Linguistics*. Trenton, New Jersey, 375–392.
- Mukuria, D. M. (1987). *Mpangilio wa ngeli: ulinganishi wa ngeli za kiswahili sanifu na kikuyu cha kiambu* (Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Kikuu Cha Nairobi).
- Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahilina Kimeru: Mfano Kutokana na wanafunzi wa Tigania , Kenya*. Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and Its Expanding Roles of Development in East African Cooperation : A Case of Uganda, 15(2), 154–165.
- Mukuthuria, M. (2004). 'Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: mfano kutokana na wanafunzi wa Tigania, Kenya'. *Unpublished PhD Thesis: Egerton University*.
- Mukwana, S. M. O. & A. M. (2019). *Muundo wa Kiswahili*. The Jomo Kenyatta Foundation.
- Mulei, M. (2014). *Uchanganuzi wa Athari za Kigisu katika Lugha ya Mazungumzokwa Kiswahili, Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Mbale,*

- Nchini Uganda*. Chuo Kikuu cha Uislamu, Uganda.
- Mulei, M (2020) Athari ya Ukopaji wa Kanuni za Ukanushaji katika Mazungumzo ya Kiswahili. Book Article: In *Kiswahili na Maendeleo ya Afrika Mashariki, TATAKI, Tanzania*.
- Mulei, M., Amukowa, D., & Ambuyo, B. (2021). Athari za Kimofosintaksia za Ngeli za Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu Miongoni mwa Wanafunzi Shuleni, Uganda. *Jarida La Afrika Mashariki La Masomo Ya Kiswahili*, 3(1), 10-23. <https://doi.org/10.37284/jammk.3.1.331>.
- Mulei, M., Ambuyo, B., Amukowa, D (2021). Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda Katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu: *Jarida la idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*.
- Munyua, J. G. (2002). The Emerging Viswahili and Kiswahili Research. Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Moi University Press
- Muriungi, P. K., & Mbui, M. K. (2013). The influence of mother-tongue maintenance on acquisition of English language skills among day secondary school students in Imenti South District, Kenya. *International Journal of Linguistics*, 5(1), 296–305.
- Musa, Y. (2008). *Athari za lugha ya Kigweno katika Kiswahilina jinsi kinavyoathiri matokea mabaya ya mitihani ya kitaifa*. Chuo Kikuu cha Uislamu, Uganda.
- Mutale , T. na Muwanga, D. (2009) *Ettaalaya Ggulama*. TTESUPA Booklex; Kamoga,
- Mutugu, B. N. (2001). Makosa ya Kileksia katika Insha na Chanzo chake: Uchunguzi wa Shule Tano za Upili Wilayani Kiambu. *Tasnifu ya Uzamili* (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mutwiri, F. J. (2019). *Muundo wa Sentensi ya Kiigembe: Mtazamo wa Eksibaa* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Chuka).
- Mwamzandi, M. Y. (2014). Swahili word order choices: insights from information structure. Doctoral Dissertation. The University of Texas at Arlington.
- Namugala, S. (2014). *Diminutive and Augmentative Functions of some Luganda Noun Class Markers.[Tasnifu ya Uzamili]* ya, Norges teknisk-naturvitenskapelige universitet, Det humanistiske fakultet, Institutt for språk of litteratur).
- NCDC, (2019). National Curriculum Development Centre: The National Secondary School Curriculum; *Kiswahili*; Published by National curriculum Development Centre, Kyambogo, Uganda.
- Ndomba, R. (2006). *Samatengo noun phrase structure. Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

- Ngamau, W. N. (2004). *A morpho-syntactic analysis of agreement in Gikuyu in the minimalist program* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, CEES, Kenya).
- Ngonyani, D. (2001). The morphosyntax of negation in Kiswahili.
- Ngonyani, I. (2019). An analysis of semantic and syntactic negation in Oshiwambo and English. *JULACE: Journal of the University of Namibia Language Centre*, 4(2), 30-40
- Nicola, G., & Montermini, F. (2005). Prefix-suffix neutrality in evaluative morphology. In *Proceedings of the 4th Mediterranean Meeting of Morphology*. Available at: <http://mmm.lingue.unibo.it/mmm-proc/MMM4/143-156-Grandi-Montermini-MMM4.pdf>.
- Nicuolo, G. (1991) *Problems of Testing Communicative Performance*. Baltimore: University Park Press.
- Njogu, K. (2007). *Kiswahilina elimu nchini Kenya*. Twaweza Communications.
- Nordquist, Richard. (2020, August 27). Proximity Agreement in Grammar. Retrieved from <https://www.thoughtco.com/proximity-agreement-grammar-1691697>.
- Nsimbi, Walusimbi, Mpalanyi na Mukasa (2015). *Tuyige Oulganda: Luganda Series*. Oxford: Oxford University Press
- Nurse, D., Hinnebusch, T. J., & Philipson, G. (1993). *Swahili and Sabaki: A linguistic history* (Vol. 121). Univ of California Press.
- Nurse, D., na Philippon, G. (2003). Towards a historical classification of the Bantu languages. *The Bantu Languages*, 164–181.
- Nurse, D., na Philippon, G. (2006). *The Bantu Languages*. Routledge.
- Nurse, D., Spear, T., & Spear, T. T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the history and language of an African society, 800-1500*. University of Pennsylvania Press.
- Ntawiyanga, S (2020). Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi katika Ujifunzaji Lugha ya Pili: Mfano wa Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda. *Kioo cha Lugha* 17, no. 1 (2020).
- Ntawiyanga, S. (2015). Changamoto za Kimofosintaksia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda. *Tasnifu ya Uzamili* (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Nyanda, J. (2015). Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. The Open University Of Tanzania.
- Nyandago, F. O. (2013). Uchanganuzi linganishi wa sintaksia ya Sentensi Sharti Ya Kiswahili sanifu Na Ekegusii.
- Obara, J. M. (2014). *Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Oberhauser M., Dreyer D., Mamessier S., Convard T., Bandow D., Hillenbrand A. (2015) Bridging the Gap Between Desktop Research and Full Flight Simulators for Human Factors Research. In: Harris D. (eds) Engineering Psychology and Cognitive Ergonomics. EPCE 2015. Lecture Notes in Computer Science, vol 9174. Springer, Cham. https://doi.org/10.1007/978-3-319-20373-7_44.
- Obondo, M. A. (2007). Tensions between English and mother tongue teaching in post-colonial Africa. In *International handbook of English language teaching* (pp. 37–50). Springer.
- Obuchi, S. & A. M. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Frame Publishers.
- Odeo, I. & Maina, G. 2008. *Fani ya Isimu Jamii kwa shule za Sekondari*. Oxford University press.
- Oduor, C., Inyani, K. S., & Kobia, M. J. (2017). Athari za uhamishaji wa sarufi ya Kiluo kwenye upatanisho wa sarufi ya Kiswahili. *Kiswahili*, 76(1).
- Oichoe, M. P. (2005). *Ulinganishi wa kirai tenzi cha Kiswahili na Ekegusii kimofo sintaksia: mtazamo wa uminimalisti*. Tasnifu ya Uzamili-Haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Okumu, N. B (2006). Tathimini ya Mpangilio wa Kisintaksia wa Ngeli za Nomina za Kiswahili: Ufunzafl katika Shule za Nairobi. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Ontieri, J. O. (2016). Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya.

- Onyango, V. O. (2018). *Daftari la Isimujamii Kwa Shule za Upili na Vyuho*. (A. B. P. Limited, Ed.) (Tolea la k). Kenya: Susmo Enterprises.
- Orodho, J. A. (2009). *Elements of Education and Science Research Methods*. (second). Maseno: Kanezja Publisher. Ouhalla,.
- Otiende, M. A. (2013). *Athari za Kimofonolojia za Kiolusuba katika Matumizi ya Kiswahili sanifu kama Lugha ya Pili*. Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Owino, N. A. (2016), Mifanyiko ya kimofonolojia ya ukuzaji na udunishaji nomino za kiwanga, kakamega, Kenya. [Tasnifu ya uzamili] Chuo Kikuu cha EgertonM, Kenya.
- Pak, M. (2007). Relative clauses without CPs in Luganda. *WECOL 2007*, 189.
- Palmer, F. 1986. *Mood and Modality*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Patrick, P. L. (2005) *Sociolinguistic Methods*. England: University of Essex
- Pawlikov, V. (2004). White Fathers, Islam and Kiswahili in Nineteenth-Century Uganda. *Asian and African Studies*, 73(2), 198–213.
- Peterson, R. (2017). Mwingiliano wa Lugha ya Mazungumzo na Maandishi katikauandishi wa Kitaaluma wa Insha za Wanafunzi. *Kiswahili*, 75(1).
- Philipo, Z. T. (2012). 125 Tofauti baina ya Vivumishi na Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili. *Kioo Cha Lugha University of Dar Elsalaam Journal (UDSM)*, (1874), 125–143.
- Philipo, Z.T & Kuyenga, F E (2017) *Sintaksia ya Kiswahili: Nadharia za Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili*. Karljamerpublishers Limited, Tanzania.
- Philipo, Z. T. (2017). Tofauti Baina ya Vivumishi na Viambishi katika Lugha ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 13(1).
- Pilkington, G. L. (1892). *A hand-book of Luganda/by GL Pilkington*.
- Pokorn, N. (2005) *Challenging the Traditional Axioms: Translation into Mother Tongue*. New York : John Bejamins.
- Polomé, E. (1967) *Swahili Language Handbook*. Center for Applied Linguistics.
- Polomé, E. C. (1967). *Swahili language handbook*.

- Radford, A. (1981). *Transformational syntax: A student's guide to Chomsky's extended standard theory*. Cambridge University Press.
- Radford, A. (1997). *Syntactic theory and the structure of English: A minimalist approach*. Cambridge University Press.
- Radford, A. (2004). *Minimalist syntax: Exploring the structure of English*. Cambridge University Press.
- Rapando, M. M. (2005). Makosa ya kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa na wanafunzi wa shule za upili jijini. Tasnifu ya Uzamili-Haichachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Reichenbach, H. (1947). *Elements of Symbolic Logic*. New York: Macmillan.
- Richard Norquist. (2020). Types of word formation in English.
- Richards, J. C. (1974). A non-contrastive approach to error analysis. *Error analysis: Perspectives on second language acquisition*, 172-188.
- Riedel, K. (2009). *The syntax of object marking in Sambia: A comparative Bantu perspective*. Netherlands Graduate School of Linguistics.
- Rijkhoff, J. (2002). *The noun phrase*. Oxford University Press.
- Rijkhoff, J. N. M. (1986). Word order universals revisited: The principle of head proximity. *Belgian Journal of Linguistics* 1. 95-125.
- Rose, S. (2009). Luganda Structure, 1–14.
- Rubanza, Y.I (1996). *Mofolojia ya Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. TUKI*.
- Rugemalira, J. M. (2007). The structure of the Bantu noun phrase.
- Ryanga, C. W. A. (2007). *Dhana, Mbinu za Utafiti na Utendakazi Wake*. Kenyatta University.
- Schadeberg, Thilo C., (1992). *A Sketch of Swahili Morphology*, 3rd ed., Köln: Köppe.

- Scottman, C. (1970), A look at Swahili of two groups of reproductory speakers. TUKI, Dar-es-salaam.
- Selinker, L. (1969). Language transfer. *General linguistics*, 9(2), 67.
- Selinker, L. (1972). *Interlanguage*.
- Shabani, A. N. & R. (2015). Nadharia ya Utawala na Ufunjanisho Inavyojihusisha na Aina za Vikundi Nomino katika Kiswahili, (2004), 1–8.
- Siemund, P. (2008). Language contact. *Language contact and contact languages*, 7, 3.
- Skutnabb-Kangas, T. (1981) *Linguistic Genocide*. UK: Lawrence Erlbaum Associates.
- Snoxall, R. A. (1955). A Luganda Grammar. By EO Ashton, EMK Mulira, EGM Ndawula, AN Tucker. London: Longmans, Green & Co., 1954. Pp. 516. 25s. *Africa*, 25(1), 106-108.
- Spencer, A. (2003). Sentence negation and realization-based morphosyntax.
- Ssekiryango, J. (2006). Observations on double object construction in Luganda. In *Selected proceedings of the 36th annual conference on African linguistics* (pp. 66–74).
- Ssempuuma, J. (2019). *Morphological and Syntactic Feature Analysis of Ugandan English: Influence from Luganda, Runyankole-Rukiga, and Acholi-Lango* (Vol. 58).
- Ssendanda Ersisa & Asimwe Allen (2016). A Comparative study of Runyankore-Rukiga and Luganda noun class system. [https://typecraft.org/tc2wiki/A comparative analysis of Runyankore-Rukiga and Luganda pronominal agreement](https://typecraft.org/tc2wiki/A%20comparative%20analysis%20of%20Runyankore-Rukiga%20and%20Luganda%20pronominal%20agreement).
- Ssentumbwe, A. M., Kim, B., & Lee, H. (2019). English to Luganda SMT : Ganda Noun Class Prefix Segmentation for Enriched Machine Translation International Journal of Advanced Trends in Computer Science and Engineering.
- Steinberg, D. D., Nagata H. & Aline D.P. (1982). *Psycholinguistics, Language, Mind and World*. (Second Edition). Pearson Education Limited.
- Sternefeld, L., Nickshere, & S. F. (2015). A Luganda grammar. Yiga Olu-ganda.
- Stump, G. T. (2001). *Inflectional morphology: A theory of paradigm structure*. Cambridge studies in linguistics. Cambridge University Press.
- Suleiman A. Mirikau. (2008). *Msururu wa PTE Kiswahili* (Toleo la kwanza). East African

Educational Publishers Ltd. Kenya.

Swaleh, R. H. (2005). *Mofosintaksia ya kishazi cha kitikuu: mtazamo wa uminimalisti* (Shahada ya Uzamili), Chuo Kikuu Cha Nairobi. Kenya.

Swaleh, R. H. (2017). *Njeo, Hali na Dhamira katika Kitenzi cha Kitikuu: Mtazamo wa Uminimalisti* (Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Pwani. Kenya.

Sylvain, N. (2020). Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi katika Ujifunzaji Lugha ya Pili: Mfano wa Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda. *Kioo cha Lugha*, 17(1).

TaaitaToweet (1979). A study of Kallenjin Linguistics. Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Taher, M. A. (2013). *Tofauti ya Viambishi Kanushi Kati ya Kiswahili na Kiarabu*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania).

Taher, M. E. (2021). Uyakinishi Na Ukanushi Katika Kiswahili. *Journal of Human Sciences*, 20(1), 141-148.

Taljard, E., & Bosch, S. E. (2006). A comparison of approaches to word class tagging: Disjunctively vs. conjunctively written Bantu languages. *Nordic journal of African studies*, 15(4).

Tembe, J., & Norton, B. (2008). Promoting local languages in Ugandan primary schools: The community as stakeholder. *Canadian Modern Language Review*, 65(1), 33–60.

The Republic of Uganda. (1992). Government white paper on the educational policy review commission report. Kampala: UPPC.

Thompson, S. G., & Kaufman, T. (2001). *Language contact*. Citeseer.

Thompson, K. D., & Schleicher, A. F. (2001). *Swahili Learners' Reference Grammar*. *African Language Learners' Reference Grammar Series*. National African Language Resource Center (NALRC), University of Wisconsin-Madison, 4231 Humanities Building, 455 North Park Street, Madison, WI 53706.

- Trommer, J. (2003). The interaction of morphology and syntax in affix order. In *Yearbook of morphology 2002* (pp. 283-324). Springer, Dordrecht.
- TUKI. (1990). Kamusi ya Isimu na Lugha. 1990 .. Dar es Salaam: TUKI. *Dar Es Salaam: TUKI*.
- Uchanganuzi wa Ngeli ya 9/10kutumia kigezo cha uainishaji wa ngeli kimofolojia. (1981), *10(Mimi)*, 10.
- Uganda, G. of. (1992). Government White Paper on the Education Policy Review Commission Report. UPPC Kampala.
- Van der Wal, J., na Namyalo, S. (2016). The interaction of two focus marking strategies in Luganda. *Diversity in African Languages*, 355.
- VanPatten, B., & Williams, J. (2015). Early theories in SLA. *Theories in second language acquisition: An introduction*, 2, 17-33.
- Van de Velde, M. (2019). Nominal morphology and syntax. *The Bantu Languages*, 237-269.
- Van de Velde, M. (2005). The order of noun and demonstrative in Bantu. *Studies in African Comparative Linguistics with special focus on Bantu and Mande*, 425-441.
- Vitale, Anthony. 1981. *Swahili syntax*. Cinnaminson N.J: Foris Publications.
- Vittrant, A. (2005). Burmese as a modality-prominent language Discourse and stylistic register. In *Studies in Burmese linguistics*. Pacific Linguistics.
- Waihiga, G. (1999). *Sarufi fafanuzi ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.
- Wani, S. H. 2010. *Language Interaction Continuum*. University of Kashmir. Retrieved June 8, 2011 from wikipedia, en.wikipedia.org/wiki/wikipedia.com.
- Ward, M., Penny, A., & Read, T. (2006). *Education reform in Uganda-1997 to 2004*:

reflections on policy, partnership, strategy and implementation. Department for International Development London.

Were, E. A. (1996). *First Language Influence on Kiswahili Composition Writing: The case of*

Bukusu students of Kanduyi, Bungoma. Kenyatta University.

Wilkins, D. A. (1972). *Linguistics in language teaching* (Vol. 111). London: Edward Arnold.

Woodrum, E. (1984). Mainstreaming content analysis in social science: Methodological

advantages, obstacles, and solutions. *Social Science Research*, 13, 1-19.

Yule, G., & Widdowson, H. G. (1996). *Pragmatics.* Oxford university press.

Zerbian, S., & Krifka, M. (2008). Quantification across Bantu languages. *Quantification: A*

cross-linguistic perspective, 64, 383-414.

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Kiongozi cha Maswali ya Mjarabu kwa Wanafunzi

CHUO KIKUU CHA MASENO, KENYA

MASWALI YA KUCHUNGUZA MATUMIZI YA VIPASHIO VYA KISARUFI VYA

LUGANDA NA KISWAHILI

Mjarabu huu na Mjadala umeandaliwa kwa ajili ya utafiti unaohusu “**Uchanganuzi wa Mofosintaksia ya Luganda katika Matumizi ya Kiswahili sanifu Wilayani Kampala, Uganda.** Tafadhali unaombwa kujibu maswali haya kwa mujibu wa uwezo wako. Majibu yako yatumika kwa ajili ya utafiti huu wala sio kwa shughuli nyinginezo.

Kiambatisho 1A: Mjarabu wa Kisarufi kwa Wanafunzi Darasani

1. Orodhesha ngeli za Luganda na Kiswahili kwa kutumia vitabu teule vya Luganda na Kiswahili sanifu.
2. Onyesha kufanana na kutofautiana kwa ngeli za Luganda na katika jedwali.
3. Kwa kutumia jedwali, linganisha vivumishi vya –a unganifu, vimilikishi na vionyeshi vya Luganda na Kiswahili mkabala wa ngeli za Luganda na Kiswahili kwa umoja na wingi
4. Kwa kutumia nomino za Kiswahili, tunga sentensi mbili kwa umoja na wingi kuonyesha matumizi ya kila ngeli za Kiswahili ukishirikisha;
 - a) Vimilikishi -angu, -ako, -ake/-etu/-enu/-ao
 - b) Vionyeshi kwa nafsi ya kwanza, pili na tatu
 - c) –a unganifu kwa umoja na wingi
5. Tambua viwakilishi vya nafsi, njeo na hali katika Luganda na Kiswahili
6. Tunga sentensi tatu kwa kila kiwakilishi cha nafsi kwa umoja na wingi ukizingatia
 - a) Wakati uliopita
 - b) Wakati ujao
 - c) Wakati uliopo
 - d) Wakati uliopo hali timilifu
7. Onyesha tofauti ambayo inajitokeza baina ya
 - a) Viwakilishi vya nafsi ya Luganda na Kiswahili sanifu
 - b) Njeo na hali ya Kiswahili na Luganda

- | | |
|-------------------------------------|----------------------------------|
| b) Nilipenda kula siku hiyo | Tulipenda kula siku hiyo |
| c) Ulipenda kula chakula kila mara | Mlipenda kula chakula kila mara |
| d) Ulipendeza sana | Mlipendeza sana |
| e) Ulipita mtihani wa mwalimu wangu | Ulipita mtihani wa mwalimu wangu |
| f) Aliuliza maswali mengi leo | Waliuliza maswali mengi leo |
| g) Alitaka majibu yote | Walitaka majibu yote |
| h) Aliomba msaada wa utafiti wake | Waliomba msaada wa utafiti |

6. Kanusha sentensi zifuatazo

- Watoto wali**o**fika wamepewa chakula*
- Walimu wana**o**cheza mpira wameshinda*
- Kalamu ataka**o**yununua ni yangu*
- Kitabu kili**o**choletwa kiliraruka*
- Mti uli**o**katwa umekauka*

Kiambataisho 1C:

- Tunga sentensi kwa umoja na wingi kuonyesha matumizi ya vionyeshi vitatu kwa umjoa na wingi
- Kamilisha sentensi zifuatazo kutumia vionyeshi vinavyofaa. Una uhuru wa kutunga sentensi zako kwa umoja na wingi kutumia nomino hizi.
 - Mbuzi/...../.....anakula nyasi
 - Ng;mbwe/...../.....alikamwa na wazazi jana
 - Mkono...../...../.....una saa nzuri
 - Mkate...../...../.....
 - Mguu...../...../.....
 - Ujinga...../...../.....
 - Ugonjwa...../...../.....
 - Kiziwi...../...../.....
 - Kiongozi...../...../.....
 - gari...../...../.....
- Tunga sentensi kwa umoja na wingi kutumia nomino kuonyesha matumizi ya vionyeshi vya mbali, mbali kidogo na mbali sana kutumia nomino mbalimbali.
- Andika sentensi kwa kwa umoja na wingi kutumia nomino zifuatazo
 - Daktari
 - Polisi
 - Kifaru

- d) Dereva
 e) Bawabu
 f) Muuguzi
 g) Kiongozi
 h) Ng'ombe
 i) Askari
 j) Mbuzi
 k) Paka
5. Tambua ngeli katika ngeli ya U-I na kutunga sentensi kwa umoja na wingi.
6. Andika sentensi zifuatazo kwa wingi
- a) *Macho yananiuma*
 b) *Mkate umeletwa*
 c) *Mikate imeletwa*
 d) *Mbuzi imepelekwa malishoni*
 e) *Miti imekatwa*
 f) polisi alikuja hapa
 g) Askari wamekamata mutu
7. Tumia vimilikishi vinavyofaa na vitenzi kukamilisha sentensi zifuatazo
- a) *Ng'ombe...../...../..... Majani (kula)*
 b) *Ngombe...../...../.....majani (kula)*
 c) *Mpira/...../..... (pendeza)*
 d) *Kiatu/...../.....(raruka)*
 e) *Gari...../...../.....(anguka)*
 f) *Magari/...../.....(anguka)*
8. Tunga sentensi moja kwa kila ngeli kwa umoja na wingi kuonyesha matumizi ya -a unganifu.
9. Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia –a unagnifu
- | | |
|------------------------------------|-------------------------------|
| a) Kiongoziwa Kijiji amefika | Viongozi Kijiji amefika |
| b) Mbuzi.....anakula majani | Mbuziwanakulamajani |
| c) Derevea.....gari ameondoka | Derevaameondoka |
| d) Mguuunaniuma | Miguu.....inaniuma |
| e) Kikoikizuri kimeoshwa | Vikoi.....vizuri vimeoshwa |
| f) Chumvi.....imekwisha | Chumvi.....imekwisha |
| g) Maji.....yamemwagika | Maji.....yamemwagika |

10. Tunga sentensi kamili kutumia nomino zifuatazo kuonyesha matumizi ya
-a unganifu kwa umoja na wingi.
- a) Kondoo
 - b) Kondoo
 - c) Mpira
 - d) Jicho
 - e) Macho

MWISHO

Kiambatisho 2: Mjadala wa wanafunzi darasani kuhusu athari ya Mwingiliano

KIAMBATISHO CHA

MJADALA WA ATHARI ZA MWINGILIANO WA LUGANDA KATIKA

KISWAHILI SANIFU

1. Kwa kurejelea matokeo ya mijarabu ya mwenzako ni athari gani ambayo umeona ikijitokeza pale ambapo amekosea katika ngeli nomino, vivumishi, viwakilishi na ukanushaji?
2. Baada ya kutambua alipokosea mwenzako katika matokeo yake, tambua mwingiliano wowote wa Kimofosintaksia (Kimofolojia-maumbo) na (kisintaksia- muundo) wa Luganda ambao umejitokeza katika matokeo hayo ya mwanafunzi mweza.
3. Eleza uhusiano wa tungo za mwanafunzi mwenzako kimofolojia na kisintaksia na ile ya Luganda.
4. Eleza jinsi athari za mwingiliano wa kanuni (utaratibu wa matumizi) za Luganda ulivyoathiri (ulivyojitokeza) matumizi ya Kiswahili sanifu ya vipashio vya kimofosintaksia vya:
 - a) Nomino (ngeli katika nomino)
 - b) Vivumishi
 - i) Vimilikishi
 - ii) Idadi siyo dhahiri
 - iii) Vionyeshi
 - c) Viwakilishi
 - d) Vikanusho
5. Baada ya kutambua mwingiliano wa matumizi, kwa utaratibu na kwa kufuata masharti ya darasa, simama na kueleza kwa kukosoa mwingiliano wa Luganda ambao umejitokeza katika maandishi ya mwanafunzi mwenzako.
6. Eleza kanuni zilizokuongoza katika kutunga sentensi za Luganda na Kiswahili kwa umoja na wingi.
7. Onyesha jinsi kanuni za matumizi ya vipashio hivi huingiliana kati ya Luganda na Kiswahili sanifu kimofosintaksia.
8. Jadili athari za mwingiliano wa kanuni za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.
9. Je, ni nini unachoweza kusema kuhusu vipashio vya kimofosintaksia (ngeli, vivumishi, viwakilishi nafsi na vikanushi) vya Luganda na Kiswahili sanifu.

Kiambatanisho 3: Orodhahakiki ya Vipashio vya Mofosintaksia

1. Nomino katika ngeli za Luganda na Kiswahili
2. Vivumishi vimilikishi, -a unganifu na vya idadi isiyo kamili vya Luganda na Kiswahili
3. Viwakilishi vya nafsi, njeo na hali ya Luganda na Kiswahili
4. Vikanusho vya vipashio vya kimofosintaksia (1, 2 na 3) katika Luganda na Kiswahili
5. Uwiano wa vipashio vya kimofosintaksia (1,2 na 3) katika Luganda na Kiswahili
6. Tofauti ya vipashio vya kimofosintaksia (1,2 na 3) katika Luganda na Kiswahili sanifu.
7. Kanuni za matumizi ya vipashio vya kisarufi (1,2 na 3) za Luganda katika matumizi ya Kiswahili
8. Mwingiliano wa Kanuni za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu

MWISHO

Kiambatisho 4: Kifaa cha Orodha ya Uchunzaji cha Vipashio vya Mofosintaksia

Utafiti huu uliongozwa na kifaa hiki katika kuchunguza matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili kwa ajili ya kutambua uwiano na tofauti wa vipashio vya kimofosintaksia, kanuni za matumizi, mwingiliano na athari katika matumizi ya vipashio vya Luganda katika Kiswahili sanifu

1. Nomino
 - a) Uainishaji wa nomino katika ngeli
 - b) Mfumo wa uainishaji wa ngeli (kimofolojia na kisintaksia)
 - c) Mfumo wa Idadi za ngeli kimofolojia na kisintaksia (mpangilio wa nomino katika ngeli)
 - d) Maumbo ya nomino katika ngeli kimofolojia na kisintaksia
 - e) Mfumo uwiano wa kisarufi (mfumo milikifu na unganifu)
 - f) Nafasi tokeaji wa viambishi katika tungo
 - g) Mfumo wa uambishaji nomino na maneno mengine katika tungo
2. Vivumishi (Vimilikishi, -a unganifu, vionyeshi na idadi isiyo kamili)
 - a) Mfumo wa matumizi ya vivumishi
 - b) Mfumo wa idadi ya vivumishi
 - c) Maumbo ya vivumishi
 - d) Mfumo wa uambishaji (matumizi) wa vivumishi
 - e) Mfumo milikifu na unganifu wa vivumishi na maneno mengine katika tungo
 - f) Mfumo wa nafasi ya utokeaji wa vivumishi kuonyesha umilikifu na unganifu
3. Viwakilishi (Nafsi, Njeo na Hali)
 - a) Mfumo wa uwakilishi nafsi (je kuna uwakilishi)
 - b) Mfumo wa uainishaji wa viwakilishi nafsi
 - c) Mfumo wa uambishaji
 - d) Mfumo wa nafasi ya utokeaji
 - e) Mfumo milikifu na unganifu wa matumizi ya viwakilishi
4. Vikanusho
 - a) Mfumo wa ukanushaji (kuna mfumo kanushi)
 - b) Mfumo wa uainishaji/uwakilishi wa ukanushaji (njeo, hali, ngeli, nafsi)
 - c) Maumbo ya ukanushaji
 - d) Utaratibu wa ukanushaji
 - e) Mfumo wa nafasi ya utokeaji wa maumbo ya ukanushaji
 - f) Mfumo milikifu na unganifu wa maumbo kanushi

Kiambatisho 5: Data ya athari za mwingiliano iliyodondolewa nyanjani

Data hii ya athari katika matumizi ya ngeli, vimilikishi, Viwakilishi nafsi na vikanushi ni ile iliyodondolewa kutoka katika maandishi ya mijarabu na mazungumzo kutokana na mijadala ya wanafunzi nyanjani.

Kiambatisho 5A: Mwingiliano wa Matumizi ya Nomino katika Ngeli

| | | |
|----------------------------|------------------------|--------------------------|
| <i>Mutoto muzuri</i> | <i>Muwalimu murefu</i> | <i>Mupolisi/wapolisi</i> |
| <i>Mudaktari/wadaktari</i> | <i>Muti mukubwa</i> | <i>Mukati/mugati</i> |
| <i>Muguu gubwa</i> | <i>Vitabu byangu</i> | <i>Kiatu yangu</i> |
| <i>Kiatu change</i> | <i>Viatu zangu</i> | <i>Maji mangi/maingi</i> |
| <i>Mayai mangi/maingi</i> | <i>Sikio gupana</i> | |

Athari za Luganda kwa Kiswahili

Ng'ombe **zimeletwa** nyumbani Mbuzi **zinakula** majani Paka **zimekamata** panya

Athari za Luganda kwa Kiswahili

Mukate gumeisha jokoni Miti **gimekatwa**
Mugulu gunaluma **Maguu gananiuma**

Athari za Luganda kwa Kiswahili

Wamikate gimeletwa **Wamutoto banayimba** **Kiongozi kinaongeya**
Kifaru kinakimbia **Wapolisi walibakamata waizi**
Leta vitu mubiingize ndani **Mapolisi waliwakamata wezi** **Wadaktari balitibu sisi**
Mbuzi imepelekwa malishoni kula nyasi **Mbuzi imepelekwa malishoni kula nyasi**
Mbuzi zimepelekwa malishoni kula nyasi **Ng'ombe zimeletwa nyumbani**
Paka zimekamata panya **Meno gananiuma** **Muti gumevunjika** **Miti gimeanguka**
Kiongozi kinaongeya **Kifaru kinakimbia** **Mupolisi alikuja hapa** **Wapolisi walikuja hapa**
Musirikari amekamata mutu **Waaskari wamekamata mutu**

Kiambatisho 5B: Mwingiliano wa Matumizi ya Vivumishi Vivumishi vya Idadi Isiyodhahiri

Matumizi ya [-ngi na ingi]

Watu **mingi/bengine** wamekuja kulala Chakula **mingi/mingine** imepikwa
Maji mingi/maingine inamwagika **Maji maangi/maingi/mangine/maingine**
Viberiti bingi/bingine **Ugonjwa mingi/mingine**

Matumizi ya lala na -ingine

Watu waingine wanakuja Bintu bingine binasumbua Gari ingine inakuja
Kalamu ingine **Tunayenda kucheza muchezo ingine**

Matumizi ya -tono/Chache

Ng'ombe muchache/n-chache Nisaidie kalamu yako kadogo

Matumizi ya Onna na ote

Watu yote nasimama Amekula chakula yangu yote

Magari zote zimeenda Wanafunzi wawote/boote Penda yeye na moyo gwako gwote

Kiambatisho 5C: Mwingiliano wa matumizi ya Vivumishi Vionyeshi

Kitanda hichi ni kyangu Kitabu hikiyo china picha Muzuri

Viti hibi binaenda ofisini Bitabu hibiyo bipeleke darasani

Mutoto muzuri Kitanda muzuri Mchungwa

muzuri Ugonjwa mubaya Daktari muzuri

Kiambatisho 5D: Mwingiliano wa kanuni katika matumizi ya vivumishi vya idadi isiyodhahiri

Matumizi ya [-ngi na ingi]

Bageni baingi/bengine banakula Chakula mingi/mingine imepikwa

Maji mingi/maingine inamwagika Maji maaingi/maingi/mangine/maingine

Viberiti bingi/ bingine

Kiambatisho 5E: Mwingiliano wa kanuni za Vivumishi Vimilikishi

Ng'ombe yangu/ yako/ yake [zangu/ zako/ zake] Ng'ombe yetu/ yenu/ yao [Zetu/ zenu/ zao]

Mupira gwangu ngwako gwake [Gyangu/ gyako/ gyake]

Mipira yangu yako yake [Zangu/ zako/ zao]

Mipira yetu yenu yao [Zetu/ zenu/ zao]

Kyatu yangu yako yake [Kyangu/ kyako /kyake]

Viatu zangu zako zake [Zetu/ zenu/ zao]

Kitabo kyangu kyako kyake Kyetu kyenu kyao

Vitabu byangu, byako byake Byetu byenu byao

Gari yangu yako yake Yetu yenu yao

Magari zangu zako zake Zetu zenu zao

Paka hii enapenda kucheza Mbuzi hizi/ zile zinakula sana

Mlima hugu/ gule guna kima Nipatiye mugati gule/ guli

Hugwo mukeka ni gwange Bikopo hibi/bile binapendeza

Viatu hiyo ni bya nani?

Viatu zile zinapendeza

Nilimpatia zile vitu ulimpa

Mandazi huyo mutamu sana

Magari hizi/hizo/zile zimeanguka

Kiambatisho 5F: Vivumishi Vya –a Uganifu

Kondoo ya Kasibante imepoteya

Kondoo za Kasibante zimepoteya

Viongozi vya shule yetu

Mupira gwa gari kumepasuka

Mioyo gya watu ni mubaya sana

Jicho lya mutoto limevimba

Macho ga mutoto gamevimba

Machungwa ga Kenya matamu

Ulimi lwa nyoka lunatisha

Lugha lwa mwalimu ni ngumu

Muimbo lwa Chameleon unapendwa

Kiambatisho 5G: Mwingiliano katika Viwakilishi Nafsi vya Kiswahili

Mi naona wewe njiani

We aliona mimi wapi

Ye aliomba pesa mingi

Mimi nacheza mpira

Mimi nasema na wewe

Mi naona wewe njiani

We aliona mimi wapi?

Ye- aliomba pesa mingi

We onacheza mupila

Mimi iko jokoni

Mimi iko jokoni

We iko nalia sana

Wewe iko nalia sana

Ye iko nacheza

Yeye iko nacheza

Askari alibakimbiza waizi

Shangazi alimukimbiza mbuzi

Wewe alipiga mimi

Mimi niliomba yeye

Ye anajua wewe

Wanafunzi waliona wao

Mtoto alitoroka wewe

Lubega alimuleta yeye

Mupishi aliletaya sisi kyakula

Mpira ulipiga yeye

Mimi nilifanyia wewe kazi

Watoto wanasumbua sisi

Gari iligonga mimi

Baba atakuja kuona sisi

Yeye aliwomba msamaha kwa wewe

Mwalimu aliita yeye kwa ofisi

Kiambatisho 5H: Athari za Mwingiliano katika Ukanushaji wa Ngeli nomino za Kiswahili NGELI

Mtoto taenda shuleni

Mwalimu talinunua kalamu

Ng'ombe taletwa nymbani

Shangazi tameondoka leo

Watoto wataofika wamepewa sare.

Walimu wataocheza mpira wamelala.

Kalamu atayonunuwa ni yangu.

Kitabu kitacholetwa kiliraruka

Kiambatisho 5I: Viwakilishi Nafsi na Njeo

Mti utaokatwa umekauka

Shangazi tameondoka leo

Kiboko taonekana muzuri

Mimi sili mutoto

Sisi ni batoto

Sisi teli watoto

Mimi apana mutoto

Sisi apana watoto

Wewe toli maskini

| | | |
|--------------------------------------|-----------------------------------|----------------------------------|
| <i>Nyinyi temuli</i> | <i>Yeye tali maskini</i> | <i>Wao tewali maskini</i> |
| <i>Sinapenda kucheza Kandanda</i> | <i>Sinayimba wimbo na mwalimu</i> | |
| <i>Silikuomba kalamu yake</i> | <i>Silikimbia peke yangu</i> | |
| <i>Tonaenda shuleni mapema mara.</i> | <i>Tonajua kupika chapati</i> | <i>Tonapenda kulia kila</i> |
| <i>Apendi kulima</i> | <i>Asinapenda kulima</i> | <i>Aongei vizuri</i> |
| <i>Asileta chai tamu</i> | <i>Asilileta chai tamu</i> | <i>Asilitazama runinga</i> |
| <i>Atacheza mpira kesho</i> | <i>Asitacheza mpira kesho</i> | <i>Simeondoka</i> |
| <i>Simeona muwalimu</i> | <i>Simelala nyumbani</i> | <i>Usimekula Chakula</i> |

MWISHO

Kiambatisho 5J: Kiambatisho katika maandishi ya wanafunzi ya mijarabu

14

d) Kembe huu ni mkali sana. | Nyembe hizi ni kali sana.
 e) Ufagio huu ni mchafu. | Fagio hizo ni chafu.

8. Tungasentensitanokatikangeliya u-yakwaumojanawingi

a) Utete wangu huu umekuka. | Matete yangu si ya mekuka.
 b) Ushuzi wake huu unanuka. | Mashuzi yake si yananuka.
 c) Ung'anya wetu uli umepata. | Ung'anya yetu si yanapendeza.
 d) Ulezi wenu uli unapendeza. | Ulezi yenu si yanapendeza.
 e) Uganjwa wake huu umepan. | Maganjwa yake si yamepana.

9. Tungasentensitanokatikangeliyaya-ya

a) Maji hii haijanwagika.
 b) Majani hii haijakuka.
 c) Mkati hii haiharibika.
 d) Mdame hii haiwachungu.
 e) Mkano hii haikatawa.

10. Tungasentensitanokatikangeliyai-ikwaumojanawingi

a) Mkano huu hukuka has.
 b) Mkati huu huheribika.
 c) Majani huu hukuka.
 d) Mdame huu huwachungu.
 e) Maji huu husijamagika.

16

d) Ufungu wenu umewajika. (Fungu zetu zimewajika.)
 e) Uzi uli si mfupi. (Mizi zile si fupi.)

8. Tungasentensitanokatikangeliya u-yakwaumojanawingi

a) Utete wangu umekauka. (Matete yangu yamekauka.)
 b) Ushuzi wake unanuka. (Mashuzi yake yananuka.)
 c) Uganjwa wake umepana. (Maganjwa yake yamepana.)
 d) Ung'anya wetu umepata. (Majanya yetu yamepata.)
 e) Ulezi wenu unapendeza. (Malesi yenu yanapendeza.)

9. Tungasentensitanokatikangeliyaya-ya

a) Maji haya yamewagika.
 b) Majani haya yanakauka.
 c) Mkati haya yameharibika.
 d) Mdame haya ya mwachungu.
 e) Mkano haya ya likatwa.

10. Tungasentensitanokatikangeliyai-ikwaumojanawingi

a) Maji hii imewajika.
 b) Majani hii imekauka.
 c) Mkati hii imeharibika.
 d) Mdame hii imewachungu.

8

d) Uta huu kimepotea. | Uta hizo vimepotea.
 e) Upopo ni haraka sana. | Papa ni haraka sana.

8. Tungasentensitanokatikangeliya u-yakwaumojanawingi

a) Utete wangu umekauka. | Matete wangu yamekauka.
 b) ulezi yake ni mbaya sana. | ulezi wako ni mbaya sana.
 c) Umbile ya nyumba hiya ni nzuri. | Mabile ya nyumba hizo ni nzuri.
 d)
 e) Ung'anya yatawii ni urembo. | Majanya yatawii ni mrembo.
Utambeezi wako ni haraka. | Matambeezi wako ni nakara.

9. Tungasentensitanokatikangeliyaya-ya

a) Chatula wangu ni nzuri. | chatula yetu ni nzuri.

Kiambatisho 6: Kiambatisho cha Kibali cha kushiriki katika utafiti

Mimi ninakubali kushirikishwa katika utafiti huu bila kulazimishwa na mtafiti wala mtu yeyote. Ninatoa maoni yangu kwa uaminifu bila malipo yoyote. Mungu ndiye shahidi wangu.

Jina la Mtafitiwa

Umri wake

Darasa

Tarehe

Sahihi

Maoni yako yatawekwa siri na mtafiti na hayatatolewa kwa vyovyote vile.

Mtafiti

Sahihi

Kiambatisho7: Barua ya Kamati ya maadili



RESEARCH ETHICS COMMITTEE

(+256) 0312 307400
 rec@ciu.ac.ug
 www.rec.ciu.ac.ug

To: Mulei Martin

21/03/2022

Clarke international university

Type: Initial Review



Re: CLARKE-2022-343: Analysis of Morphosyntax Interference of Luganda on Standardized Kiswahili Usage in Secondary Schools in Kampala District, Uganda

I am pleased to inform you that at the 27th convened meeting on 21/03/2022, the Clarke International University REC, committee meeting, etc voted to approve the above referenced application. Approval of the research is for the period of 21/03/2022 to 21/03/2023.

As Principal Investigator of the research, you are responsible for fulfilling the following requirements of approval:

1. All co-investigators must be kept informed of the status of the research.
2. Changes, amendments, and addenda to the protocol or the consent form must be submitted to the REC for re- review and approval **prior** to the activation of the changes.
3. Reports of unanticipated problems involving risks to participants or any new information which could change the risk benefit: ratio must be submitted to the REC.
4. Only approved consent forms are to be used in the enrollment of participants. All consent forms signed by participants and/or witnesses should be retained on file. The REC may conduct audits of all study records, and consent documentation may be part of such audits.
5. Continuing review application must be submitted to the REC **eight weeks** prior to the expiration date of 21/03/2023 in order to continue the study beyond the approved period. Failure to submit a continuing review application in a timely fashion may result in suspension or termination of the study.
6. The REC application number assigned to the research should be cited in any correspondence with the REC of record.
7. You are required to register the research protocol with the Uganda National Council for Science and Technology (UNCST) for final clearance to undertake the study in Uganda.

The following is the list of all documents approved in this application by Clarke International University REC:

| No. | Document Title | Language | Version Number | Version Date |
|-----|------------------------|-----------|----------------|--------------|
| 1 | Informed Consent forms | English | 1.0 | 2022-03-18 |
| 2 | Data collection tools | English | 1.0 | 2022-03-18 |
| 3 | Protocol | English | 2.0 | 2022-03-18 |
| 4 | Protocol | Kiswahili | 2.0 | 2022-03-18 |
| 5 | Risk management plan | English | 1.0 | 2022-03-18 |
| 6 | Informed Consent Form | Kiswahili | 2.0 | 2022-03-18 |

Yours Sincerely

Samuel Kabwigu

For: Clarke International University REC



Kiambatisho 8: Barua ya Kuomba Idhini ya Kufanya Utafiti Shuleni

Maseno University,
School of Post Graduate,
S. L. P 3275-40100,
Kisumu, Kenya.
20/02/2021.

Through the Head of Department Kiswahili

TO

The Head teacher,

.....
.....

Dear Sir/Madam

REF: Request to carry out research in your Schools

I am writing to request for your permission to allow me collect data for Educational purpose from your School. My name is Mulei Martin, (registration number, PHD/FA/00087/2016). I am a Ugandan citizen studying from Maseno University in Kenya. The study is in the field of language (Linguistics). The topic of my study is “Analysis of Morphosyntax Interference of Luganda on Standard Kiswahili Usage in Kampala District. The study intends to collect data from senior six Kiswahili class.

The data collection is for academic purpose and not any other purpose. The period and time of study will not be interrupted but will be used constructively during the Kiswahili periods. I will also request you to allow the Kiswahili teacher to be part of the class to support me in the process of Data collection. Your permission will be of great use and shall be appreciated in the contribution and successful completion of this study. Looking forward for your considering.

Yours faithfully



Mulei Martin (+256704176271)

Kiambatisho 9: Barua ya kuidhinisha kuendelea na Utafiti kutoka Chuoni



**MASENO UNIVERSITY
SCHOOL OF GRADUATE STUDIES**

Office of the Dean

Our Ref: PHD/FA/00087/2016

Private Bag, MASENO, KENYA
Tel: (057) 351 22/351008/351011
FAX: 254-057-351153/351221
Email: mas@maseno.ac.ke

Date: 16th March 2020

TO WHOM IT MAY CONCERN

RE: PROPOSAL APPROVAL FOR MULEI MARTIN —PHD/FA/087/2016

The above named is registered in the Doctor of Philosophy programme in the School of Arts and Social Sciences, Maseno University. This is to confirm that his research proposal titled "Analysis of morphosyntax interference of Luganda on standardized Kiswahili usage in Secondary schools Kampala District, Uganda." has been approved for conduct of research subject to obtaining all other permissions/clearances that may be required beforehand.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'J.O. Agure'.

Prof. J.O. Agure

DEAN, SCHOOL OF GRADUATE STUDIES

Maseno University

ISO 9001:2008 Certified



KIAMBATISHI 10

Kiambatisho 10: Orodha ya Vitabu na Matini Teule katika Utafiti

Uchanganuzi matini wa orodha ya Vitabu vya Luganda vilivyoteuliwa

1. Abudonia, R. A. (2014). The Syntax of Luganda Adjectives: Katika Egyptian Journal of Linguistics and Translation, 1(1), 35–44.
2. Ashton, E. O., Mulira, E. M. K., Ndawula, E. G. M., na Tucker, A. N. (1954). A Luganda grammar. London: Longmans.
3. Bernander, R., Devos, M., & Gibson, H. (2018). The negative existential cycle in Bantu. *Unpublished manuscript. University of Helsinki, Royal Museum of Central Africa, University of Essex.*
4. Dixon, R. M. W. (2010). *Where have all the adjectives gone?: and other essays in semantics and syntax* (Vol. 107); Walter de Gruyter.
5. F. K., & Stevick, E. W. (1968). *Luganda: basic course*. Foreign Service Institute;
6. Ferrari-Bridgers, F. (2008). A unified syntactic analysis of Italian and Luganda nouns. *The Bantu-Romance Connection*, 239-258
7. Hyman, L. (2018). The First Person Singular Subject Negative Portmanteau in Luganda and Lusoga. *Berkeley Papers in Formal Linguistics*, 1(1)
8. Kiyinikibi, N. D. (2021). *The locative in Luganda: a syntax-interfaces approach* (Doctoral dissertation, Stellenbosch: Stellenbosch University)
9. Kyagaba, D (1996) Ggulama W'oluganda Omusengejje. Mk Publishers;
10. Leah, S na Sseguya, F.N. (2015). A Luganda grammar. Yiga Olu-ganda. Accessed on 9 February 2016 from <http://learn-luganda.com>
11. Mugerwa Johnson (2012) Ggulama mu Luganda : N'empaniika etongole ; ("O" and "A" levels), Kampala: National Education Research and examination Bureau;
12. Mutale , T. na Muwanga, D. (2009) Ettaalaya Ggulama. TTESUPA Booklex; Kamoga,
13. Namugala, S. (2014). *Diminutive and Augmentative Functions of some Luganda Noun Class Markers.[Tasnfu ya Uzamili] ya, Norges teknisk-naturvitenskapelige universitet, Det humanistiske fakultet, Institutt for språk of litteratur*);
14. Nurse, D., na Philippson, G. (2003). Towards a historical classification of the Bantu languages. *The Bantu Languages*, 164–181;

15. Ssekiryango, J. (2006). Observations on double object construction in Luganda. In *Selected proceedings of the 36th annual conference on African linguistics* (pp. 66–74);
16. Ssentumbwe, A. M., Kim, B., na Lee, H. (2019). English to Luganda SMT : Ganda Noun Class Prefix Segmentation for Enriched Machine Translation International Journal of Advanced Trends in Computer Science and Engineering;

Uchanganuzi Matini wa Vitabu vya Kiswahili sanifu

1. Beaudoin-Lietz, C. (1999). Formatives of Tense , Aspect, Mood and Negation in the Verbal Constuction of Standard Swahili. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Memorial Newfoundland.(Haijachapishwa).
2. Besha, Ruth M . (1996). Misingi ya uainishaji ngeli - Besha.pdf. Kioo cha Lugha;
3. Chomi, E. (2013) *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam; Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
4. Habwe J. na Karanja P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd
5. Kawale, F. R. (2015). *Ukanushi wa vishazi katika kiswahili sanifu* (Doctoral dissertation, University of Dar es Salaam).
6. Kihore, Yared Magori, Massamba, D. P. B., na Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam
7. Lupogo, I. (2021). Ulinganishaji wa Maumbo na Miundo ya Ukanushi katika Lugha ya Kiswahili na Kiingereza. *Journal of Linguistics and Language in Education*, 14(2)
8. Mulei, M., Ambuyo, B., & Amukowa, D. (2021). Uhakiki Linganishi wa Kimofosintaksia Katika Ngeli za Luganda na Kiswahili Sanifu. TAALUMA. Jarida la CHAKITA, Juzuu 1(1), 139-149.(<http://chakita.org/makala/uhakiki-linganishi-wa-kimofosintaksia-katika-ngeli-za-luganda-na-kiswahili-sanifu/>)
9. Mulei, M., Amukowa, D., na Ambuyo, B. (2021). Athari za Kimofosintaksia za Ngeli za Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu Miongoni mwa Wanafunzi Shuleni, Uganda. *Jarida La Afrika Mashariki La Masomo Ya Kiswahili*, 3(1), 10-23. <https://doi.org/10.37284/jammk.3.1.331> [a peer reviewed article in the East African Journal of Swahili Studies].
10. Mulei. M., Ambuyo, B., Amukowa, D (2021). Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda Katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu:

Jarida la idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Moi, Kenya;

11. Matasi, B., H., na Furaha, C., (2016) Ulinganishaji wa Kimofosintaksia Baina ya Kiswahili na Kiarabu katika Viwakilishi-nafsi: *RUWAZA AFRICA. Journal of Contemporary Research in Humanities and Social Sciences. Juzuu la 4 (144-151)*,
12. Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Ltd, Nairobi Kenya;
13. Mulei, M (2020) Athari ya Ukopaji wa Kanuni za Ukanushaji Katika Mazungumzo ya Kiswahili. Book Article: In *KISWAHILI NA MAENDELEO YA AFRIKA MASHARIKI, TATAKI, Tanzania*;
14. Ngonyani, D. (2001). The morphosyntax of negation in Kiswahili;
15. Philipo, Z. T. (2017). Tofauti Baina ya Vivumishi na Viambishi katika Lugha ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha, 13(1)*.
16. Philipo, Z.T na Kuyenga, F E (2017) Sintaksia ya Kiswahili: Nadharia za Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili. Karljamer publishers Limited, Tanzania.
17. Sakwa, T., Masaba, V, Kajoka, J., na Gashengeshi, A (2013) Msingi bora wa Kiswahili darasa la 5, 6 na 7: Kitabu cha Mwanafunzi. Longhorn Publishers Uganda Ltd.
18. Taher, M. A. (2013). *Tofauti ya Viambishi Kanushi Kati ya Kiswahili na Kiarabu*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania).